**22 MEI, 2023**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA MOJA

**Kikao cha Thelathini – Tarehe 22 Mei, 2023**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Daniel B. Sillo) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZILIZOWASILISHA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na: -

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE):**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

**MHE. ALLY A. J. MLAGHILA K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kwa mwaka wa fedha 2022/2023 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Katibu.

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**MWENYEKITI:** Maswali Waheshimiwa Wajumbe, tunaanza Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Mheshimiwa Ally Anyigulile Jumbe Mlaghila, Mbunge wa Kyela, sasa aulize swali lake.

Na. 386

### Kukamilisha ujenzi wa wodi ya mama na mtoto – Kyela

**MHE. MASACHE N. KASAKA K.n.y. MHE. ALLY A. J. M. JUMBE** aliuliza: -

Je, lini Serikali itamaliza ujenzi wa wodi ya mama na mtoto katika Halmashauri ya Wilaya ya Kyela ambayo ujenzi wake umesimama?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ally Anyigulile Jumbe Mlaghila Jumbe, Mbunge wa Jimbo la Kyela, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Kyela inatekeleza ujenzi wa jengo la ghorofa la kutoa huduma ya mama na mtoto katika hospitali ya wilaya. Utekelezaji wa mradi ulianza Septemba, 2019 chini ya Wakala wa Majengo Tanzania (*TBA*) kwa gharama ya shilingi bilioni 3.81. Aidha, hadi kufikia Aprili, 2023 Serikali imeshatoa shilingi bilioni 2.75 na ujenzi umefikia asilimia 72.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2023/2024 Serikali imetenga shilingi milioni 800 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi, na Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa mradi huo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mlaghila, swali la nyongeza.

**MHE. ALLY A. J. M. JUMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kwa majibu ya Serikali, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapozungumzia hospitali ambazo ni kielelezo na zipo mpakani ni Hospitali ya Kyela, lakini hospitali hii ni hospitali kongwe sana ambayo kwa sasa hivi haitamaniki na hata ukifanya usafi haioneshi kwamba ni hospitali ambapo watu wanaweza wakatibiwa na kupata faraja.

Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka kwa Serikali kuhakikisha majengo haya yanajengwa upya na yanakuwa mapya kwa ajili ya kuwa na manufaa kwa wananchi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; ikama ya wafanyakazi walioko katika Wilaya ya Kyela imepungua sana na iko kiwango cha chini kukidhi mahitaji ya magonjwa mengi ambayo yako Kyela.

Je, Serikali haioni haja ya kuongeza wafanyakazi kwa kipindi hiki?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nijibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mlaghila Jumbe; la kwanza la fedha kutengwa kwa jili ya ukarabati wa hospitali hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kama nilivyokuwa nimeshasema kwenye majibu yangu ya msingi, tayari Serikali imeshatenga fedha zaidi ya bilioni 2.75 ambazo zimekwenda katika Hospitali ya Wilaya ya Kyela ili kuhakikiusha kwamba inafanyiwa ukarabati; na

katika mwaka huu wa fedha tumetenga shilingi milioni 800 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi huo. Nimtoe mashaka Mheshimiwa Mbunge, kwamba ni adhma ya Serikali hii ya awamu ya sita ya Dkt. Samia Suluhu Hassan kuhakikisha inakarabati hospitali kongwe zote nchini, ikiwemo ya Kyela, na tutaendelea kutafuta fedha kufanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda kwenye swali la pili la ikama ya watumishi. Bunge lako tukufu hili ni mashahidi, Serikali imetangaza ajira zaidi ya 21,300 kwenye sekta ya elimu na sekta ya afya. Ajira hizi zitakapokamilika tutahakikisha vilevile Hospitali ya Kyela inapata wataalamu ambao wanatakiwa kuhudumia Watanzania waliopo Kyela pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Ahsante, tunaendelea na Wizara hiyo hiyo, Mheshimiwa Esther Edwin Malleko, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 387

**Serikali kumalizia ujenzi wa maboma Kilimanjaro**

**MHE. ESTHER E. MALLEKO** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaunga mkono jitihada za wananchi wa Kilimanjaro kwa kumalizia ujenzi wa maboma ya zahanati na vituo vya afya?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Esther Edwin Malleko, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2021/2022 na 2022/2023, Serikali ilitenga shilingi bilioni 1.96 kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma ya zahanati 37 katika Mkoa wa Kilimanjaro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2023/2024, Serikali imetenga shilingi bilioni 2.35 kwa ajili ya ujenzi na ukamilishaji wa vituo vya afya vitatu na zahanti 17.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma ya vituo vya afya na zahanati nchini kote.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther Malleko, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER E. MALLEKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Pamoja na maswali mazuri sana na Serikali lakini nilitaka kujua, je, ni lini katika ajira hizi zilizotangazwa watumishi hawa wataingia kazini ili waende wakawatibu Watanzania wengi ambao wanahitaji huduma hiyo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ajira hizi zilizotzngazwa zote 21,300 katika sekta ya elimu na afya zitaanza kutumika au wataingia kazini baada ya mchakato wa ajira hizi kukamilika ndani ya mwaka huu wa fedha. Kwa hiyo muda siyo mrefu Mheshimiwa Malleko kule Kilimanjaro lakini na Waheshimiwa Wabunge wote hapa wataanza kuona wale watumishi wapya wanaaanza kwenda kwenye maeneo yao.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Amsabi Mrimi, swali la nyongeza.

**MHE. JEREMIAH M. AMSABI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kuna jitihada nyingi katika Jimbo la Serengeti Kijiji cha Nyamatale pale Nyirongwa wamejenga boma, pale Kitalahota Kitongoji katika Kijiji cha Nyamakobiti, pia wamejenga

boma kwa jajili ya zahanati, Kijiji cha Bisalala, Ngalawani na Kenokwi.

Je, ni lini sasa Serikali itatoa mchango wake kusaidia jitihada hizi za wananchi kukamilisha zahanati hizi? ahsante

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Amsabi la zahanati hizi za vijiji ambavyo amevitaja Serikali itaunga mkono juhudi za wananchi hawa kadri ya upatikanaji wa fedha. Na tutajitahidi, kwa sababu ni adhma ya Serikali hii ya awamu ya sita kuhakikisha afya za Watanzania zinaimarika zaidi kwa kupata huduma iliyobora. Tutahakikisha kadri ya upatikanaji wa fedha tunachangia nguvu za wananchi wa pale.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, swali la nyongeza.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Mheshimiwa Waziri katika Wilaya ya Rungwe Mheshimiwa Mbunge wa jimbo pamoja na Diwani wa Kata ya Kiwila na wananchi wameweza kujenga Zahanati ya Kiwila lakini bado haijamalizika.

Je, ni lini, Serikali mtaenda kuweka nguvu ili tuweze kumaliza zahanati ile?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Zahanati hii ya Kiwila kule Rungwe itatengewa fedha kadri ya upatikanaji wa fedha; na tutaangalia katika mwaka wa fedha huu 2023/2024 ambao tunaenda kuanza kuutekeleza kama imetengewa fedha. Kama haijatengewa fedha tutaangalia kuitengea fedha katika mwaka wa fedha 2024/2025.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Condester Sichalwe, swali la nyongeza.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipatia nafasi. Katika Jimbo la Momba kuna vijiji zaidi ya 20 ambavyo wananchi wamejenga maboma na wanahitaji kuungwa mkono na Serikali. Mfano, Kijiji cha Mwenehemba, Mamsinde *one*, Namsinde *two*, Kakozi, Chilangu na vinginevyo.

Je, ni lini, Serikali itatusaidia ili kumalizia maboma haya?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itasaidia umalizaji wa maboma haya 20 aliyotaja Mheshimiwa Condester Sichalwe kadri ya upatikanaji wa fedha. Nitumie nafasi hii kuwataka Wakurugenzi wote wa Halmashauri nchini kuhakikisha wanatenga fedha katika mapato yao ya ndani kuunga mkono juhudi za wananchi katika maeneo yao ya kiutawala ili kuweza kumalizia iwe ni katika zahanati iwe ni katika shule.

**MWENYEKITI:** Tunaendela na Wizara hiyo hiyo. Mheshimiwa *Engineer* Ezra John Chiwelesa, Mbunge wa Biharamulo, sasa aulize swali lake.

Na. 388

**Uhaba wa Watendaji wa Kata na Vijiji – Biharamulo**

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itatoa kibali cha ajira za watendaji wa kata na vijiji katika Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa *Engineer* Ezra John Chiwelesa, Mbunge wa Jimbo la Biharamulo Magharibi kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo ilikuwa na upungufu wa watendaji wa vijiji 33. Katika mwaka wa fedha wa 2021/2022 na 2022/2023 Serikali kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Biharamuro imeajiri watendaji wa vijiji 20.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2023/2024 Halmashauri ya Wilaya ya Biharamuro imeomba kibali cha kuajiri watendaji wa kata saba na watendaji wa vijiji 13.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendela kuajiri watendaji wa vijiji na kata katika halmashauri zote inchini iliwemo Halmashauri ya Wilaya ya Biharamuro kadri ya bajeti itakavyoruhusu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ezra, swali la nyongeza.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Nishukuru kwa majibu mazuri ya Serikali ambayo ameyatoa Mheshimiwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Biharamulo kijiografia ni eneo kubwa sana na tumekuwa katika *scarcity* hiyo ya watendaji kwa muda mrefu sana. Sasa kwa sababu umesema tayari maombi yetu mnayo.

Swali la kwanza; je, ni nili tutapatiwa kibali tuweze kuajiri watendaji ku-*cover* zile nafasi ambazo zimebaki?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini swali la pili kama unavyojua Wilaya ya Biharamulo sasa *population* yetu ni watu 457,114. Jimbo hili ndilo linaloongoza kwa idadi kubwa ya watu kwa Mkoa wa

Kagera, lakini kijiografia pia ni Jimbo kubwa zaidi lina vijiji 79, kata 17 lakini zilizotawanyika sana.

Je, huoni kwamba iko haja ya Serikali kutupatia usafiri kwa ajili ya watendaji wa vijiji na kata ili huduma za wananchi ziweze kufika kwa haraka zaidi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikijibu swali la kwanza la Mheshimiwa Ezra Chiwelesa, la lini kibali hiki cha ajira. Nikirejea majibu yangu ya msingi, tutatoa vibali hivi kadri ya bajeti itakavyoruhusu, lakini tayari Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo imeshapata watendaji wa vijiji 20 katika mwaka wa fedha 2021/2022 na 2022/2023. Kwa hiyo, nimtoe mashaka Mheshimiwa Mbunge Serikali inatambua upungufu huu na inaendelea kulifanyia kazi na muda si mrefu mtaona watendaji hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda kwenye swali la pili la usafiri. Wote humu ndani ni mashahidi katika awamu hii ya sita ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan imefanya kwa mara ya kwanza kuanza kutoa pikipiki kwa watendaji wa kata zetu zote nchini. Tayari walikuja Dodoma hapa na wakakabidhiwa pikipiki hizo. Na zile kata ambazo bado zimesalia kuna baadhi ya Wakurugenzi ambao wameanza kununua kwa mapato yao ya ndani na kuunga mkono juhudi za Mheshimiwa Rais wetu. Kwa hiyo niwatake tena Wakurugenzi wa Halmashauri kote nchini kuhakikisha wanatenga fedha ya kununua usafiri kwa ajili ya watendaji wa kata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na inaporuhusu bajeti basi hadi kwa watendaji wa vijiji, lakini mpaka sasa Serikali itaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kupunguza upungufu huu wa usafiri.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Catherine Magige, swali la nyongeza.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Katika Mkoa wa Arusha kuna watendaji wa vijiji wengi wamekuwa wakikaimu. Mfano tu, katika Wilaya ya Longido kuna watendaji wa vijiji 23 wamekaimu kwa muda mrefu na wana sifa.

Je, ni lini Serikali itatoa ajira kwa watendaji wa vijiji hawa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itatoa ajira za watendaji wa vijiji kadri ya bajeti itakavyoruhusu. Niseme tu, kukaimu utendaji wa kijiji huu, hawa 23 hai-*guarantee* kwamba ajira zitakapotangazwa kwamba wao ndi wataingia, zitafuata mchakato kama inavyotaka kwa ushindani na wale ambao wataonekana wana sifa za kuajiriwa ndio ambao wataajiriwa na kuwa watendaji wa vijiji. Kwa hiyo Mheshimiwa Mbunge avute subira na kadri ya bajeti itakavyoruhusu Serikali itaajiri.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Amandus swali la nyongeza.

**MHE. AMANDUS J. CHINGUILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Jimbo la Nachingwea lina kata 36, kati ya hizo kata mbili hazina watendaji wa kata, lakini lina vijiji 127 na vijiji 37 havina watendaji wa vijiji. Na kwa kuwa tunajua watendaji hawa ndio wanaosukuma shughuli zote za maendeleo katika maeneo yetu;

Je, ni lini Serikali itatoa vibali kwa ajili ya kupata hawa watendaji ambao watatusaidia kwenye maendeleo kwenye maeneo yetu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kata mbili ambazo hazina watendaji na vijiji 37

ambavyo havina watendaji kule Nachingwea ni adhma ya Serikali kuhakikisha kwamba kila kata, kila kijiji kina watendaji. Kadri ya bajeti itakavuoruhusu basi viabali hivi vitaendelea kutolewa. Na nikutaarifu tu Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali iko mbioni kuajiri watendaji wa kata katika kata zote ambazo ziko wazi nchini. Kwa hiyo ni kuvuta Subira, nikuhakikishie kwamba hilo linafanyiwa kazi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Asenga, swali la nyongeza.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwa kuwa Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan analeta fedha nyingi sana za miradi katika Halmashauri ya Mji wa Ifakara, na kwa kuwa miradi hiyo mingi haiendi vizuri na sababu moja wapo ni kukosekana kwa mtumishi Mkuu wa Idara ya Ujenzi;

Je, ni lini Serikali inapeleka injinia mzoefu wa majengo ya ujenzi Halmashauri ya Mji wa Ifakara ili kunusuru miradi hii?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikiajiri mainjinia, kulitokea changamoto ya kuwa na upungufu wa mainjinia katika halmashauri zetu nchini, baada ya kuanzishwa *TARURA;* mainjinia wengi wa halmashauri walihamia wakala wa *TARURA*. Mwaka wa fedha uliopita Serikali iliajiri mainjinia zaidi ya 265 ambapo kila halmashauri nchini ilipata injinia mmoja, na hivi sasa Serikali ipo katika mchakato wa kuajiri tena mainjinia kwa ajili ya kutoa upungufu huu ambao upo ikiwemo kule kwa Mheshimiwa Asenga na tutaangalia pale ambapo ajira hizi zitapatikana basi kule kwa Mheshimiwa Asinga nao watapata injinia.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chege, swali la nyongeza.

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Halmashaui ya Wilaya ya Rorya ni mwaka wa tatu sasa haijawahi kuajiri watendaji wa vijiji wala wa kata na kwa

kuwa sasa tumeomba kibali kwa ajili ya kupata kuajiri watendaji hawa;

Je, Serikali inachelewa nini kutupa kibali na sisi tuweze kuajiri kwenye maeneo ambayo yana upungufu wa watendaji wa vijiji na watendaji wa kata?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itatoa vibali hivi vya ajira kadri ya bajeti itakavyoruhusu, na tutaangalia katika bajeti iliyotengwa mwaka 2023/2024, kama kuna nafasi hizi zilizotangazwa basi kule Rorya ambapo kuna upungufu na wameomba kibali, kibali kiweze kutolewa. Kama hakuna iliyotengwa basi tutaipa kipaumbele katika mwaka wa fedha wa 2024/2025.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Wizara hiyohiyo. Mheshimiwa Cecil David Mwambe, Mbunge wa Ndanda sasa aulize swali lake. Kwa niaba yake Mheshimiwa Issa Mchungahela.

Na. 389

**Kukarabati shule chakavu - Masasi**

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA K.n.y. MHE. CECIL D. MWAMBE** aliuliza: -

Je, lini Serikali itakarabati majengo ya shule za msingi chakavu Wilayani Masasi yaliyojengwa kati ya mwaka 1905 na 1960?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais -TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Daniel Cecil Mwambe, Mbunge wa Jimbo la Ndanda, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Masasi ina jumla ya shule za msingi 40 ambazo ni kongwe na chakavu. Kwa mwaka wa fedha wa 2022/2023 Serikali imepeleka shilingi milioni 200 katika shule kongwe na chakavu za Liloya na Lusonje kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vitano vya madarasa na tayari yamekamilika. Aidha, shilingi milioni 180 zimepelekwa katika Shule Kongwe ya Luatala kwa ajili ya ujenzi wa vyumba tisa vya madarasa, na taratibu za ujenzi zimeanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shule nyingine kongwe za Mkalapa, Rivango, Chikoropola, Mwena na Lulindi Maalum zimetengewa fedha kupitia mradi wa *BOOST* na utekelezaji unatarajiwa kuanza hivi karibuni.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Issa Mchungahela, swali la nyongeza.

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Namshukuru Mheshimiwa Naibu kwa kutupatia baadhi ya shule chache, kama alivyosema, miongoni mwao zikiwepo Rivango, Chikolopola pamoja na Lulindi Maalum, lakini kama Waziri anavyoona shule zilizokuwa mbovu au chakavu ni nyingi sana kwenye majimbo hayo mawili, hususan kwenye Jimbo la Lulindi anaweza akaona, ziko zaidi ya 20 na kitu. Ni lini atafanya jitihada kwa ajili ya kumalizia hizo shule nyingine chakavu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mwambe. Serikali inatambua kwamba, shule nyingi za msingi nchini ni chakavu na tayari tumeona jitihada kubwa za Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan za kutafuta fedha kwa ajili ya kupunguza uchakavu huu katika shule zetu za msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari katika Halmashauri ya Wilaya ya Masasi ambayo ina Jimbo la Mheshimiwa Mchungahela na Mheshimiwa Mwambe, Shule ya Chikolopa imepokea shilingi milioni 331, Shule ya Rivango imepokea shilingi milioni 101, Shule ya Mkalapa imepokea milioni 120, Shule ya Mwena milioni120 na Shule ya Lulindi Maalum imepokea milioni 54. Fedha hizo ni kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vipya vya madarasa na ukarabati katika shule hizi. Hizi ni jitihada za wazi za Serikali ya Awamu ya Sita ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kuhakikisha upungufu huu wa majengo katika shule za msingi na uchakavu unakwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwatoe mashaka Waheshimiwa Wabunge, Serikali itaendelea kujitahidi kutafuta fedha hizi kwa ajili ya kukarabati shule nyingi zaidi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Minza Mjika, swali la nyongeza.

**MHE. MINZA S. MJIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika Wilaya ya Itilima kuna shule mbili, shule ya kwanza ni Shule ya Msingi Itubilo ambayo imejengwa mwaka 1965. Majengo yake yamechakaa sana, lakini pia kuna Shule ya Msingi Mwagindu, imejengwa mwaka 1950, nayo majengo yake yamechakaa sana. Je, ni lini Serikali itakarabati majengo hayo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema hapo awali kwamba, ni azma ya Serikali kuhakikisha kwamba, inakarabati shule zote ambazo ni za siku nyingi au kongwe katika halmashauri zote nchini. Hivyo basi, Mheshimiwa Mbunge awe na subira, Serikali itaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kukarabati shule hizi kongwe zilizopo Itilima.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Iddi Kassim, swali la nyongeza.

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nataka kufahamu ni upi sasa mkakati wa Serikali wa kutenga fedha kuweza kwenda kurekebisha shule chakavu kwenye

Halmashauri ya Msalala, ikiwemo Shule ya Msingi Isaka, Kata ya Isaka, Shule ya Msingi Kilimbu, Kata ya Mwaruguru na Shule ya Msingi Butegwa, Kata ya Ngaya? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, shule hizi za kule Jimbo la Msalala alizozitaja Mheshimiwa Iddi Kassim zitakarabatiwa kadiri ya upatikanaji wa fedha. Tayari Halmashauri ya Msalala pia imepokea fedha ya kukarabati shule kongwe na chakavu na kujenga shule nyingine kutokana na Mradi wa *BOOST* ambao fedha zimekwenda. Ni zaidi ya bilioni 230 ambayo Serikali hii ya Awamu ya Sita imetoa kwa kila halmashauri hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii mbele ya Bunge lako Tukufu kuwaelekeza Wakurugenzi wote wa Halmashauri Nchini, kuhakikisha wanatenga fedha na kuanza ukarabati wa shule chakavu katika maeneo yao ya halmashauri zao kwa sababu, tayari Serikali hii imeshasaidia sana katika ujenzi wa miundombinu mbalimbali kwa kutafuta fedha kutoka Serikali Kuu na wao sasa waanze kutenga kutoka kwenye mapato yao ya ndani.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther Midimu, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER L. MIDIMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa, Shule ya Mwanhale, Kata ya Mkula, Wilaya ya Busega, majengo yake yamechakaa sana. Je, ni lini Serikali itakarabati majengo hayo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itakarabati shule hizi chakavu zilizokuwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Busega kadri ya upatikanaji wa fedha.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru sana kwa majibu ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Amina Daudi Hassan, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 390

**Fedha za mabadiliko ya tabianchi kusaidia wananchi wa Zanzibar**

**MHE. AMINA DAUDI HASSAN** aliuliza:-

Je, kuna mpango gani wa kutenga fedha ya mabadiliko ya tabianchi kusaidia wananchi wenye visima vya maji chumvi Zanzibar?

**MWENYEKITI:**

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Amina Daudi Hassan, Mbunge wa Viti Maalum, kutoka Mkoa wa Kusini Unguja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikishirikiana na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, inatekeleza miradi mbali mbali ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kwa pande mbili za Muungano ambayo inahusika na uchimbaji wa visima. Kwa upande wa Zanzibar, Mradi wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi kwa Kutumia Mifumo ya Ikolojia Vijijini *(EBBAR)* umechimba visima sita katika Wilaya ya Kaskazini "A". Pia, Mradi wa Kurejesha Ardhi Iliyoharibika na Kuongeza Usalama wa Chakula *(LDFS)* umechimba visima viwili katika Shehia ya Maziwa Ng'ombe na Shehia ya Kiuyu katika Kisiwa cha Pemba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Amina, swali la nyongeza.

**MHE. AMINA DAUDI HASSAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Swali la kwanza; licha ya majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, je, Serikali ina mpango gani wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi katika fukwe za hindi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikishirikiana na Serikali ya Zanzibar, je, haioni haja ya kujenga kuta kandokando ya bahari ili kuzuia uendelezaji wa athari za mabadiliko ya tabianchi? Mfano kama Nungwi, Jambiani, Paje na vijiji vingine vyote vyenye fukwe ya bahari? Ahsante .

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa na mpango kabambe na mipango mingi ya kuhakikisha kwamba, tunakabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi, hasa katika maeneo ya fukwe, ama maeneo haya ya ukanda wa Bahari, hasa katika Bahari ya Hindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, tumekuwa tunahamasisha jamii ambazo zinaishi humu pembezoni mwa bahari, hasa maeneo ya ufukwe, kwanza kurejesha ama kupanda mikoko ambayo ilikuwepo lakini imekatwa, lakini hatua nyingine ambayo tumeichukua kama sehemu ya mpango kabambe wa Serikali ni kuendelea kuwaambia wananchi kwamba, wasiendelee kutupa taka hatarishi, lakini vilevile kufanya shughuli za uchimbaji wa mchanga katika maeneo haya ya fukwe. Kikubwa zaidi tumekuwa tuykiwaeleza shughuli za uvuvi, lakini pia shughuli za ulimaji ama uvunaji wa mwani zisiharibu fukwe zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa suala la ujenzi wa kingo ama kuta za kuzuia maji ya bahari au maji ya chumvi yasiingie maeneo mengine, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tayari imeshaanza ujenzi wa ukuta kwa upande wa Tanzania Bara katika Mkoa wa Mtwara katika maeneo ya Mikindani, lakini kwa upande wa Kusini Pemba katika eneo linaitwa Sepwese, tayari tumeshaanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa maeneo ya Paje, Jambiani, Bwejuu, Nungwi na maeneo mengine, cha kwanza tunaenda kufanya utafiti kujua ni aina gani ya ukuta ambao unatakiwa, lakini tumwambie Mheshimiwa tunakwenda kutafuta fedha, ili tuone namna ambavyo tunakwenda kujenga hizi kuta ambazo zita-*control* uingiaji wa maji na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Fatma Toufiq, swali la nyongeza.

**MHE. FATMA TOUFIQ:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza. Waathirika wakuu wa suala zima la tabianchi ni wanawake na hasa wale wanawake wanaoishi maeneo ya pembezoni. Nini mkakati wa Serikali wa kuwa na program maalum kwa ajili ya hawa wanawake wa pembezoni waweze kupata mafunzo kukabiliana na hali ya tabianchi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Toufiq, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, tayari alichokiomba Mheshimiwa Toufiq tumeshakianza. Tumeanza na Mkoa wa Kaskazini Unguja, tayari kule viko vikundi vya akinamama vya ujasiriamali katika Jimbo la Chaani. Tumeshaanza hiyo program ya kuwapa taaluma akinamama ili

waweze kujua namna bora ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Haya tumeyafanya kwa sababu, tumeona baadhi ya shughuli za uvuvi, lakini hata shughuli za ulimaji na uvunaji wa mwani, wengi wao tumegundua ni akinamama. Kwa hiyo, tumeona tuendelee kuwapa hii elimu ili waweze kuepukana na hizi athari za mabadiliko ya tabia nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri nakushukuru sana kwa majibu ya Waheshimiwa Wabunge. Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya, Mbunge wa Manyoni Mashariki, sasa aulize swali lake.

Na. 391

**Ujenzi wa Kampasi ya Chuo Kikuu cha Mzumbe, Singida**

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga *campus* ya Chuo Kikuu Mzumbe katika Mkoa wa Singida?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Elimu, Mheshimiwa Kipanga, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya, Mbunge wa Manyoni Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea na mpango wa kupeleka huduma ya elimu ya juu katika mikoa isiyokuwa na Chuo Kikuu au Taasisi ya Elimu ya Juu ukiwemo Mkoa wa Singida. Kwa sasa Serikali kupitia Mradi wa *Higher Education for Economics Transformation (HEET)* imetenga jumla ya Dola za Kimarekani milioni nane kwa ajili ya upanuzi na ukarabati wa Kampasi ya

Taasisi ya Uhasibu Tanzania *(TIA)* katika Mkoa wa Singida. Maandalizi ya shughuli za ujenzi yameshaanza ambapo hadidu za rejea za kumpata Mshauri Elekezi na Mkandarasi, Michoro na Mpango kabambe wa Ripoti ya Tathmini ya mazingira na Jamii *(Environmental and Social Impact Assessment)* vimeshaanza kuandaliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jitihada hizo za kusogeza elimu ya juu kwenda mikoa ambayo haina taasisi hizo, Chuo Kikuu cha Mzumbe pia kupitia mradi wa *HEET* kimepangiwa kujenga kampasi mpya katika Mkoa wa Tanga katika Wilaya ya Mkinga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Chaya, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza; katika Wilaya ya Manyoni tuna uhitaji mkubwa sana wa chuo ambacho kinaweza kikatoa elimu ya afya katika ngazi ya cheti na diploma. Je, nini mpango wa Serikali kuhakikisha kwamba, sasa wanasogeza kampasi ya chuo cha afya cha ngazi ya *certificate and diploma* katika Wilaya ya Manyoni?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kwa kuwa, kuna uhitaji mkubwa sana wa Wahadhiri katika vyuo vikuu vyetu na vyuo vya kati; na kwa kuwa, hivi karibuni Serikali imekuwa ikitumia mfumo wa usaili kuwapata Wahadhiri, hususan *Tutorial Assistants,* je, Serikali haioni haja ya kurudi kwenye mfumo wa zamani ambapo vijana waliokuwa wakipata *first class* walikuwa wakibakizwa vyuoni na kuendelezwa? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dkt. Chaya, Mbunge wa Manyoni Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza na jambo la kwanza, swali lake la kwanza analozungumzia suala la chuo cha afya. Naomba tuubebe ushauri wake tuweze kuangalia namna gani ya kufanya upande wa hivi vyuo vya afya, tukishirikiana na wenzetu wa Wizara ya Afya au na taasisi nyingine binafsi, tuweze kuangalia namna bora ya kufanya katika upatikanaji wa vyuo hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwondoe wasiwasi Mheshimiwa Dkt. Chaya, pale katika jimbo lake katika wilaya yake tayari sisi kama Wizara ya Elimu, kama Serikali, tumeshapeleka fedha kwa ajili ya ujenzi wa chuo cha *VETA* ambavyo huenda baadaye tukatohoa tu na hizo kada za afya vilevile zikaweza kufundishwa katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili, anazungumzia suala la wahadhiri. Ni kweli zamani tulikuwa na utaratibu katika vyuo vikuu, wale wanafunzi wanaofanya vizuri huwa wanabaki palepale chuoni kwa ajili ya kuwa Wahadhiri. Utaratibu huu hapa katikati ulisitishwa ili kuweza kuweka ushindani kwanza, lakini vilevile kuondoa upendeleo kwa namna moja au nyingine. Kwa hiyo, mamlaka yale sasa yalikasimiwa au yalipelekwa moja kwa moja kwenye Tume ya Utumishi wa Umma kwa lengo la kutoa vibali vya kuajiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunapokea ushauri huo hata wakati tunakusanya maoni wakati wa mapitio ya mitaala suala hili lilizungumzwa sana. Kwa hiyo, tuachie kama Serikali twende tukalifanyie kazi, ili tuweze kuangalia namna bora ya kurudisha utaratibu ambao utakuwa mzuri na kutoa fursa kwa kila Mtanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Deo Mwanyika, swali la nyongeza.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niulize swali dogo la

nyongeza. Mkoa wa Njombe ndio Mkoa ambao hauna chuo kikuu wala chuo cha juu na Mheshimiwa Rais alipotembelea Mkoa wa Njombe tarehe 9 Agosti, 2022 alipokea ombi la wazee wa Njombe kuhusu kujengewa chuo kikuu katika Mkoa wa Njombe na Mji wa Njombe. Je, Serikali itaanza lini mchakato wa kuhakikisha kwamba na sisi tunapata chuo kikuu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Mwanyika, Mbunge wa Njombe Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni kweli Mheshimiwa Rais alifanya ziara katika Mkoa wa Njombe, tarehe 9 Agosti, 2022 na miongoni mwa ahadi alizozitoa ni ujenzi wa kampasi mojawapo ya chuo kikuu pale Njombe, ingawa katika mgawanyo huu wa miradi ya *HEET* katika mikoa ambayo haitapata fursa katika awamu hii ya kwanza ni Mkoa wa Njombe. Kwa vile tayari Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, alishatoa hiyo ahadi na sisi kama Serikali ahadi hii ya Mheshimiwa Rais tunaendelea kuifanyia kazi, hivyo, nimwondoe wasiwasi Mheshimiwa Mwanyika na wananchi wa Mkoa wa Njombe, tuko njiani kuja Njombe na tutahakikisha kwamba, tunaleta taasisi ya elimu ya juu katika Mkoa wa Njombe.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru sana kwa kujibu maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mheshimiwa Nusrat Shaabani Hanje, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 392

**Kanuni ya Kimtandao ya *Network Neutrality Principle***

**MHE. NUSRAT S. HANJE** aliuliza:-

Je, kwa namna gani Serikali inatekeleza Kanuni ya Kimtandao ya *Network Neutrality* katika utoaji na upatikanaji wa huduma za jamii?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri Wizara ya Habari, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Nusrat Shaaban Hanje, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya *Network Neutrality* ni hali ya kuweka usawa katika huduma zote zinazopatikana kwenye mtandao wa intaneti bila kuathiri kasi, gharama wala upendeleo wa tovuti fulani au maudhui ya aina fulani mtandaoni. Serikali inasimamia Sekta ya Mawasiliano kwa kuzingatia kikamilifu Kanuni ya Kimtandao ya *Network Neutrality* ambapo mtoa huduma yeyote wa mtandao wa intaneti anaruhusiwa kutoa huduma ya mtandao kwa kuzingatia taratibu zilizowekwa. Aidha, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania *(TCRA)* imeweka utaratibu wa kuwezesha watoa huduma kutoza gharama za *data* bila kujali ni ya matumizi ya mitandao gani ya kijamii, tovuti au programu tumizi mbalimbali.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nusrat, swali la nyongeza.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa kuwa, tunafahamu kwamba, Serikali inatumia *e-Government* na TEHAMA kwa ajili ya kutoa huduma za kijamii kiserikali, lakini mara kadhaa wananchi wamekuwa wakikosa huduma kwenye ofisi za Serikali kwa sababu ya kwamba, mtandao uko chini. Ni kwa nini sasa Serikali isije na mkakati mahususi wa kuhakikisha kwamba, utolewaji wa huduma kwa kutumia *e-Government* na TEHAMA kwenye ofisi za Serikali unatengenezewa upekee na kuhakikisha

kwamba, wananchi hawakosi huduma kwa sababu za mtandao uko chini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kwa kuwa, tumekuwa tunaona Serikali inafanya udhibiti wa mitandao, hususan katika kipindi cha uchaguzi, lakini pia tunafahamu kwamba, sasa hivi Serikali inachagiza uchumi wa kidijitali na wananchi wengi wamekuwa wakitumia mitandao ya kijamii kwa ajili ya kuhakikisha wanafanya shughuli zao za kiuchumi. Ni kwa nini sasa Serikali isione umuhimu wa kuhakikisha kwamba, majukwaa haya ya mitandaoni hayakosi mawasiliano, hususan kipindi ambacho Serikali inafanya udhibiti wa kasi hususan kipindi cha uchaguzi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA WIZARA YA WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Nusrat Shaaban Hanje, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kwanza kuhusu matumizi ya *internet* katika ofisi za Serikali. Serikali imewekeza katika miundombinu, Ujenzi wa Mkongo wa Taifa. Katika ujenzi huo tuna *capacity* mbalimbali, tuna kitu kinaitwa *Synchronize Transport Module* maana yake *STMA*. Hizi *STM* kuna 1, 2 na 3; 1, 2, 3, 4 maana yake kwamba, ni *capacity* na *speed* ambapo kwa mfano *STM 1* ambayo ina *MBPS 155* maana yake hiyo ni *capacity* yake, lakini kuna ya 491, kuna ya 2488, lakini sasa niombe na kuwashauri wataalam wa *eGA* na wataalam ambao wako katika Wizara mbalimbali, wafanye tathmini ya mahitaji halisi ili waweze kujua kwamba, wanaweza wakapata *capacity* ipi itakayoendana na *traffic* wakati wanapokuwa wanahudumia wananchi wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipengele cha pili cha udhibiti. Kuna Profesa mmoja anaitwa Tim Wu kutoka *Colombia Law School* alisema kwamba, ili ubunifu uendelee na ili tuwe na *freedom* ya *access to information* na ili *business* na *innovation* zizidi kukua ni lazima tusiweke *restrictions* katika aina gani ya mtandao tuweze ku-*access* na aina gani ya *contents* tuweze ku-*access.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Serikali yetu kupitia *TCRA* tumeweka utaratibu kwa watoa huduma kuhakikisha kwamba hakuna *restriction* ya aina ya *content* ambayo mwananchi anaweza kui-*access.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Soud Mohammed Jumah, Mbunge wa Donge, sasa aulize swali lake.

Na. 393

**Kudhibiti mifugo Bonde la Ihefu na Mto Kilombero**

**MHE. SOUD MOHAMMED JUMAH** aliuliza: -

Je, kuna mikakati gani ya kudhibiti mifugo katika Bonde la Ihefu na Mto Kilombero?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Silinde, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa niaba ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Soud Mohammed Jumah, Mbunge wa Jimbo la Donge, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwezi Oktoba, 2022 Serikali kupitia Kamati ya Mawaziri Nane wa Kisekta inayoshughulikia migogoro ya ardhi katika vijiji 975 nchini, ilitoa tamko kuhusu utatuzi wa mgogoro wa mpaka kati ya Hifadhi ya Taifa Ruaha na baadhi ya vijiji vya Wilaya za Mbarali na Chunya. Ili kudhibiti mifugo katika Bonde la Ihefu na Mto Kilombero, jumla ya vijiji 16 vimeandaa

mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji na kutenga maeneo kwa ajili ya malisho ili kuwezesha ufugaji katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kudhibiti mifugo kutoka katika maeneo mengine kwenda kwenye Bonde la Mto Kilombero kutafuta malisho na maji katika mwaka wa fedha 2022/2023 Serikali inajenga mabwawa ya maji kwa ajili ya mifugo katika Halmashauri za *Morogoro DC* Kijiji cha Kongwa na *Kibaha DC* Kijiji cha Viyenze. Aidha, katika mwaka wa fedha 2022/2023, Serikali imeanzisha mashamba darasa 100 ya malisho katika Halmashauri 44 zikiwemo Halmashauri zinazopakana na Bonde la Ihefu na Mto Kilombero ili wafugaji waweze kujifunza kuzalisha malisho na hivyo kutulia katika maeneo yao ya ufugaji.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Soud, swali la nyongeza.

**MHE. SOUD MOHAMMED JUMAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, ili kuzifanya juhudi hizi ambazo Mheshimiwa Waziri amezieleza hapa kuwa endelevu, Je, hatuoni haja ya kuja na mkakati wa pamoja ambao utazishirikisha sekta za maliasili, kilimo, mifugo pamoja na sekta ya maji ili kulimaliza kabisa tatizo hili ambalo ni la muda mrefu?

Swali la pili, kwa kuwa kuna *good practices* kwa wenzetu Uganda ambao wanawashurutisha wafugaji wenye mifugo wengi kutenga maeneo ya malisho toshelezi kwa ajili ya mifugo yao. Je, Serikali haioni haja ya kuiga mfano huu mzuri ili kuweza kupambana na changamoto hii ambayo inaleta migogoro kati ya wakulima, watu wa maliasili pamoja na mifugo? Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza ni kwamba mkakati upo wa Wizara zote ambazo Mheshimiwa Mbunge amezitaja, Wizara ya Maliasili na Utalii, Wizara ya Mifugo na Uvuvi pamoja na Wizara ya

Maji, tukiungana na watu wa Wizara ya Ardhi, kuandaa mipango endelevu kwa ajili ya kusiadia wafugaji wetu ili kuondoa hii migogoro ambayo imejitokeza. Kwa hiyo, jambo hilo lipo Mheshimiwa Mbunge, na tutaendelea kuliboresha zaidi ili tuondoe hii dhana ambayo imekuwa ikijengeka kila wakati ya migogoro inayotokana na wafugaji pamoja na wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kutenga maeneo, hilo tayari ni agizo ambalo Serikali ilishalitoa katika Halmashauri zote nchini kutenga maeneo kwa ajili ya wafugaji, hususan wale wenye mifugo wengi ili kuondoa hii kuhamahama kutafuta malisho pamoja na maji. Utaratibu huu kwanza utaboresha mifugo wetu wa kisasa na kuongeza ubora wa malisho na mifugo ambao tunao. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Francis Ndulane, swali la nyongeza.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnamo mwaka 2006 Serikali iliridhia mifugo kuhamishwa kutoka Bonde la Ihefu kupelekwa Mkoani Lindi, hivi ninavyozungumza katika Wilaya za Liwale, Kilwa na Nachingwea kuna mafuriko makubwa ya mifugo na hivyo kusababisha kuwa na uhaba wa malisho, maji pamoja na huduma nyingine za mifugo.

Je, kuna utaratibu gani ambao Serikali imeupanga kwa ajili ya kidhibiti mifugo hii? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Jambo la kwanza ambalo Mheshimiwa Mbunge amelieleza hapa lina ukweli kwa sababu idadi kubwa ya mifugo sasa hivi wamekuwa wakielekea upande wa kusini, ndiyo maana moja ya mipango mikakati ambayo Wizara ya Mifugo na Uvuvi tunayo sasa hivi ni kuongeza maeneo ya malisho, tunapeleka mabwawa ili ku-*control* sasa ule ufugaji holela. Kwa

hiyo, jambo hilo tumelipokea kwa umuhimu mkubwa na tutaleta mpango kazi kwa ajili ya maeneo hayo ambayo Mheshimiwa Mbunge ameyaainisha, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Wizara ya Maji Mheshimiwa Jonas William Mbunda, Mbunge wa Mbinga Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 394

**Hitaji la maji Vijiji vya Mbinga Mjini**

**MHE. JONAS W. MBUNDA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itajenga miradi ya maji katika Vijiji vya Mateka, Tukuzi, Kitelea na Sepukila Wilayani Mbinga?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa *Eng.* Maryprisca Mahundi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jonas William Mbunda, Mbunge wa Jimbo la Mbinga Mjini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kuboresha hali ya upatikanaji wa huduma ya maji Wilayani Mbinga ambapo kwa Vijiji vya Kitelea na Sepukila utekelezaji wa miradi ya maji unaendelea na utakamilika mwezi Juni, 2023. Aidha, kwa Kijiji cha Tukuzi usanifu umekamilika na kwa Kijiji cha Mateka usanifu utafanyika katika mwaka wa fedha 2023/2024 na ujenzi wa miradi ya maji kwenye vijiji hivyo utafanyika katika mwaka wa fedha 2023/2024.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jonas, swali la nyongeza.

**MHE. JONAS W. MBUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie nafasi hii kuishukuru Serikali kwa kuanza kutekeleza miradi katika Vijiji vya Sepukila na Kitelea pia kuandaa kutekeleza miradi ya maji katika Vijiji vya Tukuzi na Mateka. Vijiji vya Nzokai, Kilimani, Rudisha, Mikolola na Njomlole vina changamoto kubwa ya upatikanaji wa maji. Nataka nijue sasa ni lini Serikali itaandaa fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi kwenye maeneo haya. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Jonas William Mbunda, Mbunge wa Jimbo la Mbinga Mjini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nipokee shukrani zake kwa Serikali, lakini zote ni jitihada zake za ufuatiliaji wa karibu na ushirikiano wake mzuri ndani ya Wizara yetu ta Maji. Mheshimiwa Mbunge, nawe tunakupongeza katika hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijiji hivi alivyovitaja Mheshimiwa Mbunge tayari vipo katika hatua mbalimbali za kuona kwamba na vyenyewe tunavifikishia maji safi na salama bombani. Hivyo, katika mwaka ujao wa fedha, vijiji hivi navyo tutavigusa katika namna ya kuona huduma inapelekwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Getere, swali la nyongeza.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naomba kujua katika bajeti ya mwaka 2022/2023, Serikali iliahidi kupeleka maji ya Ziwa Victoria katika Jimbo la Bunda. Je, ni lini ahadi hii itatimizwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, Mbunge wa Jimbo la Bunda, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tayari mradi ambao unatarajiwa kupelekwa Bunda umefikia hatua nzuri, Mhandisi

Mshauri yuko *site*. Mheshimiwa Mbunge nakupongeza kwa kufuatilia, kama tulivyoongea wiki iliyopita ofisini, tayari Mhandisi Mshauri anakamilisha na wiki hii tunamtarajia arejeshe taarifa ya kuona tathmini ya thamani ya mradi ambao tutakwenda kuujenga.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Cecil Mwambe, swali la nyongeza.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Ninapenda kufahamu kwenye Vijiji vya Mpanyani Shule ya Sekondari, Huria, Chiroro, Masiku pamoja na Namichi tayari pameshachimbwa visima virefu. Je, ni lini sasa Serikali iko tayari kuweka pampu kwenye maeneo haya ili wananchi waweze kupata maji?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Cecil David Mwambe, Mbunge wa Jimbo la Ndanda, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijiji hivi alivyovitaja vyote tunatarajia viweze kuendelezwa visima vilivyochimbwa. Tumshukuru Mheshimiwa Rais tumeendelea kupata fedha za *P4R,* Mikoa yote itapelekwa fedha, kwa hiyo tunatarajia sasa *distribution* itakwenda kufanyika na wananchi wataanza kunufaika na visima vilivyochimbwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Pallangyo, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami niulize swali la nyongeza. Mradi mkubwa wa maji uliogharimu takribani shilingiza bilioni 520 za Kitanzania kule Arusha sasa hivi karibu unamalizika. Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga miundombinu ya kusambaza maji katika vijiji ambavyo bomba kuu limepita?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. John Danielson Pallangyo, Mbunge wa Jimbo la Arumeru Mashariki, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli mradi huu tuko mwishoni kabisa na tayari vijiji vingi vimenufaika, tayari maji haya kutoka kwenye mradi yameingizwa kwenye laini ambazo zina-*exist*. Vilevile maeneo yote ya vijiji hivyo alivyovitaja na vingine vyote ambavyo vimepitiwa na bomba kuu vinakwenda kupata huduma ya maji safi na salama.

**MWENYEKITI:** Wizara hiyohiyo, Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 395

**Uhitaji wa maji katika Mji Mdogo wa Gairo**

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA** aliuliza: -

Je, ni lini wananchi wa Mji Mdogo Gairo watapata maji ya kutosha?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua tatizo la maji linaloukabili Mji wa Gairo na jitihada zinaendelea kuchukuliwa ili kupunguza adha ya maji kwa wakazi wa Mji huo. Jitihada zinazofanyika ni pamoja na uchimbaji wa visima virefu viwili na

sasa mkandarasi yupo eneo la mradi anaendelea na kazi. Vilevile, Serikali itafanya ukarabati wa mradi wa maji ya mserereko Gairo, Mkandarasi ameajiriwa na kazi inayoendelea ni mapitio ya mradi na ujenzi utaanza mwezi Juni, 2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa muda mrefu ni kutumia chanzo cha Mto Chagongwe utakaohudumia wananchi wa Mji wa Gairo na kwa sasa Wizara inaendelea kufanya usanifu na ujenzi utafanyika katika Mwaka wa Fedha 2023/2024.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naishukuru Serikali kwa majibu mazuri, hasa kwa mradi wa Chagongwe kusikia kuwa utaanza. Licha ya hivyo, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata 29 za Manispaa ya Morogoro zinapata maji ya mgao. Je, kuna mkakati gani wa kupata maji safi na salama kila siku kwenye Kata hizo 29 za Manispaa ya Morogoro? *(Makofi)*

Swali la pili, mradi wa Magadu ambao upo kwenye Manispaa ya Morogoro umechukua muda mrefu na haujakamilika; je, ni lini utakamilika na kuanza kutoa maji kwa wananchi kwenye Kata hizo zinazozunguka? Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, kwenye maeneo yote ya Mji wa Morogoro tuna mradi mkubwa wa *AFD* ambao tunatarajia ukaongeze uzalishaji wa maji na tatizo hili la mgao mkali wa maji pale Morogoro tunatarajia litapungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile mradi wa Magadu tayari tumeutekeleza kwa asilimia 90, Mheshimiwa Mbunge anafahamu tulishaongea pamoja hili na tumefuatilia kwa pamoja Wakandarasi wanaendelea na kazi na tayari Wizara tumeshapeleka fedha, tunatarajia kufika mwezi Juni huu mradi wa Magadu nao uanze kutoa huduma kwa wananchi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shally Raymond swali la nyongeza.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilio cha maji safi na salama Tanzania ni kama wimbo wa Taifa na wanaoteseka zaidi ni wanawake. Sasa hivi tunavyoongea ni masika na maji yanapotea na hakuna kinachoendelea kutoka Serikalini.

Je, ni lini sasa Serikali itatumia kuvuna maji haya ya mvua kuwaponya wanawake wa Makanya, Hedaru, Hundugai, Ngoyoni na Holili kule Kilimanjaro? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani, sijamuelewa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shally, swali halijasikika vizuri naomba ulirudie kwa ufupi.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa ufupi tunavyoongea hapa ni masika na maji yanapotea yanarudi baharini na wanaoteseka kutafuta maji safi na salama kwa familia ni wanawake wa Tanzania, miaka nenda rudi kimekuwa ni kilio chao kupatiwa maji safi na salama.

Je, ni lini Serikali itatumia maji haya ya mvua yanayoharibu barabara na miundombinu kurudi baharini, kuleta mradi mkubwa wa kukinga maji na kuwaponya wanawake hawa wa Ngoyoni,

Hedaru, Makanya kule Same mpaka wale wa tambarare yote ya Mkoa wa Kilimanjaro? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Shally Josepha Raymond, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli ni tabia ya maji ya mvua kupotea, lakini sasa hivi Wizara tumejipanga kujenga mabwawa maeneo yote ambayo yamekuwa na mafuriko na maji yanapotea kuelekea baharini. Tutachimba mabwawa Mheshimiwa Mbunge na tayari mitambo tunayo. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais, Mama Samia Suluhu Hassan kwa kuruhusu fedha nyingi kutumika kuleta mitambo mikubwa mitano ya kuchimbia mabwawa.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Yahya Ally Mhata, Mbunge wa Nanyumbu, sasa aulize swali lake.

Na. 396

**Ujenzi wa Barabara ya Mangaka hadi Morogoro**

**MHE. YAHYA A. MHATA** aliuliza: -

Je, lini ujenzi wa barabara ya Mangaka hadi Morogoro kupitia Mbuga ya Selous utaanza kwa kiwango cha lami?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Yahya Ally Mhata, Mbunge wa Nanyumbu, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imepanga kuunganisha Mikoa ya Mtwara na Morogoro kwa barabara ya kutoka Masasi – Nachingwea – Liwale hadi Mahenge Mkoani Morogoro. Sehemu ya kutoka Masasi – Nachingwea – Liwale yenye urefu wa kilometa 175 itajengwa kwa utaratibu wa *EPC + F*. Kutoka Liwale – Mahenge kupitia Hifadhi ya Mbuga ya Selous Serikali imepanga kuanza kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina katika mwaka wa fedha 2023/2024. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Yahya Mhata, swali la nyongeza.

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa masikitiko makubwa, Serikali inaniletea majibu siyo sahihi. Barabara niliyouliza mimi ni ya kutoka Mangaka – Nachingwea – Liwale hadi Mahenge, iko ndani ya Jimbo langu la Nanyumbu. Napatiwa majibu ya Wilaya nyingine ambayo mimi sijauliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Serikali iko tayari kurudi ikajipange upya iniletee majibu sahihi ya swali langu? Hilo la kwanza.

Swali la pili, barabara ninayoiuliza mimi ni ahadi ya Mheshimiwa Rais, Mama Samia Suluhu Hassan, alipokuja ndani ya Jimbo langu mwezi Oktoba, 2020. Je, Serikali inatuambia nini juu ya ahadi hii?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Yahya Ally Mhata, Mbunge wa Nanyumbu, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba barabara aliyoisema ya kutoka Mangaka – Kilimarondo ambayo inaunganisha na Mkoa wa Morogoro, sehemu ndogo inahudumiwa na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, lakini sehemu kubwa inahudumiwa na wenzetu wa barabara za vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakubaliana naye kwamba pia yalikuwa ni maelekezo ya viongozi wa Kitaifa kwamba barabara hiyo ijengwe. Kitu cha kwanza ambacho tutaifanya ni kuipandisha hadhi ile barabara – Mheshimiwa Mbunge atakubaliana nami, kuipandisha hadhi ije *TANROADS* tufanye upembuzi yakinifu na usanifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilichosema kuhusu barabara niliyoitaja, ni barabara ambazo zinakwenda sambamba, ukitoka Masasi – Nachingwea kwenda Liwale hii barabara inakwenda sambamba na barabara ya kutoka Mangaka – Kilimarondo kwenda Liwale. Sasa hiyo kwa kuwa ni ahadi ya Mheshimiwa Rais, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba itapandishwa hadhi halafu itakuja *TANROADS* tutafanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ili kuijenga hiyo barabara. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Aida, swali la nyongeza.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya kutoka Sumbawanga – Mpanda imetengenezwa kimebakia kipande kidogo cha kutoka Chala – Mpalamawe.

Je, ni lini hiki kipande kitajengwa kwa kiwango cha lami?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge wa Nkasi Kaskazini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kipande hiki alichokisema cha Chala – Mpalamawe, kimsingi ndiyo barabara kuu, lakini kwa sababu Makao Makuu ya Wilaya ya Nkasi yako nje ya barabara kuu, Serikali iliona ni busara barabara ya lami badala ya

kujengwa huko porini ipite Makao Makuu ya Wilaya ambayo ndiyo inaunganisha pale Mpalamawe kwenda Mpanda. Mpango ni kuja kuijenga hii barabara kwa kiwango cha lami ili kukamilisha hiyo barabara kuu pia, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nawaona mko wengi, na muda wetu unakwisha. Tunaendelea Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mheshimiwa Ameir Abdallah Ameir Mbunge wa kutoka Baraza la Wawakilishi aulize swali lake.

Na. 397

**Balozi kutumia fursa ya kukua kwa lugha ya Kiswahili kutafuta ajira kwa Watanzania**

**MHE. AMEIR ABDALLAH AMEIR** aliuliza:-

Je, Balozi za Tanzania zinatumia vipi fursa ya kukua kwa Kiswahili duniani kutafuta ajira kwa Watanzania?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa niaba yake Waziri wa Ardhi, Mheshimiwa Pinda, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ameir Abdallah Ameir, Mbunge kutoka Baraza la Wawakilishi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia Balozi zetu nje ya nchi zimekuwa zikichukua hatua mbalimbali katika kukuza Kiswahili na kuchangia ongezeko la ajira kwa Watanzania ikiwemo kuanzisha programu za kufundisha, kutafsiri na kufanya ukalimani wa Kiswahili duniani, hatua ambayo inatoa ajira kwa Watanzania. Jumla ya Balozi 13 zimeweza kuanzisha madarasa, vituo na *clubs* za Kiswahili. Aidha, zaidi ya Watanzania 95

wamepata ajira katika maeneo hayo. Vilevile, vyuo na vituo binafsi zaidi ya 150 vinafundisha Kiswahili duniani. Kwa sasa, Baraza la Kiswahili Tanzania (BAKITA) limepewa kazi ya kufundisha walimu 10 wa *Diaspora* katika Ubalozi wetu wa Abu Dhabi ambapo ni uhitaji wa walimu kwenda kufundisha Kiswahili katika Umoja wa Falme za Kiarabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya Balozi zetu zipo katika mazungumzo na vyuo vikuu kwenye maeneo yote ya uwakilishi ili Lugha ya Kiswahili iweze kujumuishwa katika mitaala ya vyuo hivyo ikiwa ni pamoja na kupata Wahadhiri wa Kiswahili kutoka Tanzania. Vyuo hivyo ni pamoja na Chuo Kikuu cha Kuwait, Chuo Kikuu cha *Holon Institute of Technology* nchini Israel na Chuo Kikuu cha Buraimi, nchini Oman, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ameir Abdallah Ameir, swali la nyongeza.

**MHE. AMEIR ABDALLAH AMEIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza. Tumeshuhudia hivi karibuni nchi ya Afrika Kusini wametangaza uhitaji wa walimu wa lugha ya Kiswahili katika nchi hiyo; je, Serikali sasa inatumiaje fursa hii katika kuhakikisha kwamba walimu wetu waliobobea katika lugha ya Kiswahili wanafaidika na fursa hii hususan walimu kutoka Tanzania Bara na Tanzania Visiwani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Miongoni mwa Balozi ambazo zimekuwa zikifanya vizuri katika kuikuza lugha ya Kiswahili ni Ubalozi wa Tanzania nchini Italy, tayari wameshasajiisha Vyuo Vikuu vitatu ndani ya nchi hiyo, vinafundisha lugha ya Kiswahili, kikiwemo Chuo Kikuu cha Torino, Chuo Kikuu cha Roma na Chuo Kikuu cha Napoli. Vilevile nauliza swali; je, Serikali haioni haja kwamba Balozi zetu ambazo zinatuwakilisha katika nchi mbalimbali ziweze kufuata *modality* hii ya Ubalozi wa *Italy* nchini Tanzania, ambapo kwa muda mfupi tu tunaweza tukafaidika kwa hali ya juu? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuna uhitaji wa Serikali ya Afrika Kusini kuanza kufundisha Kiswahili. Hizi ni juhudi za Serikali vile vile kwa ushirikiano na Serikali ya Afrika Kusini. Kama nilivyoeleza katika jibu la msingi, kimsingi walimu wetu wamenufaika na hizi fursa na wanapelekwa kwa kasi sana kwa sababu ni matangazo yanakuwa ya hadhara kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Balozi zetu kuiga mfano wa Italy, tumepokea ushauri wa Mheshimiwa Mbunge na tunasisitiza kabisa kabisa. Yapo mambo mengi ambayo katika hali ya kawaida sisi kama Watanzania tunatakiwa kujivunia, Kiswahili chetu kinauzika duniani kote. Tuna redio zaidi ya 13 nje ya Tanzania ambazo zinatumia Kiswahili. Kwa mfano, tuna Idhaa ya Kiswahili ya *BBC,* tuna Sauti ya Amerika, tuna Redio Japani, Tuna Sauti ya Ujerumani, tuna Sauti ya Umoja wa Mataifa, tuna Redio China na nchi zetu zote hizi za Afrika Mashariki zote zinatumia Kiswahili katika baadhi ya matangazo yake. Kwa hiyo, ni sisi Watanzania kujitangaza katika mazingira yote tunapokuwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naziomba Balozi zetu huko nje zianzishe majukwaa mbalimbali yakiwepo matamasha ya Kiswahili katika nchi wanazotuwakilisha ili kukitangaza Kiswahili katika uhalisia wake.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu. Tunaenda Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Profesa Patrick Alois Ndakidemi, Mbunge wa Moshi Vijijini, sasa aulize swali lake.

Na. 398

**Kurejesha ruzuku za pembejeo kwa wakulima wa kahawa**

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI** aliuliza:-

Je, lini Serikali itarejesha utoaji ruzuku ya pembejeo za dawa kwa Wakulima wa Kahawa ili wazalishe zaidi kama awali?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Mavunde, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Profesa Patrick Alois Ndakidemi, Mbunge wa Moshi Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi ya viuatilifu katika zao la kahawa ni njia ya udhibiti wa visumbufu vya zao la kahawa ili kulinda ubora wa mazao yanayozalishwa dhidi ya magonjwa ya Kutu ya Majani na Chole Buni. Aidha, utafiti wa zao la kahawa umebaini kuwa upandaji wa miche bora ya kahawa ni njia pekee inayowezesha kuzalisha mazao yenye tija nzuri, ukinzani dhidi ya wadudu waharibifu na magonjwa ya zao la kahawa na kupunguza matumizi ya viuatilifu kwenye kahawa kwa takriban asilimia 40.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa Serikali haina utaratibu wa kutoa ruzuku ya viuatilifu vya kahawa bali kupitia Taasisi ya Utafiti wa Kahawa *(TaCRI)* na Bodi ya Kahawa Tanzania imeendelea kuzalisha, kusambaza na kuhamasisha wakulima kubadilisha mikahawa ya zamani kwa kupanda miche mipya ambayo ina ukinzani dhidi ya magonjwa ambapo katika kipindi cha mwaka 2019/2020 hadi 2021/2022 jumla ya miche 41,348,628 imezalishwa na kugawiwa bure kwa wakulima.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Profesa Ndakidemi, swali la nyongeza.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa fursa. Nina maswali mawili ya nyongeza. Nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali na kwamba mmeanza kugawa miche ili tuboreshe uzalishaji wa Kahawa. Kwa kuwa mmegawa miche; je, sasa Serikali ina mikakati gani ya kuboresha zile skimu za umwagiliaji za asili ili

tuweze kuongeza tija kwenye kuzalisha kahawa, kwani bila maji hata hiyo miche haitakuwa inafanya vizuri sana?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Je, Serikali ina mkakati gani wa kusindika kahawa aina ya Arabica kwa sababu kahawa hii ina soko zuri sana katika soko la Dunia na kuna teknolojia nyingi za kawaida tu ambazo zinaweza zikatumika tukapata chapa au *brand* yetu: Je, Serikali ina mkakati gani wa kutusaidia kusindika kahawa hizi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi sana.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza la kuhusu skimu za umwagiliaji wa mifereji ya asili, tunao wakandarasi ambao wako katika Mkoa wa Kilimanjaro, wanaotekeleza miradi ya umwagiliaji, wameshapata maelekezo watakwenda kukarabati na kujenga mifereji yote ya asili inayogusa jimboni kwa Mheshimiwa Ndakidemi, kwa Mheshimiwa Saashisha pamoja na kwa Mheshimiwa Dkt. Kimei.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili, Serikali inao mkakati wa dhati kabisa kuhakikisha kwamba tunaendelea kusindika kahawa yetu na tusiuze kahawa ambayo haijasindikwa. Hivi sasa Bodi ya Kahawa imeshatoa zaidi ya leseni 20 kwa ajili ya wasindikaji ili kuchochea usindikaji wa zao la kahawa na mwisho wa siku tutengeneze masoko ya uhakika. Hivi sasa tumepata nafasi kahawa yetu inauzwa sana na kupekekwa Japani ikiwa ni sehemu ya kazi nzuri ambayo imefanywa katika hatua ya awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge, kazi hii inaendelea.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu. Wizara ya Afya, Mheshimiwa Benardeta Kasabago Mushashu, Mbunge wa Viti Maalum aulize swali lake.

Na. 399

**Hitaji la hospitali kubwa Kagera**

**MHE. BENARDETA K. MUSHASHU** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga hospitali kubwa katika Mkoa wa Kagera?

**MWENYEKITI:** Naibu Waziri wa Afya, Mheshimiwa Mollel, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Afya, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Bernadetha Kasabago Mushashu, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Kagera una Hospitali kubwa ya Mkoa ambapo kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Serikali imekamilisha jengo la huduma za dharura *(EMD)* ambalo limegharimu shilingi 560,000,000, jengo la uangalizi *(ICU)* lililogharimu shilingi 650,000,000, jengo la huduma za mionzi *(Radiology)* lililogharimu shilingi 237,000,000, nyumba ya mtumishi iliyogharimu shilingi 90,000,000 pamoja na ununuzi na ufungaji wa mashine ya *CT-Scan* ambayo imegharimu kiasi cha shilingi 1,810,000,000 na huduma zimeanza kutolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kupeleka fedha zaidi kwa ajili ya kuboresha miundombinu katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Kagera ikizingatia pia kuboresha eneo la majanga na magonjwa ya mlipuko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mushashu, swali la nyongeza.

**MHE. BENARDETA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu ya Naibu Waziri ninayo maswali mawili ya nyongeza. *Bukoba Government Referral Hospital* haijafikia hadhi

ya kuwa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Kagera. Hata Mheshimiwa Waziri wa Afya alisimama hapa na yeye mwenyewe akakiri kwamba ile hospitali bado haijafikia ile hadhi, na mkatuahidi kwamba mtatuletea fedha kusudi tuweze kujenga hospitali nyingine au kukarabati ile ifikie hadhi hiyo: Je, ni lini Serikali italeta fedha za kutosha kuweza kutuhakikishia kwamba wanatujengea hospitali yenye hadhi ya Rufaa ya Mkoa wa Kagera?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Mkoa wa Kagera uko mpakani na unapakana na nchi kadhaa. Kwa hiyo, yakitokea magonjwa ya mlipuko ni rahisi kuingia Mkoa wa Kagera kwa sababu magonjwa hayana mipaka. Kwa kuwa juzi juzi uliingia mgonjwa mbaya sana wa *Marburg* na mkaona Wizara na Mkoa walivyokuwa wanahangaika kutafuta mahali pa kuweka wale watu waliokuwa wamechangamana na wagonjwa, kwa sababu hakuna *isolation centers* ikabidi wawaweke mpaka kwenye mahoteli na hayo mahoteli yakafungwa yakawa hayatoi huduma kwa wakati huo: Je, ni lini sasa Serikali itaujengea Mkoa wa Kagera *Isolation center? (Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa ufatiliaje wake makini wa masuala ya afya ya Mkoa wake wa Kagera. Pia nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali itaendelea, hata mwaka huu inatarajia kupeleka zaidi ya shilingi bilioni nne kwa ajili ya kuendelea kuboresha hospitali yao ya Mkoa. Vile vile nimhakikishie kwamba hospitali ya Mkoa wa Kagera ni sawa na Hospitali ya Mkoa wa Dodoma, *level* yake ni moja, lakini tutaendelea kuwaongezea wataalam na vitu vingine ambavyo vimepungua kwenye hospitali yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili, Mheshimiwa Mushashu anazungumzia suala la ugonjwa wa *Marburg*. Nimwambie Mheshimiwa Mbunge kwamba, tumeshapata heka 90 ndani ya Mkoa wa Kagera kwa ajili ya kujenga hiyo *isolation center*. Wakati huo tunapojenga *isolation center* tunahitaji tafakuri ya kina, kwa sababu ninyi Wabunge wa Mkoa wa Kagera

mnajua kuna mwenzetu, Dkt. Mahona Ndulu wakati akihudumia wagonjwa wa *Marburg* alipata matatizo ya figo na moyo ambapo ilihitaji awepo kwenye sehemu ambazo hizo huduma zitakuwepo. Wakati tunatafakari hayo, tutaendelea kuona namna gani tutaitumia hiyo sehemu ya heka 90.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza Wabunge wa Mkoa wa Kagera kwa nia yao ya kwenda kumpongeza daktari huyo.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu. Wizara ya Nishati Mheshimiwa Kavejuru Eliadory Felix, Mbunge wa Buhigwe sasa aulize swali lake.

Na. 400

**Mradi wa umeme wa Gridi ya Taifa kutoka Nyakanazi hadi Kigoma**

**MHE. KAVEJURU E. FELIX** aliuliza:-

Je, lini mradi wa kuunganisha umeme wa Gridi ya Taifa kutoka Nyakanazi hadi Kigoma utaanza?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kavejuru Eliadory Felix, Mbunge wa Buhigwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni habari njema kwamba Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, tayari imeunganisha Mkoa wa Kigoma katika Gridi ya Taifa tangu mwezi Septemba, 2022 kwa kuanzia Wilaya za Kakonko, Kibondo, Kasulu na Buhigwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hatua nyingine kubwa zaidi, hadi kufika mwezi Aprili, 2023, Mkandarasi aitwaye *TATA Projects*

*Ltd*. amefikia 53% ya utekelezaji wa mradi wa kuunganisha Mkoa wa Kigoma katika Gridi ya Taifa kwa kujenga njia ya kusafirisha umeme yenye msongo wa kilovolti 400 toka Nyakanazi (Biharamulo) mpaka Kidahwe (Kigoma) kwa urefu wa kilometa 280. Mradi huu unatarajiwa kukamilika mwezi Januari, 2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ya ziada ambayo Serikali inaitafutia fedha ni njia ya kusafirisha umeme (kilovoti 220) ya kutoka Kasulu hadi Buhigwe pamoja na Kituo cha Kupooza Umeme cha Kasulu ambapo thamani ya mradi ni Dola za Kimarekani milioni 20.5. Pia njia ya kusafirisha umeme (kilovolti 220) kutoka Buhigwe hadi Kigoma na Kituo cha Kupooza Umeme cha Buhigwe kwa thamani ya mradi ya dola milioni 19.8 za Kimarekani, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kavejuru, swali la nyongeza.

**MHE. KAVEJURU E. FELIX:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu ya Serikali, nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza. Serikali inatoa kauli gani ya kutatua changamoto ya umeme mdogo *(low voltage)* katika Wilaya ya Buhigwe wakati mkandarasi anaendelea na kazi? *(Makofi)*

Mheshimwa Mwenyekiti, swali la pili. Pamoja na kwamba Gridi ya Taifa imeshaifikia Wilaya ya Kankonko, Kibondo, Kasulu na Buhigwe, bado taasisi za Serikali kama shule, taasisi za kijamii (misikiti, makanisa) pamoja na vitongoji havijapata umeme: Lini Serikali itapeleka umeme? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la umeme hafifu *(low voltage)* ambalo ameliataja, ni suala la kawaida katika matumizi ya umeme na linatokea pale ambapo watumiaji wanakuwa wengi katika eneo husika, na hivyo vifaa vyetu kuzidiwa. Ni suala kama la kufanya *service* ya magari. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba *TANESCO* na Serikali tayari tumetenga fedha kuhudumia maeneo yote yenye

matatizo ya *low voltage* kwa kuongeza vitu vinavyoitwa *auto-voltage regulator*a na pia kwa kuweka *transformer* kubwa ili kuweza kusuka umeme mwingi na kuwafikia wahitaji. Katika maeneo anayoyasema nitawasiliana naye ili tujue maeneo mahususi, tuone hatua zilizochukuliwa na zilizofikiwa katika kutatua tatizo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye swali la pili, ni kweli kwamba Desemba mwaka huu tunatarajia kukamilisha vijiji vyote, lakini tutatafuta fedha kwa ajili ya kupeleka umeme kwenye vitongoji vyote nchini na taasisi zote alizozisema zikiwemo shule, makanisa na maeneo mengine yatapelekewa umeme kufuatia kupatikana kwa fedha, takribani shilingi trilioni tano au sita kwa ajili ya kumaliza maeneo yote yanayohitaji umeme yakiwemo maeneo ya Buhigwe na maeneo mengine ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante kwa majibu ya Waheshimiwa Wabunge. Tunawashukuru sana.

Waheshimiwa Wabunge, tumefikia mwisho wa kipindi chetu cha maswali na majibu asubuhi hii, ninayo matangazo machache. Tangazo la kwanza ni wageni walioko Bungeni asubuhi hii.

Waheshimiwa Wabunge, kwanza ni wageni walioko Jukwaa la Spika ambao ni Mheshimiwa Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais Mstaafu, Mheshimiwa Jaji Joseph Sinde Warioba. *(Makofi)*

Ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge.

Wapo Kamati ya Bajeti kutoka Baraza la Wawakilishi Zanzibar ambao ni Mheshimiwa Abdalla Hussein Kombo, Mbunge ambaye ni Mwenyekiti, Mheshimwa Asha Abdalla Musa, Mbunge na Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Fatma Ramadhani Mohamed, Mbunge na Mjumbe, Mheshimiwa Miraji Hamis Mussa, Mbunge na Mjumbe, Mheshimiwa Professa Omar Fakih Hamad,

Mbunge na Mjumbe pia na Mheshimiwa Ndugu Abbas Vuai ambaye ni Katibu wa Kamati, ahsante na karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni Mheshimiwa Profesa Makame Mbarawa, Mbunge na Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi ambao kwanza ni Balozi Mheshimiwa Aisha Amour ambaye ni Katibu Mkuu - Sekta ya Ujenzi; Mheshimiwa Gabriel Migire, Katibu Mkuu - Sekta ya Uchukuzi; Bwana Ludovick Nduhiye, Naibu Katibu Mkuu - Sekta ya Ujenzi; Dkt. Ally S. Possi, Naibu Katibu Mkuu - Sekta ya Uchukuzi; *Architecture* Dkt. Ombeni Swai, Mwenyekiti wa Bodi – *TBA;* Bwana Octavian Mshiu, Mwenyekiti wa Bodi ya *RFB;* na Mhandisi Deogratius Nyanda, Mwenyekiti wa Bodi ya TEMESA.

Wengine ni *Advocate* Menye David Manga - Mwenyekiti wa Bodi – *ERB;* Mhandisi Joseph Nyamhanga, Mwenyekiti wa Bodi – *CRB, Architecture* Dkt. Ludigija Bulamile - Mwenyekiti wa Bodi – *AQRB*, Profesa Ame Ahamed Ame - Mwenyekiti wa Bodi *LATRA,* Balozi Ernest J. Mangu - Mwenyekiti wa Bodi – *TPA,* Meja Jenerali Mstaafu, John Mbungo - Mwenyekiti wa Bodi – *MSCL, Captain* Ernest Bupamba - Mwenyekiti wa Bodi – *DMI,* Profesa Longinus Rutasitara - Mwenyekiti wa Bodi – *TCAA,* Bwana Mussa Mandia - Mwenyekiti wa Bodi – *TASAC,* Bwana, George Makuke Mwenyekiti wa Baraza - *LATRA – CCC,* Dkt. Samweli Werema Mwenyekiti wa Bodi ya – *KADCO,* Ndugu, Olingeta Mbamba - Mwenyekiti wa Bodi – *NIT,* Dkt. Buruhani Nyenzi - Mwenyekiti wa Bodi ya – *TMA,* Profesa Neema Mori - Mwenyekiti wa Bodi ya – *ATCL. (Makofi)*

Tunao wageni watatu Mheshimiwa Profesa Makame Mbarawa, Mbunge, Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, ambao ni familia yake wakiongozwa na Mke wa Mheshimiwa Mbarawa Profesa Eunice Mbarawa. *(Makofi)*

Tunao wageni saba wa Mheshimiwa Godfrey Kasekenya ambao ni watoto wake na shemeji zake wakiongozwa mke wa Mheshimiwa Naibu Waziri, Ndugu Subilaga Kasekenya. *(Makofi)*

Wageni 33 wa Mheshimiwa Spika ni Maafisa Itifaki wakiongozwa na Ndugu George Geofrey, ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea; tunao wageni 15 wa Mheshimiwa Naibu Spika ambao ni wanafunzi wa *The Maritime Student Representative Council (MSRC)*. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wengine wa Mheshimiwa Profesa Makame Mbarawa, Mbunge na Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi ambao ni Wakurugeni wa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, wapo pia Wakuu wa Taasisi zilizoko chini ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi. *(Makofi)*

Tunao pia wawakilishi wa benki za NMB, CRDB, NBC, Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika na *Central Corridor Transport Facilitation Agency,* ahsante na karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wataalam wanawake maalum kutoka *ATCL, MSCL, TPA* na *DMI* wanaofanya kazi zinazodhaniwa kuwa ni za wanaume kama vile rubani wa ndege, dereva wa treni, *captain* wa meli na mwendesha mitambo, mtawaona mchana. *(Makofi/Kicheko)*

Tunao Mameneja wa Mikoa ya *TANROADS* Tanzania, ahsanteni na karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao viongozi wa Chama cha Wamiliki wa Malori Tanzania wakiongozwa na Mwenyekiti wao Ndugu Elias Lukumay, ahsante na karibuni. *(Makofi)*

Tunao wageni wanane wa Mheshimiwa *Engineer* Andrea Mathew Kundo Mbunge na Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari ambao ni wasanii kutoka Dar es Salaam na Simiyu, ahsante na karibuni. *(Makofi)*

Tunae mgeni wa Mheshimiwa Zuberi Kuchauka, Mbunge, viongozi wa Chama cha CCM kutoka Liwale Mkoa wa Lindi. *(Makofi)*

Wageni watano wa Mheshimiwa Condester Sichwale, Mbunge kutoka Momba Mkoani Songwe. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Antipas Mgungusi kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Eric Shigongo kutoka Jijini Dar es Salaam, ahsante na karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 19 wa Mheshimiwa Stanslaus Nyongo ambao ni walimu wakuu wa shule za msingi kutoka Maswa. *(Makofi)*

Tunao wageni 15 wa Mheshimiwa Jacqueline Msongozi kutoka Jijini Dodoma, ahsante na karibuni. *(Makofi)*

Wapo wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; tunao wageni kumi wa Taasisi ya *Eternal Perspective Foundation*, kutoka Mkoa wa Shinyanga. *(Makofi)*

Tunao wanafunzi 110 na walimu watano kutoka shule ya Msingi Ignatus ya Jijini Dodoma. Ahsante na karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni saba wa Mheshimiwa George Simbachawene, Waziri wa Nchi, Nchi Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ambao ni viongozi wa Kikundi cha Bodaboda *Titanic,* kutoka Kata ya Vingunguti Dar es Salaam. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, naomba tusikilizane; vijana hawa walikopeshwa mkopo na halmashauri ya Manispaa ya Ilala, shilingi milioni 12.5 wakafanikiwa kurejesha, wakakopeshwa tena shilingi milioni 50, wamefanikiwa kuongeza idadi ya pikipiki na kufungaua *mobile money centre* ambapo wanatoa huduma za kifedha kwa vijana wengine na kwa sasa wako mbioni kuingia kwenye biashara ya daladala. Ahsanteni sana vijana kwa kazi nzuri mnayoifanya. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tangazo kutoka kwa Katibu wa Bunge; Mheshimiwa Katibu wa Bunge anawakumbusha Waheshimiwa Wabunge wote kuwa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Manendeleo ya Makazi itaendesha semina kuhusu muundo na majukumu ya Wizara pamoja na sera ya ubia ya Shirika la

Nyumba la Taifa *(NHC)*. Semina hiyo itafanyika leo siku ya Jumatatu tarehe 22 Mei, 2023 mara baada ya kusitisha shughuli za Bunge saa saba mchana katika ukumbi wa Pius Msekwa. Waheshimiwa Wabunge wote wanakaribishwa kuhudhuria semina hiyo muhimu ili kuwajengea uelewa kuhusu shughuli mbalimbali zinazotekelezwa na Wizara.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea.

Katibu.

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makdario ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kwa mwaka wa fedha 2023/2024

**MWENYEKITI**: Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, namuita sasa Mheshimiwa Profesa Mbarawa, Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, awasilishe hoja yake mbele ya Wabunge. *(Makofi)*

**WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, bada ya kupokea taarifa iliyowasilishwa hapa Bungeni na Kamati ya Kudumu ya Miundombinu, naomba kutoa hoja ya kwamba Bunge lako tukufu likubali kupokea, kujadili na kupitisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya fedha kwa Wizara ya Ujenzi kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kukutana leo

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuungana na Bunge lako Tukufu katika kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutimiza miaka miwili katika kutuongoza kwa umahiri na mafanikio makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda pia kumpongeza na mumshukuru kwa dhati Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango, Makamu wa Rais kwa namna anavyomsaidia Mheshimiwa Rais katika kuongoza nchi yetu kwa kuliletea Taifa letu maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake mahiri na makini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutumia nafasi hii kumpongeza kwa dhati kazi kubwa anayoifanya ya kusimamia Bunge letu Mheshimiwa Spika kwa weledi mkubwa. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Naibu Spika kwa kuendelea kutekeleza vyema shughuli za Bunge. Vilevile, nichukue fursa hii kuwapongeza wenyeviti wa Bunge kwa kuchaguliwa kwao. Tunawaahidi ushirikiano katika kutimiza wajibu wetu wa kusimamia na kuliongoza Bunge letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima, ninaomba nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuniamini katika kutekeleza majukumu yangu nikiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi tangu aliponiteua tarehe 12 Septemba, 2021. Ninaomba kumhakikishia kuwa, nitaendelea kutekeleza majukumu yangu kwa uwezo na uaminifu mkubwa ili kuliletea Taifa letu maendeleo. Ninamuahidi kuwa nitatumia weledi, maarifa na uwezo wangu wote katika kutekeleza wajibu wangu kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee naomba nimpongeze Mheshimiwa Selemani Moshi Kakoso, Mbunge wa Mpanda Vijijini kwa kuchaguliwa tena kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu na Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mbunge wa Same Mashariki kwa kuchaguliwa kwa mara nyingine kuwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati. Aidha, nawapongeza Wajumbe wote walioteuliwa kwenye Kamati hii. Nichukue fursa hii kuishukuru Kamati kwa kuendelea kutoa ushauri na kuisimamia Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kutoa salamu za pole kwa Bunge lako tukufu na wote walioguswa na msiba wa kifo cha Mbunge, Mussa Hassan Mussa aliyekuwa Mbunge wa

Jimbo la Amani. Tutaendelea kuthamini na kuenzi mchango wake katika Bunge hili na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, naomba sasa nitoe taarifa ya Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kwa mwaka wa fedha 2022/2023 pamoja na Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi na maombi ya fedha kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa fedha 2022/2023. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi imegawanywa katika mafungu mawili kibajeti ambayo ni Fungu 62 (Sekta ya Uchukuzi) na Fungu 98 (Sekta ya Ujenzi). Naanza kutoa maelezo kuhusu utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2022/2023 kwa Sekta ya Ujenzi ikifuatiwa na Sekta ya Uchukuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Sekta ya Ujenzi,* Bajeti ya Matumizi ya Kawaida. katika mwaka wa fedha 2022/2023, Sekta ya Ujenzi ilitengewa jumla ya shilingi 44.293 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Hadi Aprili, 2023 jumla ya shilingi bilioni 32.893 sawa na asilimia 74.26 ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge zilikuwa zimetolewa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bajeti ya Miradi ya Maendeleo *kwa* upande wa miradi ya maendeleo, katika mwaka wa fedha 2022/2023, Sekta ya Ujenzi ilitengewa shilingi trilioni 1.377 Kiasi cha pesa hizo kinajumuisha shilingi trilioni 1.124, fedha za ndani na shilingi bilioni 252.965, fedha za nje. Fedha za ndani zilijumuisha fedha za Mfuko Mkuu wa Serikali ni shilingi bilioni 777.785 na fedha za Mfuko wa Barabara ni shilingi bilioni 599.756. Hadi Aprili, 2023 fedha zilizopokelewa ni shilingi trilioni 1.312 sawa na asilimia 95.3 ya fedha zilizoidhinishwa kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Kati ya fedha hizi, shilingi trilioni 1.069 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 243.321 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kuipongeza na kuishukuru sana Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuendelea kulipa hati

za madai kwa wakati. Aidha, kutokana na malipo hayo kufanyika kwa wakati, kasi ya utekelezaji wa miradi imeongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile naishukuru sana Serikali kwa kuendelea kutoa fedha kwa ajili ya kuwalipa makandarasi na washauri elekezi ambapo katika mwaka wa fedha 2022/2023 jumla ya shilingi bilioni 184.459, zimetolewa kwa ajili ya malipo ya madeni ya makandarasi hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa miradi ya barabara na madaraja. Katika mwaka wa fedha 2022/2023, miradi ya Barabara Kuu iliyopangwa kutekelezwa ni ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara zenye urefu wa kilometa 470 pamoja na ukarabati kwa kiwango cha lami wa barabara zenye urefu wa kilometa 33. Kazi nyingine ni kuendelea na ujenzi wa madaraja makuu manne ambayo ni Daraja la Kigongo – Busisi, Mwanza, Daraja la Gerezani huko Dar es salaam, Daraja la Pangani na Daraja la Wami Mkoani Pwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi Aprili huu, ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara zenye urefu wa kilometa 179.18 umekamilika na ujenzi wa kilometa 290.82 unaendelea. Aidha, ujenzi wa daraja la Wami umekamilika. Ujenzi wa madaraja mawili ya Wami na Gerezani umekamilika. Vilevile, ujenzi wa daraja la Kigongo – Busisi, Mwanza umefikia asilimia 72 na ujenzi wa daraja la Pangani (Tanga) umefikia asilimia tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ya barabara za mikoa iliyopangwa kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2022/2023 ni ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara zenye urefu wa kilometa 103.01. Kazi nyingine ni kufanya ukarabati kwa kiwango cha changarawe wa barabara zenye urefu wa kilometa 1,042.43. Hadi kufikia Aprili, 2023 jumla ya kilometa 23.11 za barabara za mikoa zilijengwa kwa kiwango cha lami na jumla ya kilometa 253.67 zilikarabatiwa kwa kiwango cha changarawe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ya barabra na madaraja yaliyokamilika. Serikali ya Awamu ya sita chini ya uongozi mahiri wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya

Muungano wa Tanzania imeweza kupiga hatua kubwa ya mafanikiuo katika eneo la ujenzi wa barabara na madaraja.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, samahani kidogo.

Waheshimiwa Wabunge naomba tupunguze sauti zetu kidogo tumsikilize mtoa hoja. Tafadhari sana. Mheshimiwa Waziri, endelea.

**WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi chake cha miaka miwili ya uongozi wa Mheshimiwa Rais, barabara katika maeneo mbalimbali zimejengwa na kukamilika. Barabara hizo ni kama ifuatavyo:-

(i) Barabara ya Loliondo – Mto wa Mbu yenye urefu wa kilometa 201, Sehemu ya Waso – *Sale Junction* yenye urefu wa kilometa 49 Mkoani Arusha imekamilika;

(ii) Barabara ya Morocco – Mwenge yenye urefu wa kilometa 4.3 kutoka njia tano hadi Sita yenye urefu wa kilometa 3.2 Mkoani Dar es Salaam imekamilika;

(iii) Barabara ya Kongwa *Junction* – Mpwapwa – Gulwe – Kibakwe yenye urefu wa kilometa 98, Sehemu ya Mbande – Kongwa *junction* yenye urefu wa kilometa 5.8 Mkoani Dodoma imekamilika;

(iv) Barabara ya Tabora – Koga – Mpanda Sehemu ya tatu, Kasinde – Mpanda yenye urefu wa kilometa 108 pamoja na kipande cha barabara ya Urwira yenye urefu wa kilometa 3.7 Mkoani Katavi imekamilika;

(v) Barabara ya Kidahwe – Kasulu – Kibondo – Nyakanazi yenye urefu wa kilometa 268, Sehemu za Kidahwe – Kasulu yenye urefu wa kilometa 63 na Kakonko – Nyakanazi yenye urefu wa kilometa 50 Mkoani Kigoma imekamilika;

(vi) Barabara ya Bulamba – Kisorya yenye urefu wa kilometa 51Mkoani Mara imekamilika.

(vii) Barabara ya Makutano – Nyamuswa – Ikoma *Gate* yenye urefu 153, Sehemu ya Makutano – Sanzate yenye urefu wa kilometa 50 Mkoani Mara imekamilika;

(viii) Barabara ya Musoma – Makojo – Busekela, Sehemu ya Kuseni – Suguta yenye urefu wa kilometa tano Mkoani Mara imekamilika.

(ix) Barabara ya Chunya – Makongorosi (yenye urefu wa kilometa 39 Mkoani Mbeya imekamilika;

(x) Barabara ya Mtwara – Newala – Masasi yenye urefu wa kilometa 210, Sehemu ya Mtwara – Mnivata yenye urefu wa kilometa 50 Mkoani Mtwara imekamilika;

(xi) Barabara ya Njombe – Ndulamo – Makete yenye urefu wa kilometa 107.4 Mkoani Njombe imekamilika;

(xii) Barabara ya Itoni – Ludewa – Manda, Sehemu ya Lusitu – Mawengi yenye urefu wa kilometa 50 Mkoani Njombe imekamilika;

(xiii) Barabara ya Sumbawanga – Matai – Kasanga *Port* yenye urefu wa kilometa 112 Mkoani Rukwa imekamilika;

(xiv) Barabara ya Masasi – Songea Mbamba Bay, Sehemu ya Sita, Mbinga Mbamba Bay yenye urefu wa kilometa 66 Mkoani Ruvuma imekamilika;

(xv) Barabara ya Mpemba – Isongole (yenye urefu wa kilometa 50.3 Mkoani Songwe imekamilika;

(xvi) Barabara ya Urambo – Kaliua – Ilunde – Uvinza, Sehemu ya Urambo – Kaliua yenye urefu wa kilometa 280 Mkoani Tabora imekamilika;

(xvii) Barabara ya Manyoni – Itigi – Tabora, Sehemu ya Nyahua – Chaya yenye urefu wa kilomet 85 Mkoani Tabora imekamilika;

(xviii) Barabara ya Tabora – Koga – Mpanda, Sehemu Usesula – Komanga yenye urefu wa kilometa 108 pamoja na Sikonge *Spur Road* yenye urefu wa kilometa 7.5 na Sehemu ya Komanga - Kasinde yenye urefu wa kilometa 108 pamoja na Inyonga *Spur* yenye urefu wa kilometa 4.8 Mkoani Tabora imekamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha kuna miradi mbalimbali mikubwa ya ujenzi wa madaraja inayoendelea na iko katika hatua mbalimbali za utekelezaji miradi hiyo ni kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa Barabara ya Mianzini – Olemringaringa – Ngaramtoni Juu na Olemringaringa – Sambasha/Timbolo yenye urefu wa kilometa 18 Kazi za ujenzi zinaendelea na zimefikia asilimia 18 Mkoani Arusha.

Upanuzi wa Barabara ya Kimara – Kibaha kuwa Njia Nane yenye urefu wa kilometa 19.2 na Madaraja matatu ya Kibamba, Kiluvya na Mpiji Mkoani Dar es Salaam unaendelea.

Ujenzi wa Miundombinu ya Mabasi yaendayo haraka, Awamu ya Pili yenye urefu wa kilometa 19.3 na Awamu ya Tatu *Nyerere Road corridor* kutoka *CBD* mpaka Gongolamboto yenye urefu wa kilometa 23.33 Mkoani Dar es Salaam unaendelea.

Barabara za Mzunguko wa Nje Jijini Dodoma *(Dodoma City Outer Ring Roads);* Sehemu ya Nala – Veyula – Mtumba – Ihumwa *Dry Port* yenye urefu wa kilometa 52.30 (Lot ya kwanza) na Sehemu ya Ihumwa – *Dry Port* – Matumbulu – Nala yenye urefu wa kilometa 60.00 *(Lot ya pili)* Mkoani Dodoma unaendelea.

Barabara ya Kumunazi – Bugene – Kasulo na Kyaka – Mutukula yenye urefu wa kilometa 124; Sehemu ya Bugene – Burigi *Chato National Park* yenye urefu wa kilometa 60; Mkoani Kagera unaendelea.

Barabara ya Kabingo – Kasulu – Manyovu yenye urefu wa kilometa 260.0; sehemu za *Kanyani Junction* – Mvugwe kilometa 70.5; Mvugwe – Nduta *Junction* yenye urefu wa kilometa 59.35; Kibondo *Junction* – Kabingo yenye urefu wa kilometa 62.5; Nduta

*Junction* – Kibondo yenye urefu wa kilometa 25.9 na Kasulu – Manyovu pamoja na barabara za kuingia Kasulu mjini yenye urefu wa kilometa 68 Mkoani Kigoma ujenzi unaendelea.

Barabara ya Kazilambwa – Chagu yenye urefu wa kilometa 36 mkoani Kigoma ujenzi unaendelea.

Barabara ya Malagarasi – Ilunde – Uvinza yenye urefu wa kilometa 51.1; Mkoani Kigoma unaendelea.

Barabara ya Dumila – Kilosa; Sehemu ya Ludewa – Kilosa yenye urefu wa kilometa 18 mkoani Morogoro unaendelea.

Barabara ya Mikumi – Kidatu – Ifakara; Sehemu ya Kidatu – Ifakara yenye urefu wa kilometa 66.9: Mkoani Morogoro inendelea.

Barabara ya Karatu – Mbulu – Hydom – Sibiti River – Lalago – Maswa yenye urefu wa kilometa 389; Sehemu ya Mbulu – Garbabi yenye urefu wa kilometa 25 Mkoani Manyara ujenzi unaendelea.

Barabara ya Tarime – Mugumu yenye urefu wa kilometa 87.14; Sehemu ya Tarime – Nyamwaga (Lot ya kwanza): yenye urefu wa kilometa 25 Mkoani Mara ujenzi unaendelea.

Barabara ya Nyamuswa – Bunda – Bulamba yenye urefu wa kilometa 56.4 Mkoani Mara ujenzi unaendelea.

Barabara ya Itoni – Ludewa – Manda Mkoani Njombe ujenzi unaendelea.

Barabara ya Tanga – Pangani – Mkange; Sehemu ya Tanga – Pangani yenye urefu wa kilometa 50 na Sehemu ya Tungamaa – Mkange yenye urefu wa kilometa 95.2 Mkoani Tanga ujenzi unaendelea.

Barabara ya Handeni – Kibirashi – Kwamtoro – Singida yenye urefu wa kilometa 434.33 Sehemu ya Handeni – Mafuleta yenye urefu wa kilometa 20: Ujenzi unaendelea na umefikia

asilimia 11. Sehemu ya Mafuleta – Kileguru yenye urefu wa kilometa 30 taratibu za manunuzi kwa ajili ya ujenzi zinaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa ujenzi wa madaraja jumla ya madaraja nane yamejengwa na kukamilika madaraja hayo ni kama yafuatayo: - Daraja la Wami Mkoani Pwani, Daraja la Tanzanite Mkoani Dar es salaam, Daraja la Gerezani Dar es salaam, Daraja la Mpwapwa Dodoma, Daraja la Kiyegeya Mkoani Morogoro na Daraja la Ruhuhu Mkoani Ruvuma, pamoja na Daraja la Kitengule Mkoani Kagera na Daraja la Msingi huko Mkoani Singida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ya barabara na viwanja vya ndege iliyosainiwa mwaka 2022/2023. Mikataba ya ujenzi na ukarabati wa miradi mbalimbali ya barabara, madaraja na viwanja vya ndege ilisainiwa katika mwaka wa fedha 2022/2023. Miradi hiyo ni; ujenzi wa Barabara za Lusahunga – Rusumo yenye urefu wa kilometa 92, Kitulo – Iniho yenye urefu wa kilometa 36.3; Sengerema – Nyehunge yenye urefu wa kilometa 54, Utete – Nyamwage yenye urefu wa kilometa 33.7, Kibondo – Mabamba yenye urefu wa kilometa 48, Igawa – Songwe – Tunduma Sehemu ya Uyole – Ifisi - A*irport* yenye urefu wa kilometa 32, Ibanda – Itungi yenye urefu wa kilometa 28, Kajunjumele – Kiwira *Port* yenye urefu wa kilometa sita, barabara unganishi katika Daraja la Sibiti yenye urefu wa kilometa 24.83 na barabara ya Makongolosi – Rungwa – Itigi – Mkiwa sehemu ya Noranga – Doroto yenye urefu wa kilometa sita, na Itigi – Mkiwa yenye urefu wa kilometa 25.569. Miradi mingine ni ujenzi wa Madaraja ya Mpiji Chini na Mbambe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, mikataba ya ujenzi wa viwanja vya ndege iliyosainiwa ni viwanja vya ndege vya Kigoma na Sumbawanga. Utekelezaji wa miradi hii uko katika hatua za maandalizi ya kuanza kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Miradi ya Barabara itkayojengwa kwa utaratibu wa *EPC+F*, katika mwaka wa fedha 2023/2024 Wizara ilianza utaratibu wa manunuzi kwa ajili ya kuwapata wakandarasi wa kujenga kwa kiwango cha lami barabara saba zenye jumla ya urefu wa kilometa 2,035 kwa kutumia utaratibu wa zitaanza kujengwa kwa kiwango cha lami kwa kutumia utaratibu

wa *Engineering Procurement Construction and Financing (EPC+F)*. Barabara hizi zitafungua fursa za kiuchumi katika maeneo zinapopita na kwa Taifa letu kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua iliyofikiwa hadi sasa ni kuwa Wakandarasi wa miradi yote saba wamepatikana na mikataba ya kazi za ujenzi inatarajiwa kusainiwa kabla ya mwisho wa mwezi Juni mwaka huu. Barabara ambazo zitajengwa kwa utaratibu huu wa *EPC+F* ni kama ifuatavyo: -

i. Barabara ya Kidatu – Ifakara – Lupiro – Malinyi – Kilosa kwa Mpepo – Londo – Lumecha/Songea yenye urefu wa kilometa 435.

ii. Barabara ya Karatu – Mbulu – Haydom – *Sibiti River* – Lalago – Maswa (Simiyu) yenye urefu wa kilometa 339.

iii. Barabara ya Handeni – Kibirashi – Kijungu – Kibaya – Njoro – Olboroti – Mrijochini – Dalai – Chambalo – Chemba – Kwa Mtoro – Singida yenye urefu wa kilometa 460.

iv. Barabara ya Arusha – Kibaya – *Kongwa Junction* yenye urefu wa kilometa 453.42.

v. Barabara ya Masasi – Nachingwea – Liwale yenye urefu wa kilometa 175.

vi. Barabara ya Igawa – Songwe – Tunduma yenye urefu wa kilometa 218 ambayo itajengwa kwa njia nne pamoja na barabara ya mchepuo ya Uyole – Songwe yenye urefu wa kilometa 48.9, na

vii. Barabara ya Mafinga – Mtwango – Mgololo yenye urefu wa kilometa 81.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni mara ya kwanza katika historia ya nchi yetu kuwa na miradi mikubwa yenye jumla ya kilometa 2,035 ambayo itaanza kutekelezwa kwa wakati mmoja katika maeneo mbalimbali nchini, na itagharamu zaidi ya shilingi trilioni 3.7. Haya ni maono na maelekezo ya Mheshimiwa Dkt.

Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kutaka kuifungua nchi yetu kwa haraka sana. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa maono haya makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ya barabara Itakayotekelezwa kwa Utaratibu wa *PPP*, kuhusu ujenzi wa barabara kwa kutumia utaratibu wa kushirikisha Sekta Binafsi *(Public Private Partnership - PPP),* Wizara inaendelea na manunuzi ya wakandarasi kwa ajili ya ujenzi wa *Expressway* kutoka Kibaha – Chalinze – Morogoro yenye urefu wa kilometa 205. Hadi sasa kazi inayoendelea ni uchambuzi *(evaluation)* wa wakandarasi walioonesha nia *(Expression of Interest)* ya kutekeleza mradi huu kwa sehemu ya kutoka Kibaha – Chalinze yenye urefu wa kilometa 78.9. Kwa upande wa sehemu ya Chalinze – Morogoro yenye urefu wa kilometa 126.1, Mshauri Elekezi anaendelea na kazi ya upembuzi yakinifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii itakuwa ni mara ya kwanza katika historia ya nchi yetu kuwa na mradi mkubwa wa ujenzi wa barabara hapa nchini ambao utatekelezwa kwa utaratibu huu wa *PPP*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa miradi ya barabara na madaraja umenyeshwa katika kitabu changu cha hotuba ya bajeti kutoka ukurasa wa saba mpaka ukurasa wa 43.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu viwanja vya ndege, *TANROADS* imeendelea kutekeleza miradi ya uendelezaji wa viwanja vya ndege ambapo ukarabati na upanuzi wa Viwanja vya Ndege vya Songea na Mtwara umekamilika. Aidha, kazi za ukarabati wa barabara za kutua na kuruka ndege pamoja na eneo la usalama, usimikaji wa taa za usalama na taa za kuongozea ndege katika Kiwanja cha Ndege cha Songwe zimekamilika. Kwa sasa Mkandarasi anaendelea na kazi ya kumalizia ujenzi wa jengo la abiria ambapo utekelezaji wake umefikia asilimia 98.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya ukarabati na upanuzi wa Viwanja vya Ndege vya Sumbawanga, Shinyanga, Tabora na

Kigoma umeanza na wakandarasi wako katika hatua za maandalizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mradi wa ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato, hadi kufikia mwezi Aprili mwaka huu utekelezaji wa *package one* unaohusisha ujenzi wa barabara ya kuruka na kutua ndege, barabara ya maungio maegesho ya ndege, uzio wa usalama, barabara za kuingia na kutokea kiwanjani na maegesho ya magari na usimikaji wa mfumo wa taa za kuongozea ndege umefikia asilimia 18. Aidha, utekelezaji wa *package two* unaohusisha ujenzi wa jengo la abiria, jengo la kuongozea ndege, kituo cha zimamoto, kituo cha hali ya hewa na vituo vidogo nane vya kufua umeme unaendelea na umefikia asilimia mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kiwanja cha Ndege cha Musoma, kazi ya upanuzi na ukarabati wa barabara ya kutua na kurukia ndege, maegesho ya ndege, barabara ya kiungio na uzio wa usalama inaendelea na utekelezaji wake umefikia asilimia 47. Utekelezaji wa miradi ya viwanja vya ndege umeoneshwa kwenye kitabu changu cha hotuba ya bajeti kutoka ukurasa wa 51 hadi 54.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2022/2023, Wizara kupitia Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania *(TEMESA)* imeendelea kutekeleza miradi ya ujenzi na ukarabati wa vivuko na maegesho *ya* vivuko katika maeneo mbalimbali hapa nchini. Kuhusu utekelezaji wa kina wa miradi ya ukarabati, ununuzi na ujenzi wa vivuko hadi mwezi Aprili mwaka huu umeonyeshwa katika kitabu changu cha hotuba ya bajeti kuanzia ukurasa wa 45 hadi 47.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia Wakala wa Majengo Tanzania *(TBA)* imeendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya ujenzi na ukarabati wa nyumba na majengo ya Serikali katika mwaka wa fedha 2022/2023. Utekelezaji wa kina wa miradi ya Wakala wa Majengo Tanzania *TBA* umeoneshwa katika kitabu changu cha hotuba ya bajeti kuanzia ukurasa wa 47 hadi ukurasa wa 49.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia mwezi Aprili mwaka huu utendaji wa taasisi zilizo chini ya sekta ya ujenzi kuanzia Bodi ya Mfuko, Wakala wa Majengo Tanzania, Bodi ya Usajiri Wahandisi, Bodi ya Usajiri Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majengo, Bodi ya Usajiri wa Wakandarasi, Baraza la Taifa la Ujenzi, Kituo cha Usambazaji wa Teknolojia Katika Sekta ya Ujenzi na Usafirishaji umeonyeshwa katika hotuba yangu ya kitabu cha bajeti kuanzia ukurasa wa 54 hadi 67.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Uchukuzi Fungu 62, bajeti iliyoidhinishwa na fedha zilizotolewa kwa mwaka wa fedha 2022/2023, bajeti ya matumizi ya kawaida. Katika mwaka wa fedha 2022/2023 sekta ya uchukuzi iliidhinishiwa shilingi bilioni 94.546 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Hadi kufikia mwezi Aprili mwaka huu shilingi bilioni 71.955 sawa na asilimia 76.11 zilikuwa zimetolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ya maendeleo, katika mwaka wa fedha 2022/2023 sekta ya uchukuzi iliidhinishiwa shilingi tirioni 2.041 kwa jili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Hadi kufikia mwezi aprili mwaka huu jumla ya shilingi tirioni 1.847 sawa na asilimia 90.51 zilikuwa zimetolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa miradi ya maendeleo na utoaji huduma; kwanza udhibitiwa usafiri kwa njia ya barabara. Udhibiti wa Usafiri wa Barabara unatekelezwa na Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini *(LATRA)*. Mamlaka hiyo inadhibiti utoaji wa huduma za usafiri wa kibiashara kwa abiria na mizigo ikijumuisha mabasi, malori, teksi, pikipiki za magurudumu matatu na pikipiki za magurudumu mawili. utendaji kazi wa udhibiti wa usafiri kwa njia ya barabara umeoneshwa katika kitabu changu cha hotuba ya bajeti kuanzia ukurasa wa 69 hadi 74.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma za usafiri kwa njia ya reli, Shirika la Reli Tazania *(TRC)*. Serikali kupitia Wizara imeendelea na ujenzi wa awamu ya awamu ya kwanza ya mradi wa reli ya kati kwa kiwango cha *standard gauge* kutoka Dar es Salaam hadi Mwanza yenye urefu wa kilometa 1,219 unaogawanyika katika vipande vitano kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia Aprili, mwaka huu hatua ya utekelezaji iliyofikiwa kwa kipande cha Dar es Salaam – Morogoro yenye urefu wa kilometa 300 ni asilimia 98.14, Morogoro hadi Makutupora (kilometa 422) asilimia 93.83, Isaka hadi Mwanza (kilometa 341) asilimia 31.07. Makutupora hadi Tabora (kilometa 368) asilimia saba na Tabora hadi Isaka (kilometa 165) asilimia 2.39.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba yangu ya mwaka 2022/2023 tuliahidi kuanza maandalizi ya ujenzi wa awamu ya pili ya reli ya *standard gauge*. Napenda kulihalifu Bunge lako Tukufu kuwa Serikali imeanza ujenzi wa reli ya *SGR* kwa awamu ya pili katika kipande cha Tabora Kigoma yenye urefu wa kilometa 506 ambapo ilisaini mkataba na kampuni ya *CCECC* na *CRCC* kutoka China na kwa sasa mkandarasi anakamilisha maandalizi ya ujenzi. Utendaji na utekelezaji wa miradi ya reli kupitia *TRC* umeoneshwa katika kitabu change cha hotuba ya bajeti kuanzia ukurasa wa 75 hadi 77.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande Mamlaka ya Reli Tanzania na Zambia *(TAZARA)*, hadi Aprili 2023, *TAZARA* ilisafirisha jumla ya tani 244,492 za mizigo na jumla ya abiria 765,706 kwa njia ndefu. Utendaji wa *TAZARA* umeonyeshwa katika kitabu changu cha hotuba ya bajeti kuanzia ukurasa wa 78 hadi ukurasa wa 80.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa udhibiti wa huduma za usafiri kwa njia ya maji, Serikali kupitia Shirika la Wakala wa Meli Tanzania *(TASAC)* imeendelea kusimamia ulinzi na usalama wa vyombo vya usafiri kwa njia ya maji na kudhibiti uchafuzi wa mazingira unaotokana na shughuli za usafiri majini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TASAC* imeendelea kusimamia ujenzi wa kituo kikuu cha uratibu wa shughuli za utafutaji na uokoaji za kikanda kitakachojengwa eneo la ilemera huko mkoani Mwanza. Kwa sasa mkandarasi tayari amekabidhiwa eneo kwa ajili ya kuanza shughuli za ujenzi na kazi hiyo inatarajiwa kukamilika ndani ya miezi 18.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile mkandarasi amepatikana kwa ajili ya kujenga vituo vidogo vitatu vya utafutaji na uokoaji

katika maeneo ya kanyala mkoani Geita, Nansio huko Ukerewe na Musoma mkoani Mara na kwa sasa maandalizi ya ujenzi yanaendelea. Utendaji wa udhibiti wa huduma za usafiri kwa njia ya maji na utekelezaji wa miradi mbalimbali umeoneshwa katika kitabu changu cha hotuba ya bajeti kuanzia ukurasa wa 80 hadi 84.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu huduma za uchukuzi katika Maziwa Makuu Serikali kupitia Kampuni ya Huduma za Meli *(MSCL)* imeendelea kutoa huduma za usafiri na usafirishaji kwenye Maziwa Makuu ya Victoria, Tanganyika na Nyasa. hadi kufikia mwezi Aprili, 2023 *MSCL* ilisafirisha abiria 170,137 na tani za mizigo 18,909.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Serikali imeendelea kutekeleza miradi ya ujenzi na ukarabati wa meli zinazotoa huduma katika Maziwa Makuu. Hadi kufikia mwezi Aprili mwaka huu ujenzi wa meli ya Mv. Mwanza ulifikia asilimia 83, ukarabati wa meli ya Mv. Umoja umefikia asilimia 75.8 na ukarabati wa Mt. Sangara ulifikia asilimia 90.7.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha Serikali kupitia *MSCL* iko katika hatua za mwisho za majadiliano na mkandarasi ili kuwezesha kuanza ujenzi wa meli mbili katika ziwa Tanganyika, meli moja katika Ziwa Victoria na Chelezo katika Ziwa Tanganyika. Hatua iliyofikiwa ya ukarabati wa *MV* Liemba hadi sasa ni kuwa mkandarasi amepatikana na makataba wa kuanza kazi za ukarabati wa meli hiyo unatarajiwa kusainiwa kabla ya mwisho wa mwezi wa Juni mwaka huu. Kazi ya ukarabati itafanyika kwa muda wa miezi minane. Pia kazi ya matengenezo ya utulivu, yaani *stability* ya *MV Mwongozo* itaanza hivi karibuni. Utendaji na utekelezaji wa miradi ya *MSCL* umeoneshwa katika kitabu changu cha hotuba ya bajeti kuanzia ukurasa wa 85 hadi 87.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kw upande wa huduma za bandari, hadi kufikia mwezi aprili mwaka huu Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania *(TPA)* ilihudumia shehena yenye jumla ya tani milioni 20.851na makasha 765,504. Aidha *TPA* iliendelea na utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika bandari za mwambao na bandari za maziwa makuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa uboreshaji wa huduma za Bandari ya Dar es salaam umefikia asilimia 96. Aidha, bandari ya Mtwara *TPA* imekamilisha awamu ya pili ya uboreshaji wa bandari hiyo kwa kuimarisha na kuboresha gati namba moja na namba mbili zenye urefu wa mita 450 ambapo mradi umekamilika kwa asilimia 99.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa bandari za maziwa makuu, ujenzi wa Bandari ya Karema umekamilika na imeanza kutumika. Aidha ujenzi wa gati, ghala ya kuhifadhia makaa ya mawe, jengo la abiria, ofisi na sehemu ya kuegesha meli katika Bandari ya Ndumbi, Ziwa Nyasa umekamilika. utendaji na utekelezaji wa miradi ya *TPA* umeoneshwa katika kitabu changu cha hotuba ya bajeti kuanzia ukurasa wa 87 hadi 95.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Udhibiti wa Huduma za Usafiri wa Anga; Wizara kupitia Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania *(TCAA)* imeendelea kutoa huduma za udhibiti wa usafiri wa anga, viwanja vya ndege, masuala ya kiusalama na kiuchumi katika huduma za usafiri wa anga pamoja na kutoa huduma ya uongozaji wa ndege katika viwanja 14 hapa nchini. Utendaji na utekelezaji wa miradi ya mamlaka ya usafiri wa anga umeoneshwa katika kitabu changu cha hotuba ya bajeti kuanzia ukurasa 95 hadi 100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Huduma ya Viwanja vya Ndege; Serikali kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege ina jukumu la kusimamia, kuendesha, kuboresha na kuendeleza viwanja vya ndege 58 vinavyomilikiwa na Serikali. Serikali kupitia *TAA* imekamilisha maandalizi ya mahitaji ya kiufundi na ununuzi wa kandarasi kwa ajili ya ujenzi wa majengo ya abiria katika Viwanja vya Ndege vya Mpanda, Songea na Kahama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia imeanza maandalizi ya ujenzi wa Jengo la Waongoza Ndege katika Kiwanja cha Ndege cha Bukoba. Pia *TAA* imeanza matayarisho ya ukamilishaji wa ujenzi wa jengo la abiria kwa Kiwanja cha Ndege cha huko Mwanza. Hadi kufikia mwezi Aprili mwaka huu kazi ya uwekaji wa mfumo wa taa za kuongozea ndege katika Kiwanja cha Ndege cha Dodoma ili kiweze kutumika masaa 24 kwa siku imefikia asilimia 40.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu wa urejeshaji wa shughuli za uendeshaji wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro *(KIA)* chini ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege *TAA*. Wizara imeendelea na taratibu za kutunga sheria mahususi ya *TAA* kwa ajili ya kuwezesha viwanja vya ndege vyote nchini ikiwepo *KIA* kuwa chini ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania. Utekelezaji wa majukumu ya viwanja vya ndege umeoneshwa katika kitabu cha hotuba yangu ya bajeti kuanzia ukurasa wa 101 hadi 107.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Huduma za Usafiri kwa Njia ya Anga; Serikali imeendelea na juhudi za kuimarisha Kampuni ya Ndege Tanzania. Juhudi hizo ni pamoja na kuendelea na usimamizi wa utengenezaji wa ndege mpya nne. Ambapo ndege ya *Boeing* 767-300F, ndege moja ya mizigo inayotarajiwa kuwasili mwishoni mwa mwezi huu. Ndege mbili za Boeing 737-9 zinazotarajiwa kuwasili mwezi Agosti na Disemba, 2023 na Ndege moja ya *Boeing* 787-8 *Dreamliner* inayotarajiwa kuwasili mwezi Februari mwakani. Kutokana na mpango wa Serikali wa kuongeza ndege mpya nne, *ATCL* inatarajiwa kupanua wigo wa safari zake kwa kuongeza vituo vipya sita vya nje na vituo vitatu vya ndani. Utendaji wa utoaji huduma za usafiri na usafirishaji kwa njia ya anga umeainishwa katika kitabu changu cha hotuba ya bajeti kuanzia ukurasa wa 107 hadi 110.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Huduma ya Hali ya Hewa; Serikali kupitia Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania imeendelea kutekeleza mradi wa kununua na kufunga *radar* nne za hali ya hewa. *Radar* mbili tayari zimeshapokelewa na kazi ya ufungaji inaendelea katika M ikoa ya Mbeya na Kigoma. *Radar* nyingine mbili nyingine zitakazofungwa Mkoani Dodoma na Kilimanjaro na zinatarajiwa kuwasili mapema mwakani. Utendaji na utekelezaji wa miradi ya huduma za hali ya hewa umeoneshwa katika kitabu changu cha hotuba ya bajeti kuanzia ukurasa wa 111 hadi 113.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taasisi za mafunzo; utendaji wa taasisi za mafunzo zilizo chini ya Wizara, Sekta ya Uchukuzi umeoneshwa katika kitabu changu cha hotuba ya bajeti kuanzia ukurusa wa 113 hadi 120.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto zilizoikabili Wizara na Mikakati ya Kuzitatua; Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi ilikabiliwa na changamoto mbalimbali katika utekelezaji wa majukumu yake na changamoto hizo na mikakati ya kuzitatua zimeoneshwa katika kitabu changu cha hotuba ya bajeti kuanzia ukurasa wa 137 hadi 142.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango na makadirio ya mapato na matumizi ya fedha kwa Wizara kwa mwaka wa fedha 2023/2024; mpango huu umeandaliwa kwa kuzingatia Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa ya miaka mitano na Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020 pamoja na Maelekezo ya Serikali. Makadirio ya bajeti ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo kwa sekta ya Ujenzi na Uchukuzi ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Ujenzi, Fungu 98; makadirio ya bajeti ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo; katika mwaka wa fedha 2023/2024, Sekta ya Ujenzi imetengewe shilingi bilioni 48.395 ikiwa ni bajeti ya matumizi ya kawaida. Aidha, Bajeti ya Maendeleo kwa mwaka 2023/2024 ni shilingi trilioni 1.49. Kati ya fedha hizo, shilingi trilioni 1.084 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 335.17 ni fedha za nje. Kati ya fedha za ndani shilingi bilioni 595.756 ni fedha kutoka Mfuko wa Barabara na fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali ni shilingi bilioni 884.909.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vipaumbele vya mpango na bajeti kwa Sekta ya Ujenzi; kwenye Sekta ya Ujenzi katika mpango wetu wa mwaka unaokuja wa fedha tumepanga kwanza, kuanza ujenzi wa miradi saba ya barabara yenye urefu wa kilometa 235 kwa kutumia utaratibu wa *Engineering Procurement Construction and Financing (EPC + F)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kuanza utekelezaji wa ujenzi wa barabara kutoka Kibaha – Chalinze – Morogoro *express* yenye urefu wa kilometa 205 kwa kutumia utaratibu wa kushirikisha sekta binafsi *(Public Private Partnership) (PPP)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, kuendelea na ujenzi wa miradi mikubwa ya barabara katika maeneo mbalimbali nchini yenye jumla ya kilometa 1,031.98.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, kuendelea na miradi ya ujenzi wa barabara iliyosainiwa katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 yenye jumla ya kilometa 393.6.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tano, kuendelea na ujenzi wa madaraja makuu mawili yaani Daraja la Kigongo Busisi Mkoani Mwanza na Pangani Mkoani Tanga, pamoja na kujenga madaraja mengine katika maeneo mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sita, kuanza utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa barabara zenye jumla ya kilometa 269 ambazo zinatarajiwa kusainiwa kabla ya mwisho wa mwaka huu wa fedha 2022/2023 na saba kuendelea na utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Kimataiifa Msalato pamoja na kuendelea na kazi za ukarabati na upanuzi wa viwanja vya ndege vingine katika mikoa mbalimbali hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi yote hiyo ya barabara na madaraja ikikamilika itakuwa na jumla ya kilometa 3,934.7 za barabara zilizojengwa kwa kiwango cha lami, ambazo zitaongeza urefu wa mtandao wa barabara za lami zilizopo kwa sasa, ambazo ni kilometa 11,387.82 na kufikia kilometa 15,522.52 ambazo ni sawa na ongezeko la asilimia 34.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Uchukuzi, Fungu 62; Makadirio ya Bajeti na Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo; kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Sekta ya Uchukuzi, Fungu 62 imetengewa jumla ya shilingi trilioni 2.086 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 118.215 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi trilioni 1.968 kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Mgawanyo wa fedha za maendeleo pamoja na miradi iliyotengewa fedha imeoneshwa katika kiambatisho namba sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vipaumbele vya mpango na bajeti kwa Sekta ya Uchukuzi ni kama ifuatavyo:-

(i) Mradi wa Kuwezesha Taasisi *(Institutional Support)* ambao umetengewa shilingi bilioni 18.3;

(ii) Mradi wa Uboreshaji wa Usalama wa Usafiri katika Ziwa Victoria ambao umetengewa shilingi bilioni 1.73;

(iii) Mradi wa Uboreshaji wa Bandari ya Dar es Salaam uliotengewa bilioni 93.80;

(iv) Miradi iliyotekelezwa kupitia Mfuko wa Reli imetengewa jumla ya shilingi bilioni 294.80;

(v) Mradi wa Ukarabati wa Njia Kuu ya Reli iliyopo *NGR*, Mradi wa Tanzania *Intermodal Railway* sehemu ya pili umetengewa shilingi bilioni 11.72;

(vi) Mradi wa Ujenzi wa Reli Mpya ya Kisasa ya *SGR* umetengewa shilingi trilioni 1.113;

(vii) Mradi wa Ununuzi wa Rada, Vifaa vya Ujenzi wa Miundombinu ya Hali ya Hewa umetengewa shilingi bilioni 13;

(viii) Mradi wa Uboreshaji wa Kampuni ya Ndege ya Tanzania *ATCL* umetengewa shilingi bilioni 300;

(ix) Mradi wa Ujenzi wa Meli Mpya na Ukarabati wa Meli umetengewa shilingi bilioni 100;

(x) Mradi wa Uboreshaji wa Miundombinu na Ununuzi wa Vifaa vya Kufundishia umetengewa shilingi bilioni 2.27;

(xi) Mradi wa Uboreshaji wa Reli ya *TAZARA* umetengewa shilingi bilioni 13.19; na

(xii) Mradi wa Ununuzi wa Mitambo ya Kuongezea Ndege na Uendelezaji wa Chuo cha Mafunzo ya Usafiri ya anga umetengewa shilingi bilioni 6.5.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mara nyingine tena nichukue fursa hii kuwapongeza na kutambua mchango mkubwa

unaotolewa na viongozi wenzangu katika kutekeleza majukumu ya Wizara yangu. Nikianza na Naibu Mawaziri, Mheshimiwa Mhandisi Godfrey Kasekenya, Mheshimiwa Fredy Mwakibete, Makatibu Wakuu, Balozi Mhandisi Aisha Salmini Amour ambaye anasimamia Sekta ya Ujenzi, Ndugu Gabriel Migire ambaye anasimamia Sekta ya Uchukuzi, Manaibu Katibu Wakuu nikianza na Ndugu Ludovick Nduhiye anayesimamia Sekta ya Ujenzi na Ndugu Doctor Ally Possi anayesimamia Sekta ya Uchukuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile kipekee napenda kuishukuru Menejimenti ya Wizara, Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara na watumishi wote wa Wizara na Taasisi kwa jitihada zao kubwa katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Nawashukuru sana kwa msaada wao mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Wizara naomba kutumia fursa hii kuwashukuru kwa dhati na kuwatambua wadau wote wa Wizara ikiwa ni pamoja na washiriki mbalimbali wa maendeleo ambao wamechangia kwa kiasi kikubwa katika utekelezaji wa programu, miradi na mipango mbalimbali ya Wizara. Aidha, napenda kuwatambua wafuatao:-

Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Anga, Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Majini, Shirika la Hali ya Hewa Duniani, *UNESCO*, Benki ya Maendeleo ya Afrika, Benki ya Dunia, Japan *(JICA)*, *OPEC Fund*, Korea Kusini *(KOICA)*, Abu Dhabi *Fund*, Ujerumani *(KfW)*, Shirika la Maendeleo la Ufaransa, Jumuiya ya Nchi za Ulaya, Benki ya Uwekezaji ya Ulaya, Shirika la Maendeleo la Marekani, Kuwait *(KFAED)*, *HSBC*, *TMEA*, Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, Sekretarieti ya Jumuiya ya Nchi za *SADC*, Dubai, China, Denmark, Norway, Belgium, Ujerumani na Uturuki. Mifuko yote ya Hifadhi ya Jamii na Taasisi zote za kifedha hapa nchini pamoja na Benki zote hapa nchini pamoja na taasisi mbalimbali zisizokuwa za Serikali, Sekta Binafsi pamoja na wadau wengine wote ambao sitoweza kuwataja kwa muda nilionao hapa, nasema tu nyote ahsanteni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila kumsahau mke wangu yuko pale, Profesa Eunice Mbarawa ametoa msaada mkubwa kwa

familia yangu na amefanya kazi kubwa kuijenga familia ya Mbarawa. Ahsante sana mama, tunakushukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe shukurani zangu za dhati kwanza kwako wewe mwenyewe binafsi, kwa Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika na kwa Wabunge wote kwa kusikiliza hotuba hii. Naomba pia waelewe hotuba hii inapatikana katika tovuti ya Wizara www.mwt.go.tz.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muhtasari wa maombi ya fedha ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Katika mwaka wa fedha 2023/2024 Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi inaomba kuidhinishwa jumla ya shilingi 3,554,783,957,000 kati ya fedha hizo shilingi 1,468,238,449 ni kwa ajili ya Sekta ya Ujenzi na shilingi 2,086,545,508,000 kwa ajili ya Sekta ya Uchukuzi. Mchanguo wa fedha zinazoombwa kwa kila Kifungu ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, Sekta ya Ujenzi, Fungu 98; shilingi 1,468,238,449,000 za Fungu 98 zinaombwa ambazo zinajumuisha shilingi 48,395,392,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 1,419,843,057,000 kwa ajili ya Bajeti ya Maendeleo kwa Sekta ya Ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Uchukuzi, Fungu 62; Sekta ya Uchukuzi inaombewa jumla ya shilingi 2,086,545,508,000. Kati ya fedha hizo shilingi 118,215,599,000 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi 1,968,329,909,000 kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hotuba hii nimeambatanisha miradi ya Wizara itakayotekelezwa katika mwaka wa fedha 2023/2024, kuanzia kiambatisho namba moja hadi namba sita. Naomba viambitisho hivyo vichukuliwe kama sehemu ya vielelezo vya hoja hii.

**22 MEI, 2023**

**HOTUBA YA WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI, MHESHIMIWA PROF. MAKAME MNYAA MBARAWA (MB), AKIWASILISHA BUNGENI MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2023/24 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

## A. UTANGULIZI

1. ***Mheshimiwa Spika,*** kufuatia taarifa iliyowasilishwa hapa Bungeni na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu iliyochambua utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi ya mwaka wa fedha 2022/23, ninaomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu sasa likubali kupokea na kujadili Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kwa mwaka wa fedha 2022/23. Aidha, ninaliomba Bunge lako tukufu liridhie kupitisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kwa mwaka wa fedha 2023/24.

2. ***Mheshimiwa Spika,*** awali ya yote nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kukutana leo. Ninamuomba Mwenyezi Mungu atuongoze vyema katika kujadili Hotuba hii ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi pamoja na bajeti nzima kwa ajili ya kutuwezesha kuwahudumia Watanzania wenzetu.

3. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutumia fursa hii kuungana na Bunge lako Tukufu katika kumpongeza kwa dhati Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutimiza miaka miwili katika kutuongoza kwa umahiri na mafanikio makubwa. Mheshimiwa Rais ameendelea kuweka mkazo na kipaumbele katika kuboresha na kuendeleza miundombinu na huduma za ujenzi na uchukuzi ikiwemo ujenzi wa barabara, reli ya SGR, bandari, vivuko, meli, viwanja vya ndege, ununuzi wa ndege, ujenzi wa Ofisi za Serikali na nyumba za watumishi na rada za hali ya hewa. Miradi hiyo ya miundombinu imeendelea kutekelezwa kwa kasi kubwa na hivyo kuboresha uchumi wa Taifa na wa mtu mmoja mmoja. Aidha, Umoja wa Kitaifa na Diplomasia ya Uchumi imeendelea

kuimarika na kuifanya nchi yetu kuwa kielelezo cha kuigwa na Mataifa mengine.

4. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda pia kutoa pongezi na shukrani za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Philip Isdory Mpango, Makamu wa Rais kwa namna anavyomsaidia Mheshimiwa Rais katika kuongoza nchi yetu kwa kuliletea Taifa letu maendeleo.

5. ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Kiongozi wa shughuli za Serikali hapa Bungeni, kwa uongozi wake mahiri na makini. Sote ni mashuhuda wa kazi anayoifanya katika utekelezaji wa majukumu yake ndani na nje ya Bunge.

6. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kutumia nafasi hii kukupongeza wewe binafsi kwa kazi kubwa unayoifanya ya kusimamia na kuliongoza Bunge letu Tukufu kwa weledi mkubwa. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu (Mb.), Naibu Spika kwa kuendelea kutekeleza vyema shughuli za Bunge. Vilevile, nichukue fursa hii kuwapongeza wenyeviti wa Bunge, Mhe. Najma Murtaza Giga (Mb.) na Mhe. David Mwakiposa Kihenzile (Mb.) kwa kuendelea kuaminiwa na Waheshimiwa Wabunge na kuwachagua kwa mara nyingine tena kuwa Wenyeviti wa Bunge letu. Kipekee nimpongeze Mwenyekiti mpya wa Bunge Mhe. Daniel Baran Sillo (Mb.) kwa kuchaguliwa kwa kishindo kushika nafasi hiyo muhimu. Tunawaahidi ushirikiano katika kutimiza wajibu wenu katika kumsaidia Mheshimiwa Spika kusimamia na kuliongoza Bunge letu.

7. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa heshima na taadhima, ninaomba nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuniamini katika kutekeleza majukumu yangu nikiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi tangu aliponiteua tarehe 12 Septemba, 2021. Ninaomba kumhakikishia kuwa, nitaendelea kutekeleza majukumu yangu kwa uwezo na uaminifu mkubwa ili kuliletea Taifa letu maendeleo. Ninamuahidi kuwa nitatumia weledi, maarifa na uwezo wangu wote katika kutekeleza wajibu wangu kwa ufanisi mkubwa.

8. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa namna ya pekee naomba nimpongeze Mheshimiwa Selemani Moshi Kakoso, Mbunge wa Mpanda Vijijini kwa kuchaguliwa tena kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu na Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mbunge wa Same Mashariki kwa kuchaguliwa kwa mara nyingine kuwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati. Aidha, nawapongeza Wajumbe wote walioteuliwa kuwa katika Kamati hiyo. Nichukue fursa hii kuishukuru Kamati kwa kuendelea kutoa maelekezo na ushauri wenye tija kwa Wizara yangu. Nikiri kuwa, Kamati hii imekuwa chachu ya kuongeza ufanisi katika utendaji wa Wizara. Napenda pia kuishukuru Kamati kwa uchambuzi makini iliyoufanya kwenye Taarifa ya Utekelezaji kwa mwaka wa fedha 2022/23 na Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2023/24. Maoni na ushauri wao umeiwezesha Wizara kukamilisha maandalizi ya bajeti tunayoiwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu.

9. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa masikitiko makubwa nichukue fursa hii kutoa pole nyingi kwa Bunge lako Tukufu na wote walioguswa na kifo cha Mbunge mwenzetu Mussa Hassan Mussa aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Amani, Zanzibar kupitia Chama cha Mapinduzi kilichotokea tarehe 13 Oktoba, 2022. Tutaendelea kuthamini na kuenzi mchango wake katika Bunge hili na Taifa kwa ujumla.

10. ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie fursa hii pia kutoa pole kwa familia na wananchi kwa ujumla kufuatia ajali ya ndege aina ya ATR 42-500 ya Shirika la Ndege la Precision Air iliyotokea tarehe 6 Novemba, 2022 katika Ziwa Victoria karibu na Kiwanja cha Ndege cha Bukoba kutokana na hali mbaya ya hewa. Ajali hiyo, ilisababisha maafa makubwa ambapo Watanzania 19 walipoteza maisha. Vile vile, natoa pole kwa wote waliopoteza ndugu zao kutokana na ajali za vyombo vya usafiri na matukio mengine yaliyotokea hapa nchini. Tunamuomba Mwenyezi Mungu aziweke roho za marehemu wote mahali pema peponi, Amina. Aidha, ninawaombea kwa Mwenyezi Mungu awaponye wananchi walioathirika na ajali mbali mbali ili warejee kwenye majukumu ya kustawisha maisha yao na Taifa kwa ujumla.

11. ***Mheshimiwa Spika,*** naungana na viongozi wenzangu walionitangulia kuwapongeza watoa hoja wote waliozungumza kabla yangu. Kipekee nimshukuru Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa hotuba yake ambayo ilitoa picha ya ujumla ya utendaji wa Serikali kwa mwaka 2022/23 pamoja na kuonesha dira ya mustakabali wa Taifa letu katika sekta mbalimbali ikiwemo Sekta ya Ujenzi na Uchukuzi kwa mwaka 2023/24.

12. ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya maelezo hayo ya utangulizi, naomba sasa nitoe taarifa ya mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kwa mwaka wa fedha 2022/23 pamoja na Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2023/24.

## B. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA WIZARA NA TAASISI ZAKE KWA MWAKA WA FEDHA 2022/23

13. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi imegawanywa katika mafungu mawili kibajeti yaani; Fungu 62 (Sekta ya Uchukuzi) na Fungu 98 (Sekta ya Ujenzi). Nitaanza na maelezo kuhusu utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2022/23 kwa Sekta ya Ujenzi ikifuatiwa na Sekta ya Uchukuzi.

### B.1 SEKTA YA UJENZI

### Bajeti ya Matumizi ya Kawaida

14. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2022/23, Sekta ya Ujenzi ilitengewa jumla ya **Shilingi 44,293,050,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 40,638,652,000.00** ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Wizara na Taasisi zake na **Shilingi 3,654,398,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo ya Wizara na Taasisi zake. Hadi Aprili, 2023 jumla ya **Shilingi 32,893,801,963.57,** sawa na asilimia 74.26 ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania zilikuwa zimetolewa na HAZINA kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 30,556,729,477.52** ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Wizara na Taasisi na **Shilingi**

**2,337,072,486.05** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo ya Wizara na Taasisi zake.

**Bajeti ya Miradi ya Maendeleo**

15. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa miradi ya maendeleo, katika mwaka wa fedha 2022/23, Sekta ya Ujenzi ilitengewa **Shilingi 1,377,542,185,800.00**. Kiasi hicho kinajumuisha **Shilingi 1,124,576,368,800.00** fedha za ndani na **Shilingi 252,965,817,000.00** fedha za nje. Fedha za ndani zilijumuisha fedha za Mfuko Mkuu wa Serikali (Consolidated Funds) ambazo ni **Shilingi 524,819,901,000.00** na fedha za Mfuko wa Barabara ni **Shilingi 599,756,467,800.00**Hadi Aprili, 2023 fedha zilizopokelewa ni **Shilingi 1,312,357,869,886.81** sawa na **asilimia 95.3** ya fedha zilizoidhinishwa kwa mwaka wa fedha 2022/23. Kati ya fedha hizi, **Shilingi 1,069,036,515,494.30** ni fedha za ndani na **Shilingi 243,321,354,392.51** ni fedha za nje. Kati ya fedha za ndani zilizopokelewa, **Shilingi 556,358,520,728.99** ni kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali na **Shilingi 512,677,994,765.31** ni za Mfuko wa Barabara.

16. ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie fursa hii kuipongeza na kuishukuru sana Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kulipa hati za madai kwa wakati. Aidha, kutokana na malipo hayo kufanyika kwa wakati, kasi ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo imeongezeka. Vilevile, tunaishukuru sana Serikali kwa kuendelea kutoa fedha kwa ajili ya malipo kwa Makandarasi na Washauri Elekezi ambapo katika mwaka wa fedha 2022/23 jumla ya shilingi **184,459,708,389.61** zimetolewa kwa ajili ya malipo ya madeni.

**UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO**

**Miradi ya Barabara na Madaraja**

17. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) ina jukumu la kusanifu, kujenga, kukarabati na kufanya matengenezo ya Barabara Kuu na za Mikoa zenye jumla ya **kilometa 36,760.29** kwa mujibu wa tathmini ya mwaka 2022. Katika mwaka wa fedha 2022/23, miradi ya Barabara Kuu

iliyopangwa kutekelezwa ni ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara zenye urefu wa **kilometa 470** pamoja na ukarabati kwa kiwango cha lami wa barabara zenye urefu wa **kilometa 33.** Kazi nyingine ni kuendelea na ujenzi wa madaraja makubwa matatu (3), ambayo ni Daraja la JPM (Kigongo – Busisi, Mwanza), Daraja la Pangani (Tanga) na Daraja la Wami (Pwani). Aidha, Wizara ilipanga kuanza ujenzi wa madaraja saba (7), ambayo ni Godegode (Dodoma), Sukuma (Mwanza), Mirumba (Katavi), Simiyu (Mwanza), Sanza (Singida), Mkenda (Ruvuma) na Mpiji Chini (Dar es Salaam). Vilevile, ilipanga kuanza ukarabati wa daraja moja (1) la Kirumi pamoja na kufanya Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa madaraja sita (6).

18. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili, 2023, ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara zenye urefu wa **kilometa 179.18** umekamilika na ujenzi wa **kilometa 290.82** unaendelea ambapo **kilometa 161.49** za tabaka la juu la msingi (basecourse), **kilometa 192.03** za tabaka la kati la msingi (Sub - Base) na **kilometa 259.94** za tuta la barabara zimejengwa. Aidha, ujenzi wa daraja la Wami umekamilika. Ujenzi wa madaraja mawili **(2)** ya JPM (Kigongo – Busisi, Mwanza) umefikia asilimia 72 na kwa daraja la Pangani (Tanga) ujenzi umeanza na umefikia asilimia 3. Manunuzi ya Makandarasi kwa ajili ya ujenzi wa madaraja mengine sita **(6)** yapo kwenye hatua mbalimbali. Aidha, ukarabati wa Daraja la Kirumi utaanza kulingana na upatikanaji wa fedha. Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa madaraja mawili (2) ya Mtera na Nzali umekamilika na kwa madaraja manne (4) ya Malagarasi Chini, Nguyami, Chakwale na Mbangala Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina unaendelea.

19. ***Mheshimiwa Spika,*** miradi ya barabara za mikoa iliyopangwa kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2022/23 ni ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara zenye urefu wa **kilometa 103.01** zinazohusisha **kilometa 61.82** kwa kutumia fedha za Mfuko Mkuu wa Serikali na **kilometa 41.19** kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara. Kazi nyingine ni kufanya ukarabati kwa kiwango cha changarawe wa barabara zenye urefu wa **kilometa 1,042.43** zinazohusisha **kilometa 672.77** kwa kutumia fedha za Mfuko Mkuu wa Serikali na **kilometa 369.66** kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara. Aidha, Wakala ulipanga kujenga

na kufanya ukarabati wa madaraja/makalavati **31** kwa kutumia fedha za Mfuko Mkuu wa Serikali na **44** kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara.

20. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili, 2023 jumla ya kilometa **23.11** za barabara za mikoa zilijengwa kwa kiwango cha lami na jumla ya **kilometa 253.67** zilikarabatiwa kwa kiwango cha changarawe. Aidha, utekelezaji wa miradi ya madaraja/makalavati ulifikia asilimia **88.82** ambapo madaraja madogo **40** yalijengwa kwa kutumia fedha za Mfuko Mkuu wa Serikali na madaraja madogo **26** yalijengwa kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara.

21. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Aprili, 2023 mikataba ya ujenzi/ukarabati wa miradi mbalimbali mipya ya barabara, madaraja na viwanja vya ndege ilisainiwa katika mwaka wa fedha 2022/23. Miradi hiyo ni ujenzi wa barabara za Lusahunga – Rusumo (km 92); Kitulo – Iniho (km 36.3); Sengerema – Nyehunge (km 54); Utete – Nyamwage (km 33.7); Kibondo – Mabamba (km 48); Igawa – Songwe – Tunduma Sehemu ya Uyole –Ifisi (km 29); Ibanda – Itungi Port (km 26); Kajunjumele (Iponjola) – Kiwira Port (km 6); Barabara unganishi katika daraja la Sibiti (km 24.83) na barabara ya Makongolosi – Rungwa – Itigi – Mkiwa sehemu ya Noranga – Doroto (km 6) na Itigi – Mkiwa (km 25.569). Miradi mingine ni ujenzi wa Madaraja ya Mpiji Chini na Mbambe pamoja na ujenzi wa Viwanja vya Ndege vya Kigoma na Sumbawanga. Makandarasi wengi wa miradi hii wako kwenye maandalizi ya kuanza kazi.

22. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara vilevile ilipanga kufanya matengenezo katika Barabara Kuu na Barabara za Mikoa yaliyohusisha matengenezo ya kawaida **kilometa 33,615.68,** matengenezo ya muda maalum **kilometa 4,081.7,** matengenezo ya sehemu korofi **kilometa 435.07** pamoja na matengenezo ya madaraja **3,350**. Aidha, Wizara ilipanga kuendelea na udhibiti wa uzito wa magari na eneo la hifadhi ya barabara, kazi za dharura pamoja na mradi wa matengenezo ya barabara kwa mikataba ya muda mrefu.

Hadi kufikia Aprili, 2023 kazi zilizofanyika katika Barabara Kuu na Barabara za Mikoa ni matengenezo ya kawaida **kilometa**

**23,227.58,** matengenezo ya muda maalum **kilometa 2,314.65,** matengenezo ya sehemu korofi **kilometa 274.3** pamoja na matengenezo ya madaraja **2,052**. Kwa ujumla, mpango wa matengenezo katika Barabara Kuu na za Mikoa ulikuwa umekamilika kwa asilimia 67.

23. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu udhibiti wa uzito wa magari, hadi Aprili, 2023 jumla ya magari **7,669,368** yalikuwa yamepimwa katika vituo **70** vya mizani iliyopo nchini ambapo kati ya hayo, magari **21,527** sawa na asilimia 0.28 yalikuwa yamezidisha uzito zaidi ya asilimia 5 ya uzito unaoruhusiwa. Jumla ya **Shilingi bilioni 5.478** zilikusanywa kutokana na tozo ya uharibifu wa barabara. Aidha, vibali **47,420** vilitolewa na jumla ya **Shilingi 12,323,391,709.00** zilikusanywa kutokana na tozo ya upitishaji wa mizigo maalum.

Vilevile, Wizara kupitia TANROADS ipo katika hatua mbalimbali za kujenga mizani mpya katika mtandao wa Barabara Kuu nchini ili kudhibiti uharibifu wa barabara unaosababishwa na uzidishaji uzito wa magari. Mizani hizo ni pamoja na mizani ya Rubana mkoani Mara ambapo ujenzi wa barabara za maingilio, majengo ya Ofisi na eneo la mizani unaendelea, mizani ya Matundasi katika barabara ya Chunya – Makongorosi mkoani Mbeya, mizani ya Bulamba katika barabara ya Bulamba – Kisorya mkoani Mara, mizani ya Igagala katika barabara ya Njombe - Moronga – Makete mkoani Njombe, mizani ya Mingoyo za upande wa pili mkoani Lindi itakayopima uzito wa magari yanayotoka mikoa ya Ruvuma na Mtwara, mizani ya Mdori mkoani Manyara ambayo itapima uzito wa magari yanayotoka Singida na Dodoma na mizani ya Kizengi mkoani Tabora.

24. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2022/2023, Wizara ilianza taratibu za manunuzi kwa ajili ya kuwapata Makandarasi wa kujenga barabara saba (7) kwa kiwango cha lami kwa kutumia utaratibu wa *Engineering, Procurement, Construction and Financing* (EPC + F). Barabara hizi zitafungua fursa za kiuchumi katika maeneo zinapopita na kwa Taifa kwa ujumla.

Hatua iliyofikiwa hadi sasa ni kuwa Makandarasi wa miradi yote saba wamepatikana na mikataba ya kazi za ujenzi inatarajiwa kusainiwa kabla ya mwisho wa mwezi Juni, 2023. Barabara ambazo zitajengwa kwa utaratibu huu wa EPC + F ni: -

i. Barabara ya Kidatu – Ifakara – Lupiro – Malinyi – Kilosa kwa Mpepo – Londo – Lumecha/Songea (km 435).

ii. Barabara ya Karatu – Mbulu – Haydom – Sibiti River – Lalago – Maswa (Simiyu) (km 339).

iii. Barabara ya Handeni – Kibirashi – Kijungu – Kibaya – Njoro – Olboroti – Mrijochini – Dalai – Chambalo – Chemba – Kwa Mtoro – Singida (km 460).

iv. Barabara ya Arusha – Kibaya – Kongwa Junction (km 453.42).

v. Barabara ya Masasi – Nachingwea – Liwale (km 175).

vi. Barabara ya Igawa – Songwe – Tunduma (km 218) pamoja na barabara ya mchepuo ya Uyole – Songwe yenye urefu wa kilometa 48.9, na vii. Barabara ya Mafinga – Mtwango – Mgololo (km 81).

25. ***Mheshimiwa Spika***, hii ni mara ya kwanza katika historia ya nchi yetu kuwa na miradi mikubwa yenye jumla ya kilometa 2,035 na ambayo itagharamu zaidi ya **Shilingi Trilioni 3.7** kutekelezwa kwa wakati mmoja kwa utaratibu huu.

26. ***Mheshimiwa Spika***, kuhusu ujenzi wa barabara kwa kutumia utaratibu wa kushirikisha Sekta Binafsi (Public Private Partnership - PPP), Wizara inaendelea na manunuzi ya Makandarasi kwa ajili ya ujenzi wa *Expressway* kutoka Kibaha – Chalinze – Morogoro yenye urefu wa kilometa 205.

Hadi sasa kazi inayoendelea ni uchambuzi (evaluation) wa Makandarasi waliyoonesha nia (Expression of Interest) ya kutekeleza mradi huu kwa sehemu ya kutoka Kibaha – Chalinze yenye urefu wa kilometa 78.9. Kwa sehemu ya Chalinze –

Morogoro yenye urefu wa kilometa 126.1, Mshauri Elekezi anaendelea na kazi ya Upembuzi Yakinifu.

27. ***Mheshimiwa Spika***, hii itakuwa ni mara ya kwanza katika historia ya nchi yetu kuwa na mradi mkubwa wa ujenzi wa barabara hapa nchini ambao utatekelezwa kwa utaratibu wa PPP.

28. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba sasa nieleze kwa muhtasari utekelezaji wa miradi ya barabara kwa mwaka 2022/23 hadi kufikia Aprili, 2023.

29. ***Mheshimiwa Spika,*** kazi ya Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa **Barabara ya Soni – Bumbuli – Dindira – Korogwe (km 74)** ipo katika hatua za mwisho. Zabuni kwa ajili ya kazi za ujenzi zinatarajiwa kutangazwa kabla ya Mwezi Julai, 2023.

30. ***Mheshimiwa Spika,*** katika **Barabara ya Mtwara – Newala – Masasi (km 210)**, taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mkandarasi wa ujenzi wa sehemu ya ***Mnivata – Tandahimba – Newala – Masasi (km 160)*** kwa kiwango cha lami ziko kwenye hatua za mwisho.

31. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa **Barabara ya Likuyufusi – Mkenda (km 122.50)**, taratibu za manunuzi ya kumpata Mkandarasi wa ujenzi wa barabara hii sehemu ya ***Likuyufusi – Mhukuru (km 60)*** zinaendelea ambapo mkataba unatarajiwa kusainiwa mwezi Juni, 2023.

32. ***Mheshimiwa Spika,*** taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mkandarasi wa ujenzi wa **Barabara ya Ubena Zomozi – Ngerengere (km 11)** kwa kiwango cha lami zinaendelea. Kwa sasa majadiliano na Mkandarasi yanaendelea.

33. ***Mheshimiwa Spika,*** ujenzi kwa kiwango cha lami wa **Barabara ya TAMCO – Vikawe – Mapinga (km 24),** unafanyika kwa awamu ambapo ujenzi wa kilometa 4.7 umekamilika na ujenzi wa kilometa 3.6 unaendelea na umefikia asilimia 20. Aidha, Mkataba kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii sehemu ya ***Pangani – Mapinga (km 13.59)*** kwa kiwango cha lami umesainiwa na

Mkandarasi yupo kwenye hatua ya maandalizi ya kuanza ujenzi (mobilization).

34. ***Mheshimiwa Spika,*** kazi za Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa **Barabara ya Makofia – Mlandizi (km 36.7)** zimekamilika. Serikali inaendelea kutafuta fedha za ujenzi.

35. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa **Barabara ya Musoma – Makojo – Busekela** (km 92), hadi kufikia Aprili, 2023, ujenzi wa barabara hii kwa sehemu ya ***Suguti – Kusenyi (km 5)*** umekamilika.

36. ***Mheshimiwa Spika,*** ujenzi wa **Barabara ya Kongwa Jct – Mpwapwa – Gulwe – Kibakwe (km 98)** unafanyika kwa awamu. Hadi Aprili, 2023, ujenzi wa sehemu ya ***Mpwapwa – Idilo (km 3)*** ulikuwa unaendelea na umefikia asilimia 70. Zabuni za ujenzi wa sehemu ya ***Kongwa Jct – Ngambi – Mpwapwa (km 32)*** na ***Mpwapwa – Gulwe – Kibakwe (km 46.9)*** zimetangazwa na ujenzi utaanza baada ya mikataba kusainiwa.

37. ***Mheshimiwa Spika,*** ujenzi wa **Barabara ya Muhutwe – Kamachumu – Muleba (km 54)** kwa kiwango cha lami unafanyika kwa awamu. Hadi Aprili, 2023, mradi huu unaendelea ambapo kilometa 38 zimekamilika. Aidha, ujenzi wa sehemu za ***Kamachumu – Lutenge (km 1)*** na ***Nshamba – Mlela (km 3)*** kwa kiwango cha lami umeanza.

38. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu ujenzi wa Barabara ya **Iringa – Ruaha National Park (km 104**), Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina umekamilika na Mkataba wa Mkopo nafuu kati Serikali na Benki ya Dunia umesainiwa. Aidha, zabuni za kumpata Mkandarasi wa ujenzi zinatarajiwa kutangazwa mwezi Juni, 2023.

39. ***Mheshimiwa Spika,*** ujenzi wa **Barabara ya Muheza – Amani (km 36)** unafanyika kwa awamu. Hadi Aprili, 2023, kazi za ujenzi wa **kilometa 7** zimekamilika. Aidha, ujenzi wa **kilometa 4** unaendelea na umefikia asilimia 35.

40. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu mradi wa ukarabati kwa kiwango cha lami wa **Barabara ya Mtwara – Mingoyo – Masasi (km 200),** hadi kufikia Aprili, 2023, Upembuzi Yakinifu na Usanifu

wa Kina umekamilika na Mkataba wa Mkopo nafuu kati ya Serikali na Benki ya Dunia umesainiwa. Aidha, zabuni za kumpata Mkandarasi wa ukarabati zinatarajiwa kutangazwa mwezi Juni, 2023.

41. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa **Barabara ya Kibaoni – Majimoto – Muze – Kilyamatundu (km 189)** hadi kufikia Aprili, 2023, kazi za Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya ***Kibaoni – Majimoto – Inyonga (km 152)*** zimekamilika. Aidha, kazi za ujenzi wa sehemu ya ***Ntendo – Kizungu (km 25)*** kwa kiwango cha lami zinaendelea na mradi umefikia asilimia 14 na kwa sehemu ya ***Kizungu – Muze (km 12)*** Mhandisi Mshauri anakamilisha Usanifu wa Kina baada ya kupata maoni kutoka kwa Mwajiri.

42. ***Mheshimiwa Spika,*** ujenzi wa **Daraja la Kigongo – Busisi (J.P. Magufuli) na Barabara Unganishi** unaendelea na hadi Aprili, 2023, mradi umefikia asilimia 72. Aidha, ujenzi wa **Daraja la Kitengule na Barabara Unganishi (km 18)** na **Daraja Jipya la Wami** umekamilika. Kuhusu **Daraja la Mzinga** na **Daraja la Ugalla,** Serikali inaendelea kutafuta fedha za ujenzi wa madaraja haya.

43. ***Mheshimiwa Spika,*** kazi ya Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa **Barabara ya Morogoro – Dodoma pamoja na Daraja la Mkundi** inaendelea. Aidha, katika mradi wa ujenzi wa **Barabara ya Njombe – Makete – Isyonje (km 157.4)**, hadi kufikia Aprili, 2023, ujenzi kwa kiwango cha lami umekamilika kwa sehemu ya ***Njombe – Moronga (km 53.9)*** na ***Moronga – Makete (km 53.5)***. Vilevile, ujenzi wa barabara ya ***Isyonje – Makete (km 50)*** *sehemu ya* ***Kitulo – Iniho (km 36.3)*** unaendelea na ujenzi wa sehemu ya ***Njombe – Njombe Referral Hospital (km 3)*** unaendelea kwa awamu ambapo meta 900 zimekamilika.

44. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu **Barabara ya Omugakorongo – Kigarama – Murongo (km 105),** hadi kufikia Aprili, 2023 taratibu za manunuzi ya kumpata Mkandarasi wa ujenzi sehemu ya **Businde – Murongo (km 53.4)** zinaendelea. Mkataba unatarajiwa kusainiwa mwezi Juni, 2023.

45. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa **Barabara ya Nanganga – Ruangwa – Nachingwea (km 145)**, hadi kufikia Aprili, 2023 ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu ya ***Nanganga – Ruangwa (km 53.2)*** umefikia asilimia 59. Aidha, taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mkandarasi wa sehemu ya ***Ruangwa – Nachingwea (km 55.7)*** zinaendelea**.** Kwa sehemu ya ***Nangurukuru – Liwale (km 210),*** kazi za Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina zinaendelea na zitakamilika mwishoni mwa mwezi Juni, 2023.

46. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Aprili 2023, ujenzi kwa kiwango cha lami wa **Barabara ya Mpemba – Isongole (km 50.3)** umekamilika. Aidha, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu ya **Ruanda – Iyula – Nyimbili (km 21)** baada ya Upembuzi – Yakinifu na Usanifu wa Kina kukamilika**.** Aidha, taratibu za kumpata Mkandarasi wa ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya **Katumbasongwe – Kasumulu – Ngana – Ileje (km 90.1)** zinaendelea. Mkataba unatarajiwa kusainiwa mwezi Juni, 2023.

47. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa **Barabara ya Uyogo – Nyamilangano – Nyandekwa – Kahama (km 54)** baada ya Upembuzi – Yakinifu na Usanifu wa Kina kukamilika. Aidha, kuhusu ujenzi kwa kiwango cha lami wa **Barabara ya Sengerema – Nyehunge (km 54)** Mkataba wa ujenzi umesainiwa mwezi Aprili 2023.

48. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa **Barabara ya Omurushaka – Nkwenda – Murongo (km 125)** mkataba wa ujenzi wa sehemu ya ***Kyerwa – Chonyonyo (km 50***) utasainiwa kabla ya mwezi Julai, 2023. Aidha, taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina kwa sehemu iliyobaki ya kilometa 75 zinaendelea. Mkataba utasainiwa mwezi Juni, 2023.

49. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Aprili, 2023 katika mradi wa **Upanuzi wa Barabara Kuu zinazoingia katikati ya Jiji la Dodoma (Widening up of Dodoma Outer Roads Sections km 220)** kazi za Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina kwa ajili ya upanuzi wa barabara hizo zinazoingia katikati ya Jiji la Dodoma (km 220)

zinazohusisha barabara za ***Dodoma – Morogoro (km 70), Dodoma – Iringa (km 50), Dodoma – Singida (km 50)*** na ***Dodoma – Arusha (km 50)*** zilikuwa zinaendelea. Kwa upande wa barabara ya Morogoro - Dodoma Mhandisi Mshauri amewasilisha rasimu ya usanifu wa kina kwa ajili ya mapitio na kwa barabara za Dodoma – Iringa (km 50), Dodoma – Singida (km 50) na Dodoma – Arusha (km 50) Mhandisi Mshauri anakamilisha rasimu ya usanifu wa kina. Aidha, Serikali inaendelea na majadiliano ya maandalizi ya kupata fedha za mkopo wenye masharti nafuu kutoka Benki ya Dunia kwa ajili ya upanuzi wa barabara hizi kwa kuanzia sehemu za ndani ya mji wa Dodoma chini ya mradi wa *Dodoma Intergrated and Sustainable Transport project* (DIST)

50. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu ujenzi kwa kiwango cha lami wa **Barabara ya Ntyuka Jct – Mvumi Hospital – Kikombo Jct (km 76.07)** hadi Aprili, 2023 ujenzi wa barabara hii sehemu ya ***Ntyuka Jct – Ntyuka (km 8)*** na ***Kikombo Jct – Mapinduzi (km 16.4)***, unaendelea na umefikia asilimia 6.5. Aidha, zabuni za kumpata Mkandarasi wa Ujenzi wa barabara ya ***Ntyuka – Kikombo (km 56)*** imetangazwa.

51. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa mradi wa ujenzi wa **Barabara ya Tarime – Mugumu (km 86)** kwa kiwango cha lami, ujenzi wa barabara hii sehemu ya ***Mogabiri – Nyamongo (km 25)*** unaendelea na umefikia asilimia 8. Aidha, majadiliano na mzabuni aliyeshinda zabuni ya kazi za ujenzi wa sehemu ya ***Nyamongo – Mugumu (km 61)*** yanaendelea. Mkataba unatarajiwa kusainiwa mwezi Juni, 2023.

52. ***Mheshimiwa Spika,*** kazi ya Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina kwa ajili ya ukarabati kwa kiwango cha lami wa **Barabara ya Shelui – Nzega (km 110)** inaendelea na Mhandisi Mshauri amewasilisha rasimu ya uchambuzi wa kiuchumi kwa ajili ya mapitio.

53. ***Mheshimiwa Spika,*** Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa **Barabara ya Nzega – Kagongwa (km 65)** na **Barabara ya Isabdula (Magu) – Bukwimba Station – Ngudu – Ng'hungumalwa (km 50)** umekamilika. Ujenzi kwa kiwango cha lami utaanza kulingana na upatikanaji wa fedha.

54. ***Mheshimiwa Spika,*** Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya **Nyololo – Mtwango (km 40.4)** umekamilika. Ujenzi wa barabara hii utaanza kulingana na upatikanaji wa fedha.

55. ***Mheshimiwa Spika,*** taratibu za kumpata mkandarasi wa ujenzi kwa kiwango cha lami wa **Barabara ya Singida – Sepuka – Ndago (km 75.0**) zinaendelea na zipo kwenye hatua za tathmini ya zabuni.

56. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu mradi wa ujenzi kwa kiwango cha lami wa **Barabara ya Kitai – Lituhi (km 90.0) pamoja na daraja la Mnywamaji,** ujenzi wa barabara hii sehemu ya ***Amanimakoro – Ruanda (km 35)*** unaendelea na umefikia asilimia 22. Aidha, taratibu za kumpata Mkandarasi wa ujenzi wa sehemu ya ***Ruanda – Ndumbi Port (km 50)*** zinaendelea na mkataba unatarajiwa kusainiwa mwezi Juni, 2023.

57. ***Mheshimiwa Spika,*** taratibu za manunuzi kwa ajili ya ujenzi wa **Barabara za Kuelekea Katika Vituo vya Reli ya Kisasa ya SGR (km 87.6)** zinaendelea. Barabara hizo ni Morogoro – Kihonda SGR Station (km 10), Rudewa – Kilosa SGR Station (km 3), Gulwe – Gulwe SGR Station (km 2), Igandu – Igandu SGR Station (km 27), Ihumwa – Ihumwa Marshalling Yard (km 5.50), Kizota – Zuzu SGR Station (km 14), Bahi – Bahi SGR Station (km 4), Mlandizi – Ruvu SGR Station (km 22) na barabara za ndani za kituo cha SGR cha Dodoma (Access Roads to Dodoma SGR Station).

58. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Aprili, 2023 katika Barabara ya **Tanga – Pangani – Makurunge (km 174.5),** ujenzi wa sehemu ya ***Tanga – Pangani (km 50)*** unaendelea na umefikia asilimia 62. Ujenzi wa sehemu ya ***Pangani – Mkange (km 124.5)*** sehemu ya Tungamaa – Mkange (km 95.2) umefikia asilimia 19.20 na ujenzi wa ***Daraja la Pangani*** umefikia asilimia 2.

59. ***Mheshimiwa Spika,*** ujenzi wa **Barabara ya Kisarawe – Maneromango – Mloka (km 150.46)** sehemu ya ***Kisarawe - Maneromango (km 54)*** unafanyika kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha. Hadi Aprili, 2023 kilometa 20.1 sehemu ya

***Kisarawe – Kisanga*** zimekamilika na ujenzi wa kilometa 3.4 sehemu ya ***Kisanga – Sungwi*** umefikia asilimia 30. Aidha, kwa Sehemu ya ***Sungwi – Maneromango*** ujenzi utaendelea kulingana na upatikanaji wa fedha.

60. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu **Barabara ya Geita – Bulyanhulu – Kahama (km 120),** hadi kufikia Aprili, 2023 maandalizi ya kuanza ujenzi wa sehemu ya ***Bulyanhulu Jct – Kahama (km 61.7)*** yalikuwa yamekamilika na zabuni za kazi za ujenzi zinatarajiwa kutangazwa mwisho wa mwezi Mei, 2023. Mradi huu utatekelezwa kwa ushirikiano wa Serikali na Kampuni ya Uchimbaji Madini ya Barrick. Aidha, kwa sehemu ya ***Geita – Bulyanhulu Jct (km 58.3)*** kazi ya mapitio ya Usanifu inaendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami utagharamiwa na Serikali.

61. ***Mheshimiwa Spika,*** kazi ya Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa **Barabara ya Nyamirembe Port – Katoke (km 50)** na sehemu ya ***SIDO – Chato Zonal Hospital (km 5.3***) na ***Chato Ginery – Bwina (km 8.1)*** zimekamilika. Ujenzi wa barabara hizi utaanza kulingana na upatikanaji wa fedha. Aidha, zabuni za kumpata Mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa **Barabara ya Geita – Nzera (km 54)** sehemu ya ***Nzera – Nkome (km 20)*** kwa kiwango cha lami zimefunguliwa tarehe 11 Mei, 2023 na tathmini ya zabuni inaendelea. Mkataba unatarajiwa kusainiwa mwezi Juni, 2023.

62. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu **Barabara ya Arusha – Moshi – Himo – Holili (km 199.51)**, hadi kufikia Aprili 2023, ujenzi wa barabara ya ***Kijenge – Usa River (Nelson Mandela AIST - km 20)*** unaendelea na umefikia asilimia 95 na kwa barabara ya ***Mianzini – Ngaramtoni (km 18)*** ujenzi kwa kiwango cha lami umefikia asilimia 24. Aidha, taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri kwa ajili ya kazi ya Usanifu wa Kina wa barabara ya ***Tengeru – Moshi – Himo na Mizani ya Himo (km 105)*** zinaendelea.

63. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mradi wa ujenzi wa **Barabara za Kuelekea Kwenye Mradi wa Kufua Umeme Katika Maporomoko ya Mto Rufiji,** hadi Aprili, 2023, taratibu za manunuzi ya kumpata Mkandarasi wa ujenzi wa sehemu ya ***Bigwa – Matombo – Mvuha – Kisaki (km 78)*** kwa kiwango cha lami zinaendelea na

zinatarajiwa kukamilika ifikapo Juni, 2023. Mkataba unatarajiwa kusainiwa mwezi Juni, 2023. Aidha, taratibu za manunuzi ya Mhandisi Mshauri wa kufanya kazi ya Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa barabara ya ***SGR Station – Mvuha – Kisaki – Mtemele Jct (km 159)*** kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami zinaendelea na mkataba unatarajiwa kusainiwa kabla ya mwisho wa mwezi Juni, 2023. Vilevile, kazi za matengenezo kwa kiwango cha changarawe wa barabara ya ***Maneromango – Vikumburu – Mloka (km 100)*** na ***Kibiti – Mloka – Mtemele – Rufiji JNHHP (km 203)*** zinaendelea.

64. ***Mheshimiwa Spika,*** kazi za ukarabati (overlay) wa sehemu ya ***Mlandizi – Chalinze (km 44)*** zinaendelea ikiwa ni mpango wa Serikali kuifanya barabara hii ipitike kabla ya kujenga barabara ya kiwango cha *Expressway* kwa utaratibu wa *PPP*. Vilevile, ujenzi wa barabara ya ***Kwa Mathias (Morogoro Road) – Msangani (km 8.3***) unafanyika kwa awamu ambapo ujenzi wa kilometa 3 umekamilika na ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu ya kilometa 5.3 unaendelea. ***Maboresho ya maeneo hatarishi Morogoro na Pwani*** na Ujenzi wa ***Kituo cha Pamoja cha Ukaguzi (One Stop Inspection Station – OSIS) cha Vigwaza*** yamekamilika. Ukarabati kwenye ***Barabara ya Msoga – Msolwa (Chalinze Bypass)*** unaendelea kufanyika kwa awamu.

65. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa **Barabara ya Wazo Hill – Bagamoyo – Msata (km 118.10),** Serikali inaendelea kutafuta fedha za ukarabati wa sehemu ya ***Tegeta – Bagamoyo (km 46.9)*** na ujenzi wa barabara ya ***Mbegani – Bagamoyo (km 7.2)*** kwa kiwango cha lami baada ya Usanifu wa Kina wa barabara hizi kukamilika.

66. ***Mheshimiwa Spika,*** ujenzi wa Barabara za ***Usagara – Geita – Buzirayombo – Kyamyorwa (km 310), Uyovu – Bwanga (km 43) na Bwanga – Biharamulo (km 67)*** umekamilika. Aidha, kazi za Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa Barabara za ***Nyakahura – Kumubuga – Rulenge – Kabanga Nickel (km 141)*** kwa sehemu za ***Rulenge – Kabanga Nickel (km 32), Kumubuga – Rulenge – Murusagamba (km 75)*** na ***Nyakahura – Kumubuga – Murusagamba (km 34)*** zimekamilika na Serikali inaendelea kutafuta fedha za ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara hizi**.**

67. ***Mheshimiwa Spika,*** katika **Barabara ya Kigoma – Kidahwe – Uvinza – Kaliua – Tabora (km 429),** miradi iliyokamilika ni ujenzi wa sehemu za ***Tabora – Ndono (km 42)***, ***Ndono – Urambo (km 51.98), Chagu – Malagarasi (km 48), Kaliua – Kazilambwa (km 56), Kigoma – Kidahwe – Uvinza (km 115.92)*** na ***Urambo – Kaliua (km 28).*** Aidha, hadi Aprili, 2023 ujenzi wa sehemu ya ***Kazilambwa – Chagu (km 36)*** umefikia asilimia 74.4 na ujenzi wa sehemu ya ***Uvinza – Malagarasi (km 51.1)*** umefikia asilimia 26. Vilevile, ujenzi wa ***Urambo Roundabout*** unaendelea na umefikia asilimia 60.

68. ***Mheshimiwa Spika,*** katika **Barabara ya Ifakara – Kihansi – Mlimba – Madeke – Kibena (km 346.43),** taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mkandarasi wa ujenzi kwa kiwango cha lami sehemu za ***Ifakara – Mbingu (km 62.5)*** na ***Mbingu – Chita JKT (km 37.5)*** zinaendelea na Mkataba unatarajiwa kusainiwa mwezi Juni, 2023. Aidha, taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa sehemu ya ***Kihansi – Mlimba – Taweta – Madeke – Lupembe – Kibena (km 220)*** kwa ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) zipo katika hatua za mwisho kukamilika.

69. ***Mheshimiwa Spika,*** katika **Barabara ya Karatu – Mbulu – Haydom – Sibiti River – Lalago – Maswa (km 389**), kazi za ujenzi wa sehemu ya ***Mbulu – Garbabi (km 25***) zinaendelea. Aidha, majadiliano na Mkandarasi aliyeshinda zabuni ya ujenzi kwa kiwango cha lami sehemu ya ***Labay – Haydom (km 25)*** yanaendelea.

70. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu **Barabara ya Marangu – Tarakea – Rongai – Kamwanga /Bomang'ombe – Sanya Juu (km 105.16),** kazi za ujenzi zimekamilika kwa sehemu ya ***Marangu – Rombo Mkuu – Tarakea (km 64), Sanya Juu – Kamwanga (sehemu ya Sanya Juu – Elerai, km 32), KIA –Mererani (km 26)*** na ***Kwa Sadala – Masama – Machame Junction (km 16).*** Kwa upande wa barabara ya ***Kiboroloni – Kiharara – Tsuduni – Kidia (km 10.8)*** ujenzi unaendelea kwa awamu. Aidha, taratibu za manunuzi ya Mkandarasi wa ujenzi wa sehemu ya ***Sanya Juu – Kamwanga (Elerai – Kamwanga: km 44)*** zinaendelea na zabuni zitafunguliwa tarehe 01 Juni, 2023 na Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya

***Tarakea – Holili (km 53)*** unaendelea na rasimu ya usanifu wa kina imewasilishwa kwa ajili ya mapitio. Vilevile, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ukarabati wa sehemu ya ***Bomang'ombe – Sanya Juu (km 25).***

71. ***Mheshimiwa Spika,*** katika **Barabara ya Tukuyu – Mbambo – Katumba (km 60.6),** hadi Aprili, 2023 ujenzi wa sehemu ya ***Bujesi – Mbambo (km 26)*** unaendelea na umefikia asilimia 95. Taratibu za manunuzi ya Mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa sehemu za ***Katumba – Lupaso (km 35.3)*** na ***Mbaka – Kibanja (km 20.7)*** zinaendelea na mkataba unatarajiwa kusainiwa mwezi Juni, 2023**.** Aidha, kazi za Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu ya ***Mbambo – Ipinda (km 19.7)*** zimekamilika ambapo kwa sasa Serikali inaendelea na juhudi za kutafuta fedha za ujenzi.

72. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi wa ujenzi wa **Barabara ya Dodoma – Manyoni (km 127) na Barabara ya Kuingia Manyoni Mjini (km 4.8)** umekamilika lakini mradi huu pia unahusisha ujenzi wa ***Kituo cha Pamoja cha Ukaguzi (One Stop Inspection Station – OSIS) cha Muhalala (Manyoni).*** Mkataba wa awali wa utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa ***OSIS*** umesitishwa kutokana na changamoto za kimkataba ambapo utekelezaji wake ulikuwa umefikia asilimia 50. Ujenzi utaendelea baada ya kumpata Mkandarasi mpya wa kumalizia kazi hizo.

73. ***Mheshimiwa Spika,*** Usanifu wa Kina wa **Barabara ya Tabora – Mambali – Bukene – Itobo** (km 114) umekamilika. Aidha, kazi ya Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa **Barabara ya Namanyere – Katongoro – New Kipili Port (km 64.8)** imekamilika na Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara hizi.

74. ***Mheshimiwa Spika,*** katika **Barabara ya Dumila – Kilosa – Mikumi (km 141),** ujenzi wa sehemu ya **Dumila – Rudewa (km 45)** umekamilika na ujenzi wa sehemu ya ***Rudewa – Kilosa (km 24)*** unaendelea na umefikia asilimia 93. Aidha, Usanifu wa Kina wa Sehemu ya ***Kilosa – Ulaya – Mikumi (km 72)*** umekamilika na kwa sasa Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami.

75. ***Mheshimiwa Spika,*** ujenzi wa **Barabara ya Sumbawanga – Matai – Kasanga Port (km 107)** umekamilika. Aidha, ujenzi wa barabara ya ***Matai – Kasesya (km 50)*** sehemu ya ***Matai – Tatanda (km 25)*** unaendelea na umefikia asilimia 12 na Mkataba wa ujenzi wa sehemu ya ***Tatanda – Kasesya (km 25***) unatarajiwa kusainiwa hivi karibuni.

76. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kutekeleza mradi wa **Ujenzi wa Madaraja Makubwa** ambapo hadi Aprili, 2023, ujenzi wa daraja la Mpwapwa ulikuwa umekamilika. Aidha, Mkandarasi wa ujenzi wa barabara unganishi katika Daraja la Sibiti (Singida) amepatikana na yupo katika maandalizi ya kuanza kazi za ujenzi. Usanifu wa kina wa daraja la Mirumba (Katavi), Simiyu (Simiyu), Sanza (Singida), Mpiji Chini (Dar es Salaam), Mkenda na Mitomoni (Ruvuma) umekamilika. Usanifu wa kina wa daraja la Malagarasi Chini (Kigoma) unaendelea. Vilevile, taratibu za manunuzi ya Makandarasi wa ujenzi wa madaraja ya Mirumba, Simiyu, Sanza, Godegode, Mitomoni na Mkenda zinaendelea na kwa daraja la Mpiji Chini mkataba wa ujenzi umesainiwa.

77. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ukarabati wa Daraja la Kirumi (Mara) pamoja na ujenzi wa madaraja ya Mitomoni (Ruvuma) na Mtera, Nzali, Kibakwe, Kerema na Munguli yaliyopo Dodoma.

78. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu mradi wa **Barabara ya New Bagamoyo (Kawawa Jct – Tegeta km 18.3)** kazi za upanuzi wa sehemu ya ***Morocco – Mwenge (km 4.3)*** zimekamilika.

79. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu **Barabara ya Kyaka – Bugene – Kasulo** (**km 183.10),** ujenzi wa sehemu ya ***Bugene – Kasulo – Kumunazi & Kyaka – Mutukula (km 124)*** sehemu ya ***Bugene – Burigi Chato National Park (km 60)*** unaendelea na umefikia asilimia 12. Aidha ujenzi wa sehemu ya ***Kyaka – Bugene (km 59.10)*** umekamilika.

80. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mradi wa **Barabara ya Isaka – Lusahunga (km 242),** kazi za ukarabati wa sehemu ya ***Ushirombo***

***– Lusahunga (km 110)*** zimekamilika. Mkandarasi wa ukarabati kwa kiwango cha lami wa sehemu ya ***Lusahunga – Rusumo (km 92)*** yupo katika hatua ya maandalizi ya kuanza kazi (mobilization). Kwa upande wa ujenzi wa ***Kituo cha Ukaguzi wa Pamoja (OSIS) cha Nyakanazi,*** mkataba wa awali umesitishwa kutokana na changamoto za kimkataba na ujenzi utaendelea baada ya kumpata Mkandarasi mpya wa kumalizia kazi hizo. Aidha, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu ya ***Nyakasanza – Kobero (km 58***).

81. ***Mheshimiwa Spika,*** ujenzi wa **Barabara ya Manyoni – Itigi – Tabora (km 259.75)** umekamilika. Kuhusu ukarabati wa **Barabara ya Mwanza/Shinyanga Border – Mwanza (km 102)** kwa kiwango cha lami, kazi za Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina umekamilika.

82. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2022/23, kazi zilizopangwa kutekelezwa kwa ajili ya miradi ya **Barabara za Mikoa** ni ukarabati kwa kiwango cha changarawe wa kilometa **672.77**, ujenzi kwa kiwango cha lami wa kilometa **61.82** na ujenzi wa Madaraja/Makalavati **31.** Hadi kufikia Aprili 2023, kilometa **253.67** za mikoa zilikuwa zimekarabatiwa kwa kiwango cha changarawe na kilometa **23.11** zimejengwa kwa kiwango cha lami. Aidha, ujenzi wa madaraja ulikamilika kwa asilimia 88.82.

83. ***Mheshimiwa Spika,*** katika **mradi wa barabara za kupunguza msongamano wa magari katika jiji la Dar es Salaam**, mradi uliokamilika kwa mwaka 2022/23 ni ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Ardhi – Makongo – Goba (sehemu ya Ardhi **–** Makongo MM 5). Ujenzi wa barabara ya Goba – Matosa – Temboni (km 6) unaendelea kufanyika kwa awamu ambapo kilometa moja (1) imekamilika. Taratibu za kumpata mkandarasi wa kipande kingine cha barabara hii zinaendelea. Aidha, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa upanuzi wa barabara ya Mwai Kibaki (km 9) na ujenzi wa barabara za Mjimwema – Kimbiji – Pembamnazi (km 27), Kongowe – Mjimwema – Kivukoni Ferry (km 25.1) na Kibamba – Kisopwa – Kwembe – Makondeko (km 14.66) sehemu ya Mloganzila – Kisopwa – Kwembe – Makondeko (km 10.66).

84. ***Mheshimiwa Spika,*** ujenzi wa barabara ya **Nyamuswa – Bunda – Kisorya (km 107.4)** umekamilika. Vilevile, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa **Barabara ya Kolandoto – Lalago – Ng'oboko – Mwanhuzi (km 122*)*** kwa awamu.

85. ***Mheshimiwa Spika,*** ujenzi kwa kiwango cha lami wa **Barabara ya Ndundu – Somanga (km 60)** umekamilika. Mkataba wa ujenzi wa ***barabara ya Utete – Nyamwage (km 33.7)*** na ujenzi wa ***daraja la Mbambe (m 81)*** katika ***barabara ya Ikwiriri – Mkongo (km 95)*** umesainiwa. Aidha, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ukarabati wa sehemu za ***Kongowe – Malendego (km 160.65)*** na ***Nangurukuru – Mbwemkuru (km 95)***.

86. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili 2023, utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa ***Barabara ya Kasulu – Manyovu pamoja na barabara za kuingia Kasulu Mjini (km 68)*** ulikuwa unaendelea na umefikia asilimia 46.

87. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu mradi wa **Barabara ya Mzunguko katika Jiji la Dodoma (Dodoma City Outer Dual Carriageway Ring Road Lot1 & 2 - km 112.3),** hadi Aprili, 2023 ujenzi wa sehemu ya ***Nala – Veyula – Mtumba – Ihumwa Dry Port (km 52.3)*** unaendelea na umefikia asilimia 25 na ujenzi wa sehemu ya ***Ihumwa Dry Port – Matumbulu – Nala (km 60)*** umefikia asilimia 19.

88. ***Mheshimiwa Spika,*** Kuhusu ujenzi kwa kiwango cha lami wa ***barabara ya Mzunguko wa Ndani katika Jiji la Dodoma: Bahi R/About – Image R/About – Ntyuka R/About – Makulu R/About (km 6.3)*** kazi ya Upembuzi na usanifu wa kina imekamilika. Taratibu za kukamilisha mkopo kutoka Serikali ya Japan kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii zinaendelea. Aidha, kazi ya Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa ***Dodoma City Middle Ring Road*** inayoanzia ***Nanenane – Miyuji – Mnadani Sekondari – Mkonze – Ntyuka – Nanenane (km 47.2)*** inaendelea.

89. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa barabara ya **Kidatu – Ifakara – Lupiro – Malinyi – Londo – Lumecha/Songea (km 499),** hadi Aprili 2023, kazi za ujenzi kwa sehemu ya ***Kidatu – Ifakara (km***

***66.9)*** zilikuwa zinaendelea na zimefikia asilimia 77. Vilevile, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya ***Chalinze – Magindu – Lukenge – Seregete B – Kabwe Jct – Mkulazi (km 77.50).*** Ukarabati kwa kiwango cha changarawe wa barabara ya ***Dakawa Jct – Mbigiri (km 7***) umekamilika na ujenzi wa barabara za kuelekea mashamba ya wakulima wa miwa ya Mbigiri (km 50) unaendelea na umefikia asilimia 60.

90. ***Mheshimiwa Spika,*** utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa **Barabara ya Tabora – Ipole – Koga – Mpanda (km 365.36)** umekamilika. Aidha, katika **Barabara ya Makutano – Natta – Mugumu/Loliondo – Mto wa Mbu (km 185**), hadi Aprili 2023, kazi za ujenzi wa sehemu ya ***Waso – Sale (km 49)*** na ***Makutano – Natta (Sanzate) (km 50)*** zilikuwa zimekamilika na kwa sehemu ya ***Sanzate – Natta (km 40)*** ujenzi umefikia asilimia 32. Maandalizi ya ujenzi kwa awamu wa barabara ya ***Natta – Mugumu (km 35)*** yanaendelea. Aidha, manunuzi ya kumpata Mkandarasi wa ujenzi wa barabara ya Wasso – Loliondo (km 10.0) yanaendelea na Mkataba utasainiwa mwezi Juni, 2023.

91. ***Mheshimiwa Spika,*** katika ***Barabara ya Ibanda – Itungi Port/Kajunjumele – Kiwira Port (km 32.0),*** kazi za ujenzi wa sehemu ya ***Kikusya – Ipinda – Matema (km 39.1)*** na ukarabati wa barabara ya ***Uyole – Kasumulu,*** sehemu ya ***Ilima Escarpment (km 3)*** zimekamilika. Ujenzi wa ***Kasumulu/ Songwe – Tanzania/Malawi Border OSBP*** unaendelea na umefikia asilimia 88.45. Aidha, Mkandarasi wa kazi za ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu ya ***Ibanda – Itungi Port (km 26) na Kajunjumele (Iponjola) – Kiwira Port (km 6)*** yuko katika maandalizi ya kuanza ujenzi.

92. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu **Barabara ya *Sumbawanga – Mpanda – Nyakanazi* (km 803.6),** ujenzi wa sehemu za ***Sumbawanga – Kanazi – Kizi – Kibaoni (km 151.6), Sitalike – Mpanda – Ifukutwa – Vikonge (km 73.65)*** umekamilika. Aidha, ujenzi wa barabara ya ***Mpanda – Mishamo – Uvinza; Sehemu ya Vikonge – Uvinza (km 159)*** kazi za ujenzi wa barabara hii sehemu ya ***Vikonge – Luhafwe (km 25)*** zinaendelea na zimefikia asilimia 11 na Mkataba wa ujenzi wasehemu ya ***Luhafwe – Mishamo/Bulamata Jct (km 37.35)*** unatarajiwa kusainiwa hivi karibuni. Kwa barabara ya ***Kibaoni – Sitalike (km 71)*** sehemu ya

Kibaoni – Mlele Jct (Km 50) ujenzi umefikia asilimia 5 na taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mkandarasi wa ujenzi wa sehemu ya ***Sitalike – Mlele Jct (km 21)*** zinaendelea ambapo tarehe 26 Aprili, 2023 *pre – qualification tenders* zilifunguliwa. Kwa barabara ya ***Kagwira – Ikola – Karema Port (km 112)*** zabuni za ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami zimetangazwa. Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa sehemu ya ***Kizi – Lyambalyamfipa – Sitalike (km 86) na Lyazumbi – Kabwe (km 65).***

93. ***Mheshimiwa Spika,*** katika **Barabara ya Nyanguge – Musoma/ Mchepuo wa Usagara – Kisesa (km 202.25)** ujenzi wa sehemu ya ***Usagara – Kisesa (Mwanza Bypass, km 16.35), upanuzi wa barabara ya kuelekea uwanja wa Ndege wa Mwanza (km 12) na Daraja la Furahisha*** pamoja na ukarabati wa sehemu ya ***Simiyu/Mara Border – Musoma (km 85.5)*** umekamilika. Aidha, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ukarabati wa Barabara ya ***Nyanguge – Simiyu/Mara Border (km 100.4)***.

94. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu **Barabara ya Magole – Mziha – Handeni (km 152.8),** mradi umekamilika kwa sehemu ya ***Magole – Turiani (km 45.2)***. Aidha, hadi kufikia Aprili, 2023, Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa sehemu ya ***Turiani – Mziha – Handeni (km 104)*** ulikuwa umekamilika na Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami.

95. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mradi wa **Ujenzi wa Barabara za Juu (Flyovers) Jijini DSM na Barabara Unganishi,** ujenzi wa flyover ya ***Mbezi Mwisho*** umekamilika. Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kufanya maboresho ya ***Makutano ya barabara kwenye maeneo ya KAMATA, Magomeni, Mwenge, Tabata/ Mandela, Fire, Selander (Ali Hassan Mwinyi/ UN Roads JCT), Buguruni na Morocco).*** Aidha, kazi za usanifu wa *flyover* za Fire na Magomeni zinaendelea.

96. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu **Barabara ya Mwigumbi – Maswa – Bariadi – Lamadi (km 181.8),** mradi umekamilika kwa sehemu za ***Bariadi – Lamadi (km 71.8), Mwigumbi – Maswa (km 50.3) na Maswa – Bariadi (km 49.7***). Aidha, hadi Aprili, 2023 ujenzi wa

barabara ya ***Mchepuo wa Maswa (km 11*)** unaendelea na umefikia asilimia 97.

97. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Aprili 2023, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa **Barabara ya Tabora – Ipole – Rungwa (*Sehemu ya Ipole – Rungwa, km 172)***. Aidha, katika **Barabara ya Kidahwe – Kasulu – Kibondo – Nyakanazi (km 341.25),** ujenzi wa sehemu ya ***Kidahwe – Kasulu (km 63)*** na ***Nyakanazi – Kakonko (Kabingo) (km 50)*** umekamilika. Ujenzi wa sehemu ya ***Kanyani Junction – Mvugwe (km 70.5)*** umefikia asilimia 56.00, ***Mvugwe –Nduta Junction (km 59.35)*** umefikia asilimia 66.00, ***Kibondo Junction – Kabingo (km 62.5)*** umefikia asilimia 77.00 na ***Nduta Junction – Kibondo (km 25.9)*** umefikia asilimia 58.00. Vilevile, Mkandarasi anaendelea na maandalizi ya kuanza kazi ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya ***Kibondo – Mabamba (km 48)***.

98. ***Mheshimiwa Spika,*** kazi za ujenzi wa **Barabara ya Kwenda Kiwanja cha Ndege cha Mafia (km 16)** zimekamilika. Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa sehemu ya ***Kilindoni – Ras Mkumbi (km 54.4)*** baada ya Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa barabara hii kukamilika.

99. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu mradi wa ujenzi wa **Daraja la Nyerere (Kigamboni) na Barabara Unganishi (km 46.3),** ujenzi wa ***Daraja la Nyerere,*** barabara ya ***Kigamboni (Daraja la Nyerere) – Vijibweni (km 1.5)*** na barabara ya ***Tungi – Kibada (km 3.8)*** umekamilika. Aidha, hadi Aprili, 2023 taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mkandarasi wa ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya ***Kibada – Mwasonga – Tundwisongani Jct/Tundwisongani – Kimbiji (Km 41)*** zilikuwa zinaendelea na mkataba unatarajiwa kusainiwa mwezi Julai, 2023.

100. ***Mheshimiwa Spika,*** **Barabara ya Mutukula – Bukoba – Muhutwe – Kagoma (km 215.8)** hadi Aprili, 2023 kazi za Upembuzi Yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya ***Kanazi (Kyetema) – Ibwera – Katoro – Kyaka II (km 60.7)*** zimekamilika. Aidha, taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina kwa ajili ya ukarabati kwa kiwango cha lami wa barabara za ***Mutukula – Bukoba – Muhutwe***

***– Kagoma (km 112)*** na ujenzi wa barabara ya ***Bukoba – Busimbe – Maluku – Kanyangereko – Ngongo (km 19.1)*** zinaendelea na Mkataba unatarajiwa kusainiwa mwezi Juni, 2023.

101. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu mradi wa upanuzi wa **Barabara ya Kimara – Kibaha (km 19.2) ikijumuisha Upanuzi wa Madaraja ya Kibamba, Kiluvya na Mpiji**, upanuzi wa barabara hii unaendelea. Hadi Aprili, 2023 mradi umefikia asilimia 86.00 baada ya nyongeza ya kazi za mkataba. Aidha, Serikali inaendelea kutafuta fedha za ujenzi wa **Barabara ya Kisarawe – Mlandizi (Km 119)** kwa kiwango cha lami.

102. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu mradi wa ujenzi wa **Barabara ya Pugu – Kifuru – Mbezi Mwisho – Mpiji Magoe – Bunju (Km 34)**, hadi kufikia Aprili, 2023 kazi za Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa barabara za ***Bunju – Kibamba – Pugu Kajiungeni – Mzinga – Tuangoma – Kigamboni (km 61.0)*** na ***Mbezi – Mbezi Mwisho – Kifuru – Banana – Kipara – Kigamboni (km 49.0)*** zinaendelea na zinatarajiwa kukamilika mwezi Aprili, 2024.

103. ***Mheshimiwa Spika,*** katika **Barabara ya Singida – Shelui (km 110)** Usanifu wa Kina kwa ajili ya ukarabati kwa kiwango cha lami unaendelea. Aidha, Serikali inaendelea kutafuta fedha za ujenzi wa ***Barabara ya Ulemo – Kinampanda – Gumanga (Singida) – Mkalama (km 46)*** kwa kiwango cha lami baada ya kazi za Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa barabara hii kukamilika.

104. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu **Barabara ya Dar es Salaam – Mbagala (Kilwa Road) – Gerezani (Sehemu ya Kamata – Bendera Tatu Km 1.3),** hadi Aprili, 2023 kazi za ***Upanuzi wa Daraja la Gerezani*** zilikuwa zimekamilika. Aidha, katika mwaka wa fedha 2023/24 Serikali imepanga kuanza kazi ya upanuzi na ukarabati wa sehemu ya ***Mbagala Rangi Tatu – Kongowe (km 3.8).***

105. ***Mheshimiwa Spika,*** katika **Barabara ya Msimba – Ruaha Mbuyuni/Ikokoto Mafinga (km 535.25)** hadi kufikia Aprili, 2023, kazi za ukarabati kwa sehemu ya ***Mafinga – Igawa (km 137.9)*** zimekamilika. Vilevile, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa sehemu ya ***Rujewa – Madibira – Mafinga (km 152.0)*** kwa kiwango cha lami baada ya kazi za Upembuzi Yakinifu na

Usanifu wa Kina wa barabara hii kukamilika. Kuhusu barabara ya ***Morogoro – Iringa (Tumbaku Jct. Mangae/Melela – Mikumi – Iyovi) (km 158.45) pamoja na Daraja la Doma,*** taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina kwa ajili ya ukarabati wa barabara hii zinaendelea.

106. ***Mheshimiwa Spika,*** katika **Barabara ya Same – Mkumbara – Korogwe (km 147.5),** hadi Aprili, 2023 taratibu za manunuzi ya kuwapata Makandarasi wa ujenzi wa sehemu za ***Same – Kisiwani – Mroyo (Km 56.83)*** na ***Ndungu – Mkomazi (km 36)*** zimekamilika na mikataba ya ujenzi kwa kiwango cha lami inatarajiwa kusainiwa Juni, 2023. Aidha, kazi za Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina umekamilika na Serikali inaendelea kutafuta fedha za ukarabati kwa kiwango cha lami kwa barabara za ***Same – Himo (km 76), Mombo – Lushoto (km 32)*** na ujenzi wa barabara ya ***Lushoto – Magamba – Mlola (km 34.5).***

107. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mradi wa **Barabara ya Mbeya – Makongolosi (km 267.9),** kazi za ujenzi zimekamilika kwa sehemu za ***Mbeya – Lwanjilo – Chunya (km 72),*** na ***Chunya – Makongolosi (km 39)***. Hadi Aprili, 2023 ujenzi wa sehemu ya ***Noranga – Itigi – Mkiwa (km 56.9) sehemu ya Noranga – Itigi (Mlongoji) km 25*** umefikia asilimia 12, ujenzi wa ***barabara za Itigi Mjini (km 10)*** umefikia asilimia 70 na taratibu za manunuzi za kumpata Mkandarasi wa ujenzi sehemu ya ***Noranga – Doroto (km 6)*** na ***Itigi – Mkiwa (km 25.6)*** zimekamilika na Mkataba na Mzabuni aliyeshinda zabuni tayari umesainiwa. Aidha, kazi za Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa barabara za ***Makongolosi – Rungwa – Noranga (km 356)*** na ***Mbalizi – Makongolosi (km 50)*** zimekamilika na kwa sasa Serikali inaendelea kutafuta fedha za ujenzi wa barabara hizi kwa kiwango cha lami.

108. ***Mheshimiwa Spika,*** katika **Barabara ya Itoni – Ludewa – Manda (km 211),** kazi za ujenzi kwa kiwango cha zege kwa sehemu ya ***Lusitu – Mawengi (km 50)*** zimekamilika. Aidha, hadi kufikia Aprili 2023, ujenzi wa sehemu ya ***Itoni – Lusitu (km 50)*** kwa kiwango cha zege umefikia asilimia 2.

109. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mradi wa **Handeni – Kibirashi – Kijungu – Kibaya – Njoro – Olboloti – Mrijo Chini – Goima – Chemba – Kwa Mtoro – Singida (km 424.24) na Goima – Dalai – Bicha (km 35.76)**, hadi kufikia Aprili, 2023 ujenzi wa sehemu ya ***Handeni – Mafuleta (km 20)*** umefikia asilimia 11.61 na taratibu za manunuzi kwa ajili ya ujenzi wa sehemu ya ***Mafuleta – Kileguru (km 30)*** zinaendelea na Mkataba utasainiwa mwezi Juni, 2023.

110. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu **Barabara ya Makambako – Songea na Barabara ya Mzunguko ya Songea (km 295)**, hadi kufikia Aprili 2023, Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa sehemu za ***Lutukila – Songea (km 95)*** na ***Mchepuo wa Songea (km 11)*** umekamilika na Mkataba wa Mkopo nafuu kati ya Serikali na Benki ya Dunia umesainiwa na zabuni za kumpata Mkandarasi wa ujenzi zinatarajiwa kutangazwa mwezi Juni, 2023. Aidha, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya ***Ramadhani – Ilembula Hospital – Iyayi (km 75)*** na ukarabati wa barabara ya ***Makambako – Lutukila (km 200)*** kwa kiwango cha lami.

111. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu ujenzi wa **Barabara ya Dodoma – Iringa (km 260),** hadi kufikia Aprili 2023, ujenzi kwa kiwango cha lami wa mita 450 za ***Barabara ya Mchepuo wa Iringa (km 7.3)*** ulikuwa umekamilika na ujenzi wa madaraja madogo 7 kwenye sehemu iliyobaki ya ***Igumbilo – Tumaini Jct*** unaendelea. Kazi za uimarishaji wa matabaka ya barabara katika barabara ya ***Iringa – Dodoma (km 264)*** zinafanyika kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha. Aidha, ujenzi wa mizani katika barabara ya Iringa – Dodoma umekamilika.

112. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi wa ujenzi wa **Barabara ya Dodoma – Babati (km 263.4)** umekamilika. Aidha, taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata mkandarasi wa ujenzi wa barabara ya ***Dareda – Dongobesh (km 60)*** sehemu ya ***Dareda Mjini – Dareda Mission (Km 8)*** zinaendelea na Mkataba unatarajiwa kusainiwa mwezi Juni, 2023. Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya ***Mchepuo wa Babati (km 27.5)*** na ***Miteremko ya Magara (Magara Escarpment - km 3).***

113. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu mradi wa **Barabara za Chuo cha Uongozi (Uongozi Institute, km 8.8)** hadi kufikia Aprili 2023, kazi za Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa barabara hii zilikuwa zimekamilika na kwa sasa Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami.

114. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa **Barabara za Igawa – Songwe – Tunduma na Mchepuo wa Mbeya (km 266.9),** hadi kufikia Aprili 2023, Mkandarasi wa kazi za upanuzi wa sehemu ya ***Uyole – Ifisi (km 29)*** yupo kwenye maandalizi ya kuanza kazi. Aidha, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya ***Iwambi – Mbalizi Bypass (km 6.5)*** kwa kiwango cha lami.

115. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu mradi wa **Miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya Pili hadi Tano (km 69.8),** kazi za ujenzi wa barabara ya ***Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya Pili*** (CBD – Mbagala, Km 20.3) zimefikia asilimia 90 na ujenzi wa miundombinu ya ***Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya Tatu*** (CBD – Gongolamboto km 23.33) zimefikia asilimia 5. Taratibu za manunuzi ya Mkandarasi wa kazi za ujenzi wa miundombinu ya ***Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya Nne*** (Ali Hassan Mwinyi – Morocco – Mwenge – Tegeta na Mwenge – Ubungo (km 30.12) zinaendelea**.** Aidha, mradi wa ***Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya Tano*** unaohusisha ujenzi wa barabara ya Nelson Mandela kuanzia Ubungo hadi Daraja la Mwalimu Nyerere pamoja na barabara ya Tabata kutoka Segerea kupitia Tabata Dampo hadi Mzunguko wa Kigogo katika barabara ya Kawawa (km 27.6), kazi za Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina zimekamilika na zabuni zitatangazwa mwishoni mwa mwezi Mei, 2023.

116. ***Mheshimiwa Spika,*** Kuhusu ***Maboresho ya Barabara za BRT Awamu ya Kwanza (Jangwani)***, hadi kufikia Aprili, 2023, Mkataba wa upanuzi wa Awamu ya Kwanza: Kimara – Kivukoni, Sehemu ya Kimara – Ubungo utasainiwa hivi karibuni. Aidha, maandalizi ya kutangaza zabuni kwa ajili ya ujenzi wa daraja la Jangwani yanaendelea na kwa sasa nyaraka za zabuni zinaandaliwa na zabuni zitatangazwa baada ya kupata ridhaa (No Objection) ya Benki ya Dunia.

117. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu mradi wa **Ujenzi wa Jengo la Makao Makuu ya Taasisi ya Teknolojia ya Ujenzi (Institute of Construction Technology – ICoT),** hadi Aprili, 2023, mkataba wa ujenzi wa jengo jipya la Taaluma na Utawala ICoT Morogoro umesainiwa na Mkandarasi yupo katika maandalizi ya ujenzi. Aidha, **Ujenzi wa Makao Makuu ya Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS),** unaendelea na mradi umefikia asilimia 61. Ujenzi wa Ofisi za Mikoa ya Dar es Salaam, Katavi, Geita, Simiyu, Njombe, Lindi na Songwe unasubiri upatikanaji wa fedha.

118. ***Mheshimiwa Spika***, fedha za Mfuko wa Barabara zinatumika kutekeleza miradi mbalimbali ya barabara nchini. Kazi zilizopangwa kutekelezwa kwa mwaka 2022/23 kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara katika Barabara Kuu ni kufanya Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa kilometa **5,605** za barabara. Hadi Aprili, 2023 kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara katika Barabara Kuu ni kufanya Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa kilometa **5,605** za barabara. Hadi Aprili, 2023 Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa miradi **24** umekamilika na miradi mingine tisa (**9)** ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji, ambapo miradi **16** ipo katika hatua ya usanifu wa kina, na miradi **29** ipo katika hatua ya ununuzi kama ifuatavyo:-

***a.* Miradi ambayo Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina umekamilika:**

*i. Barabara ya Kibaoni – Majimoto – Inyonga (km 152);*

*ii. Barabara ya Utete – Nyamwage (km 34);*

*iii. Barabara ya Mbamba Bay – Lituhi (km 121);*

*iv. Barabara ya Magu – Bukwimba – Ngudu – Hungumalwa (km 64);*

*v. Barabara ya Singida Bypass (km 46);*

*vi. Barabara ya Nyakato – Veta – Buswelu (km 3);*

vii. *Barabara ya Makete – Ndulamo – Nkenja – Kitulo (km 42);*

viii. *Barabara ya Goba – Matosa – Temboni/Morogoro Road Jct na Makabe/Mbezi Mwisho – Goba Jct – Msakuzi (km 15);*

ix. *Barabara ya Mwanza Urban Along Mwanza – Nyanguge (km 25);*

x. *Barabara ya Airport – Igombe – Nyanguge (km 46);*

xi. *Barabara ya Babati (Dareda) – Dongobesh (km 60);*

xii. *Barabara ya Mbulu – Magugu (Mbuyu wa Mjerumani) (km 63);*

xiii. *Barabara ya Ngopito – Kimotorok – Singe (Babati) (km 255);*

xiv. *Madaraja ya Mjonga (m60), Chakwale (m 100) na Nguyami (m 75);*

xv. *Barabara ya Kagwira – Ikola – Karema (km 112);*

xvi. *Barabara ya Ntendo – Muze – Kilyamatundu (km 200);*

xvii. *Sehemu ya Kizungu – Muze – Kilyamatundu (km 175);*

xviii. *Barabara ya Old Bagamoyo, Jijini Dar es Salaam (Dual Carriage way km 32.8);*

xix. *Barabara ya Mika – Utegi – Shirati – Ruari Port na Masonga – Kirogwe (km 48.73);*

xx. *Barabara ya Ushirombo – Nyikonga – Geita (Katoro) (km 59*);

xxi. *Barabara ya Mbalizi – Mkwajuni (Galula – Mkwajuni – Makongolosi (km 61);*

xxii. *Barabara ya Mkalama – Gumanga – Nduguti – Iguguno - Shamba (km 89);*

xxiii. *Barabara ya Namanyere – Katongoro – New Kipili Port (km 64.8);*

xxiv. *Barabara ya Mkuyuni – Nyakato (Km 10); na*

xxv. *Barabara ya Singida Mjini – Ilongero – Haydom (km 93).*

***b.*** **Miradi ambayo Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina unaendelea:**

i. *Barabara ya Ulemo – Kinampanda – Gumanga – Mkalama (km 49);*

ii. *Barabara ya Nangurukuru – Liwale (km 210);*

iii. *Barabara ya Mpwapwa – Gulwe – Rudi – Chipogoro; Sehemu ya Kibakwe – Chipogoro (km 75.84);*

iv. *Barabara ya Simanjiro (Orkesumet) – KIA – Mererani (Sehemu ya Kongwa Ranch – Kiteto – Simanjiro – KIA (km 60);*

v. *Barabara ya Morogoro (Msamvu Roundabout) – Morogoro Centre – Bigwa Junction (km 10); Upanuzi wa Barabara ya Arusha – Kisongo (km 8.8);*

vi. *Daraja la Kyabakoba na Kamashango na Barabara unganishi katika barabara ya Muhutwe – Kamachumu – Muleba ;*

vii. *Barabara ya Kimotorok – Sukuro Terati/Rotiane (km 128); na*

viii. *Barabara ya Nanenane – Miyuji – Mnadani Sekondari – Ntyuka Jct – Nanenane (km 47.2).*

**c. Miradi ambayo ipo katika taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina:**

*i. Daraja la Bujonde;*

*ii. Barabara ya Omurushaka – Murongo (km 125);*

*iii. Barabara ya Ihumwa – Hombolo – Mayamaya (km 55);*

*iv. Mteremko wa Mlima Kitonga (km 10);*

*v. Barabara ya Mpanda – Ugalla – Kaliua – Ulyankulu – Kahama (km 457);*

*vi. Barabara ya Morogoro (Tumbaku Roundabout) – Mangae/Melela – Mikumi – Iyovi (km 156.45) na Daraja la Doma;*

*vii. Barabara ya Kibaha - Mlandizi – Chalinze (km 75);*

*viii. Barabara ya Bariadi – Salama - Ng'haya - Magu (km 76);*

*ix. Barabara ya Old Korogwe – Kwamndolwa – Magoma – Mabokweni (km 127.4);*

*x. Barabara ya Longido – Siha (km 38);*

*xi. Barabara ya Tengeru – Mererani (km 28);*

*xii. Barabara ya Geita - Nzera - Nkome Port (km 58.3);*

*xiii. Barabara ya Chalinze – Manga along Chalinze - Segera (km 93);*

*xiv. Barabara ya Bungu – Nyamisati (km 40.2);*

*xv. Barabara ya Katesh – Haydom (km 63)*

xvi. *Barabara ya Kuruya – Kinesi Junction (km 18.42);*

xvii. *Barabara ya Ikungi (Singida) - Londoni - Kilimatinde (Solya) (km 117.9);*

xviii. *Barabara ya Nyankanga - Rung'abure (km 91);*

xix. *Barabara ya Nyankumbu - Kharumwa - Nyang'holongo - Kahama (km 149);*

xx. *Barabara ya Geita Town Section (Mtakuja - Buhalahala) along Nyamuhama - Bwanga - Ibanda Trunk Road (km 24);*

xxi. *Barabara ya Mkuranga - Kisiju Road (Pwani) (km 39);*

xxii. *Barabara ya Kiluvya - Mpuyani Road (Pwani) (km 19.8);*

xxiii. *Barabara ya Bariadi - Kisesa - Mwandoya - Ngh'oboko (km 102);*

xxiv. *Barabara ya Nyakahanga - Nyabiyonza - Nyakakika (km 96);*

xxv. *Barabara ya Mkongo 2 - Ikwiriri (km 24.74);*

xxvi. *Barabara ya Katumba - Kafwafwa - Kyimo (km 21.98);*

xxvii. *Barabara ya Mbalizi - Shigamba (km 52) Daraja la Sanga; na*

xxviii. *Uandaaji wa 'Master Plan' ya Barabara zinazosimamiwa na TANROADS.*

***d.* Miradi Mingine inayotekelezwa ni:**

***i Kuimarisha Uwezo wa Maabara (Central Materials Labolatory – CML) Katika Kupima Vifaa vya Ujenzi na Kuanzisha Teknolojia ya Kisasa ya (Asphalt Mix Design)***

Kazi ya kuimarisha uwezo wa maabara ya vifaa vya ujenzi na mafunzo mbalimbali kwa ajili ya utumiaji wa Mwongozo wa uchanganyaji wa lami zinaendelea.

***ii Kuwajengea Uwezo Makandarasi wa Ndani***

Katika mwaka wa fedha 2022/23, Serikali imetenga miradi mikubwa minne (4) ya ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami kwa ajili ya kuwajengea uwezo Makandarasi wa ndani. Zabuni za kazi hizi zimetangazwa.

***iii Kuwajengea Uwezo Makandarasi Wanawake***

Katika mwaka wa fedha 2022/23, jumla ya kilometa 20 za ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami zimetengwa kwa ajili ya Makandarasi Wanawake peke yao. Kazi hizi zitagawanywa katika sehemu za kilometa tano (5) tano (5) ambapo Makandarasi wanawake pekee ndiyo wanastahili kuomba kazi hizo.

***iv Matumizi ya Teknolojia Mpya katika Ujenzi na Matengenezo ya Barabara***

Ili kukabiliana na changamoto za barabara hususan za changarawe na udongo kuharibika hasa wakati wa mvua na kusababisha mahitaji ya matengenezo ya mara kwa mara, Wizara (Ujenzi) inaendelea na majaribio ya Teknolojia mbalimbali ili kubaini teknolojia yenye ufanisi na kusaidia kwenye ujenzi na matengenezo ya barabara na kuzifanya zidumu kwa muda mrefu bila kuhitaji matengenezo. Teknolojia mojawapo iliyojaribiwa ni ya matumizi ya *Water – Based RESIN Primer* ambayo tayari imetumika hapa nchini kwa upande wa Tanzania Visiwani. Hivyo, Wizara (Ujenzi) kwa kushirikiana na TAMISEMI inafuatilia kwa karibu ufanisi wa Teknolojia hii ili ianze kutumika katika ujenzi na matengenezo ya barabara.

**Utekelezaji wa Miradi ya Ujenzi na Ukarabati wa Vivuko na Maegesho ya Vivuko**

119. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2022/23, Wizara kupitia Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania (TEMESA) iliendelea kutekeleza miradi ya ***ujenzi na ukarabati wa maegesho ya vivuko.*** Hadi Aprili, 2023, miradi iliyokamilika ni ukarabati wa maegesho ya Magogoni – Kigamboni upande wa Magogoni na upanuzi wa eneo la maegesho katika kituo cha Magogoni – Kigamboni upande wa Kigamboni Jijini Dar es Salaam awamu ya kwanza ikiwa ni pamoja na kukamilisha usimikaji wa mfumo wa kielektroniki wa kukatia tiketi (N-Cards System). Kazi nyingine zilizokamilika ni ujenzi wa maegesho ya Iramba – Majita upande wa Majita, ujenzi wa maegesho ya Bugolora – Ukara na miundombinu katika kituo cha Chato (Geita).

120. ***Mheshimiwa Spika,*** miradi inayoendelea ni upanuzi wa eneo la maegesho ya Magogoni – Kigamboni upande wa Kigamboni awamu ya pili ambapo zoezi la tathmini ya watu wanaopaswa kupisha mradi linaendelea. Ujenzi wa maegesho ya Mayenzi – Kanyinya (Ngara) umefikia asilimia 50, Ijinga - Kahangala (Magu) umefikia asilimia 40, Bwiro – Bukondo (Ukerewe) umefikia asilimia 80, Mlimba – Malinyi upande wa Mlimba umefikia asilimia 40 na upande wa Malinyi umefikia asilimia 85. Kazi nyingine zinazoendelea ni ujenzi wa miundombinu (jengo la abiria, ofisi na uzio), Kinesi (Mwigobero) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 20 na Mwaya – Kajunjumele (Itungi Port) utekelezaji umefikia asilimia 95.

121. ***Mheshimiwa Spika,*** kazi nyingine zinazoendelea ni Upembuzi Yakinifu na uandaaji wa michoro katika miradi ya ujenzi wa maegesho ya vituo vya Utete – Mkongo, Nyakarilo – Kome, Kasharu – Buganguzi na Muleba – Ikuza. Vilevile, ujenzi wa maegesho ya Iramba – Majita upande wa Iramba pamoja na uboreshaji wa Mfumo wa Tiketi katika kituo cha Kigongo – Busisi upo katika hatua za manunuzi. Aidha, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuanza utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa maegesho ya Kilambo – Namoto na kuboresha mfumo wa

tiketi za kielektroniki katika vituo vya Kisorya – Rugezi, Pangani – Bweni na Ilagala – Kajeje.

122. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu miradi ya ***ununuzi/ujenzi wa vivuko,*** hadi Aprili, 2023, ujenzi wa kivuko kipya kitakachotoa huduma kati ya Kisorya - Rugezi (Ukerewe) umefikia asilimia 57 na kazi inayoendelea kwa sasa ni ujenzi wa umbo la kivuko (super structure). Miradi mingine ni ujenzi wa vivuko vya Ijinga – Kahangala (Magu), Bwiro – Bukondo (Ukerewe), Nyakarilo – Kome (Buchosa) ambapo utekelezaji wa kila kivuko umefikia asilimia 35. Aidha, maandalizi ya kuanza ujenzi wa kivuko kipya cha pili kitakachotoa huduma kati ya Nyamisati – Mafia (Pwani) yanaendelea. Ujenzi wa kivuko kipya kitakachotoa huduma kati ya Buyagu – Mbalika (Misungwi) upo katika hatua za awali na ujenzi wa vivuko viwili vidogo (Sea Tax Ferries) katika kituo cha Magogoni – Kigamboni upo katika hatua ya manunuzi. Vilevile, ununuzi wa vifaa vya karakana za TEMESA kwa ajili ya kuboresha utoaji huduma umekamilika kwa kununua vifaa ya umeme, elektroniki, viyoyozi na majokofu na kusambazwa kwenye vituo vyote vya TEMESA.

123. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu miradi ya ***Ukarabati wa Vivuko***, hadi Aprili, 2023, ukarabati mkubwa wa vivuko vya MV Kazi, MV TEMESA, MV Musoma na MV Tanga umekamilika. Aidha, ukarabati mkubwa wa kivuko MV Misungwi awamu ya pili umefikia asilimia 95. Vilevile, ukarabati mkubwa wa vivuko MV Kilombero II umefikia asilimia 75, MV Nyerere umefikia asilimia 70 na MV Ujenzi umefikia asilimia 68. Kazi nyingine inayoendelea ni ukarabati mkubwa wa kivuko MV Mara, MV Kitunda na MV Kyanyabasa ambapo utekelezaji wa kila kivuko umefikia asilimia 30. Ukarabati mkubwa wa kivuko MV Magogoni umeanza na utekelezaji wa mradi wa ukarabati mkubwa wa kivuko MV Kome II unasubiri upatikanaji wa kivuko mbadala.

**Utekelezaji wa Miradi ya Ujenzi na Ukarabati wa Nyumba na Majengo ya Serikali**

124. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) imeendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya

ujenzi na ukarabati wa nyumba na majengo ya Serikali katika mwaka wa fedha 2022/23.

125. ***Mheshimiwa Spika***, hadi Aprili, 2023, Awamu ya II ya ujenzi wa nyumba nyingine 20 za Viongozi Jijini Dodoma ipo katika hatua za maandalizi ya ujenzi. Ujenzi wa nyumba 150 za watumishi Jijini Dodoma Awamu ya I umefikia asilimia 92. Vilevile, ujenzi wa nyumba nyingine 150 (Awamu ya II) za Watumishi wa Umma Jijini Dodoma umefikia asilimia 3. Ujenzi wa nyumba tano (5) za majaji Tanzania Bara katika mikoa ya Tabora, Kilimanjaro, Shinyanga na Mtwara umekamilika na katika Mkoa wa Kagera utekelezaji wa mradi umefikia asilimia 40. Ujenzi wa Ghorofa za Watumishi wa Umma katika eneo la Magomeni Kota Awamu ya II "Block" A umekamilika, kwa upande wa "Block" B utekelezaji wa mradi umefikia asilimia 72. Aidha, ujenzi wa Ghorofa za Watumishi wa Umma za Temeke Kota umefikia asilimia 19 na ujenzi wa jengo la Ofisi za Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi katika Mji wa Serikali - Mtumba Jijini Dodoma umefikia asilimia 62.

126. ***Mheshimiwa Spika***, vilevile, katika mradi wa ukarabati wa nyumba 40 za Viongozi Dodoma uliohusisha nyumba sita (6), hadi Aprili, 2023 ukarabati wa nyumba hizo umekamilika. Kwa upande wa ukarabati wa nyumba 30 za Viongozi Mikoani, utekelezaji umefikia asilimia 60. Ukarabati wa nyumba nyingine 66 kati ya 431 zilizohamishiwa TBA kutoka kwa iliyokuwa CDA umekamilika. Aidha, ukarabati wa nyumba zilizokuwa zinamilikiwa na TAMISEMI katika mikoa 20 zilizohamishiwa TBA umefikia asilimia 15.

127. ***Mheshimiwa Spika,*** Mradi wa Kuwajengea Uwezo Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi unaendelea kutekelezwa. Aidha, maandalizi ya Sheria ya Majengo (Building Act), Taratibu za Majenzi (Building Codes) na Viwango Msawazo (Standard Specifications) kwa ajili ya kazi na miradi ya ujenzi na ukarabati wa nyumba na Majengo ya Serikali yameanza.

128. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi mwingine unaotekelezwa ni ***Ujenzi na Ukarabati wa Karakana za TEMESA na TBA.*** Hadi Aprili, 2023, miradi iliyokamilika ni ujenzi wa karakana za TEMESA katika Mkoa wa Simiyu Awamu ya I na ukarabati mkubwa wa karakana za Vingunguti na MT Depot Awamu ya I. Aidha, ukarabati wa

karakana za TEMESA mikoa ya Mwanza, Tabora, Kigoma, Mara, Arusha na Mtwara unaendelea na upo katika hatua mbalimbali. Vilevile, usanifu wa miradi ya Ukarabati wa Karakana za Dodoma, Ruvuma, Pwani, MT Depot Awamu ya II na Mbeya Awamu ya II umekamilika.

Mradi wa kusanifu na kusimika Mfumo wa Usimamizi na Ufuatiliaji wa Matengenezo ya Magari, Umeme na Elektroniki umekamilika na kwa sasa upo kwenye majaribio katika mikoa ya Iringa, Dodoma na Dar es Salaam. Ukarabati wa karakana ya Kisasa katika Mkoa wa Dodoma upo katika hatua ya usanifu. Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya uanzishaji wa karakana mpya za TEMESA katika Wilaya ya Simanjiro, Masasi, Ukerewe, Mafia, Chato na Kyela. Kwa upande wa Karakana za TBA, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ukarabati wa karakana sita (6) za TBA katika Mikoa ya Arusha, Mwanza, Morogoro, Tabora, Dar es Salaam na Mbeya.

**Usalama Barabarani na Mazingira**

129. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2022/23 Wizara iliendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya usalama barabarani na kudhibiti uzito wa magari yanayotumia barabara zetu. Katika mradi wa **usalama barabarani,** kazi zilizotekelezwa hadi kufikia Aprili, 2023 ni pamoja na ufungaji wa vifaa vya kisasa vya upimaji uzito wa magari (Digital Load Cell) katika mizani sita (6) ambayo ni Mikumi, Mutukula, Himo 2, Mingoyo, *Mikese North* na *Mikese South* na hivyo kufanya idadi ya mizani iliyofungwa vifaa hivyo kufikia kumi (10). Maandalizi ya kutekeleza mradi wa maboresho ya Mfumo wa Utunzaji Kumbukumbu za Ajali za Barabarani yanaendelea. Kwa sasa maandalizi ya hadidu za rejea kwa ajili ya kumpata Mshauri Elekezi wa kufanya kazi hiyo yanaendelea. Vilevile, taratibu za manunuzi ya mradi wa kuunda na kufunga Mfumo wa Usimamizi wa Utendaji kazi katika vituo vya mizani zinaendelea. Mfumo wa kuwasaidia watembea kwa miguu kuvuka barabara kwa usalama (Push Button Pedestrian Signal) umefungwa Jijini Dar es Salaam kwenye barabara zinazopita katika shule za msingi Kinyerezi (Ilala), Kifuru (Kinondoni), Liwiti (Ilala), Tabata JICA (Ilala), Kibasila (Temeke) na Gate 1 katika chuo cha ualimu (DUCE). Kuhusu mapitio ya Sera ya Taifa ya

Usalama Barabarani, taratibu za manunuzi ya Mshauri Elekezi atakayefanya kazi hiyo zinaendelea.

Vile vile, katika kuongeza ufanisi na kupunguza foleni katika vituo vya mizani, Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Ujenzi) kupitia TANROADS inaendelea kufanya maboresho (upgrading) ya vituo vya mizani ikiwa ni pamoja na kubadili mizani ya kupima uzito wa gari kwa ekseli moja (Single Axle Weigher) kuwa mizani inayopima uzito wa gari kwa kundi la ekseli (Group of Axles). Mizani hiyo inayofanyiwa maboresho ni pamoja na mizani ya Mghamo – Singida, Uvinza – Kigoma, Uyole – Mbeya na mizani ya Himo II – Kilimanjaro.

130. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu mradi wa **kujenga uwezo wa taasisi katika masuala ya usalama barabarani na mazingira,** Wizara ilipanga kufanya utafiti ili kubaini athari za kijamii na kiuchumi zinazotokana na ajali za barabarani na kufanya mapitio ya miongozo ya usalama barabarani. Hadi kufikia Aprili, 2023, Wizara imempata Mshauri Elekezi kwa ajili ya kufanya utafiti ili kubaini athari za kijamii na kiuchumi zinazotokana na ajali za barabarani. Aidha, taratibu za kuchapisha miongozo ya usalama barabarani inayohusu Sekta ya Ujenzi zinaendelea.

131. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu mradi wa **menejimenti ya usimamizi wa mazingira**. Wizara ilipanga kuandaa Mkakati wa Kukabiliana na Majanga katika Sekta ya Ujenzi, kuandaa Mpango Tekelezi wa Mazingira wa miaka mitano wa Sekta (*Sector Environment Action Plan, 2022-2027)*, kuwezesha mikutano inayohusu masuala ya mazingira, kufanya mapitio ya miongozo ya tathmini na usimamizi wa mazingira pamoja na kuanzisha Mfumo wa Kusimamia na Kukusanya Taarifa za Mazingira.

132. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Aprili, 2023, Wizara ilifanya mafunzo ya menejimenti ya maafa kwa baadhi ya watumishi ili kuwajengea uwezo wa kuandaa Mkakati wa Kukabiliana na Majanga kwa Sekta ya Ujenzi. Maandalizi ya nyaraka za zabuni kwa ajili ya kuwapata Washauri Elekezi wa kufanya mapitio ya miongozo ya tathmini na usimamizi wa mazingira, kuandaa Mpango tekelezi wa Mazingira wa miaka mitano kwa Sekta

(*Sector Environment Action Plan, 2022-2027)* pamoja na kuanzisha Mfumo wa Kusimamia na Kukusanya Taarifa za Mazingira yanaendelea. Aidha, Wizara ilishiriki katika Mkutano wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabia Nchi uliofanyika nchini Misri tarehe 30 Oktoba hadi 18 Novemba, 2022.

**MIRADI YA UJENZI WA MIUNDOMBINU YA VIWANJA VYA NDEGE**

133. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2022/23, Wizara ilipanga kuendelea na ujenzi wa viwanja vipya vya Ndege vya Geita, Simiyu na Msalato. Aidha, Wizara ilipanga kufanya ukarabati, upanuzi na uboreshaji wa viwanja vya ndege 20 nchini ambavyo ni pamoja na Viwanja vya Ndege vya Kigoma, Mpanda, Tabora, Songwe, Mwanza, Arusha, Mtwara, Sumbawanga, Shinyanga, Iringa, Musoma, Songea, Dodoma, Tanga, Lake Manyara, Lindi, Moshi, Bukoba, Julius Nyerere International (JNIA) na Viwanja vingine vya Ndege vya Mikoa.

134. ***Mheshimiwa Spika,*** uboreshaji na ukarabati wa **Viwanja vya Ndege vya Sumbawanga, Shinyanga, Tabora na Kigoma** unatekelezwa kwa ufadhili wa Benki ya Uwekezaji ya Ulaya (European Investment Bank - EIB). Hadi Aprili, 2023, utekelezaji wa miradi hii umeanza na Makandarasi wako kwenye hatua za maandalizi (mobilization).

135. ***Mheshimiwa Spika,*** katika **Kiwanja cha Ndege cha Songwe,** kazi za ukarabati wa barabara ya kutua na kuruka ndege pamoja na eneo la usalama (Runway End Safety Area-RESA), usimikaji wa taa za usalama na taa za kuongozea ndege (AGL) zimekamilika. Aidha, Mkandarasi kwa ajili ya kazi ya kumalizia jengo la abiria anaendelea na utekelezaji wake umefikia asilimia 98.

136. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu **Kiwanja cha Ndege cha Mwanza**, Serikali inaendelea kukamilisha ujenzi wa jengo la muda la abiria. Aidha, mazungumzo na Washirika wa Maendeleo kwa ajili ya kupata fedha za kugharamia ujenzi wa jengo la abiria la kudumu pamoja na miundombinu yake yanaendelea. Kwa upande wa **Kiwanja cha Ndege cha Mtwara**, kazi ya upanuzi na

ukarabati kwa awamu ya kwanza imekamilika na mradi upo katika kipindi cha uangalizi.

137. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu mradi wa ujenzi wa **Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato,** hadi Aprili, 2023 utekelezaji wa *Package I* unaohusisha ujenzi wa barabara ya kuruka na kutua ndege (runway), barabara ya viungio (taxiway), maegesho ya ndege (apron) pamoja na usimikaji wa taa za usalama na kuongozea ndege umefikia asilimia 18. Aidha, utekelezaji wa *Package II* unaohusisha ujenzi wa jengo la abiria, jengo la kuongozea ndege, Kituo cha Zimamoto, Kituo cha Hali ya Hewa na Vituo vidogo nane (8) vya kufua umeme unaendelea na umefikia asilimia 2. Mradi huu unafadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB).

138. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu **kiwanja cha Ndege cha Musoma,** kazi ya upanuzi na ukarabati wa barabara ya kutua na kuruka ndege, maegesho ya ndege, barabara ya kiungio na uzio wa usalama inaendelea na utekelezaji umefikia asilimia 47. Aidha, Kazi ya upanuzi na ukarabati wa **kiwanja cha ndege cha Songea** imekamilika na mradi upo kwenye muda wa matazamio (Defect Liability Period - DLP). Vilevile, katika **Kiwanja cha Ndege cha Moshi,** kazi ya upanuzi na ukarabati wa kiwanja hicho inaendelea na utekelezaji umefikia asilimia 22. Kwa upande wa mradi wa uboreshaji wa **Viwanja vya ndege vya Lindi, Bukoba**, **Mpanda na Arusha,** Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kazi hizo**.**

139. ***Mheshimiwa Spika,*** katika **kiwanja cha Ndege cha Iringa,** ukarabati na upanuzi wa barabara ya kutua na kuruka ndege, maegesho ya ndege, mitambo na taa za kuongozea ndege, barabara ya kiungio na uzio wa usalama (Awamu ya Kwanza) umefikia asilimia 50. Kwa upande wa **Kiwanja cha Ndege cha Geita,** hadi kufikia Aprili, 2023, Mkandarasi kwa ajili ya kazi ya ujenzi wa uzio wa usalama na barabara ya mzunguko tayari yupo kwenye hatua za maandalizi ya kuanza kazi. Aidha, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi Jengo la Abiria na Jengo la kuongozea ndege.

140. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu mradi wa ukarabati na upanuzi wa **Viwanja vya ndege vya Tanga, Lake Manyara na Iringa (Awamu ya II)** hadi Aprili, 2023, Serikali imekamilisha ulipaji wa fidia kwa wananchi wote watakaopisha ujenzi wa viwanja hivyo. Kuhusu kiwanja cha ndege cha Iringa, kazi zitakazotekelezwa katika Awamu ya II ni ujenzi wa jengo la abiria. Aidha, tayari Mfadhili ametoa kibali (No Objection) na taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mshauri Elekezi zimeanza. Kwa upande wa Mkandarasi, Serikali inasubiri kibali kutoka kwa Mfadhili ili kuanza taratibu za manunuzi.

**UTENDAJI WA TAASISI ZILIZO CHINI YA SEKTA YA UJENZI**

**Bodi ya Mfuko wa Barabara**

141. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2022/23, Bodi ilipanga kukusanya jumla ya **Shilingi 856,794,954,000.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi 534,662,653,430** ni kwa ajili ya kugharamia kazi za barabara za Kitaifa (Barabara Kuu na Barabara za Mikoa) ambazo husimamiwa na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi. Aidha, kiasi cha **Shilingi 254,601,263,538** zilitengwa kwa ajili ya kugharamia kazi za barabara za Wilaya ambazo husimamiwa na Ofisi ya Rais – TAMISEMI.

Mgawanyo wa fedha hizo ni kama ifuatavyo: Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Ujenzi) **Shilingi 59,406,961,492**; TANROADS **Shilingi 534,662,653,430**; Ofisi ya Rais – TAMISEMI **Shilingi 25,460,126,354,** TARURA **Shilingi 229,141,137,184** na **Shilingi 8,124,075,539** ni kwa ajili ya kugharamia shughuli za uendeshaji wa Mfuko wa Barabara. Hadi Aprili, 2023, Bodi imekusanya jumla ya **Shilingi 653,794,981,271** sawa na asilimia 76.3 ya bajeti ya mwaka.

142. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Bodi ilifanya ukaguzi wa ubora wa kazi za matengenezo ya barabara kwa miradi 1,279 ili kuhakikisha kuwa Fedha za Mfuko zinatumika ipasavyo na kuwa na thamani halisi ya fedha. Idadi ya miradi iliyokaguliwa imeongezeka kutoka miradi 594 iliyokaguliwa mwaka 2021/22.

143. ***Mheshimiwa Spika,*** Bodi pia imeendelea kuratibu na kutekeleza zoezi la kuchukua takwimu na taarifa za hali ya

barabara (*road inventory and condition survey*) kwa lengo la kuzitumia katika kuandaa mipango kazi na utekelezaji wa kazi za barabara. Aidha, Bodi imeendelea kutoa elimu ya matumizi ya Mfumo wa Kielektroniki wa Kutoa Taarifa ya Hali ya Barabara kwa njia ya redio, runinga, mitandao ya kijamii, maonesho na mikusanyiko mbalimbali.

**Wakala wa Majengo Tanzania**

144. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2022/23 Wakala wa Majengo Tanzania ulipanga kutekeleza majukumu yake yanayohusisha ujenzi wa nyumba na majengo ya Serikali. Miradi hii ilitekelezwa kwa kutumia fedha za Ruzuku ya Serikali pamoja na mapato ya ndani ya Wakala. Kazi zilizotekelezwa ni pamoja na kutoa huduma za ushauri kwa miradi ya ujenzi wa majengo ya Serikali, kujenga majengo ya Washitiri mbalimbali; kuuza Nyumba zinazojengwa na TBA kwa Watumishi wa Umma; kupangisha nyumba za Serikali kwa Watumishi wa Umma na kupangisha baadhi ya majengo ya Serikali kwa wasio watumishi wa umma ili kuongeza uwezo wa Wakala kujiendesha.

145. ***Mheshimiwa Spika,*** miradi iliyotekelezwa kwa kutumia ***fedha za ruzuku*** ni kama inavyoonekana katika **Aya. 124- 128**.

146. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu miradi inayotekelezwa kwa kutumia ***fedha za ndani za Wakala*** ni umaliziaji wa miradi miwili (2) ya ujenzi katika mikoa ya Arusha na Pwani (Simeoni-Arusha na Chalinze -Pwani) ambao utekelezaji wake umefikia asilimia 74.3 na ujenzi wa jengo la ghorofa kwa watumishi wa Umma eneo la Canadian Village Dar es Salaam umekamilika. Miradi mingine ni ukarabati wa Majengo mbalimbali nchini ambao utekelezaji wake umefikia asilimia 30.

147. ***Mheshimiwa Spika,*** Wakala pia umetekeleza miradi 167 ya ***Washitiri***. Miradi hiyo ni pamoja na miradi 18 ya Buni Jenga (Design and Build). Baadhi ya miradi hiyo ni; Ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Manispaa ya Mji wa Ifakara ambao umefikia asilimia 50 ya utekelezaji, ujenzi wa Ofisi ya Halmashauri ya Wilaya ya Butiama – Mara umefikia asilimia 97 ya utekelezaji na ujenzi wa

Makazi ya Rais wa Awamu ya Tano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Hayati J.P. Magufuli umefikia asilimia 92.

148. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Wakala umeendelea kutekeleza miradi mbalimbali katika ***Mji wa Serikali*** eneo la Mtumba Dodoma ikiwemo ujenzi wa Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora awamu ya pili ambao umefikia asilimia 70. Wakala pia umeendelea kutoa huduma ya ushauri katika mradi huo awamu ya pili kwa Wizara 13, Taasisi nne (4) na ujenzi wa jengo la Wizara moja (1) ambazo zipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

149. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Wakala umetekeleza miradi 93 ya ***Ushauri (Consultancy***). Miradi hiyo ni pamoja na Ukarabati wa jengo la Utawala la Ofisi za Bunge awamu ya pili na ujenzi wa Ofisi ya Ikulu Chamwino ambayo imekamilika. Miradi mingine ni ujenzi wa Ofisi ya Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (PCCB) katika eneo la NCC Dodoma ambao upo asilimia 56; Ujenzi wa jengo la utawala la Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda ambao upo asilimia 90; Ujenzi wa jengo la Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Mbogwe Geita awamu ya pili ambao upo asilimia 80; na Ujenzi wa jengo la "Radiotherapy", "nuclear medicine" na "chemotherapy" Hospitali ya Benjamin Mkapa Dodoma ambao umefikia asilimia 15.

150. ***Mheshimiwa Spika,*** Wakala vilevile umetekeleza miradi 25 ya ***Ujenzi na Ukarabati***. Miradi ya ujenzi na ukarabati iliyotekelezwa inajumuisha: Ujenzi wa jengo la Ofisi ya TANESCO Makao Makuu eneo la Medeli Dodoma ambao umefikia asilimia 97; Ujenzi wa jengo la Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Butiama ambao umefikia asilimia 10; Ukarabati wa Ofisi ya Mamlaka ya Hali ya Hewa – Dar es Salaam ambao umefikia asilimia 40; na Ujenzi wa jengo la Ofisi ya Halmashauri ya Wilaya ya Loliondo Arusha ambao umefikia asilimia 48.

151. ***Mheshimiwa Spika,*** Wakala pia ulitekeleza miradi minne (4) ya ***Usimamizi (Project Management).*** Miradi hiyo ni ujenzi wa Vihenge (Silos) vya kuhifadhia nafaka pamoja na maghala ya Wakala wa Taifa wa Hifadhi Chakula (NFRA) katika mikoa nane (8) ya Dodoma, Katavi, Manyara, Njombe, Rukwa, Ruvuma,

Shinyanga na Songwe. Ujenzi umekamilika katika mikoa mitatu (3) ya Manyara, Katavi na Rukwa ambapo kwa mkoa wa Manyara, mradi umezinduliwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tarehe 22 Novemba, 2022. Kwa mikoa iliyosalia, mradi umefikia asilimia 51.7.

Wakala pia umeendelea kusimamia mifumo katika Ukumbi wa Bunge Dodoma. Mifumo hiyo ni pamoja na Mifumo ya joto, hewa na viyoyozi, Mifumo ya umeme, Mifumo ya vitambua moto na vitoa sauti, Mifumo ya majisafi na majitaka, Mitambo ya kangavuke (generators) na transfoma pamoja na usimamizi wa samani. Vilevile, Wakala umeendelea na ujenzi wa ngazi, "View point" na Kituo cha Taarifa cha Maporomoko ya Kalambo awamu ya tatu kilichopo Rukwa ambapo utekelezaji umefikia asilimia 75. Vilevile, hadi Aprili, 2023 mradi wa usimamizi wa ujenzi wa majengo ya Kituo cha Pamoja cha Forodha Mipakani cha Kasumulu umefikia asilimia 88.4.

**Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania**

152. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2022/23, Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania (TEMESA) ulipanga kufanya matengenezo ya magari, pikipiki na mitambo ya Serikali; kusimika na kufanya matengenezo ya mifumo ya umeme, elektroniki, majokofu na viyoyozi kwenye majengo ya Serikali na kutoa ushauri wa kihandisi kwa miradi ya usimikaji wa mifumo ya umeme, mitambo, elektroniki, viyoyozi na majokofu katika nyumba ya Serikali. Kazi nyingine ni kuendesha shughuli za usafiri wa Vivuko vya Serikali zinazohusisha ujenzi na ukarabati wa vivuko, maegesho na miundombinu ya vivuko (majengo na uzio).

153. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili, 2023, utekelezaji wa miradi ya ***maegesho ya vivuko***, ***Ukarabati wa Vivuko, Ujenzi wa Vivuko Vipya*** na ***Ujenzi na Ukarabati wa Karakana*** kwa kutumia fedha za ruzuku ni kama inavyooneshwa katika **Aya 119 – 123.**

154. ***Mheshimiwa Spika,*** Wakala pia ulipanga kutekeleza ***Miradi ya Washitiri na Ushauri*** iliyohusisha kufanya matengenezo ya magari 30,365, matengenezo na usimikaji wa mifumo 256 ya umeme, 704 ya majokofu na viyoyozi na mifumo 25 ya elektroniki.

Aidha, Wakala ulipanga kutoa ushauri wa Kihandisi kwa miradi ya usimikaji wa mifumo 90 ya umeme, mitambo, elektroniki, viyoyozi na majokofu na kusimamia mifumo hiyo inayofikia 50. Wakala pia ulipanga kuendelea na usimamizi wa vivuko vya Serikali 33 ambavyo vinatarajiwa kutoa huduma kwa abiria wapatao 42,460,356; magari 1,745,311 na tani za mizigo 530,220 kwa mwaka. Vilevile, Wakala utaendelea na ukodishaji wa mitambo ya ujenzi wa barabara.

155. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili, 2023, Wakala umefanya matengenezo ya magari 14,341, umesimika mifumo ya umeme 52, elektroniki 17, viyoyozi na majokofu 18. Aidha, miradi ya usanifu ya umeme, mitambo na electroniki 11 imetekelezwa. Aidha, Wakala unaendelea na usimamizi na uendeshaji wa vivuko vya Serikali 33 pamoja na ukodishaji mitambo.

**Bodi ya Usajili wa Wahandisi**

156. ***Mheshimiwa Spika,*** Bodi hii ina majukumu ya kuratibu, kusimamia na kudhibiti mienendo na shughuli za kihandisi nchini kwa lengo la kulinda maslahi ya Taifa na watumiaji wa huduma hizo. Katika mwaka wa fedha 2022/23, Bodi ilipanga kusajili Wahandisi **3,200**, Mafundi Sanifu **400** na Kampuni za Ushauri wa Kihandisi **8,** kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Mafunzo kwa vitendo kwa Wahandisi wahitimu **3,692**.

157. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Aprili, 2023 Bodi imesajili Wahandisi **4,259,** Mafundi Sanifu **418** na Kampuni za Ushauri wa Kihandisi **10** na kufikisha jumla ya Wahandisi waliosajiliwa katika ngazi mbalimbali kuwa **35,614** na Kampuni za Ushauri wa Kihandisi kuwa **340**. Kati ya jumla ya Wahandisi waliosajiliwa, **32,664** ni wa ndani na **2,950** ni wageni. Kampuni za Ushauri wa Kihandisi za ndani zilizosajiliwa ni **230** na za kigeni ni **110**. Aidha, Bodi ilifuta usajili kwa Wahandisi Watalaam **590** na Kampuni za Ushauri wa Kihandisi **2** kwa kukiuka Sheria ya Usajili wa Wahandisi. Vilevile, Bodi ilisajili miradi **437** kati ya miradi **600** iliyopanga kutekeleza, viwanda na Majengo **113** kati ya **130** iliyopanga kutekeleza pamoja na kukagua jumla ya miradi **144.**

158. ***Mheshimiwa Spika,*** Bodi pia iliandaa warsha **2,** moja ikiwa kwa Wahandisi Wahitimu na Mafundi Sanifu. Vilevile, Bodi

iliendelea kuwaapisha Wahandisi Wataalam Kiapo cha Utii kwa Taaluma (Professional Oath) ambapo jumla ya wahandisi **4,940** hadi sasa wameshaapishwa. Aidha, Bodi iliendelea kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Mafunzo kwa Vitendo kwa Wahandisi Wahitimu **3,326**. Jumla ya Wahandisi Wahitimu **11,399** wameshapitia Mpango huu tangu uanzishwe mwaka 2003.

159. ***Mheshimiwa Spika,*** Bodi pia iliandaa na kuadhimisha Siku ya Wahandisi ya mwaka 2022 (Annual Engineers' Day 2022) ambayo ilihudhuriwa na wahandisi zaidi ya **4,520**. Mada iliyojadiliwa katika Siku ya Wahandisi ilikuwa ni "Ubunifu na Ukuzaji Ujuzi katka Kuimarisha Maendeleo Endelevu ya Kitaifa ya Kiuchumi; Mtazamo wa Uhandisi" (Innovation and Skills Development in Enhancing National Sustanable Ecomomic Development; Engineering Perspective).

160. ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na majukumu hayo, Bodi imetekeleza majukumu mengine ikiwemo kushiriki katika kuimarisha utendaji wa Taasisi ya Teknolojia ya Ujenzi Morogoro (ICoT) na Campus ya Mbeya pamoja na kushiriki kutoa ushauri wa kitaalamu kuhusu Mapitio ya Mwongozo wa Manunuzi ya Umma kwa Mfumo wa *Force Account* katika Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA) na mchakato wa uanzishwaji wa Chuo cha Kilimo cha Mwalimu Nyerere, Butiama – Mara. Kazi nyingine ni uchunguzi wa ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Kanda iliyoko Ukerewe, Mwanza chini ya Wizara ya Afya; Usuluhishi wa changamoto zilizokuwepo kwenye ujenzi wa Mradi wa Barabara za Mabasi Yaendayo Haraka Jijini Dar es Salaam - BRT Phase II; Kupitia michoro ya usanifu wa ujenzi wa majengo ya Wizara katika Mji wa Serikali Mtumba, Dodoma pamoja na kufanya uchunguzi wa ujenzi wa jengo la UTT- AMIS katika Mji wa Serikali Mtumba.

Vilevile, Bodi imeshiriki katika kazi mbalimbali ikiwemo Kamati ya Uwezeshaji wa Mradi wa Ujenzi wa Bwawa la Kufua Umeme la Julius Nyerere, kuandaa Mpango wa Ujenzi unaozingatia "Green Infrastructure" katika kuzingatia uhifadhi wa mazingira chini ya usimamizi wa Benki ya Dunia, pamoja na ujenzi na majaribio ya Mfumo mpya wa Kielektroniki wa Manunuzi ya Umma wa PPRA.

**Bodi ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi**

161. ***Mheshimiwa Spika,*** jukumu la msingi la Bodi hii ni kusajili, kusimamia na kuratibu mwenendo wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi pamoja na Kampuni zao za ushauri. Katika mwaka wa fedha 2022/23, Bodi ilipanga kusajili Wataalam **125,** katika fani za Ubunifu Majengo, Ukadiriaji Majenzi, Ubunifu wa Ndani ya Majengo, Ubunifu wa Mandhari ya Nje ya Majengo, Usanifu Teknolojia ya Majengo, Utathmini Majengo, Usimamizi Ujenzi na Usimamizi Miradi. Aidha, Bodi ilipanga kusajili kampuni **25** za Ubunifu Majengo na Ukadiriaji Majenzi.

Vilevile, Bodi ilipanga kufanya ukaguzi wa miradi ya ujenzi **3,120** katika mikoa yote **26** ya Tanzania Bara pamoja na kusajili miradi ya ujenzi **1,400.** Aidha, Bodi ilipanga kuwajengea uwezo wahitimu **225** katika fani za Ubunifu Majengo, Ukadiriaji Majenzi, Ubunifu wa Ndani ya Majengo, Ubunifu wa Mandhari ya Nje ya Majengo, Usanifu Teknolojia ya Majengo, Utathmini Majengo, Usimamizi Ujenzi na Usimamizi Miradi kupitia Mpango Maalumu wa Mafunzo kwa Vitendo (EAPP) kwa Wahitimu. Kazi nyingine ni kuendesha mitihani ya kitaalam kwa wahitimu **218** katika fani za Ubunifu Majengo na Ukadiriaji Majenzi na kufanya mikutano mitano (5) na wanafunzi wa Shule za Msingi na Sekondari.

162. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Aprili, 2023, Bodi imesajili Wataalam **136** sawa na asilimia 108 ya lengo na kampuni **14** zimesajiliwa ikiwa ni asilimia 56 ya lengo. Aidha, hadi Aprili, 2023 Wahitimu **212** wamepatiwa mafunzo ikiwa ni asilimia 94 ya malengo yaliyopangwa. Miradi ya ujenzi **1,960** imekaguliwa ikiwa ni asilimia 63 ya lengo. Kwa miradi iliyokutwa na kasoro mbalimbali, wataalam au waendelezaji wake walichukuliwa hatua kwa mujibu wa Sheria. Miradi ya ujenzi **719** ilikuwa imesajiliwa ambayo ni asilimia 51 ya malengo yaliyopangwa. Aidha, Bodi ilifanikiwa kuendesha mitihani ya kitaalamu kwa wahitimu **97** katika fani za Ubunifu Majengo, Ukadiriaji Majenzi, Ubunifu wa Ndani ya Majengo, Ubunifu wa Mandhari ya Nje ya Majengo, Usanifu Teknolojia ya Majengo na Usimamizi Miradi ambayo ni asilimia 44 ya lengo na kufanya mikutano mitano (**5**) na Wanafunzi wa Shule za Msingi na Sekondari.

163. ***Mheshimiwa Spika,*** kazi nyingine zilizotekelezwa na Bodi ni pamoja na kutoa ushauri wa kisheria kwa wadau mbalimbali, kuandaa mikataba ya kisheria pamoja na kufanya marekebisho ya Sheria Namba 4 ya mwaka 2010. Vilevile, Bodi imefanya usuluhishi wa migogoro kati ya wamiliki na washauri kwenye miradi ya ujenzi pamoja na kufungua kesi 37 mahakamani kutokana na makosa ya uvunjifu wa sheria kwenye miradi ya ujenzi na inaendelea kufanya ufuatiliaji wa kesi hizo.

**Bodi ya Usajili wa Makandarasi**

164. ***Mheshimiwa Spika,*** Bodi hii ina majukumu ya kusajili, kuratibu na kuendeleza shughuli za ukandarasi nchini. Katika mwaka wa fedha 2022/2023, Bodi ilipanga kusajili Makandarasi **960** na kukagua jumla ya miradi ya ujenzi **3,200.** Vilevile, Bodi ilipanga kuendesha kozi nne **(4)** za mafunzo katika mikoa ya Arusha, Iringa, Mwanza na Dar es Salaam pamoja na kuuendeleza Mfuko Maalum wa Kusaidia Kutoa Dhamana kwa Makandarasi (Contractor’s Assistance Fund - CAF). 165. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili, 2023, Bodi ilisajili Makandarasi wapya **1,014** hivyo kufanya jumla ya Makandarasi waliosajiliwa kufikia **14,341.** Aidha, jumla ya miradi **3,101** ilikaguliwa sawa na asilimia 97 ya malengo. Miradi **1,038** sawa na asilimia 33.5 ilipatikana na mapungufu mbalimbali yakiwemo kutozingatia usalama kazini, kutosajili miradi na kufanya kazi za thamani inayozidi kiwango kinachoruhusiwa kwa daraja husika. Makandarasi waliokutwa na mapungufu hayo walichukuliwa hatua mbalimbali kwa mujibu wa sheria ikiwemo kutozwa faini, kupewa onyo, kusimamishwa kufanya biashara ya ukandarasi na kufutiwa usajili. Aidha, pale ambapo miradi ilikutwa ikifanyika bila kutumia Makandarasi, wawekezaji walifikishwa mahakamani.

166. ***Mheshimiwa Spika,*** Bodi iliendesha mafunzo ya ushirikiano wa ubia (Joint Venture) katika kituo kimoja (1) Jijini Dodoma. Jumla ya Makandarasi **116** walihudhuria mafunzo. Aidha, Bodi iliendesha kozi za mafunzo kupitia Mpango Maalum wa Mafunzo Endelevu kwa Makandarasi (Sustainable Structured Training Programme – SSTP) katika mikoa ya Arusha, Iringa, Mwanza na Dar es Salaam. Jumla ya Makandarasi **486** walishiriki katika mafunzo hayo.

167. ***Mheshimiwa Spika,*** Bodi iliendelea kuendesha Mfuko wa Kusaidia Makandarasi (Contractors Assistance Fund - CAF) unaotoa dhamana za zabuni na malipo ya awali kwa Makandarasi wa ndani ili kuwezesha ushiriki wa makandarasi wa ndani katika zabuni na utekelezaji wa miradi mbalimbali. Mtaji wa mfuko huu umeendelea kuwa **Shilingi bilioni 4.0** kwa mwaka 2022/23 kama ulivyokuwa kwa mwaka wa 2021/22. Aidha idadi ya wanachama wa mfuko imeongezeka kutoka wanachama **1,317** mwaka 2021/22 hadi kufikia wanachama **1,380** mwaka 2022/23.

168. ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na majukumu yake ya kusajili, kudhibiti na kuendeleza Makandarasi, Bodi ya Usajili wa Makandarasi (CRB) pia imekuwa ikitekeleza majukumu mengine ikiwemo kutoa elimu yenye lengo la kuhamasisha uzingatiaji wa sheria ya usajili wa Makandarasi; kuandaa matangazo ya redio na runinga na kuandaa na kutoa mada katika vyuo vya maafisa wa polisi na mikutano ya mwaka ya wanasheria wa Serikali.

Kazi nyingine ni kuwaunganisha Makandarasi wa hapa nchini na wafanyabiashara mbalimbali nje ya Nchi wanaojihusisha na masuala ya Sekta ya Ujenzi. Katika kutekeleza suala hili, Bodi imekuwa ikiratibu ziara za mafunzo nje ya nchi kwa Makandarasi ili kuweza kujifunza na kupata uzoefu kutoka katika nchi zingine. Vilevile, Maafisa wa Bodi hushiriki katika majukumu mbalimbali yanayohitaji taaluma zao za uhandisi, usanifu na ukadiriaji majenzi pale wanapokuwa wameombwa na taasisi zingine na katika kutekeleza majukumu ya kiserikali kwa ujumla. Majukumu hayo ni kama vile vikosi kazi vya kukagua miradi ya ujenzi (Technical project audit), kamati za kitaalam (technical committees) na katika tathmini za zabuni (tender evaluations).

**Baraza la Taifa la Ujenzi**

169. ***Mheshimiwa Spika,*** majukumu ya Baraza la Taifa la Ujenzi ni kushughulikia uratibu na uendelezaji wa Sekta ya Ujenzi nchini. Kazi zinazofanyika ni kutoa ushauri, miongozo ya kimkakati, uratibu wa shughuli za utafiti na mafunzo, ukusanyaji na uwekaji wa taarifa za ujenzi, tathmini ya utendaji kazi wa Sekta ya Ujenzi,

uhamasishaji wa ubora wa kazi, ikiwa ni pamoja na ukaguzi wa kiufundi (technical audit) na utatuzi wa migogoro ya Ujenzi.

170. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/23, kazi zilizofanyika ni pamoja na kuendelea na mapitio ya Sheria iliyoanzisha Baraza la Ujenzi na kuandaa Kanuni zake; kuanza taratibu za kutunga Sheria ya Majengo (Building Act); kuandaa Taratibu za Majenzi (Building Codes) na viwango msawazo (standard specifications) kwa ajili ya majengo ya Serikali na samani; kuratibu utatuzi wa migogoro kwa njia ya usuluhishi na maridhiano ambapo migogoro mipya kumi na moja (11) imesajiliwa, migogoro inayoendelea ipo 17 na migogoro nane (8) imepatiwa uamuzi.

171. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kushirikiana na Bodi ya Mfuko wa Barabara (RFB), Baraza limeweza kuandaa mwongozo wa bei na gharama za ujenzi na ukarabati wa barabara hapa nchini ambapo Rasimu ya Mapendekezo ya Gharama za Msingi za Ujenzi wa Barabara (base unit rates) kwa kila mkoa (Tanzania Bara) imekamilika. Aidha, Baraza limekamilisha kuandaa Kanuni za Baraza la Taifa la Ujenzi na kutoa ushauri wa kiufundi na kitaalam kwa wadau wa Sekta ya Ujenzi ili kuongeza thamani ya mradi (value for money) na kupunguza migogoro.

**Kituo cha Usambazaji wa Teknolojia Katika Sekta ya Ujenzi na Usafirishaji (Tanzania Transportation Technology Transfer Centre)**

172. ***Mheshimiwa Spika,*** majukumu ya Kituo hiki ni kuimarisha/kuboresha Sekta ya Ujenzi na Uchukuzi kwa kutumia mbinu ya ukusanyaji na usambazaji wa teknolojia kwa Wadau kutoka ndani na nje ya nchi ili kukuza weledi na ufanisi katika utendaji. Mkazo umekuwa katika sekta ndogo ya barabara na usafirishaji kwa kuzingatia mahitaji ya maendeleo.

173. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2022/23. Kituo kimefanikiwa kuandaa Semina ya Ukanda wa Afrika inayohusu Usimamizi wa Mikataba ya Ujenzi wa Barabara kulingana na Utendaji (*Africa Regional Seminar and Workshop on Performance-Based Contracts (PBC) and Framework Agreements for Roads* iliyofanyika Desemba, 2022 Jijini Arusha pamoja na kushiriki katika mkutano wa Kamati ya Kujenga Uwezo ya SADC

(*Regional Technology Transfer and Capacity Building Committee*) kwenye masuala yanayohusu usambazaji wa teknolojia katika Sekta ya Ujenzi na usafirishaji cha ASANARA (*36th Regional Technological Transfer and Capacity Building Committee and other Committee meetings*) kilichofanyika Maputo, Msumbiji kuanzia 14 hadi 18 November, 2022.

Vilevile, Kituo kimeandaa na kuendesha mafunzo ya muda mfupi kwa wataalam nane (8) wa Wizara yaliyohusu Usanifu wa Barabara na Madaraja (*Roads and bridge geometric design training course*) yaliyofanyika Makao Makuu ya TANROADS Jijini Dar es Salaam, kununua *Software* ya *Civil 3D for Geometric design for highways and bridges* ili wataalam wa Wizara kuendelea kujiimarisha katika usanifu wa barabara na madaraja pamoja na kuandaa na kuchapisha Nakala 300 za jarida la kituo Na. 6 lenye mada mbalimbali zinazohusu teknolojia, usalama barabarani, taarifa za miradi mbalimbali ya kimkakati na agenda mbalimbali za Serikali katika kuimarisha miundombinu ya usafirishaji. Aidha, awamu ya saba ya jarida hilo ipo katika hatua za maandalizi.

**B.2 SEKTA YA UCHUKUZI**

174. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2022/23, Sekta ya Uchukuzi iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 2,135,781,440,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 94,546,502,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ya Wizara na Taasisi zake na **Shilingi 2,041,234,938,000.00** ni kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo.

**Bajeti ya Matumizi ya Kawaida**

175. ***Mheshimiwa Spika***, kati ya **Shilingi 94,546,502,000.00** zilizoidhinisha kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, **Shilingi 67,475,558,000.00** ni fedha za Mishahara na **Shilingi 27,070,944,000.00** ni fedha za Matumizi Mengineyo kwa Wizara na Taasisi zilizo chini ya Sekta ya Uchukuzi. Hadi kufikia Aprili, 2023 jumla ya **Shilingi 71,955,448,034.75** sawa na asilimia 76.11 ya bajeti iliyoidhinishwa zilikuwa zimetolewa ambapo **Shilingi**

**57,048,372,547.00** zilikuwa kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Wizara na Taasisi na **Shilingi 14,907,075,487.75** zilikuwa kwa ajili ya Matumizi Mengineyo ya Wizara na Taasisi.

**Bajeti ya Maendeleo**

176. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2022/23, Sekta ya Uchukuzi ilitengewa jumla ya **Shilingi 2,041,234,938,000.00** kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 1,927,771,622,000.00** ni fedha za ndani na **Shilingi 113,463,316,000.00** ni fedha za nje. Hadi kufikia Aprili, 2023 jumla ya **Shilingi 1,847,575,297,974.02** sawa na asilimia 90.51 ya bajeti iliyoidhinishwa zilikuwa zimetolewa kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 1,797,993,533,111.02** ni fedha za ndani na **Shilingi 49,581,764,863.00** ni fedha za nje.

177. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara (Sekta ya Uchukuzi) baada ya kupokea fedha hizo, iliendelea kutekeleza shughuli na miradi ya maendeleo katika maeneo mbalimbali kama ifuatavyo:-

**UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO NA UTOAJI WA HUDUMA**

**HUDUMA ZA USAFIRI MIJINI NA VIJIJINI**

**Udhibiti wa Usafiri kwa Njia ya Barabara**

178. ***Mheshimiwa Spika,*** Udhibiti wa Usafiri wa Barabara unatekelezwa na Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) chini ya Sheria ya LATRA, Sura ya 413. Mamlaka hiyo inadhibiti utoaji wa huduma za usafiri wa kibiashara kwa abiria na mizigo ikijumuisha mabasi, malori, teksi, pikipiki za magurudumu matatu (maarufu kwa jina la bajaji), na pikipiki za magurudumu mawili (maarufu kwa jina la bodaboda). Majukumu ya LATRA ni pamoja na kutoa leseni, kupanga nauli, kupanga ratiba za safari, kukagua ubora wa huduma, kudhibiti uchafuzi wa mazingira, kutoa elimu kwa umma na kusuluhisha migogoro. Hadi kufikia Aprili, 2023, Mamlaka ilitoa jumla ya leseni 229,408. Kati ya leseni hizo, leseni 42,902 ni za mabasi, leseni 137,580 za magari ya mizigo, leseni 1,914 za teksi za kawaida, leseni 2,471 za teksi

mtandao pamoja na leseni 23,557 za bodaboda na leseni 20,984 za bajaji.

179. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia LATRA imeendelea kusimamia usalama wa huduma zinazodhibitiwa kwa kusajili madereva wa vyombo vya moto vinavyotoa huduma za usafiri kibiashara kwa lengo la kuwathibitisha (certification of drivers). Hadi kufikia Aprili, 2023 jumla ya madereva 15,202 walikuwa wamesajiliwa ili kuweza kuthibitishwa baada ya kufanya mtihani, kufaulu na kupewa Cheti cha Uthibitisho. Uthibitishaji wa madereva hufanyika kielektroniki kwa kutumia Mfumo wa Kutahini Madereva (Drivers Testing System - DTS). Kupitia mfumo huo, jumla ya madereva 1,340 walifanya mtihani husika na kati yao madereva 842 walifaulu na kuthibitishwa. Vilevile, mfumo huu unaboreshwa ili utumike kutathmini madereva wa treni kwa ajili ya kuimarisha usalama wa huduma za usafiri kwa njia ya reli.

180. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia LATRA imeendelea kusimamia utekelezaji wa Mfumo wa Ufuatiliaji wa Mwenendo wa Mabasi ya masafa marefu na treni za TAZARA na TRC kwa kutumia Mfumo wa Ufuatiliaji wa Mwenendo wa Magari (Vehicle Tracking System – VTS). Lengo ni kuimarisha shughuli za udhibiti wakati wote na mahali popote vyombo vilipo. Hadi kufikia Aprili 2023, mabasi yote 7,370 ya masafa marefu yalikuwa yameunganishwa kwenye mfumo huo. Aidha, vichwa vya treni vinane (8) vya TAZARA na viwili (2) vya TRC vilikuwa vimeunganishwa kwenye mfumo huo. Juhudi za kuuboresha Mfumo wa VTS ili uweze pia kudhibiti mwendo kasi (speed governor) na mpango wa kufunga mfumo huu kwenye magari ya mizigo na mabasi ya masafa mafupi unaendelea.

181. ***Mheshimiwa Spika,*** Sheria ya LATRA Sura ya 413 Kifungu cha 5(f) kinaipa LATRA mamlaka ya kuthibitisha usalama wa magari ya kibiashara kabla ya kupewa leseni. Hatua hii ilikusudia kuongeza ufanisi wa usafiri ardhini, kupunguza ajali na gharama za uendeshaji kwa watoa huduma pamoja na kuongeza usalama na ubora wa huduma za usafiri wa ardhini. Serikali kupitia LATRA ilikamilisha Upembuzi Yakinifu kuhusu njia bora ya kuanzisha na kuendesha vituo vya ukaguzi wa lazima kwa magari ya biashara. Aidha, LATRA na Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama

Barabarani watatekeleza ukaguzi huu kwa kushirikiana. Ni matarajio ya Serikali kwamba, suala hili litatekelezwa kwa ufanisi zaidi kwa manufaa ya nchi.

182. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuboresha huduma za usafiri wa mabasi yaendayo mikoani na nchi jirani pamoja na kudhibiti nauli za mabasi hayo, Serikali kupitia LATRA, ilisimamia utekelezaji wa mfumo wa tiketi za kielektroniki (e-tiketing system) kuanzia mwezi Julai, 2022. Mfumo huu ulitekelezwa na LATRA kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Kituo cha Taifa cha Mtandao (NIDC), watoa huduma wa tiketi za kielektroniki (e-ticketing vendors) na Chama cha Wamiliki wa Mabasi Tanzania (TABOA). Mfumo wa tiketi za kielektroniki umesaidia kupunguza kero kwa abiria zinazotokana na 'wapiga debe' na pia wamiliki wa mabasi wanaweza kudhibiti mapato yao na kujua idadi ya abiria waliosafirishwa.

183. ***Mheshimiwa Spika***, pamoja na manufaa mengine yanayopatikana, mfumo huu unadhibiti abiria kuongezewa nauli kwa safari na unaongeza ufanisi katika kutambua mapato halisi ya mtoa huduma katika kukokotoa kodi ya Serikali. Vilevile, mfumo unasaidia kutambua abiria walio kwenye chombo cha usafiri hasa inapotokea dharura. Hadi kufikia Aprili 2023, jumla ya miamala 4,712,390 yenye thamani ya **Shilingi bilioni 160.15** ilifanyika kwenye mfumo huu wa tiketi jumuishi (Universal Ticketing System – UTS). Serikali kupitia LATRA kwa kushirikiana na Wakala wa Serikali Mtandao (eGA) na wadau wa mfumo huu itaendelea kuuboresha mfumo ili kumwezesha abiria kukata tiketi mwenyewe kwa kuchagua kampuni ya usafirishaji, daraja la basi, namba ya kiti na kuilipia kisha kupata tiketi ya kielektroniki.

184. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia LATRA kwa kushirikiana na eGA imeendelea kufanya maboresho katika mfumo wa huduma za udhibiti usafiri ardhini (Railways and Roads Information Management System – RRIMS). Lengo ni kutatua changamoto mbalimbali za kimfumo kwa wananchi na kuwasogezea zaidi huduma za LATRA kwa njia za kidijitali. Aidha, LATRA imejenga mfumo (LATRA App) unaotumia simu janja kuwezesha kujua nauli sahihi na huduma zingine zinazodhibitiwa na LATRA.

185. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa usafiri wa kukodi (teksi za kawaida), LATRA kwa kushirikiana na Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA) na Shirika la Viwango Tanzania (TBS) imeanza kutekeleza mpango wa matumizi ya mita za teksi za kukokotoa nauli (fare meter) kwa lengo la kuboresha huduma ya usafiri wa teksi na kuongeza udhibiti wa nauli katika vyombo vya usafiri wa kukodi. LATRA imeanza kukusanya maoni ya wadau jijini Dar es Salaam na zoezi hilo litaendelea kwenye mikoa mingine ili kuweza kukusanya maoni ya watumiaji wa usafiri wa kukodi wa teksi.

**Udhibiti wa Usafiri kwa Njia ya Reli**

186. ***Mheshimiwa Spika***, katika kudhibiti usafiri wa reli, Serikali kupitia LATRA imeendelea kudhibiti huduma na miundombinu ya Shirika la Reli Tazania (TRC). Hadi kufikia Aprili, 2023 LATRA ilikagua miundombinu ya TRC ya *Meter Gauge Railway (MGR)* kutoka Dar es Salaam – Kigoma, Tabora – Mwanza, Kaliua – Mpanda, Ruvu – Korogwe – Moshi – Arusha pamoja na kufanya uchunguzi wa vyanzo vinavyosababisha ajali za treni zilizotokea na kuweka mikakati ya kuzuia ajali nyingine zisitokee. Aidha, LATRA imeendelea kufanya kaguzi mbalimbali katika ujenzi unaoendelea wa Reli ya Kisasa (SGR) ili kujiridhisha na ubora wake pamoja na viwango vya kazi na usalama. Vilevile, LATRA ilikagua miundombinu ya reli ya TAZARA kutoka Dar es Salaam – Tunduma na kutoka Msolwa – Kidatu. Matokeo ya ukaguzi huo yalisaidia kuboresha miundombinu na matengenezo ya mitambo inayotumika kwenye usafiri wa reli ya TAZARA.

187. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia LATRA imeendelea kujiridhisha na vichwa na mabehewa ya treni yanayonunuliwa kwa kukagua ubora ambapo mabehewa mapya 22 yaliyonunuliwa na Serikali kutoka Korea kwa ajili ya kuboresha huduma za reli ya kawaida (MGR) za TRC yalikaguliwa na kutoa ithibati ya ubora na usalama. Aidha, LATRA, imeendelea kuhakiki usalama wa mabehewa ya abiria na vichwa vya treni vinavyoendelea kukarabatiwa katika karakana za TRC na TAZARA nchini.

**Udhibiti wa Usafiri wa Waya**

188. ***Mheshimiwa Spika,*** udhibiti wa usafiri wa waya (cable transport regulation) ni moja kati ya majukumu ya msingi ya LATRA. Hata hivyo, kwa kuwa eneo hili la udhibiti ni jipya nchini na ni usafiri wa kitalii zaidi, Serikali kupitia LATRA, imeanza maandalizi ya kuandaa Kanuni za Udhibiti wa Usafiri wa Waya kwa kushirikisha taasisi na wadau mbalimbali wa Sekta ya Uchukuzi. Aidha, ili kuwa na rasilimaliwatu itakayosimamia utekelezaji wa suala la usafiri wa waya wataalamu watatu (3) wanatarajiwa kujengewa uwezo wa masuala ya udhibiti wa huduma husika.

**HUDUMA ZA USAFIRI KWA NJIA YA RELI**

**Shirika la Reli Tanzania (TRC)**

189. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Shirika la Reli Tanzania (TRC) imeendelea kutoa huduma kwa wananchi. Katika kipindi cha Julai 2022 hadi Aprili, 2023 jumla ya abiria waliohudumiwa kati ya Stesheni ya Kamata – Ubungo – Pugu ni 1,963,163 ikilinganishwa na abiria 2,653,318 waliosafirishwa katika kipindi kama hicho mwaka 2021/22 sawa na upungufu wa asilimia 26. Upungufu huo umetokana na uchache wa vitendea kazi (vichwa vya treni na mabehewa) hali iliyosababisha kupunguza idadi ya treni kutoka sita (6) kwa siku hadi nne (4) kwa siku.

190. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Shirika la Reli Tanzania (TRC) imeendelea kusimamia, kuboresha na kuendeleza miundombinu na huduma za usafiri wa reli katika mtandao wa reli wenye urefu wa jumla ya Kilometa 2,706 unaohudumia nchi jirani za Burundi, Rwanda, Uganda na Kenya. Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Aprili, 2023 TRC ilisafirisha tani 339,122 za mizigo ikilinganishwa na tani 341,784 zilizosafirishwa katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2021/2022. Kwa upande wa abiria wa masafa marefu, abiria 408,383 walisafirishwa ikilinganishwa na abiria 351,189 waliosafirishwa katika kipindi kama hicho mwaka 2021/22 sawa na ongezeko la asilimia 16. Ongezeko hili limetokana na kuongeza treni mpya ya *Deluxe* pamoja na ukarabati wa njia.

191. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Wizara inaendelea na ujenzi wa Awamu ya Kwanza ya mradi wa Reli ya Kati kwa kiwango cha *Standard Gauge* kutoka Dar es Salaam hadi Mwanza (km 1,219), hususan kwenye vipande vya Dar es Salaam hadi Morogoro (km 300), Morogoro hadi Makutupora (km 422), Makutupora hadi Tabora (km 368), Tabora hadi Isaka (km 165) na Isaka hadi Mwanza (km 341). Hadi kufikia Aprili, 2023 ujenzi wa kipande cha Dar es Salaam hadi Morogoro (km 300) umefikia asilimia 98.14. Kazi zinazoendelea katika kipande hiki ni pamoja na ujenzi wa njia kuelekea bandarini (port link), Ujenzi wa uzio, Ujenzi wa vivuko vya juu vitatu (Vingunguti, Airport na Njia panda ya Segerea), ujenzi wa vivuko vya chini na ujenzi wa mifumo ya ishara na mawasiliano. Kwa kipande cha reli kutoka Morogoro hadi Makutupora (km 422), ujenzi wake umekamilika kwa asilimia 93.83 ambapo kazi zinazoendelea ni pamoja na majaribio ya miundombinu ya njia na mifumo, ujenzi wa stesheni, ujenzi wa mifumo ya umeme na ujenzi wa uzio.

192. ***Mheshimiwa Spika,*** kazi ya ujenzi katika kipande cha Mwanza hadi Isaka (km 341) imekamilika kwa asilimia 31.07 na Mkandarasi anaendelea na kazi za ujenzi wa tuta, majengo ya stesheni, madaraja na vivuko. Kwa kipande cha Makutupora hadi Tabora (km 368), kazi ya ujenzi imekamilika kwa asilimia 7 na kazi zinazoendelea ni pamoja na usanifu wa kina, ujenzi wa kambi, ukataji wa miinuko na ujazaji mabonde pamoja na utwaaji wa ardhi. Aidha, ujenzi wa kipande cha kutoka Tabora hadi Isaka (km 165) umefikia asilimia 2.39.

193. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeanza utekelezaji wa ujenzi wa Reli ya SGR kwa awamu ya pili inayojumuisha ujenzi wa njia ya reli kwa vipande vya Tabora – Kigoma (km 506), Kaliua – Mpanda – Karema (km 321), Uvinza-Musongati-Gitega (km 282) na IsakaRusumo (km 371). Aidha, Serikali kupitia TRC imesaini mkataba na kampuni ya CCECC na CRCC kutoka China mnamo tarehe 20 Desemba, 2022 kwa ajili ya ujenzi wa Reli ya *Standard Gauge* kwa Kipande cha Tabora – Kigoma (km 506). Mkataba huu utatekelezwa kwa muda wa miezi 42 na mkandarasi anakamilisha maandalizi ya ujenzi.

194. ***Mheshimiwa Spika,*** katika hatua za kupanua huduma za reli kwa kushirikiana na nchi jirani, Serikali ya Tanzania na Burundi zimesaini makubaliano na kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa njia ya reli SGR ya Uvinza – Musongati-Gitega (km 282). Reli hii inatarajia kuunganisha nchi ya Tanzania, Burundi na Demokrasia ya Kongo. Aidha, Serikali zote tatu zimefanya mazungumzo na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) na benki hiyo imeonesha nia ya kufadhili ujenzi wa reli hii.

195. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuanza kutoa huduma za usafiri wa Reli ya SGR, Serikali kupitia TRC inaendelea na ununuzi wa vichwa vya treni, mabehewa na mitambo itakayotumika kutoa huduma ya usafiri kwenye reli hiyo. Aidha, hadi kufikia Aprili 2023, Serikali imepokea mabehewa ya abiria 14 kati ya 59 ya treni ya *Standard Gauge* yatakayotumika kutoa huduma pindi ujenzi utakapokamilika. Utengenezaji wa mabehewa 45 ya abiria yaliyosalia umefikia asilimia 95 na yanatarajiwa kuwasili kati ya mwezi Juni, 2023 hadi mwezi Novemba, 2023. Aidha, Serikali inatarajia kupokea vichwa vya treni viwili (2) vya umeme na seti ya treni ya kisasa moja mwezi Juni, 2023.

196. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia TRC inaendelea kusimamia utekelezaji wa mkataba wa ununuzi wa mabehewa 1,430 ya mizigo yatakayotumika kutoa huduma katika reli ya Standard Gauge. Aidha, mkataba huu ulisainiwa tarehe 8 Februari, 2022 na Kampuni ya China Railway Rolling Stock Corporation (CRRC)-International Corporation Limited ya China. Kazi ya utengenezaji wa mabehewa inaendelea vizuri na imefikia asilimia 42 na mabehewa hayo yanatarajiwa kuwasili nchini ifikapo Februari, 2024.

197. ***Mheshimiwa Spika***, kazi nyingine zilizotekelezwa na TRC kwa mwaka 2022/23 ni pamoja na:-

i. Ununuzi wa mabehewa 22 ya abiria yanayotumika kutoa huduma katika njia ya reli iliyopo ya Meter Gauge. Mabehewa haya yaliwasili nchini tarehe 19 Novemba, 2022 na yameanza kutoa huduma;

ii. Kuanza kazi ya ukarabati wa njia ya reli iliyopo ya *Meter Gauge* kwa kipande cha Kaliua hadi Mpanda (km 210);

iii. Kukamilisha kazi ya Upembuzi Yakinifu na usanifu wa awali kwa ajili ya ujenzi wa njia ya reli ya mjini Dodoma;

iv. Kukamilisha kazi ya uboreshaji wa mifumo ya ishara, mawasiliano na umeme katika njia ya reli iliyopo ya *Meter Gauge* ambapo maboresho ya umeme yamekamilika kwa njia nzima na maboresho ya ishara na mawasiliano yanaendelea katika maeneo ya Tabora -Mwanza;

v. Kuanza taratibu za ununuzi wa vipuri kwa ajili ya ukarabati wa mabehewa 600 ya mizigo na mabehewa ya abiria 37 yatakayotumika kutoa huduma katika njia ya reli iliyopo. Hadi kufikia Aprili, 2023 mabehewa 52 ya mizigo na mabehewa sita (6) ya abiria yalikamilika na kuanza kutoa huduma;

vi. Kusaini mkataba kwa ajili ya ununuzi wa vichwa vya treni 8 vya njia kuu kwa ajili ya kutoa huduma katika njia ya reli iliyopo;

vii. Kusaini mkataba kwa ajili ya uundwaji wa vichwa vya treni vitano (5) vya njia kuu na vichwa vinne (4) vya sogeza vitakavyotumika kutoa huduma katika njia ya reli iliyopo ya *Meter Gauge*;

viii. Kusaini mkataba kwa ajili ya ujenzi wa njia ya reli yenye urefu wa kilometa 6.2 na daraja katika eneo la Godegode – Gulwe; na

ix. Kuanza kazi ya uboreshaji wa mifumo ya TEHAMA.

**Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA)**

198. ***Mheshimiwa Spika,*** Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA) imeendelea kutekeleza jukumu lake la msingi la kutoa huduma za kusafirisha abiria na mizigo kwa njia ya reli kati ya Dar es Salaam, Tanzania na New Kapiri Mposhi, Zambia. Jukumu lingine ni kulinda na kuimarisha miundombinu ya reli yenye urefu wa jumla ya kilometa 2,153 ikijumuisha njia za kupishania, pamoja

na maeneo yote yaliyo ndani ya ukanda wa reli (Mita 50 pande zote kutoka katikati ya reli). Mamlaka hii inamilikiwa na Serikali mbili za Tanzania na Zambia kwa hisa za asilimia 50 kwa 50.

199. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Aprili 2023, Mamlaka ya reli ya TAZARA ilisafirisha jumla ya tani 244,492 za mizigo ikilinganishwa na tani 210,161 zilizosafirishwa katika kipindi kama hicho 2021/22 sawa na ongezeko la asilimia 16.3**.** Aidha, Mamlaka imeingia mkataba wa kutumia njia ya reli kwa kulipia tozo (Access Fee) na Kampuni mbili (2) binafsi za kusafirisha mizigo kwa kutumia njia ya reli. Kampuni hizo ni *Ms Callabash Freight Limited* kutoka Zambia na *Ms African Inland Container Deport (AFICD)* kutoka Tanzania. Katika kipindi husika Kampuni binafsi zilisafirisha jumla ya mizigo ya tani 93,293 ikilinganishwa na mizigo ya tani 84,858 iliyosafirishwa katika kipindi kama hicho mwaka 2021/22 sawa na ongezeko la asilimia 9.94. Mizigo hiyo inasafirishwa kupitia Bandari ya Dar es Salaam kwenda au kutoka nchi za Zambia na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC). Utaratibu huu umeiingizia TAZARA mapato ya **Shilingi bilioni 5.03**.

200. ***Mheshimiwa Spika***, Treni ya Abiria ya Udzungwa inayofanya safari zake kati ya stesheni za Kidatu na Makambako (km 365), katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Aprili, 2023 ilisafirisha abiria 300,476 ikilinganishwa na abiria 296,307 waliosafirishwa katika kipindi kama hicho mwaka 2021/22, sawa na ongezeko la asilimia 1.4. Aidha, treni ya jijini Dar es Salaam ilisafirisha jumla ya abiria 1,567,225 ikilinganishwa na jumla ya abiria 1,537,528 waliosafirishwa katika kipindi kama hicho mwaka 2021/22. Sawa na ongezeko la asilimia 1.9. Hata hivyo, jumla ya abiria wa njia ndefu (Udzungwa a treni za kwenda Zambia) waliosafirishwa walikuwa jumla ya abiria 765,706 ikilinganishwa na jumla ya abiria 685,712 waliosafirishwa katika kipindi kama hicho 2021/22, ikiwa sawa na ongezeko la asilimia 11.7.

## USAFIRI NA UCHUKUZI KWA NJIA YA MAJI

### Udhibiti wa Huduma za Usafiri kwa njia ya Maji

201. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC) imeendelea kusimamia ulinzi na usalama wa vyombo vya usafiri kwa njia ya maji na kudhibiti uchafuzi wa mazingira unaotokana na shughuli za usafiri majini.

202. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Aprili, 2023 Shirika la Uwakala wa Meli (TASAC) limeendelea kutoa elimu kuhusu umuhimu na majukumu ya Kituo cha Kuratibu Shughuli za Utafutaji na Uokoaji Majini (Maritime Rescue Coordination Centre – MRCC/ISC) kilichopo Dar es Salaam pamoja na kushiriki mikutano ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa kwa lengo la kuweka mikakati ya kufanikisha zoezi la utafutaji na uokoaji baharini. Aidha, Shirika limeendelea kushirikiana na wadau wa usafiri kwa njia ya maji katika kufanya chunguzi za ajali za vyombo vya usafiri majini kila zinapotokea na kutoa taarifa kwa umma juu ya chanzo na matokeo ya ajali.

203. ***Mheshimiwa Spika,*** Shirika limekamilisha hatua za ununuzi na kumpata Mzabuni wa kujenga boti moja (1) ya matibabu (Ambulance Boat) na boti mbili (2) za Utafutaji na Uokoaji zitakazotumika katika Ziwa Victoria ambapo kwa sasa Taarifa ya Uchambuzi wa Zabuni imewasilishwa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) kwa ridhaa (No Objection) kabla ya kuingia mkataba husika. Aidha, mkandarasi amepatikana kwa ajili ya ujenzi wa Kituo Kikuu cha Uratibu wa shughuli za Utafutaji na Uokoaji (Maritime Rescue Coordination Centre – MRCC) cha kikanda kitakachojengwa eneo la Ilemela Mwanza, ambapo kwa sasa mkandarasi tayari amekabidhiwa eneo kwa ajili ya kuanza shughuli za ujenzi na kazi hiyo inatarajiwa kukamilika katika kipindi cha miezi 18. Vilevile, mkandarasi amepatikana kwa ajili ya kujenga vituo vingine vidogo vitatu (3) vya Utafutaji na Uokoaji (Search and Rescue Stations – SARS) katika maeneo ya Kanyala - Geita, Nansio - Ukerewe na Musoma – Mara na sasa amekabidhiwa maeneo ya ujenzi na anaendelea na maandalizi ya awali. Kazi ya ujenzi inatarajiwa kukamilika ndani ya miezi 12.

204. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha usalama wa usafiri majini, TASAC iliendelea kushirikiana na TMA katika utoaji wa taarifa za hali ya hewa kwa wadau wa usafiri majini. Kutokana na jitihada hizo pamoja na kuwepo kwa matukio ya upepo mkali, hadi kufikia Aprili, 2023 TASAC haikupokea taarifa ya ajali kwa vyombo vya usafiri majini vyenye uzito kuanzia Tani 50 na zaidi. Kwa vyombo vidogo vyenye uzito chini ya Tani 50 TASAC ilipata taarifa za ajali zipatazo nne (4) ikilinganishwa na ajali tano (5) zilizotokea katika kipindi cha mwaka wa 2021/22. Shirika limefanya uchunguzi na kugundua kwamba kutokuwepo kwa matukio ya ajali ya vyombo vya usafiri majini vyenye uzito kuanzia Tani 50 na zaidi kwa kipindi husika kumechangiwa na kuboreshwa kwa kanuni za usimamizi wa vyombo vya usafiri kwa njia ya maji; kuongezeka kwa uelewa wa wananchi kuhusu sheria na kanuni za kuzingatia katika matumizi ya vyombo vya usafiri majini; na kurahisishwa kwa utoaji wa taarifa za hali ya hewa kwa watumiaji wa vyombo vya usafiri kwa njia ya maji.

205. ***Mheshimiwa Spika,*** TASAC pia ilifanya kaguzi kwenye maeneo saba (7) ya bandari kwa kuzingatia miongozo na kanuni za Shirika la Bahari Duniani (IMO). Maeneo hayo ni katika Bandari ya Dar es Salaam eneo la mizigo ya kichele (General Cargo), Gati la Mafuta la Kurasini (Kurasini Oil Jetty – KOJ), Gati la Mafuta Nje ya Bandari ya Dar es Salaam (Single Bouy Mooring – SBM), Kitengo cha Makasha, Bandari ya Kilwa, Bandari ya Tanga na Bandari ya Mtwara.

206. ***Mheshimiwa Spika,*** Shirika liliendelea kutekeleza jukumu lake la kusimamia wataalam wa usafiri kwa njia ya maji. Kwa kuzingatia hili, hadi kufikia Aprili, 2023 TASAC imetoa jumla ya vyeti 14,868 vya Umahiri na Ustadi kwa Mabaharia. Aidha, vyeti vya umahiri na ustadi vilitolewa kwa kuzingatia marekebisho katika Mkataba wa *Standards of Training, Certification and Watchkeeping* (STCW) kwa Mabaharia wa mwaka 2010 ili kuhakikisha kuwa vyombo vya usafiri majini vinaendeshwa na mabaharia wenye sifa na uzoefu unaostahili.

207. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha ushindani, TASAC iliendelea kutoa leseni kwa watoa huduma zinazodhibitiwa na kusimamia masharti ya leseni hizo; kuhakikisha utoaji wa huduma

bora kwa watoa huduma zinazodhibitiwa; kuweka vigezo na viwango vya ubora wa huduma kwa watoa`huduma za bandari na usafiri kwa njia ya maji; na kuweka usawa wa ushindani wa kibiashara. Katika kipindi cha kuanzia Julai, 2022 hadi Aprili, 2023 Shirika lilifanya ukaguzi na ufuatiliaji wa bandari nchini ili kuhakiki uzingatiaji wa viwango vya utendaji kazi na vigezo vya huduma ambapo asilimia 75 kati ya lengo la asilimia 90 ya vigezo vya utendaji vilifikiwa. Aidha, ukaguzi ulibaini kuwa, waendeshaji wa bandari hawakuweza kufikia viwango vilivyowekwa kwenye vigezo vya ujazo wa eneo la kutunza shehena bandarini (Yard Density); muda wa meli kuingia na kutoka bandarini (Ship Turn Around Time); muda wa mizigo kukaa bandarini (Dwell Time). Sababu kubwa ya kutofikia viwango ni ongezeko kubwa la shehena ikilinganishwa na miundombinu iliyopo pamoja na kazi za ujenzi zinazoendelea katika Bandari ya Dar es Salaam.

208. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kipindi cha Julai, 2022 hadi Aprili, 2023 Shirika lilifanya ufuatiliaji kwa vituo 43 ikilinganishwa na vituo vya bandari 30 vilivyofuatiliwa katika kipindi kama hicho kwa Mwaka 2021/22, ikiwa sawa na ongezeko la asilimia 43. Aidha, TASAC ilisajili watoa huduma za bandari kwa kuzingatia Kanuni za Huduma za Bandari kwa asilimia 90 ikilinganishwa na lengo la asilimia 85 kwa mwaka. Ufanisi huu ulifikiwa kutokana na ziara zinazofanyika mara kwa mara za ufuatiliaji na tathmini. Aidha, Shirika lilifanikiwa kufikia lengo la asilimia 85 ya watoa huduma za usafirishaji kwa njia ya maji wanaozingatia viwango vya utendaji na vigezo vya huduma za usafirishaji.

209. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kuzingatia majukumu yake, TASAC imekuwa ikitoa elimu kwa wadau kuhusu marekebisho ya sheria yaliyotokana na Sheria ya Fedha Na. 5 ya mwaka 2022 ambayo yamepunguza mawanda ya majukumu ya kipekee ya TASAC katika kazi za ugomboaji wa shehena. Elimu ilitolewa katika mikoa ya Mtwara, Tanga, Dar es Salaam, Mwanza na Kigoma. Wadau waliopewa elimu hiyo ni pamoja na taasisi za Serikali, sekta binafsi pamoja na wateja ambao wanaingiza na kuondosha bidhaa za kipekee zilizobakia katika majukumu ya TASAC. Elimu hii ililenga kuwajulisha wadau kuondolewa kwa shughuli za uhakiki wa shehena na uwakala wa meli kutoka TASAC na kuhamishiwa sekta binafsi. Aidha, Serikali kupitia TASAC

iliratibu na kufanya kikao kazi na wadau kutoka taasisi mbalimbali za umma na sekta binafsi kwa lengo la kujadili na kutatua changamoto mbalimbali za kiutendaji zinazojitokeza katika utekelezaji wa majukumu ya ugomboaji na uondoshaji shehena. Taasisi hizo ni pamoja na: Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari (TPA), Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA), Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Tume ya Mionzi Tanzania (TAEC), Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (TAA) pamoja na Tume ya Madini Tanzania (TMC).

210. ***Mheshimiwa Spika***, Serikali kupitia TASAC imefanya tathmini ya kiasi cha bidhaa za kipekee itakazozihudumia baada ya mabadiliko ya Sheria ya Fedha Na. 5 ya mwaka 2022. Tathmini hiyo ilifanyika katika mipaka ya Tunduma, Sirari, Kabanga, Rusumo, Namanga, Mutukula, Mwanza, Soko la Madini la Chunya na Katavi. Lengo la tathmini hiyo ilikuwa kupata kiasi cha uingizaji na uondoshaji wa bidhaa zilizobaki ili kuweza kupanga rasilimali mbalimbali katika maeneo hayo.

**Huduma za Uchukuzi Baharini**

211. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu huduma za uchukuzi katika Bahari, Kampuni ya Meli ya China na Tanzania (SINOTASHIP) inayojishughulisha na huduma za uchukuzi wa masafa marefu baharini ambayo inamilikiwa kwa uwiano wa asilimia 50:50 kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China imeendelea kutekeleza majukumu yake. Katika mwaka 2022, kampuni iliendelea kutoa huduma za uchukuzi baharini kwa kutumia meli yake yenye uwezo wa kubeba jumla ya tani 57,000 kwa wakati mmoja.

212. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Januari, 2022 hadi Desemba, 2022 SINOTASHIP ilisafirisha jumla ya tani 610,774 za shehena ya mizigo ikilinganishwa na jumla ya tani 613,112 zilizosafirishwa katika kipindi kama hicho mwaka 2021 ikiwa ni pungufu ya tani 2,338 za mizigo sawa na asilimia 0.3. Upungufu huo ni kutokana na matengenezo ya meli yaliyofanyika katika kipindi hicho. Pia, kampuni iliendelea na biashara ya uwakala na hivyo kuongeza idadi ya meli zilizohudumiwa. Jumla ya makasha 63,529 yalihudumiwa katika bandari ya Dar es Salaam

ikilinganishwa na makasha 56,198 mwaka 2021, sawa na ongezeko la asilimia 13. Mafanikio hayo ni kutokana na kutekeleza mikakati ya kimasoko ya kutafuta mizigo inayoenda nje ya nchi kwa bei shindani.

**Huduma za Uchukuzi Katika Maziwa Makuu**

213. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/23, Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) imeendelea kutoa huduma za uchukuzi na usafiri kwenye Maziwa Makuu ya Victoria, Tanganyika na Nyasa. Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Aprili, 2023 Kampuni ya Huduma za Meli ilisafirisha abiria 170,137 ikilinganishwa na abiria 143,468 waliosafirishwa katika kipindi kama hicho mwaka 2021/22. Aidha, jumla ya tani za mizigo 18,909 zilisafirishwa ikilinganishwa na tani 12,354 zilizosafirishwa katika kipindi kama hicho mwaka 2021/22.

214. ***Mheshimiwa Spika,*** MSCL imeendelea kutekeleza kazi zifuatazo: -

i. Mradi wa Ujenzi wa meli mpya ya MV. Mwanza (Hapa Kazi tu) yenye Uwezo wa kubeba abiria 1,200 na tani 400 za mizigo katika Ziwa Victoria. Ujenzi wa meli hii umekamilika kwa asilimia 83;

ii. Mradi wa ukarabati mkubwa wa meli ya MV Umoja. Meli hii ina uwezo wa kubeba tani 1200 za mizigo na hufanya safari zake kati ya Tanzania na Nchi jirani za Kenya na Uganda katika Ziwa Victoria. Utekelezaji wa mradi umefikia asilimia 75.8; na

iii. Mradi wa ukarabati mkubwa wa meli ya MT Sangara katika Ziwa Tanganyika Mkoani Kigoma. Meli hii ina uwezo wa kubeba mzigo wa mafuta lita 400,000 na hufanya safari zake kati ya Tanzania na nchi Jirani za Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), Burundi, na Zambia. Utekelezaji wa mradi umefikia asilimia 90.7.

215. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia MSCL ipo katika hatua za mwisho za majadiliano na Mkandarasi ili kuwezesha kuanza ujenzi wa meli mpya tatu (3) pamoja na chelezo. Kati ya meli hizo meli

mbili (2) ambazo ni: Meli ya mizigo yenye uwezo wa kubeba tani 3,500 na Meli ya abiria na mizigo yenye uwezo wa kubeba abiria 600 na tani 400 za mizigo zitajengwa katika Ziwa Tanganyika; Meli moja (1) ya mizigo yenye uwezo wa kubeba tani 3,000 za mabehewa ya mizigo itajengwa katika Ziwa Victoria; na Chelezo itakayojengwa Ziwa Tanganyika.

Vilevile, MSCL ilikamilisha taratibu za zabuni kwa ajili ya kumpata Mkandarasi wa ukarabati wa meli ya MV. Liemba tarehe tarehe 5 Machi, 2023. Kwa sasa, majadiliano na Mkandarasi kabla ya kusaini mkataba yanaendelea. Mkataba huo unatarajiwa kusainiwa Julai, 2023. Aidha, MSCL inakamilisha taratibu za kumwajiri Mhandisi Mshauri kwa ajili kufanya tathmini ya kina na kuishauri Serikali kuhusu ukarabati wa meli ya MV. Mwongozo ambayo ilisimamishwa kutokana na changamoto ya msawazo (stability). Kazi hii inatarajia kuanza mwezi Juni, 2023 na kukamilika mwezi Novemba, 2023.

216. ***Mheshimiwa Spika,*** katika jitihada za kufanya maboresho ya utendaji wa Kampuni ya MSCL ikiwa ni pamoja na kukabiliana na upungufu wa watumishi, katika kipindi cha kuanzia Julai, 2022 hadi Aprili, 2023 Serikali imepeleka watumishi watatu (3) kwa kuhamia, imeteua Mkurugenzi Mtendaji na imetoa kibali cha kuajiri watumishi wapya 54. Utekelezaji wa kibali cha kuajiri watumishi wapya unaendelea hadi mwezi Juni, 2023.

**Huduma za Bandari**

217. ***Mheshimiwa Spika,*** Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) imeendelea kusimamia Bandari za Mwambao wa Bahari ya Hindi na za Maziwa Makuu kwa kuendeleza miundombinu na huduma za kibandari; kuweka viwango na masharti kwa watoa huduma za bandari nchini; kusimamia na kudhibiti huduma za bandari, kulinda mazingira na usalama wa bandari kwa viwango vinavyokubalika; na kuweka mazingira mazuri yatakayowavutia wawekezaji kuwekeza katika sekta ya bandari. Aidha, Mamlaka imeendelea kutangaza bandari kimasoko pamoja na kushirikisha na kusimamia sekta binafsi katika uendeshaji wa shughuli za kibandari.

218. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwezi Julai, 2022 hadi Aprili, 2023 TPA ilihudumia shehena yenye jumla ya tani milioni 20.851 ikilinganishwa na shehena ya tani milioni 16.339 iliyohudumiwa katika kipindi kama hicho mwaka 2021/22. Hii ni sawa na ongezeko la asilimia 27.6.

219. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu uhudumiaji wa makasha, katika kipindi cha kuanzia mwezi Julai, 2022 hadi mwezi Aprili, 2023 TPA ilihudumia makasha 765,504 ikilinganishwa na makasha 667,172 yaliyohudumiwa katika kipindi kama hicho mwaka 2021/22 sawa na ongezeko la asilimia 14.7. Ongezeko hilo limetokana na mikakati mbalimbali inayoendelea kutekelezwa ikiwemo ya uboreshaji wa Bandari ya Dar es Salaam.

220. ***Mheshimiwa Spika,*** takwimu zinaonesha kuwa shughuli za kibandari zimeendelea kuwa na mchango mkubwa katika mapato yatokanayo na kodi ya forodha nchini. Mapato hayo yamekua kutoka **Shilingi trilioni 4.621** mwaka 2015/16 hadi kufikia **Shilingi trilioni 7.756** mwaka 2021/22.

221. ***Mheshimiwa Spika,*** katika hatua nyingine, Serikali kupitia TPA inaendelea na utekelezaji wa miradi katika Bandari za Mwambao wa Bahari ya Hindi na
Maziwa Makuu kama ifuatavyo: -

222. ***Mheshimiwa Spika***, kuhusu Awamu ya Pili ya Uboreshaji wa Bandari ya Tanga, Serikali kupitia TPA iliingia Mkataba na Kampuni ya China Harbour Engineering Co. Ltd mwezi Julai, 2020 na kuanza utekelezaji mwezi Desemba 2020 kwa gharama ya **Shilingi bilioni 256.8**. Kazi zinazotekelezwa kwenye Mradi zinajumuisha kuimarisha na kuboresha Gati Na. 1 na 2 zenye urefu wa mita 450. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2023 Mkandarasi amekamilisha na kukabidhi Gati lenye urefu wa mita 300 ambalo limeanza kutumika. Kwa ujumla mradi umekamilika kwa asilimia 99 na kazi zilizobaki zinaendelea kutekelezwa kama ilivyopangwa.

223. ***Mheshimiwa Spika***, kuhusu ujenzi wa Gati la kupokelea mafuta kutoka Uganda lililoko eneo la Chongoleani – Tanga, TPA imekamilisha maandalizi ya miundombinu wezeshi ya mradi huo,

ambapo utekelezaji wake unafanywa kwa pamoja na nchi ya Uganda na kusimamiwa na EACOP (East African Crude Oil Pipeline).

224. ***Mheshimiwa Spika,*** kazi nyingine zilizotekelezwa katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Aprili, 2023 katika miradi ya kuboresha Bandari za Mwambao wa Bahari ya Hindi za Dar es Salaam na Mtwara ni pamoja na:-

i. Kuendelea na kazi za kupanua, kuchimba na kuongeza kina cha lango la kuingilia na kutokea meli katika Bandari ya Dar es Salaam hadi kufikia kina cha mita 15.5, ambapo hadi kufikia Aprili, 2023 mradi ulikuwa umefikia asilimia 96 za utekelezaji;

ii. Utekelezaji wa Mradi wa kuendeleza miundombinu ya kupokea mafuta (Single Receiving Terminal - SRT) katika Bandari ya Dar es Salaam

iii. Serikali kupitia TPA ipo katika hatua za mwisho za kumpata mkandarasi kwa ajili ya ujenzi, sambamba na mshauri mwelekezi wa kusimamia mradi. Aidha, kazi ya ujenzi inatarajiwa kuanza katika mwaka wa Fedha 2023/24; na

iv. Kuendelea na ujenzi wa barabara unganishi kuelekea kwenye gati jipya katika Bandari ya Mtwara, ambapo hadi kufikia Aprili, 2023 mradi ulikuwa umefikia asilimia 90.

225. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa Bandari za Maziwa Makuu, kazi zilizotekelezwa ni pamoja na:-

i. Ujenzi wa Bandari ya Karema katika Ziwa Tanganyika uliohusisha ujenzi wa gati, majengo ya abiria, maghala ya mizigo na ofisi mbalimbali; uongezaji wa kina, *breakwaters* na usawazishaji wa eneo, ambapo mradi huu umekamilika kwa asilimia 100 na umeanza kutumika;

ii. Ujenzi wa Bandari ya Kibirizi na Ujiji katika Ziwa Tanganyika unaohusisha ujenzi wa Gati, majengo ya abiria, maghala ya mizigo, minara ya matanki ya maji, ofisi ya meneja wa Bandari,

uzio na nyumba ya mlinzi, hadi kufikia Aprili, 2023 mradi umefikia asilimia 77;

iii. Mradi wa ujenzi wa gati, ghala la kuhifadhia makaa ya mawe, ghala la abiria, ofisi na sehemu ya kuegesha meli (ramp) Bandari ya Ndumbi katika Ziwa Nyasa, umekamilika kwa asilimia 100 na sasa upo katika kipindi cha matazamio;

iv. Serikali kupitia TPA tayari imeanza maboresho ya ujenzi wa Bandari za Bukoba, Kemondo Bay na Mwanza South, ambapo kazi ya maboresho imefikia asilimia 5 za utekelezaji. Mradi huu unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2024.

v. Serikali kupitia TPA ipo katika hatua za kuandaa makabrasha ya zabuni ya kumpata Mkandarasi atakayefanya maboresho ya ujenzi wa Bandari ya Mwanza North kulingana na mahitaji ya meli mpya.

226. ***Mheshimiwa Spika,*** katika hatua za kurasimisha bandari zisizo rasmi, Serikali kupitia TPA imefanya ukaguzi wa bandari zisizo rasmi **26**, ambapo bandari **20** zilikidhi vigezo na kurasimishwa kwa **GN No. 293** ya tarehe 06 Mei, 2022. Awamu ya Pili ilihusisha bandari zisizo rasmi **14**, ambapo Bandari **10** zimependekezwa kurasimishwa. Awamu ya tatu ya ukaguzi inatarajiwa kufanyika kabla ya Juni, 2023 na itahusisha Bandari zisizo rasmi **78**.

227. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia TPA imefanikiwa kununua vifaa na mitambo 35 kwa ajili ya kutoa huduma za kibandari. Vifaa na mitambo iliyonunuliwa ni kama ifuatavyo:

i. Mashine nne (4) za kunyanyulia makasha (SemiAutomatic Spreader) katika Bandari ya Tanga;

ii. Mashine mbili (2) za kunyanyulia mizigo (16 and 50 Tons Forklift) katika Bandari ya Tanga;

iii. Kreni tatu (3) kubwa za kubeba makasha kutoka katika Meli (Ship to Shore Gantry Cranes) katika Bandari za Dar es Salaam na Mtwara;

iv. Boti nne (4) za kuingiza na kutoa Meli Bandarini (Tug Boats) katika bandari ya Tanga;

v. Mashine ya kuhudumia makasha tupu yenye uwezo wa kubeba tani 8 (Empty Container Handler) katika Bandari ya Tanga;

vi. Kifaa cha kupakulia shehena ya kichele (15 Tons Automatic Grab) katika Bandari ya Dar es Salaam;

vii. Mashine saba (7) za kubeba makasha nchi kavu – (45 Tons Reach Stackers) katika Bandari za Dar es Salaam, Tanga na Kigoma;

viii. Boti tatu (3) za Rubani (Pilot Boats) katika Bandari za Dar es Salaam, Tanga na Mtwara;

ix. Kreni tano (5) kati ya hizo tatu zenye uwezo wa kubeba tani 60 na mbili zenye uwezo wa kubeba tani 25 (Tons All Terrain Mobile Crane) katika Bandari za Dar es Salaam, Itungi na Mtwara;

x. Magari mawili (2) ya zima moto;

xi. Trekta mbili (2) za kuvuta makasha (45 Tons- Terminal Tractor) katika Bandari ya Tanga; na

xii. Mashine ya kubeba na kupanga makasha nchi kavu (41 Tons - Rubber Tyred Gantry Crane) katika bandari ya Tanga.

228. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwezi Julai, 2022 hadi Aprili, 2023 Serikali kupitia TPA iliwajengea uwezo watumishi wake kwa kutekeleza mafunzo mbalimbali kwa watumishi 1,931. Kati ya hao, watumishi 1,440 walishiriki mafunzo ya vikundi, watumishi 389 walishiriki mafunzo ya kitaaluma, watumishi 10 walishiriki mafunzo ya mtu mmoja mmoja na watumishi 92 walishiriki mafunzo ya muda mrefu.

**Ushirikishwaji wa Sekta Binafsi Katika Shughuli za Uendelezaji na Uendeshaji wa Bandari**

229. ***Mheshimiwa Spika,*** Ushirikishaji wa Sekta Binafsi katika uendeshaji wa shughuli za bandari zilianza kuchukuliwa na Serikali mwishoni mwa miaka ya 1990 kupitia Tume ya Kurekebisha Mashirika ya Umma (Parastatal Sector Reform Commission-PSRC). Mwaka 2000, Serikali iliamua kuingia Mkataba na Kampuni binafsi ya Tanzania International Container Terminal Services (TICTS) kwa ajili ya uendeshaji wa Kitengo cha Makontena Gati Na. 8 – 11 katika Bandari ya Dar es Salaam. Katika kipindi chote cha utendaji kazi wa TICTS, Serikali kupitia TPA imepata mafanikio yafuatayo katika kipindi cha mwaka 2001 hadi 2021.

i. Uwekezaji katika manunuzi ya mitambo ya kuhudumia shehena, miundombinu, mifumo ya TEHAMA na kuwajengea uwezo wafanyakazi;

ii. Kuongezeka kwa shehena ya makasha kutoka makasha ya futi ishirini 382,000 mwaka 2012 hadi kufikia makasha 642,000 mwaka 2021 sawa na ongezeko la wastani wa asilimia 8.0 kwa mwaka; na

iii. Kampuni hiyo iliweza kulipa kodi na tozo nyinginezo za Bandari kutoka kiasi cha **Shilingi bilioni 235** mwaka 2012 hadi kufikia **Shilingi bilioni 635** mwaka 2021.

230. ***Mheshimiwa Spika,*** Hata hivyo, pamoja na mafanikio hayo kumekuwa na changamoto kadhaa zikiwemo: -

i. Kushindwa kuchagiza shughuli za kibandari katika mnyororo wa usafirishaji;

ii. Uwekezaji mdogo katika mitambo ya kupakia na kupakua mizigo;

iii. Urasimu wa uondoshaji wa mizigo bandarini; kutokuwa na maeneo ya kutosha nje ya bandari ili kupunguza msongamano bandarini;

iv. Kutofanya ukarabati wa miuondombinu ya bandari, kutofanya ukarabati wa mitambo kwa wakati; na

v. Kutokuwa na mikakati ya kuvutia shehena kupitia Bandari ya Dar es Salaam; kutowekeza katika mifumo ya TEHAMA ya kisasa inayosomana na mifumo iliyopo TPA.

Kwa kutambua kuwa, TPA pekee haitaweza kutatua changamoto za Bandari zilizopo na kuongeza ufanisi wa bandari nchini, Serikali iliamua kuanzisha jitihada za kutafuta wawekezaji ambao watakuwa na uwezo wa kutatua changamoto zilizobainishwa hapo juu.

231. ***Mheshimiwa Spika,*** hatua hizo zimehusisha kukutana na kufanya majadiliano na wawekezaji mbalimbali. Baadhi ya wawekezaji waliojitokeza wameonesha nia ya kuwekeza katika maeneo mbalimbali ya bandari nchini ikiwemo; Bandari ya Dar es Salaam, Bandari ya Tanga, Bandari ya Mtwara, Maeneo ya Bandari Kavu na Bandari za Maziwa Makuu ili kulenga soko la nchi zinazotuzunguka, ambalo linakua kwa kasi. Kama ilivyo kawaida, Bunge lako Tukufu litashirikishwa ipasavyo wakati wa kuridhia Mkataba baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Dubai (Inter Governmental Agreement – IGA) kwa ajili ya ushirikiano wa kuboresha, kuendesha na kuendeleza maeneo ya bandari nchini.

**USAFIRI NA USAFIRISHAJI KWA NJIA YA ANGA**

**Udhibiti wa Huduma za Usafiri kwa Njia ya Anga**

232. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA) imeendelea kutoa huduma za udhibiti wa usafiri wa anga, viwanja vya ndege, masuala ya kiusalama na kiuchumi katika huduma za usafiri wa anga pamoja na kutoa huduma za uongozaji ndege katika viwanja 14 vya Dar es Salaam, Zanzibar, Mwanza, Arusha, Pemba, Tabora, Kigoma, Dodoma, Iringa, Songwe, Mtwara, Tanga, Songea na Kilimanjaro.

233. ***Mheshimiwa Spika,*** Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA) imekuwa ikikaguliwa na Shirika la Kimataifa la Usafiri wa

Anga Duniani (ICAO) kulingana na masharti na viwango vya Shirika hilo. Katika mwaka 2022/23 TCAA ilipata alama za juu katika udhibiti wa sekta ndogo ya Usafiri wa Anga, ambapo TCAA ilipatiwa tuzo yenye jumla ya Dola za Marekani 1,000,000 na Shirika la Usafiri wa Anga Duniani kwa ajili ya kuendelea kuimarisha udhibiti wa usafiri wa anga. Fedha hizo za tuzo pamoja na mambo mengine, zitasaidia kugharamia mafunzo kwa walengwa 170. Mafunzo hayo yanatolewa ndani na nje ya Tanzania katika fani za ukaguzi na utoaji huduma za Usafiri wa Anga; Uchunguzi wa ajali za ndege; Uhandisi wa miundombinu ya viwanja vya ndege; Utoaji wa huduma za ndege (Operators).

234. ***Mheshimiwa Spika,*** TCAA imeendelea kutoa vyeti vya ubora kwa ndege ambapo hadi kufikia Aprili, 2023 jumla ya ndege 16 zilisajiliwa na kufanyiwa ukaguzi na kupewa vyeti vya ubora (Certificate of Airworthiness). Aidha, jumla ya ndege nne (4) ziliondolewa kwenye daftari la usajili baada ya kumalizika kwa mikataba ya ukodishaji. Ndege nyingine 158 zilikaguliwa na kupewa vyeti vya ubora wa kuendelea kufanya kazi. Kwa sasa daftari la usajili wa ndege lina jumla ya ndege 406.

235. ***Mheshimiwa Spika,*** TCAA iliendelea kutoa huduma za uongozaji ndege zinazoruka na kupita katika anga la juu katika nchi za Rwanda na Burundi hadi tarehe 30 Novemba, 2022, ambapo tarehe 1 Desemba, 2022 Tanzania ilikabidhi anga la juu la Rwanda kwa Jamhuri ya Rwanda. Hata hivyo, anga la juu la Burundi limeendelea kukasimishwa kwa Tanzania na Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Anga Duniani (ICAO).

236. ***Mheshimiwa Spika,*** TCAA imeendelea kuonesha ufanisi katika anga za kimataifa ambapo Tanzania kupitia Mamlaka hiyo imechaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Uratibu wa Usafiri wa Anga Barani Afrika (The African Flight Procedure Programme - AFPP) kwa kipindi cha Miaka mitatu (3) kuanzia mwaka 2022/23 – 2024/25. Kazi kubwa ya Kamati hii ni kujadili uendelezaji wa miundombinu ya njia za ndege angani.

237. ***Mheshimiwa Spika,*** pia TCAA imeendelea kudhibiti Viwanja vya Ndege vinavyomilikiwa na Mamlaka ya Hifadhi ya Taifa (TANAPA), Wizara ya Maliasili na Utalii, Mamlaka ya Hifadhi ya

Ngorongoro (NCAA) na Sekta Binafsi. Lengo ni kuimarisha utoaji huduma, kukuza utalii nchini na kuendelea kuhakikisha utekelezaji wa Sheria na Kanuni za uendeshaji wa viwanja vya ndege zinafuatwa.

238. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia TCAA imeendelea kusaini upya na kupitia Mikataba ya usafiri wa Anga (Bilateral Air Services Agreements - BASA) kati ya Tanzania na nchi nyingine ili kufungua soko la usafiri wa anga kwa lengo la kuboresha huduma za usafiri wa anga, kuvutia mashirika mengine kutoa huduma nchini na kuimarisha ushindani katika utoaji wa huduma za usafiri wa anga nchini. Katika kipindi cha kuanzia Julai, 2022 hadi Aprili, 2023 Serikali imeingia Mikataba mipya ya usafiri wa Anga (BASA) kati yake na nchi ya Sudani Kusini na Ufaransa. Aidha, Mikataba ya BASA kati ya Tanzania na nchi za Cameroon, Togo, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Nigeria, Czech, Namibia, Cape Vede na Kenya ilipitiwa upya. Hivyo, hadi kufikia mwezi Aprili, 2023 Tanzania ilikuwa imeingia Mikataba ya BASA na nchi 80 ikilinganishwa na nchi 79 zilizoingiwa katika mwaka 2021/22. Kati ya Mikataba hiyo, Makampuni/Mashirika ya Ndege 25 kutoka nchi 21 yanafanya safari za Ndege 274 kwa juma kati ya Tanzania na nchi hizo.

239. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Aprili, 2023 idadi ya abiria waliotumia usafiri wa anga imeongezeka hadi abiria 4,614,380 ikilinganishwa na abiria 1,748,278 waliotumia usafiri huo katika kipindi kama hicho cha mwaka wa fedha 2021/22 sawa na ongezeko la asilimia 164. Ongezeko hilo limetokana na kuendelea kuimarika kwa biashara ya usafiri wa anga iliyodhoofika wakati wa mlipuko wa UVIKO -19. Kati ya abiria waliosafirishwa, abiria waliosafiri ndani ya nchi ni 2,640,560 na abiria 1,973,820 walisafirishwa nje ya nchi. Tunaendelea kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ubunifu wake wa filamu ya Royal Tour ambayo imechangia kwa kiasi kikubwa katika kutangaza vivutio vya utalii nchini na kuongeza idadi ya watalii.

240. ***Mheshimiwa Spika,*** kupitia usafiri wa anga hadi kufikia Aprili, 2023 mizigo iliyosafirishwa ndani ya nchi ilikuwa tani 4,174.40 ikilinganishwa na tani 2,070.30 zilizosafirishwa katika kipindi cha

mwaka 2021/22. Vilevile, mizigo iliyosafirishwa nje ya nchi ilikuwa tani 24,806.20 ikilinganishwa na tani 12,115.05 zilizosafirishwa katika mwaka 2021/22. Ongezeko la mizigo iliyosafirishwa linatokana na kuendelea kuimarika kwa usafiri wa Anga baada ya kupungua kwa UVIKO -19.

241. ***Mheshimiwa Spika,*** miruko ya safari za ndege hadi kufikia Aprili, 2023 ilikuwa 152,449 ikilinganishwa na miruko 70,931 kwa mwaka 2021/22. Ongezeko hili linadhihirisha kuimarika kwa biashara ya usafiri wa anga baada ya kupungua kwa UVIKO-19 ambao ulisababisha kufungwa kwa anga za nchi nyingi duniani. Aidha, takwimu hizo zinatarajiwa kuongezeka hadi mwaka 2022/23 unaoendelea kumalizika.

242. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Aprili, 2023 TCAA ilitekeleza kazi nyingine kama ifuatavyo:

i. Ufungaji wa mifumo ya kurekodi mawasiliano ya sauti na data kati ya waongoza ndege na marubani katika viwanja vya Pemba, Songwe, Dodoma na JNIA;

ii. Mradi wa ununuzi na ufungaji wa mitambo ya kuongozea ndege kwa njia ya mawasiliano ya sauti (VHF AREA COVER Relay Systems) kati ya waongoza ndege na marubani unaendelea kutekelezwa ambapo uko katika hatua ya uundaji wa mitambo na umefikia asilimia 55. Aidha, mitambo hii itafungwa kwenye viwanja vya ndege vya JNIA, KIA, AAKIA, Pemba, Tanga, Dodoma, Mtwara, Kigoma, Arusha, Songea, Mwanza na Tabora. Vile vile, mitambo hiyo itafungwa kwenye vituo 18 (Relay stations) ambavyo ni Gairo (Morogoro), Matogoro (Songea), Michakaini (Pemba), Nambunga (Newala-Mtwara), Lokisale (Arusha), Kwenjugo (Handeni-Tanga), Mwasen i(Rufiji-Pwani), Kitulo (Njombe), Kaluwe(Mbeya), Mwisi (Igunga-Tabora), Kasulu (Kigoma, Nyamanyama(Biharamulo-Kagera), Ndiso-Sitalike (Katavi), Muganza (Butiama-Mara), Mugumu (Serengeti), Oldean Malanja (Ngorongoro-Arusha), Lubuli (Dodoma) na Ngoli (Dodoma). Mradi huu unatarajiwa kukamilika mwezi Machi, 2024;

iii. Kuhakiki na kuboresha michoro inayoonesha taratibu za utuaji wa ndege (GNSS procedures) kwa kutumia vifaa vya

mawasiliano vya angani (Satellite) na vya ardhini katika viwanja vya Zanzibar, Dodoma, Tabora na Kigoma;

iv. Kufanya matengenezo kinga (Preventive Maintenance) ya mitambo ya kuongozea ndege katika vituo vya mawasiliano vya Gairo, Nyanshana, Lokisale, Kaluwe, Matogolo, Mnyusi, Kasulu na Kazehi pamoja na viwanja vya ndege vya Julius Nyerere Dar es Salaam (JNIA), Abeid Amani Karume Zanzibar (AAKIA), KIA, Mwanza, Dodoma, Songea, Pemba, Tanga, Arusha, Iringa na Songwe;

v. Kufanya matengenezo kinga katika mtambo wa kufundishia waongoza ndege wa Chuo cha Usafiri wa Anga (3D Tower Simulator and Radar Simulator);

vi. Kuhakiki taratibu za utuaji wa ndege (GNSS procedures) kwa kutumia miruko ya ndege (Flight checks) kabla ya kuruhusiwa kutumika katika viwanja vya Mwanza, Arusha na Kilimanjaro;

vii. Uchoraji wa ramani zinazoonyesha vikwazo (obstacle) zinazozunguka kiwanja cha ndege (visual Approach charts) katika viwanja vya Mtwara, Bukoba na KIA;

viii. Uchoraji wa ramani ya kuonyesha njia ya ndege ndani ya uwanja (Aerodrome ground movement charts) katika kiwanja cha Bukoba; na

ix. Jumla ya watumishi 112 walijengewa uwezo katika fani mbalimbali ili kuweza kuongeza tija na uwezo wa kufanya kazi.

**Huduma za Viwanja vya Ndege**

243. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (TAA) imeendelea kutoa huduma kwa kuzingatia Sera, Sheria, Kanuni na Miongozo mbalimbali ya Kitaifa na Kimataifa inayohusiana na Usafiri wa Anga. TAA ina jukumu la kusimamia, kuendesha, kuboresha na kuendeleza viwanja vya ndege 58 vinavyomilikiwa na Serikali.

244. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia TAA imeendelea kusimamia shughuli za uendeshaji wa viwanja vya ndege nchini; kuboresha huduma za usalama katika viwanja kwa kutoa huduma kwa ndege, abiria na mizigo ambapo hadi kufikia Aprili, 2023 idadi ya abiria 3,237,041 waliohudumiwa kupitia viwanja vya ndege vilivyo chini ya TAA sawa na ongezeko la asilimia 35 ikilinganishwa na abiria 2,400,229 waliohudumiwa katika kipindi kama hicho mwaka 2021/22.

245. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia TAA kwa kushirikiana na Wizara ya Afya inaendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuimarisha masuala ya kiafya kwa wasafiri wanaotumia viwanja vya ndege nchini kwa kutenga maeneo maalum katika viwanja vya ndege nchini kwa ajili ya utoaji wa huduma mbalimbali kwa abiria zinazohusiana na magonjwa ya mlipuko kama vile UVIKO-19, EBOLA na homa ya Marburg.

246. ***Mheshimiwa Spika,*** uendeshaji, uendelezaji na usimamizi wa viwanja vya ndege unaongozwa na Kanuni za Kitaifa na Kimataifa. Ili kukidhi matakwa hayo na kuendelea kuvutia mashirika ya ndege, Wizara kupitia TAA imeendelea kuboresha shughuli za ulinzi na usalama katika viwanja vya ndege nchini. Hadi kufikia Aprili, 2023, kazi ya ujenzi wa uzio wa usalama katika Kiwanja cha Ndege cha Dodoma iliendelea ambapo utekelezaji ulifikia asilimia 75; kazi ya uwekaji wa mfumo wa taa za kuongozea ndege katika Kiwanja cha Ndege cha Dodoma ili kukiwezesha kiwanja hicho kutumika kwa saa 24 imeanza na imefikia asilimia 40, na inatarajiwa kukamilika mwezi Agosti, 2023; uboreshaji wa uzio wa usalama wa Kiwanja cha Ndege cha Julius Nyerere pamoja na kufunga mfumo wa ufuatiliaji mienendo ya shughuli za kiusalama na uendeshaji (CCTV) katika eneo linalozunguka barabara ya kutua na kuruka ndege (Runway 05) katika kiwanja hicho ulikamilishwa; na leseni za uendeshaji wa viwanja vya ndege vya Iringa, Musoma, Kigoma na Mtwara zilihuishwa.

247. ***Mheshimiwa Spika,*** TAA inaendelea na maandalizi ya ukaguzi wa Usalama wa Kiwanja cha Kimataifa cha JNIA unaotarajiwa kufanywa na Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Anga Duniani (ICAO) mwishoni mwezi Mei, 2023. Aidha, TAA iliandaa na

kukamilisha programu za ulinzi na usalama katika Viwanja vya Ndege vya Lake Manyara, Arusha, Mwanza, Iringa, Mafia, Lindi, Mpanda, Tanga, Tabora, Songea, Songwe, Moshi na Nachingwea na kufanya maandalizi ya zoezi la kujipima na dharura ya uokozi (Emergency Drills) katika Viwanja vya Ndege vya Mwanza na Kahama.

248. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha huduma za zimamoto viwanjani, Wizara kupitia TAA imeendelea kuhakikisha kunakuwepo na madawa ya kuzima moto, vifaa mbalimbali vya uokoaji pamoja na kufanya matengenezo ya mitambo na vituo vya zimamoto katika viwanja vya ndege vinavyomilikiwa na Serikali. Hadi kufikia Aprili, 2023, kazi ya utengenezaji wa mitambo miwili (2) ya zimamoto kwa ajili ya Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNIA) na Kiwanja cha Ndege cha Dodoma iliendelea.

249. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia TAA imekamilisha maandalizi ya mahitaji ya kiufundi na ununuzi wa Mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa majengo ya abiria katika viwanja vya ndege vya Mpanda, Songea, Kahama na maandalizi ya kiufundi kwa ajili ya ununuzi wa Mhandisi Mshauri wa kusanifu Jengo la Waongoza Ndege katika Kiwanja cha Ndege Bukoba. Mamlaka ipo katika hatua za mwisho za ununuzi wa huduma za ushauri wa kitaalam kwa ajili ya kufanya tathmini ya matabaka ya lami katika barabara za kuruka na kutua ndege kwa viwanja vya ndege vya JNIA, Tabora, Mwanza, Dodoma na Mpanda. Pia, TAA imeendelea kuratibu utekelezaji wa Hati ya Makubaliano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Ufaransa juu ya usanifu wa maboresho na upanuzi wa Jengo la Pili la Abiria (JNIA Terminal II). Ujenzi wa mradi unatarajiwa kuanza katika mwaka wa fedha 2023/24.

250. ***Mheshimiwa Spika,*** Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (TAA) imeendelea kuimarisha utendaji wake katika utoaji wa huduma katika viwanja vya ndege nchini. hadi kufikia Aprili, 2023 TAA ilitoa mafunzo kwa wafanyakazi 583 katika nyanja mbalimbali ikiwemo zimamoto na uokoaji, uendeshaji na usalama. Mafunzo hayo yanalenga kuongeza ufanisi wa utoaji huduma katika viwanja vya ndege nchini.

251. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha kuwa, TAA inaendana na kasi ya ukuaji wa shughuli za usafiri wa anga nchini unaopelekea mahitaji ya upanuzi na ujenzi wa viwanja vipya, imeendelea na juhudi za utwaaji, upimaji na upatikanaji wa Hati Miliki. Hadi kufikia Aprili 2023 jumla ya Hati Miliki kumi (10) za viwanja vya ndege vya Iringa, Chunya, Biharamulo, Morogoro, Kahama, Ifakara, Urambo, Njombe, Lake Manyara na Bukoba zimepatikana. TAA imekamilisha ulipaji wa fidia kwa ajili ya utwaaji wa eneo la ziada litakalosimikwa mifumo ya taa za kuongozea ndege katika Kiwanja cha Ndege Dodoma na eneo la upanuzi katika kiwanja cha ndege cha Kibondo. Pia, TAA imekamilisha uthamini wa wananchi wanaopisha upanuzi wa Kiwanja cha Ndege JNIA, Simiyu, Kilwa Masoko, Ukerewe na Nachingwea na taratibu za malipo ya fidia kwa wananchi hao zipo katika hatua mbalimbali za kupata idhini. Vilevile, TAA imeshughulikia mgogoro wa ardhi katika kiwanja cha Mtwara, ambapo imefanya vikao na Viongozi wa Mkoa na wawakilishi wa wananchi. Matarajio mwafaka utapatikana kabla ya Julai, 2023.

252. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia TAA inaendelea kuboresha huduma katika viwanja vya ndege ili kuongeza ufanisi na mapato. Aidha, TAA inaendelea kuimarisha mifumo ya maegesho ya magari ambapo kazi za ufungaji mifumo ya kielektroniki ya maegesho ya magari katika viwanja vya ndege vya Dodoma na Mwanza zimekamilika kwa asilimia 75 na asilimia 30 mtawalia. Vilevile, TAA inatarajia kuanza kutoa huduma kwa watu mashuhuri (VIP) katika viwanja vya ndege vya Dodoma na Arusha ambapo taratibu za kuwapata wawekezaji kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya kupumzikia wasafiri (Lounges) zinaendelea.

253. ***Mheshimiwa Spika,*** kuna suala muhimu ambalo kila mara Waheshimiwa Wabunge wamekuwa wakilihoji ambalo ni kurejesha jukumu la ujenzi wa Viwanja vya ndege kwa TAA kutoka TANROADS. Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa Serikali imechukua maamuzi ya kulirejesha jukumu hilo kwa TAA kama ilivyokuwa awali. Hata hivyo, kwa kuwa jukumu hili limetekelezwa kwa muda mrefu (tangu 2018) na TANROADS, Serikali imeona ni busara na ili kutoathiri utekelezaji wa miradi

inayoendelea, baadhi ya miradi ambayo imefikia hatua kubwa ya utekelezaji ikamilishwe na TANROADS na miradi mipya na iliyoanza hivi karibuni (isipokuwa ile inayogharamiwa kwa fedha za wafadhili) itekelezwe na TAA. Kwa sasa uchambuzi zaidi unaendelea ili kukamilisha taratibu mbalimbali ikiwemo kufanya marekebisho ya miundo na masuala ya kisheria.

254. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu utaratibu wa urejeshaji wa shughuli za uendeshaji wa kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro (KIA) chini Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (TAA), Wizara kwa kushirikiana na wadau muhimu ikiwemo Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, imewasilisha Serikalini mapendekezo ya kutungwa kwa Sheria mahsusi ya TAA kwa ajili ya kuwezesha Viwanja vyote vya Ndege nchini, ikiwemo KIA, kuwa chini ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege. Kupitia Sheria hii, TAA inaweza kukasimu jukumu la uendeshaji wa kiwanja kwa taasisi nyingine pale ambapo itaonekana inafaa.

255. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai hadi Aprili 2023, Kiwanja cha Ndege cha Kilimanaro (KIA) kilitoa huduma za usafiri wa anga kwa Mashirika 12 ya Ndege yenye ratiba maalum za safari. Aidha, KADCO ilihudumia mashirika mengine yasiyokuwa na ratiba maalum ambapo hivi karibuni KIA ilipokea Ndege (Charter Flights) kutoka Israel, India, Mashariki ya Kati na Maldives. Mashirika hayo huleta watalii na watu mashuhuri wanaotembelea vivutio mbalimbali vilivyomo nchini kama vile Mlima Kilimanjaro, mbuga za wanyama, visiwa vya Zanzibar pamoja na kushiriki mikutano ya kimataifa.

256. ***Mheshimiwa Spika,*** uendeshaji wa KIA umeendelea kuimarika baada ya kupita kwa Janga la UVIKO-19. Hadi kufikia Aprili, 2023 jumla ya abiria 783,669 walihudumiwa ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 48 ikilinganishwa na abiria 528,125 waliohudumiwa katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2021/22. Ongezeko hili la abiria lilichangiwa na kuongezeka kwa idadi ya watalii baada ya uzinduzi wa filamu ya *Royal Tour* uliofanywa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, pamoja na juhudi za kuendelea kukitangaza Kiwanja cha KIA kwenye masoko ya kimataifa.

257. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Aprili, 2023 KIA ilihudumia mizigo kiasi cha tani 4,340 ikilinganishwa na tani 3,491 iliyohudumiwa katika kipindi kama hicho mwaka 2021/22 ikiwa ni ongezeko la tani 849 za mizigo sawa na ongezeko la asilimia 24. Ongezeko la mizigo limetokana na kuanza usafirishaji wa mbogamboga na matunda kwa wastani wa tani 6 hadi tani 11 kwa safari moja ya ndege na pilipili ambazo husafirishwa kwa wastani wa tani 3 kwa safari moja ya ndege. Mazao haya husafirishwa na mashirika ya ndege ya Kimataifa kuelekea Miji ya London – Ungereza, Frankfurt–Ujerumani na Liege – Ubelgiji ambayo yanafanya safari katika Kiwanja cha Ndege cha KIA mara nane (8) kwa wiki.

258. ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na kuendelea kuimarika kwa shughuli na makusanyo katika uwanja wa ndege wa KIA, kuna changamoto ya uvamizi wa ardhi. Mchakato wa kutatua changamoto hii unaendelea ambapo hadi kufikia Aprili, 2023 mambo yafuatayo yalifanyika: -

i. Uwekaji wa alama za kudumu kwenye mpaka wote wa kiwanja umefanyika ambapo mawe (beacons) 186 yalisimikwa kwa kufuata mpaka wenye urefu Kilometa 153;

ii. Jumla ya wananchi 1,712 waliobainika kuwa kwenye eneo la KIA wamefanyiwa uthamini wa maendelezo waliyofanya kwa hatua zaidi; na

iii. Kuendelea na zoezi la uhakiki wa taarifa za wananchi kwa lengo la kukamilisha taarifa ya uthamini kabla ya hatua ya kulipa fidia.

259. ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie fursa hii kuwashukuru wananchi walioridhia kupisha eneo hilo kwa ajili ya shughuli za kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro. Aidha, tunashukuru kwa ushirikiano wa waheshimiwa wabunge wa maeneo hayo hasa Mhe. Mhe. Saashisha Mafuwe, Mbunge wa Hai na Mhe. Dkt. John Pallangyo, Mbunge wa Arumeru Mashariki na uongozi wa mikoa ya Kilimanjaro na Arusha, pamoja na Kamati ya Mawaziri iliyoshughulikia migogoro ya ardhi nchini.

**Huduma za Usafiri kwa Njia ya Anga**

260. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2022/23 Serikali imeendelea na juhudi za kuimarisha Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL). Juhudi hizo zinajumuisha ununuzi wa ndege mpya na uboreshaji wa miundombinu ya uendeshaji. Uboreshaji wa miundombinu unalenga kuipunguzia ATCL gharama za uendeshaji na kuifanya iwe shindani katika soko la usafiri wa anga duniani.

261. ***Mheshimiwa Spika,*** miongoni mwa maeneo muhimu ambayo Serikali imeendelea kutekeleza katika uimarishaji wa ATCL ni pamoja na kuendelea na usimamizi wa utengenezaji wa ndege mpya nne (4). Ndege hizo zitasaidia kuiongezea ATCL kupanua mtandao wa safari za ndani na nje ya nchi ili kuchochea ukuaji wa sekta nyingine za uchumi kama utalii, biashara, kilimo, mifugo, uvuvi, nk. Ndege mpya zilizonunuliwa ni: Boeing 767-300F moja (1) ya mizigo inayotarajiwa kuwasili mwishoni mwa mwezi Mei, 2023; Boeing 737-9 mbili (2) zinazotarajiwa kuwasili mwezi Agosti na Disemba, 2023; na Boeing 787-8 Dreamliner ndege moja (1) inayotarajiwa kuwasili mwezi Februari, 2024.

262. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwezi Julai, 2022 hadi Aprili, 2023 ATCL kwa kutumia ndege 11 ilizonazo imeendelea kutoa huduma ya usafiri wa anga ndani na nje ya nchi. Jumla ya vituo ambavyo ATCL imetoa huduma ni 24 ambapo vituo 14 ni vya ndani ya nchi na vituo 10 ni vya nje ya nchi. Vituo vya ndani ya nchi ni Arusha; Bukoba; Dar es Salaam; Dodoma; Geita; Kilimanjaro; Kigoma; Songwe; Mpanda; Mtwara; Mwanza; Songea; Tabora na Zanzibar na vituo vya nje ya nchi ni: Bujumbura; Entebbe, Hahaya; Guangzhou; Harare; Lubumbashi; Lusaka; Mumbai; Nairobi na Ndola.

263. ***Mheshimiwa Spika,*** abiria waliosafirishwa katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Aprili, 2023 ni 905,905 ikilinganishwa na abiria 660,766 waliosafirishwa katika kipindi kama hicho mwaka 2021/22 sawa na ongezeko la asilimia 37. Kati ya hao, abiria 682,154 walikuwa wa ndani ya nchi na abiria 223,751 walikuwa wa nje ya nchi. Ongezeko hili limechangiwa na kufanya vizuri kwa vituo

vipya vya Ndola, Lubumbashi na Nairobi ambapo, ujazo wa ndege (load factors) katika vituo hivyo umeongezeka kufikia asilimia 59 ikilinganishwa na asilimia 31 katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2021/22. Pia, idadi ya abiria imeongezeka kutokana na ATCL kurejesha safari zake Guangzhou nchini China, pamoja na ongezeko la miruko kwa baadhi ya vituo vya ndani.

264. ***Mheshimiwa Spika,*** kipindi cha Julai, 2022 hadi Aprili, 2023 ATCL iliweza kusafirisha jumla ya tani za mizigo 2,893 ndani na nje ya nchi ikilinganishwa na tani 1,958 zilizosafirishwa katika kipindi kama hicho mwaka 2021/22. Ongezeko hilo la mizigo ni sawa na asilimia 48 ambalo limechangiwa kwa kiasi kikubwa na kuongezeka kwa mizigo kutoka Guangzhou na Mumbai ambayo ilijumuisha mizigo ya ndani ya nchi na mizigo iliyopitia nchini kuelekea vituo vya Lusaka, Harare, Juba na Afrika Kusini.

265. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha ATCL inaongeza wigo wa uuzaji wa tiketi zake na utoaji wa huduma imeingia mashirikiano ya kibiashara ya kubebeana abiria (interline) na mashirika mengine ya ndege. Hadi kufikia Aprili 2023, ATCL imeingia mikataba ya ushirikiano na mashirika 11 ambayo ni Air India, Qatar Airways, Emirates, Ethiopian Airlines, APG Airlines, Hahn Air, Rwanda Air, Precision Air, Oman Air, KLM na LAM Mozambique. Pia, ATCL ipo kwenye hatua za mwisho za kuingia kwenye mashirikiano na mashirika mengine ambayo ni Turkish Airlines, Fly Dubai na Egypt Air.

266. ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na mpango wa Serikali wa kuongeza ndege mpya nne (4), ATCL inatarajia kupanua wigo wa safari zake kwa kuongeza vituo vipya sita (6) vya nje ambavyo ni Juba; Dubai; Kinshasa; Lagos; London na kurejesha safari katika kituo cha Johannesburg nchini Afrika Kusini. Aidha, kwa safari za ndani ya nchi, ATCL inatarajia kuanzisha safari katika kituo cha Iringa, Musoma na Nachingwea.

267. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuhakikisha kuwa gharama zake za uendeshaji zinapungua, ATCL imeweka mikakati mbalimbali ya kuifanya kuwa shindani katika soko duniani. Miongoni mwa mikakati hiyo ni pamoja na ATCL kujihudumia yenyewe kwa kuhudumia abiria, mizigo, na ndege kiwanjani, kufanya

matengenezo makubwa na madogo kwa ndege zote na kuongeza uwezo wa kutoa mafunzo nchini kwa marubani, wahandisi wa ndege na wahudumu wa ndege kwa kushirikiana na vyuo vya ndani ikiwa ni pamoja na Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) na Chuo cha Usafiri wa Anga (CATC).

268. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kutekeleza mikakati hiyo, Serikali imeendelea kuiwezesha ATCL kuendelea na ukarabati na maboresho ya karakana kubwa ya matengenezo ya ndege iliyopo Mkoani Kilimanjaro (Kilimanjaro Maintenance Facility – KIMAFA) ambayo imefikia asilimia 85. Ukarabati huu umeiwezesha ATCL kufanya matengenezo ya kiwango cha "C Check" kwa ndege aina ya Boeing 787-8 Dreamliner na Dash 8 Q400 na kufanya matengenezo yote madogo madogo kwa ndege zake zote.

269. ***Mheshimiwa Spika,*** mikakati mengine inayotekelezwa na ATCL ni kuajiri na kuwaendeleza watumishi katika kada maalum ambazo ni pamoja na Urubani na Uhandisi. Hadi kufikia Aprili, 2023 ATCL iliajiri marubani tisa (9) na hivyo kufanya jumla ya marubani kuwa 108. Aidha, ATCL inatarajia kuajiri wahudumu wa ndege 43 na hivyo kufanya jumla ya wahudumu wa ndege kufikia 164**.** Watumishi wa kada nyingine zilizobaki wameongezeka hadi kufikia 389 ikilinganishwa na watumishi 382 waliokuwepo Juni, 2022**.** Ongezekeo hilo la watumishi limefanya ATCL kuwa na watumishi 792 ikilinganishwa na watumishi 613 katika mwaka 2021/22.

## HUDUMA ZA HALI YA HEWA

270. ***Mheshimiwa Spika,*** Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) imeendelea kutoa, kusimamia, kudhibiti na kuratibu utoaji wa huduma za hali ya hewa nchini. TMA pia imeendelea kutoa tahadhari kuhusiana na hali mbaya ya hewa, kufanya tafiti za kisayansi za mabadiliko ya hali ya hewa na tabianchi, kubadilishana taarifa za hali ya hewa katika mtandao wa dunia (Global Telecommunication System – GTS) kulingana na makubaliano ya Kimataifa pamoja na kuiwakilisha nchi katika masuala ya hali ya hewa Kikanda na Kimataifa.

271. ***Mheshimiwa Spika,*** TMA imeendelea kutoa huduma za utabiri wa hali ya hewa wa kila siku, siku kumi na ule wa muda mrefu pamoja na tahadhari ya matukio ya hali mbaya ya hewa na kusambaza kwa wananchi ili kuhakikisha usalama wa watu na mali zao pamoja na kuchangia katika kuimarisha utendaji wa shughuli za kiuchumi na kijamii. Usahihi wa utabiri wa hali ya hewa unaotolewa na TMA kwa sasa umefikia asilimia 94 ambao ni juu ya asilimia 70 ya kiwango cha usahihi kinachokubalika na Shirika la Hali ya Hewa Duniani.

272. ***Mheshimiwa Spika***, usahihi wa utabiri umechangiwa kwa kiasi kikubwa na uboreshaji wa miundombinu na huduma za hali ya hewa ikiwemo ununuzi wa vifaa na mitambo ya kisasa ya hali ya hewa. Serikali imeendelea kutekeleza mradi wa kununua na kufunga Rada nne (4) za hali ya hewa. Rada mbili (2) tayari zimeshapokelewa na kazi ya ufungaji wa rada hizo inaendelea katika mikoa ya Mbeya na Kigoma na Rada nyingine mbili (2) zitakazofungwa mkoani Dodoma na Kilimanjaro zinaendelea kutengenezwa nchini Marekani.

273. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia TMA imetekeleza kazi nyingine kama ifuatavyo:-

i. Kukamilika kwa ukarabati wa Ofisi za hali ya hewa za Mahenge na Songea pamoja na nyumba tatu (3) za wafanyakazi zilizopo Mahenge;

ii. Kuendelea kutekeleza mpango wa mafunzo kwa watumishi 74 kati yao 64 waliendelea na masomo na wengine 10 walihitimu mafunzo katika vyuo mbalimbali ndani na nje ya nchi;

iii. Kufanya tafiti mbalimbali za hali ya hewa na mabadiliko ya tabianchi. Jumla ya tafiti nne (4) zilichapishwa katika majarida ya kimataifa ya kisayansi;

iv. Kutekeleza mifumo ya udhibiti wa ubora katika utoaji wa huduma za hali ya hewa kwa usafiri kwa njia ya maji, uendeshaji wa Kituo Maalum cha Kanda kilichopo Dar es Salaam kwa ajili ya kutoa miongozo ya utabiri wa hali ya hewa kwa nchi zilizopo katika ukanda wa Ziwa Victoria;

v. Kuendelea kupanua wigo na kuongeza ufanisi wa kufikisha huduma za hali ya hewa kwa wananchi kwa kuongeza idadi ya redio, luninga pamoja na magazeti yanayotoa matangazo ya hali ya hewa na elimu. Hadi kufikia Aprili, 2023, taarifa za hali ya hewa zinatolewa katika luninga 14 na vituo vya redio 86 pamoja na magazeti mawili (2); na

vi. Kuiwakilisha Tanzania Kikanda na Kimataifa katika masuala ya hali ya hewa. Mamlaka ilishiriki katika mikutano 56 ikiwemo mkutano wa 15 wa watumiaji wa data na huduma zitolewazo na Shirika la EUMETSAT Barani Afrika, uliofanyika Dar es Salaam. Aidha, watumishi 18 walishiriki katika semina 25 za mafunzo ya hali ya hewa na hivyo kujenga uwezo wa utoaji wa huduma za hali ya hewa nchini.

**B.3 TAASISI ZA MAFUNZO**

274. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi inasimamia Taasisi za Mafunzo ili kuandaa wataalam na kujenga uwezo wa rasilimali watu wanaotoa huduma katika Sekta ya Usafiri na Usafirishaji. Utekelezaji wa majukumu ya Taasisi hizo kwa mwaka 2022/23 ni kama ifuatavyo:

**Taasisi ya Teknolojia ya Ujenzi**

275. ***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi ya Teknolojia ya Ujenzi (Institute of Construction Technology – ICoT) ina jukumu la kutoa mafunzo ya muda mrefu katika fani za Ujenzi, Umeme na Mitambo katika ngazi za Astashahada na Stashahada ili kuzalisha wataalam watakaohudumia Sekta ya Ujenzi; kuendesha mafunzo maalum kwa wahitimu wa fani za kihandisi ili kuwaandaa na kuwajengea uwezo wahitimu ikiwa ni pamoja na kuendesha mafunzo ya matumizi ya Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi katika kazi za ujenzi na matengenezo na ukarabati wa barabara. Majukumu mengine ni: kufanya utafiti wa teknolojia mbalimbali katika Sekta ya Ujenzi, kuandaa, kuchapisha na kusambaza majarida yahusuyo teknolojia hizo, kufanya tathmini ya mafunzo yanayotolewa kulingana na mahitaji ya wakati husika ili kubainisha maeneo ambayo wataalam wa Sekta ya Ujenzi na Uchukuzi wanahitaji maarifa mapya ili kuandaa mafunzo ya

kupunguza pengo lililopo katika masuala ya maarifa, ujuzi na teknolojia. Kituo kina Kampasi mbili; Morogoro na Mbeya.

276. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili, 2023, ICoT Kampasi ya Morogoro ilidahili wanafunzi wapya 98 sawa na asilimia 65 ya malengo ya udahili kwa ngazi ya Astashahada ambapo wanafunzi waliojiunga na kuanza masomo kwa ngazi ya astashahada kwa mwaka 2022/23 ni wanafunzi 74 sawa na asilimia 49 ya malengo; na wanafunzi 66 wanaendelea na mafunzo kwa ngazi ya Astashahada ya Juu na Stashahada. Taasisi inaendelea kudahili wanafunzi wapya katika ngazi ya VET I, ambapo wanafunzi 141 wameanza masomo ya mwaka wa kwanza kati ya wanafunzi 200 waliokadiriwa kudahiliwa ikiwa ni sawa na asilimia 70.5 ya lengo la udahili. Wanafunzi 212 wanaendelea na masomo ya ngazi ya VET II. Aidha, Taasisi inaendelea kutoa mafunzo kwa wanafunzi 353 kwa ngazi ya ufundi stadi.

277. ***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi vilevile inaendelea kutoa mafunzo mbalimbali ya kozi za muda mfupi kwa washiriki 270 katika Nyanja za udereva wa awali, udereva wa magari ya abiria na Mafunzo ya matengenezo na uendeshaji wa mitambo ya kazi za barabara. Taasisi inaendelea kufanya matengenezo ya magari na mitambo na imeweza kununua vipuri vya matengenezo ya magari na mitambo. Aidha, maandalizi ya ujenzi wa jengo jipya la Taaluma na Utawala katika Kampasi ya Morogoro yanaendelea.

278. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Kampasi ya Mbeya, hadi Aprili, 2023 Taasisi imeweza kuendesha kozi tano (5) zenye jumla ya washiriki 89 sawa na asilimia 89 ya lengo. Aidha, Taasisi imeshiriki mikutano iliyoandaliwa na Bodi ya Wahandisi (ERB), Bodi ya Wasanifu na Wakadiriaji Majenzi (AQRB) na Taasisi ya Wahandisi Tanzania (IET).

Vilevile, Taasisi inaendelea kufanya matengenezo ya miundombinu ya maji safi, maji taka, majengo, umeme na usafi wa mazingira. Kwa sasa Taasisi inaendelea kufanya matengenezo ya magari na mitambo, imeweza kukarabati jengo

moja (1) litakalokuwa na vyumba vya madarasa, Ofisi na maktaba.

**Chuo cha Bahari Dar es Salaam (DMI)**

279. ***Mheshimiwa Spika,*** Chuo cha Bahari Dar es Salaam (Dar es Salaam Maritime Institute - DMI) kimeendelea kutoa Kozi za Umahiri (Certificates of Competency) katika masuala ya usafiri kwa njia ya maji kwa kuzingatia viwango vilivyowekwa na Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC) na Shirika la Bahari Duniani (IMO). Aidha, Chuo hiki kinaendesha mafunzo yake kwa kuzingatia Ubora wa Viwango vya Kimataifa yaani *ISO 9001:2015* na kinatambuliwa na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET).

280. ***Mheshimiwa Spika,*** Chuo cha DMI katika mwaka 2022/23 kilidahili jumla ya wanafunzi 8,080 ikilinganishwa na wanafunzi 5,091 waliodahiliwa katika mwaka 2021/22 sawa na ongezeko la asilimia 58.7. Kati ya hao, wanafunzi 4,575 wamejiunga na mafunzo ya muda mfupi na wanafunzi 3,505 wamejiunga na mafunzo ya muda mrefu. Chuo kimeendelea kuwajengea uwezo watumishi wake ambapo jumla ya watumishi 15 wanaendelea na mafunzo ya muda mrefu ambayo ni Shahada ya Uzamivu (5), Shahada ya Uzamili (8) na mafunzo ya vitendo (2).

281. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2022/23, Serikali kupitia DMI iliendelea kuratibu ununuzi wa mtambo wa kufundishia (full mission crane simulator) ili kuongeza ubora na umahiri katika utoaji wa mafunzo ya kutumia mitambo maalum ya kuhudumia mizigo kwenye meli na vyombo vingine vya Usafirishaji. Aidha, malipo ya awali ya mtambo huo yamefanyika.

**Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT)**

282. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) imeendelea kutoa mafunzo, kufanya tafiti, kutoa ushauri wa kitaalam na machapisho kwa lengo la kufundisha wataalam katika njia za usafirishaji ambazo ni Barabara, Anga, Reli, Maji na Bomba (Pipeline). Katika mwaka wa masomo 2022/23, Chuo kilitoa mafunzo ya kozi ndefu 34 ikilinganishwa na

kozi 33 zilizotolewa katika mwaka wa masomo 2021/22 ikiwa ni ongezeko la kozi moja (1) sawa na asilimia 3. Kwa sasa Chuo kina wanafunzi wa kozi ndefu 14,920 ikilinganishwa na wanafunzi 12,942 katika mwaka wa masomo 2021/22 ikiwa ni ongezeko la wanafunzi 1,978 sawa na asilimia 15. Aidha, jumla ya wanafunzi 2,772 walihitimu mafunzo ya kozi za muda mrefu katika mwaka wa masomo 2021/22 ikilinganishwa na wanafunzi 1,843 katika Mwaka wa Masomo 2020/21. Hili ni ongezeko la wahitimu 929 sawa na asilimia 50.4.

283. ***Mheshimiwa Spika,*** NIT imeendelea kutekeleza mradi wa kuanzisha Kituo cha Umahiri cha Mafunzo ya Usafiri wa Anga na Operesheni za Usafirishaji unaofadhiliwa na Benki ya Dunia. Mradi huo utaimarisha miundombinu na ununuzi wa vifaa vya kufundishia ambapo unajumuisha ujenzi wa majengo nane (8) ikiwa majengo matano (5) yanajengwa katika Kampasi ya Mabibo Dar-es-Salaam kwa ajili ya kufundishia Wahandisi wa Ndege na Wahudumu wa Ndani ya Ndege na majengo matatu (3) yatajengwa katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA) kwa ajili ya mafunzo ya Marubani. Aidha, ujenzi wa majengo matano (5) unaendelea ambapo umefikia hatua ya kusimamisha nguzo za jengo hilo na ujenzi wa majengo matatu (3) upo katika hatua za kumpata Mshauri elekezi wa usanifu.

284. ***Mheshimiwa Spika***, vilevile kupitia kituo cha umahiri cha mafunzo ya taaluma za usafiri wa anga na operesheni za usafirishaji kilichoanzishwa chini ya mradi unaofadhiliwa na Benki ya Dunia, NIT imenunua vifaa vya mafunzo. Vifaa hivyo ni: *Aircraft Engineering System Trainers; Virtual Maintenance Trainer* kwa ajili ya mafunzo ya Uhandisi wa Matengenezo ya Ndege; na *Fixed Cabin Crew Mock – Up* kwa ajili ya mafunzo ya Wahudumu wa ndani ya Ndege.

285. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuimarisha mafunzo ya taaluma za usafiri wa anga, Serikali kupitia NIT imenunua Ndege mbili (2) zenye injini moja (1) kwa ajili ya kufundishia Marubani pamoja na *Full Motion Cabin Crew Mock-Up* yaani kifaa maalum cha kufundishia Wahudumu wa ndani ya Ndege.

286. ***Mheshimiwa Spika***, NIT imeendelea kuwajengea uwezo wakufunzi ili kuweza kutoa mafunzo yenye ubora na yanayoendana na mabadiliko ya sayansi na teknolojia duniani. Katika Mwaka wa Fedha 2022/23, jumla ya watumishi saba (7) wamepelekwa katika mafunzo ya muda mrefu na kufanya jumla ya watumishi 66 kuwa katika mafunzo. Kati ya watumishi hao, 35 wanasoma Shahada ya Uzamivu, 19 Shahada ya Uzamili, mmoja (1) Shahada ya Kwanza, watatu (3) mafunzo ya Urubani (Integrated Commercial Pilot License Course - ICPL) na wanane (8) mafunzo ya Leseni ya Matengenezo ya Ndege (Basic Aircraft Maintenance Technician License). Aidha, Chuo kinaendelea kuandaa rasimu za nyaraka za uanzishwaji wa Chuo Kikuu cha Taifa cha Usafirishaji kwa ufadhili wa Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China ambapo rasimu za nyaraka 30 kati ya 38 zimekamilika.

287. ***Mheshimiwa Spika***, NIT kupitia Kituo cha Kikanda cha Umahiri cha Mafunzo ya Usalama Barabarani kilichoanzishwa kwa ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) kimeendelea kutekeleza majukumu yake. Hadi kufikia Aprili, 2023, tathmini ya kumpata Mshauri Elekezi ambaye ataandaa mitaala na miongozo ya kufundishia pamoja na kupata ithibati ya kimataifa ipo kwenye hatua za mwisho. Aidha, Kituo kupitia ufadhili wa AfDB kinaendelea na hatua za ununuzi wa vifaa vya kufundishia mafunzo ya Usalama Barabarani ikiwemo *Teleconferencing System* pamoja na *Geographic Information System (GIS) and Remote Sensing.*

**Chuo cha Usafiri wa Anga Dar es Salaam (CATC)**

288. ***Mheshimiwa Spika,*** Chuo cha Usafiri wa Anga (CATC) ni Chuo kilichosajiliwa kutoa Mafunzo ya Usafiri wa Anga. Chuo hiki kina jumla ya wakufunzi 21 ambao ni Watanzania waliothibitishwa na TCAA (Certified National Aviation Security Instructors). Kati ya hao, wakufunzi tisa (9) wamethibitishwa na ICAO (ICAO Aviation Security Certified Instructors). Hatua hii ya uthibitisho (Certification) inakifanya chuo hiki kuwa na hadhi ya kutoa mafunzo kimataifa kwenye eneo la usalama wa usafiri wa anga.

289. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza azma ya Serikali ya kutekeleza mkakati wa kujenga uwezo na kutumia wataalam wa ndani, CATC imeendelea kutoa mafunzo katika taaluma mbalimbali zikiwemo za: uongozaji ndege (Air Traffic Controllers); ufundi wa mitambo ya kuongozea ndege na mawasiliano (Communication, Navigation and Surveillance); Mawasiliano ya Taarifa za Anga (Aeronautical Information); na Usalama wa Anga na Upekuzi (Aviation Security). Aidha, taalum nyingine ni katika usimamizi na uandaaji wa safari za ndege (Flight Operations); Usafirishaji wa Bidhaa Hatarishi (Dangerous Goods); Makosa ya Kibinadamu (Human factor); urushaji wa ndege zisizokuwa na rubani (Drone pilot training); na usimamizi wa viwanja vya ndege (Airport Management).

290. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Aprili 2023, CATC kilitoa mafunzo kwa washiriki 1,750 kati ya hao washiriki wa ndani walikuwa 1,529 wanaotoka mashirika ya ndege, viwanja vya ndege vya Serikali na binafsi, Mamlaka ya Usafiri wa Anga (TCAA), mashirika mbalimbali yanayotoa huduma kwenye viwanja vya ndege, Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), Polisi na wananchi kwa ujumla; na washiriki wa Nje walikuwa 221 wanaotoka kutoka nchi za Uganda, Botswana, Namibia, Swaziland, Zambia, Burundi, Rwanda, Somalia, Nigeria, Liberia, Sierra Leone na Guinea Conakry.

**Chuo cha Bandari**

291. ***Mheshimiwa Spika,*** Chuo cha Bandari kimeendelea kutoa mafunzo ya Ujuzi na Utaalamu ngazi ya Cheti cha Msingi, Cheti cha Ufundi na Stashahada katika masuala ya usafiri kwa njia ya maji kwa kuzingatia viwango vilivyowekwa na Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC) na Shirika la Bahari Duniani (IMO). Aidha, Chuo hiki kinaendesha mafunzo yake kwa kuzingatia Viwango vya ubora vya Kimataifa yaani ISO 9001:2015 na kinatambuliwa na Baraza la Usimamizi wa Elimu ya Ufundi Tanzania (NACTE).

292. ***Mheshimiwa Spika,*** Mafunzo yanayotolewa katika Chuo cha Bandari ni pamoja na Usimamizi wa Wakala wa Forodha na Usafirishaji wa Mizigo; Mipango ya Usafiri wa Majini; Usimamizi wa

Mipango ya Uchukuzi na Usafirishaji; Usimamizi wa Shughuli za Meli na Bandari; Usimamizi wa Vifaa vya Bandari na Matengenezo; na Uhandisi na Usimamizi wa Matengenezo. Katika mwaka 2022/23, Chuo hiki kilidahili jumla ya wanafunzi 937 wa mafunzo ya muda mrefu ikilinganishwa na wanafunzi 898 waliodahiliwa katika mwaka 2021/22 sawa na ongezeko la asilimia 4. Vilevile, kwa upande wa mafunzo ya muda mfupi Chuo kilidahili wanafunzi 824 kati ya hao, wanafunzi 606 wamejisomesha (private), wanafunzi 41 ni kutoka Taasisi mbalimbali na 177 ni wanafunzi kutoka Mamlaka ya Bandari (waajiriwa wa TPA).

**Chuo cha Taifa cha Hali ya Hewa**

293. ***Mheshimiwa Spika,*** Chuo cha Taifa cha Hali ya Hewa kilichopo Kigoma kimeendelea kutoa mafunzo ya hali ya hewa katika ngazi ya awali na ya kati. Serikali kupitia Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) imeendelea kukiboresha Chuo hicho ili kuimarisha utoaji wa mafunzo na wigo wa udahili ikiwemo nchi jirani. Katika mwaka 2022/23, jumla ya wanafunzi 42 walidahiliwa katika ngazi za mafunzo ya awali na Diploma.

**B.4 MASUALA MTAMBUKA**

**Rasilimaliwatu na Maendeleo ya Watumishi**

294. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuhakikisha kuwa inakuwa na watumishi wenye uwezo wa kutekeleza majukumu yao kwa weledi kwa kuwapatia mafunzo. Kwa upande wa Sekta ya Uchukuzi, katika mwaka wa fedha 2022/23 watumishi 138 wa Idara na Vitengo vya Wizara walipatiwa mafunzo ya muda mfupi ndani ya nchi. Aidha, watumishi watatu (3) walipatiwa mafunzo ya muda mrefu ndani ya nchi na watumishi saba (7) walipatiwa mafunzo ya muda mrefu nje ya nchi. Vilevile, watumishi 60 wa Sekta ya Ujenzi walihudhuria mafunzo. Kati ya hao, watumishi 14 wamehudhuria mafunzo ya muda mrefu na watumishi 46 wamehudhuria mafunzo ya muda mfupi.

295. ***Mheshimiwa Spika,*** Aidha, Sekta ya Uchukuzi imeandaa Mpango wa Mafunzo wa Rasilimaliwatu (Human Resources Plan)

na Urithishanaji Madaraka (Succession Plan) wa miaka mitatu (3). Lengo la mpango huu ni kukabiliana na changamoto za uhaba wa watumishi wenye weledi kulingana na mahitaji ya Sekta ya Uchukuzi.

**Ushirikishwaji wa Wanawake Katika Kazi za Barabara**

296. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mujibu wa takwimu za Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022, idadi ya wanawake nchini ni asilimia 51 ya wananchi wote. Hata hivyo, idadi hiyo kubwa ya wanawake ikilinganishwa na ile ya wanaume haiakisi kiwango cha ushiriki wa kundi hili katika kazi za kihandisi na kazi za barabara kwa ujumla. Wizara yangu imejiwekea mikakati mahsusi ya kuongeza ushiriki wa wanawake katika kazi za barabara. Mikakati hiyo inahusisha kuwajengea uwezo wanawake wanaoshiriki kazi za barabara kupitia mafunzo na kuwasaidia kusajili kampuni zao za ujenzi pamoja na ufuatiliaji wa kazi za barabara wanazofanya. Mkakati mwingine ni ufuatiliaji wa wanawake katika taasisi za elimu ya juu wanaosoma masomo ya uhandisi, sayansi na hisabati na uhamasishaji wa wasichana kupenda masomo ya sayansi na hisabati.

297. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili, 2023, Wizara imefanya ufuatiliaji na tathmini ya ushirikishwaji wa wanawake katika kazi za barabara katika mikoa ya Manyara, Arusha, Kilimanjaro na Tanga. Lengo lilikuwa ni kubaini changamoto wanazokabiliana nazo wakati wa utendaji kazi wao. Pamoja na masuala mengine, tathmini hii itasaidia katika kuandaa na kuboresha mafunzo ya kuwajengea uwezo wanawake katika kazi za barabara. Maandalizi ya awali ya mafunzo katika Kanda ya Kaskazini kwa kuzingatia matokeo yaliyotokana na tathmini hiyo yanaendelea.

Vilevile, Wizara imefanya uchambuzi wa miradi ya ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami yenye urefu wa jumla ya kilometa 20 kwa ajili ya kutekelezwa na kampuni nne (4) za Makandarasi wanawake ili kuwajengea uwezo.

**Ushirikishwaji wa Sekta Binafsi**

298. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kushirikiana kwa karibu na Sekta Binafsi ili kubaini changamoto zilizopo na namna ya kuzitatua. Katika kutekeleza azma hiyo, Wizara ilikutana na wadau wa Sekta Binafsi katika Sekta ya Uchukuzi tarehe 11 Aprili, 2023 ambapo takriban wadau 300 walishiriki. Maoni yote yaliyotolewa yanaendelea kufanyiwa kazi na Wizara kwa lengo la kuboresha mazingira ya kufanya biashara kwa maslahi mapana ya Taifa letu.

**B.5 MASUALA MENGINE YALIYOTEKELEZWA NA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2022/23**

**Maboresho ya Sheria za Kisekta**

299. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imekamilisha marekebisho ya Kanuni za Usajili wa Makandarasi (The Contractors Registration Criteria) zilizotungwa chini ya Sheria ya Usajili wa Makandarasi Sura ya 235. Kanuni hizo zimetangazwa katika Gazeti la Serikali Na. 744/ 2022 la tarehe 16/12/2022. Aidha, marekebisho ya Sheria ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi Sura ya 269 yamewasilishwa Bungeni na kusomwa kwa mara ya kwanza katika Mkutano wa 10 wa Bunge la 12. Wizara pia imekamilisha Tafsiri ya Sheria zinazosimamiwa na Sekta ya Ujenzi kwa lugha ya Kiswahili na kuwasilisha Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa hatua zaidi. Vilevile, taratibu za marekebisho ya Sheria ya Baraza la Taifa la Ujenzi Sura ya 162 zinaendelea.

300. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuendelea *kushirikisha* Sekta Binafsi katika uendeshaji na utoaji huduma za usafiri na usafirishaji nchini, Wizara kwa kushirikiana na wadau ilikamilisha mapitio ya sheria mbalimbali ikiwemo Sheria ya Reli Sura ya 170 ambayo ilifanyiwa marekebisho (miscellenious amendment) ili kuruhusu watoa huduma binafsi kutumia miundombinu ya reli inayomilikiwa na TRC katika kutoa huduma za usafiri kwa njia ya reli. Mapendekezo ya marekebisho ya sheria hiyo yaliwasilishwa Bungeni katika Mkutano wa 10 na kusomwa kwa mara ya kwanza kupitia Muswada wa marekebisho ya sheria mbalimbali (miscellenious amendment). Ni matumaini ya Wizara kuwa marekebisho hayo

yatasaidia katika kushirikisha Sekta Binafsi na kuchochea matumizi ya miundombinu ya reli kwa tija zaidi.

301. ***Mheshimiwa Spika,*** sheria nyingine iliyofanyiwa maboresho ni Sheria ya Uwakala wa Meli Tanzania Sura ya 415 (Tanzania Shipping Agencies Corporation Act, Cap 415). Sheria hii ilifanyiwa marekebisho kwa kupunguza mawanda ya shughuli za TASAC ambazo kwa sasa zinatekelezwa na sekta binafsi. Baada ya marekebisho ya Kifungu cha 7 cha Sheria ya TASAC kupitia Sheria ya Fedha Na. 5 ya mwaka 2022, Shirika katika eneo la biashara ya meli limebakia na jukumu la uwakala wa forodha pekee katika bidhaa mahsusi zenye maslahi mapana ya Taifa.

302. ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na marekebisho hayo ya sheria ya TASAC, Shirika limebakia na majukumu ya kutoa huduma ya ugomboaji na uondoshaji wa shehena zifuatazo: silaha na vilipuzi; makinikia; wanyama hai kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Wanyamapori; nyara za Serikali; na kemikali zinazotumiwa na kampuni za madini.

303. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Zambia zimeendelea kushirikiana katika kufanya marekebisho ya Sheria ya TAZARA ya mwaka 1995 ili kuiwezesha TAZARA kujiendesha kwa tija zaidi. Katika kikao cha Baraza la Mawaziri la TAZARA kilichofanyika Lusaka, Zambia tarehe 14 Machi, 2023, Serikali ya Zambia iliomba ipewe muda zaidi ili kuhakikisha kuwa mabadiliko yanayopendekezwa yanaendana na sera na mwelekeo wa Serikali mpya iliyopo madarakani hivi sasa. Aidha, tulikubaliana Serikali ya Zambia itupe mrejesho kabla au ifikapo tarehe 30 Juni, 2023.

**Mifumo ya TEHAMA**

304. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuboresha matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) ili kuongeza ufanisi na kutoa huduma kwa wakati. Wizara iko katika hatua za mwisho za ujenzi wa Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini ambao utawezesha Wizara pamoja na Taasisi zake kufanya ufuatiliaji na tathmini za miradi yote chini ya Wizara (Ujenzi). Aidha, Wizara

inasimamia Mfumo wa Usimamizi wa Mizani kwa kutumia kamera za CCTV (Weighbridge Management System) kwenye vituo 13 vya mizani ambao unatoa taarifa za uzito wa magari pamoja na shughuli zinazoendelea katika vituo vya mizani. Mfumo wa utoaji wa vibali vya kusafirisha Mizigo maalumu (Special Loads Permit System) kwa njia ya kielektroniki unaendelea kutoa huduma kwa wasafirishaji nchini na nje ya nchi. Vilevile, Tovuti ya Wizara imeboreshwa ili kuhakikisha kuwa wananchi wengi wanapata taarifa mbalimbali zinazohusiana na Sekta ya Ujenzi kwa wakati.

## B.6 MAFANIKIO YA MIAKA MIWILI (2) YA SERIKALI YA AWAMU YA SITA KATIKA SEKTA ZA UJENZI NA UCHUKUZI

305. ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na maelezo niliyoyatoa kuhusu utendaji wa Wizara kwa mwaka 2022/23, naomba kwa muhtasari niainishe baadhi ya mafanikio yaliyopatikana katika Sekta za Ujenzi na Uchukuzi katika kipindi cha miaka miwili (2) ya Serikali ya Awamu ya Sita.

306. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi mahiri wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeweza kupiga hatua kubwa ya mafanikio katika maeneo mbalimbali. Katika kipindi hicho, Wizara imeendelea kutekeleza shughuli na miradi ya reli; barabara; viwanja vya ndege; vivuko; usimamizi wa utengenezaji wa Ndege; ujenzi na uboreshaji wa bandari; ujenzi na ukarabati wa meli katika maziwa; na uboreshaji wa vyuo. Hatua hizo zimechochea sekta nyingine za kiuchumi na kijamii katika kuwaletea wananchi maendeleo.

307. ***Mheshimiwa Spika,*** mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na ujenzi wa barabara na madaraja makubwa ambapo barabara zenye jumla ya **kilometa 15,563** ziko katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Kati ya hizo, barabara zenye jumla ya urefu **kilometa 1,152** zimekamilika kujengwa kwa kiwango cha lami, barabara zenye jumla ya urefu wa **kilometa 1,484** zinaendelea kujengwa kwa kiwango cha lami na barabara zenye urefu wa jumla ya **kilometa 4,141** zimefanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami. Baadhi ya barabara zilizojengwa na kukamilika katika kipindi hicho ni:

i Barabara ya Loliondo – Mto wa Mbu (km 201); Sehemu ya Waso – Sale Jct (km 50) mkoani Arusha;

ii Barabara ya Morocco – Mwenge (km 4.3) kutoka Njia tano hadi Sita (km 3.2) Mkoani Dar es Salaam;

iii Barabara ya Kongwa Jct – Mpwapwa – Gulwe – Kibakwe (km 98); Sehemu ya Mbande – Kongwa Jct (km 5.80) Mkoani Dodoma;

iv Barabara ya Tabora – Koga – Mpanda; Sehemu ya 3: Kasinde – Mpanda (km 108) pamoja na kipande cha Barabara ya Urwira (km 3.7) Mkoani Katavi;

v Barabara ya Kidahwe – Kasulu – Kibondo – Nyakanazi (km 268); Sehemu za Kidahwe –Kasulu (km 63) na Kakonko – Nyakanazi (km 50) Mkoani Kigoma; vi. Barabara ya Bulamba – Kisorya (km 51) Mkoani Mara;

vi Barabara ya Makutano – Nyamuswa – Ikoma Gate (km 153); Sehemu ya Makutano – Sanzate (km 50) Mkoani Mara;

vii Barabara ya Musoma – Makojo – Busekela; Sehemu ya Kuseni – Suguta (km 5) Mkoani Mara;

viii Barabara ya Chunya – Makongorosi (km 39) Mkoani Mbeya;

ix Barabara ya Mtwara – Newala – Masasi (km 210); Sehemu ya Mtwara – Mnivata (km 50) Mkoani Mtwara;

x Barabara ya Njombe – Ndulamo – Makete (km 107.4) Mkoani Njombe;

xi Barabara ya Itoni – Ludewa – Manda; Sehemu ya Lusitu – Mawengi (km 50) Mkoani Njombe;

xii Barabara ya Sumbawanga – Matai – Kasanga Port (km 112) Mkoani Rukwa

xiii Barabara ya Masasi – Songea Mbamba Bay; Sehemu ya Mbinga – Mbamba Bay (km 66) Mkoani Ruvuma;

xiv Barabara ya Mpemba – Isongole (km 50.3) Mkoani Songwe;

xv Barabara ya Urambo – Kaliua – Ilunde – Uvinza; Sehemu ya Urambo – Kaliua (km 280) Mkoani Tabora;

xvi Barabara ya Manyoni – Itigi – Tabora; Sehemu ya Nyahua – Chaya (km 85) Mkoani Tabora; na

xvii Barabara ya Tabora – Koga – Mpanda; Sehemu Usesula – Komanga (km 108) pamoja na Sikonge *Spur Road* (km 7.5) na Sehemu ya Komanga - Kasinde (km 108) pamoja na Inyonga Spur (km 4.8) mkoani Tabora.

308. ***Mheshimiwa Spika,*** miradi mikubwa ya barabara inayoendelea kutekelezwa ni pamoja na:

i. Barabara ya Mianzini – Olemringaringa – Ngaramtoni Juu na Olemringaringa – Sambasha/ Timbolo (km 18) – Kazi za ujenzi zinaendelea na zimefikia asilimia 18 Mkoani Arusha;

ii. Upanuzi wa Barabara ya Kimara – Kibaha kuwa Njia Nane (8 lanes), (km 19.2) na Madaraja matatu ya Kibamba, Kiluvya na Mpiji Mkoani Dar es Salaam;

iii. Ujenzi wa Miundombinu ya Mabasi yaendayo haraka; Awamu ya Pili (BRT Phase II) (km 19.3) na Awamu ya Tatu (Phase III): Nyerere Road corridor from CBD to Gongolamboto (km 23.33) Mkoani Dar es Salaam;

iv. Barabara za Mzunguko wa Nje Jijini Dodoma (Dodoma City Outer Ring Roads); Sehemu ya Nala – Veyula – Mtumba – Ihumwa Dry Port (km 52.30) (Lot 1) na Sehemu ya Ihumwa – Dry Port – Matumbulu – Nala (km 60.00) (Lot 2) Mkoani Dodoma;

v. Barabara ya Kumunazi – Bugene – Kasulo na Kyaka – Mutukula (km 124); Sehemu ya Bugene – Burigi Chato National Park (km 60); Mkoani Kagera;

vi. Barabara ya Kabingo – Kasulu – Manyovu (km 260.0); sehemu za Kanyani Junction – Mvugwe (km 70.5); Mvugwe – Nduta Junction (km 59.35); Kibondo Junction – Kabingo (km 62.5); Nduta Junction – Kibondo (km 25.9) na Kasulu – Manyovu pamoja na barabara za kuingia Kasulu mjini (km 68) mkoani Kigoma;

vii. Barabara ya Kazilambwa – Chagu (km 36) mkoani Kigoma;

viii. Barabara ya Malagarasi – Ilunde – Uvinza (km 51.1); Mkoani Kigoma;

ix. Barabara ya Dumila – Kilosa; Sehemu ya Ludewa – Kilosa (km 18) mkoani Morogoro;

x. Barabara ya Mikumi – Kidatu – Ifakara; Sehemu ya Kidatu – Ifakara (km 66.9): Mkoani Morogoro;

xi. Barabara ya Karatu – Mbulu – Hydom – Sibiti River – Lalago – Maswa (km 389); Sehemu ya Mbulu – Garbabi (Lot 1) (km 25) Mkoani Manyara;

xii. Barabara ya Tarime – Mugumu (km 87.14); Sehemu ya Tarime – Nyamwaga (Lot 1: Mogabiri - Nyamongo) (km 25) Mkoani Mara;

xiii. Barabara ya Nyamuswa – Bunda – Bulamba (km 56.4) Mkoani Mara;

xiv. Barabara ya Itoni – Ludewa – Manda Mkoani Njombe;

xv. Barabara ya Tanga – Pangani – Mkange; Sehemu ya Tanga – Pangani (km 50) na Sehemu ya Tungamaa – Mkange (km 95.2) Mkoani Tanga; na

xvi. Barabara ya Handeni – Kibirashi – Kwamtoro – Singida (km 434.33) Sehemu ya Handeni – Mafuleta (Lot 1) (km 20): Ujenzi unaendelea na umefikia asilimia 11; Sehemu ya Mafuleta – Kileguru (km 30): Taratibu za manunuzi kwa ajili ya ujenzi zinaendelea.

309. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa ujenzi wa madaraja jumla ya madaraja makubwa nane (8) yamejengwa na kukamilika ambayo ni Daraja la Wami (Pwani), Daraja la Tanzanite (DSM), Daraja la Gerezani (DSM), Daraja la Mpwapwa (Dodoma), Daraja la Kiegeya (Morogoro), Daraja la Ruhuhu (Ruvuma), Daraja la Kitengule (Kagera) na Daraja la Msingi (Singida).

310. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu ujenzi na ukarabati wa viwanja vya ndege, Wizara imekamilisha miradi ya ujenzi wa viwanja vya ndege vya Geita, Songea na Mtwara. Aidha, Wizara inaendelea na wa ujenzi wa Kiwanja kipya cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato kwa ufadhili wa Serikali (GOT) na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB). Utekelezaji wa awamu ya kwanza (Package 01) ya kiwanja hiki unaohusisha kazi za ujenzi wa barabara ya kuruka na kutua ndege, maegesho ya ndege, barabara ya kuingia na kutoka kiwanjani, barabara za viungio na usimikaji wa taa za kuongezea ndege na taa za usalama umefikia asilimia 18. Utekelezaji wa awamu ya pili (Package 02) unaohusisha kazi za ujenzi wa Jengo la abiria na majengo mengine umefikia asilimia 02.

311. ***Mheshimiwa Spika,*** miradi mingine inayoendelea ni pamoja na viwanja vya ndege vya Songwe (kazi inayoendelea ni ujenzi wa jengo la abiria na imefikia asilimia 98), Musoma (kazi zinazofanyika ni ukarabati na upanuzi wa *runway, taxiway, apron, power house* na *fire station* na zimefikia asilimia 47), Iringa Awamu ya I (kazi zinazotekelezwa zimefikia asilimia 50 ambazo ni ukarabati na upanuzi wa *runway, taxiway, apron, power house, control tower, fire station* na uzio wa usalama) na Moshi (kazi zinazotekelezwa zimefikia asilimia 20 na zinahusisha ukarabati wa *runway, taxiway* na *apron*). Vilevile, utekelezaji wa ujenzi na ukarabati wa viwanja vya ndege vya Sumbawanga, Shinyanga, Tabora na Kigoma kwa Ufadhili wa Serikali (GoT) na Benki ya Uwekezaji ya Ulaya (EIB) umeanza na Makandarasi wako kwenye hatua za Maandalizi (Mobilization). Serikali imekamilisha ulipaji wa fidia kwa wananchi wote watakaopisha ujenzi wa viwanja vya ndege vya Iringa (Awamu ya II), Tanga na Lake Manyara vitakavyofadhiliwa na Benki ya Dunia (WB). Kuhusu kiwanja cha ndege cha Iringa, kazi zitakazotekelezwa katika Awamu ya II ni

ujenzi wa jengo la abiria na miundombinu yake. Kwa sasa, Mfadhili ametoa Kibali (No Objection) na taratibu za manunuzi kwa ajili ya kuwapata Washauri Elekezi zimeanza. Kwa upande wa Makandarasi, Serikali inasubiri Kibali (No Objection) kutoka kwa Mfadhili ili kuanza taratibu za manunuzi.

312. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali ya Awamu ya Sita imeendelea kutekeleza kwa mafanikio miradi mbalimbali ya vivuko kwa lengo la kutoa huduma ya usafiri na usafirishaji kwa wananchi wanaoishi katika maeneo yanayohitaji usafiri kwa njia ya maji. Katika kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020, Serikali imeanza ujenzi wa vivuko vipya ambavyo vitatoa huduma katika maeneo ya Kisorya-Rugezi, Ijinga-Kahangala, Bwiro-Bukondo, Nyakarilo-Kome na Mafia-Nyamisati na Buyagu-Mbarika. Aidha, taratibu za ununuzi wa 'Sea Taxi' mbili zitakazotoa huduma eneo la Magogoni na Kigamboni zinaendelea. Vilevile, ukarabati wa vivuko sita (6): MV. KAZI, MV. MUSOMA, MV. KILAMBO, MV. SABASABA, MV. TEMESA NA MV. TANGA umekamilika na ukarabati wa vivuko vingine kumi (10) unaendelea.

313. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu miradi ya majengo inayotekelezwa na Wizara kupitia Wakala wa Majengo Tanzania (TBA), miradi mbalimbali ya majengo kwa ajili ya sekta mbalimbali kama vile Afya, Ofisi, Makazi ya Viongozi na Watumishi wa Umma imetekelezwa kwa gharama nafuu na katika ubora unaotakiwa. Katika kipindi hicho, miradi iliyotekelezwa kwa mafanikio makubwa ni pamoja na mradi wa ujenzi wa nyumba 20 za viongozi jijini Dodoma ili kukabiliana na uhaba wa nyumba za makazi ya viongozi uliojitokeza mara baada ya Serikali kuhamishia makao yake makuu jijini Dodoma. Vilevile, Serikali kupitia TBA imekamilisha ujenzi wa nyumba nne (4) za Majaji katika Mikoa ya Tabora, Kilimanjaro, Mtwara na Shinyanga na inaendelea na umaliziaji wa nyumba ya Jaji katika Mkoa wa Kagera. Miradi mingine ni ujenzi wa nyumba za watumishi wa Umma katika eneo la Magomeni Kota Awamu ya kwanza na ya pili katika eneo la Temeke Kota pamoja na ukarabati wa nyumba za Serikali zinazosimamiwa na TBA kwa lengo la kuboresha makazi na kuchochea uwajibikaji kwa watumishi na viongozi.

314. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu reli, wakati Serikali ya Awamu ya Sita (6) inaingia madarakani ujenzi wa SGR ulikuwa umeanza kwa vipande viwili (2) vya kutoka Dar es Salaam – Morogoro na Morogoro – Makutupora vyenye jumla ya kilometa 722. Katika kipindi cha miaka miwili (2) ya Serikali ya Awamu ya Sita (6), kazi za vipande vya reli vya Mwanza - Isaka (km 341), Makutupora - Tabora (km 371), Tabora - Isaka (km 165), Tabora – Kigoma (km 506) na Uvinza – Musongati (km 283) vyenye jumla ya kilometa 1,666 zilianza na kwa sasa viko kwenye hatua mbalimbali za utekelezaji kama ifuatavyo:

i. Ujenzi wa reli ya SGR kipande cha Dar es Salaam – Morogoro (km 300) umekamilika kwa asilimia 98.14;

ii. Ujenzi wa reli ya SGR kipande cha Morogoro – Makutupora (km 422) umekamilika kwa asilimia 93.83;

iii. Ujenzi wa reli ya SGR kipande cha Mwanza - Isaka (km 341) umekamilika kwa asilimia 31.07;

iv. Ujenzi wa reli ya SGR kipande cha Makutupora - Tabora (km 371) imekamilika kwa asilimia 7; na

v. Ujenzi wa reli ya SGR kipande cha Tabora - Isaka (km 165). Ujenzi wa kipande hiki umezinduliwa rasmi tarehe 18 Januari, 2023 na umefikia asilimia 2.39.

315. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali pia imeanza ujenzi wa Awamu ya Pili ya reli ya SGR ambapo mkataba wa kipande cha Tabora – Kigoma (km 506) ulisainiwa tarehe 20 Desemba, 2022 na mkandarasi anaendelea na maandalizi ya vifaa, makambi ya wafanyakazi na kuajiri wafanyakazi. Aidha, taratibu za ununuzi kwa ajili ya kumpata mkandarasi wa ujenzi wa reli ya Uvinza – Musongati (km 283) zinaendelea ambapo Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) imeshatoa kibali na mkandarasi anatarajiwa awe amepatikana ifikapo Juni, 2023. Reli hii itasaidia kuunganisha nchi za Tanzania, Burundi na DRC.

316. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali pia imeendelea na juhudi za upatikanaji wa vifaa vya uendeshaji wa SGR kama ifuatavyo:

i. Kupokelewa kwa mabehewa mapya 14 ya abiria kati ya mabehewa 59 ya abiria yaliyonunuliwa. Mabehewa 45 yaliyosalia ambayo utengenezaji wake umefikia asilimia 95 yanatarajiwa kuwasili mwezi Julai, 2023;

ii. Utengenezaji wa vichwa vya treni 17 vya umeme umefikia asilimia 42.1 na seti za treni 10 za kisasa (Electric Multiple Unit - EMU) kwa ajili ya treni ya abiria umefikia asilimia 38.2. Aidha, vichwa vya treni viwili (2) vya umeme na seti ya treni moja (1) zinatarajiwa kuwasili mwezi Juni, 2023;

iii. Ujenzi wa mabehewa mapya 1,430 ya mizigo umefikia asilimia 42; na

iv. Serikali inatarajia kupokea mabehewa ya abiria sita (6) yanayotarajiwa kuwasili mwezi wa Juni, 2023 kutoka nchini Ujerumani.

317. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuhakikisha huduma za reli iliyopo zinaboreshwa, Serikali pia imeweza kugharamia:

i. Ununuzi wa mabehewa mapya 22 ya abiria kwa ajili ya reli ya MGR yaliyowasili nchini tarehe 19 Novemba, 2022 na kuanza kutumika; na

ii. Ununuzi wa vipuri vya ukarabati wa mabehewa 600 ya mizigo na mabehewa 37 ya abiria kwa ajili ya reli ya iliyopo (MGR). Aidha, ukarabati wa mabehewa 52 ya mizigo kati ya 600 na mabehewa sita (6) ya abiria kati ya 37 umekamilika na kuanza kutoa huduma.

318. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali ya Awamu ya Sita kwa muda wa miaka miwili (2) imeshapokea ndege mpya tatu (3). Aidha, ndege moja ya mizigo inatarajiwa kupokelewa mwishoni mwa mwezi Mei, 2023. Aidha, yamefanyika malipo ya ndege nyingine tatu (3) mpya ambazo zitawasili katika kipindi cha mwaka 2023/24.

319. ***Mheshimiwa Spika,*** miradi ya ujenzi na ukarabati wa meli umekuwa na mafanikio kama ifuatavyo:

i. Meli ya MV. Mwanza *Hapa Kazi Tu* ilifanikiwa kutolewa kwenye chelezo na kushushwa majini kwa ajili ya hatua inayofuata ya ukamilishaji (finishing) ambapo ujenzi umekamilika kwa asilimia 83;

ii. Ukarabati wa meli ya MV. Umoja umefikia asilimia 75.8;

iii. Ukarabati wa meli ya MT. Sangara umefikia asilimia 90.7; na

iv. Wajenzi wa meli mpya tatu (3) pamoja na *shipyard* moja wamepatikana na taratibu za kusaini mikataba zinakamilishwa. Meli mbili (2) na *shipyard* zitajengwa katika Ziwa Tanganyika na meli moja (1) itajengwa katika Ziwa Victoria.

320. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kufanya maboresho ya Bandari za Dar es Salaam, Tanga na Mtwara. Maboresho hayo yamewezesha ongezeko la mizigo inayohudumiwa kutoka tani milioni 1.5 kwa mwezi mwaka 2022 hadi tani milioni 1.93 kwa mwezi mwaka 2023. Aidha, huduma za bandari zimeweza kuchangia asilimia 43 ya mapato ya kodi ya forodha yaliyokusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) mwaka 2021/22 ikilinganishwa na asilimia 37 katika mwaka 2020/21. Lengo ni kuchangia hadi asilimia 50 ya makusanyo ya TRA. Pia, uwezo wa kuhudumia shehena ya magari umeongezeka ambapo TPA inapokea meli mbili (2) za magari kwa juma.

321. ***Mheshimiwa Spika,*** mafanikio mengine chini ya TPA ni pamoja na:

i. Kuanza maandalizi ya ujenzi wa Bandari ya Bagamoyo ambapo mapitio ya upembuzi yapo katika hatua za mwisho na yatakamilika Juni 2023;

ii. Bandari ya Mtwara kwa sasa ni bandari pekee inayohudumia mzigo wa makaa ya mawe hadi tani 60,000 kwa mwezi kwa ajili ya Soko la Ulaya. Bandari hii imehudumia zaidi ya tani 600,000 za shehena ya makaa ya mawe katika kipindi cha mwaka 2021/22;

iii. Kazi za kuongeza kina cha bandari ya Tanga kutoka mita tatu (3) hadi mita 13, kuimarisha na kuboresha Gati Na. 1 - 2 zenye urefu wa mita 450. Kazi imekamilika kwa mita 300 na kuanza kutumika mwishoni mwa Machi, 2023 ambapo meli yenye urefu wa mita 150 iliyobeba tani 51,000 ilipokelewa; na

iv. Kukamilika kwa ujenzi wa Bandari ya Karema katika Ziwa Tanganyika na kuanza kutumika.

322. ***Mheshimiwa Spika,*** mafanikio mengine kwenye utoaji wa huduma za hali ya hewa, mafunzo na udhibiti wa usalama barabarani ni pamoja na:

i. Ununuzi wa rada mbili (2) za hali ya hewa zitakazofungwa katika mikoa ya Mbeya na Kigoma. Hii inafanya idadi ya rada za hali ya hewa zilizowasili nchini kufikia tano (5);

ii. Ununuzi wa ndege mbili (2) aina ya Cessna Skyhawk - 172) zenye injini moja (1) kwa ajili ya mafunzo ya urubani katika Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT). Ndege hizo ziliwasili nchini tarehe 08 Januari, 2023; na

iii. Kuanza kutumika kwa tiketi mtandao katika usafiri wa mabasi ya abiria ya masafa marefu hivyo kupunguza usumbufu kwa abiria.

## B.7 CHANGAMOTO ZILIZOIKABILI WIZARA NA MIKAKATI YA KUZITATUA

323. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi imekabiliwa na changamoto mbalimbali katika utekelezaji wa majukumu yake. Baadhi ya changamoto hizo na mikakati ya kuzitatua ni: -

### i. Mahitaji Makubwa ya Fedha za Utekelezaji wa Miradi

Mahitaji makubwa ya fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Miundombinu na utoaji wa huduma za uchukuzi na hali ya hewa yanasababisha baadhi ya miradi ya maendeleo kutotekelezwa kwa wakati. Aidha, mahitaji halisi ya utekelezaji wa miradi ya barabara, madaraja na viwanja vya ndege yamekuwa

makubwa ikilinganishwa na upatikanaji wa rasilimali fedha, na hivyo kusababisha malimbikizo ya madeni ya Makandarasi na Wahandisi Washauri.

**Mikakati:**

a. Kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango kuendelea kutafuta fedha kutoka katika vyanzo mbalimbali ikiwemo kuendelea kutangaza miradi ya maendeleo kutekelezwa kwa njia ya ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi;

b. Serikali inaendelea kutafuta vyanzo mbalimbali vya fedha kutoka Washirika wa Maendeleo, uhamasishaji wa matumizi ya utaratibu wa PPP, EPC+F na uboreshaji wa makusanyo katika hifadhi za barabara kwa ajili ya matengenezo ya barabara;

c. Serikali imeendelea na jitihada za kulipa madeni ya Makandarasi na Wahandisi Washauri wa miradi mbalimbali. Hadi Aprili, 2023, jumla ya **Shilingi 184,459,708,389.61** zimetolewa kwa ajili ya malipo ya madeni yaliyohakikiwa. Aidha, Serikali inaendelea kutoa fedha kwa ajili ya malipo ya madeni ya miradi ya barabara inayoendelea; na

d. Kuendelea kutumia Teknolojia mpya ya ujenzi na matengenezo ya barabara ambayo itasaidia barabara zitakazotengenezwa kudumu kwa muda mrefu bila kuhitaji matengenezo ya mara kwa mara hasa kwa barabara za changarawe au udongo ambazo huathiriwa sana na mvua.

ii. **Uchafuzi wa mazingira**

Uchafuzi wa mazingira kwenye njia na maeneo ya vivuko, hasa katika kituo cha Magogoni - Kigamboni (Dar es Salaam) na Kigongo - Busisi (Mwanza) unasababisha uharibifu wa mara kwa mara wa vivuko kutokana na mifuko na chupa za plastiki pamoja na nyavu za samaki zinazotupwa majini kunasa kwenye mifumo ya uendeshaji wa vivuko. Hali hii husababisha gharama kubwa za matengenezo ya vivuko na uendeshaji wa vivuko kwa ujumla. Aidha, takataka zinazotupwa katika madaraja na mitaro ya maji barabarani zinasababisha uharibifu wa miundombinu hiyo.

Vilevile mabadiliko ya matumizi ya ardhi kwenye njia za maji yanasababisha mikondo ya maji kuhama na hivyo kuharibu barabara na madaraja.

**Mkakati**

Wizara (Ujenzi) inaendelea kutoa elimu kwa wavuvi kutofanya shughuli za uvuvi kwenye njia za vivuko. Aidha, watumiaji wa vivuko wanahamasishwa kutotupa taka kwenye maji wakati wa safari. Vilevile, TANROADS kupitia vikao vya Kamati za Ushauri za Mikoa inasisitiza matumizi sahihi ya miundombinu na Wizara inaendelea kushirikiana na Taasisi mbalimbali zenye dhamana ya ardhi ili kuwa na matumizi sahihi ya ardhi.

iii. **Mabadiliko ya Hali ya Hewa**

Mabadiliko ya tabianchi yamekuwa yakiathiri shughuli za usafiri na usafirishaji ambayo husababisha mvua za mafuriko na kufanya uharibifu wa miundombinu, hususan ya reli.

**Mkakati:**

Kuendelea kufanya matengenezo ya mara kwa mara katika maeneo korofi ya reli pamoja na kuangalia uwezekano wa kufufua mabwawa ya Msagali, Kimaghai, Kidete na Hombolo kwa ajili ya kupunguza kasi ya maji yanayoathiri njia ya reli. Aidha, Kazi ya kuelekeza mkondo wa maji mbali na njia ya reli (River training) imekamilika na kazi ya ujenzi wa mabwawa katika eneo la Kilosa, Mpwapwa na Kinyasungwi imepangwa kuanza mwaka wa fedha 2023/24.

iv. **Uhaba wa Wataalam katika Sekta**

Wataalam katika Sekta ndogo za usafiri wa anga, reli, barabara, hali ya hewa na usafiri majini wanatakiwa kupata elimu maalum kwenye maeneo yao ili kukidhi viwango vya kimataifa. Sekta hizi zinakabiliwa na changamoto ya uhaba wa Wataalam wenye ujuzi na uzoefu.

**Mkakati:**

Wizara kupitia Vyuo vyake vya Kisekta kuendelea kutoa mafunzo kwa Wataalam waliopo, kuajiri wapya na kuvijengea uwezo Vyuo hivyo. Lengo ni kuviwezesha kuzalisha rasilimaliwatu wenye elimu inayokidhi mahitaji ya Sekta.

v. **Uvamizi, uharibifu na Wizi wa miundombinu ya Reli**

Kumekuwepo na tatizo la uvamizi, uharibifu na hujuma kwa miundombinu ya reli, hususan reli zenyewe, mataruma, vifungio na madaraja kwenye baadhi ya maeneo ambako reli inapita.

**Mkakati:**

Wizara imeendelea kushirikiana na vyombo vya dola pamoja na jamii inayozunguka maeneo ya reli ili kusimamia Sheria zilizopo kuhusu uharibifu huo pamoja na kutoa elimu na hamasa kwa jamii inayopakana na maeneo ya reli kwa lengo la kuwaelewesha umuhimu wa kutunza na kuwafanya wananchi hao kuwa walinzi wa miundombinu hiyo.

vi. **Ukosefu wa taa za kuongozea ndege katika baadhi ya Viwanja vya Ndege**

Baadhi ya Viwanja vya ndege nchini havina taa za kuongozea ndege zinazowezesha ndege kuruka na kutua nyakati za usiku. Kutokuwepo kwa taa hizo na miundombinu kwa ajili ya kuwezesha usafiri wa anga nyakati za usiku kunalazimisha makampuni ya ndege kupanga safari za ndege wakati wa mchana tu. Hii ni moja ya changamoto inayokabili usafiri wa anga nchini kwa sababu ndege hazitumiki kwa kiwango kinachotakiwa nyakati za usiku.

**Mkakati:**

Serikali imeendelea kuvifanyia maboresho Viwanja vya Ndege nchini kwa awamu kulingana na upatikanaji wa bajeti ili kuwezesha ndege kuruka nyakati za usiku na pia kuboresha barabara za kurukia ndege kuweza kuhimili aina ya ndege

zilizopo. Aidha, miradi yote mipya ya viwanja vya ndege itatakiwa kujumuisha ufungaji wa taa.

## C. MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2023/24

324. ***Mheshimiwa Spika,*** Makadirio ya Bajeti ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo kwa Sekta ya Ujenzi na Sekta ya Uchukuzi ni kama ifuatavyo:-

### C.1 SEKTA YA UJENZI

### Makadirio ya Bajeti ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo

325. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2023/24, Sekta ya Ujenzi imetengewa **Shilingi 48,395,392,000.00** ikiwa ni Bajeti ya Matumizi ya Kawaida**.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi 43,958,274,000.00** ni Bajeti ya Mishahara na **Shilingi 4,437,118,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo.

326. ***Mheshimiwa Spika,*** Bajeti ya Maendeleo kwa Sekta ya Ujenzi katika mwaka 2023/24 ni **Shilingi 1,419,843,057,000.00.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi 1,084,666,369,000.00** ni fedha za ndani na **Shilingi 335,176,688,000.00** ni fedha za nje. Kati ya fedha za ndani **Shilingi 599,756,467,800.00** ni fedha zilizotengwa kwa ajili ya bajeti ya Mfuko wa Barabara na fedha kutoka katika Mfuko Mkuu wa Serikali ni **Shilingi 484,909,901,200.00.**

Mgawanyo wa fedha za maendeleo pamoja na miradi iliyotengewa fedha ni kama inavyooneshwa katika ***Kiambatisho Na.1.*** Maelezo kuhusu Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha katika mwaka wa fedha 2023/24 ni kama ifuatavyo:

### MRADI WA KUJENGA UWEZO (INSTITUTIONAL CAPACITY BUILDING)

327. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 246.37** fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya mradi huu kwa lengo la kujenga uwezo wa watumishi wa Sekta ya Ujenzi kwa kuwapatia mafunzo na vitendea kazi vya ofisi kwa ajili ya kuboresha utendaji kazi.

**MIRADI YA VIVUKO, UJENZI WA NYUMBA NA MAJENGO YA SERIKALI**

**Ujenzi na Ukarabati wa Vivuko na Maegesho ya Vivuko**

328. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2023/24 mradi wa Ujenzi na Ukarabati wa Vivuko na Maegesho ya Vivuko umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 14,281.58** kwa ajili ya kazi zifuatazo:

329. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi wa **Ujenzi wa Maegesho ya Vivuko** umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 2,444.05** kwa ajili ya kufanya tathmini kwa ajili ya kulipa fidia kwa wakazi wa Kigamboni watakaoathiriwa na upanuzi wa maegesho Kigamboni; ujenzi na ukarabati wa maegesho 11 (Magogoni – Kigamboni, Kilambo – Namoto, Utete – Mkongo, Iramba Majita, Nyakarilo – Kome, Irunda - Luchelele, Kisorya Rugezi, Ilagala – Kajeje, Rusumo - Nyakiziba, Musoma – Kinesi na Kasharu – Buganguzi). Aidha, fedha hizi zitatumika kwa ajili ya ujenzi wa maegesho ya Zumacheli katika kituo cha Chato – Nkome na ujenzi wa maegesho mapya ya vivuko vya Kayenze – Kanyinya, Muleba – Ikuza, Ijinga – Kahangala na Bwiro – Bukondo.

Kazi nyingine ni ujenzi/ukarabati wa maegesho ya Buyagu, Mbalika, Ilunda, Luchelele, Bukimwi, Kisorya, Rugezi, Kahunda na Maisome; ujenzi wa ofisi, majengo ya abiria na uzio kwenye vituo sita (06) vya vivuko ambavyo ni; (Kahunda – Maisome, Msangamkuu – Msemo, Kisorya – Rugezi, Bezi – Bukimwi, Nyakarilo – Kome na Bugolora – Ukara); kusimika Mfumo wa kielektroniki wa usimamizi wa vivuko na Mifumo ya Tiketi katika vituo 21, kufanya matengenezo kinga ya maegesho ya vivuko vyote pamoja na ufuatiliaji na tathmini ya miradi hiyo.

330. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi wa **Ujenzi wa Vivuko Vipya** umetengewa **Shilingi milioni 5,748.02** kwa ajili ya ununuzi wa vivuko vipya vya Kisorya – Rugezi, Ijinga – Kahangala, Bwiro – Bukondo, Nyakarilo – Kome, Nyamisati – Mafia na Buyagu – Mbalika. Kazi nyingine ni ununuzi wa boti mbili ndogo (sea taxi ferries) zitakazotoa huduma katika kituo cha Magogoni -

Kigamboni, ununuzi wa vifaa vya karakana za TEMESA, huduma za ushauri pamoja na usimamizi na ufuatiliaji wa miradi hiyo.

331. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi wa ***Ukarabati wa Vivuko*** umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 6,089.51** kwa ajili ya kukamilisha ukarabati wa kivuko MV Ujenzi; ukarabati wa MV Mara, MV Kome II, MV Misungwi, MV Nyerere, MV Kyanyabasa, MV Tanga, MV Malagalasi, MV Mafanikio, MV Magogoni na MV Kitunda. Aidha, Kazi nyingine ni kuanza ukarabati wa vivuko MV Mwanza, MV Kigamboni, MV Ukara 1, MV Ukara II, MV Sabasaba na MV Pangani II.

Vilevile, kazi nyingine ni ukarabati wa boti ya uokozi ya MV SAR II, ukarabati wa kivuko MV Kilombero II na kukihamisha kwenda Mlimba – Malinyi pamoja na ufuatiliaji na tathmini ya miradi hiyo.

**Ujenzi na Ukarabati wa Nyumba na Majengo ya Serikali**

332. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2023/24 jumla ya **Shilingi milioni 38,823.63** zimetengwa kwa ajili ya mradi wa Ujenzi na Ukarabati wa Nyumba na Majengo ya Serikali. Kazi zitakazotekelezwa ni kama ifuatavyo:

333. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi wa **Ujenzi wa Nyumba za Viongozi wa Serikali** umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 181.42** kwa ajili ya Awamu ya II ya ujenzi wa nyumba 20 za Viongozi Dodoma. Aidha, Awamu ya II ya mradi wa **Ujenzi wa nyumba 150 za Watumishi wa Umma** umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 6,000.00** kwa ajili ya ujenzi wa nyumba hizo Jijini Dodoma.

334. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi wa **Ujenzi wa jengo la Ofisi ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (awamu ya II)** katika eneo la Mtumba jijini Dodoma umetengewa **Shilingi milioni 6,000.00.**

335. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 5,700.00** zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa **Ujenzi wa jengo la makazi kwa ajili ya Watumishi wa Umma katika eneo la Temeke Kota.** Aidha, mradi wa **Ujenzi wa jengo la makazi kwa ajili ya Watumishi wa Umma katika eneo la Magomeni Kota Wilaya ya Kinondoni** umetengewa **Shilingi milioni 3,145.86** na

**Shilingi milioni 1,300.00** zimetengwa kwa ajili ya mradi wa **ujenzi wa jengo la Makazi kwa ajili ya Watumishi wa Umma katika eneo la Ghana Kota (Block II) katika Mkoa wa Mwanza.**

336. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi wa **ujenzi wa jengo la Makazi kwa ajili ya watumishi wa Umma katika eneo la Kaloleni Kota (Block II) katika Mkoa wa Arusha** umetengewa **Shilingi milioni 1,300.00.** Aidha, kiasi cha **Shilingi milioni 3,000.00** kimetengwa kwa ajili ya **Ujenzi wa nyumba (Apartments) za Watumishi wa Umma, Dar es Salaam.**

337. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi wa **Ukarabati wa Nyumba na Ununuzi wa Samani kwa Ajili ya Ikulu Ndogo** umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 5,234.40.** Kazi zitakazofanyika ni ukarabati wa nyumba 40 za viongozi Dodoma na nyumba 30 mikoa mingine pamoja na matengenezo kinga katika nyumba za makazi ya Magomeni Kota. Kazi nyingine ni ununuzi wa samani za Ikulu Ndogo, ukarabati wa nyumba 66 zilizokuwa zinamilikiwa na iliyokuwa Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu Dodoma (CDA) zilizohamishiwa Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) na ukarabati wa nyumba zilizokuwa zinamilikiwa na TAMISEMI zilizohamishiwa TBA katika mikoa 20.

338. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi wa **Kujenga Uwezo wa Wabunifu Majengo, Wakadiriaji Majenzi na Huduma za Ushauri** umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 1,549.26** katika mwaka wa fedha 2023/24, kwa ajili ya kuwajengea uwezo Wabunifu Majengo (Architects) na Wakadiriaji Majenzi (Quantity Surveyors) kupitia Bodi ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi (AQRB). Kazi nyingine ni huduma za ushauri katika ujenzi wa jengo la Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (awamu II) katika eneo la Mtumba Jijini Dodoma, kuendeleza kazi ya utungaji wa Sheria ya Majengo, kanuni pamoja na miongozo ya viwango msawazo (standard specifications).

339. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi wa **Ujenzi na Ukarabati wa Karakana za TEMESA na TBA** umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 4,015.46.** Kazi zitakazohusika ni ukarabati wa karakana 13 za TEMESA katika Mikoa ya Tabora, Mwanza, Arusha, Mtwara, Mbeya, M.T Depot - Dar es Salaam, Kigoma, Mara, Ruvuma,

Pwani, Dodoma, Tanga na Kagera. Aidha, fedha hizi zitatumika kufanya ukarabati wa karakana ya TEMESA iliyopo Morogoro inayotumika kutengeneza mitambo ya barabara ambayo baadae itatumika kama karakana ya Mkoa wa Morogoro. Vilevile, zitatumika kuendelea na ujenzi wa karakana za TEMESA katika Mikoa ya Songwe, Simiyu, Geita, Njombe, Katavi na karakana mpya ya kisasa Jijini Dodoma pamoja na kugharamia ushauri na usimamizi wa miradi ya Karakana za TEMESA.

Kazi nyingine ni ukarabati wa karakana sita (6) za TBA katika mikoa ya Arusha, Mwanza, Morogoro, Tabora, Dar es Salaam na Mbeya.

340. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2023/24, mradi wa **Kusanifu na kusimika Mfumo wa Usimamizi na Ufuatiliaji wa Matengenezo ya Magari, Umeme na Elektroniki** umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 770.00**. Aidha, jumla ya **Shilingi milioni 627.23** zimetengwa kwa ajili ya Ufuatiliaji na tathmini kwenye miradi ya ujenzi na ukarabati wa Nyumba na Majengo ya Serikali pamoja na wahitimu wa Ubunifu Majengo na Ukadiriaji Majenzi.

**MIRADI YA BARABARA NA MADARAJA**

341. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2023/24 barabara saba (7) zenye jumla ya urefu wa kilometa 2,035 zitaanza kujengwa kwa kiwango cha lami kwa kutumia utaratibu wa EPC + F. Barabara hizo ni: -

i. Barabara ya Kidatu – Ifakara – Lupiro – Malinyi – Kilosa kwa Mpepo – Londo Lumecha/Songea (km 435);

ii. Barabara ya Karatu – Mbulu – Haydom – Sibiti River – Lalago – Maswa (Simiyu) (km 339);

iii. Barabara ya Handeni – Kibirashi – Kijungu – Kibaya – Njoro – Olboroti – Mrijochini – Dalai – Chambalo – Chemba – Kwa Mtoro – Singida (km 460);

iv. Barabara ya Arusha – Kibaya – Kongwa Junction (km 453.42);

v. Barabara ya Masasi – Nachingwea – Liwale (km 175);

vi. Barabara ya Igawa – Songwe – Tunduma (km 218) pamoja na barabara ya mchepuo ya Uyole – Songwe yenye urefu wa kilometa 48.9; na vii. Barabara ya Mafinga – Mtwango – Mgololo (km 81).

342. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, katika mwaka wa fedha 2023/2024 Wizara itaendelea na utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa barabara ya Kibaha – Chalinze – Morogoro (km 205) ya kiwango cha *Express Way* kwa kutumia utaratibu wa kushirikisha Sekta Binafsi (*Public – Private Partnership* - PPP).

343. ***Mheshimiwa Spika,*** miradi mingine ya barabara na madaraja itakayotekelezwa katika mwaka wa fedha 2023/24 ni kama ifuatavyo:

**Barabara ya Soni – Bumbuli – Dindira – Korogwe (km 74)**

344. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 3,500.00** kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Mtwara – Newala – Masasi (km 210)**

345. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 13,410.00** zinazojumuisha **Shilingi Milioni 2,410.00** fedha za ndani na **Shilingi milioni 11,000.00** fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kulipa madeni ya Mkandarasi wa barabara ya Mtwara – Newala – Masasi: sehemu ya Mtwara – Mnivata (km 50) na kuanza ujenzi wa sehemu za Mnivata – Mitesa (km 100), Mitesa – Masasi (km 60) na barabara ya Namichiga – Ruangwa (km 20) kwa kiwango cha lami. Kazi nyingine ni kuanza maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Mangamba – Madimba – Msimbati (km 35) kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Likuyufusi – Mkenda (km 122.50)**

346. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 3,000.00** zimetengwa katika mwaka wa fedha 2023/24, kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara ya Likuyufusi – Mkenda, sehemu ya Likuyufusi – Mhukuru (km 60) kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Ubena Zomozi – Ngerengere (km 11.6)**

347. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 2,500.00** zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara ya Ubena Zomozi – Ngerengere Jeshini – Ngerengere SGR Station kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya TAMCO – Vikawe – Mapinga (km 24)**

348. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 2,500.00** kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Makofia – Mlandizi (km 36.7)**

349. ***Mheshimiwa Spika,*** barabara ya Makofia – Mlandizi imetengewa jumla ya **Shilingi milioni 600.00** kwa ajili ya kuendelea na maandalizi ya ujenzi kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Musoma – Makojo – Busekela (km 92)**

350. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2023/24, barabara hii imetengewa jumla ya **Shilingi milioni 1,510.00** kwa ajili ya kulipa madai ya Mkandarasi na Mhandisi Mshauri wa Sehemu ya Kusenyi – Suguti (km 5.0) na kuanza ujenzi wa sehemu ya Musoma – Kusenyi (km 40) kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Kongwa Jct – Mpwapwa – Gulwe – Kibakwe (km 98)**

351. ***Mheshimiwa Spika,*** barabara hii imetengewa jumla ya **Shilingi milioni 4,500.00** kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa sehemu za Kongwa Jct – Ngambi – Mpwapwa (km 32) na Mpwapwa – Gulwe – Kibakwe (km 46.9) kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Muhutwe – Kamachumu – Muleba (km 54)**

352. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 1,000.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Iringa – Ruaha National Park (km 104)**

353. ***Mheshimiwa Spika,*** barabara hii imetengewa jumla ya **Shilingi milioni 500.00** fedha za ndani na **Shilingi milioni 6,000.00** fedha za nje kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara ya Iringa – Ruaha National Park (km 104) pamoja na barabara ya Iringa (Ipogolo) – Kilolo (km 33.2) kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Muheza – Amani (km 36)**

354. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 800.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Mtwara – Mingoyo – Masasi (km 200.51)**

355. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 500.00** fedha za ndani na **Shilingi milioni 10,000.00** fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kuanza ukarabati wa sehemu za Mtwara – Mingoyo (km 82.27) na Mingoyo – Nanganga – Masasi (km 118.24) kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Kibaoni – Majimoto – Muze – Kilyamatundu (km 189)**

356. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 4,500.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Ntendo – Muze – Kilyamatundu; sehemu ya Ntendo – Kizungu (km 25), kuanza ujenzi wa sehemu ya Kizungu – Muze (km 12) na kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Kibaoni – Majimoto – Inyonga (km 152) kwa kiwango cha lami.

**Daraja la Kigongo – Busisi (J.P. Magufuli) na Barabara Unganishi**

357. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 15,162.38** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa daraja hili na barabara unganishi.

**Daraja la Mzinga**

358. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 250.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa daraja hili katika Barabara ya Mbagala Rangi Tatu – Kongowe Jijini Dar es Salaam. Aidha, ujenzi wa daraja hili utajumuishwa kwenye upanuzi wa barabara ya Mbagala Rangi Tatu – Kongowe – Vikindu toka njia mbili za sasa na kuwa njia sita ambapo njia mbili za katikati zitakuwa kwa ajili ya Mabasi yaendayo kwa Haraka (BRT).

**Daraja la Ugalla**

359. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 500.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa daraja hili lililopo katika mkoa wa Katavi.

**Daraja la Kitengule na Barabara Unganishi**

360. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 3,010.00** zimetengwa kwa ajili ya kulipa sehemu ya madeni ya Mkandarasi na Mhandisi Mshauri wa ujenzi wa Daraja la Kitengule pamoja na barabara unganishi zenye urefu wa kilometa 18 na kuanza ujenzi wa barabara ya Kagera Sugar Jct – Kakunyu; sehemu ya Kagera Sugar Jct – Kitengule Jct (km 25).

**Barabara ya Morogoro – Dodoma (km 260) pamoja na Daraja la Mkundi**

361. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 1,000.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na kazi za Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa barabara ya Morogoro – Dodoma (km 260) pamoja na Daraja la Mkundi ili kuikarabati kwa kiwango cha lami. Kazi nyingine ni kuanza maandalizi ya ujenzi wa barabara

ya SUA Main Gate – Mzinga Factory Gate (km 11) kwa kiwango cha lami.

**Daraja Jipya la Wami**

362. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 10.00** zimetengwa kwa ajili ya kulipa sehemu ya madeni ya Mkandarasi na Mhandisi Mshauri wa ujenzi wa Daraja Jipya la Wami lililopo katika barabara ya Chalinze – Segera.

**Barabara ya Njombe – Makete – Isyonje (km 157.4)**

363. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 4,020.00** zimetengwa kwa ajili ya kulipa madeni ya Makandarasi na Wahandisi Washauri wa barabara ya Njombe – Makete – Isyonje, Sehemu za Njombe – Moronga (km 53.90) na Moronga – Makete (km 53.50). Kazi nyingine ni kuendelea na ujenzi wa barabara ya Isyonje – Makete; Sehemu ya Kitulo – Iniho (km 36.30) na barabara ya Njombe – Njombe Referral Hospital (km 3) kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Omugakorongo – Kigarama – Murongo (km 105)**

364. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 4,000.00** zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi wa sehemu ya Businde – Murongo (km 53.4) kwa kiwango cha lami pamoja na maandalizi ya ujenzi wa sehemu ya Omugakorongo – Businde (km 51.6).

**Barabara ya Nanganga – Ruangwa – Nachingwea (km 108.9)**

365. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 7,050.00** fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa sehemu za Nanganga – Ruangwa (km 53.2), kuanza ujenzi wa sehemu ya Nachingwea – Ruangwa (km 55.7) kwa kiwango cha lami pamoja na kuanza maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Nangurukuru – Liwale (km 228) Sehemu ya Choya – Liwale (km 72).

**Barabara ya Mpemba – Isongole (km 50.3)**

366. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 2,600.00** zimetengwa kwa ajili ya kulipa madeni ya Mkandarasi wa barabara ya Mpemba – Isongole (km 50.3). Kazi nyingine ni kuanza maandalizi ya ujenzi wa barabara za Mlowo – Kamsamba (km 147), Chang'ombe – Mkunguri – Makongorosi (km 61) na ujenzi wa kituo cha pamoja cha ukaguzi cha Iboya (One Stop Inspection Station – OSIS).

**Barabara ya Ruanda – Iyula – Nyimbili (km 21)**

367. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 1,000.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Katumbasongwe – Kasumulu – Ngana – Ileje (km 90.10)**

368. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 4,000.00** zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara ya Katumbasongwe – Kasumulu – Ngana – Ileje (km 90.10) na sehemu ya Isongole II – Ndembo (km 46) na Barabara ya kuingia Mji wa Ndembo (Ndembo Spur Road) kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Uyogo – Nyamilangano – Nyandekwa – Kahama (km 54)**

369. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 500.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Sengerema – Nyahunge (km 54)**

370. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 4,000.00** zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara ya Sengerema – Nyehunge (km 54) na maandalizi ya ujenzi wa sehemu ya Kamanga – Katunguru – Sengerema (km 35) kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Omurushaka – Nkwenda – Murongo (km 125)**

371. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 3,000.00** zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara hii sehemu ya Kyerwa – Chonyonyo (km 50) kwa kiwango cha lami.

**Upanuzi wa Barabara Kuu Zinazoingia Katikati ya Jiji la Dodoma (km 220)**

372. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 1,000.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina kwa ajili ya upanuzi wa barabara kuu zinazoingia katika Jiji la Dodoma (km 220) zinazohusisha barabara ya Dodoma – Morogoro (km 70), Dodoma – Iringa (km 50), Dodoma – Singida (km 50) na Dodoma – Arusha (km 50).

**Barabara ya Ntyuka Jct – Mvumi Hospital – Kikombo Jct. (km 76.07**)

373. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 5,000.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara ya Ntyuka Jct – Mvumi Hospital – Kikombo Jct (km 76.07); sehemu za Ntyuka Jct – Ntyuka (km 8.6) na kuanza ujenzi wa barabara ya Ntyuka – Kikombo (km 56.07), Sehemu ya Ihumwa – Hombolo (km 25) na barabara ya kuingia Hospitali ya JKT Msalato (km 5.5) kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Tarime – Mugumu (km 86.05)**

374. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 5,500.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara hii sehemu ya Mogabiri – Nyamongo (km 25) na kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu ya Tarime – Mogabiri (km 9.3), Nyamongo – Mugumu (km 48.15) pamoja na barabara ya kuelekea Mugumu Roundabout (km 3.6). Kazi nyingine ni kuanza maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Mika – Utegi – Shirati – Kirongwe yenye urefu wa kilometa 56.8.

**Barabara ya Shelui – Nzega (km 110)**

375. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 1,500.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina kwa ajili ya ukarabati kwa kiwango cha lami wa barabara ya Shelui – Nzega (km 110) na kuanza maandalizi ya ujenzi wa barbara ya Shelui – Senkeke – Tulia – Tiegelo (km 61.1) kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Nzega – Kagongwa (km 65**)

376. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 500.00** fedha za ndani na **Shilingi milioni 2,000.00** fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara ya Nzega – Kagongwa (km 65) kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Isabdula (Magu) – Bukwimba Station – Ngudu – Ng'hungumalwa (km 50)**

377. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 2,000.00** zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara ya Isabdula (Magu) – Bukwimba Station – Ngudu – Ng'hungumalwa (km 10) na kuanza maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Mwanangwa – Misasi – Salawe – Kahama (km 136) kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Nyololo – Mtwango (km 40.4)**

378. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 500.00** zimetengwa kwa ajili kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Nyololo – Mtwango (km 40.4) kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Singida – Sepuka – Ndago (km 75)**

379. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 3,000.00** zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara ya Singida – Sepuka – Ndago (km 75) kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Kitai – Lituhi pamoja na Daraja la Mnywamaji (km 90)**

380. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 5,500.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Kitai – Lituhi (km 90) pamoja na daraja la Mnywamaji; sehemu ya Amanimakoro – Ruanda (km 35) na kuanza ujenzi wa sehemu ya Ruanda – Ndumbi Port (km 50) kwa kiwango cha lami.

**Barabara za Kuelekea Katika Vituo vya Reli ya Kisasa ya SGR (km 87.6)**

381. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 14,600.00** zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara za kuelekea katika vituo vya reli ya kisasa (SGR) ambazo ni Morogoro – Kihonda SGR Station (km 10), Rudewa – Kilosa SGR Station (km 3), Gulwe – Gulwe SGR Station (km 2), Igandu – Igandu SGR Station (km 27), Ihumwa – Ihumwa Marshalling Yard (km 5.5), Kizota – Zuzu SGR Station (km 14), Bahi – Bahi SGR Station (km 4), Mlandizi – Ruvu SGR Station (km 22) na barabara za ndani za kituo cha SGR cha Dodoma (Access Roads to Dodoma SGR Station).

**Barabara ya Tanga – Pangani – Makurunge (km 174.5)**

382. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 3,500.00** fedha za ndani na **Shilingi milioni 27,559.40** fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara za Tanga – Pangani (km 50), Pangani – Mkange (km 124.5) kwa kiwango cha lami na Daraja la Pangani (m 525). Kazi nyingine ni kuanza ujenzi wa barabara ya Mkata – Kwa Msisi (km 36) kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Kisarawe – Maneromango – Mloka (km 150.46)**

383. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 2,000.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Geita – Bulyanhulu – Kahama (km 120)**

384. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 1,500.00** fedha za ndani na **Shilingi milioni 5,000.00** fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya maandalizi ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu ya Geita – Bulyanhulu Jct (km 58.3) na kuanza ujenzi wa sehemu ya Bulyanhulu Jct – Kahama (km 61.7). Kazi nyingine ni kuanza ujenzi wa barabara za Nyikonga – Kashelo (km 10.5), Kashelo – Ilolangulu (km 15) na Ushirombo – Kilimahewa – Nanda (km 15.7) kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Nyamirembe Port – Katoke (km 50)**

385. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 2,400.00** zimetengwa kwa ajili ya maandalizi ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara za Nyamirembe Port – Katoke (km 50), Chato Ginery – Bwina (km 8.1) na SIDO – Chato Zonal Hospital (km 5.3).

**Barabara ya Geita – Nzera – Nkome (km 54)**

386. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 3,000.00** zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Geita – Nzera – Nkome (km 54) sehemu ya Nzera – Nkome (km 20).

**Barabara ya Arusha – Moshi – Himo – Holili (km 199.51)**

387. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 2,810.00** fedha za ndani na **Shilingi milioni 4,400.00** za nje zimetengwa kwa ajili ya kulipa sehemu ya madeni ya Mkandarasi na Mhandisi Mshauri wa mradi wa ujenzi wa barabara ya Sakina – Tengeru na barabara ya mchepuo ya Arusha (Arusha Bypass). Kazi nyingine ni kuendelea na ujenzi wa barabara za Kijenge – Usa River (km 20), Mianzini – Ngaramtoni (km 18) na maandalizi ya upanuzi wa sehemu ya Tengeru – Moshi – Himo (km 105) pamoja na Mizani ya Himo.

**Barabara za Kuelekea Kwenye Mradi wa Kufua Umeme Katika Maporomoko ya Mto Rufiji (Access Roads To Rufiji Hydropower Project)**

388. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 5,800.00** kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Bigwa – Matombo – Mvuha (km 78) pamoja na ukarabati kwa kiwango cha changarawe wa barabara za Maneromango – Vikumburu – Mloka (km 100) na Kibiti – Mloka – Mtemele – Bwawa la Kufua Umeme la Julius Nyerere. Aidha, mradi huu utahusisha kuendelea kufanya Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa barabara za Chalinze – Utete (km 354.9) na Ubena Zomozi – Mvuha – Kisaki – Mtemele Jct (km 178); sehemu ya Ngerengere – Mvuha – Kisaki – Mtemele Jct (km 166.4) ikiwa ni mandalizi ya kuijenga kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Dar es Salaam – Chalinze – Morogoro Expressway (km 245)**

389. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 5,330.00** fedha za ndani kwa ajili ya kuanza upanuzi wa barabara ya Kibaha – TAMCO (km 4.5), ukarabati wa barabara ya Msoga – Msolwa (Chalinze Bypass km 10) na kuendelea na ukarabati (overlay) wa barabara ya Mlandizi – Chalinze (km 44.24), kuendelea na Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Awali wa sehemu ya Chalinze – Morogoro (km 126.1) na ujenzi wa barabara ya Kwa Mathiasi (Morogoro Road) – Msangani (Km 8.3). Kazi nyingine ni kulipa madeni ya Mkandarasi aliyefanya kazi ya kuboresha maeneo hatarishi (Assorted Accident Blackspot) ya barabara ya Dar es Salaam – Morogoro na kulipa madeni ya Mkandarasi wa ujenzi wa Kituo cha Pamoja cha Ukaguzi (One Stop Inspection Station – OSIS) cha Vigwaza.

**Barabara ya Wazo Hill – Bagamoyo – Msata (km 118.1)**

390. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 1,000.00** kwa ajili ya kuanza ukarabati na upanuzi wa barabara ya Wazo Hill – Bagamoyo – Msata (Sehemu ya Tegeta – Bagamoyo: Km 46.9).

**Barabara ya Usagara – Geita – Buzirayombo – Kyamyorwa (km 110)**

391. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 10.00** kwa ajili ya kulipa sehemu ya madeni ya Makandarasi kwa sehemu za Uyovu – Bwanga (km 43) na Bwanga – Biharamulo (km 67).

**Barabara ya Nyakahura – Kumubuga – Rulenge – Kabanga Nickel Road (km 141)**

392. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 3,000.00** kwa ajili ya maandalizi ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara za Nyakahura – Kumubuga – Murusagamba (km 34), Kumubuga – Rulenge – Murugarama (km 75) na Rulenge – Kabanga Nickel (km 32).

**Barabara ya Kigoma – Kidahwe – Uvinza – Kaliua – Tabora (km 429)**

393. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 840.00** fedha za ndani na **Shilingi milioni 19,266.50** fedha za nje kwa ajili ya kulipa madeni ya Makandarasi waliojenga barabara za Tabora – Ndono (km 42), Ndono – Urambo (km 52), Kaliua – Kazilambwa (km 56) na Urambo – Kaliua (km 28). Aidha, kazi nyingine ni kuendelea na ujenzi wa sehemu za Uvinza – Malagarasi (km 51.1), Kazilambwa – Chagu (km 36) na Urambo Roundabout.

**Barabara ya Ifakara – Kihansi – Mlimba – Madeke – Kibena (Njombe) (km 346.43)**

394. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 7,555.00** fedha za ndani na **Shilingi milioni 1,815.00** fedha za nje kwa ajili ya kuanza Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa sehemu za Njombe (Kibena) – Lupembe – Madeke (km 126) na Kihansi – Mlimba – Madeke (km 95.26) ili ziweze kujengwa kwa kiwango cha lami. Aidha, mradi huu utahusisha pia kuanza ujenzi wa barabara za Ifakara – Kihansi (km 124); Sehemu za

Ifakara – Mbingu (km 62.5) na Mbingu – Chita (km 37.5) kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Karatu – Mbulu – Haydom – Sibiti River – Lalago – Maswa (km 389)**

395. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 5,550.00** kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Karatu – Mbulu – Haydom – Sibiti River – Lalago – Maswa (km 389): Sehemu ya Mbulu – Garbabi (km 25) na kuanza ujenzi wa sehemu ya Labay – Haydom (km 25). Aidha, kazi nyingine ni kuanza maandalizi ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Mogitu – Hydom (km 68).

**Barabara ya Marangu – Tarakea – Rongai – Kamwanga /Bomang'ombe – Sanya Juu (km 105.16)**

396. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 7,830.00** kwa ajili ya kulipa madeni ya Makandarasi na Wahandisi Washauri wa barabara za Marangu – Rombo Mkuu – Tarakea (km 64), Sanya Juu – Kamwanga (sehemu ya Sanya Juu – Elerai, km 32) na KIA – Mererani (km 26). Kazi nyingine ni kuendelea na ujenzi wa barabara za Kwa Sadala – Masama – Machame Junction (km 16) na Kiboroloni – Kikarara – Tsuduni – Kidia (km 10.8) na kuanza ujenzi wa barabara ya Sanya Juu – Kamwanga (sehemu ya Elerai – Kamwanga - km 44). Mradi huu utahusisha pia ukarabati wa barabara ya Bomang'ombe – Sanya Juu (Kkm 25) na ujenzi wa barabara ya Tarakea – Holili (km 53).

**Barabara ya Tukuyu – Mbambo – Katumba (km 60.6)**

397. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 7,100.00** kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami wa kilometa 10 za sehemu za Bujesi – Mbambo na Kibanja – Tukuyu (km 7). Kazi nyingine ni kuanza ujenzi wa sehemu za Katumba – Lupaso (km 35.3), Mbaka – Kibanja (km 20.7) na maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Mbambo – Ipinda (km 19.7).

**Barabara ya Dodoma – Manyoni (km 127) na Barabara Kuingia Manyoni Mjini (km 4.8)**

398. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 50.00** kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa Kituo cha Pamoja cha Ukaguzi (One Stop Inspection Station – OSIS) cha Muhalala (Manyoni).

**Barabara ya Tabora – Mambali – Bukene – Itobo (km 114)**

399. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 500.00** kwa ajili ya kuendelea na maandalizi ya ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya Tabora – Mambali – Bukene (km 114).

**Barabara ya Namanyere – Katongoro – New Kipili Port (km 64.8)**

400. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 1,000.00** kwa ajili ya maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Namanyere – Katongoro – New Kipili Port kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Dumila – Kilosa – Mikumi (km 141)**

401. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 1,320.00** kwa ajili ya kulipa madeni ya Makandarasi na Mhandisi Mshauri wa sehemu za Dumila – Rudewa (km 45) na Rudewa – Kilosa (km 24). Kazi nyingine ni kufanya maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Kilosa – Ulaya – Mikumi (km 72) kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Sumbawanga – Matai – Kasanga Port (km 107)**

402. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 5,010.00** kwa ajili ya kulipa madeni ya Mkandarasi na Mhandisi Mshauri wa ujenzi wa barabara ya Sumbawanga – Matai – Kasanga Port (km 107), kuendelea na ujenzi wa barabara ya Matai – Kasesya (km 50); sehemu ya Matai – Tatanda (km 25) na kuanza ujenzi wa sehemu ya Tatanda – Kasesya (km 25).

Aidha, mradi huu utahusisha kuanza maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Laela – Mwimbi – Kizombwe (km 93) kwa kiwango cha lami.

**Ujenzi wa Madaraja Makubwa**

403. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 15,430.00** kwa ajili ya kulipa sehemu ya madeni ya Makandarasi na Wahandisi Washauri wa ujenzi wa Madaraja ya Magufuli (Morogoro), Ruhuhu (Ruvuma), Momba (Rukwa), Mara (Mara), Magara (Manyara), Msingi (Singida) na Kiyegeya (Morogoro). Kazi nyingine ni kuanza ukarabati wa daraja la Kirumi (Mara), kuendelea na ujenzi wa barabara unganishi za Daraja la Sibiti (Singida), kuendelea na ujenzi wa Madaraja ya Sukuma (Mwanza), Godegode (Dodoma), Mpiji Chini (Dar es Salaam), Sanza (Singida), Mirumba (Katavi), Simiyu (Mwanza) pamoja na Mitomoni na Mkenda (Ruvuma). Kazi nyingine ni kuanza ujenzi wa Madaraja ya Chakwale (Morogoro), Nguyami (Morogoro) na Mbambe (Pwani)

Aidha, mradi huu utahusisha kuanza maandalizi ya ujenzi wa Madaraja ya Mtera, Nzali, Kibakwe, Mpwapwa, Kerema na Munguli yaliyopo Dodoma; Doma (Morogoro); Mbangala (Mtwara), Kinyerezi (Dar es Salaam), Kisorya/Ukerewe (Mara/Mwanza) na Suguti (Mara). Kazi nyingine ni kuendelea na Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa Daraja la Malagarasi Chini (Kigoma) ma kununua Vipuri vya Madaraja ya Dharura.

**Barabara ya New Bagamoyo (Kawawa Jct – Tegeta (km 17.2)**

404. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 10.00** zimetengwa kwa ajili ya kulipa madeni ya Mkandarasi na Mhandisi Mshauri wa ujenzi wa Barabara ya Morocco – Mwenge (km 4.3).

**Barabara ya Kyaka – Bugene – Kasulo (km 183.1)**

405. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 3,010.00** zimetengwa kwa ajili ya kulipa madeni ya Mkandarasi wa sehemu ya Kyaka – Bugene (km 59.1) na kuendelea na ujenzi

kwa kiwango cha lami wa barabara ya Kumunazi – Kasulo – Bugene (km 133) sehemu ya Bugene – Burigi Chato National Park (km 60).

**Barabara ya Isaka – Lusahunga (km 242)**

406. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 560.00** fedha za ndani na **Shilingi milioni 16,718.90** fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kulipa madeni ya Makandarasi na Mhandisi Mshauri wa sehemu ya Ushirombo – Lusahunga (km 110). Kazi nyingine ni kuendelea na ujenzi wa Kituo cha Pamoja cha Ukaguzi – OSIS cha Nyakanazi na kuanza ukarabati wa sehemu ya Lusahunga – Rusumo (km 92). Mradi huu utahusisha pia maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Nyakasanza – Kobero (Km 58) kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Manyoni – Itigi – Tabora (km 259.75)**

407. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 30.00** fedha za ndani na **Shilingi milioni 1,100.00** fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kulipa madeni ya Makandarasi na Wahandisi Washauri wa ujenzi wa sehemu za Manyoni – Itigi – Chaya (km 89.35), Nyahua – Chaya (km 85.4) na Tabora – Nyahua (km 85).

**Barabara za Mikoa (km 595.02)**

408. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2023/24, jumla ya **Shilingi milioni 61,585.00** zimetengwa kwa ajili ya barabara za mikoa na madaraja katika mikoa yote 26 ya Tanzania Bara. Kazi zilizopangwa kutekelezwa ni ukarabati wa jumla ya **kilometa 544.94** kwa kiwango cha changarawe, kujenga **kilometa 50.08** kwa kiwango cha lami na ujenzi wa Madaraja/Makalavati **59**. Aidha, kati ya fedha hizi, **Shilingi milioni 798.6** zitatumika kwa ajili ya programu ya mafunzo kwa vitendo (Structured Engineers Apprentinceship Programme – SEAP) kwa wahandisi wahitimu. Orodha ya miradi ya barabara za Mikoa itakayotekelezwa kwa kutumia fedha za Bajeti ya Maendeleo kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali imeoneshwa katika **Kiambatisho Na. 2.**

**Barabara ya Mwanza/Shinyanga Border – Mwanza (km 102)**

409. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 400.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina ili kuifanyia ukarabati barabara hii.

**Mradi wa Kupunguza Msongamano Barabara za Dar es Salaam (km 138.5)**

410. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 10,190.00** kwa ajili ya kulipa madeni ya Makandarasi wa barabara za Mbezi – Malambamawili – Kinyerezi – Banana (km 14), Mbezi Mwisho – Goba (km 7), Tangi Bovu – Goba (km 9), Kimara Baruti – Msewe – Changanyikeni (km 2.6), Banana – Kitunda – Kivule – Msongola (km 14.7): Sehemu ya Kitunda – Kivule (km 3.2), Ardhi – Makongo – Goba; Sehemu ya Goba – Makongo (km 4), Tegeta Kibaoni – Wazo Hill – Goba – Mbezi/Morogoro Road (Mbezi Mwisho); sehemu ya Madale – Goba (km 5) na Tegeta Kibaoni – Wazo Hill – Goba – Mbezi/Morogoro Road (Mbezi Mwisho); sehemu ya Wazo Hill – Madale (km 6) na Ardhi – Makongo – Goba; sehemu ya Ardhi – Makongo (km 5).

Kazi nyingine ni kuendelea na ujenzi wa barabara ya Goba – Matosa – Temboni (km 6), kuanza ujenzi wa barabara za Kibamba – Kisopwa – Kwembe – Makondeko (km 14.66), Kongowe – Mjimwema – Kivukoni Ferry Road (One Lane Widening: km 25.1), kuanza upanuzi wa barabara ya Mwai Kibaki (km 9.1) pamoja na kuanza maandalizi ya ujenzi wa barabara za Mji Mwema – Kimbiji – Pembamnazi (km 27), Kipata (m 700), Livingstone (m 350), Msikitini – Sharif Shamba (km 1), Kibamba Shule – Mpiji Magoe (km 9.2), Mbezi Victoria – Magoe Mpiji (km 9.55), Chanika – Mbande (km 4), Mbezi Msakuzi – Makabe Jct (km 8.36) na Kimara – Bonyokwa – Kinyerezi (km 6.73).

**Barabara ya Nyamuswa – Bunda – Kisorya (km 107.4)**

411. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 20.00** zimetengwa kwa ajili ya kulipa madeni ya Mkandarasi na

Mhandisi Mshauri wa ujenzi wa sehemu za Kisorya – Bulamba (km 51) na Nyamuswa – Bunda – Bulamba (km 56.4).

**Barabara ya Kolandoto – Lalago – Ng'oboko – Mwanhuzi (km 122)**

412. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 2,000.00** zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara za Kolandoto – Lalago (km 62) na Iguguno Shamba – Nduguti – Mkalama (km 89).

**Barabara ya Ndundu – Somanga (km 60)**

413. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 7,010.00** zimetengwa kwa ajili ya kulipa sehemu ya madeni ya Mkandarasi wa ujenzi wa barabara ya Ndundu – Somanga (km 60), kuendelea na ujenzi wa barabara ya Utete – Nyamwage (km 33.7), kuendelea na maandalizi ya ukarabati wa barabara za Kongowe – Malendego (km 160.65) na Nangurukuru – Mbwemkuru (Km 95). Kazi nyingine ni kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Ikwiriri – Mkongo (km 27.74).

**Barabara ya Kasulu – Manyovu (km 68)**

414. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 250.00** fedha za ndani na **Shilingi milioni 12,540.00** fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara ya Kasulu – Manyovu pamoja na barabara za kuingia Kasulu mjini (km 68).

**Barabara ya Dodoma *City Outer Dual Carriageway Ring Road Lot1 & 2* (km 112.3)**

415. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 4,000.00** fedha za ndani na **Shilingi milioni 45,080.00** fedha za nje kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa Barabara ya Mzunguko wa Nje katika Jiji Dodoma (Dodoma City Outer Dual Carriageway Ring Road) sehemu ya Nala – Veyula – Mtumba – Ihumwa Dry Port (km 52.3), sehemu ya Ihumwa Dry Port – Matumbulu – Nala (km 60), Kikombo Jct – Chololo – Mapinduzi (JWTZ HQ) (km 18). Kazi nyingine ni kuanza ujenzi wa barabara ya Msalato – Mtumba – Chamwino IKULU (km 30.0) kwa kiwango

cha lami na kuendelea na maandalizi ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara za Mzunguko wa Ndani katika Jiji la Dodoma (Dodoma Inner Ring Road) kwa sehemu ya Bahi R/About – Image R/About – Ntyuka R/About – Makulu R/About (km 6.3) na Mzunguko wa Kati katika Jiji la Dodoma (Dodoma City Middle Ring Road) inayoanzia Nanenane – Miyuji – Mnadani Sekondari – Mkonze – Ntyuka – Nanenane (km 47.2).

**Barabara ya Kidatu – Ifakara – Lupilo – Malinyi – Londo – Lumecha/ Songea (km 499)**

416. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 1,250.00** kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa sehemu ya Kidatu – Ifakara (km 66.9) na kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Chalinze – Magindu – Lukenge – Seregete B – Kabwe Jct – Mkulazi (km 77.50). Mradi huu utahusisha pia kuendelea na ukarabati kwa kiwango cha changarawe wa barabara ya Dakawa Jct – Mbigiri (km 7) na barabara zenye jumla ya kilometa 50 kuelekea mashamba ya wakulima wa miwa ya Mbigiri.

**Barabara ya Tabora – Ipole – Koga – Mpanda (km 365.36)**

417. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 540.00** fedha za ndani na **Shilingi milioni 6,457.00** fedha za nje kwa ajili ya kulipa madeni ya Makandarasi na Wahandisi Washauri wa ujenzi wa sehemu za Usesula – Komanga (km 115.5), Komanga – Kasinde (km 112.8), Kasinde – Mpanda (km 111.7) na Tabora – Sikonge (km 30). Aidha, mradi huu utahusisha ujenzi wa barabara ya Mpanda Airport – Kasimba Junction (km 3) kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Makutano – Natta – Mugumu/Loliondo – Mto wa Mbu (km 235)**

418. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 4,020.00** kwa ajili ya kulipa madeni ya Makandarasi na Wahandisi Washauri wa barabara za Makutano – Sanzate (km 50) na Waso – Sale Jct (km 49), kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami kwa sehemu ya Sanzate – Natta (km 40), kuanza ujenzi

wa sehemu ya Waso – Loliondo (km 10), Ngaresero Engaruka (km 39) na Mto wa Mbu – Selila (km 20) pamoja na kuendelea na maandalizi ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu ya Natta – Mugumu (km 35).

**Barabara ya Ibanda – Itungi Port (km 26)**

419. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 4,520.00** kwa ajili ya kuendelea ukarabati wa barabara za Ibanda – Itungi (km 26) na ujenzi wa sehemu ya Iponjola – Kiwira Port (km 6). Kazi nyingine ni kukamilisha ujenzi wa Kituo cha Pamoja cha Ukaguzi mpakani Kasumulu/Songwe (Kasumulu/Songwe – Tanzania/Malawi Border – OSBP), pamoja na kulipa madeni ya Mkandarasi na Mhandisi Mshauri wa ujenzi wa barabara ya Kikusya – Ipinda – Matema Beach (km 39.1) na barabara ya Uyole – Kasumulu (sehemu ya Ilima Escarpment, km 3).

**Barabara ya Nzega – Tabora (km 289.7)**

420. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 20.00** kwa ajili ya kulipa madeni ya Makandarasi na Wahandisi Washauri wa ujenzi wa sehemu za Nzega – Puge (km 58.6) na Puge – Tabora (km 56.1).

**Barabara ya Sumbawanga – Mpanda – Nyakanazi (km 803.6)**

421. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 15,540.00** kwa ajili ya kulipa madeni ya Makandarasi na Wahandisi Washauri wa sehemu za Sumbawanga – Kanazi (km 75), Kanazi – Kizi – Kibaoni (km 76.6), Sitalike – Mpanda (km 36) na Mpanda – Ifukutwa – Vikonge (km 37.65). Kazi nyingine ni kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami barabara za Mpanda – Mishamo – Uvinza; Sehemu ya Vikonge – Luhafwe (km 25) na Kibaoni – Mlele Jct (km 50) na kuanza ujenzi wa sehemu za Luhafwe – Mishamo Jct (km 37.7), Mlele Junction – Stalike (km 23.5) na Kagwira – Ikola – Karema Port (km 112). Mradi huu utahusisha pia maandalizi ya ujenzi wa barabara za Kizi – Lyambalyamfipa – Sitalike (km 86.31) na Lyazumbi – Kabwe (km 65).

**Barabara ya Nyanguge – Musoma/ Usagara – Kisesa Bypass (km 202.25)**

422. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 530.00** kwa ajili ya kulipa sehemu ya madeni ya Makandarasi wa barabara za Simiyu/Mara Border – Musoma (Km 85.5) na Usagara – Kisesa (Mwanza Bypass km 17.35). Kazi nyingine ni kuendelea na maandalizi ya ukarabati wa sehemu ya Nyanguge – Simiyu/Mara Border (km 100.4) na kulipa madeni ya Mkandarasi wa barabara ya kuelekea Uwanja wa Ndege wa Mwanza.

**Barabara ya Magole – Mziha – Handeni (km 152.8)**

423. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 1,010.00** kwa ajili ya kulipa sehemu ya madeni ya Mkandarasi wa barabara ya Magole – Turiani (km 45.2) na kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Turiani – Mziha – Handeni (km 104).

**Ujenzi wa Barabara za Juu (Flyovers) Jijini DSM na Barabara Unganishi**

424. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 320.00** fedha za ndani na **Shilingi milioni 1,100.00** fedha za nje kwa ajili ya kulipa madeni ya Makandarasi na Wahandisi Washauri wa ujenzi wa barabara za juu katika makutano ya Ubungo (Ubungo Interchange) pamoja na kuendelea na maandalizi ya kuboresha makutano ya barabara katika maeneo ya KAMATA, Magomeni, Mwenge, Tabata/Mandela, Morocco, Buguruni, Mbezi Mwisho, Fire pamoja na makutano ya barabara za Kinondoni/Ali Hassan Mwinyi na Selander (Ali Hassan Mwinyi/UN Road Jct).

**Barabara ya Mwigumbi – Maswa – Bariadi – Lamadi (km 171)**

425. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 1,520.00** kwa ajili ya kulipa madai ya Makandarasi na Wahandisi Washauri wa barabara za Mwigumbi – Maswa (km 50.3) na Maswa – Bariadi (km 49.7). Aidha, kazi nyingine ni

kukamilisha ujenzi kwa kiwango cha lami kwa barabara ya Mchepuo wa Maswa (Maswa Bypass; km 11).

**Barabara ya Tabora – Ipole – Rungwa (Sehemu ya Ipole – Rungwa (km 172)**

426. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 1,000.00** kwa ajili ya kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Kidahwe – Kasulu – Kibondo – Nyakanazi (km 341.25)**

427. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 6,520.00** fedha za ndani na **Shilingi milioni 49,504.96** fedha za nje kwa ajili ya kulipa madai ya Makandarasi na Wahandisi Washauri wa barabara za Kidahwe – Kasulu (km 63) na Nyakanazi – Kakonko (km 50). Kazi nyingine ni kuendelea na ujenzi wa barabara za Kanyani Jct. – Mvugwe (km 70.5), Mvugwe – Nduta Jct. (km 59.35), Nduta Jct. – Kibondo Jct. – Kabingo (km 62.5), Nduta Jct. – Kibondo (km 25.9) na Kibondo – Mabamba (km 48).

**Barabara ya Kwenda Kiwanja cha Ndege cha Mafia (Mafia Airport Access Road (km 16)**

428. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 1,010.00** kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara ya Kilindoni – Ras Mkumbi (km 54.4)

**Daraja la Kigamboni (Nyerere) na Barabara Unganishi**

429. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 3,030.00** kwa ajili ya mchango wa Serikali kwenye ujenzi wa Daraja la Nyerere, kulipa madai ya Makandarasi na Wahandisi Washauri wa barabara za Daraja la Nyerere – Vijibweni na Tungi – Kibada (km 3.8). Kazi nyingine ni kuanza ujenzi wa barabara ya Kibada – Mwasonga – Tundwisongani Jct/Tundwisongani – Kimbiji (km 41).

**Barabara ya Mutukula – Bukoba – Muhutwe – Kagoma (km 215.8)**

430. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 1,400.00** kwa ajili ya kuendelea na Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa barabara za Bukoba Mjini – Busimbe – Maruku – Kanyangereko – Ngongo (km 19.1) na Kyaka – Bukoba – Muhutwe – Kagoma (km 106). Kazi nyingine ni kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Kanazi (Kyetema) – Ibwera – Katoro – Kyaka II (km 60.7).

**Fedha za Matengenezo na Ukarabati wa Barabara**

431. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 599,756.4678** zimetengwa katika mwaka wa fedha 2023/24 kwa ajili ya mradi huu. Kazi zitakazofanyika ni matengenezo na ukarabati wa barabara, Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina, udhibiti wa uzito wa magari, usalama barabarani na mazingira, matengenezo na ukarabati wa vivuko pamoja na kujenga uwezo wa Wizara na Taasisi zinazosimamia masuala ya barabara na vivuko. Fedha hizi zinasimamiwa na Bodi ya Mfuko wa Barabara.

**Ujenzi wa Njia za Magari Mazito na Maegesho ya Dharura Katika Barabara Kuu ya Ukanda wa Kati (Providing Lane Enhancement Including Climbing Lanes, Passing Bays, Rest and Emergency Lay Bays on Central Corridor)**

432. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 300.00** kwa ajili ya maandalizi ya kuanza kazi ya Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa maeneo ya kujenga njia za magari mazito kwenye miinuko na kujenga maegesho ya dharura katika Barabara Kuu ya Ukanda wa Kati. Aidha, ujenzi wa mradi huu utajumuishwa kwenye Usanifu wa Kina kabla ya kufanya ukarabati wa barabara za Ukanda wa Kati zilizopangwa kufanyiwa Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina ambazo ni Morogoro – Dodoma (km 260), Singida – Shelui (km 110) na Shelui – Nzega (km 110) ambazo usanifu wa kina unaendelea.

**Upanuzi wa Barabara ya Kimara – Kibaha (km 25.7) Ikijumuisha Upanuzi wa Madaraja ya Kibamba, Kiluvya na Mpiji**

433. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 1,500.00** kwa ajili ya kulipa madai ya Makandarasi na Mhandisi Mshauri wa barabara ya Kimara – Kibaha (km 25.7); sehemu ya Kimara – Kibaha Mizani (km 19.2) na madaraja ya Kibamba, Kiluvya na Mpiji.

**Barabara ya Kisarawe – Mlandizi (km 119)**

434. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 800.00** kwa ajili ya kuanza maandalizi ya ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Pugu – Kifuru – Mbezi Mwisho – Mpiji Magoe – Bunju (km 34)**

435. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 440.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa sehemu za Bunju – Kibamba – Pugu Kajiungeni – Mzinga – Tuangoma – Kihamboni (km 61.0) na Mbezi – Mbezi Mwisho – Kifuru – Banana – Kipara – Kigamboni (km 49.0).

**Barabara ya Kagoma – Lusahunga (km 172.50)**

436. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 10.00** zimetengwa kwa ajili ya kulipa madeni ya Mkandarasi na Mhandisi Mshauri wa barabara ya Muleba – Kanyambogo – Rubya (km 18.5).

**Barabara ya Singida – Shelui (km 110)**

437. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 2,500.00** zimetengwa kwa ajili ya kukamilisha usanifu wa kina ikiwa ni maandalizi ya kuanza ukarabati kwa kiwango cha lami wa barabara ya Singida – Shelui (km 110) na kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Ulemo – Kinampanda – Gumanga (Singida) – Mkalama (km 46).

**Barabara ya Dar es Salaam – Mbagala (Kilwa Road) – Gerezani (*sehemu* ya Kamata – Bendera Tatu: km 1.3)**

438. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 2,275.73** zimetengwa kwa ajili ya kulipa madeni ya Mkandarasi na Mhandisi Mshauri wa ujenzi wa daraja la Gerezani. Kazi nyingine ni kuanza upanuzi wa sehemu ya Mbagala Rangi Tatu – Kongowe – Vikindu (10.3) kutoka njia mbili kuwa njia sita kati ya hizo njia mbili za katikati zitakuwa za Mabasi Yaendayo Haraka (BRT).

**Barabara ya Msimba – Ruaha Mbuyuni/Ikokoto Mafinga (km 365.9)**

439. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 730.00** zimetengwa kwa ajili ya kulipa madeni ya Makandarasi na Wahandisi Washauri wa ukarabati wa sehemu za Mafinga – Nyigo (km 74.1) na Nyigo – Igawa (km 63.8). Kazi nyingine ni kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Rujewa – Madibira – Mafinga (km 152) na kuendelea na Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina kwa ajili ya ukarabati wa barabara ya Morogoro – Iringa sehemu ya Tumbaku Jct – Mangae/Melela – Mikumi – Iyovi (km 158.45) ikiwa ni pamoja na daraja la Doma.

**Barabara ya Same – Mkumbara – Korogwe (km 239.5)**

440. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 7,660.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na maandalizi ya ukarabati wa sehemu za Same – Himo (km 76) na Mombo – Lushoto (km 32). Aidha, kazi nyingine ni kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa barabara za Lushoto – Magamba – Mlola (km 34.5) na kuendelea na ujenzi wa barabara ya Same – Kisiwani – Mkomazi (km 97); sehemu za Same – Kisiwani – Mroyo (km 56.83) na Ndungu – Mkomazi (km 36).

**Barabara ya Mbeya – Makongolosi – Mkiwa (km 479.9)**

441. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 6,355.00** zimetengwa kwa ajili ya kulipa sehemu ya madeni ya Makandarasi na Wahandisi Washauri wa sehemu za Mbeya –

Lwanjilo (Km 36), Lwanjilo – Chunya (km 36) na Chunya – Makongolosi (km 39). Kazi nyingine ni kuendelea na ujenzi wa barabara za Itigi Mjini (km 10) na sehemu ya Noranga – Itigi (Mlongoji) Km 25, kuanza ujenzi wa sehemu ya Itigi – Mkiwa (km 31.6) pamoja na kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Mbalizi – Makongolosi (km 50), Makongolosi – Rungwa – Noranga; sehemu ya Makongolosi – Rungwa (km 50).

**Barabara ya Itoni – Ludewa – Manda (km 211)**

442. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 4,010.00** zimetengwa kwa ajili ya kulipa sehemu ya madeni ya Mkandarasi na Mhandisi Mashauri wa ujenzi wa barabara ya Lusitu – Mawengi (km 50) kwa kiwango cha zege na kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha zege wa sehemu ya Itoni – Lusitu (km 50). Kazi nyingine ni kuanza maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Nkomang'ombe – Mchuchuma (km 7) kwa kiwango cha lami.

**Ujenzi wa Daraja Jipya la Selander (Tanzanite)**

443. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 10.00** zimetengwa kwa ajili ya kulipa sehemu ya madeni ya Mkandarasi na Mhandisi Mshauri wa ujenzi wa Daraja Jipya la Selander (km 1.03) na barabara unganishi zenye jumla ya urefu wa kilometa 5.2.

**Barabara ya Handeni – Kibirashi – Kijungu – Kibaya – Njoro – Olboloti – Mrijo Chini – Goima – Chemba – Kwa Mtoro – Singida (Km 424.24) na Goima – Dalai – Bicha (km 35.76)**

444. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 5,250.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendela na ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara hii kwa sehemu ya Handeni – Mafuleta (km 20) na kuanza ujenzi wa sehemu ya Mafuleta – Kileguru (km 30).

**Barabara ya Makambako – Songea na Barabara ya Mchepuo ya Songea (Songea Bypass) (km 295)**

445. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 1,320.00** fedha za ndani na **Shilingi milioni 21,417.30** fedha za nje zimetengwa

kwa ajili ya kuanza ukarabati wa barabara ya Makambako – Songea sehemu ya Lutukila – Songea (km 95.18) pamoja na ujenzi wa barabara ya Mchepuo wa Songea (Songea Bypass) km 11. Kazi nyingine ni kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Ramadhani – Ilembula Hospital – Iyayi (km 75).

**Barabara ya Dodoma – Iringa (km 260)**

446. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 2,510.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya mchepuo ya Iringa (Iringa Bypass km 7.3), kuimarisha matabaka ya barabara ya Iringa – Dodoma, kulipa madeni ya Mkandarasi wa ujenzi wa Mizani kwenye barabara ya Iringa – Dodoma na kuanza ujenzi wa barabara ya Iringa – Pawaga (km 71.93).

**Barabara ya Dodoma – Babati (km 263.4)**

447. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 1,327.00** zimetengwa kwa ajili ya kulipa madeni ya Makandarasi na Wahandisi Washauri wa ujenzi wa sehemu za Dodoma – Mayamaya (km 43.65), Mayamaya – Mela (km 99.35), Mela – Bonga (km 88.8) na kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa barabara ya mchepuo wa Babati (Babati Bypass km 27.5) pamoja na Miteremko ya Magara (Magara Escarpment) (km 3). Mradi huu utahusisha pia maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Dareda – Dongobesh (km 60) sehemu ya Dareda Mjini – Dareda Mission (km 8) kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Masasi – Songea – Mbamba Bay (km 343.2)**

448. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 40.00** fedha za ndani na **Shilingi milioni 3,300.00** fedha za nje kwa ajili ya kulipa madeni ya Makandarasi na Wahandisi Washauri wa ujenzi wa sehemu za Tunduru – Matemanga (km 59), Matemanga – Kilimasera (km 68.2), Kilimasera – Namtumbo (km 60) na Mbinga – Mbamba Bay (km 66).

**Ujenzi wa Barabara za Chuo cha Uongozi (Uongozi Institute)**

449. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 200.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa barabara za ndani ya eneo la Chuo cha Uongozi Bagamoyo.

**Barabara ya Igawa – Songwe – Tunduma na Mbeya *Bypass* (km 266.9)**

450. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 5,150.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na upanuzi wa sehemu ya Uyole – Ifisi –Songwe Airport (Km 36).

**Miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka (BRT Phase I – V: km 69.8)**

451. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 2,255.00** fedha za ndani na **Shilingi milioni 42,630.00** fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya Pili. Kazi nyingine ni kuendelea na ujenzi wa Miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya Tatu na Nne. Aidha, fedha hizi zitatumika kuanza maboresho ya miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka iliyojengwa katika Awamu ya Kwanza, kuanza ujenzi wa daraja la Jangwani na kuanza ujenzi wa Miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya Tano.

**Ujenzi wa Jengo la Makao Makuu ya Taasisi ya Teknolojia ya Ujenzi (Institute of Construction Technology – ICoT)**

452. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 2,000.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya Taasisi ya Teknolojia ya Ujenzi (Institute of Construction Technology – ICoT) Mkoani Morogoro na majengo ya ICoT tawi la Mbeya.

**Ujenzi wa Makao Makuu ya Wakala wa Barabara Tanzania**

453. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 4,000.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa jengo la Makao

Makuu ya Wakala ya Barabara (TANROADS) pamoja na Ofisi za Mikoa ya Dar es Salaam, Katavi, Geita, Simiyu, Njombe, Lindi na Songwe.

**MIRADI YA USALAMA BARABARANI NA MAZINGIRA**

454. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ina jukumu la kuratibu shughuli za usalama barabarani, mazingira na kudhibiti uzito wa magari yanayotumia barabara nchini. Katika mwaka wa fedha 2023/24, mradi wa **Usalama Barabarani** umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 1,095.00** kwa ajili ya kuwezesha huduma ya ushauri kwa kufanya mapitio ya Sera ya Taifa ya Usalama Barabarani na ujenzi wa Vituo vya Ukaguzi wa Pamoja (One Stop Inspection Stations - OSIS) vya Idofi (Iringa), Mpemba (Songwe), Himo (Kilimanjaro) na Segera (Tanga). Kazi nyingine ni kufanya utafiti wa athari na gharama kutokana na uzidishaji wa uzito wa gari dhidi ya uharibifu wa barabara kuu ya TANZAM; kutoa mafunzo ya udhibiti uzito wa magari kwa Wahandisi na Mafundi Sanifu. Vilevile, kazi nyingine ni usanifu, usambazaji, ufungaji wa mfumo wa kuwasaidia watembea kwa miguu kuvuka barabara kwa usalama; ujenzi wa vituo vya mizani vya Kidyama katika barabara ya Kasulu - Manyovu na Marolegwa katika barabara ya Kasulu- Kibondo na kuendelea na ufungaji wa vifaa vya kisasa vya upimaji uzito wa magari katika vituo vya mizani 42 katika barabara kuu. Vilevile, fedha za mradi huu zitatumika kuwezesha utengenezaji na kufungwa kwa Mfumo wa Ufuatiliaji wa Utendaji Kazi katika mizani 42; maboresho ya Mfumo wa Utunzaji Kumbukumbu wa Ajali za Barabarani (Road Accidents Information System - RAIS) na ufungaji wa kamera za kudhibiti mwendokasi katika barabara ya Morogoro – Dodoma.

455. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi wa Kujenga **Uwezo wa Taasisi Katika Masuala ya Usalama Barabarani na Mazingira** umetengewa **Shilingi milioni 127.407** kwa ajili ya uchapishaji wa Mwongozo wa Ukaguzi wa Usalama wa Barabara; kufanya utafiti ili kubaini athari za kijamii na kiuchumi kutokana na ajali za barabarani pamoja na kushiriki katika mikutano inayohusu masuala ya usalama barabarani katika Sekta ya Ujenzi. 456. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi wa **Menejimenti ya Usimamizi wa Mazingira** umetengewa **Shilingi milioni 147.740** kwa ajili ya

kuandaa Mkakati wa Kukabili Majanga kwa Sekta ya Ujenzi (Works Sector Disaster Management Strategy), kufanya mapitio ya miongozo ya tathmini na usimamizi wa mazingira ya Sekta ya Ujenzi na kuandaa Mpango Tekelezi wa Mazingira Kisekta wa Miaka Mitano (Sector Environmental Action Plan, 20242029). Kazi nyingine ni kuwezesha mafunzo kwa Wahandisi na Mafundi Sanifu kuhusu kuhimili mabadiliko ya tabianchi.

**MIRADI YA UJENZI WA MIUNDOMBINU YA VIWANJA VYA NDEGE**

457. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2023.24 miradi ya ujenzi wa miundombinu ya viwanja vya ndege imetengewa jumla ya **Shilingi milioni 96,830.676** Kiasi hicho kinajumuisha **Shilingi milioni 48,543.056** fedha za ndani na **Shilingi milioni 48,287.60** fedha za nje. Miradi ifuatayo imepangwa kutekelezwa:

**Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kigoma**

458. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 9,593.99** zinazojumuisha **Shilingi milioni 5,057.80** fedha za ndani na **Shilingi milioni 4,536.19** fedha za nje. Fedha hizi ni kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa Jengo la Abiria pamoja na miundombinu yake (ukarabati na upanuzi wa maegesho ya ndege, maegesho ya magari na barabara ya kuingia na kutoka kiwanjani). Kazi nyingine ni ujenzi wa uzio wa usalama, jengo la kuongozea ndege na jengo la uchunguzi wa hali ya hewa na usimikaji wa taa na mitambo ya kuongozea ndege.

**Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Mpanda**

459. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 10.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na maandalizi ya kufanya usanifu wa Jengo la abiria kwa ajili ya ujenzi wa jengo hilo.

**Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Tabora**

460. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 5,264.85.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi milioni 728.66** ni fedha za ndani na **Shilingi milioni 4,536.19** ni fedha za nje kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa Jengo la Abiria na miundombinu

yake, jengo la kuongozea ndege, barabara ya kuingia kiwanjani, maegesho ya magari, uzio wa usalama pamoja na jengo la uchunguzi wa hali ya hewa.

**Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Songwe**

461. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 6,117.11** zimetengwa kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa Jengo la Abiria na mifumo yake pamoja na kulipa madai ya Makandarasi na Mshauri Elekezi waliotekeleza na kusimamia kazi za usimikaji wa taa za kuongozea ndege pamoja na ujenzi wa uzio wa usalama.

**Ukarabati wa Kiwanja cha Ndege cha Mwanza**

462. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 5,830.53** zimetengwa kwa ajili ya kulipa madai ya Mkandarasi na Mshauri Elekezi waliotekeleza na kusimamia kazi za upanuzi na ukarabati wa barabara ya kuruka na kutua ndege, maungio ya ndege, maegesho ya ndege, jengo la kuongozea ndege, jengo la mizigo pamoja na ujenzi wa mifumo ya maji safi na majitaka.

**Ukarabati wa Kiwanja cha Ndege cha Arusha**

463. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2023/24, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 266.22** kwa ajili ya ujenzi wa uzio wa usalama.

**Ukarabati wa Kiwanja cha Ndege cha Mtwara**

464. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 5,442.57** zimetengwa kwa ajili ya kulipa madai ya Mkandarasi na Mshauri Elekezi waliotekeleza na kusimamia kazi zilizokamilika ambazo ni ukarabati wa barabara ya kuruka na kutua ndege, viungio vyake, maegesho ya ndege, kusimika taa za kuongozea ndege, ujenzi wa barabara ya kuingia na kutoka kiwanjani, maegesho ya magari pamoja na uzio wa usalama.

**Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Sumbawanga**

465. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 5,262.19.** zinazojumuisha **Shilingi milioni 726.00** fedha za ndani na **Shilingi milioni 4,536.19** fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya mradi huu. Kazi zitakazotekelezwa ni ujenzi wa barabara ya kutua na kuruka ndege na kiungio chake, maegesho ya ndege, jengo la abiria, jengo la kuongozea ndege, jengo la uchunguzi wa hali ya hewa, barabara ya kuingia kiwanjani na maegesho ya magari. Kazi nyingine ni usimikaji wa taa na mitambo ya kuongozea ndege na ujenzi wa uzio wa usalama.

**Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Shinyanga**

466. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi milioni 5,262.19** zinazojumuisha **Shilingi milioni 726.00** fedha za ndani na **Shilingi milioni 4,536.19** fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu. Kazi zitakazotekelezwa ni kuendelea na ujenzi wa barabara ya kutua na kuruka ndege na kiungio chake, maegesho ya ndege, jengo la abiria, jengo la kuongozea ndege, jengo la uchunguzi wa hali ya hewa, barabara ya kuingia kiwanjani, maegesho ya magari na usimikaji wa taa. Aidha, kazi nyingine ni usimikaji wa mitambo ya kuongozea ndege pamoja na ujenzi wa uzio wa usalama.

**Uendelezaji wa Viwanja vya Ndege vya Mikoa**

467. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 24,250.87** zinazojumuisha **Shilingi milioni 22,480.80** ni fedha za ndani na **Shilingi milioni 1,770.07** ni fedha za nje. Fedha hizi zimetengwa kwa ajili ya kulipa madai ya Mkandarasi na Mshauri Elekezi waliotekeleza na kusimamia kazi za ujenzi wa barabara ya kuruka na kutua ndege, barabara za maungio, maegesho ya ndege, barabara ya kuingia na kutoka kiwanjani, Jengo la Watu Mashuhuri pamoja na ujenzi wa mfumo wa majisafi na majitaka katika kiwanja cha ndege cha Mkoa wa Geita. Kazi nyingine ni kuendelea na ujenzi wa viwanja vya ndege katika mikoa ya Iringa (Awamu ya I), Kilimanjaro (Moshi), Ruvuma (Songea) na Mara (Musoma); kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa Kiwanja kipya cha Simiyu, Kiwanja cha Lake

Manyara, Tanga na Lindi pamoja na ujenzi wa uzio wa usalama na barabara ya kufanyia ukaguzi kwenye viwanja hivi. Aidha, kazi nyingine ni kuendelea na ujenzi wa uzio wa usalama pamoja na barabara ya kufanyia ukaguzi kwenye kiwanja cha ndege cha Dodoma.

**Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Msalato**

468. ***Mheshimiwa Spika***, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 29,479.29** zinazojumuisha **Shilingi milioni 1,106.50** fedha za ndani na **Shilingi milioni 28,372.79** fedha za nje kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa kiwanja kipya cha ndege cha Kimataifa Msalato mkoani Dodoma.

**Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Bukoba**

469. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 10.00** kwa ajili ya kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa jengo la Watu Mashuhuri (VIP Lounge), jengo la kuongozea ndege pamoja na usimikaji wa taa za kuongozea ndege.

**Ujenzi wa Jengo la Tatu la Abiria Katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNIA)**

470. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 40.87** fedha za ndani kwa ajili ya kuunganisha umeme wa 33 KV kutoka Gongolamboto hadi Kipawa *substation* katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere.

**FEDHA ZA MFUKO WA BARABARA**

471. ***Mheshimiwa Spika,*** fedha za Mfuko wa Barabara zilizotengwa kwa ajili ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Ujenzi) katika mwaka wa fedha 2023/24 ni jumla ya **Shilingi 599,756,467,800.00.** Fedha hizi zitatumika kufanya kazi za matengenezo na ukarabati wa barabara kuu na za mikoa. Kati ya fedha hizo, TANROADS imetengewa **Shilingi 534,662,653,430.00** kwa ajili ya matengenezo ya barabara na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Ujenzi) imetengewa **Shilingi 59,406,961,492.00** kwa ajili

ya kazi za ukarabati wa barabara za mikoa, Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa barabara, ukarabati na ununuzi wa vivuko, usalama barabarani pamoja na usimamizi na ufuatiliaji wa miradi hiyo. Aidha, **Shilingi 8,124,075,540.00** zitatumika kugharamia uendeshaji wa Bodi ya Mfuko wa Barabara.

472. ***Mheshimiwa Spika,*** mgawanyo wa **Shilingi 59,406,961,492.00** zilizotengwa kwa ajili ya Wizara (Ujenzi) ni kama ifuatavyo:

**Shilingi 15,820,073,000.00,** ni kwa ajili ya kufanya Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa barabara zenye urefu wa kilometa **7,177.91** na **Shilingi 30,731,221,000.00** zimetengwa kwa ajili ya miradi ya barabara za mikoa itakayohusisha ukarabati wa jumla ya kilometa **399.23** kwa kiwango cha changarawe, ujenzi wa kilometa **44.49** kwa kiwango cha lami pamoja na ujenzi na ukarabati wa madaraja/makalavati **44** katika mikoa mbalimbali nchini. Aidha, **Shilingi 4,467,403,504.00** ni kwa ajili ya manunuzi na ukarabati wa vivuko pamoja na ujenzi wa maegesho na miundombinu ya vivuko; **Shilingi 3,920,860,484.00** ni kwa ajili ya miradi ya usalama Barabarani na Mazingira na **Shilingi 4,467,403,504.00** ni kwa ajili ya kazi za usimamizi na ufuatiliaji wa miradi inayotekelezwa na Wizara (Ujenzi) pamoja na kujenga uwezo wa watumishi.

*Mchanganuo wa miradi itakayotekelezwa kwa fedha za Mfuko wa Barabara zilizotengwa kwa ajili ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Ujenzi) umeoneshwa katika* ***Viambatisho Na. 3*** *na* ***4.***

473. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi 534,662,653,430.00** fedha za Mfuko wa Barabara ambazo zimetengwa kwa ajili ya Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) zitatumika kufanya matengenezo ya barabara kuu, barabara za mikoa, madaraja na uendeshaji wa mizani.

*Mchanganuo wa matumizi ya fedha hizo umeoneshwa katika* ***Viambatisho Na. 5, 5A - 5D.***

## USHIRIKISHWAJI WA WANAWAKE KATIKA KAZI ZA BARABARA

474. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara (Ujenzi) ina lengo la kuongeza ushiriki wa wanawake katika kazi za barabara ili kuongeza uwiano wa ushiriki baina ya wanaume na wanawake katika sekta ya ujenzi. Katika mwaka wa fedha 2023/24. Wizara imepanga kuendelea kutoa mafunzo kwa wanawake na vikundi vya wanawake juu ya kufanya matengenezo na ukarabati wa barabara, kwa kutumia teknolojia ya nguvu kazi; kuwasaidia kusajili kampuni zao za ujenzi; kutoa mafunzo kwa Makandarasi wanawake ya namna ya kuomba zabuni na kujaza zabuni kwa ufanisi; pamoja na kufuatilia kwa karibu kazi za barabara zinazofanywa na wanawake Makandarasi.

Wizara pia itaendelea kutembelea shule za sekondari ili kuhamasisha wasichana kusoma masomo ya Sayansi na Hisabati pamoja na kuelimisha Umma juu ya ushirikishwaji wa wanawake katika kazi za barabara. Vilevile, Wizara (Ujenzi) imepanga kuendelea kutembelea Vyuo vya Elimu ya Juu ili kutoa ushauri (Mentorship and Coaching) kwa wasichana wanaosoma fani za sayansi zinazohusiana na Sekta ya Ujenzi.

## KUWAJENGEA UWEZO MAKANDARASI WA NDANI NA WANAWAKE

475. ***Mheshimiwa Spika*** Ili kuwajengea uwezo ***Makandarasi*** Wanawake, Serikali imetenga jumla ya kilometa 20 za barabara kwa ajili ya kuwashindanisha Makandarasi wanawake peke yao. Kazi hizi zimegawanywa katika sehemu za kilometa tano tano.

Vilevile, Serikali imetenga miradi mikubwa minne ya ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami kwa ajili ya kuwajengea uwezo Makandarasi wa ndani. Zabuni za kazi zimetangazwa na zitakuwa ni kwa ajili ya Makandarasi wa ndani tu kushindanishwa.

## MATUMIZI YA TEKNOLOJIA MPYA (NEW TECHNOLOGY) KATIKA UJENZI NA MATENGENEZO YA BARABARA

476. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara (Ujenzi) itaendelea na majaribio ya teknolojia mbalimbali ili kubaini teknolojia yenye ufanisi na kusaidia kwenye ujenzi na matengenezo ya barabara na

kuzifanya zidumu kwa muda mrefu bila kuhitaji matengenezo. Lengo ni kukabiliana na changamoto za barabara hasa za changarawe na udongo kuharibika na kusababisha kuhitaji matengenezo ya mara kwa mara. Teknolojia mojawapo ni ya matumizi ya *Water – Based RESIN Primer* ambayo tayari imetumika hapa nchini kwa upande wa Tanzania Visiwani (Zanzibar). Aidha, Wizara (Ujenzi) kwa kushirikiana na TAMISEMI inaendelea kufuatilia ufanisi wa Teknolojia hii ili iweze kutumika.

**USIMAMIZI WA ENEO LA HIFADHI YA BARABARA LILILOONGEZWA UPANA WA MITA SABA NA NUSU (M 7.5)**

477. ***Mheshimiwa Spika,*** Sheria ya Barabara Na. 13 ya Mwaka 2007 na Kanuni zake za mwaka 2009 iliongeza upana wa eneo la hifadhi ya Barabara Kuu na za Mikoa kutoka mita 45 hadi 60 ikiwa na nyongeza ya mita 7.5 kutoka katikati ya barabara kila upande. Kufuatia utekelezaji wa Sheria hii, alama ya "X" yenye rangi ya kijani iliwekwa kwenye nyumba zote za wananchi zilizo katika eneo hili ikiwa na maana kuwa wananchi hao waendelee kuwepo katika eneo hilo ila wasifanye maendelezo mapya. Hii imesababisha malalamiko mengi kutolewa na wananchi walio kwenye eneo hili la nyongeza ya mita 7.5 ikiwa ni pamoja na kudai walipwe fidia. Kwa kuwa hakuna uwezekano wa Serikali kuyahitaji maeneo hayo yote hivi karibuni, Serikali inaangalia upya nyongeza hii ya upana wa eneo la hifadhi ya barabara kwa nchi nzima na itaandaa mapendekezo ya maeneo gani yabakie na nyongeza hii ya upana wa barabara na maeneo gani wananchi waruhusiwe kuendelea na shughuli zao.

**MPANGO WA KAZI ZA TAASISI ZILIZO CHINI YA SEKTA YA UJENZI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/24**

**Wakala wa Barabara Tanzania**

478. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2023/24, Wakala wa Barabara Tanzania umepanga kujenga barabara kuu zenye urefu wa **kilometa 350** kwa kiwango cha lami, ukarabati wa **kilometa 25** kwa kiwango cha lami, ujenzi wa **madaraja 13,** ukarabati wa **daraja 1,** kufanya maandalizi mbalimbali ya ujenzi wa **madaraja 11** na kufanya Upembuzi

Yakinifu na Usanifu wa Kina wa **daraja 1** katika barabara kuu na baadhi ya barabara za Mikoa. Kati ya **kilometa 350** zilizopangwa kujengwa kwa kiwango cha lami **kilometa 282** ni za Miradi inayoendelea na **kilometa 68** ni za Miradi mipya.

479. ***Mheshimiwa Spika,*** miradi ya barabara za mikoa iliyopangwa kutekelezwa na Wakala ni ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara zenye urefu wa **kilometa 84.** Kati ya hizo, **kilometa 50** zitajengwa kwa kutumia fedha za Mfuko Mkuu wa Serikali na **kilometa 34** zitajengwa kwa fedha za Mfuko wa Barabara. Vile vile, Wakala umepanga kufanya ukarabati kwa kiwango cha changarawe wa barabara zenye urefu wa **kilometa 844**. Kati ya hizo, **kilometa 545** zitakarabatiwa kwa kutumia fedha za Mfuko Mkuu wa Serikali na **kilometa 299** zitakarabatiwa kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara. Aidha, fedha hizi zitatumika kujenga na kufanya ukarabati wa madaraja/makalavati **103** ambapo kati ya hayo madaraja/makalavati **59** yatatumia fedha za Mfuko Mkuu wa Serikali na **44** yatatumia fedha za Mfuko wa Barabara.

Kazi nyingine ni kufanya matengenezo ya barabara kuu na barabara za mikoa ambayo yatahusisha matengenezo ya kawaida (routine and recurrent maintenance) kwa **kilometa 34,383.67,** matengenezo ya muda maalum **kilometa 3,598.59,** matengenezo ya sehemu korofi **kilometa 402.65** pamoja na matengenezo ya madaraja **3,129**. Mpango huu pia unajumuisha shughuli za udhibiti wa uzito wa magari na hifadhi za barabara, kazi za dharura pamoja na mradi wa matengenezo ya barabara kwa mikataba ya muda mrefu.

480. ***Mheshimiwa Spika,*** Wakala vilevile umelenga kuendelea na majukumu ya kusimamia miradi ya ujenzi na ukarabati wa Viwanja vya Ndege. Miradi iliyopangwa kutekelezwa imeainishwa katika **Aya 457 – 470.**

**Wakala wa Majengo Tanzania**

481. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2023/24 Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) utaendelea kutekeleza majukumu yake kwa kutumia fedha za Ruzuku ya Serikali pamoja

na mapato ya ndani ya Wakala. Kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na kutoa huduma za ushauri kwa miradi ya ujenzi wa majengo ya Serikali, kujenga majengo ya Washitiri mbalimbali; kuuza nyumba zinazojengwa na TBA kwa Watumishi wa Umma; kupangisha nyumba za Serikali kwa Watumishi wa Umma na kupangisha baadhi ya majengo ya Serikali kwa wasio watumishi wa Umma ili kuongeza uwezo wa Wakala kujiendesha.

482. ***Mheshimiwa Spika,*** miradi iliyopangwa kutekelezwa kwa kutumia ***fedha za ruzuku*** imeoneshwa katika **Aya 332- 338**.

483. ***Mheshimiwa Spika,*** miradi itakayotekelezwa kwa kutumia ***mapato ya ndani ya Wakala*** ni ujenzi wa nyumba 72 za watumishi wa Umma mikoani; upatikanaji wa Hati Miliki za viwanja vya TBA; ununuzi wa samani katika jengo la Chimala jijini Dar es Salaam; ujenzi wa jengo la Ofisi za TBA Geita na TBA Makao Makuu Dodoma; ujenzi wa jengo la ghorofa kwa Watumishi wa Umma eneo la Canadian Village Dar es Salaam na ujenzi wa jengo la ghorofa la Watumishi wa Umma eneo la Misheni Kota Geita, Ghana Kota (Block I) jijini Mwanza na Kaloleni Kota (Block I) Jijini Arusha.

484. ***Mheshimiwa Spika,*** miradi mingine ni ukarabati wa karakana 2 katika Mikoa ya Ruvuma na Rukwa; ukarabati wa majengo ya ofisi 20 za TBA mikoani; ukarabati wa majengo 50 katika maeneo mbalimbali nchini; kuanza ujenzi wa maabara ya upimaji/majaribio ya malighafi za ujenzi Jijini Dodoma pamoja na ununuzi wa mitambo saba (7) ya ujenzi.

485. ***Mheshimiwa Spika,*** Wakala pia umepanga kutekeleza miradi **193** ya ***Washitiri***. Mchanganuo wa miradi hiyo ni kama ifuatavyo:

486. ***Mheshimiwa Spika,*** miradi **28** ni ya Sanifu Jenga (Design and Build) ambapo hadi sasa miradi 18 inaendelea kutekelezwa. Miradi inayoendelea inajumuisha ujenzi wa Ofisi ya Halmashauri ya Mji wa Bariadi (Simiyu); Ofisi ya Utawala ya Halmashauri ya Wilaya ya Butiama (Mara); Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya ya Chunya (Mbeya) Awamu ya II; Ofisi ya Tume ya Maadili Dodoma na Ofisi ya Wakala wa Misitu (TFS) Dodoma.

487. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Wakala utaendelea kutekeleza miradi mbalimbali katika ***Mji wa Serikali*** eneo la Mtumba Dodoma ikiwemo ujenzi wa Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Aidha, Wakala utatekeleza miradi **15** ya Ushauri Elekezi ya ujenzi wa majengo ya Ofisi za Wizara na Taasisi za Serikali.

488. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Wakala umepanga kutekeleza miradi **108** ya ***Ushauri (Consultancy***) ambapo kati ya hiyo miradi 76 inaendelea. Miradi inayoendelea ni pamoja na ujenzi wa Hosteli za Wanafunzi katika Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere Kampasi ya Karume Zanzibar; Ukumbi wa Mafunzo wa ADEM eneo la Iwambi Mbeya Mjini; Ofisi za Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma Dodoma; Ofisi za Mkuu wa Mkoa wa Morogoro na Ofisi za Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Dodoma.

489. ***Mheshimiwa Spika,*** Wakala pia umepanga kutekeleza miradi **38** ya ***Ujenzi*** ambapo miradi **17** inaendelea. Miradi ya ujenzi inayoendelea ni pamoja na ujenzi wa Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya ya Ngorongoro iliyopo Wasso Loliondo Arusha; Jengo la Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mtumba, Dodoma na Jengo la Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Mkunwa Mtwara.

490. ***Mheshimiwa Spika,*** Wakala pia umepanga kutekeleza miradi minne **(4)** ya ***Usimamizi (Project Management)*** ambapo kati ya hiyo miradi mitatu (3) inaendelea. Miradi inayoendelea ni Usimamizi na Uendeshaji wa Jengo la Ukumbi wa Bunge; ujenzi wa Kituo cha Pamoja cha Forodha Mpakani cha Kasumulu (One stop Border Post) Awamu ya II na ujenzi wa kituo cha mawasiliano *Kalambo falls* mkoani Rukwa awamu ya III.

**Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania**

491. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2023/24, Wakala umepanga kuendelea na usimamizi na uendeshaji wa vivuko vya Serikali, kutoa huduma ya ukodishaji wa magari na mitambo ya ujenzi wa barabara pamoja na kufanya

matengenezo ya magari, usimikaji wa mifumo ya umeme, majokofu, viyoyozi na elektroniki.

492. ***Mheshimiwa Spika,*** miradi ya Ruzuku itakayotekelezwa na Wakala katika mwaka wa fedha 2023/24 inayohusisha ***maegesho ya vivuko, Ukarabati wa Vivuko, Ujenzi wa Vivuko Vipya*** na ***Ujenzi na Ukarabati wa Karakana*** ni kama inavyoonekana kwenye **Aya 328 – 331** na **Aya 339 340**.

493. ***Mheshimiwa Spika,*** Aidha, Wakala umepanga kuendelea na usimamizi na uendeshaji wa vivuko vya Serikali vipatavyo **33** ambavyo vinatarajiwa kutoa huduma kwa abiria **42,618,348** magari **1,542,691** na tani za mizigo **557,220** kwa mwaka. Wakala umepanga kufanya matengenezo ya magari **31,581**, matengenezo na usimikaji wa mifumo **267** ya umeme, **665** ya majokofu na viyoyozi na mifumo **23** ya elektroniki. Vilevile, Wakala umepanga kutoa ushauri wa kihandisi kwa miradi ya usimikaji wa mifumo **90** ya umeme, mitambo, elektroniki, viyoyozi na majokofu na kusimamia mifumo hiyo inayofikia **50.** Wakala pia utaendelea kutoa huduma ya ukodishaji wa mitambo ya magari na mitambo ya ujenzi wa barabara.

494. ***Mheshimiwa Spika,*** miradi itakayotekelezwa kwa kutumia mapato ya ndani ya Wakala ni ununuzi wa vipuri kwa ajili ya matengenezo kinga na ukarabati wa vivuko, ununuzi wa magari mawili (02) kwa ajili ya usimamizi wa miradi ya maendeleo pamoja na kukamilisha ujenzi wa Jengo la Makao Makuu ya Wakala eneo la NCC – Tambukareli, Dodoma.

**Bodi ya Mfuko wa Barabara**

495. ***Mheshimiwa Spika,*** Mfuko wa Barabara unatarajia kukusanya jumla ya **Shilingi 856,794,954,000** katika mwaka wa fedha 2023/24 kwa ajili ya kugharamia matengenezo ya barabara nchini. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 599,756,467,800** ni kwa ajili ya matengenezo ya barabara za Kitaifa (Barabara Kuu na Barabara za Mikoa) ambazo husimamiwa na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Fungu 98). Aidha, **Shilingi 257,038,486,200** ni kwa ajili ya kugharamia barabara za Wilaya ambazo husimamiwa na Ofisi ya Rais –TAMISEMI (Fungu 56).

Mgawanyo wa fedha za Mfuko wa Barabara kwa kila taasisi ni kama ifuatavyo: Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Ujenzi) **Shilingi 59,406,961,492.00**; TANROADS **Shilingi 534,662,653,430.00**; Ofisi ya Rais – TAMISEMI **Shilingi 25,460,126,354.00;** TARURA **Shilingi 229,141,137,184.00;** na Bodi ya Mfuko wa Barabara **Shilingi 8,124,075,540.00.**

496. ***Mheshimiwa Spika,*** kazi nyingine zitakazotekelezwa na Bodi ni pamoja na kuendelea kufuatilia matumizi ya fedha zinazopelekwa kwa wakala za barabara (TANROADS na TARURA) ili kuhakikisha kuwa zinatumika kwa madhumuni yaliyowekwa. Aidha, Bodi itaendelea kufanya kaguzi za ubora wa kazi za barabara katika mikoa yote nchini ili kuhakikisha kuwa miradi inayotekelezwa inakidhi thamani ya fedha zilizotumika (value for money).

Ili kukabiliana na changamoto ya uhaba wa fedha za matengenezo ya barabara. Bodi kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imepanga kuendelea kufanya utafiti katika maeneo mbalimbali ili kupata vyanzo vipya vya mapato na teknolojia ya gharama nafuu ya matengenezo ya barabara, kufanya mazungumzo na Wadau wa Maendeleo ili kuwashawishi kutoa msaada wa kifedha na kitaalam ili kujenga uwezo wa Mfuko na kufanya tathmini ya mtandao wa barabara (Road inventory and condition survey). Takwimu hizi zitasaidia kuandaa mkakati endelevu wa matengenezo ya barabara.

497. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Bodi imepanga kuoanisha (intergration) mifumo ya usimamizi wa matengenezo ya barabara, ili kurahisisha upatikanaji wa taarifa za mpango kazi na utekelezaji wake na kupunguza gharama za uendeshaji wa mifumo mingi. kuelimisha watumiaji wa barabara na wananchi kwa ujumla juu ya umuhimu wa kutunza na kulinda miundombinu ya barabara katika maeneo yao; kuendelea na ukaguzi wa ubora wa kazi za matengenezo ya barabara katika mikoa yote nchini na kuhakikisha mipango ya matengenezo ya barabara inazingatia mabadiliko ya tabia nchi ili kupunguza kiwango na athari za mabadiliko hayo katika kazi za barabara.

**Bodi ya Usajili wa Wahandisi**

498. ***Mheshimiwa Spika,*** malengo ya Bodi ya Usajili wa Wahandisi (ERB) katika mwaka wa fedha 2023/24 ni kusajili Wahandisi **3,200**, Mafundi Sanifu **400** na Kampuni za Ushauri wa Kihandisi **08.** Vilevile, Bodi imepanga kusimamia utekelezaji wa mpango wa mafunzo kwa vitendo kwa Wahandisi Wahitimu **3,692** ambapo Wahandisi Wahitimu watakaokuwa wanaendelea na mafunzo ni **2,492** na **1,200** ni wapya.

499. ***Mheshimiwa Spika,*** Bodi vilevile itaendelea kutembelea na kukagua miradi yote ya ujenzi ya kimkakati pamoja na barabara za Halmashauri, kusimamia mafunzo ya kujiendeleza kitaaluma kwa wahandisi watalaam na washauri na kuwashawishi wahandisi wataalam ili waanzishe kampuni za ushauri wa kihandisi mikoani ili kusogeza huduma hii muhimu karibu na watumiaji. Vilevile, Bodi itaendelea kufanya kaguzi za shughuli za kihandisi nchini ili kuhakikisha kuwa shughuli zote za kihandisi zinafanywa na wahandisi waliosajiliwa na kwa kufuata maadili ya utendaji kazi za kihandisi.

**Bodi ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi**

500. ***Mheshimiwa Spika,*** Bodi ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi imepanga kusajili Wataalamu **156** katika fani za Ubunifu Majengo, Ukadiriaji Majenzi, Ubunifu wa Ndani ya Majengo, Ubunifu wa Mandhari ya Nje ya Majengo, Usanifu Teknolojia ya Majengo, Utathmini Majengo, Usimamizi Ujenzi na Usimamizi wa Miradi. Aidha, Bodi imepanga kusajili kampuni **24** za Ubunifu Majengo na Ukadiriaji Majenzi. Bodi vilevile imepanga kufanya ukaguzi wa miradi ya ujenzi **3,744** katika mikoa yote 26 ya Tanzania Bara pamoja na kusajili miradi ya ujenzi **1,400**.

501. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza programu za kujengea uwezo wataalam wa fani za Ubunifu Majengo, Ukadiriaji Majenzi, Ubunifu wa Ndani ya Majengo, Ubunifu wa Mandhari ya Nje ya Majengo, Usanifu Teknolojia ya Majengo, Utathmini Majengo, Usimamizi Ujenzi na Usimamizi Miradi. Vilevile, Bodi imepanga kuwajengea uwezo wahitimu **180** wa fani hizo kupitia mpango maalumu wa Mafunzo kwa Vitendo (Enhanced Articled Pupilage

Programme - EAPP). Aidha, Bodi imepanga kuendesha mitihani ya kitaalamu kwa wahitimu **272** katika fani za Ubunifu majengo na Ukadiriaji majenzi. Bodi pia imepanga kufanya mikutano **5** na wanafunzi wa Shule za Msingi na Sekondari pamoja na kuendesha mashindano ya insha kwa lengo la kuhamasisha wanafunzi hao kusoma masomo ya sayansi na hatimaye kusomea taaluma za Ubunifu Majengo, Ukadiriaji Majenzi na taaluma nyingine zinazoshabihiana nazo.

**Bodi ya Usajili wa Makandarasi**

502. ***Mheshimiwa Spika,*** Bodi imepanga kusajili jumla ya Makandarasi wapya **1,200** na kukagua jumla ya miradi ya ujenzi **3,200.** Aidha, Bodi inatarajia kuendesha kozi sita (**6)** za mafunzo katika vituo vitano **(5)** katika mikoa ya Dodoma, Dar es Salaam, Mwanza, Arusha na Iringa. Pia Bodi imepanga kuendesha warsha moja **(1)** ya mafunzo ya ushirikiano wa ubia (Joint Venture) katika mkoa wa Mtwara.

Bodi pia itaendeleza Mfuko maalum wa kutoa dhamana ya kusaidia Makandarasi wa ndani (Contractor's Assistance Fund – CAF) pamoja na kuendelea na jitihada za kuhamasisha Makandarasi wazalendo kujiunga ili kuomba zabuni kwa mfumo wa ubia.

**Baraza la Taifa la Ujenzi**

503. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2023/24 Baraza limepanga kutekeleza kazi mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuendelea kufuatilia utekelezaji wa Sera ya Ujenzi nchini; kuandaa na kutekeleza Mpango Mkakati wa Maendeleo wa Sekta ya Ujenzi na kuandaa jukwaa la Sekta ya Ujenzi na Wiki ya Huduma za Ujenzi. Baraza vilevile litaendelea na kazi ya kutunga Sheria ya Majengo (Building Act), Taratibu za Majengo (Building Codes) na viwango msawazo vya ujenzi wa majengo ya Serikali. Baraza pia litaendelea kutoa ushauri wa kiufundi na kitaalam kwa wadau wa sekta ya ujenzi; kuchapisha taarifa ya utendaji wa Sekta ya Ujenzi; kuratibu utatuzi wa migogoro inayotokea katika miradi ya ujenzi pamoja na kufanya utafiti katika maeneo mbalimbali kwa ajili ya kuimarisha Sekta ya Ujenzi nchini.

504. ***Mheshimiwa Spika,*** kazi nyingine ni kutoa huduma za ukaguzi wa kiufundi katika miradi ya ujenzi kwa wadau wa Sekta ya Ujenzi na kutoa mafunzo ya kujenga uwezo wa wadau wa Sekta ya Ujenzi nchini. Aidha, kazi nyingine ni kukusanya na kuchapisha takwimu, kuandaa miongozo na taarifa za Sekta ya Ujenzi, kutoa huduma za ushauri wa kiufundi kwa wadau wa Sekta ya Ujenzi, na kuanzisha kituo cha Taarifa za Sekta ya Ujenzi ambacho kitakuwa muhimu kwa wadau kupata taarifa muhimu za Sekta ya Ujenzi ikiwa ni pamoja na kuendeleza tafiti, teknolojia na ubunifu. Pia, Baraza pamoja na kuanzisha mfumo wa kuboresha utendaji kazi wa mafundi stadi (skilled labourers) katika Sekta ya Ujenzi.

**Kituo cha Usambazaji wa Teknolojia Katika Sekta ya Ujenzi na Usafirishaji Tanzania (Tanzania Transportation Technology Transfer Centre)**

505. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2023/24, Kituo kimepanga kuendelea kusambaza teknolojia katika Sekta ya Ujenzi na Uchukuzi hapa nchini pamoja na majarida kutoka kwa wadau mbalimbali. Aidha, kituo kitaendelea kuandaa, kuchapisha na kusambaza majarida yake yanayoandaliwa mara nne (4) kwa mwaka yanayohusu teknolojia, maarifa na taarifa mbalimbali muhimu katika Sekta za Ujenzi na Uchukuzi.

506. ***Mheshimiwa Spika,*** kazi nyingine zilizopangwa ni kununua *software* mbalimbali kwa ajili ya kupanga, kusimamia na kuendeleza miundombinu ya barabara na kuendesha mafunzo ya namna ya kuzitumia; kuendesha makongamano ya Watalaam wa taasisi mbalimbali zinazohusika na miundombinu na usafirishaji ili kujadili na kutafuta majibu ya changamoto mbalimbali zinazoikabili Sekta za Ujenzi na Uchukuzi pamoja na kushiriki katika kuandaa na kufanyika kwa Mkutano wa Vituo vya usambazaji wa Teknolojia Afrika (yaani 10th T2 Centre Conference) unaofanyika kila mwaka.

## C.2 SEKTA YA UCHUKUZI

### Makadirio ya Bajeti ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo

507. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2023/24, Sekta ya Uchukuzi (Fungu 62) imetengewa jumla ya **Shilingi 2,086,545,508,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 118,215,599,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 1,968,329,909,000** kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Mgawanyo wa fedha za maendeleo pamoja na miradi iliyotengewa fedha ni kama inavyooneshwa katika **Kiambatisho Na. 6.** Fedha za Matumizi ya Kawaida zinajumuisha **Shilingi 89,291,108,000** kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi na **Shilingi 28,924,491,000** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Katika Fedha za Miradi ya Maendeleo zilizotengwa, **Shilingi 1,861,064,800,000** ni fedha za ndani na **Shilingi 107,265,109,000** ni fedha za nje.

### Udhibiti wa Usafiri Ardhini

508. ***Mheshimiwa Spika,*** Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) imetenga **Shilingi bilioni 40.1** kutoka katika vyanzo vyake vya ndani katika mwaka wa fedha 2023/24, ili kudhibiti huduma za usafiri ardhini katika sekta ndogo za reli, barabara na waya. Fedha hizo zitatumika kutekeleza kazi zifuatazo:

i. Kuimarisha usalama wa huduma za usafiri wa umma kwa kuendelea na mkakati wa kuanzisha vituo vya ukaguzi wa magari Tanzania Bara;

ii. Kuboresha mfumo wa kufuatilia mwenendo wa mabasi na treni (VTS) na kuwezesha kudhibiti mwendo kasi (speed governors) kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi, Kikosi cha Usalama Barabarani ili kupunguza na kuzuia ajali za barabarani na kwenye reli;

iii. Kufanya maboresho ya Mfumo wa huduma za udhibiti usafiri ardhini (Road and Railway Information Management

System – RRIMS) pamoja na kuboresha Mfumo wa kuwathibitisha madereva na kusajili wahudumu wa mabasi na treni kwa lengo la kuboresha usalama katika usafiri ardhini;

iv. Kufanya maboresho katika Mfumo wa tiketi za kielektroniki (e-ticketing system) ili kuwawezesha abiria kuchagua usafiri wanaoutaka na kukata tiketi mahali popote bila kufika vituoni. Kupitia Mfumo huu wananchi wataweza kupata taarifa za safari za mabasi yanayokwenda mikoani kwa wakati (realtime) pamoja na kuwezesha kufanyika ukaguzi kwa kutumia TEHAMA;

v. Kuimarisha ushindani katika utoaji wa huduma za usafiri ardhini kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Taratibu ili kuleta tija kwa watoa huduma na watumiaji wa huduma hizo;

vi. Kuandaa Kanuni za Udhibiti Usafiri wa Waya ili kuchochea ukuaji wa shughuli za utalii nchini; na

vii. Kufanya mapitio ya Kanuni za udhibiti wa huduma za usafiri ardhini hususan za pikipiki za magurudumu mawili na magurudumu matatu ili kuwezesha udhibiti binafsi (self-regulation) wa watoa huduma wake kupitia vyama vyao vilivyosajiliwa na kuwawezesha kwa kuwarejeshea sehemu ya ada ya leseni wanayolipa ili kuimarisha vyama vyao na kuwakwamua kiuchumi.

**Usafiri kwa Njia ya Reli**

509. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2023/24 jumla ya **Shilingi trilioni 1.113** kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali zinatarajiwa kutumika kugharamia ujenzi wa Reli ya Kisasa (*Standard Gauge Railway – SGR)*, ununuzi wa injini na mabehewa ya mizigo na abiria na upembuzi yakinifu kwa ajili ya miradi ya reli. Kazi zitakazotelekezwa ni pamoja na:-

i. Kukamilisha ujenzi wa reli ya SGR kwa kipande cha Dar es Salaam - Morogoro (km 300) na Morogoro - Makutupora (km 422);

ii. Kuendelea na ujenzi wa njia ya reli ya SGR kwa kipande cha Mwanza – Isaka (km 341); Makutupora – Tabora (km 368); Tabora – Isaka (km 165); na Tabora – Kigoma (km 506);

iii. Kuendelea na ujenzi wa reli ya Uvinza – Musongati-Gitega (km 282) na taratibu za upatikanaji wa fedha za ujenzi wa reli ya SGR kwa sehemu za Kaliua – Mpanda - Karema (km 321) na Isaka - Rusumo (km 371);

iv. Kuendelea na ununuzi wa injini, mabehewa na mitambo kwa ajili ya matengenezo ya njia ya reli ya SGR;

v. Kugharamia uendeshaji wa reli ya SGR;

vi. Kuendelea kuwezesha mafunzo ya wataalamu wa uendeshaji na usimamizi wa treni ya SGR;

vii. Ulipaji wa fidia kwa wananchi wanaopisha ujenzi wa reli;

viii. Kuendelea na uratibu wa utekelezaji wa shughuli za utunzaji wa mazingira na jamii katika utekelezaji wa ujenzi wa reli ya SGR; na

ix. Kuendelea na taratibu za kutafuta mwekezaji kwa ubia baina ya Sekta ya Umma na Binafsi (PPP) kwa mradi wa reli ya Mtwara – Mbambabay na matawi yake ya Liganga na Mchuchuma na Tanga – Arusha – Musoma.

509. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha wa 2023/24, Mfuko wa Reli *(Railway Infrastructure Fund)* ambao unasimamiwa na Shirika la Reli Tanzania (TRC) unatarajia kutumia jumla ya **Shilingi bilioni 294.80** fedha za ndani ili kugharamia ukarabati wa miundombinu ya reli iliyopo na kujenga reli ya SGR, ukarabati wa vitendea kazi na kugharamia maandalizi ya miradi ya ujenzi wa reli. Kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na:-

i. Ukarabati wa njia ya reli ya Kaliua-Mpanda (km 210), Tabora – Kigoma (km 411), na Tabora – Isaka – Mwanza (km 385);

ii. Ujenzi wa njia ya reli ya Kilometa 6.2 na daraja kati ya Godegode – Gulwe (km 345 – Km 355);

iii. Matengenezo ya njia ya reli ya Tanga - Arusha (Km 470) na Kilosa – Gulwe (km 100);

iv. Ufufuaji wa njia za reli zilizofungwa za KilosaKidatu (Km 108) na Manyoni-Singida (km 115); Ukarabati wa karakana, stesheni na majengo ya reli;

v. Ukarabati wa mfumo wa ishara na mawasiliano wa reli iliyopo;

vi. Ununuzi wa vipuri kwa ajili ya ukarabati wa mabehewa 600 ya mizigo na mabehewa 37 ya abiria;

vii. Ununuzi wa mabehewa 245 ya mizigo, mabehewa 22 ya abiria na injini 10 kwa ajili ya reli iliyopo;

viii. Upimaji na uwekaji alama katika maeneo ya reli nchi nzima;

ix. Ufufuaji wa Mgodi wa kuzalisha Kokoto wa Pangani (Tanga) na uboreshaji wa Mgodi wa Tura;

x. Ukarabati wa Mgodi wa unyooshaji wa mataruma ya reli (Pugu Sleeper Reconditioning Plant) uliopo Pugu – Dar es Salaam;

xi. Ulipaji wa madeni ya watoa huduma; na

xii. Uandaaji wa Mpango Kabambe wa Reli (Railway Master Plan).

511. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha wa 2023/24 Mradi wa Ukarabati wa Reli ya Kati iliyopo kutoka Dar es Salaam hadi Isaka (km 970) umetengewa jumla ya **Shilingi bilioni 11.72** fedha za nje. Kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na:-

i. Kuboresha vituo vya kuhudumia mizigo vya Ilala na Isaka;

ii. Kukamilisha ukarabati wa maeneo yaliyobaki katika eneo la Makutupora – Manyoni na Kitaraka – Malongwe – Igalula; na

iii. Kugharamia huduma za ushauri wa kitaalam katika utekelezaji wa miradi ya ukarabati wa miundombinu ya reli iliyopo inayogharamiwa kwa fedha za Benki ya Dunia.

512. ***Mheshimiwa Spika,*** Shirika la Reli Tanzania (TRC) katika mwaka 2023/24, linalenga kusafirisha tani za mizigo 525,000 na abiria wapatao 716,435 kwa upande wa masafa marefu, abiria 696,730 kwa treni ya kisasa toka Dar es Salaam hadi Morogoro na abiria kwa usafiri wa treni ya mjini (Dar es Salaam Commuter Train) ni 4,368,000.

513. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha wa 2023/24 TRC pia imepanga kutekeleza Mpango wa Miaka Mitano ambao unalenga yafuatayo:-

i. Kuendelea na utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa reli ya *Standard Gauge*, kuinua kiwango cha reli na madaraja yaliyopo kwa kutandika reli nzito zaidi za angalau ratili 80 kwa yadi na kukarabati madaraja kuweza kupitisha tani 18.5 kwa ekseli;

ii. Kushirikiana na vyombo vya dola pamoja na jamii inayozunguka miundombinu ya reli ili kuzuia uharibifu wa miundombinu ya reli;

iii. Kukabarati sehemu korofi za miundombinu ya reli na kununua vitendea kazi kwa awamu;

iv. Kuweka mifumo ya TEHAMA kwa ajili ya kuboresha utoaji wa huduma; na

v. Kuendeleza maeneo yanayomilikiwa na TRC ili kuongeza vyanzo vya mapato ya Shirika.

514. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha wa 2023/24 Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA) imetenga jumla ya **Shilingi bilioni 22.2** kutoka katika vyanzo vyake vya mapato ya ndani na **Shilingi bilioni 13.19** kutoka Mfuko Mkuu wa

Serikali kwa ajili ya kuboresha na kuimarisha miundombinu ya reli pamoja na maeneo yote yaliyo ndani ya ukanda wa reli (ndani ya mita 50). Fedha hizo zitatumika kutekeleza kazi zifuatazo: -

i. Kukamilisha ununuzi wa *Tamping Machine* moja (1) kwa ajili ya kunyoosha reli na kushindilia kokoto kwenye reli;

ii. Kukamilisha ununuzi *Excavator* mbili (2) kwa ajili ya matengenezo ya njia;

iii. Kununua mataruma 20,000 ya mbao kwa ajili ya kuwekwa katika maeneo ya madaraja na kwenye njia za kupishana;

iv. Kununua *scanner* na mzani katika stesheni ya TAZARA Tunduma kwa ajili ya mizigo inayoingia na kutoka kupitia mpaka wa Tunduma/Nakonde; na

v. Kufanya ujenzi wa njia mbili (2) za reli katika Stesheni ya Tunduma kwa ajili ya kufunga *scanner* na mzani na kufanya matengenezo kinga ya injini, mabehewa na miundombinu.

**Udhibiti wa Usafiri Majini**

515. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24 Shirika la Uwakala wa Meli (TASAC) limetengewa jumla ya **Shilingi bilioni 1.73** fedha za nje kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) na **Shilingi bilioni 70.905** zinazotokana na makusanyo yake ya ndani kwa ajili ya kutekeleza kazi zifuatazo: -

i. Uongezaji wa wigo wa upatikanaji wa mawasiliano kwenye Ziwa Victoria;

ii. Ujenzi wa Kituo cha kikanda cha kuratibu Utafutaji na Uokozi Ilemela, Mwanza (MRCC);

iii. Ujenzi wa vituo vitatu (3) vya Kitaifa vya Utafutaji na Uokozi;

iv. Ununuzi na ufungaji wa mfumo wa kuwezesha upatikanaji wa taarifa za hali ya hewa kwenye Ziwa Victoria;

v. Ununuzi wa Boti mbili (2) za Utafutaji na Uokozi pamoja na boti moja (1) ya matibabu;

vi. Kudhibiti gharama, nauli na tozo mbalimbali za usafiri majini kwa kuzingatia Sheria na Kanuni ili kuhakikisha tozo hizo zinaleta ushindani katika soko;

vii. Kufanya ukaguzi wa meli za nje zinazokuja katika bandari za Tanzania Bara na meli zilizosajiliwa nchini ili kuhakikisha vyombo hivyo vinazingatia viwango vya ubora;

viii. Kuimarisha mifumo ya TEHAMA kwa ajili ya utoaji wa Vyeti vya Mabaharia;

ix. Kuweka mifumo thabiti ya kukabiliana na uchafuzi wa mazingira majini utokanao na meli;

x. Kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Usalama wa Vyombo Majini (Merchant Shipping Act – 2003);

xi. Kusimamia utekelezaji wa Mikataba ya Kimataifa kuhusu Usafirishaji kwa njia ya Maji inayoratibiwa na Shirika la Bahari Duniani (International Maritime Organization-IMO);

xii. Uwakala wa ugomboaji na uondoshaji wa shehena zifuatazo: Silaha na vilipuzi; Makinikia; wanyama hai kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Wanyamapori; nyara za Serikali na Kemikali zinazotumiwa na kampuni za madini;

xiii. Kushirikisha wadau katika kufanya mapitio na marekebisho ya Sheria na Kanuni mbalimbali; na

xiv. Kuimarisha mifumo na kukuza matumizi ya TEHAMA katika kudhibiti huduma za usafiri kwa njia ya maji na ufanyaji biashara ya meli.

**Huduma za Usafiri Baharini**

516. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2023/24, Kampuni ya Ubia kati ya Tanzania na China (SINOTASHIP) imetenga **Shilingi**

**bilioni 6.00** ili kuendelea kutoa huduma ya usafirishaji wa mizigo katika masafa marefu kwa njia ya bahari, kusimamia usalama wa mabaharia, mizigo na meli pamoja na kutoa huduma ya uwakala wa meli. Kazi zitakazofanyika ni pamoja na:-

i. Kuendelea kutoa huduma ya usafirishaji wa mizigo kutoka tani 610,774 mwaka 2022 na kufikia tani 615,000 mwaka 2023;

ii. Kuendelea na jitihada za kuongeza mapato kwa kushawishi wamiliki wa meli kuongeza idadi ya meli na mizigo itakayoingia katika bandari nchini kutoka makasha 63,529 mwaka 2022 na kufikia makasha 65,000 mwaka 2023;

iii. Kupunguza gharama za uendeshaji kampuni kutoka **Shilingi bilioni 13.37** mwaka 2022/23 na kufikia **Shilingi bilioni 13.01** mwaka 2023/24; na

iv. Kushirikiana na taasisi za fedha nje na ndani ya nchi ili kufanikisha kupata mikopo itakayowezesha kununua meli moja (1) ya mizigo kutegemeana na hali ya soko.

**Huduma za Usafiri na Usafirishaji katika Maziwa Makuu**

517. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha wa 2023/24, Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) imetengewa jumla ya **Shilingi bilioni 100.00** fedha za ndani**.** Kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na:-

i. Kujenga meli mpya ya kubeba shehena ya mizigo yenye uwezo wa kubeba tani 3,500, na ujenzi wa meli mpya ya kubeba abiria 600 na tani 400 za mizigo katika Ziwa Tanganyika;

ii. Ujenzi wa *shipyard* kwa ajili ya ujenzi wa meli katika Ziwa Tanganyika;

iii. Kufanya Ukarabati mkubwa wa meli ya MV. Liemba katika Ziwa Tanganyika;

iv. Kufanya ukarabati mkubwa wa meli ya MT. Ukerewe; na MT. Nyangumi (tanker vessel) katika Ziwa Victoria;

v. Kufanya ukarabati wa boti moja (1) ya mwendokasi (Sea Warrios) kwa ajili ya kusaidia kazi za uokozi sambamba na usafirishaji wa watalii wanaotembelea Kisiwa cha Gombe yenye uwezo wa kubeba abiria 10 katika Ziwa Tanganyika;

vi. Ujenzi wa meli mpya ya mizigo (Wagon Ferry) yenye uwezo wa kubeba tani 3,000 za mabehewa ya mizigo katika Ziwa Victoria;

vii. Ujenzi wa meli mpya ya mafuta (tanker vessel) katika Ziwa Tanganyika;

viii. Kufanya ukaguzi wa kina (Comprehensive) kuhusu Meli ya MV. Mwongozo katika Ziwa Tanganyika;

ix. Kuendelea na ufungaji wa mifumo ya TEHAMA katika vituo vya Maziwa Makuu (Victoria, Tanganyika na Nyasa); na

x. Kufanya Upembuzi Yakinifu kuhusu biashara ya usafirishaji baharini ili kuwezesha ujenzi wa meli moja baharini.

**Huduma za Bandari**

518. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2023/2024, Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari (TPA) imetenga jumla ya **Shilingi bilioni 820.03** kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi bilioni 662.976** ni fedha kutoka katika vyanzo vya ndani ya TPA na **Shilingi bilioni 93.80** ni fedha za nje za mkopo kutoka Benki ya Dunia. Fedha hizo zimetengwa ili kutekeleza kazi zifuatazo: -

i. Kuboresha mtandao wa Reli (improvement of rail layout) ndani ya Bandari ya Dar es Salaam;

ii. Kuendelea kuongeza kina na upana wa lango la kuingilia meli na eneo la kugeuzia meli (deepening and widening of entrance channel and turning basin) hadi kufikia kina cha mita 15.5;

iii. Kuongeza kina na kuimarisha Gati Na. 8 – 11 hadi kufikia kina cha mita 14.5;

iv. Kuendelea na Upembuzi Yakinifu wa ujenzi wa Gati Na. 12 - 15;

v. Kuhudumia Shehena ya tani za uzito milioni 25.478, ikijumuisha tani za shehena ya makasha (TEUs) 1,000,300 zitakazo hudumiwa na vitengo vya TPA;

vi. Kuendelea na utekelezaji wa mradi wa Ujenzi wa Matanki ya kuhifadhia Mafuta katika Bandari ya Dar es Salaam na Tanga;

vii. Kuendelea na ujenzi na uendeshaji wa Bandari Kavu ya Kwala, Ruvu;

viii. Kuendelea na maboresho ya maeneo ya kuhudumia shehena katika Bandari ya Mtwara;

ix. Kuendelea na mradi wa awamu ya pili ya maboresho katika Bandari ya Tanga;

x. Kuendelea na ununuzi wa mitambo na vifaa mbalimbali kwa bandari zote;

xi. Kuanza utekelezaji wa mradi wa Bandari ya Mbegani – Bagamoyo;

xii. Kuanza ujenzi wa Bandari ya Kisiwa Mgao kwa ajili ya kuhudumia shehena ya mizigo michafu (dirty cargo);

xiii. Kuendelea kuimarisha mifumo ya TEHAMA; na

xiv. Kuendelea na ukamilishaji wa miradi ya uboreshaji wa Bandari katika Maziwa.

519. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara inaendelea na kukamilisha taratibu za kushirikisha Sekta Binafsi katika kuendeleza na kuendesha sekta ndogo ya bandari nchini. Mapendekezo hayo kwa sasa yamewasilishwa katika ngazi mbalimbali za maamuzi

ndani ya Serikali na hatua husika zikikamilika yatawasilishwa Bungeni kwa ajili ya kujadiliwa kwa kina kuhusu umuhimu wa suala hilo kwa manufaa mapana ya nchi. Lengo ni kuongeza tija katika utendaji wa bandari ili kuifanya ichangie zaidi katika ukuaji wa uchumi.

**Udhibiti wa Usafiri wa Anga**

520. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24, Mamlaka ya Usafiri wa Anga (TCAA) imetenga **Shilingi 90,282,850,366.17** kutoka katika vyanzo vyake ili kusimamia ubora wa huduma za usafiri wa anga kulingana na viwango vya kimataifa vilivyowekwa na Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Anga Duniani (The International Civil Aviation Organization – ICAO).

Aidha, katika mwaka 2023/24 Serikali imetenga **Shilingi bilioni 6.5** kwa ajili ya kuboresha huduma za kuongozea Ndege katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNIA) na ujenzi wa chuo cha kisasa cha usafiri wa anga (CATC) ambapo kazi zitakazofanyika ni pamoja na: -

i. Malipo ya ununuzi na ufungaji wa mitambo ya kuongozea ndege ya *Doppler Very High Frequency Omnidirectional Radio Range (DVOR), Distance Measuring Equipment (DME)* na *Instrument Landing Systems (ILS)*;

ii. Ujenzi wa Chuo cha Kisasa cha Usafiri wa Anga Tanzania (CATC); na

iii. Kuendelea na usimamizi na ufuatiliaji wa utekelezaji wa mradi.

521. ***Mheshimiwa Spika,*** TCAA inatoa leseni na kudhibiti utoaji wa huduma za usafiri wa anga; kuweka viwango katika utoaji wa huduma za usafiri wa anga na kusimamia, kukuza na kuendeleza shughuli za biashara ya usafiri wa anga ndani na nje ya nchi ili wananchi wapate huduma bora na nafuu zaidi. Katika kufikia malengo hayo, kazi zilizopangwa kufanyika katika mwaka wa fedha 2023/24 ni pamoja na:

i. Kuendelea na mradi wa kufunga mitambo ya kuongozea ndege kwa njia ya mawasiliano ya sauti (VHF AREA COVER Relay Systems) kati ya waongoza ndege na marubani;

ii. Kuendelea kutafuta rasilimali fedha kwa ajili ya Ujenzi wa Chuo cha Kisasa cha Usafiri wa Anga;

iii. Kuendelea kuboresha daftari la usajili wa ndege (Aircraft register);

iv. Kusimamia udhibiti wa usalama wa usafiri wa anga (Aviation Security) katika viwanja vya ndege, mashirika ya ndege pamoja na watoa huduma zinazoendana na usafiri wa anga;

v. Kushiriki katika mazungumzo na nchi nyingine duniani kwa ajili ya kuingia na kupitia upya mikataba ya usafiri wa anga;

vi. Kusimamia na kudhibiti ubora wa viwanja vya ndege nchini;

vii. Kuweka mikakati ya kudhibiti matukio na ajali zinazotokana na usafiri wa anga;

viii. Kuendelea na juhudi za kutafuta fedha ili kuweza kufadhili wanafunzi wengi zaidi kwenye mafunzo ya urubani na uhandisi wa ndege;

ix. Kushiriki kikamilifu katika masuala mbalimbali ya Jumuiya za Kimataifa zinazohusu usafiri wa anga;

x. Kuimarisha uwezo wa Tanzania katika kusimamia sekta na kudhibiti usalama wa anga; na

xi. Kuboresha miundombinu na vifaa vya kuongozea ndege.

**Huduma za Viwanja vya Ndege**

522. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2023/2024, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (TAA) imetengewa **Shilingi**

**bilioni 46.30** fedha za ndani kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali ili kutekeleza kazi zifuatazo:

i. Kugharamia uendeshaji na uwekaji wa miundombinu katika jengo la tatu la abiria (JNIA TB III) unaohusisha matengenezo (preventive maintanance) ya mitambo na mifumo mbalimbali (switch gears 33 kV, lift 14, escallators saba (7), travelators mbili (2) za abiria, mashine 20 za ukaguzi wa abiria na mizigo, mifumo ya tiketi za abiria na mifumo ya TEHAMA;

ii. Kuweka mfumo wa taa za kuongozea ndege katika Kiwanja cha Ndege cha Arusha;

iii. Kuendelea na ujenzi wa jengo la abiria katika Kiwanja cha Ndege cha Mwanza na kuanza ujenzi wa jengo la abiria katika kiwanja cha ndege cha Mtwara;

iv. Ujenzi wa Jengo la kuongozea Ndege katika Kiwanja cha Ndege cha Bukoba; na ununuzi wa gari moja (1) la zimamoto kwa Kiwanja cha Ndege cha Arusha; na

v. Kuanza ukarabati wa Jengo la Pili la Abiria (TB II) katika Kiwanja cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNIA).

523. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya **Shilingi bilioni 33.5** zinazotokana na mapato ya ndani ya TAA zimetengwa ili kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwemo:-

i. Ununuzi wa mashine za kisasa za ukaguzi wa abiria na mizigo kwa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere;

ii. Kusimika Mfumo wa kuhudumia abiria katika Viwanja vya Ndege vya Mwanza, Bukoba, Arusha, Songwe na Dodoma;

iii. Ukarabati wa Jengo la abiria katika Kiwanja cha Ndege cha Mpanda;

iv. Ujenzi wa Jengo jipya la abiria na miundombinu yake katika Kiwanja cha Ndege cha Kahama kinacho milikiwa kwa asilimia 100 na Serikali kwa sasa; na

v. Ukarabati wa Mfumo wa taa za kuongozea ndege katika Kiwanja cha ndege cha Kimataifa cha JNIA na Mwanza.

524. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2023/2024, KIA imepanga kutumia kiasi cha **Shilingi bilioni 26.8** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na mishahara na **Shilingi bilioni 6.49** katika kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Malengo ya KIA kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2023/24 yanaoneshwa kama ifuatavyo: -

i. Kufanya matengenezo ya eneo la maegesho ya magari;

ii. Kugharamia malipo ya awali kwa ajili ya ununuzi wa gari moja (1) la zimamoto;

iii. Usanifu wa kina na kuanza ujenzi wa uzio wa Uwanja awamu ya kwanza;

iv. Kuendelea kuwajengea uwezo watumishi wake kwa kuwapatia mafunzo mbalimbali ya kitaalamu kulingana na majukumu yao;

v. Kuendelea kuimarisha huduma za ulinzi na usalama kiwanjani kwa kununua mashine za x-ray tatu (3);

vi. Kununua magari mawili (2) kwa ajili ya shughuli za uendeshaji wa uwanja;

vii. Ununuzi wa transfoma na vifaa mbalimbali kwa ajili ya uendeshaji wa Uwanja; na

viii. Kuendelea kubadilisha nyaya chakavu za taa za kuongezea ndege. Aidha, katika mwaka wa fedha 2023/24 itafanyika kazi ya Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa mfumo mpya na wa kisasa wa taa za kuongozea ndege katika Kiwanja hiki.

**Huduma za Usafiri wa Anga**

525. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2023/24 Serikali imepanga kutumia jumla ya **Shilingi bilioni 271.00** kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali kwa ajili ya:-

i. Kukamilisha malipo ya kimkataba ya ununuzi wa ndege tatu (3) mpya – Ndege moja (1) aina ya Boeing 787-8 Dreamliner na Ndege mbili (2) aina ya Boeing 7379;

ii. Kufanya malipo ya awali kwa ajili ya ununuzi wa Ndege mpya aina ya Boeing 737–7 moja (1) na DeHavilland Q400 moja (1);

iii. Kugharamia matumizi ya awali ikiwa ni pamoja na uletaji wa Ndege tatu (3) mpya – Ndege moja (1) aina ya Boeing 787-8 Dreamliner na Ndege mbili (2) aina ya Boeing 737-9; gharama za bima; gharama za watalaam wa kukagua na gharama za vipuri muhimu vya ndege;

iv. Kufanya ununuzi wa injini moja (1) ya ziada ili kurahisisha shughuli za matengenezo ya Ndege aina ya Boeing 737-9;

v. Kugharamia ununuzi wa vifaa vya kuhudumia Ndege na Abiria viwanjani;

vi. Kuendelea na ukarabati na ununuzi wa vifaa vya karakana (Hangar) za matengenezo ya ndege katika Viwanja vya Ndege vya JNIA na KIA;

vii. Kuendelea na ujenzi wa karakana (Hangar) mpya ya kutengenezea ndege kubwa aina ya Boeing 7878 Dreamliner;

viii. Kuendelea na ukarabati wa jengo la ofisi za ATCL Makao Makuu na lililopo Kiwanja cha Ndege cha JNIA Terminal I;

ix. Kuendelea na ukarabati wa nyumba 38 zilizopo KIA, na kujenga eneo la mafunzo ya awali kwa Wanaanga;

x. Kukarabati na kujenga majengo ya kuhifadhia mizigo katika Viwanja vya Ndege vya JNIA, KIA na Songwe;

xi. Kuendelea kulipa madeni ya Kampuni;

xii. Kujenga jengo moja la sakafu tatu (3) katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNIA) litakalotumika

kwa matumizi yafuatayo: stoo ya kuhifadhia vipuri vya ndege; vifaa na mahitaji ya huduma za ndani ya ndege (inflight catering facility and amenities); na madarasa kwa ajili ya mafunzo ya Wahudumu wa ndani ya ndege (cabin crew); na

xiii. Kujenga Ofisi za ATCL katika Mji Mkuu wa Serikali eneo la Medeli, Dodoma.

**Huduma za Hali ya Hewa**

526. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2023/24 Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania imetengewa **Shilingi bilioni 15.77** ikiwa ni Bajeti ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, **Shilingi bilioni 15.31** ni Bajeti ya Mishahara na **Shilingi milioni 464.23** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Aidha, Bajeti ya Maendeleo kwa ajili ya mradi wa Rada, Vifaa na Miundombinu ya hali ya hewa katika mwaka 2023/24 ni **Shilingi bilioni 13.00**. Kazi zitakazofanyika ni pamoja na:

i. Kukamilisha malipo ya mwisho ya Rada mbili (2) za hali ya hewa zitakazofungwa Dodoma na Kilimanjaro pamoja na kukamilisha miundombinu yake;

ii. Ununuzi wa Rada mbili (2) za uangazi wa hali ya hewa baharini pamoja na ujenzi wa miundombinu yake;

iii. Kuendelea na ujenzi wa maabara ya uhakiki wa vifaa vya hali ya hewa;

iv. Kugharamia ununuzi wa mitambo ya uhakiki wa vifaa vya kupima hali ya hewa;

v. Kuendelea na ujenzi wa kituo cha Kanda ya Mashariki pamoja na kituo cha kutoa tahadhari ya matukio ya Tsunami (Tsunami Warning Centre);

vi. Kuanza ujenzi wa Ofisi za Makao Makuu Jijini Dodoma;

vii. Ununuzi wa vifaa vya hali ya hewa vikiwemo vifaa visivyotumia zebaki na mitambo ya mawasiliano ya hali ya hewa;

viii. Ujenzi wa mabweni na majengo ya utawala katika Chuo cha Hali ya Hewa;

ix. Ujenzi na ukarabati wa vituo vya hali ya hewa;

x. Kudhibiti na kuratibu huduma za hali ya hewa zinazotolewa nchini kwa kuhakikisha taratibu na matakwa ya kisheria yanafuatwa katika utoaji wa huduma za hali ya hewa;

xi. Kuendelea kutoa huduma za utabiri wa hali ya hewa wa kila siku, siku tano, siku kumi na msimu;

xii. Kuendesha na kuimarisha mtandao wa vituo vya hali ya hewa hapa nchini; na

xiii. Kuendelea kutekeleza mfumo wa udhibiti wa ubora wa huduma za hali ya hewa kwa sekta za usafiri wa anga na kwenye maji kulingana na viwango vya ubora vya kimataifa (ISO 9001:2015).

**C.3 TAASISI ZA MAFUNZO**

**Taasisi ya Teknolojia ya Ujenzi (Institute of Construction Technology – ICoT)**

527. ***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi ya Teknolojia ya Ujenzi Kampasi ya Morogoro katika mwaka wa fedha 2023/24 imepanga kudahili wanafunzi wapya **150** katika ngazi ya cheti (NTA level 4) na kutoa mafunzo kwa wanafunzi **138** wanaoendelea na masomo ya stashahada katika fani za uhandisi Ujenzi, Umeme na Mitambo. Kazi nyingine ni kudahili wanafunzi wapya **200** na kuendelea kutoa mafunzo kwa wanafunzi **353** wanaoendelea na masomo katika Elimu ya ufundi stadi (Vocational Education Training - VET).

528. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Taasisi imepanga kutoa kozi fupi **10** kwa washiriki **400** zinazohusisha kozi za umeme wa magari, maopareta wa mitambo ya kazi za ujenzi, matumizi ya" software"

katika kufanya kazi za kihandisi, matengenezo ya madaraja pamoja na udereva wa awali na udereva wa magari ya abiria. Aidha, Taasisi imepanga kukamilisha upatikanaji wa usajili wa mafunzo ya Elimu ya ufundi Stadi ngazi ya (VET level 3) pamoja na kufanya tathmini ya mafunzo kwa vitendo yanayofanyika viwandani na kwa wanafunzi wa kozi ndefu za Stashahada ('NTA level 4' na 'NTA level 5') pamoja na wanafunzi wa kozi za VET.

529. ***Mheshimiwa Spika,*** kazi nyingine ni kuendelea na ujenzi wa jengo jipya la Utawala la Taasisi; kutangaza shughuli za Taasisi kupitia maonesho katika semina/ warsha na mikutano mitatu (3) ya bodi za kitaaluma; kufanya manunuzi ya vipuri na vifaa vya kufundishia; kufanya matengenezo ya mitambo pamoja na kuwajengea uwezo watumishi.

530. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu Kampasi ya Mbeya katika mwaka wa fedha 2023/24 imepanga kutoa mafunzo ya kozi nane **(8)** za matumizi ya Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi katika ujenzi, ukarabati na matengenezo ya barabara za changarawe pamoja na Lami; kufanya uhamasishaji na ushauri wa matumizi ya Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi katika Halmashauri za Mikoa sita **(6)**.

**Chuo cha Bahari Dar es Salaam (DMI)**

531. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha wa 2023/24, Serikali imetenga **Shilingi bilioni 1.00** kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali kwa ajili ya Chuo cha Bahari Dar es Salaam (DMI) kwa ajili ya kugharamia ununuzi wa kifaa cha kufundishia (Full Mission Crane Simulator). Aidha, Chuo kitaendelea kutekeleza shughuli mbalimbali kwa kutumia fedha za ndani ikiwa ni pamoja na kuanza programu ya ujenzi wa majengo mapya katika Jiji la Dar es Salaam na hatua za awali za ujenzi wa kampasi ndogo katika mikoa ya Simiyu, Lindi na Mwanza. Aidha, Chuo kitaendelea kuboresha miundombinu ya chuo hususan karakana ya utengenezaji wa meli na masuala yahusuyo TEHAMA.

**Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT)**

532. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2023/24, Serikali imetenga jumla ya **Shilingi bilioni 2.27** kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kutekeleza yafuatayo: -

i. Ununuzi wa Mafuta na Matengenezo ya Ndege za kufundishia;

ii. Ununuzi wa Ndege moja (1) ya kufundishia Marubani;

iii. Ununuzi wa vifaa maalum vya kufundishia wataalam wa Sekta ya Anga;

iv. Kuendelea na ujenzi wa Jengo la Maktaba - NIT Mabibo; na

v. Kufanya upembuzi yakinifu kwa ajili ya ujenzi wa Kampasi ya uanzishwaji wa Mafunzo na Kituo Atamizi cha kuandaa mafundi mahiri kwenye Sekta ya Usafiri wa Majini, Mafuta na Gesi Mkoani Lindi.

**C.4 MASUALA MTAMBUKA**

533. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2023/24, Wizara kwa kushirikiana na Taasisi zake itaendelea kutekeleza Mkakati wa Kuzuia na Kupambana na Rushwa wa Miaka Mitano (5) kuanzia 2021/22 hadi 2025/26. Mikakati hiyo ni pamoja na kuendelea kutoa mafunzo yanayohusu maadili na kuzuia vitendo vya rushwa kupitia semina na vikao mbalimbali vya Wafanyakazi. Hivyo, natoa wito kwa Wafanyakazi na Wananchi kwa ujumla waendelee kutoa taarifa katika vyombo husika pale wanapohisi vitendo vya rushwa.

534. ***Mheshimiwa Spika,*** magonjwa yanayoambukizwa ya UKIMWI na UVIKO-19 pamoja na yasiyoambukizwa kama vile kisukari, bado ni tatizo kubwa kwa Taifa letu. Katika mwaka wa fedha 2023/24, Wizara itaendelea kutoa elimu kwa watumishi kuhusu mbinu za kujikinga na maambukizi mapya ya VVU. Pia, Wizara itaendelea kuhimiza upimaji wa hiari wa VVU na magonjwa mengine yasiyoambukizwa pamoja na kuhimiza

ushiriki wa watumishi kwenye bonanza na michezo ikiwa ni njia mojawapo ya kuboresha afya za watumishi. Aidha, Wizara itaendelea kuhimiza watumishi wake kupata chanjo dhidi ya UVIKO-19.

535. ***Mheshimiwa Spika,*** hivi karibuni nchi yetu ilikumbwa na ugonjwa mpya uliotambulika kwa jina la Marburg. Ugonjwa huo ulisababisha taharuki kwa wananchi, hususan katika kutumia vyombo vya usafiri. Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Afya itaendelea kutoa miongozo ya namna ya kujikinga na maambukizi ya magonjwa ya mlipuko ambayo yanaweza kuathiri utekelezaji wa shughuli mbalimbali za kiuchumi ikiwemo biashara na usafiri.

**D. SHUKRANI**

536. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara katika utekelezaji wa majukumu yake kwa mwaka 2022/23, ilipata ushirikiano kutoka kwa Washirika wa Maendeleo, Sekta Binafsi na wananchi kwa ujumla. Ninapenda kutumia fursa hii kuwashukuru wadau wote waliotoa michango mbalimbali ikiwemo ushauri, rasilimali fedha na nguvu kazi na wale walioshiriki moja kwa moja katika utendaji wa shughuli mbalimbali za ujenzi na uchukuzi. Shukrani za kipekee ziwaendee Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa michango yao ambayo imesaidia katika kuimarisha utendaji wa Wizara yangu katika kutoa huduma kwa wananchi. Aidha, ili Wizara iendelee kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na kuchangia katika maendeleo ya nchi yetu, niwaombe Waheshimiwa Wabunge msichoke kuendelea kuishauri Serikali katika masuala mbalimbali hasa yanayohusu Sekta ninazozisimamia. Pia, niwaombe wananchi na wadau wengine kuendelea kutoa michango yao ya hali na mali pamoja na kuendelea kushirikiana na Serikali katika kulinda miundombinu ya usafiri na usafirishaji ambayo Serikali imekuwa ikitumia kiasi kikubwa cha fedha kuijenga na kuikarabati miundombinu hiyo.

537. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mara nyingine tena nichukue fursa hii kuwapongeza na kutambua mchango mkubwa unaotolewa na viongozi wenzangu katika kunisaidia kutekeleza majukumu ya Wizara yangu, nikianzia na Naibu Mawaziri, Mheshimiwa Mhandisi

**Godfrey Msongwe Kasekenya (Mb.)** na Mheshimiwa **Atupele Fred Mwakibete (Mb.);** Makatibu Wakuu, Balozi Mhandisi **Aisha Salim Amour** (Ujenzi), na Ndugu **Gabriel Joseph Migire** (Uchukuzi); Naibu Makatibu Wakuu Ndugu **Ludovick James Nduhiye** (Ujenzi) na Dkt. **Ally Saleh Possi** (Uchukuzi). Vilevile, kipekee napenda kuishukuru Menejimenti ya Wizara, Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara na Watumishi wote wa Wizara na Taasisi kwa jitihada zao katika utekelezaji wa Majukumu ya Wizara.

538. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa niaba ya Wizara naomba kutumia fursa hii kuwashukuru kwa dhati na kuwatambua wadau wote wa Wizara ikiwa ni pamoja na Washirika mbalimbali wa Maendeleo ambao wamechangia kwa kiasi kikubwa katika utekelezaji wa Programu, Miradi na Mipango mbalimbali ya Wizara. Aidha, napenda kuwatambua wafuatao: Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Anga (ICAO), Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Majini (IMO), Shirika la Hali ya Hewa Duniani (WMO), "Third World Organization for Women in Science (TWOWS)", UNESCO, Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Benki ya Dunia (WB), Japan (JICA), Benki ya Kiarabu ya Maendeleo ya Afrika (BADEA), OPEC Fund, Korea Kusini (KOICA), Abu Dhabi Fund, Ujerumani (KfW), Foreign, Commonwealth and Development Office (FCDO), Uholanzi (ORIO), Shirika la Maendeleo la Ufaransa (AFD), Jumuiya ya Nchi za Ulaya (EU), Benki ya Uwekezaji ya Ulaya (EIB), Shirika la Maendeleo la Marekani (USAID), Kuwait (KFAED), HSBC, TMEA, Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, Sekretarieti ya Jumuiya ya Nchi za SADC, Nchi za Urusi, Afrika Kusini, Uingereza, Marekani, Uholanzi, Japan, India, China, Denmark, Norway, Ubelgiji, Ujerumani na Uturuki, Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ya NSSF na PSSSF, Taasisi za fedha za CRDB, NMB, NBC na TCB na Asasi mbalimbali zisizokuwa za Serikali; Sekta Binafsi pamoja na wadau wengine wengi ambao sitamaliza endapo nitawataja wote.

539. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba nitoe shukrani zangu za dhati kwako wewe binafsi Mhe. Spika, Mhe. Naibu Spika na kwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Hotuba hii pia inapatikana katika tovuti ya Wizara (**www.mwt.go.tz**).

## D. MUHTASARI WA MAOMBI YA FEDHA YA WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI KATIKA MWAKA WA FEDHA 2023/24

540. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2023/24, Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi 3,554,783,957,000.00.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi 1,468,238,449,000.00** ni kwa ajili ya Sekta ya Ujenzi na **Shilingi 2,086,545,508,000.00** ni kwa ajili ya Sekta ya Uchukuzi. Mchanganuo wa fedha zinazoombwa kwa kila Fungu ni kama ifuatavyo:

**SEKTA YA UJENZI (FUNGU 98)**

541. ***Mheshimiwa Spika,*** Sekta ya Ujenzi (Fungu 98) imetengewa **Shilingi 1,468,238,449,000.00** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 48,395,392,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ya Wizara (Ujenzi) na Taasisi na **Shilingi 1,419,843,057,000.00** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizi za utekelezaji wa miradi ya maendeleo, **Shilingi 1,084,666,369,000.00** ni fedha za ndani na **Shilingi 335,176,688,000.00** ni fedha za nje. Fedha za ndani zinajumuisha **Shilingi 599,756,467,800.00** kutoka Mfuko wa Barabara na **Shilingi 484,909,901,200.00** ni Mfuko Mkuu wa Serikali. Kati ya fedha za Matumizi ya Kawaida, **Shilingi 43,958,274,000.00** ni za Mishahara ya Watumishi na **Shilingi 4,437,118,000.00** ni za Matumizi Mengineyo.

**SEKTA YA UCHUKUZI (FUNGU 62)**

542. ***Mheshimiwa Spika,*** Sekta ya Uchukuzi imetengewa jumla ya **Shilingi 2,086,545,508,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Kati ya hizo, **Shilingi 118,215,599,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo **Shilingi 89,291,108,000.00** ni za Mishahara ya Watumishi na **Shilingi 28,924,491,000.00** ni za Matumizi Mengineyo. Aidha, Miradi ya Maendeleo imetengewa **Shilingi 1,968,329,909,000.00**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 1,861,064,800,000.00** ni fedha za ndani na **Shilingi 107,265,109,000.00** ni fedha za nje.

543. ***Mheshimiwa Spika***, pamoja na Hotuba hii, nimeambatisha Miradi ya Wizara itakayotekelezwa katika mwaka wa fedha 2023/24 **(Kiambatisho Na. 1 – 6)** ikionesha kiasi cha fedha kilichotengwa kutekeleza kila mradi. Naomba viambatisho hivyo vichukuliwe kama sehemu ya vielelezo vya hoja hii.

544. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi na hoja imeungwa mkono. Tunakushuru sana Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge nina tangazo dogo, wapo wageni 30 wa Mheshimiwa *Doctor* Christine Ishengoma ambao ni kutoka KKKT Ubungo, wako humu ndani. Karibuni sana. *(Makofi)*

Sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, Mheshimiwa Kakoso atoe maoni ya Kamati yake. *(Makofi)*

**MHE. MOSHI S. KAKOSO – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naomba taarifa hii yote iingie katika Taarifa Rasmi ya Bunge kama ilivyowasilishwa mezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 118(9) ya Kanuni za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kwa mwaka wa fedha 2022/2023, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Kwanza ni Utangulizi ambayo inajumuisha maelezo ya jumla, muundo wa taarifa, pamoja na ufafanuzi wa namna Kamati ilivyotekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Pili ni Uchambuzi wa Tathmini ya Utekelezaji wa Majukumu ya Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2022/2023; pamoja na Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati pia ilifanya ziara ya ukaguzi ili kujionea utekelezaji wa miradi iliyo chini ya Wizara iliyotengewa fedha katika mwaka wa fedha 2022/2023. Katika hatua hii, Kamati ilifanya tathmini kuhusu hali ya upatikanaji wa fedha, ufanisi na utekelezaji wa miradi husika pamoja na tija ambayo inapatikana katika miradi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maoni na Ushauri wa Kamati; kwa upande wa Sekta ya Ujenzi, Kamati ilitoa maoni kwa maeneo ambayo bado hayajatekelezwa kikamilifu na utekelezaji wake bado unaendelea. Kwa mfano, kuhusu kuongeza fedha katika ujenzi wa miradi ya barabara na matengenezo. Kamati inaendelea kusisitiza kuwa Serikali ianze kutumia mfumo wa *PPP* na *EPC+ Finance* katika ujenzi wa barabara zake ili kuwezesha barabara nyingi kujengwa na kufanyiwa matengenezo. Pia, Serikali itafute vyanzo vya kutunisha Mfuko wa Barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Sekta ya Uchukuzi, Kamati inaendelea kusisitiza Serikali kuharakisha mchakato wa marekebisho ya sheria mbalimbali ili kuruhusu wawekezaji binafsi katika uendeshaji wa reli na bandari nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hali ya Upatikanaji wa Fedha; katika mwaka wa fedha 2022/2023, Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi iliidhinishiwa jumla ya shilingi trilioni 3.8. Kati ya fedha hizo, shilingi trilioni 1.46 zilikuwa ni kwa ajili ya Fungu 98 - Sekta ya Ujenzi na shilingi trilioni 2.4 ziliidhinishwa kwa ajili ya Fungu 62 - Sekta ya Uchukuzi. Katika Sekta ya Ujenzi, shilingi bilioni 44.2 zilikuwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi trilioni 1.42 zilikuwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia Februari, 2023, kiasi cha fedha za matumizi ya kawaida kilichopelekwa kwa Sekta ya Ujenzi ni shilingi bilioni 25.9 sawa na asilimia 58.49 ya bajeti iliyoidhinishwa, wakati miradi ya maendeleo ilipokea shilingi trilioni 1.2 sawa na asilimia 85.87 ya bajeti iliyoidhinishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Sekta ya Uchukuzi, kati ya bajeti iliyotengwa ya shilingi bilioni 94.5 zilikuwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi trilioni 2.3 kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Hadi kufikia Februari 2023, kiasi cha fedha za matumizi ya kawaida kilichopokelewa kwa Sekta ya Uchukuzi ni shilingi bilioni 57.99 sawa na asilimia 61 ya bajeti iliyoidhinishwa wakati miradi ya maendeleo ilipokea shilingi trilioni 1.38 sawa na asilimia 59.83 ya bajeti iliyoidhinishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa wastani, hali ya mapokezi ya fedha kwa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kufikia Februari, 2023 ilikuwa ya kuridhisha. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kutoa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makusanyo ya maduhuli; katika mwaka wa fedha 2022/2023, Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi pamoja na taasisi zilizo chini yake ziliidhinishiwa na kukusanya jumla ya shilingi trilioni 2.3. Hadi kufikia Februari, 2023, makusanyo yalikuwa shilingi trilioni 1.4 sawa na asilimia 60.53 ya malengo. Kwa ujumla mwenendo wa makusanyo ya Wizara ni wa kuridhisha. Hata hivyo, Kamati imebaini kwamba, baadhi ya taasisi zilizo chini ya Sekta ya Uchukuzi zina mwenendo wa makusanyo usioridhisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali kuzingatia malengo yaliyowekwa katika ukusanyaji wa mapato na pia makadirio ya makusanyo yaendane na uhalisia wa vyanzo vilivyopo pamoja na uwezo wa kila taasisi kukusanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tathmini na utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Katika mwaka wa fedha 2022/2023 Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi iliidhinishiwa jumla ya shilingi trilioni 1.42 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika Fungu 98 – Sekta ya Ujenzi, ambapo kati ya fedha hizo, shilingi trilioni 1.16 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 252 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia mwezi Februari, 2023 jumla ya shilingi trilioni 1.22 sawa na asilimia 70 ya lengo zilipatikana. Kati ya fedha zilizopatikana, shilingi bilioni 243 ni fedha za nje sawa na asilimia 96 ya lengo na shilingi bilioni 977 fedha za ndani sawa na asilimia 66. Fedha za ndani zilizopatikana zinajumuisha shilingi bilioni 573 za Mfuko wa Serikali na shilingi bilioni 403 ni za Mfuko wa Barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ya ujenzi, barabara na madaraja; Kamati ilitembelea ujenzi wa barabara njia nane kuanzia Kimara – Kibaha ambapo umegharimu shilingi bilioni 161 bila *VAT* na utekelezaji wake umefikia asilimia 98. Taarifa ilieleza kuwa mradi huu ulitarajiwa kukamilika ifikapo tarehe 15 Aprili, 2023. Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua iliyofikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia tarehe 15 Machi, 2023, taarifa ya utekelezaji wa miradi mingine ya barabara ni kama ifuatavyo: -

a) Ujenzi na ukarabati wa barabara kuu kwa kiwango cha lami umekamilika kwa asilimia 40; na

b) Barabara za mikoa kwa jumla ya kilometa 23.11 kati ya kilometa 103.10 za barabara za mikoa sawa na asilimia 22.43 zimejengwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio hayo, Kamati imebaini changamoto mbalimbali ikiwemo zifuatazo:-

a) Changamoto ya gharama kuongezeka kabla ya ujenzi kukamilika;

b) Malalamiko kuhusu uwepo wa vituo vya mafuta ndani ya hifadhi ya barabara;

c) Ucheleweshaji wa fedha kwa ajili ya malipo ya Wakandarasi;

d) *TANROADS* kutosimamia kwa karibu tozo kwa wakandarasi wanaochelewesha miradi; na

e) Wananchi wengi kutotumia vivuko vya madaraja ya juu kutokana na sababu mbalimbali na kuhatarisha usalama wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa miundombinu ya barabara na mabasi yaendayo haraka *(BRT)*. Mradi huu una jumla ya kilometa 148.7 na umegawanyika katika awamu sita, ambapo awamu ya kwanza ya ujenzi tayari imeshakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio yaliyobainika, kamati imebaini kuwepo kwa changamoto mbali mbali katika awamu ya mradi zinazoendelea kama ifuatavyo:-

a) Mkandarasi amechelewa kukamilisha kazi ndani ya muda wa mkataba;

b) Kuongezeka wa gharama ya mkataba kwa kutoka shilingi bilioni 217.48 hadi shilingi bilioni 253.91, ongezeko hili ni sawa na asilimia 16.7; na

c) Kukosekana umakini wa mkandarasi katika ubora wa kazi ya zege la barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa ujenzi wa ukarabati wa maegesho na vivuko. Katika utekelezaji wa mradi huu Kamati imebaini mambo yafuatayo: -

a) Upanuzi wa jengo la abiria katika maegesho ya Magogoni – Kigamboni upande wa Kigamboni umekamilika; na

b) Ukarabati mkubwa wa vivuko vya *MV* Kazi, *MV TEMESA*, *MV* Musoma, *MV* Tanga na *MV* Sabasaba umekamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imebaini kuwepo kwa changamoto zinazoikablili *TEMESA* ni pamoja na :-

a) Madeni ambayo *TEMESA* wanazidai Taasisi za Serikali; na

b) Baadhi ya vivuko kuwa na eneo finyu la watumiaji na hivyo kusababisha usumbufu. Mfano, Kivuko cha Kigamboni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ya ujenzi wa nyumba na majengo ya Serikali. Tarehe 18 Machi, 2023 Kamati ilitembelea na kukagua miradi ya maendeleo, mradi wa maendeleo wa ujenzi wa Temeke Kota. Kamati ilielezwa kuhusu mradi huu unaohusisha ujenzi wa majengo saba yenye ghorofa tisa ambapo kila jengo litakuwa na uwezo wa kubeba kaya 144. Mradi huu unatekelezwa kwa fedha za ruzuku za Serikali kwa gharama ya shilingi bilioni 19 kwa jengo moja. Ujenzi umefikia asilimia Nane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa ujenzi wa nyumba na majengo ya Serikali imeonesha mafanikio yafuatayo ikiwemo kuzalisha fursa mbalimbali za ajira kwa wataalam wa ujenzi, mafundi, wazalishaji, wauzaji na wasambazaji na vifaa vya ujenzi, watoa huduma kama vile Baba Lishe na Mama Lishe. Pamoja na hayo kamati imebaini kuwepo kwa changamoto zifuatazo:-

a) Ongezeko la gharama kwenye miradi inayotekelezwa kwa fedha za ruzuku ya Serikali na mapato ya ndani;

b) Kucheleweshwa kulipwa fedha kwa baadhi ya washitiri; na

c) Changamoto ya uvamizi wa ardhi ya *TBA* isiyokuwa na hati miliki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ya viwanja vya ndege. Mradi huu ulitengewa jumla ya shilingi bilioni 86. Kati ya fedha, shilingi bilioni 54 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 31 ni fedha za nje. Miradi inakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

a) Kutokuwepo kwa sheria mama na mahsusi kwa ajili ya usimamizi, uendeshaji na uendelezwaji wa viwanja vya ndege Tanzania;

b) *TANROADS* kuendelea kujenga viwanja vya ndege badala ya *TAA;* na

c) Changamoto ya usalama wa Uwanja wa Ndege wa Mkoa Kagera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ya Sekta ya Uchukuzi. Kwa upande wa Fungu Namba 62 – Sekta ya Uchukuzi, ilitengwa shilingi trilioni 2.3 kutekeleza miradi ya maendeleo, shilingi trilioni 2.1 zilikuwa ni fedha za ndani, na shilingi bilioni 113 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia Februari, 2023, shilingi trilioni 1.38 sawa na asilimia 67.85 ya bajeti iliyoidhinishwa zilitolewa. Kati ya fedha zilizotolewa ni shilingi trilioni 1.35 ni fedha za ndani sawa na asilimia 66.31 ya bajeti iliyoidhinishwa na shilingi bilioni 31.29 ni fedha za nje sawa na asilimia 1.53 ya bajeti iliyoidhinishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa ujenzi wa Reli ya Kisasa *(SGR),* Mradi Na. 4281. Katika mwaka wa 2022/2023, mradi ulitengewa shilingi trilioni 1.11. Lengo la mradi ni kukamilisha ujenzi wa Reli ya *SGR* kipande cha Dar es Salaam hadi Morogoro (kilometa 300), Morogoro hadi Makutupora (kilometa 422), Mwanza - Isaka (kilometa 341). Kamati ilipokea taarifa za utekelezaji wa mradi huu kama ifuatavyo: -

a) Jumla ya shilingi trilioni 1.09 zilitolewa ikiwa ni sawa na asilimia 98.14 kwa kipindi cha robo tatu ya muda wa utekelezaji na

b) Kipande cha Dar es Salaam – Morogoro umefikia asilimia 97.94, Morogoro - Makutupora asilimia 92.88.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo kamati imebaini kuwepo kwa changamoto zifuatazo:-

a) kutokamilika kwa reli ya kisasa kipande cha kutoka Dar es Salaam – Morogoro – Dodoma –Makutupora (*lot* namba moja na *lot* namba mbili*)* ikilinganishwa na lengo lililowekwa; na

b) Kuchelewa kufika kwa mabehewa ya treni ya *SGR* ikilinganishwa na lengo lililowekewa ambapo ilitarajiwa kukamilika Februari, 2022.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa uboreshaji wa Reli ya *TAZARA*. Katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, mradi huu

umetengewa jumla ya shilingi bilioni 13.19 ambapo *TAZARA* ilipanga kufanya ukarabati wa mabehewa 14 ya abiria kwa ajili ya treni ya Jiji la Dar es Salaam na mabehewa saba ya abiria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio hayo, Kamati imebaini kuwa sheria iliyoanzisha Shirika la Reli ya *TAZARA* haitoi nafasi ya Tanzania kufanya uwekezaji wa maboresho zaidi katika reli hiyo, hivyo basi sheria hiyo inahitaji marekebisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa uboreshaji wa Bandari za Tanzania. Katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, mradi huu wa kimkakati unatekelezwa kwa gharama za dola shilingi bilioni 421. Changamoto zilizopo ni pamoja na:-

a) Kuwepo kwa vipengele vya sheria ambavyo siyo rafiki kwa wawekezaji kuja kuwekeza nchini;

b) Ongezeko la mapato kutoendana na kasi ya uboreshaji; na

c) Mifumo ya TEHAMA isiyotosheleza na kutokuwa na mfumo wa kuunganisha wadau wa *(Single Window System)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza *TPA* kwa kuongeza mapato na inashauri Serikali itathmini kuhusu uwekezaji wa sekta binafsi katika uendeshaji wa bandari nchini pia mikataba iwe na manufaa kwa nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa uendeshaji wa Jengo la Tatu la Abiria *(JNIA),* maboresho na huduma katika viwanja vya ndege. Mradi huu ulitengewa shilingi bilioni 17.30. Hadi kufikia Februari, 2023 jumla ya shilingi bilioni 17.07 ikiwa ni sawa na asilimia 98.68 ya bajeti iliyotengwa zilitolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilielezwa changamoto zifuatazo katika viwanja vya ndege kwa ujumla wake ni pamoja na: -

a) Baadhi ya viwanja, ndege zinashindwa kutua usiku kwa sababu ya kutokuwa na taa; na

b) Kukosekana kwa sheria mahsusi kwa ajili ya usimamizi, uendeshaji na uendelezaji wa viwanja vya ndege hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa ununuzi wa ndege *ATCL*. Mradi ulitengewa shilingi bilioni 353. Hadi Februari, 2022, mradi huu umepokea shilingi bilioni 27.01 sawa na asilimia 7.7. Pamoja na mafanikio ambayo yameainishwa katika taarifa ya Kamati, mradi huu unakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na:-

a) Kuharibika kwa injini mbili za ndege; na

b) Gharama kubwa za uendeshaji na mzigo mkubwa wa madeni unaolikabili shirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee Kamati inaipongeza Serikali kwa jitihada zinazoendelea za kulifufua shirika ikiwa kununua ndege za abiria na mizigo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Usafiri wa Anga *TCAA*. *TCAA* imefanya usimikaji wa rada za kuongozea ndege katika vituo vya Dar es Salaam, Kilimanjaro, Mwanza na Songwe na gharama ya shilingi bilioni 67.3, mtambo wa kuwezesha ndege kutua kiwanja cha Abeid Amani Karume shilingi bilioni 4.6 na ukarabati wa mnara wa kuongoza ndege Pemba shilingi milioni 300. Pamoja na mafanikio haya, *TCAA* inakabiliwa na changamoto mbalimbali ambazo ni pamoja na:-

a) Uchakavu wa mitambo ya kuongozea ndege na miundombinu duni; na

b) Upungufu wa wataalam kwenye sekta ya anga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa uboreshaji wa vyuo vilivyo chini ya Sekta ya Uchukuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha Usafirishaji *(NIT)* kilitengewa jumla ya shilingi bilioni 1.77. Hadi Februari 2023 fedha iliyopokelewa ni shilingi bilioni 1.77 sawa na asilimia 100 ya bajeti iliyotengwa. Katika Chuo cha Bandari ya Dar es Salaam *(DMI)* kilipanga kununua mtambo kwa shilingi bilioni 1. Hadi kufikia

Februari 2023 umetumia jumla ya shilingi milioni 275.41 ikiwa ni sawa na asilimia 28 ya lengo. Kamati inasisitiza kuwa, Serikali ikamilishe ununuzi wa *simulator* kwenye Chuo cha *DMI*. Changamoto inayokabili vyuo ni kama ifuatavyo:-

a) Upungufu wa watumishi, uhaba wa vifaa vya kufundishia, mfano ndege maalum za kufundishia pale kwenye Chuo cha *NIT*;

b) Msongamano mkubwa wa wanafunzi na uchakavu wa miundombinu mfano hosteli na madarasa; na

c) Baadhi ya watumishi wa Serikali wanaosomeshwa na fedha za Serikali kutokurejea nchini wanapomaliza masomo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inasisitiza kuwa Serikali iboreshe vyuo vilivyo chini ya Sekta hii na kutoa fedha kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ya ujenzi na ukarabati wa meli kwenye maziwa makuu, Mradi Na. 4295.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 mradi huu umetengewa shilingi bilioni 113.7. Kamati inaipongeza Serikali kwa ujenzi na ukarabati wa meli za *MV* Mwanza, HAPA KAZI TU, *MV* Umoja na *MV* Sangara umefikia hatua ya asilimia 82, asilimia 69 na asilimia 90 kwa mtawalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na changamoto mbalimbali zilizopo, kamati imebaini kuwa mojawapo ya changamoto kubwa ni kutokuwepo kwa meli yenye uhakika katika usafirishaji wa abiria katika Ziwa Tanganyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi na Mpango wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2023. Muundo wa Bajeti, katika mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi trilioni 3.7. Kati ya fedha hizo, shilingi trilioni 1.6 inaombwa kwa Fungu Namba 98 – Sekta ya Ujenzi na shilingi trilioni 2.08 inaombwa kwenye Fungu 62 Sekta ya Uchukuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya fedha inayoombwa, kati ya Fungu 98, Sekta ya Ujenzi, shilingi bilioni 59 kwa matumizi ya kawaida wakati shilingi trilioni 1.6 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kati ya fedha inayoombwa kati ya Fungu Namba 62 Sekta ya Uchukuzi, shilingi bilioni 118 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi trilioni 1.9 ni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla Bajeti ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi imepungua kwa asilimia 2.07 ukilinganisha na bajeti ya shilingi bilioni 3.8 iliyotengwa katika Mwaka wa Fedha unaoishia mwaka 2022/2023. Aidha bajeti ya maendeleo kwa Fungu 98 na Fungu 62 zimepungua kwa asilimia 5.7 na asilimia 3.57 mtawalia. Hata hivyo bajeti ya matumizi ya kawaida kwa Fungu Namba 98 na 62 imeongezeka kwa asilimia 35 na asilimia 25 mtawalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuongeza fedha za matumizi mwengineyo *(OC),* kwa kuwa hatua hii itaongeza motisha kwa watumishi kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi. Hata hivyo, Kamati haijaridhishwa na kupungua kwa fedha za utekelezaji kwa miradi ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, malengo ya makusanyo ya maduhuli; katika mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi pamoja na taasisi zake inaomba kuidhinishiwa kukusanya jumla ya shilingi trilioni 3.1. Kiwango hiki ni ongezeko la asilimia 33.65 ukilinganisha na shilingi trilioni 2.3 iliyopangwa kukusanywa katika mwaka wa fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuongeza makadirio na makusanyo kwa Mwaka wa Fedha wa 2023/2024 kwa zile taasisi ambazo katika Mwaka wa Fedha 2023 hazikutimiza malengo ya makusanyo. Kamati inazishauri taasisi hizo kuhakikisha kwamba wanajiwekea mikakati madhubuti ya makusanyo ili kuiwezesha Serikali kutimiza malengo yake katika mwaka wa fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi ya kawaida. Kwa ujumla bajeti ya matumizi ya kawaida ya mwaka wa fedha 2023/2024

imeongezeka kwa wastani wa asilimia 30 kati ya mafungu yote ya Wizara, ukilinganisha na bajeti hiyo kwa mwaka wa fedha 2023. Ongezeko hilo linatokana na kuongezeka kwa fedha za matumizi mengine *(OC)*. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuongeza fedha za matumizi mengineyo *(OC)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa maendeleo; katika mwaka wa fedha 2023, Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi inaomba kuidhinishiwa shilingi trilioni 3.38 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ambao kwa ujumla wake ni pungufu kwa asilimia 10.4 ukilinganisha na bajeti ya maendeleo kwa mwaka wa fedha ulioisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na ushauri wa Kamati. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi ina mchango mkubwa katika maendeleo ya nchi na ukuaji wa uchumi. Kwa msingi huo, Kamati ina maoni na ushauri kwa jumla ya Serikali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imebaini kwamba katika mwaka wa fedha 2022/2023, bajeti ya matumizi ya kawaida hususan matumizi mengine *(OC)* zimeongezeka. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba fedha zilizotengwa na Bunge zinafika kwa wakati na kuiwezesha Wizara, taasisi na kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Aidha, Kamati inashauri Wizara na Taasisi hizo kuwa wabunifu wa namna bora na uendelezaji wa majukumu kwa ufanisi na kasi zaidi ili fedha za matumizi mengineyo *(OC)* zinafika na zinatumika kwa weledi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa gharama za miradi inayotekelezwa na Wizara ni kubwa, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba miradi hiyo inazingatia viwango na ubora. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba kunakuwepo na uwajibikaji wa Watendaji na Wakandarasi katika miradi yote ambayo inatekelezwa au itekelezwe chini ya viwango pia ichukue hatua za kisheria na za kinidhamu kwa wahusika wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Kamati imebaini kwamba miradi mingi ya barabara katika Sekta ya Ujenzi inashindwa kuanza utekelezaji kutokana na sababu mbalimbali

ikiwemo ukosefu wa fedha, Kamati inaishauri Serikali kuanza mpango wa kushirikisha Sekta Binafsi *(PPP)* na *EPC+ Finance* katika ujenzi wa barabara na Serikali iwe na makakati wa kuwadhibiti wakandarasi wanaoshindwa kutekeleza miradi kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na ushauri mahsusi. Baada ya kutoa maoni ya jumla sasa naomba nitoe maoni ya ushauri mahsusi katika masuala mbalimbali ya utekelezaji wa majukumu ya Sekta ya Ujenzi na Uchukuzi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Sekta ya Ujenzi, kuhusu Miundombinu ya barabara kusimamiwa na *TANROADS,* Serikali iongeze fedha za matengenezo; pili, Serikali ijenge barabara kwa kutumia mfumo wa kushirikisha wawekezaji binafsi *(PPP na EPC + Finance)* ili kuwezesha barabara nyingi kujengwa mfano, barabara ya Kibaha - Chalinze – Morogoro; naKatika mikataba ya ujenzi wa Barabara, Serikali iongeze kipengele kitakachofanya Mkandarasi na Mhandisi Mshauri wa Mradi kuongeza muda wa kuendelea kufuatilia na kukarabati barabara kwa mkataba, uwe zaidi ya mwaka mmoja kabla ya kuzikabidhi kwa Serikali kuliko ilivyo sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya wakandarasi kuchelewa kukamilisha miradi kwa wakati na kuongeza gharama, Serikali iweke kipengele katika mkataba cha kuzuia ongezeko la gharama. Kutokana na malalamiko yanayotoka kwa wananchi wa Kimara waliobomolewa nyumba na sehemu zao za biashara ili kupisha ujenzi wa barabara, Serikali kupitia *TANROADS* iondoe kituo cha mafuta kilichopo karibu na mzunguko wa barabara Kimara - *Stop Over*; Serikali iwaunganishe Wakandarasi wazawa na iwajengee uwezo katika ujenzi wa miradi ya ndani ili kuwawezesha kupata uzoefu wa kutekeleza miradi mingine mfano fedha za utaalam katika usimamizi wa miradi; Serikali iimarishe mifumo ya mifereji ya maji katika ujenzi wa barabara ili kuepusha maji kujaa kwenye makazi ya wananchi. Serikali ijenge vivuko vya waenda kwa miguu kwa kutumia madaraja ya chini ili kuwawezesha watu wengi kutumia njia hizo hasa kwa walemavu; Serikali iendelee kutoa elimu ya matumizi ya barabara kwa wananchi ili kupunguza ajali. Wakandarasi wanaochelewesha

miradi kutokamilika kwa wakati, watoe tozo kuilipa Serikali kwa ucheleweshaji huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ukarabati wa Karakana, Vivuko na Maegesho Unaosimamiwa na *TEMESA*. Serikali izisimamie taasisi zake ili zilipe madeni kwa *TEMESA* kutokana na huduma wanazopata. Pamoja na kwamba *TEMESA* wamejikita katika kutoa huduma, ni vema TEMESA ikajiendesha kibiashara, kwani gharama wanazotumia katika uendeshaji ni kubwa kuliko mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu barabara na miundombinu ya mradi wa mabasi yaendayo haraka *(BRT), TANROADS* waimarishe usimamizi kwa Mkandarasi wa mradi wa *BRT* ili ukamilike kwa wakati; *TANROADS* itumie mfumo wa gharama za mradi kutobadilika kutokana na mazingira *(fixed contract)* ambayo wenzetu wa Shirika la Reli wameitumia na kuwa na ufanisi mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ujenzi wa nyumba na majengo ya Serikali, Serikali iisaidie *TBA* ili walipwe fedha wanazozidai taasisi mbalimbali za Serikali ikiwemo madeni ya pango la nyumba za viongozi ili fedha watakazolipwa ziwasaidie katika kujiendesha kibiashara; na *TBA* iharakishe kupata umiliki wa kisheria wa ardhi zilizo chini yake ili kuziendeleza na kuepuka wavamizi hasa katika Mikoa ya Arusha na Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ujenzi wa viwanja vya ndege, Serikali iongeze fedha za ukarabati wa miundombinu katika viwanja vya ndege ili kuimarisha usalama wa ndege; Ujenzi wa miundombinu ya viwanja vya ndege ubaki kwa *TAA* badala ya kupewa *TANROADS*; na Serikali ijenge uwanja mpya wa ndege.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Chuo cha Teknolojia ya Ujenzi *(ICoT)*. Kamati inashauri kwamba, Serikali iongeze fedha kuendelea kufanya maboresho mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sekta ya uchukuzi, Utendaji wa Shirika la Reli Tanzania *(TRC)*. Serikali kupitia *TRC* imsimamie

mkandarasi anayejenga reli ya Kisasa (*SGR*) kipande cha Dar es Salaam - Makutupora – *(Lot 1 & 2)* akamilishe kazi ndani ya muda alioongezewa; Mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa uendane na ununuzi wa mabehewa na vichwa vya treni pamoja na uimarishaji wa miundombinu ya umeme. Serikali ihakikishe Chuo cha Reli kinaboreshwa ili kutoa wataalam wa kutosha watakaoweza kufanya matengenezo makubwa kwenye njia ya reli na mitambo yake kwa reli ya *SGR* na *Meter Gauge*. Serikali iharakishe mikakati ya ujenzi wa reli kwenye maeneo ya kiuchumi, mfano mkubwa ni maeneo ya Reli ya Kaliua - Karema, Mtwara – Bambabay na mengineyo. Serikali iharakishe ukarabati wa reli kutoka Kilosa – Mikumi – Kidatu ili kuunganisha reli ya kati na *TAZARA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uendeshaji wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania *(TPA)*, Serikali iharakishe mchakato wa kuruhusu uwekezaji binafsi katika sekta ya bandari nchini; Serikali iharakishe miundombinu ya reli inayounganisha bandari na reli za *SGR, Meter Gauge* na *TAZARA*; ongezeko la makusanyo ya mapato ya *TPA* yaendane na uhalisia wa maboresho ya miundombinu iliyowekezwa; na Serikali iangalie uwezekano wa kutumika kwa Bandari za Mtwara na Tanga ili uweze kuwa na uwekezaji ulio na tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uboreshaji wa huduma ya miundombinu katika Viwanja vya Ndege Tanzania vinavyosimamiwa na *TAA*, Serikali ione uwezekano wa kuiwezesha *TAA* kubakiza kiasi cha fedha walau asilimia 40 zitokanazo na makusanyo ili zisaidie katika masuala ya uendeshaji; Sheria iliyoanzisha viwanja vya ndege iboreshwe ili kuwezesha viwanja vingi kujiendesha kibiashara; Kwa kuwa Kamati imebaini kuna upungufu wa vifaa vya kuongoza ndege wakati wa kutua *(ILS)*, Serikali ihakikishe kuwa viwanja vyetu vya ndege vinakuwa na vifaa hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uendeshaji wa Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania, Serikali kwa kutumia mapato ya ndani iharakishe ujenzi wa miundombinu ya kisasa katika mafunzo ya usafiri wa Anga *(CATC)* yaani kwenye chuo kinachosimamiwa na mamlaka husika. Katika uendeshaji wa Mamlaka ya Hali ya

Hewa Nchini, *TMA* iendelee kujiimarisha ili iendane na ukuaji wa teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utendaji wa Kampuni ya Ndege Tanzania *(ATCL),* Serikali itathimini upya juu ya umiliki wa ndege zake kwa Shirika la Ndege la *ATCL* kuliko ilivyo sasa; Serikali iendelee kufuatilia kwa karibu ili matengenezo ya injini mbili za ndege zinazoharibika ikamilike; na Serikali iisaidie *ATCL* ili kuweza kukabiliana na madeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika uboreshaji wa vyuo vilivyo chini ya sekta ya uchukuzi, Serikali iongeze uwekezaji katika vyuo ili kuwezesha vyuo hivyo kujiendesha kwa ufanisi zaidi; na Serikali iandae mpango maalum ambao utasaidia wahitimu wa kozi mbalimbali wanaotoka katika vyuo hivyo kutumia utaalamu wao katika ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho. Katika kufanikisha Malengo ya Maendeleo Endelevu *(SDGs),* uboreshaji wa Sekta ya Ujenzi na Sekta ya Uchukuzi ni muhimu kwa uchumi wa nchi na itayoweza kuimarika kwa sekta nyingine kama vile viwanda, utalii na biashara (kama inavyoeleza katika Lengo Namba 9. Uboreshaji wa miundombinu ya barabara, bandari, viwanja vya ndege kutawezesha kuongeza ufanisi kwa sekta nyingine na kufikia malengo ya kitaifa. Kwa muktadha huo, Kamati ya Kudumu ya Miundombinu itaendelea kuwa mstari wa mbele kusimamia sekta hizo kwa uadilifu ili Bunge lako Tukufu liweze kuwa chachu ya maendeleo ya nchi husika kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kuongoza vema Bunge hili kwa kusaidiana na Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge, na kwa namna ambavyo umekuwa ukitoa ushirikiano wa kutosha katika utekelezaji wa majukumu ya Kamati. Aidha, nitumie fursa hii kuwashukuru sana Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu ambao wametoa maoni, ushauri na ushirikiano uliowezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na hatimaye kukamilika kwa taarifa hii, kwa umuhimu wao katika utekelezaji wa majukumu ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati, naomba nitumie fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Prof. Makame Mnyaa Mbarawa, Mbunge na Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, akisaidiwa na Naibu Mawaziri Mheshimiwa Mhandisi Geofrey Msongwe Kasekenya Mbunge – Sekta ya Ujenzi, na Mheshimiwa Atupele Fredy Mwakibete Mbunge – Sekta ya Uchukuzi kwa ushirikiano ambao wameipatia Kamati katika kipindi chote cha uchambuzi wa bajeti. Aidha, nawashukuru watendaji wote wa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, pamoja na taasisi zake wakiongozwa na Makatibu Wakuu Balozi Mhandisi Aisha S. Amour – Sekta ya Ujenzi na Bw. Gabriel J. Migire – Sekta ya Uchukuzi kwa kuendelea kutoa ushirikiano kwa Kamati kila mara na walipohitajika kufanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndugu Nenelwa Mwihambi, *ndc*. kwa kuratibu vema shughuli za Kamati na Shughuli za Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo haya, sasa naliomba Bunge lako likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha, na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**22 MEI, 2023**

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**SEHEMU YA KWANZA**

**1.0 UTANGULIZI**
**1.1 Maelezo ya Awali**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 Pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu nne zifuatazo: -

a) Sehemu ya Kwanza ni Utangulizi ambayo inajumuisha maelezo ya jumla, muundo wa taarifa, pamoja na ufafanuzi wa namna Kamati ilivyotekeleza majukumu yake;

b) Sehemu ya Pili ni Uchambuzi na Tathimini ya Utekelezaji wa Majukumu ya Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023; pamoja na Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024;

c) Sehemu ya Tatu ni Maoni na Ushauri wa Kamati; na

d) Sehemu ya Nne ni Hitimisho.

**1.2 Namna Kamati Ilivyotekeleza Majukumu Yake**
**Mheshimiwa Spika**, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, hutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia

masharti mbalimbali yaliyoainishwa katika Katiba, Sheria mbalimbali pamoja na Kanuni za Kudumu za Bunge.

**Mheshimiwa Spika,** katika kufanyia kazi utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Kamati ilifanya mambo yafuatayo: -

a) Kupokea na kufanya uchambuzi wa randama ya Wizara (Kanuni ya 115 (1));

b) Kupokea taarifa na kukagua utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha katika mwaka wa Fedha 2022/2023 (Kanuni ya 117 (1));

c) Kujadili taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara pamoja na taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023; na

d) Kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara pamoja na taasisi zake kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 UCHAMBUZI NA TATHIMINI YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 PAMOJA NA UCHAMBUZI WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

### 2.1 Msingi wa Uchambuzi

**Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 63 (3) (b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 inalipa Bunge madaraka ya kujadili utekelezaji wa kila Wizara wakati wa Mkutano wa Bunge wa kila mwaka wa bajeti. Kwa muktadha huo, Kanuni ya 118 (4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge imeweka masharti kwa Kamati za Kisekta kufanya uchambuzi

wa taarifa za utekelezaji na makadirio ya mapato na matumizi za Wizara kabla ya kujadiliwa Bungeni.[1]

## 2.2 Mawanda ya Uchambuzi

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia msingi wa uchambuzi, Kamati ilichambua taarifa za utekelezaji wa mafungu mawili ya kibajeti ya Wizara ambayo ni **Fungu 98** – Sekta ya Ujenzi na **Fungu 62** – Sekta ya Uchukuzi kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 na kufanya ulinganisho na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo, pamoja na taasisi zilizo chini yake kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (2). Katika ulinganisho huo, Kamati ilitathimini mwenendo wa makusanyo ya maduhuli, na upatikanaji wa fedha za matumizi ya kawaida na za maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

**Mheshimiwa Spika**, katika kutathimini utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo, kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (1), Kamati ilifanya ziara ya ukaguzi ili kujionea utekelezaji wa miradi iliyo chini ya Wizara iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha 2022/2023. Katika hatua hii, Kamati ilifanya tathimini kuhusu hali ya upatikanaji wa fedha, ufanisi wa utekelezaji wa miradi husika pamoja na tija ambayo inapatikana katika miradi hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati pia umezigusa taasisi zilizo chini ya Wizara ambazo ni: -

***Sekta ya Ujenzi***

i. Wakala wa Barabara (TANROADS);
ii. Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA);
iii. Wakala wa Majengo Tanzania (TBA);
iv. Bodi ya Usajili ya Wahandisi (ERB);
v. Tasisi ya Teknolojia ya Ujenzi (ICoT);
vi. Bodi ya Mfuko wa Barabara (RFB);
vii. Baraza la Taifa la Ujenzi (NCC);
viii. Bodi ya Usajili wa Wabunifu Majengo na WakadiriajiMajenzi (AQRB);

[1] Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari 2023

ix. Bodi ya Usajili wa Makandarasi (CRB); na

x. Bodi ya Usajili ya Wahandisi (ERB);

*Sekta ya Uchukuzi*

i. Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA);
ii. Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA);
iii. Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC);
iv. Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA).
v. Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA)
vi. Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA);
vii. Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (TAA);
viii. Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL);
ix. Shirika la Reli Tanzania (TRC);
x. Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL);
xi. Kampuni ya Uendelezaji wa Viwanja vya Ndege ya Kilimanjaro (KADCO);
xii. Kampuni ya Meli ya Tanzania na China (SINOTASHIP)
xiii. Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT);
xiv. Chuo cha Bahari Dar es Salaam (DMI);
xv. Baraza la Watumiaji wa Huduma za Usafiri wa Anga (TCAA-CCC); na
xvi. Baraza la Watumiaji wa Huduma za Usafiri Ardhini (LATRA - CCC).

**2.3 Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara kwa Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2022/2023**

**2.3.1 Malengo ya Utekelezaji**

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, Kamati ilifanya tathimini ya utekelezaji wa majukumu ya msingi ya Wizara ambayo yalijikita katika maeneo yafuatayo: -

**<u>Sekta ya Ujenzi</u>**

a) Kusimamia utekelezaji wa Sera ya Ujenzi (2003) pamoja na Sera ya Taifa ya Usalama Barabarani (2009);

b) Ujenzi, ukarabati na matengenezo ya barabara, madaraja na vivuko;

c) Ujenzi na uendelezaji wa miundombinu ya viwanja vya ndege;

d) Ujenzi na ukarabati wa nyumba na majengo ya Serikali;

e) Usimamizi wa masuala ya ufundi na umeme;

f) Usimamizi wa shughuli za ukandarasi, uhandisi, ubunifu majengo na ukadiriaji majenzi;

g) Usimamizi wa maabara za vifaa vya ujenzi;

h) Usimamizi wa masuala ya usalama barabarani na mazingira katika Sekta;

i) Uboreshaji, utendaji na uendelezaji wa watumishi wa Sekta; na

j) Usimamizi wa majukumu ya taasisi zilizo chini ya Sekta.

**<u>Sekta ya Uchukuzi</u>**

a) Kusimamia utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uchukuzi (2003);
b) Ujenzi na uendelezaji wa miundombinu ya reli na bandari;
c) Usafiri na usafirishaji kwa njia ya anga, reli na bandari;
d) Utoaji wa leseni za usafirishaji;
e) Usalama katika usafirishaji;
f) Usimamizi wa huduma za hali ya hewa;
g) Kuendeleza rasilimali watu katika Sekta ya Uchukuzi; na
h) Kusimamia Taasisi na Mashirika ya Umma yaliyo chini ya Sekta ya Uchukuzi.

**Mheshimiwa Spika**, katika kufanya uchambuzi wake, Kamati pia imezingatia masuala muhimu kama vile Mpango wa Taifa wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2021/2022 - 2025/2026, Ilani ya Chama cha Mapinduzi (CCM) pamoja na Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs Lengo Na. B9) ambalo linasisitiza masuala ya viwanda ubunifu na miundombinu.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati pia ilitathimini vipaumbele vilivyozingatiwa na Wizara katika mgawanyo wa fedha za kutekeleza miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2022/2023, ambapo adhima ilikuwa ni kukamilisha miradi inayoendelea pamoja na kutekelea miradi mipya kama ifuatavyo: -

a) Miradi iliyoanishwa kwenye ilani ya uchaguzi ya chama cha mapinduzi ya mwaka 2020;
b) Miradi iliyoanishwa kwenye mpango wa tatu wa taifa wa maendeleo wa miaka mitano (2021/2022 – 2025/26);
c) Miradi iliyo kwenye ahadi mbalimbali za viongozi wa Serikali;
d) Miradi ambayo washirika wa maendeleo wameonesha nia ya kutoa fedha za utekelezaji ambapo Serikali inawajibika kutoa mchango wake *(Counterpart Fund)*;
e) Miradi ya kimkakati inayohusu barabara, madaraja, viwanja vya ndege na vivuko (kama vile ulinzi wa mipakani pamoja na barabara zinazoingia na kutoka kwenye maeneo ya kimkakati);
f) Miradi ya barabara zinazokwenda kwenye vituo vya reli ya Kisasa (SGR);
g) Miradi ya barabara ambayo imekuwa ikipendekezwa na bodi za barabara za mikoa; na
h) Miradi ya makao makuu ya Jiji la Dodoma (kama vile *Dodoma Outer Ring Roads*, Uwanja wa Ndege wa Msalato, nyumba za watumishi wa umma na majengo ya Serikali.

### 2.3.2 Utekelezaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa Sekta ya Ujenzi, Kamati ilitoa maoni kwa maeneo ambayo bado hayajatekelezwa kikamilifu au utekelezaji wake bado unaendelea ambapo Kamati imeendelea kuishauri Serikali kuongeza fedha katika ujenzi wa miradi ya barabara na matengenezo. Kamati inaendelea kusisitiza kuwa Serikali ianze kutumia mfumo wa **PPP** na **EPC+F** katika ujenzi wa barabara zake ili kuwezesha barabara nyingi kujengwa na kufanyiwa matengenezo na hivyo basi, Serikali itafute vyanzo vya kutunisha Mfuko wa Barabara.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa Sekta ya Uchukuzi, Kamati inaendelea kuisisitiza Serikali kuharakisha mchakato wa marekebisho ya sheria mbalimbali ili kuruhusu wawekezaji binafsi katika uendeshaji wa reli na bandari nchini.

### 2.3.3 Hali ya Upatikanaji wa Fedha

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha2022/2023, Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi iliidhinishiwa jumla ya **Sh. 3,866,616,675,800**. Kati ya fedha hizo, **Sh. 1,465,835,235,800** zilikuwa ni kwa ajili ya **Fungu 98** - Sekta ya Ujenzi na **Sh. 2,400,781,440,000.00** ziliidhinishwa kwa ajili ya **Fungu 62** - Sekta ya Uchukuzi.

**Mheshimiwa Spika**, katika Sekta ya Ujenzi, kati ya Bajeti iliyotengwa, **Sh. 44,293,050,800** zilikuwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, na Sh. **1,421,542,185,000** zilikuwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia Februari, 2023, kiasi cha fedha za Matumizi ya Kawaida kilichopokelewa kwa Sekta ya Ujenzi ni Shilingi **Bilioni 25.9** sawa na **asilimia 58.49** ya bajeti iliyoidhinishwa, wakati Miradi ya Maendeleo ilipokea **Shilingi Trilioni 1.22** sawa na **asilimia 85.87** ya bajeti iliyoidhinishwa.

**Mheshimiwa Spika**, katika Sekta ya Uchukuzi, kati ya Bajeti iliyotengwa, **Sh. 94,546,502,000** zilikuwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, na **Sh. 2,306,234,938,000** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia Februari 2023, kiasi cha fedha za Matumizi ya Kawaida kilichopokelewa kwa Sekta ya Uchukuzi ni **Shilingi Bilioni 57.99** sawa na **asilimia 61.33** ya bajeti iliyoidhinishwa wakati Miradi ya Maendeleo ilipokea **Shilingi Trilioni 1.38** sawa na **asilimia 59.83** ya bajeti iliyoidhinishwa.

**Mheshimiwa Spika**, Kielelezo Na. 1 kinatoa picha halisi ya Hali ya Mapokezi ya Fedha kwa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kufikia Februari, 2023.

Kielelezo Na. 1 – **Hali ya Mapokezi ya Fedha Kufikia Februari, 2023**

| **FUNGU LA BAJETI** | **BAJETI YA 2022/2023** | | **MAPOKEZI KUFIKIA FEBRUARI, 2023** | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | MATUMIZI YA | MIRADI YA MAENDELE | MATUMIZI YA | ASILIMIA | MIRADI YA MAENDELE | ASILIMIA |

| | KAWAIDA (TZS) | O (TZS) | KAWAIDA (TZS) | YA MAPOKEZI | O (TZS) | YA MAPOKEZI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Fungu 98 - **UJENZI** | 44,293,050,800 | 1,421,542,185,000 | 25,907,022,882 | 58.49 % | 1,220,709,739,203 | 85.87 % |
| Fungu 62 - **UCHUKUZI** | 94,546,502,000 | 2,306,234,938,000 | 57,990,000,000 | 61.33 % | 1,380,000,000,000 | 59.83 % |

**Mheshimiwa Spika**, kwa wastani, hali ya mapokezi ya fedha kwa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kufikia Februari, 2023 ilikuwa ni ya kuridhisha. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kutoa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii.

### 2.3.4 Makusanyo ya Maduhuli

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi pamoja na taasisi zilizo chini yake ilidhinishiwa kukusanya jumla ya **Sh. 2,350,489,883,978**. Hadi kufikia Februari, 2023, makusanyo yalikuwa **Sh. 1,422,868,862,230** sawa na **asilimia 60.53** ya malengo. Kielelezo Na. 2 kinatoa mchanganuo wa makusanyo hayo ukilinganisha na malengo yaliyowekwa kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

**Kielelezo Na. 2 -** Makusanyo Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi Kufikia Februari, 2023

| TAASISI | MAKADIRIO YA MAKUSANYO 2022/2023 (TZS) | MAKUSANYO KUFIKIA FEBRUARI 2023 (TZS) | ASILIMIA YA MAKUSANYO (%) |
|---|---|---|---|
| **Fungu 98** – SEKTA YA UJENZI | | | |
| Wizara | 70,000,000 | 104,060,000 | 148.65% |
| **Fungu 62** – SEKTA YA UCHUKUZI | | | |
| LATRA | 35,100,000,000 | 20,638,842,397 | 58.8% |
| TCAA | 85,100,250,748 | 54,414,801,779 | 63.94% |
| TMA | 18,970,000,000 | 7,167,287,785 | 37.78% |
| TASAC | 63,860,000,000 | 40,730,319,181 | 63.78% |
| TPA | 1,424,405,141,301 | 869,979,657,310 | 67.07% |
| MSCL | 9,293,594,205 | 4,263,234,400 | 45.87% |
| TAA | 85,055,000,000 | 46,250,941,330 | 54.37% |
| ATCL | 341,509,000,000 | 252,924,078,568 | 74.06% |
| KADCO | 24,394,840,937 | 22,150,744,724 | 90.8% |
| TRC | 83,988,244,246 | 34,717,147,377 | 41.33% |
| TAZARA | 120,000,000,000 | 40,638,459,151 | 33.86% |
| NIT | 27,889,545,000 | 12,070,543,139 | 43.27% |
| DMI | 12,307,997,958 | 4,397,642,507 | 35.72% |
| SINOTASHIP | 18,546,269,583 | 12,388,102,583 | 66.79% |
| **JUMLA KUU** | **2,350,489,883,978** | **1,422,868,862,230** | **60.53%** |

**Mheshimiwa Spika,** kwa ujumla mwenendo wa makusanyo ya Wizara ni wa kuridhisha. Hata hivyo, Kamati imebaini kwamba, baadhi ya taasisi zilizo chini ya Sekta ya Uchukuzi zina mwenendo wa makusanyo usioridhisha. Taasisi hizo ni DMI, NIT, TMA, TRC, TAZARA, MSCL, LATRA na TAA.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Serikali kuzingatia malengo yaliyowekwa katika ukusanyaji wa mapato na pia makadirio ya

makusanyo yaendane na uhalisia wa vyanzo vilivyopo pamoja na uwezo wa kila taasisi kukusanya.

### 2.3.5 Tathimini ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika,** katika vikao vilivyofanyika mwezi Machi, 2023, Kamati ilifanya tathimini na kutembelea baadhi ya miradi ya maendeleo inayotekelezwa na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi katika mikoa ya Morogoro na Dar es Salaam kati ya tarehe 14 – 31 Machi, 2023.

**Mheshimiwa Spika**, miradi iliyotembelewa na kukaguliwa na Kamati katika Sekta ya Ujenzi ni: -

a) Mradi wa Ujenzi na Ukarabati wa Vivuko, Maegesho na Karakana unaotekelezwa na **TEMESA -** Mradi Na. 4125**;**
b) Mradi wa Ujenzi wa Miundombinu ya Viwanja vya Ndege - **Mradi Na. 6001**;
c) Mradi wa Ujenzi wa Barabara na Madaraja unaotekelezwa na TANROADS - Mradi **Na. 2005;**
d) Mradi wa Ujenzi wa Nyumba na Majengo ya Serikali unaotekelezwa na TBA - **Mradi Na. 6327**; na
e) Mradi wa Ujenzi wa Miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya II (BRT II) unaotekelezwa na TANROADS - **Mradi Na. 4285**.


**Mheshimiwa Spika**, miradi iliyotembelewa na kukaguliwa na Kamati katika Sekta ya Uchukuzi ni: -

a) Mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR) kipande cha Dodoma - Morogoro - Dar es Salaam - **Mradi Na. 4281;**
b) Karakana ya Ukarabati wa Vichwa vya Treni Morogoro
c) Mradi wa Uboreshaji Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) - **Mradi Na. 6377**;
d) Kituo cha mafunzo ya usafiri wa anga – TCAA;
e) Uendeshaji wa Jengo la Tatu la Abiria (Terminal III) Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere Dar es Salaam - **Mradi Na. 6267;**
f) Ujenzi na Ukarabati wa Bandari.

*Miradi ya Sekta ya Ujenzi*

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi iliidhinishiwa jumla ya **Sh. 1,421,542,185,800** kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo katika **Fungu 98** – Sekta ya Ujenzi, ambapo kati ya fedha hizo, Sh. **1,168,576,368,000** ni Fedha za Ndani na Sh. **252,965,817,000** ni Fedha za Nje.

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia mwezi Februari, 2023 jumla ya Sh. **1,220,709,739,202.75** sawa na asilimia **70** ya lengo zilipatikana. Kati ya fedha zilizopatikana Sh. **243,321,354,392.84** ni fedha za nje sawa na asilimia **96** ya lengo na Sh. **977,388,884,205.69** fedha za ndani sawa na asilimia **66.** Fedha za ndani zilizopatikana zinajumuisha Sh. **573,494,884,809.69** za Mfuko wa Serikali na Sh. **403,893,500,604.22** ni za Mfuko wa Barabara.




*Miradi ya Ujenzi wa Barabara na Madaraja*

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2022/23, Wizara ilitengewa Sh. **1,421,542,185,000** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya barabara, madaraja na viwanja vya ndege. Kati ya fedha hizo, Fedha za Ndani ni Sh. **1,168,576,368,000** na Sh. **252,965,817,000** ni fedha za nje. Fedha za ndani zilijumuisha fedha za Mfuko Mkuu wa Serikali Sh. **568,819,900,200** na fedha za Mfuko wa Barabara Sh. **599,756,467,800.**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitembelea ujenzi wa barabara njia nane kuanzia Kimara – Kibaha ambao umegharimu

Sh.**161,487,041,473.77** (bila VAT) na utekelezaji wake umefikia asilimia **98.** Taarifa ilieleza kuwa mradi huu ulitarajiwa kukamilika ifikapo tarehe 15 Aprili 2023.

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia tarehe 15 Machi 2023, taarifa ya utekelezaji wa miradi mingine ya barabara ni kama ifuatavyo: -

a) Ujenzi na ukarabati wa barabara kuu kwa kiwango cha lami umekamilika kwa asilimia **40;**

b) Barabara za mikoa jumla ya kilometa 23.11 kati ya kilometa 103.10 za barabara za mikoa sawa na asilimia **22.43** zimejengwa kwa kiwango cha lami. Aidha, kilometa 253.67 kati ya kilometa 1,042.43 za barabara za mikoa sawa na asilimia **24.33** ya lengo la mwaka zilifanyiwa ukarabati kwa kiwango cha changarawe;

c) Ujenzi wa madaraja makubwa 3 ulikuwa umekamilika ambayo ni Daraja la Gerezani (Dar es Salaam), Daraja la Kigongo – Busisi (Mwanza) limefikia asilimia **70** na Daraja la Pangani ujenzi wake umeanza; na

d) Jumla ya madaraja madogo 40 sawa na asilimia **125** ya mpango ni barabara za mikoa yamejengwa kwa kutumia fedha za Mfuko Mkuu wa Serikali. Aidha, madaraja madogo 26 sawa na asilimia **60** ya mpango wa mwaka yamejengwa kwa fedha za mfuko wa barabara. Kwa ujumla utekelezaji wa ujenzi wa madaraja madogo ni asilimia **88.**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini changamoto zifuatazo: -

a) Ujenzi wa barabara kuu, mikoa na matengenezo umekuwa chini ya malengo;
b) Changamoto ya kuharibika kwa barabara ndani ya muda mfupi baada ya ujenzi;
c) Changamoto ya gharama kuongezeka kabla ya ujenzi kukamilika;
d) Malalamiko kuhusu uwepo wa vituo vya mafuta ndani ya hifadhi ya barabara;
e) Ucheleweshaji wa fedha kwa ajili ya malipo ya wakandarasi na wahandisi washauri wa miradi inayogharimiwa kwa fedha za Serikali;

f) Barabara za mikoa zinatengewa fedha kidogo na hivyo kutovutia makandarasi kuomba kazi za ujenzi;
g) Changamoto ya maji ya mvua kujaa kwenye makazi ya watu;
h) Wananchi wengi hawatumii vivuko vya madaraja ya juu kutokana na sababu mbalimbali na kuhatarisha usalama wao;
i) Wizi wa vifaa;
j) Upungufu wa watumishi na majengo ya ofisi kwani wakala imeanzisha ofisi katika mikoa mipya kwa kupanga;
k) TANROADS Kutokusimamia tozo kwa wakandarasi wanaochelewesha miradi; na
l) Mamlaka ya mapato Tanzania (TRA) huchelewa kutoa kibali cha kuongeza muda wa hati za misamaha ya kodi ya ongezeko la thamani (VAT) kwa Wakandarasi.

***Ujenzi wa Miundombinu ya Barabara ya Mabasi Yaendayo Haraka Dar es Salaam (BRT)***

**Mheshimiwa Spika**, mradi huu una jumla ya Kilometa 148.7 na umegawanyika katika awamu sita, ambapo awamu ya kwanza ya ujenzi tayari imeshakamilika.

**Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa mradi unaendelea ambapo tayari malipo mbalimbali yamefanyika kama ifuatavyo: -

a) Mkandarasi wa Lot 1 ameshaidhinishiwa malipo jumla ya Sh. **188,717,312,137;**

b) Jumla ya **Sh. 182,468,333,765** kupitia hati za malipo Na. 1 hadi 23 zimeshalipwa kwa Mkandarasi;

c) Malipo ambayo bado hayajalipwa ni **Sh. 6,248,978,371.81** kwa Hati ya Madai Na. 24 ambayo yapo kwenye mchakato wa kulipwa; na

d) Mpaka sasa mkandarasi wa **Lot 2** ameshalipwa jumla ya **Sh. 40,532,661,155** kwa hati za malipo namba 1 hadi 14.

**Mheshimiwa Spika**, katika utekelezaji wa Mradi, Kamati imebaini kwamba: -

a) Hadi sasa mradi (Lot 1) umeajiri takribani watumishi 1,117 ambapo 1,041 kati yao ni Watanzania sawa na asilimia 93;

b) Ujenzi umefikia asilimia 89.9 ukilinganisha na asilimia 50 kipindi kama hiki mwaka ulioisha wa 2022;

c) Mradi umerahisisha usafiri kwa wakazi wa Dar es salaam; na

d) Kuokoa muda uliosababishwa na msongamano wa magari barabarani.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati pia imebaini kuwepo kwa changamoto mbalimbali katika utekelezaji wa mradi huu kama zifuatavyo: -

a) Mkandarasi amechelewa kukamilisha kazi ndani ya muda wa mkataba, yaani tarehe 27 Machi 2023 na kuomba nyongeza ya muda;

b) Kuongezeka wa gharama ya mkataba kwa **asilimia 16.7** kutoka **Sh. bilioni 217.48** ya awali hadi **Sh. bilioni 253.91;**

c) Daraja jipya la Kigogo kwenye barabara ya Kawawa, Ujenzi wa vituo vya mabasi na madaraja ya juu vimeshindwa kutekelezwa kutokana na ufinyu wa bajeti na mabadiliko ya usanifu;

d) Wizi wa vifaa; na

e) Kukosekana kwa umakini wa mkandarasi katika ubora wa kazi ya zege la barabara.

***Mradi wa Ujenzi na Ukarabati wa Maegesho na Vivuko***

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, Serikali kupitia TEMESA ilipanga kufanya ujenzi na ukarabati wa maegesho, ununuzi wa vivuko vipya 6, ukarabati wa vivuko na ujenzi wa miundombinu ya vivuko mbalimbali. Kwa mfano, Serikali ilipanga kufanya upanuzi wa eneo la maegesho ya Kigamboni katika kivuko cha Magogoni - Kigamboni mkoani Dar es Salaam,

ukarabati na ujenzi wa maegesho sita (6) ya vivuko (Magogoni – Kigamboni, Kilambo - Namoto, Utete - Mkongo, na maeneo mengine).

**Mheshimiwa Spika**, katika utekelezaji wa mradi huu Kamati imebaini mambo yafuatayo: -

a) Hadi Februari, 2023, ujenzi wa miundombinu ya Mwaya – Kajunjumele upo katika hatua za mwisho za utekelezaji na ujenzi wa miundombinu ya Mlimba – Malinyi eneo la Kikove Wilaya ya Ulanga unaendelea;

b) Upanuzi wa jengo la abiria katika maegesho ya Magogoni – Kigamboni upande wa Kigamboni umekamilika;

c) Upanuzi wa jengo la abiria katika maegesho ya Magogoni – Kigamboni upande wa Kigamboni Jijini Dar es Salaam umekamilika kwa awamu ya Kwanza;

d) Ujenzi wa Maegesho ya Mayenzi – Kanyinya, Ijinga – Kahangala na Bwiro – Bukondo yanaendelea kujengwa yakiwa katika hatua mbalimbali; na

e) Ukarabati mkubwa wa vivuko vya MV Kazi, MV TEMESA, MV Musoma, MV Tanga na MV Sabasaba umekamilika.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kuwepo kwa changamoto zinazoikabili TEMESA ambazo ni pamaja na: -

a) Madeni ya **Sh. bilioni 454.288** ambayo TEMESA wanazidai Taasisi za Serikali;
b) Wakala unadaiwa **Sh. bilioni 49.710**;
c) Kupanda kwa gharama za uendeshaji wa vivuko na kutopatikana kwa wakati vipuri vya vivuko;
d) Upungufu wa watumishi;
e) Baadhi ya vivuko kuwa na eneo finyu la watumiaji na hivyo kusababisha usumbufu (Mfano Kivuko cha Kigamboni); na
f) Kuchelewa kutolewa ufafanuzi pindi kunapotokea jambo linalohitaji ufafanuzi kwa jamii.

***Miradi ya Ujenzi wa Nyumba na Majengo ya Serikali***

**Mheshimiwa Spika**, Wizara inatekeleza miradi ya ujenzi wa nyumba na majengo ya Serikali katika maeneo mbalimbali nchini. Kamati imebaini kwamba miradi hiyo iko katika hatua tofauti za utekelezaji zifuatazo: -

a) Ujenzi wa ghorofa za watumishi wa umma za Temeke Kota umefikia asilimia **8**;

b) Ujenzi wa nyumba 20 za viongozi wa Serikali katika mkoa wa Dodoma kwa awamu ya kwanza umekamilika na ujenzi wa nyumba 20 nyingine upo katika hatua za maandalizi;

c) Umaliziaji wa ujenzi wa nyumba tano (5) za majaji Tanzania Bara katika mkoa wa Tabora, Kilimanjaro, Shinyanga na Mtwara umekamilika. Aidha, mkoa wa Kagera utekelezaji wa mradi umefikia asilimia **40;**

d) Ujenzi wa nyumba 150 za watumishi jijini Dodoma kwa awamu ya kwanza umefikia asilimia **85;**

e) Ujenzi wa jengo la Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi katika mji wa Serikali Mtumba Jijini Dodoma umefikia asilimia **58**; na

f) Ujenzi wa ghorofa za watumishi wa umma katika eneo la Magomeni Kota awamu ya pili "Block" A umekamilika. Kwa upande wa "Block" B utekelezaji wa mradi umefikia asilimia **27**.

**Mheshimiwa Spika**, tarehe 18 Machi, 2023 Kamati ilitembelea na kukagua maendeleo ya mradi wa ujenzi wa Temeke Kota. Kamati ilielezwa kuwa, mradi huu unahusisha ujenzi wa majengo saba [7] yenye ghorofa tisa [9] ambapo kila jengo litakuwa na uwezo wa kubeba kaya 144.

**Mheshimiwa Spika**, mradi huu unatekelezwa kwa fedha za ruzuku kutoka Serikali kuu kwa gharama ya Sh. **19,426,566,061.74** kwa jengo moja. Ujenzi wa mradi ulianza tarehe 25 Oktoba, 2022 na unatarajiwa kukamilika tarehe 24 Oktoba, 2024 ambapo hadi

Kamati inatembelea eneo la mradi, ujenzi ulikuwa umefikia asilimia **8**.

**Mheshimiwa Spika,** napenda kulitaarifu Bunge lako kwamba, miradi ya Ujenzi wa Nyumba na Majengo ya Serikali imeonesha mafanikio mbalimbali kama vile: -

a) kuzalisha fursa mbalimbali za ajira kwa wataalam wa ujenzi, mafundi, wazalishaji, wauzaji na wasambazaji wa vifaa vya ujenzi, watoa huduma kama vile baba na mama lishe;

b) Vifaa vingi vya ujenzi vimetumika kutoka viwanda vyetu vya ndani ikiwemo nondo, saruji, marine, mabomba na vifaa vinginevyo;

c) Wahitimu kutoka VETA na wanafunzi mbalimbali wa fani za ujenzi wameomba kupata mafunzo ya vitendo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kuwepo kwa changamoto zifuatazo: -

a) Kuchelewa kulipwa madeni kutoka taasisi za serikali;
b) Ongezeko la gharama kwenye miradi inayotekelezwa kwa fedha za ruzuku ya Serikali na mapato ya ndani;
c) Kucheleweshwa kulipwa fedha kwa baadhi ya washitiri;
d) Upungufu wa watumishi;
e) Changamoto ya uvamizi wa ardhi ya TBA isiyokuwa na hati miliki;
f) Kutokuwa na sheria inayoruhusu uwekezaji kutoka sekta binafsi; na
g) Uwepo wa matukio mbalimbali ya wizi kwenye maeneo ya mradi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitaarifiwa kwamba, miradi mingine iliyopangwa kutekelezwa ni pamoja na ujenzi wa nyumba za viongozi wa Serikali katika mkoa wa Dodoma, ujenzi wa nyumba za makazi 150 za watumishi wa umma - Jiji la Dodoma, ujenzi wa jengo la ofisi ya Wizara ya ujenzi na uchukuzi, na ujenzi wa ghorofa za makazi ya watumishi wa umma katika eneo la Magomeni Kota - Dar es Salaam.

**Miradi ya Viwanja vya Ndege**

**Mheshimiwa Spika**, mradi huu ulitengewa jumla ya Sh.**86,102,526,000**. Kati ya fedha hizo, Sh. **54,955,206,000** ni fedha za ndani na Sh. **31,147,320,000** ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kulitaarifu Bunge lako tukufu kwamba, Serikali imetekeleza miradi katika maeneo mbalimbali nchini. Miradi hiyo imefikia hatua mbalimbali za utekelezaji na kuonesha mafanikio kama ifuatavyo: -

a) Katika Mkoa wa Geita, kazi ya ujenzi wa barabara ya kurukia na kutua ndege barabara za viungio zimekamilika. Aidha, katika Mkoa wa Mtwara utekelezaji umefikia asilimia **96**, Musoma asilimia **43**, Iringa asilimia **42**, Songea asilimia **100,** Moshi asilimia **12**, Msalato Dodoma asilimia **14.50**;

b) Kuweza kusimamia shughuli za uendeshaji wa viwanja vya ndege nchini hasa katika kipindi cha mlipuko wa UVIKO -19.

c) Watendaji wa mamlaka kutumia muda mfupi kujifunza na kuelewa mifumo ya kisasa iliyosimikwa kwenye jengo ambayo haikuwa rafiki kwao;

d) Kutengeneza fursa mbalimbali za ajira kwa wazawa kupitia makampuni mbalimbali yanayopata kandarasi; na

e) Kuongeza hadhi ya kiwanja cha kimataifa cha Julius Nyerere kwa kuwa na mitambo ya kisasa inayopelekea kuvutia mashirika makubwa ya ndege duniani;

**Mheshimiwa Spika**, miradi inakabiliwa na changamoto zifuatazo: -

a) Ufinyu wa bajeti, uchakavu wa miundombinu, majengo, mitambo, na mifumo katika viwanja vya ndege unaohatarisha usalama wa ndege;

b) Kutokuwepo kwa sheria mama na mahususi kwa ajili ya usimamizi, uendeshaji na uendelezaji wa viwanja vya ndege Tanzania;

c) TANROADS kuendelea kujenga viwanja vya ndege badala ya TAA;

d) Changamoto ya usalama wa uwanja wa ndege wa mkoa Kagera; na

e) Upungufu wa watumishi.

**Miradi ya Usalama Barabarani na Mazingira**

**Mheshimiwa Spika**, mradi huu ulitengewa jumla ya Sh. 1,784,258,000. Katika mradi wa masuala ya usalama na mazingira Wizara (Ujenzi) ilitengewa Sh. 16,058,000 na Sh. 116,400,000 kwa ajili ya kuandaa mkakati wa kukabiliana na majanga.

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Februari, 2023, ufungaji wa vifaa vya kisasa vya upimaji uzito wa magari katika vituo vya mizani umefanyika katika mizani 10. Aidha, maandalizi ya uchapishaji wa nakala 1000 za mwongozo wa alama za barabarani na nakala 1000 za mwongozo wa ukaguzi wa usalama wa barabara upo katika utekelezaji.

***Miradi ya Kujengewa Uwezo***

**Mheshimiwa Spika,** lengo la mradi huu ni kujenga uwezo wa watumishi wa Sekta ya ujenzi kwa kuwapatia mafunzo kwa lengo la kuwaimarisha kitaaluma na kuwajengea uzoefu wa kazi. Kwa mwaka 2022/2023 mradi huu ulitengewa jumla ya Sh. milioni **273.74** fedha za ndani.

**Mheshimiwa Spika,** jumla ya watumishi 825 wa Wizara (Ujenzi) na taasisi zake wamehudhuria mafunzo.

***Taasisi ya Teknolojia ya Ujenzi (ICoT)***

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitembelea Chuo cha ICot Tawi la Morogoro mnamo tarehe 15 Machi, 2023 na kupokea taarifa. Chuo hiki kilitengewa Sh. **2,563,886,060.** Aidha, Sh. **1,500,000,000** fedha za maendeleo kutoka Wizara husika zillitengwa kwa ajili ya ujenzi wa jengo la taaluma na utawala. Hadi kufikia Februari, 2023

kiasi cha Sh. **1,267,670,546.74** sawa na asilimia **49** ya lengo zilipokelewa.

**Mheshimiwa Spika**, chuo hiki kimepata mafanikio yafuatayo: -

a) Kimesajili wanafunzi 74 ngazi ya astashahada; wanafunzi 66 wanaendelea na mafunzo kwa ngazi ya astashahada ya juu na stashahada, mafunzo ya ufundi stadi kwa ngazi ya VET yametolewa kwa wanafunzi 353 kati yao wanafunzi 160 wamehitimu, mafunzo ya muda mfupi yametolewa kwa wanafunzi 270;

b) Chuo kinaendelea na hatua za maandalizi ya ujenzi wa jengo jipya la taaluma na utawala ambapo utekelezaji upo katika hatua ya manunuzi; na

c) Taasisi inaendela na kufanya matengenezo ya miundombinu ya majengo, maji safi, maji taka na umeme.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini changamoto zifuatazo: -

a) Ufinyu wa bajeti;

b) Upungufu wa watumishi hasa wakufunzi;

c) Kukosekana kwa karakana zenye vifaa vya kisasa kwa ajili ya kutolea mafunzo;

d) Uchakavu wa miundombinu pamoja na upungufu wa vitendea kazi ikiwemo vitabu vya kufundishia, uchakavu na uchache wa magari pamoja na ukosefu wa maktaba ya kisasa; na


e) Taasisi kuwa changa na hivyo kutokujulikana kwa wadau walio wengi.

***Miradi ya Sekta ya Uchukuzi***

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa **Fungu 62** – Sekta ya Uchukuzi, zilitengwa Sh. **2,306,234,938,000** kutekeleza Miradi ya

Maendeleo, Sh. **2,192,771,662,000** zilikuwa ni Fedha za Ndani, na Sh. **113,463,316,000** ni Fedha za Nje.

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Februari, 2023, Sh. Trilioni **1.38** sawa na asilimia **67.85** ya bajeti iliyoidhinishwa zilitolewa. Kati ya fedha zilizotolewa, Sh. trilioni **1.35** ni fedha za ndani sawa na asilimia **66.31** ya bajeti iliyoidhinishwa na **Sh. bilioni 31.29** ni fedha za nje sawa na asilimia **1.53** ya bajeti iliyoidhinishwa.




***Mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR) – Mradi Na. 4281***

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2022/2023, mradi huu ulitengewa **Sh. Trilioni 1.11**. Lengo la mradi ni kukamilisha ujenzi wa Reli ya SGR kipande cha Dar es Salaam hadi Morogoro (Km 300), Morogoro hadi Makutupora (Km 422), Mwanza - Isaka (Km 341, Makutupora hadi Tabora (Km 368), Tabora hadi Kigoma (Km 506), na kukamilisha taratibu za manunuzi ya Mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa kipande cha Tabora hadi Isaka (Km 165).

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokea taarifa za utekelezaji wa mradi huu kama ifuatavyo: -

a) Jumla ya Sh. Trilioni **1.09** zilitolewa ikiwa ni sawa na asilimia **98.14** kwa kipindi cha robo tatu ya muda wa utekelezaji.

Kamati imebaini kuwa utoaji wa fedha katika mradi huu unaridhisha;

b) Kipande cha Dar es Salaam – Morogoro umefikia asilimia **97.94,** Morogoro - Makutupora asilimia **92.88**, Makutupora – Tabora asilimia **5.50,** Tabora – Isaka wenye thamani ya dola za marekani milioni **900.104** katika kipande hiki Tarehe 16 Agosti, 2022 mkandarasi alilipwa malipo ya awali ya Sh. bilioni **245.19** na ujenzi umefikia asilimia **1.64.** Mwanza - Isaka ujenzi umefikia asilimia **28.03** ya lengo;

c) Mabehewa 14 kati ya mabehewa 59 yaliwasili nchini tarehe 19 Novemba, 2022 na mabehewa 45 yalitarajiwa kuwasili mwezi Mei, 2023 imefikia asilimia 92. Utengenezaji wa vichwa vya treni vya umeme imefikia asilimia 36.8;

d) Jumla ya watumishi 480 wamepatiwa mafunzo ya uendeshaji wa reli ya SGR; na

e) Kwa kipande cha Tabora – Kigoma Serikali imelipa malipo ya awali ya Sh. bilioni **200** kwa mkandarasi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa kutoa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi. Aidha, Kamati inapongeza umakini wa Serikali katika kutekeleza masharti ya Mkataba ambayo yamesababisha kutoongezeka kwa gharama na kuokoa fedha.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na hayo, Kamati imebaini kuwepo kwa changamoto zifuatazo: -

a) kutokamilika kwa reli ya kisasa kipande cha kutoka Dar es Salaam – Morogoro – Dodoma – Makutupora (Lot 1&2) ikilinganishwa na lengo lililowekwa;

b) Kuchelewa kufika kwa mabehewa ya treni ya SGR ikilinganishwa na lengo lililowekwa ambapo ilitarajiwa kukamilika Februari, 2022;

c) Kutoimarika kwa Chuo cha Reli – Tabora; na

d) Kuchelewa kufanyika marekebisho ya sheria iliyoanzisha shirika la reli Tanzania.

***Miradi Inayotekelezwa na Mfuko wa Reli***

**Mheshimiwa Spika**, mfuko ulitengewa jumla ya Sh. bilioni **294.801.** Fedha za Mfuko zilizopokelewa ni jumla ya Sh. bilioni **187.33** sawa na asilimia **63.54** ambazo zinatumika kutekeleza miradi mbalimbali.

**Mheshimiwa Spika**, kamati ilipata nafasi ya kutembelea karakana iliyopo Morogoro na kuona ukarabati wa vichwa vya treni na mabehewa ya reli (MGR). Kamati ilitaarifiwa mambo yafuatayo:-

a) Ukarabati wa vichwa vya treni 9 aina ya 88U na vichwa saba (7) vya sogeza aina ya 64xx. Kazi imefikia asilimia 47 ya lengo;

b) Ukarabati wa reli ya MGR ya Tabora - Kigoma (Km 411), Kaliua- Mpanda (Km 210) na Tabora- Isaka- Mwanza (Km 385) mkataba wa Sh. bilioni 379.37 umesainiwa;

c) Mfuko wa reli MGR utekelezaji ni asilimia 63.54 ya lengo;

d) Ununuzi wa mabehewa ya abiria 22 (reli ya MGR) yamekamilika, mabehewa 245 ya mizigo zabuni ilitangazwa tarehe 10 Novemba, 2022 na kufunguliwa tarehe 4 Januari, 2023, na injini 10 manunuzi yanaendelea; na

e) Ukarabati wa mabehewa kumi (10) ya mizigo na mabehewa mawili (2) ya abiria kwa MGR umekamilika na kuanza kutoa huduma.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa kutoa fedha za kutosha ili kutekeleza mradi na kuendesha mradi huu kwa kutoruhusu ongezeko la fedha kabla ya mradi kuisha.

**Mheshimiwa Spika**, changamoto mbalimbali hususani katika reli ya MGR kama ifuatavyo: -

a) Miundombinu chakavu katika stesheni za MGR;

b) Changamoto ya maeneo korofi yanayosababisha uharibifu wa reli ya MGR hasa kipindi cha mvua nyingi;

c) Upungufu wa watumishi; na

d) Changamoto ya baadhi ya watumishi kuhujumu miundombinu ya reli.

***Mradi wa Uboreshaji wa Reli ya TAZARA***

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi bilioni 13.19** ambapo TAZARA ilipanga kufanya ukarabati wa mabehewa 14 ya abiria kwa ajili ya treni ya jiji la Dar es Salaam na mabehewa saba (7) ya abiria. Hadi kufikia Februari 2023, TAZARA imeendelea kuratibu ununuzi wa vifaa na mitambo kwa Kiwanda cha Kokoto - Kongolo, na ununuzi wa vipuri vya ukarabati wa mabehewa 14 ya abiria kwa ajili ya treni ya jiji la DSM na 7 kwa ajili ya Udzungwa.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na mafanikio hayo, Kamati imebaini kuwa sheria iliyoanzisha Shirika la Reli ya TAZARA haitoi nafasi kwa Tanzania kufanya uwekezaji na maboresho zaidi katika reli hiyo, kwa hiyo basi Kamati inashauri Serikali kufanya marekebisho katika sheria husika.

***Mradi wa Uboreshaji wa Bandari Tanzania***

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, mradi huu wa kimkakati unatekelezwa kwa gharama ya dola za kimarekani milioni 421. Kati ya fedha hizo dola za kimarekani milioni 345 ni mkopo kutoka benki ya dunia, dola milioni 12 kutoka DFID na dola milioni **64** ni mapato ya ndani ya Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA). Kati ya fedha hizo Sh. bilioni **100.11** zimetengwa kwa ajili ya Bandari ya Dar es Salaam.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini mafanikio yafuatayo: -

a) TPA imefanikiwa kurasimisha bandari 86 kutoka 66 zilizokuwa zinatambuliwa na Sheria ya Bandari;

b) TPA mapato yameongezeka kwa wastani wa **asilimia 106** sawa na Sh. Bilioni **48.857**;

c) Uchimbaji wa kina cha urefu wa mita 15.5 kazi umefikia asilimia **90**;

d) Ujenzi wa gati la kushushia magari 1-7 na yadi ya kuhudumia makasha yamekamilika kwa asilimia **100**;

e) Awamu ya pili ya uboreshaji wa bandari ya Tanga umefikia asilimia **95**;

f) Ujenzi wa barabara inayounganisha gati katika bandari ya Mtwara umefikia asilimia **85**;

g) Ujenzi wa bandari ya Kalema umefikia asilimia **99**; na

h) Kwa upande wa makasha, shehena ya kawaida imeongezeka asilimia **14.6**, idadi ya meli asilimia **27.7.**

**Mheshimiwa Spika**, changamoto zilizopo ni: -

a) Kuwepo kwa vipengele vya sheria ambavyo sio rafiki kwa wawekezaji kuja kuwekeza nchini;

b) Mahitaji makubwa ya uondoshaji wa shehena bandari ya DSM;

c) Uhaba wa mitambo na vifaa vya kuhudumia meli na shehena;

d) Ongezeko la mapato kutoendana na kasi ya uboreshaji;

e) Mrundikano wa shehena za nchi jirani;

f) Upungufu wa watumishi; na

g) Mifumo ya TEHAMA isiyotosheleza na kutokuwa na mfumo wa kuunganisha wadau *(Single Window System)*.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza TPA kwa kuongeza mapato na inashauri Serikali itathimini kuhusu uwekezaji wa sekta binafsi katika uendeshaji wa bandari nchini na mikataba iwe na manufaa kwa nchi.

***Mradi wa Ununuzi wa Rada, Vifaa na Ujenzi wa Miundombinu ya Hali ya Hewa***

**Mheshimiwa Spika**, mradi huu unatekelezwa na Mamlaka ya Hali ya Hewa (TMA) kwa lengo la kuboresha utabiri wa hali ya hewa nchini kwa kununua rada saba (7) na vifaa vya hali ya hewa pamoja na ujenzi wa miundombinu. Katika mwaka wa fedha 2022/2023 mradi ulitengewa jumla ya Sh. **bilioni 20.**

**Mheshimiwa Spika**, mafanikio katika mradi huu ni: -

a) Mamlaka imenunua na kufunga kompyuta maalum yenye uwezo mkubwa wa kuchakata data za hali ya hewa katika kiwanja cha ndege cha Julius Nyerere (JNIA);

b) Utengenezaji wa rada mbili (2) za mwisho kufikia asilimia **75;**

c) Ufungaji wa rada 2 zilizowasili nchini tarehe 6 Desemba, 2022 unaendelea katika mikoa ya Mbeya na Kigoma;

d) Ununuzi wa seti 20 za vifaa vya kupima joto la hali ya hewa visivyotumia zebaki vilivyofungwa katika vituo mbalimbali vya hali ya hewa nchini;

e) Ununuzi wa seti tano (5) za vifaa vya utambuzi wa matukio ya radi ambavyo vimefungwa katika maeneo ya Musoma, Mwanza, Bukoba, Tabora na Kibondo; na

f) Ununuzi wa mitambo mitatu (3) ya uangazi wa hali ya hewa katika bahari ya Hindi, mitambo miwili (2) ya uangazi wa anga la juu, vifaa 60 vya kupima mvua vinavyojiendesha vyenyewe.

**Mheshimiwa Spika**, mamlaka ina changamoto zifuatazo: -

a) Upungufu wa fedha kwani mradi ulipata Sh. bilioni **5.05** sawa na asilimia **25.26** ya lengo kwa kipindi cha robo tatu ya muda wa utekelezaji;

b) Mahitaji makubwa ya maendeleo ya sayansi na teknolojia ya masuala ya hali ya hewa kwani kuna mabadiliko ya hali ya hewa ikiwemo mvua kubwa, upepo mkali na mafuriko na kusababisha uharibifu wa miundombinu;

c) Changamoto ya kutolipwa madeni kwa wakati; na

d) Upungufu wa watumishi, miundombinu, vifaa vya kufundishia katika chuo cha hali ya hewa na uchache wa vituo vya kupima hali ya hewa.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inatoa rai kwa Serikali kuwa, mradi huu upewe fedha za kutosha.

***Mradi wa Uendeshaji wa Jengo la Tatu la Abiria (JNIA) na Maboresho ya Huduma Katika Viwanja Vya Ndege***

**Mheshimiwa Spika**, lengo la mradi huu ni kuwezesha uendeshaji wa jengo la tatu la abiria (TB III) katika kiwanja cha ndege cha JNIA kwa kulipia gharama za uendeshaji na kuweka miundombinu wezeshi katika viwanja vingine.

**Mheshimiwa Spika**, mradi huu ulitengewa Sh. Bilioni **17.30.** Hadi kufikia Februari, 2023 jumla ya Sh. bilioni **17.07** ikiwa ni sawa na asilimia **98.68** ya bajeti iliyotengwa zilitolewa.

**Mheshimiwa Spika**, mafanikio ya mradi ni ujenzi wa uzio wa usalama katika kiwanja cha ndege cha Dodoma ambao umefikia asilimia 38.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilielezwa changamoto zifuatazo: -

a) Baadhi ya viwanja, ndege zinashindwa kutua usiku kwa sababu ya kutokuwa na taa;

b) Kukosekana kwa sheria mahususi kwa ajili ya usimamizi, uendeshaji na uendelezaji wa viwanja vya ndege Tanzania;

c) Kukosekana kwa fedha za uendeshaji kwa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (TAA);

d) Upungufu wa watumishi katika kada ya marubani na wahandisi wa ndege;

e) Watumishi kukaimu kwa muda mrefu; na

f) Usalama mdogo wa viwanja vya ndege kunapotokea ajali na taharuki kwa wananchi pindi mamlaka inapotekeleza jaribio la uokoaji.

*Mradi wa Ununuzi wa Ndege (ATCL)*

**Mheshimiwa Spika**, lengo la mradi huu ni kuboresha huduma za Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL) ili iweze kutoa huduma za usafiri wa anga ndani ya nchi, kikanda na kimataifa kwa ufanisi na ushindani.

**Mheshimiwa Spika**, mradi huu ulitengewa bajeti ya **Sh. bilioni 353**. Hadi Februari, 2022, mradi huu umepokea **Sh. bilioni 27.01** sawa na asilimia **7.7.**

**Mheshimiwa Spika**, mafanikio ya mradi ni: -

a) Kampuni inaendelea kufuatilia hatua za uundaji wa ndege mpya 4 ambazo zinaendelea na zitawasili kwa nyakati tofauti; na

b) Ndege ya mizigo imeshawasili nchini tarehe 31 Machi, 2023.

**Mheshimiwa Spika,** changamoto za mradi huu ni: -

a) Kuharibika kwa ingini 2 za ndege za ATCL na kupunguza malengo yaliyokusudiwa ya ununuzi wa ndege;

b) Gharama kubwa za uendeshaji mfano kukodisha ndege za Serikali kwa ATCL na mzigo mkubwa wa madeni unaoikabili ATCL;

c) Mzigo wa madeni kwa ATCL; na

d) Upungufu wa wataalam kwenye sekta ya anga.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa jitihada ya kufufua Kampuni hii kwa ununuzi wa ndege tano (5) za abiria na mizigo.

***Mamlaka ya Usafiri wa Anga TCAA***

**Mheshimiwa Spika,** mamlaka inatoa huduma za uongozaji ndege kupitia vituo vya Dar es Salaam, Zanzibar, Mwanza, Arusha, Pemba, Tabora, Kigoma, Dodoma, Iringa, Songwe, Mtwara, Tanga, Songea na Kilimanjaro.

**Mheshimiwa Spika,** TCAA imefanya usimikaji wa rada za kuongozea ndege katika vituo vya Dar es Salaam, Kilimanjaro, Mwanza na Songwe kwa gharama ya **Sh. bilioni 67.3,** mtambo wa kuwezesha ndege kutua kiwanja cha Abeid Amani Karume kwa **Sh. bilioni 4.6,** ukarabati manara wa kuongoza ndege Pemba kwa **Sh.milioni 300,** JNIA kwa dola za kimarekani **698,960,** kifaa cha mawasiliano kati ya marubani na mwongoza ndege kwa **Euro 705,000,** kuandaa michoro na uhakiki katika viwanja kwa **Sh. milioni 300,** mtambo wa kufundiashia wanafunzi kwa dola za Kimarekani **798,044.**

**Mheshimiwa Spika,** mafanikio ni kama yafuatayo: -

a) Uwezo wa kudhibiti usafiri wa anga umepanda kutoka asilimia **37** mwaka 2013 mpaka asilimia **67.3** kwa mwaka 2023;

b) Mamlaka ilipanga kukusanya **Sh. 83,085, 907,000.** Hadi kufikia februari 2022/23 makusanyo ni **Sh. 55,872,972,357** sawa asilimia **67** ya lengo. Hali hii inaonesha makusanyo yanaendelea vizuri kwani asilimia **33** iliyobaki inaweza kufikiwa katika kipindi kilichobaki. Kamati imejulishwa kuwa kuongezeka kwa miruko imetokana na kufunguka kwa usafiri wa anga duniani;

c) Kuongeza uwezo wa kusimamia anga kwa njia ya kuangaza ndege zinazoruka;

d) Kupata eneo la kujenga chuo cha anga lenye ekari 14.7;

e) Vijana 9 wamepata udhamini wa mafunzo ya urubani nchini Uganda;

f) Hakuna matukio ya kigaidi katika usafiri wa anga; na

g) Chuo cha usafiri wa anga (CATC) kimepasishwa na shirika la usafiri wa anga duniani kuwa chuo cha mafunzo ya usalama wa usafiri wa anga cha kanda ya Afrika Mashariki na Kusini mwa Afrika (ESAF).

**Mheshimiwa Spika,** changamoto ni pamoja na: -

a) Uchakavu wa mitambo ya kuongozea ndege na miundombinu duni;

b) TCAA imeshindwa kuanza ujenzi wa chuo kutokana na fedha; na

c) Upungufu wa wataalam kwenye sekta ya anga; **Mradi wa**

**Uboreshaji wa Vyuo Vilivyo Chini ya Sekta ya Uchukuzi**

**Mheshimiwa Spika**, vyuo hivyo ni chuo cha usafirishaji (NIT), chuo cha Bahari DSM, chuo cha reli, chuo cha Mamlaka ya Anga Tanzania, chuo cha Utabiri wa Hali ya Hewa na Chuo cha Bandari.

**Mheshimiwa Spika**, katika chuo cha Usafirishaji (NIT) kilitengewa jumla ya Sh. bilioni **1.77** hadi Februari 2023 fedha zilizopokelewa kwa asilimia **100** ya bajeti iliyotengwa. Chuo cha Bahari Dar es Salaam (DMI) kilipanga kununua mtambo kwa Sh. **bilioni 1.** Hadi kufikia Februari 2023 umetumia jumla ya Sh. **milioni 275.41** ikiwa sawa na asilimia **28** ya lengo. Kamati inasisitiza kuwa, Serikali ikamilishe ununuzi wa Simulator kwa chuo cha DMI.

**Mheshimiwa Spika**, changamoto inayokabili vyuo hivi ni kama ifuatavyo: -

a) Upungufu wa watumishi, uhaba wa vifaa vya kufundishia, mfano ndege maalum za kufundishia kwa NIT;

b) Msongamano mkubwa wa wanafunzi, na uchakavu wa miundombinu mfano hosteli na madarasa; na

c) Baadhi ya watumishi wa Serikali wanaosomeshwa na fedha za Serikali kutorejea nchini katika vituo yao vya kazi pindi wanapokwenda mafunzo nchi za nje.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inasisitiza kuwa, Serikali iboreshe vyuo vilivyo chini ya Sekta hii na kutoa fedha kwa wakati.

***Mradi wa Ujenzi na Ukarabati wa Meli kwenye Maziwa Makuu (Mradi Na. 4295)***

**Mheshimiwa Spika**, lengo la mradi huu ni kuendelea na ujenzi wa meli mpya na kukarabati meli zilizopo katika Ziwa Victoria na Ziwa Tanganyika ili kuboresha usafiri wa abiria na usafirishaji wa mizigo katika maziwa makuu. Katika mwaka wa 2022/2023 mradi huu umetengewa Sh. **113.7**

**Mheshimiwa Spika**, changamoto ya mradi huu ni kama ifuatavyo: -

a) Hadi kufikia mwezi Februari, 2023, mradi ulipata fedha kiasi cha Sh. bilioni **22.79** asilimia **20.04** ya lengo. Hali hii inaonesha kuwa upatikanaji wa fedha kwa mradi huu sio wa kuridhisha; na

b) Mradi wa uboreshaji usalama wa usafiri katika ziwa Victoria ulitengewa Sh. bilioni **4.15**. Hadi Februari 2023 ulitumia Sh. milioni **298.6** sawa na asilimia **7.18** ya lengo. Kamati imebaini kuwa kiasi kilichotolewa ni kidogo.

**Mheshimiwa Spika**, mafanikio ya mradi huu ni pamoja na meli zinazoendelea na ujenzi na ukarabati ni MV Mwanza Hapa Kazi Tu, MV Umoja na MV Sangara imefikia hatua ya asilimia **82**, asilimia **69** na asilimia **90.7** mtawalia.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapongeza Serikali kwa ujenzi na ukarabati wa meli unaoendelea. Hata hivyo, Kamati imebaini kwamba hakuna usafiri wa uhakika wa meli katika Ziwa

Tanganyika. Kwa hiyo, basi Kamati inaishauri Serikali kujenga meli mpya, pamoja na kuzikarabati Meli za **MV Liemba** na **MV Mwongozo** ili usafiri wa meli katika ukanda wa Ziwa Tanganyika uwe wa uhakika.


## 2.4 Uchambuzi wa Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024

### 2.4.1 Muundo wa Bajeti

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Sh. 3,786,313,766,420.** Kati ya Fedha hizo, **Sh. 1,699,768,258,420** inaombwa kwa **Fungu 98** – Sekta ya Ujenzi, na **Sh. 2,086,545,508,000** inaombwa kwa **Fungu 62** – Sekta ya Uchukuzi.

**Mheshimiwa Spika**, kati ya fedha inayoombwa katika **Fungu 98** – Sekta ya Ujenzi, **Sh. 59,986,788,420** kwa Matumizi ya Kawaida, wakati **Sh. 1,639,781,470,000** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha inayoombwa katika **Fungu 62** – Sekta ya Uchukuzi, **Sh. 118,215,599,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, na **Sh. 1,968,329,909,000** ni kwa ajili ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 117 (2), Kamati ilifanya uchambuzi wake kwa kulinganisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 na Mwaka wa Fedha 2023/2024. Kielelezo Na. 7 kinabainisha tofauti ya makadirio hayo.




**Mheshimiwa Spika**, kwa ujumla, Bajeti ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi imepungua kwa **asilimia 2.07** ukilinganisha na Bajeti ya **Sh. 3,866,616,675,800** iliyotengwa katika Mwaka wa Fedha unaoisha wa 2022/2023. Aidha, Bajeti ya Maendeleo kwa Fungu 98 na Fungu 62 zimepungua kwa **asilimia 5.7** na **asilimia 3.57** mtawalia. Hata hivyo, Bajeti ya Matumizi ya Kawaida kwa Fungu 98 na 62 imeongezeka kwa **asilimia 35** na **asilimia 25** mtawalia.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuongeza fedha za Matumizi ya Kawaida hasa Matumizi Mengineyo (O.C) kwa kuwa hatua hii itaongeza motisha kwa Watumishi kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi. Hata hivyo, Kamati haijaridhishwa na kupungua kwa fedha za utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

### 2.4.2 Malengo ya Makusanyo ya Maduhuli

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2023/204, Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi pamoja na taasisi zake inaomba kuidhinishiwa kukusanya jumla ya **Sh. 3,141,307,000,000**. Kiwango hiki ni ongezeko la **asilimia 33.65** ukilinganisha na **Sh. 2,350,489,883,978** iliyopangwa kukusanywa katika Mwaka wa Fedha 2022/2023.

**Kielelezo Na. 8** kinaonyesha mchanganuo wa makadirio ya makusanyo ya maduhuli hayo.

**Kielelezo Na. 8 -** Makusanyo Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi Kufikia Februari, 2023

| **TAASISI** | **MAKADIRIO YA MAKUSANYO KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 (TZS)** | **MAKADIRIO YA MAKUSANYO KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 (TZS)** | **TOFAUTI KWA ASILIMIA (+/-)** |
|---|---|---|---|
| **Fungu 98** – SEKTA YA UJENZI | | | |
| Wizara | 70,000,000 | 70,000,000 | 0% |
| **Fungu 62** – SEKTA YA UCHUKUZI | | | |
| LATRA | 35,100,000,000 | 40,100,000,000 | 14.24 |
| TCAA | 85,100,250,748 | 90,200,000,000 | 5.99 |
| TMA | 18,970,000,000 | 20,100,000,000 | 5.95 |
| TASAC | 63,860,000,000 | 70,910,000,000 | 11.03 |
| TPA | 1,424,405,141,301 | 1,858,969,000,000 | 30.50 |
| MSCL | 9,293,594,205 | 17,306,000,000 | 86.22 |
| TAA | 85,055,000,000 | 136,154,720,000 | 60.07 |
| ATCL | 341,509,000,000 | 584,100,000,000 | 71.03 |
| KADCO | 24,394,840,937 | 34,814,420,000 | 42.71 |
| TRC | 83,988,244,246 | 125,120,000,000 | 48.97 |
| TAZARA | 120,000,000,000 | 98,994,410,000 | -17.50 |
| NIT | 27,889,545,000 | 25,500,000,000 | -8.56 |
| DMI | 12,307,997,958 | 20,470,000,000 | 66.32 |
| SINOTASHIP | 18,546,269,583 | 18,500,000,000 | -0.24 |
| **JUMLA KUU** | **2,350,489,883,978** | **3,141,307,000,000** | **+33.65%** |

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa kuongeza makadirio ya makusanyo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024. Kipekee, Kamati inazipongeza taasisi chini ya **Fungu 62** – Sekta ya Uchukuzi ambazo zimeongeza wigo wa makadirio ya makusanyo. Hatua hii itaongeza pato la Serikali na kuchochea uchumi. Hata hivyo, kwa kuwa Kamati imebaini kwamba hakuna

ongezeko la makadirio ya makusanyo kwa **Fungu 98** – Sekta ya Ujenzi, Kamati inaishauri Serikali kutathimini vyanzo na uwezo wa sekta hiyo katika kuchangia pato la Taifa.

**Mheshimiwa Spika**, kwa zile taasisi ambazo katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 hazikutimiza malengo ya makusanyo Kamati inazishauri taasisi hizo kuhakikisha kwamba wanajiwekea mikakati madhubuti ya makusanyo ili kuiwezesha Serikali kutimiza malengo yake katika Mwaka wa Fedha 2023/2024.

### 2.4.3 Matumizi ya Kawaida

**Mheshimiwa Spika**, kwa ujumla Bajeti ya Matumizi ya Kawaida kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 imeongezeka kwa wastani wa asilimia **30** katika mafungu yote ya Wizara ukilinganisha na Bajeti hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023. Ongezeko hilo linatokana na kuongezeka kwa fedha za Matumizi Mengineyo (O.C.).

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapongeza Serikali kwa kuongeza fedha za Matumizi Mengineyo (O.C.) kwa kuwa ongezeko hilo litasaidia masuala ya uratibu wa shughuli zinazosimamiwa na Wizara.

### 2.4.4 Mpango wa Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2023/204, Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Sh. 3,388,172,966,000** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ambayo kwa ujumla wake ni pungufu kwa **asilimia 10.4** ukilinganisha na Bajeti ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha unaoisha.

## SEHEMU YA TATU

### 3.0 MAONI NA USHAURI

### 3.1 Maoni na Ushauri wa Jumla

**Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi ina mchango mkubwa katika maendeleo ya nchi na ukuaji wa uchumi. Kwa msingi huo, Kamati ina maoni na ushauri wa jumla kwa Serikali kama ifuatavyo: -

a) Kamati imebaini kwamba, katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 Bajeti ya Matumizi ya Kawaida hususan Matumizi Mengineyo (O.C) imeongezeka. Kamati inashauri Serikali kuhakikisha kwamba fedha zilizotengwa na Bunge zinafika kwa wakati ili kuwezesha Wizara na taasisi zake kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Aidha, Kamati inashauri Wizara na taasisi hizo kuwa wabunifu wa namna bora za utendaji wa majukumu yao kwa ufanisi na kasi zaidi ili fedha za Matumizi Mengineyo (O.C) zinazofika, zinatumika kwa weledi;

b) Kwa kuwa gharama za miradi inayotekelezwa na Wizara hii ni kubwa, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba miradi hiyo inazingatia viwango na ubora. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba kunakuwepo na uwajibikaji wa watendaji na makandarasi katika miradi yote ambayo imetekelezwa au itatekelezwa chini ya viwango na pia ichukue hatua za kisheria na kinidhamu kwa wahusika wote;

c) Kwa kuwa Kamati imebaini kwamba miradi mingi ya barabara katika Sekta ya Ujenzi inashindwa kuanza utekelezaji kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo ukosefu wa fedha, Kamati inaishauri Serikali kuanza mpango wa kushirikisha sekta binafsi (PPP na EPC + F) katika ujenzi wa barabara; na

d) Serikali iwe na mkakati wa kuwadhibiti wakandarasi wanaoshindwa kutekeleza miradi kwa wakati.

### 3.2 Maoni na Ushauri Mahususi

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kutoa maoni ya jumla, sasa naomba nitoe maoni na ushauri mahususi katika masuala mbalimbali ya utekelezaji wa majukumu ya Sekta za Ujenzi na Uchukuzi kama ifuatavyo: -

**SEKTA YA UJENZI**

**a) Ujenzi wa Miundombinu ya Barabara Unaosimamiwa na TANROADS**

i) Serikali iongeze fedha za matengenezo;

ii) Serikali ijenge barabara kwa kutumia mfumo wa kushirikisha wawekezaji binafsi (PPP na EPC + F) ili kuwezesha barabara nyingi kujengwa mfano barabara ya Kibaha - Chalinze - Morogoro;

iii) Katika mikataba ya ujenzi wa barabara Serikali iongeze kipengele kitakachofanya Mkandarasi na Mhandisi mshauri wa mradi kuongeza muda wa kuendelea kufuatilia na kukarabati barabara kwa mkataba, uwe zaidi ya mwaka mmoja kabla ya kuzikabidhi kwa Serikali;

iv) Baadhi ya wakandarasi huchelewa kukamilisha miradi kwa wakati na kuongeza gharama, Serikali iweke kipengele katika mkataba cha kuzuia ongezeko la gharama;

v) Serikali ishughulikie malalamiko kuhusu uwepo wa vituo vya mafuta ndani ya hifadhi ya barabara;

vi) Serikali iwaunganishe Wakandarasi wazawa na iwajengee uwezo katika ujenzi wa miradi ya ndani ili kuwawezesha kupata uzoefu wa kutekeleza miradi mingine mfano fedha na utaalam katika usimamizi wa miradi;

vii) Serikali iimarishe mifumo ya mifereji ya maji katika ujenzi wa barabara ili kuepusha maji kujaa kwenye makazi ya wananchi;

viii) Serikali ijenge vivuko vya waenda kwa miguu kwa kutumia madaraja ya chini ili kuwawezesha watu wengi kutumia njia hizo hasa walemavu; ix) TANROADS idhibiti wizi wa vifaa katika miradi yake;

x) Serikali iendelee kutoa elimu ya matumizi ya barabara kwa wananchi ili kupunguza ajali;

xi) Serikali iongeze watumishi na vifaa vya kupima ubora katika miradi ili kuiwezesha TANROADS kutekeleza miradi kwa ufanisi;

xii) Wakandarasi wanaochelewesha miradi kutokamilika kwa wakati, watoe tozo kuilipa Serikali kwa ucheleweshaji huo; na

xiii) TRA ishughulikie maombi ya vibali vya kuongeza muda wa hati za misamaha ya kodi ya ongezeko la thamani (VAT) kwa wakati.

***b) Ukarabati wa Karakana, Vivuko na Maegesho Unaosimamiwa na TEMESA***

i) Serikali izisimamie taasisi zake ili zilipe madeni kwa TEMESA kutokana na huduma wanazopata;

ii) Pamoja na kwamba TEMESA wamejikita katika kutoa huduma, ni vema kujiendesha kibiashara kwani gharama wanazotumia katika uendeshaji ni kubwa kuliko mapato;

iii) Serikali iongeze watumishi wa TEMESA na ihakikishe vipuri vinapatikana kwa urahisi na gharama nafuu;

iv) Serikali kupitia TEMESA itafute eneo kubwa katika kituo cha Kigamboni ili kukidhi mahitaji ya kivuko; na

v) Kunapokuwa na jambo linalohitaji ufafanuzi katika jamii ni vyema Serikali ikatoa taarifa kwa wakati ili kuepusha upotoshaji mfano ni ukarabati wa kivuko cha magogoni.

***c) Barabara na Miundombinu ya Mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka (BRT)***

i) TANROADS waimarishe usimamizi kwa Mkandarasi wa mradi wa BRT ili ukamilike kwa wakati;

ii) TANROADS itumie mfumo wa gharama za mradi kutobadilika kutokana na mazingira (fixed contract);

iii) Kabla ya mradi kuanza utafiti ufanyike kwa kina ili kuepusha athari za kimazingira kwa jamii, mfano kero ya maji ya mvua kujaa barabarani na kuingia kwenye makazi ya watu; na

iv) TANROADS iweke ulinzi wa fensi katika miradi ya BRT itakayosaidia kudhibiti wizi wa vifaa, usalama wa miundombinu.

***d) Ujenzi wa Nyumba na Majengo ya Serikali***

i) Serikali iisaidie TBA ili walipwe fedha wanazozidai taasisi mbalimbali za Serikali ikiwemo madeni ya pango la nyumba za viongozi ili fedha watakazolipwa ziwasaidie katika kujiendesha kibiashara;

ii) Serikali iangalie kwa nini gharama za utekelezaji wa miradi kwa TBA zinakuwa kubwa kuliko uhalisia;

iii) Serikali iendelee kutoa fedha kwa TBA ili miradi wanayopewa kutekeleza iweze kukamilika kwa wakati;

iv) Serikali iongeze ajira ili kuondoa upungufu wa watumishi uliopo TBA;

v) TBA iharakishe kupata umiliki wa kisheria wa ardhi zilizo chini yake ili kuziendeleza na kuepuka wavamizi hasa katika Mikoa ya Arusha na Dar es Salaam;

vi) Serikali iharakishe mchakato wa sheria utakaoruhusu wawekezaji binafsi kuingia ubia na TBA katika kutekeleza miradi mbalimbali nchini; na

vii) Serikali kupitia TBA iimarishe ulinzi kwenye maeneo ya miradi.

***e) Ujenzi wa Viwanja vya Ndege***

i) Serikali iongeze fedha za ukarabati wa miundombinu katika viwanja vya ndege ili kuimarisha usalama wa ndege;

ii) Serikali ifanye mabadiliko ya sheria mahususi kwa ajili ya usimamizi, uendeshaji na uendelezaji wa viwanja vya ndege Tanzania;

iii) Ujenzi wa miundombinu ya viwanja vya ndege ubaki kwa TAA badala ya TANROADS;

iv) Serikali ijenge uwanja mpya wa ndege katika mkoa wa Kagera; na

v) Serikali iongeze watumishi ili kuondoa uhaba uliopo.

***f) Chuo cha Teknolojia ya Ujenzi (ICoT)***

i) Kamati inashauri kwamba, Serikali iongeze bajeti na kuendelea kufanya maboresho mbalimbali kwani chuo hiki ni muhimu kwa uzalishaji wa mafundi;

ii) Serikali iongeze watumishi, karakana, maktaba ya kisasa na vitendea kazi ili kuondoa upungufu na ikarabati miundombinu chakavu;

iii) Chuo kiendelee kujiimarisha katika kutoa elimu ya kada ya kati ya mafundi na ijitangaze kibiashara; na

iv) Serikali kupitia sekta ya ujenzi ifanye maboresho makubwa katika vyuo vyote vilivyo chini ya sekta hiyo, Ili viweze kufanya kazi iliyokusudiwa.

***SEKTA YA UCHUKUZI***

a) Utendaji wa Shirika la Reli Tanzania (TRC)

i) Serikali kupitia TRC imsimamie mkandarasi anayejenga reli ya Kisasa (SGR) kipande cha Dar es Salaam - Makutupora – (Lot 1 & 2) akamilishe kazi ndani ya muda alioongezewa;

ii) Mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa uendane na ununuzi wa mabehewa na vichwa vya treni pamoja na uimarishaji wa miundombinu ya umeme;

iii) Serikali ihakikishe chuo cha reli kinaboreshwa ili kutoa wataalam wa kutosha watakaoweza kufanya matengenezo makubwa kwenye njia ya reli na mitambo yake kwa reli ya SGR na MGR;

iv) Serikali ifanye marekebisho ya sheria iliyoanzisha shirika la reli Tanzania, ili reli ya kisasa itakapoanza kazi itoe nafasi kwa makampuni binafsi kuwekeza katika kutoa huduma;

v) Serikali iharakishe mikakati ya ujenzi wa reli kwenye maeneo yenye uchumi mkubwa mfano, maeneo ya Kaliua - Kalema, Mtwara – Bambabay na mengineyo;

vi) Serikali kupitia TRC ifanye ukarabati wa miundombinu katika stesheni za reli ya MGR kwani miundombinu yake ni chakavu;

vii) Kuna maeneo korofi mfano mto Mkondoa na Kidete yanayoweza kuharibu miundombinu ya reli hasa ile ya MGR, ni vema utafiti uendelee ili kutunza miundombinu na Serikali iendelee kuimarisha mradi wa kujenga mabwawa na upandaji wa miti;

viii) Serikali ifanye maboresho katika suala la ajira kwani kuna upungufu wa watumishi na ajira izingatie usawa wa kijinsia;

ix) Kutokana na tabia ya baadhi ya wafanyakazi wa karakana ya vichwa vya treni na mabehewa kuhujumu miundombinu, Serikali kupitia TRC iimarishe ulinzi mfano CCTV kamera na GPS;

x) Serikali kupitia shirika la reli ijitangaze zaidi ili ijiendeshe kibiashara; na

xi) Serikali iharakishe ukarabati wa reli kutoka Kilosa – Mikumi – Kidatu ili kuunganisha reli ya kati na TAZARA.

*b)* ***Utendaji wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA)***

i) Serikali iharakishe mchakato wa kuruhusu uwekezaji binafsi katika sekta ya bandari nchini;

ii) Serikali iharakishe miundombinu ya reli inayounganisha bandari na reli za SGR, MGR na TAZARA ili kuendana na kasi ya upanuzi wa bandari;

iii) Ongezeko la makusanyo ya mapato ya TPA yaendane na uhalisia wa maboresho ya miundombinu yaliyofanyika;

iv) Serikali isaidie TPA kupata maeneo makubwa ya ardhi kwa ajili ya uwekezaji mkubwa hasa bandari kavu mfano, ujenzi wa bandari kavu ya Kwala ukamilike ili kuondoa msongamano wa mizigo bandarini;

v) Serikali iongeze watumishi kwani upungufu uliopo ni mkubwa;

vi) Pamoja na kwamba tatizo la upotevu wa mizigo umepungua bandarini, TPA iendelee kuboresha ulinzi ili kulinda mizigo ya wateja na kujenga Imani kwa wadau;

vii) TPA iharakishe mfumo wa kuunganisha wadau wa bandari *(single window system)* ili kuondoa urasimu na kurahisisha huduma na mahusiano mazuri kwa wadau;

viii) Serikali iangalie uwezekano wa kutumika kwa bandari za Mtwara na Tanga ili uwekezaji ulete tija; na

ix) TPA iendelee kujitangaza kibiashara ili kuliteka soko na kuleta ushindani katika bandari nyingine shindani zilizo karibu na nchi yetu.

***c) Uboreshaji wa Huduma na Miundombinu Katika Viwanja vya Ndege Tanzania Vinavyosimamiwa na TAA***

i) Serikali iendelee kuboresha ujenzi wa viwanja vya ndege ili huduma ipatikane maeneo mengi sambamba na ufungaji wa taa ili ndege ziruke usiku katika viwanja vingi;

ii) Serikali ione uwezekano wa kuiwezesha TAA kubakiza kiasi cha fedha walau asilimia 40 zitokanazo na makusanyo ili zisaidie katika masuala ya uendeshaji;

iii) TAA waimarishe kitengo cha huduma ya ulinzi na usalama hasa inapotokea ajali, pia kuondoa taharuki kwa wanachi wakati wanapotekeleza jaribio la uokoaji;

iv) Sheria iliyoanzisha viwanja vya ndege iboreshwe ili kuwezesha viwanja vingi kujiendesha kibiashara;

v) Serikali ifikirie kujenga uwanja mpya wa ndege mkoani Kagera; na

vi) Kwa kuwa Kamati imebaini kuna upungufu wa vifaa vya kuongoza ndege wakati wa kutua (ILS) katika baadhi ya viwanja vya ndege. Kwa hiyo basi, Serikali ihakikishe kuwa viwanja vyote vya ndege vinakuwa na vifaa hivyo.

***d) Uendeshaji wa Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA)***

i) Serikali kwa kutumia mapato ya ndani ya TCAA iharakishe ujenzi wa miundombinu ya kisasa katika kituo cha mafunzo ya usafiri wa Anga (CATC);

ii) Serikali ione uwezekano wa kuiwezesha TCAA kubakiza kiasi cha fedha zitokanazo na makusanyo ili zisaidie katika masuala ya uendeshaji; na

iii) Serikali iwathibitishe watumishi wenye sifa wanaokaimu kwa muda mrefu ili kuwawezesha kufanya maamuzi sahihi.

***e) Uendeshaji wa Mamlaka ya Hali ya Hewa Nchini***

i) TMA iendelee kujiimarisha ili iendane na ukuaji wa teknolojia;

ii) Serikali itoe fedha kwa wakati kwani kuna upungufu wa fedha;

iii) Serikali iisaidie TMA ili iweze kulipwa madeni yake wanayodai kwa wakati;

iv) Serikali iboreshe iongeze watumishi, vituo, vifaa vya kufundishia na kuboresha miundombinu katika chuo cha hali ya hewa; na

v) Serikali iboreshe maslahi ya watumishi wa TMA.

***f) Utendaji wa Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL)***

i) Serikali itathimini upya juu ya umiliki wa ndege zake kwa shirika la ndege la ATCL kuliko ilivyo sasa;

ii) Serikali iendelee kufuatilia kwa karibu ili matengenezo ya injini mbili (2) za ndege zilizoharibika yakamilike;

iii) Serikali iisaidie ATCL ili kuweza kukabiliana na madeni; na

iv) Serikali iboreshe mafunzo ya kada ya marubani na wahandisi wa ndege ili kuongeza idadi yao hapa nchini.

***g) Uboreshaji wa Vyuo Vilivyo Chini ya Sekta ya Uchukuzi***

i) Serikali iongeze uwekezaji katika vyuo ili kuwezesha vyuo hivyo kujiendesha kwa ufanisi zaidi;

ii) Serikali iandae mpango maalum ambao utasaidia wahitimu wa kozi mbalimbali wanaotoka katika vyuo hivyo kutumia utaalamu wao katika ujenzi na uendeshaji wa miundombinu ya uchukuzi nchini;

iii) Kutokana na upungufu wa watumishi, Serikali ione umuhimu wa kuongeza watumishi katika vyuo hivyo;

iv) Serikali iwekeze katika vyuo vyote nchini na viwe na vifaa vya kisasa vya kufundishia ili kuendana na mabadiliko ya teknolojia;

v) Kwa kuwa katika baadhi ya vyuo kuna msongamano wa wanafunzi, Serikali iboreshe miundombinu ikiwa ni pamoja na kujenga hosteli na madarasa ya kutosha; na

vi) Serikali iwe na mkataba maalum kwa watumishi ili wanapoenda kusoma nje ya nchi warejee na kutumikia nchi.

## SEHEMU YA NNE

## 4.0 HITIMISHO

### 4.1 Maelezo ya Hitimisho

**Mheshimiwa Spika**, katika kufanikisha Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs), uboreshaji wa Sekta ya Ujenzi na Sekta ya Uchukuzi ni muhimu kwa uchumi wa nchi na itawezesha kuimarika kwa sekta zingine kama vile viwanda, utalii na biashara

(kama inavyoeleza katika Lengo Na. 9). Uboreshaji wa miundombinu ya barabara, bandari, viwanja vya ndege kutawezesha kuongeza ufanisi kwa sekta nyingine na kufikia malengo ya kitaifa. Kwa muktadha huo, Kamati ya Kudumu ya Miundombinu itaendelea kuwa mstari wa mbele kusimamia sekta hizo kwa uadilifu ili Bunge lako tukufu liweze kuwa chachu ya maendeleo ya nchi kwa ujumla.

**4.2 Shukrani**

**Mheshimiwa Spika**, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kuongoza vema Bunge hili ukisaidiiwa na Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge, na kwa namna ambavyo umekuwa ukitoa ushirikiano wa kutosha uliofanikisha utekelezaji bora wa majukumu ya Kamati. Aidha, nitumie fursa hii kuwashukuru sana Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na hatimaye kukamilika kwa taarifa hii. Kwa umuhimu wao katika utekelezaji wa majukumu ya Kamati naomba niwatambue kama ifuatavyo: -

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Moshi Selemani Kakoso, Mb. | **Mwenyekiti** |
| 2. | Mhe. Anne Kilango Malecela, Mb. | **Makamu** |
| 3. | Mhe. Abdallah Jafari Chaurembo, Mb. | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Abubakar Damian Asenga, Mb. | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Ahmed Mabkhut Shabiby, Mb. | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Ally Anyigulile Mlaghila Jumbe, Mb. | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Amina Ali Mzee, Mb. | Mjumbe |
| 8. | Mhe. Angelina Malembeka, Mb. | Mjumbe |
| 9. | Mhe. Capt. Abbas Ali Hassan Mwinyi, Mb. | Mjumbe |
| 10. | Mhe. Eng. Mwanaisha Ng'anzi Ulenge, Mb. | Mjumbe |
| 11. | Mhe. Fredrick Edward Lowassa, Mb. | Mjumbe |
| 12. | Mhe. Ghati Zephania Chomete, Mb. | Mjumbe |
| 13. | Mhe. Innocent Edward Kalogeris, Mb. | Mjumbe |
| 14. | Mhe. Livingstone Lusinde, Mb. | Mjumbe |
| 15. | Mhe. Mbarouk Juma Khatib, Mb. | Mjumbe |
| 16. | Mhe. Miraji Jumanne Mtaturu, Mb. | Mjumbe |
| 17. | Mhe. Mohamed Maulid Ali, Mb. | Mjumbe |
| 18. | Mhe. Mwatum Dau Haji, Mb. | Mjumbe |
| 19. | Mhe. Rose Vicent Busiga, Mb. | Mjumbe |
| 20. | Mhe. Santiel Eric Kirumba, Mb. | Mjumbe |

21. Mhe. Stella Simon Fiyao, Mb. Mjumbe
22. Mhe. Sylvia Francis Sigula, Mb. Mjumbe

**Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati naomba nitumie fursa hii kumshukuru Mhe. Prof. Makame Mnyaa Mbarawa (Mb.) - Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, akisaidiwa na Naibu Mawaziri Mhe. Mhandisi Geofrey Msongwe Kasekenya (Mb.) – Sekta ya Ujenzi, na Mhe. Atupele Fredy Mwakibete (Mb.) – Sekta ya Uchukuzi kwa ushirikiano ambao wameipatia Kamati katika kipindi chote cha uchambuzi wa bajeti. Aidha, nawashukuru watendaji wote wa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, pamoja na taasisi zake wakiongozwa na Makatibu Wakuu Balozi Mhandisi Aisha S. Amour – Sekta ya Ujenzi na Bw. Gabriel J. Migire – Sekta ya Uchukuzi kwa kuendelea kutoa ushirikiano kwa Kamati kila mara walipohitajika kufanya hivyo.

**Mheshimiwa Spika**, mwisho lakini sio kwa umuhimu, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Nenelwa Mwihambi, ***ndc*** kwa kuratibu vema shughuli za Kamati na Shughuli za Bunge. Aidha, nawashukuru Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Michael Chikokoto, ***ndc***, Mkurugenzi Msaidizi Ndg. Gerald Magili na Makatibu wa Kamati hii Ndg. Janeth Malangu na Ndg. Yona Kirumbi wakisaidiwa na Ndg. Kokuwaisa Gondo kwa kuratibu Shughuli za Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii.

### 4.3 Msimamo wa Kamati Kuhusu Hoja

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Moshi Selemani Kakoso, Mb.
**MWENYEKITI**
Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu
22 Mei, 2023

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Makamu Mwenyekiti na Wajumbe kwa taarifa nzuri mbele ya Bunge letu Tukufu.

Waheshimiwa Wabunge, nina matangazo machache; wapo wageni walioingia Bungeni muda huu ambao ni wageni wa Waheshimiwa Wabunge.

Kuna wageni wa Mheshimiwa Profesa Makame Mbarawa, Mbunge na Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi ambao ni wataalam maalum kutoka *ATCL, MSCL, TPA* na *DMI* wanaofanya kazi zinazodhaniwa kuwa ni za wanaume kama vile rubani wa ndege, dereva wa treni, Kapteni wa meli, mwendesha mitambo na wahudumu wa ndege.

Naomba popote walipo wasimame tuweze kuwaona. Karibuni sana. Kama nilivyowatangazia asubuhi kwamba mchana mtawaona, basi ndio hao mmewaona. Tunashukuru sana. *(Makofi/Vigelegele)*

Waheshimiwa Wabunge, ahsanteni sana.

Wapo wageni 21 wa Mheshimiwa Salome Makamba ambao ni Waandishi wa Habari kutoka Mkoa wa Shinyanga, ahsante na karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni 10 wa Mheshimiwa Jesca Kishoa ambao ni Chawa wa Mama kutoka Mkoa wa Mwanza, ahsanteni. *(Makofi)*

Wapo wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo, wapo viongozi 35 wa Serikali ya Wanafunzi wa Taasisi ya Ustawi wa Jamii ya kutoka Jijini Dar es Salaam, ahsante na karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, baada ya kusikia hotuba ya Mheshimiwa Waziri pamoja na Taarifa ya Kamati, sasa tunaendelea na mjadala wa hoja iliyopo mbele yetu.

Nina orodha ya wachangiaji hapa, nitaanza na Mheshimiwa Kilumbe Shabani Ng’enda, atafuatiwa na

Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu, na Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga ajiandae.

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, namshukuru Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehema kutuwezesha kuendelea kufanya kazi ya Bunge letu tukiwa tunajadili Bajeti ya Wizara mbalimbali na leo tuko Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, niendelee kukushukuru wewe Mwenyekiti pamoja na uongozi mzima wa Bunge kwa kuendelea kuendesha Bunge letu vizuri. Zaidi ya yote namshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuongoza Taifa letu vizuri na kuendelea kulipa heshima kimataifa na zaidi ya yote kuendelea kuwaletea maendeleo wananchi wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niruhusu nitoe salamu za pekee na pongezi za pekee kwa Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana na Wizara hii, Profesa Mbarawa na wasaidizi wake wote wawili, Naibu Waziri wa Uchukuzi na Naibu Waziri wa Ujenzi kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya. Hili nataka niweke maneno maalum hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi ni Wizara mbili ndani ya Wizara moja. Wizara hii ina taasisi 22 inazozisimamia, lakini ipo taasisi moja tu au zipo taasisi ambazo taasisi moja peke yake ingetosha kuwa Wizara. Kwa mfano, Taasisi kama Shirika la Reli, yaani ingeweza ikatosha kuwa Wizara. Zipo nchi nyingine Shirika la Reli ni Wizara peke yake. Kwa hiyo, unapoona watu hawa wanachapa kazi ya kusimamia taasisi 22, kwa kweli wanafanya kazi kubwa sana na wanastahili pongezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nataka nirudie maneno yangu ambayo nimekuwa nikiyasema mara nyingi, kwamba mnaposikia tunakosoa, tunaelekeza au tunashauri baadhi ya vitu, hatumaanishi kwamba kazi haifanyiki, Hapana. Isipokuwa hata kilicho bora, huboreshwa. Kwa hiyo, wanafanya kazi nzuri, lakini tunataka wafanye kazi nzuri zaidi. Ninyi ni mashahidi, mmeona

barabara zilizokamilika zilizooneshwa hapa, mmeona viwanja vya ndege vilivyokamilika na mambo chungu mzima. Kwa hiyo, nawapongeza sana hawa wachapakazi na ninawatia moyo, endeleeni kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nataka nianze na meli katika Ziwa Tanganyika. Nimesikia kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri amezungumzia meli ya Liemba ambayo sasa imesimama kwa miaka saba, wananchi wa Ziwa Tanganyika wakiwa hawapati huduma kwamba itaanza kukarabatiwa mwezi Juni mwaka huu, yaani mwezi kesho na kwamba itachukua takribani miezi minane kukamilika na kurudi majini. Nataka nimwambie Mheshimiwa Waziri kwanza hii kauli umeitoa hapa Bungeni sisi tunaiunga mkono. Nami niliyesimama hapa, mbali na kuwa ni Mbunge wa Kigoma Mjini, lakini kutokana na matatizo tuliyonayo katika Ziwa Tanganyika ya huduma mbalimbali, tumetengeneza umoja wetu wa Wabunge wa mikoa ya Ziwa Tanganyika ambayo ni Kigoma, Rukwa na Katavi, nami ndio Mwenyekiti wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nikwambie, hii ni mara ya mwisho kusimama katika Bunge hili kuunga mkono bajeti ya Wizara hii kama hakutakuwa na meli kwenye Ziwa Tanganyika. Narudia maneno haya ili Watanzania wote wasikie. Hii ni mara ya mwisho kusimama katika Bunge hili kuunga mkono bajeti ya Wizara hii kama mpaka tutakapoingia kwenye bajeti nyingine meli hazitakuwepo kwenye Ziwa Tanganyika. Nasema hivi kwa sababu zifuatazo: Wale waliosimama katika umoja na kuishinikiza Serikali katika *Lake Victoria* sasa hivi wana meli tano zinafanya kazi; MV. Clarius, MV. Victoria, MV. Butiama, MV. Umoja na sasa MV Mwanza Hapa Kazi Tu, nayo imeingia majini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Lake Tanganyika* hakuna meli hata moja inayofanya kazi. Narudia, hii itakuwa ni mara ya mwisho kuunga mkono bajeti kwa namna yoyote ile itakayokuwa, kwa shinikizo la mtu yeyote yule, hatutaunga mkono bajeti kama meli hazitakuwa ziwani mpaka tunakuja kwenye bajeti nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, MV Mwongozo mmeisimamisha sasa kwa takribani miaka mitano, mnasema

mmesimamisha kwa sababu MV Bukoba ilizama na MV Bukoba ni meli pacha wa MV Mwongozo. Mlisema mtengenezaji ni mmoja kwa hiyo hizo ni meli pacha. Mkasema kwa sababu ile ilipata ajali, mkaisimamisha na hii. Ni maneno ambayo ukimwambia mtu hawezi kuelewa. Kuna ndege imepata ajali juzi hapa, sijui mmesimamisha ndege zote za aina hiyo! Maana hii meli ilikuwa inafanya kazi *Lake Tanganyika* na haikuwa na tatizo lolote. *Lake Tanganyika* kuna mawimbi makubwa kuliko *Lake Victoria,* na imekuwa ikisaifiri, haina tatizo, mkaisimamisha. Haya, nia yenu ni njema, mmeisimamisha ili kutengeneza *stability* iwe *stable*. Mpaka leo duniani hajapatikana mtu wa kutengeneza *stability* ya meli hii kwa miaka mitano. Hili ni jambo la aibu sana kwa wataalam waliosomeshwa na Taifa la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa 94 wa Hotuba ya Mheshimiwa Waziri amezungumzia haja ya Serikali kutaka kushirikisha sekta binafsi katika kuboresha bandari zetu. Napongeza sana hatua hii na nimekuwa nikiisemea sana humu Bungeni. Hatua hii ni utekelezaji wa Ilani ya CCM. Ukienda kwenye Ilani ya CCM, Ibara 18(b) (5) kinaeleza hivi nanukuu: "Kuongeza wigo wa upatikanaji wa rasilimali fedha kwa ajili ya kutekekeleza miradi ya maendeleo kwa kutumia mfumo wa ubia baina ya Serikali na sekta binafsi *(Public Private Partnership - PPP)*."

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hii ni sera ya CCM na ambayo tunasuasua sana katika kuitekeleza. Nataka niseme hapa, katika maeneo ambayo tumejaribu, tumefanikiwa, mnachelewa nini? Kwa mfano, niseme Bandari ya Dar es Salaam, pamoja na matatizo yote ambayo tumekuwa tukiyasikia juu ya *TICTS,* lakini bado tumepata faida ya kuwaweka *TICTS* katika magati manne. Gati Na. 8, Na. 9, Na. 10 na Na. 11, kuliko hata walivyokuwa *TPA* peke yao wanasimamia magati yote 11 ya Bandari ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipokuwa wanasimamia *TPA,* Serikali ilikuwa inapata gawio kati ya Shilingi bilioni 180 hadi Shilingi bilioni 200 kwa mwaka, lakini kwa *TICTS* peke yake kwa magati manne tulikuwa tunapata kati ya Shilingi bilioni 300 hadi 345. Kwa hiyo, pamoja na matatizo ya *TICTS* yaliyokuwepo na ambayo yanatupa fundisho la kwamba tukimpata mtu mwingine

tunayetaka kuingia naye ubia, lazima tuangalie zile changamoto tulizozipata kwa *TICTS,* lakini Serikali msije mkajiingiza katika jambo la kusema acha tufanye wenyewe, hakuna. Tafuteni wabia, tuendelee kutumia mfumo wa *PPP,* huo ndio utakaotutoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukarabati wa reli kati ya Kigoma, Tabora na Mabehewa. Hili nalo limekuwa linatengwa kwenye bajeti kila mwaka na bado utekelezaji haupo. Utekelezaji unasuasua. Reli kutoka Tabora kwenda Kigoma ambayo ni kilometa 411 tu, bado hali yake ni mbaya. Nashukuru Serikali mliahidi hapa Bungeni, tena mimi mwenyewe ndiye niliyeuliza swali, mkasema mtaleta mabehewa mapya 22. Naipongeza sana Serikali, imeleta na mabehewa hayo yamesaidia sana na safari za Kigoma - Dar es Salaam zimeongezeka kutoka mbili kwa wiki hadi tatu kwa wiki. Ila mabehewa mliyoahidi ambapo mlisema mtakarabati mabehewa 37, mpaka leo hayajaingia kwenye reli ili kusaidia kuongeza safari zifike hadi nne au tano kwa wiki.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI**: Mheshimiwa Kilumbe, ahsante sana. Muda wako umeisha.

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu atafuatiwa na Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga na Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi, ajiandae.

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia hoja iliyoko mbele yetu ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kutujalia uzima na kuweza kukutana asubuhi ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nichukue nafasi hii kumshukuru sana na kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri anayoifanya ikiwemo kuridhia fedha nyingi ambazo zinakuja

kwenye Wizara hii ambayo ni Wizara inayoendesha na kusukuma uchumi wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yetu ya Ujenzi na Uchukuzi ndiyo imebeba daraja la uchumi wa nchi yetu. Kwa hiyo, Wizara hii ndiyo imebeba mabadiliko ya uchumi ambao tunautarajia. Nachukua nafasi hii kwa kweli kumpongeza Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoifanya katika kujenga barabara, kujenga miundombinu, tunajenga reli, tunanunua meli, tunanunua ndege na kadhalika. Kazi hii inafanyika vizuri na kwa hakika ataendelea kuandikwa kwenye kitabu cha dhahabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nachukua nafasi hii kumshukuru sana na kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Profesa Makame Mnyaa Mbarawa pamoja na wasaidizi wake, Manaibu Waziri, ndugu yangu Kasekenya pamoja na Atupele ambao wanafanya kazi nzuri sana ya kumsaidia Mheshimiwa Waziri; Katibu Mkuu pamoja na Manaibu Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi kubwa; na bahati sisi wengine ni Wajumbe wa Kamati ya Miundombuni, tunaona kazi nzuri inayofanyika katika Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi na shukurani hizo, nichukue nafasi hii kwa hakika nianze kuchangia maeneo kama matatu kama nitapata muda. Nianze na kuchangia upande wa *TANROADS* ambayo ndiyo imepewa dhamana ya kusimamia ujengaji wa barabara kuu na barabara zinazounganisha wilaya na wilaya katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TANROADS* wanafanya kazi nzuri sana Wizara hii chini ya *Eng.* Mativila na wenzake wote. Wanawasimamia wakandarasi katika maeneo mbalimbali kujenga barabara, kujenga madaraja makubwa na madogo na kusimamia miundombinu mbalimbali katika eneo letu. Kazi hii ni nzuri na tumesikia kwenye taarifa yetu ya Kamati pamoja na Waziri mwenyewe ameeleza vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo hili nipongeze, kwa mujibu wa utaratibu wao tuliojiwekea ni kuhakikisha kwamba

tunaunganisha barabara za mikoa na mikoa. Hii ni pamoja na kazi kubwa ambayo imefanyika na imeelezwa. Napongeza sana utaratibu mpya ambao umeanzishwa wa kujenga barabara kwa mfumo mpya wa *EPC + F*. Mfumo huu utaenda kuwa ni jibu ya barabara ambazo zilikuwa hazijakamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Waziri ametueleza hapa, tunaenda kusaini barabara zenye urefu wa kilomita 2,035. Barabara hizi ambazo zimejengwa pamoja na Barabara ya Handeni – Kiberashi – Kwa Mtoro – Kiteto mpaka Singida, barabara ya kilomita 460. Barabara hii ikikamilika itaenda kubadilisha kabisa uchumi wa eneo hili. Leo hii Bandari ya Tanga ambayo tunaiboresha, itaenda kuwa na majibu kupitia barabara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana mkandarasi apatikane mapema, tumeambiwa mwezi wa Sita mkataba utasainiwa. Namwomba Mheshimiwa Waziri kwa heshima kabisa, tuhakikishe barabara inasainiwa mapema ili Wabunge wa maeneo ya kutoka pale Handeni, ndugu yangu Mheshimiwa Omari Kigua; ndugu yangu wa Kiteto, Mheshimiwa Olelekaita; ndugu yangu Mohamed Monni pamoja na mimi tuweze kufarijika na wananchi wetu waendelee kupata raha kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikimaliza hapo, Mheshimiwa Waziri nilikuomba barabara. Mlinipa barabara ya kilomita moja ndani ya wilaya yangu. Naomba sana mniongezee kilomita 10 kwa barabara ya kutoka Ikungi – Londoni kwenda Kilimatinde (Solya) kwa ndugu yangu Mheshimiwa Dkt. Chaya ili barabara ile ijengwe kwa kiwango cha lami kwa sababu tuna mwekezaji mkubwa wa madini pale ambaye yuko maeneo ya Mang'onyi. Ikiwepo barabara hii itaongeza thamani ya mradi ule ambao tumeuweka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni wenzetu wa *ATCL* kwa maana ya Shirika letu la Ndege. Kwa muda mrefu tumeendelea kudogolesha Shirika letu na kwenye Kamati imeelezwa vizuri. Katika eneo hili nitaongea maneno mawili. Ili uweze kukuza uchumi wa nchi hii, ukiboresha Shirika la Ndege utaenda kuongeza thamani ya utalii. Watalii wengi watakuja. Biashara

zinazofanyika kwenye maeneo mbalimbali duniani, ukiwa na ndege yako mwenyewe utakuwa na uhakika wa biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunategemea kupata ndege hivi karibuni ile ya *Cargo* ambayo itakuja kubeba mazao ya mboga mboga na maua kwenda nchi za Ulaya na Asia ambapo huko wanahitaji sana bidhaa hizo. Naomba sana shirika hili liangaliwe na Serikali, liendelee kuwezeshwa ili kuhakikisha kwamba linapata faida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo hili, pamoja na changamoto nyingine, kumekuwa na changamoto za madeni la shirika hili. Kwenye taarifa yetu tumepata sisi kwenye Kamati, wao walikuwa wanadaiwa karibia Shilingi bilioni 236 ambazo ni fedha walizokuwa wanadaiwa wakati hili shirika halifanyi kazi, lakini wamejitahidi kulipa karibia Shilingi bilioni 136, wamebakiwa na Shilingi bilioni 100. Serikali iangalie namna ya kumaliza deni hili ili tuweze kuweka mizania sawa ya hesabu za shirika hili, kuondokana na hasara ambayo inaweza kujitokeza na kulifanya shirika letu lifanye kazi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ni kuondoa matatizo ya kukamatwa ndege katika nchi nyingine ambazo zinaidai Tanzania. Ndege hizi zimekuwa zinashikwa, siyo *ATCL* inadaiwa, inadaiwa Serikali, lakini kwa sababu Shirika la Ndege halimiliki zile ndege, hizi ndege zinamilikiwa na Wakala wa Ndege za Serikali, *ETGF,* maana yake ni kwamba hao ni kama Serikali. Kwa hiyo, deni lolote linaloihusu Serikali, likipatikana eneo lolote, ndege yetu inakamatwa. Maana yake mtiririko wa usafiri unaondoka. Leo hii *ATCL* ikiondoka ndege moja tu, kama inaenda Mumbai ama nchi nyingine, maana yeke unapunguza mtiririko wa abaria. Maana yake usitegemee kupata faida. Leo hii *CAG* ataenda kuona kila siku shirika linapata hasara kwa sababu ni mpango ambao tumeuweka wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Serikali iangalie uwezekano wa kurudisha ndege hizi *ATCL* ili ziweze kumilikiwa na Shirika la Ndege lenyewe ili kuleta faida na kulifanya shirika letu liweze kufanya kazi vizuri. Ambacho ni mzigo mkubwa, leo hii

Shirika la Ndege linalipa karibia Shilingi milioni 700 kwa ajili ya kukodisha ndege za Serikali. Hivi Serikali na Serikali zinakodishiana, kuna haja gani? Ndiyo maana shirika letu haliwezi kuendelea kwa sababu linakwazwa na mambo mengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana kwenye hili Mheshimiwa Waziri atakaporudi, atuambie ni mpango gani wa Serikali umefikiwa kwa ajili ya kurudisha ndege hizi *ATCL* kuondoka kwenye Wakala wa Ndege wa Serikali na changamoto ambazo shirika linapata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu ambalo ni la mwisho ni suala la Bandari. Bandari ni lango kuu la biashara. Bandari yetu kwa maana ya mkao wa kijiografia Bandari yetu ya Dar es Salaam imekaa vizuri sana kistratejia. Bandari hii tukiitumia vizuri, inaweza ikaleta mapato mengi kuliko eneo lolote. Leo hii pamoja na mchango inayotoa lakini bado, haitoi mchango wa kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeboresha sana gati Na. 8 mpaka 11, tumeweza kujitahidi kuongeza masuala ya usalama katika bandari, ni sawa, lakini tumeongeza *cranes* ambazo bado ni kidogo sana. *Cranes* mbili zile zinazofanya kazi pale, tukiangalia bandari nyingine ambazo ziko kama Mundra kule India, kule Dubai na nchi nyingi, bandari nyingine zinafanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, tumeongeza mapato ya Shilingi bilioni 700 mpaka Shilingi trilioni moja tu, ambayo kimsingi ukiangalia hizi fedha bado ni ndogo kwa bandari yetu ilivyokaa. Nchi nane zinategemea Bandari ya Dar es Salaam, maana yake ni kwamba tukiboresha vizuri, Bandari ya Dar es Salaam itakuwa ni jibu la fedha ambazo hatuzipati katika maeneo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba sana, pamoja na mambo haya, kuna changamoto chache zinakwaza bandari yetu. La kwanza, bado hatujakuwa na mifumo ya kusomana ambayo inaweza kumsaidia mteja kuvutika kuja kufanya biashara na sisi. Naomba sana tuhakikishe kwamba tunaangalia namna ya kumleta mwekezaji ambaye atashirikiana na Serikali. Siyo jambo la

dhambi, *PPP* imetajwa kwenye sheria za nchi yetu, tusiwe waoga Watanzania tunapotaka kubadilisha maisha ya Watanzania wetu. Tukiweza kuwekeza vizuri, itasaidia sana…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mtaturu, ahsante sana.

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Naam!

Mheshimiwa Mwenyekiti, dakika moja nimalizie, ni –*conclude* hii hoja.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, malizia sekunde thelathini muda wako umeisha.

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa sekunde thelathini.

Mheshimiwa Mwenhyekiti, naomba sana Watanzania tusiwe waoga kwenye mambo ya msingi ili kuhakikisha kwamba tunaweza kubadilisha na kuongeza uchumi wa nchi yetu, kusaidia Taifa hili tuweze kujenga madarasa, tujenge miundombinu mbalimbali kwa ajili ya maisha ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maneno haya, naunga mkono hoja. Nashukuru sana kwa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, ahsante sana. Mheshimiwa Ababukari Damian Asenga, atafuatiwa na Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi na Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege, ajiandae.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi ya kuchangia katika Wizara yetu ya Ujenzi na Uchukuzi. Nami kama walivyosema wenzangu, kwanza natoa shukurani za dhati kwa Rais wetu wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa moyo wake mkubwa wa kuendelea kufanya kazi katika nchi yetu. Anasema, hakuna kilichosimama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi tulikuwa Ikulu tunazindua jengo, kuna watu walifikiri litasimama, halijasimama; mradi mkubwa wa Maji wa Bwawa la Nyerere, haujasimama unaendelea; Daraja la Busisi halijasimama, linaendelea. Sana sana vile vilivyosimama, sasa hivi vinaendelea. Mfano ni barabara yetu ya Ifakara – Kidatu ilikuwa imesimama huko nyuma na sasa inaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maneno mazuri haya yanathibishwa na kauli ya kaka yangu Mheshimiwa Freeman Mbowe, anasema mama anaupiga mwingi sana na mama anafanya kazi kubwa. Mheshimiwa Mbowe ameanza kumwelewa mama sasa hivi, hawaongei tupu tupu, wanaanza hata kufanya fanya miradi ya maji, nimeona huko, na wakichangisha pesa wanazibakiza kwenye vijiji, hawaondoki nazo zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii yote ni uthibisho wa uongozi mzuri wa Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kujenga umoja wa nchi yetu na tunamuunga mkono tunampongeza sana. Mheshimiwa Waziri wewe na watumishi wako wote katika Wizara hiyo, tunawashukuru sana na tunawapongeza sana kwa kazi mnayofanya. Wenzangu wametangulia kusema Wizara hili ni kubwa na kazi ni kubwa kweli kweli na maneno ni mengi, lakini wote ambao Mheshimiwa Rais amewaamini, endeleeni kumsaidia, onyesheni uwezo wenu katika kufanya kazi kubwa na wasaidizi wako wengine kama ma *DG* Bandari na akina Kadogosa huko ni vijana wadogo, wameanika sana katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunawaambia sisi tunajua ipi ni ipi, na ipi siyo ipi? Kama kuna maneno mengine ya kuupuza, wayapuuze waendelee kufanya kazi. Watu wanataka kutoka Dodoma kwenda Dar es Salaam kwa reli. Walale Dar es Salaam waje wafanye kazi Dodoma warudi Dar es Salaam kula bata, Mji wa kibiashara, mama kashasema na kazi iendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri amekuja hapa leo anaomba *3.5 trillion* katika bajeti yake na nina imani Bunge litampitishia bajeti yake. Tunamwomba sana na tunaiomba Serikali hasa Waziri wa Fedha ahakikishe fedha hizi

zinakuja kwa wakati ili miradi hii itimie. Kwa mfano, Serikali kufikia mwaka Februari, 2023 katika sekta ya ujenzi imetoa fedha za kutosha karibu 85 *percent,* lakini ukienda kwenye uchukuzi kule kweli fedha ni chache ni asilimia 59 tu peke yake. Kwa hiyo, tunaweza tukapitisha hapa bajeti lakini utoaji wa fedha ukichelewa, *automatically* miradi itapungua sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya ujenzi, Wizara ya Ujenzi ni mambo ya fedha tu. Sasa ni muhimu sana kama kuna maeneo Mheshimiwa Waziri mnaweza kufanya uwekezaji, ambavyo Mheshimiwa Rais amesema na Wabunge wenzangu wengine wamechangia, yatakayozalisha fedha za kutosha msiyacheleweshe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimezungumza hapa, na hii ni mara ya pili nazungumza. Rais wa nchi, kiongozi wa nchi Dkt. Samia Suluhu Hassan anasema tukiwekeza katika bandari tunaweza kupata nusu ya bajeti ya nchi yetu. Hili siyo jambo dogo, ni jambo kubwa sana kusema nusu ya bajeti ya nchi yetu. Sasa hapa tunazungumza, Wabunge wote tunadai fedha. Tunadai fedha, lakini hili jambo kwanini mnalichelewesha? Kwanini mnasema mnachelewesha uwekezaji katika bandari? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu Mheshimiwa Rais, alienda Dubai mwaka 2021 katika *Dubai Expo,* tukamwona Waziri wa Kilimo na Waziri wa Viwanda. Mheshimiwa Waziri ulikuwepo pale, watu wa bandari walikuwepo pale. Mkaonesha fursa siku nzima pale za nchi yetu, mkapata wawekezaji, mkaanza kuzungumza katika mikata ya nchi na nchi kushirikiana. Jambo mojawapo likiwepo ni bandari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Dubai na *Dubai Port,* wameonesha nia nzuri ya kutusaidia katika Bandari yetu, *DP World*. *Agreement* imeingiwa pale, mchakato hatuoni unaendelea. Tumekwama wapi? Wekeni jambo hili wazi, muungeni mkono Mheshimiwa Rais tupate fedha hizi. Hii bandari imebinafsishwa huko nyuma, imeshabinafsishwa sana, wanasema ooh, usiogope, usiseme, ukisema watu wakubwa; huko nyuma ilikuwepo tangu enzi ya Mkapa mmeweka wapi? Sasa leo Dubai

inafanya vizuri duniani, watu wanakimbilia Dubai, Serikali ya Dubai, *DP World* wanataka kuja kuwekeza katika bandari yetu. Cha msingi, mtuweke wazi, mnawekeza nini? Ajira za Watanzania zitakuwa ngapi? Tunapata Shilingi ngapi? Sasa hivi tulikuwa tunapata Shilingi ngapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapato, *thirty five percent* ya *TRA* ni karibu Shilingi trilioni saba wanachukua bandarini. Akija mwekezaji tunapata Shilingi ngapi? Wafafanulieni Watanzania, wata-*support* uwekezaji huu na bandari haiuzwi, haibinafsishwi tunaingia mashirikiano ya uendeshaji. Hawa *DP World* wanaendesha nchi saba Afrika ya Bandari. Duniani wana bandari 70. Hapa tunafanya siasa, siasa nusu ya bajeti ya fedha tunaikosa. Ukienda huyu wanamkuta huyu; mfanyabiashara anataka kwenda bandarini anachafua wengine, vurugu. Muungeni mkono Mheshimiwa Rais, *agreement* hiyo imeshaingiwa, imeshasainiwa kule Dubai, mchakato wa pili ufuate na mchakato wa tatu ufuate tuweze kunufaika kama wenzetu wa Senegal, Algeria, na Egypt ambapo *DP World* wako kule na wanawekeza kitu kikubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kumalizia kwa kusema kwamba, kwa upande wangu wa Jimbo, nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri, umekuja Kilombero mara mbili. Katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 nilijua ajenda ya Barabara ya Kidatu – Ifakara ni kubwa. Pale Jimboni Kilombero hujakamilisha barabara hii, miaka yako mitano unasepa. Kwa hiyo, nikakaa na wazee wakaniambia, tumezunguka kwenye kampeni tumesema barabara ile isipojengwa hatugombei tena. Ndiyo maana unaona tumelala kwenye matope, tumekaa kwenye kapeti Bungeni, kilomita 66.6. Mheshimiwa Waziri leo karibu kilomita 50 mmeweka. Hiyo ni kasoro kama 15 au 16 hivi ambazo mimi naomba Mungu ngoma hii imalizike hiyo, iishe. Sasa Mheshimiwa Waziri unanijengea barabara mpaka *roundabout* ya Ifakara pale kibaoni, ni kama kilomita tano za mjini unaziacha, ile kilomita tano ya lami ya zamani ni ndogo sana…

**MHE. HAMISI S. TALETALE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Abubakari kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Taletale.

**TAARIFA**

**MHE. HAMISI S. TALETALE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa ndugu yangu Mheshimiwa Asenga, naona anachangia kwa furaha sana, nami natamani furaha yake ihamie kwetu jibu la Kisaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napokea taarifa. Ndiyo ukae vizuri na Profesa Mbarawa, na muda wangu ananiishia.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Asenga, taarifa unaipokea?

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea. Akae karibu vizuri na Waziri hapa apate matunda mazuri. Profesa Mbarawa ni msikivu, *Engineer* Isack ni msikivu, *Engineer* Mativila ni msikivu, watamsadia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema Waziri anatujengea barabara mpaka *roundabout* ya Kibaoni. Barabara hii ikikamilika keshokutwa, mabasi yatapita mjini kwenda Ulanga, kwenda Malinyi, kwenda Mlimba, Ifakara Mjini hapatoshi. Tunaomba ile barabara ya kilometa 10 ya mchepuko ya Mbasa – Katindyuka ijengwe kwa lami watu walipwe fidia. Ndiyo matunda ya barabara ya Ifakara – Kidatu yatatokea. Maana vinginevyo tunaenda kupeleka msongamano Ifakara Mjini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, Mheshimiwa Waziri Mkuu ameelekeza barabara kubwa hizi zinazopita kwenye vijiji, mweke taa za barabarani. Kidatu – Sanje – Mkuwe – Mang'ula A – Mang'ula B – Mwaya – Kiberege – Kisawasawa, wekeni taa kwenye vijiji barabarani. Watu wanauza maembe, wanauza ndizi jioni kwenye vituo vya daladala. Waziri Mkuu kaelekeza, nataka kujua kama mnatuletea taa za barabarani ama hamtuletei?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemwona Naibu Waziri wa Uchukuzi. Ifakara ina kituo kikubwa sana cha *TAZARA*, Ifakara tuna Uwanja wa Ndege sasa hivi kutokana na Mradi wa Kupambana na Malaria wa Ifakara *Health* ambao Mheshimiwa Rais alienda Marekani. Wanafugwa mbu Ifakara pale, ndege zinatua miruko mpaka 50 kwa mwezi. Kila siku karibu inatua ndege ndogo, uwanja wetu haufai. Waziri wa Uchukuzi tunakuomba, kwa sababu barabara hii ya Ifakara – Kidatu sasa hivi inaishia kilomita moja kwenda *Airport*, kwenda *TAZARA* tuunganishie hizo kilomita moja ama mbili tuunganishe na hii barabara kubwa na *Airport,* barabara kubwa na *TAZARA*. Ni jambo ambalo linaweza kusaidia Kata yetu ya Kibaoni ikachangamka kwa sababu ni Makao Makuu ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa taa za Ifakara Mjini na *TANROADS* barabara ile lakini ni kilomita mbili tu umefunga taa katika kilomita tano nilizokuomba. Tuletee hizo taa zilizobaki Mji wetu uendelee kuchangamka na sisi ni wauzaji wazuri wa mchele mzuri, unaonukia. Wanakuja Watanzania wengi sana kununua mchele kule, Wazanzibari wako wengi pale Ifakara. Taa zile zitasaidia mji wetu utapendeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti la mwisho. Juzi tumekutwa na mafuriko. Nimeenda na Meneja wako wa *TANROADS* Mkoa *Eng.* Razak, mtu mzuri. Baada ya mafuriko tu amekuja, ametazama makalavati yale na changamoto zake. Ameona, amesema yuko tayari kutusaidia endapo Waziri utamsaidia. Msaidie *Engineer* atusaidie jambo hilo la makalavati, atusaidie ahadi ya Mang'ula Kona. Mheshimiwa Waziri, umefika Mang'ula Kona, umeona *pressure* ya watu, ahadi ya chama ya Mang'ula Kona. Nimeambiwa karibu shilingi milioni 300 zinatakiwa kukata ule mlima wa hifadhi ambao Rais ametupatia kwa nia njema ya kuondoa kero ya wananchi. Mheshimiwa Waziri tusaidie hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi, atafutiwa na Mheshimiwa Josephat

Sinkamba Kandege na Mheshimiwa Twaha Ally Mpembenwe, ajiandae.

**MHE. JACQULINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa ili niweze kuchangia bajeti hii ya miundombinu ya mwaka 2023/2024. Naomba nianze kwa kumshukuru sana Rais Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri ambayo anaifanya na pia kwa miundombinu mizuri sana ya barabara ambazo zimeweza kujengwa katika Mkoa wetu wa Ruvuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaendelea nataka tu nikueleze kwamba sisi wana Ruvuma tumebaini kwamba Mheshimiwa Mbalawa kumbe si Mbalawa ni Mbawala wa kwetu Ruvuma. Kwa hiyo amefanya ujanja ujanja tu wa kubadilisha jina ajiite Mbalawa ili akwepe majukumu ya kupeleka miundombinu kule Ruvuma. Kwa hiyo wana Mbawala wenzako wamenituma niseme haya yafuatayo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya *bypass* ya kilometa 16 ya Songea Mjini ambayo ni barabara yenye urefu wa kilometa 16, inatoka Mletele kwenda Msamala mpaka Namanditi. Miaka mitano iliopita nikiwa hapa katika Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, nimeshaizungumza zaidi ya mara nne, na barabara hii ilikuwa wakati naizungumzia ilikuwa na urefu wa kilometa 11, sasa hivi zimezaliwa kilometa nyingine, sasa ina urefu wa kilometa 16.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa Mheshimiwa Waziri alete pesa ili tujenge ile barabara. Kuna msongamano mkubwa sana katika Manispaa ya Songea, malori ni mengi mno yanayobeba makaa ya mawe. Jamani makaa ya mawe yanayopita katikati ya mji kwa kubebwa na malori ni zaidi ya malori 1,000 kwa siku. Ndugu zangu naomba mtusaidie. Kumekuwa na ajali nyingi sana kumekuwa na mitobozano mingi sana kati kati ya mji. Kwa hiyo tunaomba, ili kuwanusuru wananchi wa Manispaa ya Songea tujengee ile barabara ya *bypass* ya kilometa 16 ili sasa mji wetu uweze kuendelea vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya Namtumbo – Tunduru, kwa maana ya Mtwara Pachani kwenda mpaka kule Lingusenguse na hatimaye kufika Mbesa, Mbesa - Tunduru, barabara hii ina urefu wa kilometa 303. *Feasibility study* tayari imekwisha fanyika, tatizo ni nini barabara hii haitangazwi ili kuleta fedha na iweze kuanza kujengwa? Mheshimiwa Mbawala mwenzetu, tunakuomba sana utusaidie ili barabra hii iweze kujengwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa barabara ya Likuyufusi - Mkenda yenye urefu wa kilometa 24, niishukuru sana Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na jitihada zinazofanywa na dada yangu Jenista Mhagama na mimi pia nasema tena, maana ninasema kila siku humu ndani. Kilometa 60 za Barabara hii tayari Serikali imeonesha *commitment* ya kuanza kuijenga. Sasa kuonesaha *commitment* ni jambo zuri lakini tunataka mafungu yaende ili sasa ianze kujengwa mwaka huu wa fedha. Barabara hii itajengwa kilometa 60 kutoka Likuyufusi mapaka pale Mkayukayu. Sasa tunataka Serikali iweke pia *commitment* kutoka Mkayukayu mpaka pale Mkenda, kilometa 64, ili ianze kujengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutoka hapo Mkayukayu hakuna *commitment* yoyote ya Serikali. Barabara hii ina urefu huo, kwa hiyo mkijenga kipande nusu halafu baadaye inasubiri tena miaka mitano hainogi kwa hiyo malizieni kilometa 124 zote ziwe na commitment ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya urefu wa kilometa 35 Kitai – Ruanda mkandarasi yuko kazini lakini barabara hii ni barabara ambayo itagharimu pesa za Kitanzania bilioni 60. Lakini mapaka sasa hivi mkandarasi amepata *advance* ya asilimia 10 tu ambayo ni sawa na bilioni 5.9. Mkandarasi anashindwa kuendelea na kazi, karibu anasimama kabisa na wakati huo huo tunaelekea kwenye masika, tunaomba sasa…

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jacqueline, kuna taarifa.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Taarifa iwe ya maana na mnanijua. Taarifa iwe ya maana.

**MWENYEKITI:** Karibu Benaya

**TAARIFA**

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Napenda kumpa taarifa mchangiaji kuhusu barabara hii ya Kitai Kwenda hadi Ruanda na inaelekea hadi Lituhi. Mkandarasi amesimama tangu mwezi wa pili kwa sababu ya kukosa malipo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jacqueline taarifa unaipokea?

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Makofi mengi sana kwa Benaya. Nimeupokea mchango huo. Ahsante sana, nataka taarifa zenye afya kama hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyofafanua na inapita kwenye jimbo lake, ni sahihi kabisa kilometa 35 ambazo sasa ndio magari yale yanayobeba makaa ya mawe yanapita kwenye barabara hiyo. Kwa hiyo tunaomba pesa iharakishwe kupelekwa pale ili barabara hii iweze kujengwa. Kutokufanya hivyo maana yake ni kudumaza hali ya uchumi katika Mkoa wa Ruvuma na katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali hadhalika Ruanda – Lituhi ameshanisaidia hapo Benaya kilometa 50 mkamalizie pale. Imetangazwa lakini pesa hazijapelekwa. Kutangazwa ni jambo moja, kupeleka pesa ni jambo jingine. Sasa Mheshimiwa Mbalawa mwenzetu tunaomba upeleke pesa kule ili barabara hizi zianze kujengwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nizungumzie suala la reli, kwa maana *SGR*. Nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri sana anayoifanya. Majuzi amesema kwamba miradi yote iliyoachwa na Hayati Dkt. John Joseph Pombe Magufuli anahakikisha anaimaliza kwa asilimia 100. Ninampongeza kwa sababu kazi ya *SGR* inaendelea. Hali

kadhalika nimpongeze sana *CEO* wa *SGR* ambaye ni kaka yangu Kadogosa ambaye anafanya kazi nzuri sana. Kaka yangu Kadogosa wewe fanya kazi kelele za chura hazimzuii tembo kunywa maji, hizo ndizo changamoto za kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama wajumbe wa kamati ya *PAC* tumekwenda tumekagua namna mradi unavyoenedelea. Mradi ni mzuri mabehewa ni mazuri, hayo mengine yote ni majungu, endelea kufanya kazi na Mungu akutie nguvu, endelea kupambana, sisi tuko nyuma ayako tutaendelea kukutia moyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nizungumzie sasa reli ya Mtwara – Mbamba Bay. Mimi naomba sana, ninaamini kabisa Mheshimiwa Mbawala hajaona yale malori ambayo yanabeba makaa ya mawe kule. Angeyaona huyu Mheshimiwa Mbawala mwenzetu kwa kweli angeweza kuchukua jukumu la kuharakisha ujenzi wa reli kutoka Mtwara Kwenda mpaka Mbamba Bay kwa sababu hali ya barabara sasa hivi ni mbaya. Malori yale yanachimba barabara haiwezekani. Ukiangalia barabara ambayo imetengenezwa hivi karibuni inayotoka Songea kwenda mpaka Tunduru pale katikati pale Namingwea mashimo yanafikia hapa kiunioni. Ndugu zangu hali ni mbaya sana. Kwa hiyo tunaomba sasa reli hiyo ikijengwa kwa haraka itarahisisha sana ubebaji wa mizigo, badala ya kubeba kidogokidogo basi itapakia mabehewa mengi na yatasafirishwa kwenda katika Bandari ya Mtwara na kupeleka maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwaambie makaa ya mawe yaliyoko katika Mkoa wa Ruvuma ni makaa *super* ni *grade number one,* na ndiyo maana yamekuwa na wateja wengi sana. Daraja ya Mitomoni mwaka jana namalizia…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Jacqueline. Muda wako umeisha

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia dakika mbili.

**MWENYEKITI:** Malizia sekunde 30.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, daraja Mitomoni mwaka jana nilipiga magoti hapa Mheshimiwa Mbawala wewe utapata laana na wana Ruvuma. Daraja lile halijajengwa watu wanaendelea kufa pale.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jacqueline…

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jacqueline, Mheshimiwa Mbunge…

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Litengwe kilometa 22 tunaomba kujengwa Kigonsela kilometa 35. Baada ya maneno hayo machache…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, Mheshimiwa Jacqueline anaitwa Profesa Mbarawa naomba uendelee kumuita Mbarawa na siyo Mbawala.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, yeye anaelewa na ndiyo maana anacheka.

**MWENYEKITI:** Nashukuru sana, muda wako umeisha nashukuru sana Mheshimiwa.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Ahsante sana, naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege, atafuatiwa na Mheshimiwa Twaha Ally Mpembenwe, Mheshimiwa Catherine Valentine Magige ajiandae.

Waheshimiwa Wabunge naomba tuwaache watoa hoja, tusiwasumbue ili waweze kutoa hoja za Waheshimiwa Wabunge, tafadhali sana. Mheshimiwa Sinkamba aendelee.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nina kila sababu ya kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehema kwa kunijalia afya ili na mimi nisimame mbele yako kuweza kuchangia hoja ambayo imeletwa kwetu leo. Naomba nianze kwa kuunga mkono hoja. Nina kila sababu ya kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri ambayo anaifanya, na sisi wana Rukwa tuna kula sababu ya kumuombea kwa Mwenyezi Mungu ampe afya katika kuendelea kuwatumikia Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tumefanyiwa tukio la kihistoria, kwa mara ya kwanza baada ya kwamba tumepiga kelele kwa muda mrefu Mheshimiwa Mbalawa umeenda kufanya tukio ambalo halitasahahulika, la Kwenda kuweka saini juu ya ujenzi wa uwanja wetu wenye thamani ya bilioni 53. Ni matarajio yetu na matumaini yetu matumaini yetu makubwa kwamba uwanja huu wa ndege utakamilika kwa mujibu wa mkataba ndani ya miezi 18, tumesubiri muda wa kutosha hatutarajii *extension* hata ya mwezi mmoja maana uwanja huu tulitamani uwe umekamilika tangu zamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo naomba niungane na mwenzetu, Mheshimiwa Kiumbe Ng'enda ambaye aliyeelezea juu ya umuhimu wa kuwepo kwa meli katika Ziwa Tanganyika. Maneno haya hayapendezi, hivi leo tunavyoongea hakuna meli ziwa Tanganyika, na ahadi imekuwa ikitolewa na Serikali, mara wanataka kufanya ukarabati wa *MV* Liemba, mara meli mpya; na ni vizuri tukawaambia Serikali, tusije tukafanya makosa kama walivyofanya wenzetu wa *DRC* tukajenga meli ambayo tunadhani kwamba itachukua abiria 600 halafu tukawakosa hao. Ni vizuri Serikali mkafikiria wakati mnaenda kuweka mkataba tukafikiria kujengewa meli mbili ili ziwe zinapishana moja ikiwa Kigoma nyingine iwe Kalambo, kulikoni kujenga meli moja na kwa bahati nzuri hatujafikia *extent* ya kuweka mkataba, kwa hiyo ni vizuri Serikali mkalitazama; kwa sababu itakuwa si busara kwamba eti meli tusubiri itoke Kigoma sisi ambao tuko Kalambo tunasubiri mpaka ije hiyohiyo haitakuwa na msaada. Kwa hiyo namuomba Mheshimiwa Waziri na Serikali kwa ujumla mlifikirie hili kwa mara ya pili kabla hamjaenda kuanza kujenga meli hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nipongeze kazi nzuri, na kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri imeonesha juu ya ukamilikaji wa ujenzi wa barabara ya kiwango cha lami kutoka Sumbawanga hadi Kasanga *Port* jumla ya kilometa 107, kazi nzuri sana hongereni. Lakini kazi nzuri hii inakuja inaunganishwa pamoja na ujenzi na upanuzi wa bandari ya Kasanga. Kazi ambayo inafanyika ni kazi nzuri lakini niiombe Serikali, kama tunataka kumaliza mzizi wa fitina ni namna gani Watanzania tunatumia fursa ya kwenda Congo *DRC* tukiwa tunatoka Tanzania bila kupita nchi Jirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri leo wapo watu wa *TATOA*, watu ambao wanaendesha malori, ninaamini wamehakwambia adha ambayo wanalazimika kukutana nayo wakati wanapoenda Congo ya Lubumbashi Kwenda kulazimika kukaa mwezi mzima kwa nchi ambazo si za kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na nimkumbushe Mheshimiwa Waziri, uchumi wa kibiashara ni uchumi ambao lazima kwa vyovyote vile tushindane. Mwenyezi Mungu ametujaalia tuna *port* ambayo mmefanya vizuri, imeebaki kazi moja tu, kuhakikisha namna gani imetoka Kasanga *Port* Kwenda Congo ya Lubumbashi. Na hili niiombe Serikali, najua kuna maboresho makubwa ambayo mnafanya juu ya Sheria ya Manunuzi, kwamba itatoa fursa kwa *PPP* ambayo kwa vyovyote vile *private sector* itaweza kushiriki. Na nimekuwa nikiiomba Serikali muda wote, kwamba si lazima Serikali ndiyo itoe fedha Kwenda kujenga upande wa pili wa Congo, lakini ikiwapendeza mtakuwa mmefanya vizuri zaidi. Wenzetu Uganda wamefanya sisi tunashindwaje ilhali tuna uhakika ni kitu ambacho tunakipata huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi ya asilimia 80 ya *copper* ambayo inapatikana *DRC* inapatikana Katanga ambayo ndiyo Lubumbashi na njia ambayo rahisi ni kupita kasanga. Nilishasema mara nyingi na Mheshimiwa Waziri naamini hii itakuwa ni kuchangia kwa mara ya mwisho, ninachotarajia *next time* tuone utekelezaji. Nimekuwa nikikwambia kwamba Wabelgiji walifanya uchunguzi, kwamba sehemu nzuri kwa ajili ya kuwa na *port* upande wa *DRC* ni eneo la Mulilo. Eneo la Mulilo unali–*access*

kiurahisi zaidi ukipitia Kasanga *Port*. Naamini haya yatakuwa yamesikilizwa.

Mheshimwa Mwenyekiti, na ninaomba nimuombe Mheshimiwa Waziri jambo lingine la pili; ni juu ya reli yetu ya *TAZARA*. Ni kuweli usiopingika, na kamati imesema kwamba mkataba ulivyo hautoi fursa kwa ajili ya sisi ambao tunataka kuwekeza na kipande cha upande wetu kiwe kizuri. Mkautazame mkataba ili tuanze kujenga kutoka Tunduma Kwenda Kasanga na nchi hii yote itakuwa na *network* ya kuwa na reli, huku iko *SGR* huku *TAZARA*. Itakuwa imesaidia sana kwa ajili ya kuhakikisha kwamba Tanzania yote inakuwa *networked*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mkautazame mkataba, yafanyike maboresho ili eneo la kwetu tufanye uwekezaji, wenzetu kama hawakao tayari kwa *speed* ambayo tunaenda nayo ni vizuri sisi ambao ni wanufaika tukahakikisha eneo hili linaenda kufanyiwa kazi. Na ukitazama tangu zamani inaonesha kwamba reli hii inatakiwa iende mpaka Mbamba Bay ikaunganishe na kule Kyela, mkatizame *study* ziko kwenye ofisi zenu, ili jambo hili liweze kukamilika mara moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nipongeze; kuna ujenzi wa barabara kutoka Matai kwenda Kasesha *border* ambayo ni kilometa 50. Jambo kubwa limefanyika na tayari katika mkataba ule unaonesha kwamba ndani ya miezi 18 kipande hicho kitakuwa kimekamilika na hakika kwa utendaji mzuri wa Wizara hii natarajia kazi hii itakamilika kwa wakati ili wnanchi wa Kalambo, Rukwa na wananchi wanaotoka Tabora, wanaotoka Mwanza wanaotaka Kwenda Zambia iwe ni rahisi Kwenda kule bila kulazimika Kwenda mpaka Mbeya, na ndiyo namna pekee ya kuweza kuifungua nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, itoshe katika hayo ambayo nimeyasema ili yachukuliwe kwa uzito mkubwa zaidi kuliko nikitoa mengi akakosa muda wa kuyafanyia kazi. Akayafanyie kazi haya tukija bajeti nyingine tuwe na uhakika meli ziko si moja, meli mbili ndogondogo badala ya kuwa na meli moja kubwa haiutatusaidia. Tuhakikishe kwamba tuna–*access* Congo *DRC*

kupitia Kasanga Kwenda Lubumbashi ili hayo matunda ambayo unahitaji kuchuma bila hata kutafuta ngazi tuanze kuyachuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Waheshimiwa Wabunge wako wageni wa Mheshimiwa Maimuna Pathan, Mbunge wa Viti Maalumu, ambao ni wanafunzi wa vyuo mbalimbali vilivyoko Dodoma na kutoka Mkoa wa Lindi. Ahsante, karibuni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Twaha Ally Mpembenwe atafuatiwa na Mheshimiwa Catherine Valentine Magige, Mheshimiwa Naghenjwa Kaboyoka ajiandae.

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi kuweza kuchangia katika Wizara hii muhimu sana. Lakini awali ya yote kwanza nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa na nzuri ambayo anaendelea kuifanya katika Taifa hili kwenye sekta hii na sekta nyingine zote. Dunia inajua, Afrika inatambua na Watanzania tunajua hilo, kwamba Mheshimiwa Rais anafanya kazi nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nichukue fursa hii vile vile kumpongeza Mheshimiwa Waziri, yeye pamoja na Naibu Mawaziri wake waendelee kuwa wanyenyekevu hivi hivi na mabega yao yaendelee kuwa chini. Tunashukuru sana kwa ushirikiano mzuri ambao mnaendelea kuutoa kwa Wabunge wote ambao tuko ndani humu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa mchoyo wa fadhila, nimpongeze sana Mkurugenzi Mtendaji wa *TASAC* kwa kazi kubwa na nzuri anayoifanya. Tunahitaji vijana wa namna hii wenye uwezo mkubwa wa kuweza kuleta mawazo yaliyo chanya katika kuweza kuibadilisha nchi hii. Lakini vilevile nimpongeze Mkurugenzi wa *TPA,* anafanya kazi nzuri sana yeye pamoja na wasaidizi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana nilikuwa jimboni tunakimbiza Mwenge wa Uhuru. Wakati nikiwa jimboni tulifika katika kata moja inaitwa Kata ya Mahege. Pale watu wakimbiza Mwenge wa Uhuru kitaifa walikuwa wanapata chakula, lakini nilikuta pale mkutano nimeandaliwa akiwepo Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi, mzee wangu alikuwepo pale pamoja na Katibu Mzee wangu Mketo walikuwa wako pale, na wananchi wamejumuika kwa pamoja. Lengo la mkutano ule walimuhitaji Mwenyekiti wa Chama, Mbunge pamoja na Katibu.

Mimi niseme tu nimshumuru sana Mwenyekiti wangu wa Chama cha Mapinduzi Wilaya, *Comrade* Juma Kassim Ndaluke kwa hekima kubwa aliyo nayo yeye pamoja na Katibu wangu Zacharia na Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya alikuwepo pale. Lengo kubwa la mkutano ule wananchi wale walikuwenda kuniuliza swali moja; hivi Mbunge, kuongea unaongea hivi hata unashindwa kuruka sarakasi na wewe upate barabara hii ya Bungu – Nyamisati? Mbona wenzio wanaruka sarakasi wanafanikiwa wewe una shida gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niseme tu, nimshukuru sana Mwenyekiti wangu wa Chama Wilaya alitumia hekima kukimaliza kikao kile kwa muda mfupi sana. Aliwaambia wananchi wale pamoja na Katibu wa Chama na Mwenyekiti wake, kwamba yeye ndiye msimamizi wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi Wilaya ya Kibiti. Kwa tafsiri hiyo aliniagiza kwamba Mbunge umekimbiza mwenge leo, lakini nakusamehe usikae kwenye mkesha huu nakuomba nenda Bungeni, tunajua kuna bajeti inaendelea kule ya Wizara hii, kwa hiyo, nenda kalisemee hili kwa msisitizo wa hali ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimwambie Mheshimiwa Waziri, Bungu – Nyamisati kimekuwa ni kilio cha muda mrefu sana. Sawa mimi utaalamu wa kuruka sarakasi sina basi hata haya ninayozungumza Profesa Mbarawa huyaelewi? Sasa nizungumze lugha gani ili niweze kueleweka? Maana nikizungumza Kindengereko huwezi kufahamu, mimi siwezi kuruka sarakasi, ninachoweza kufanya nicheze ngoma ya kwetu kinyafumbili labda unaweza ukanielewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna shida kubwa sana katika barabara ile, kuna vifo vinatokea. Nataka niseme tu Mbunge mwenzangu wa Jimbo la Mafia ambaye ni Waziri vilevile, juzi saa 10.00 usiku alinipigia simu akiniambia Mpembenwe kuna shida katika ile barabara, kuna lori limekaa vibaya pale, kwa hiyo, wananchi wanapata tabu na mvua ilikuwa inanyesha. Haya ni matatizo makubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba tu lichukuliwe jambo hili *on a serious note*. Wananchi wa Jimbo la Kibiti tunahitaji barabara hii, kwa sababu hizi habari za upembuzi yakinifu, usanifu wa kina tumechoka. Wazee wale watakwenda kunihukumu. Yuko pale ndugu yangu Mketo, Katibu wa chama, ni mkorofi kweli kweli, lakini wananchi wa pale nao ni shida moja kwa moja. Mimi pamoja na wananchi wangu tunaomba tusaidiwe katika jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema haya, naomba nizungumze jambo moja la msingi katika Wizara hii na huu utakuwa ni mchango wangu mmoja tu. Naomba nizungumze kuhusiana na suala zima la Bandari yetu ya hapa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Singapore ilipata uhuru mwaka 1965, lakini katika miaka 50 ya nyuma ambayo imepita *capital income* ya Singapore ilikuwa chini ya dola 324. Mwaka 1975 Singapore *per capita income* ikawa imebadilika, tunazungumzia dola 60,000 nendeni mkaangalie kule mtapata taarifa hizo. Nini maana yake? Maana yake ni kwamba *strategically* wameweza kuitumia bandari vizuri ili kuhakikisha kwamba inakwenda kuchangia vizuri kwenye pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha sana, Mheshimiwa Rais amezungumza katika nyakati tofauti katika hafla tofauti za Kiserikali akiwa anaonesha hisia zake za hali ya juu za kutoridhishwa kwake na jinsi gani *performance* ya bandari yetu inavyoshindwa kuchangia ipasavyo katika pato letu la Taifa. Niombe, sheria tumezitunga sisi wenyewe hapa na sisi wenyewe ndio tumezipitisha sheria hizi, hivi suala hili la *PPP* lina shida gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemfuatilia vizuri sana Mheshimiwa Profesa Mbarawa katika hotuba yake, ametenga hela bilioni 88 katika kuweza kufanya kuboresha pale, *this is a joke,* bilioni 88 haiwezi ikatuambia kitu chochote. Asilimia 46 ndio pekee inapatikana kutoka katika mapato yetu ya makusanyo ya *TRA* pale bandarini, kwenye mipaka yetu na maeneo mengine. Tunataka kuiona sasa bandari inatoka katika hatua moja inakwenda kwenye hatua nyingine. Nami niseme tu, tumefanya jaribio hilo, pale Tanga kuna fedha zimetumika na Serikali tumeweza kupanua Bandari ya Tanga kwa namna moja ama nyingine. Kwa tafsiri hiyo maana yake ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumetoka sasa katika *metric tones* 750,000 tunakimbilia *metric tones* 3,000,000. Haya yanaweza kufanyika kwenye bandari yetu ya Dar es Salaam. Katika hotuba Mheshimiwa Waziri ametuambia *tonnage* zilizokuwa zinapita pale ni milioni 20, bado hazitoshi Mheshimiwa Profesa Mbarawa. Naamini, sisi Waswahili tumezoea kusema mzigo mzito mkabidhi Mnyamwezi, lakini naamini hata Wapemba vilevile mzigo mzito wanaumudu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Profesa Mbarawa aje hapa na mpango mkakati wa kuweza kuangalia suala zima la *PPP* tuweze kuwekeza ili sasa tuweze kuona tunakwenda kutatua kero za wananchi kule katika majimbo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge wote wamesimama hapa wanazungumza suala la barabara. Wabunge wamesimama katika Wizara zilizopita wanazungumza masuala ya dawa, vituo vya afya na mambo mengine; fedha iko pale bandarini kwa hiyo, tuchangamke tuweze kuhakikisha tunaleta utaratibu uliokuwa sahihi ili sasa tuweze kuona wanakuja hapa wawekezaji wanakwenda kuwekeza pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kitu kimoja; juzi niliweza kuwasiliana na Mwalimu wangu, Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo, aliniuliza hivi Mheshimiwa Mpembenwe una nini la kusema kuhusiana na suala zima la bandari pale? Nikamwambia mimi naangalia katika eneo moja tu, katika *economic*

*perspective*. Akaniambia hapana, mbali ya *economic perspective* angalia vilevile suala zima la mambo ya *operation,* pale pana shida, halafu angalia vilevile suala zima la *ownership*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala zima la *operation* ametoka kuongea hapa ndugu yangu Mheshimiwa Kilumbe; amesema kwamba, pamoja na matatizo yote ya *TICTS,* lakini fedha walizokuwa wanatoa ni nyingi kuliko zilizokuwa zinapatikana kwa kupitia Mamlaka yetu ya Bandari. Kwa hiyo, niwaombe sana, Serikali waje na mpango mkakati wasiogope, sisi ndio tumetunga sheria. Kama leo Profesa anasimama hapa anatuambia barabara hii inajengwa kwa *EC + whatever F,* barabara hii inajengwa, *why can't we do this* pale bandarini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana tuliowapata sasa hivi Mkurugenzi Mtendaji anafanya kazi vizuri pamoja na wasaidizi wake. Twendeni tuwape moyo vijana hawa. Hizi ndio *brain* tunazohihitaji katika nchi hii ili tuweze kuibadilisha. Tusikae na yale mawazo ya kizamani eti tunakwenda kuuza nchi, nchi itauzwa na Mtanzania mwenyewe? Hiki kitu hakiwezekani. Kwa hiyo, niwaombe waje na mpango mkakati, ili sasa tuweze kuona bandari yetu ile inakwenda kuchangia pato la Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *life expectance* ya pale Singapore ya watu kuishi unazungumzia miaka 83, kwa nini? Watu wanakula bata. Bandari inatengeneza fedha za kutosha, wananchi wana-*enjoy* maisha. Hatuzungumzii *economic growth* isipokuwa tunazungumzia *economic development,* ndio maana *life expectance* ya wananchi wa Singapore ni miaka 83. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Mtanzania wa kawaida atahangaika hangaika, akishamaliza miaka 60, 60 au 62 akisha-*retire* tunachukua kamba tatu, safari imeisha. Nini? Ni kwa sababu uchumi wetu unakua, lakini kukua kwake sio uchumi endelevu. Tunapozungumzia *economic growth* kuna tofauti kubwa sana na *economic development*. Kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Profesa Mbarawa ajitahidi na wataalam wake, waje na mpango

mkakati tuweze kuhakikisha tunakwenda kuboresha bandari yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Catherine Valentine Magige, atafuatiwa na Mheshimiwa Naghenjwa Livingstone Kaboyoka.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Wizara hii ya Ujenzi na Uchukuzi. Nianze kwa kumpongeza Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoifanya ambapo amekuwa Rais wa mfano ndani ya nchi na nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Profesa Mbarawa amekuwa ni Waziri msikivu, mchapakazi na mnyenyekevu pamoja na timu yake. Naomba moja kwa moja nijielekeze katika mchango wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi naweza kusema ni moyo wa uchumi katika nchi yetu. Hatuwezi kukuza uchumi wa nchi kama miundombinu ya usafirishaji wa watu na bidhaa ni mibovu. Duniani kote katika biashara wanategemea zaidi ya asilimia 98 mawasiliano ya usafirishaji wa bidhaa kwa anga, barabara yaani nchi kavu, majini yaani meli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza kuongelea bandari yetu. Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari kwa mujibu wa Sheria Namba 7 ya Mwaka 2019 inaruhusu ushirikishwaji wa sekta binafsi katika shughuli za utendaji wa bandari tangu mwaka 2000 kimkataba. Ushauri wangu kwa Serikali, naishauri Serikali iingie mkataba na kampuni yenye uwezo, ili kuongeza ufanisi, tija na mapato kwa Serikali, ili kuepusha hasara kwa wafanyabiashara na ucheleweshaji wa mizigo yao, ma-*container* huko bandarini na kwenye kupakua mizigo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bandari ya Dar-es-Salaam ina changamoto nyingi sana, naweza nikazitaja chache; baadhi ya changamoto ni haina viwango vya tija kwa huduma za bandari, mifumo ya TEHAMA haisomani, idadi ndogo ya miundombinu ya kuendesha bandari. Vilevile Bandari ya Dar-es-Salaam imefikia ukomo kuhudumia shehena kubwa za mizigo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiangalia wenzetu, mfano majirani zetu Kenya, Bandari ya Mombasa au Durban *South Africa,* wanafanya kazi vizuri sana, lakini Bandari ya Dar-es-Salaam ni sawasawa mfano unachukua kirikuu hapa unakipeleka kuchukua magunia ya mahindi Soko la Kimataifa la Kibaigwa huku mpinzani wako anaenda na *semi-trailer* kuchukua yale magunia. Kweli hiyo inawezekana? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile imekuwa kero sana kwa wafanyabiashara, tumeona hata huu mgomo wa juzi Kariakoo. Vilevile bandari hii imekuwa inasababisha uchelewashaji huu, wafanyabiashara wanasubiri ma-*container* yao kuyatoa wiki tatu, mwezi, wengine mpaka miezi miwili, hali inayosababisha mitaji ya wafanyabiashara inakata, hali ya maisha inapanda kuanzia kwa wafanyabiashara wa juu mpaka wa chini, bidhaa zinapanda, imekuwa shida tupu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliambiwa kuwa bandari ukitoa mzigo Korea mpaka Dubai unatumia Dola 500 tu, lakini ukitoa Dubai mpaka hapa ni zaidi ya Dola 4,000 na hapa ni karibu, tubadilike. Sasa ninachotaka kumwambia Mheshimiwa Waziri, leo hii kwa kweli, shilingi yake itakuwa halali yangu. Nataka kufahamu kwa nini Serikali inasuasua kuruhusu sekta binafsi kushiriki katika uendeshaji wa bandari? Kesho Mheshimiwa Waziri anapokuja kuhitimisha, shilingi yake ni halali yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijielekeze moja kwa moja katika barabara. Tunamshukuru Mheshimiwa Rais ametenga zaidi ya shilingi trilioni tatu kwa ajili ya kuunganisha barabara katika mikoa saba. Pamoja na Mkoa wangu wa Arusha zimeguswa barabara nyingi sana, lakini kuna kipande ambacho Makamu wa Rais juzi ameenda kuzindua Waso mpaka Sale, lakini hiki cha Sale mpaka Mto wa Mbu naomba barabara hii ijengwe

kwa haraka sana. Wananchi wanaotoka Loliondo kule wamekuwa wakipata shida sana, wanakaa njiani hata siku tatu vilevile lile ni eneo kwa ajili ya watalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaona mama anatangaza *Royal Tour,* lakini pia na hizi barabara nazo tuangalie tuzipe kipaumbele. Barabara ya Sale mpaka Mto wa Mbu naomba Mheshimiwa Waziri aipe kipaumbele sana barabara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije moja kwa moja upande wa reli. Naipongeza miradi ya ujenzi wa reli za kisasa, *SGR,* lakini kinachonisikitisha *Lot 1* na *Lot 2* kwa nini mpaka sasa hivi hazijakamilika? Kadogosa tunamwamini utendaji wake, tunajua ni mtendaji mzuri sana, lakini hapa tatizo ni nini? Watanzania wana hamu na reli yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nashauri, reli hii itakapokamilika, naomba waalikwe sekta binafsi nao ikiwezekana waendeshe reli hii. Serikali imeshaweka nguvu zake kwenye miundombinu, lakini itakapokuja sekta binafsi itasaidia ushindani wa kibiashara, pia kukuza mnyororo wa ajira, pia kuongeza ushindani hatimaye ubora wa kukuza kipato kwa mtu mmoja mmoja na pato la Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie kwa kupongeza *Air Tanzania*. Tumeona Rais mwanamke, tumeona kuna marubani pale wanang'aa wanawake. Nimemwona *Captain Hilda Ringo, Captain Salha* na wengine. Tumeona ma-*air hostess* wamependeza kweli, wana kiwango cha kimataifa. Niwapongeze sana, wapige kazi waendelee kuiletea nchi yetu sifa, waendelee kuhudumia vizuri. Tunajua na wenyewe wanapokea wageni mbalimbali wakiwemo na watalii, waendelee kutangaza nchi yetu, wafanye kazi, wamependeza sana na ni warembo kiwango cha kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mchangiaji wetu wa mwisho mchana huu ni Mheshimiwa Naghenjwa Livingstone Kaboyoka.

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia katika hotuba hii ya bajeti ya Wizara ya ujenzi na uchukuzi. Niseme kweli kwamba, Wizara hii kweli ni kubwa sana na inajitahidi sana kufanya kazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaenda *straight* kwenye shirika letu la *ATCL*. Kitendo cha kusema tunafufua shirika hili na kununua ndege nyingi kilikuwa ni kitendo kizuri sana. Kwa hiyo, niseme kwamba, Serikali haikufanya makosa kuamua kufanya hivyo. Niseme Shirika hili la *ATCL* limejitahidi sana kufanya kazi pamoja na kwamba, limefanya katika mazingira magumu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua kwamba, Mheshimiwa Profesa Mbarawa amejitahidi sana kuona shirika hili linasimama, lakini jambo moja ambalo linanifanya nione kwamba, kwa nini hiki kitendo cha kuweka ndege hizi kwenye Shirika la Ndege hili, *TGFA* kwamba, ndio limiliki ndege zile kwa nia ya kwamba, ndege hizi zisingekamatwa kutokana na madeni ya Serikali, lakini imeshaonekana kwamba, hili halipo. Kama halipo kwa nini ndege hizi hazirudishwi au hazipelekwi *ATCL? (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mkataba huu wa ndege wa *ATCL* pamoja na *TGF* umekuwa ukileta madeni makubwa sana kwa shirika hili na kufanya shirika hili lionekane kwamba, linaweza lisiwe na mwendelezo, yaani tuseme *questionable going concern. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwamba, urari hasi wa kiasi cha shilingi bilioni 157.7 kwa *ATCL* umeletwa na ukodishaji huo. Kwanza tuangalie Ripoti ya *CAG* katika mwaka 2021/2022 ilionesha kwamba, *ATCL* ilitumia shilingi bilioni 29.4 kwa matengenezo ya ndege zake, lakini hapohapo ilitakiwa pia ipeleke shilingi bilioni 25.38 kwenye *TGFA* kama gharama za matengenezo licha ya kwamba, bado kuna zile gharama za ukodishaji ambazo ni kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika *speech* ya Waziri, ukurasa wa 267 umesema kwamba, *ATCL* imeweka mikakati mizuri ya kuweza kupunguza gharama za uendeshaji. Kinachonishangaza

ni kwamba, Mheshimiwa Waziri hakutaja hili tatizo la *TGFA* kuwa bado ndio wamiliki wa ndege hizi ambazo zinafanya kunakuwa na *double cost* ambazo kwa njia yoyote ile hatuwezi kupunguza deni hili au madeni haya ya *Air Tanzania*. *Commitment* iliyotolewa na Katibu Mkuu wa Ikulu mwaka 2021 alisema kwamba, ifikapo tarehe 30/06/2022 umiliki wa ndege za *ATCL* utakuwa chini ya *ATCL* yenyewe kutoka *TGFA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sasa ukiangalia tangu ahadi hii ilipotolewa kwamba, umiliki huu ungehamishwa, mpaka leo ni karibu mwaka mzima na hamna kilichofanyika. Kufuatia malimbikizo ya kukodisha ndege hizo toka *TGFA* takribani shilingi bilioni 113.5 na deni la Mfuko wa Matengenezo ya Ndege takribani shilingi bilioni 60, haya ni madeni makubwa sana ambayo yatafanya shirika hili lishindwe kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nieleze tu kwa kifupi kwamba, nini athari kubwa ambayo athari zake zitaletwa na huu uhusiano kati ya *TGFA* na *ATCL*. Ni kwamba, *ATCL* inaweza kufutiwa uanachama wake katika Shirika la Mashirika ya Ndege Duniani *(IATA)*. *ATCL* inaweza kufutiwa mifumo ya kimataifa ya ufuatiliaji wa mizigo. *ATCL* inaweza kutolewa katika mfumo wa usuluhishi wa mauzo ya tiketi duniani *(IATA Clearing House)*. Shirika hili linaweza kutolewa katika mfumo wa uuzaji na usambazaji wa tiketi duniani *(Global Distribution System),* pia *ATCL* inaweza kushindwa kupata vibali vya kufanya safari katika Mataifa mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia pamoja na mikakati kwamba, *ATCL* inataka ifanye *interlining and code sharing,* lakini kwa urari huu ambao ni hasi hili linatia mashaka sana na ukiangalia kwamba, *ATCL* haiwezi kukopesheka kutokana na hali halisi ilivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa ushauri ufuatao, kwamba, Serikali ifute malimbikizo yote ambayo yamepelekwa katika shirika hili ambayo ni takribani bilioni 113.5 na deni la Mfuko wa Matengenezo ya Ndege ambalo ni takribani shilingi bilioni 6.0 na kwamba, umiliki huu wa ndege upelekwe moja kwa moja kwa *ATCL* badala ya kuwa *TGFA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, faida gani tunatarajia kwamba, *ATCL* ikiwa mmiliki moja kwa moja? Ni kwamba, ndege zote za *ATCL* kama zile *Air Bus, Boeing 77, 787A.8, Dreamliner,* kwenda vituo vilivyopangwa kama Johannesburg, London, Nigeria na sehemu nyingine, hivyo kufanya ndege hizo kuweza kufanya kazi zake kikamilifu. *CAG* ameonesha kwamba, ndege hizi kwa kutokufanya kazi zake kikamilifu kwenye *full capacity* zimeleta hasara ya shilingi bilioni 45 katika mwaka 2021. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni wazi Waziri hili analiona na ndio maana amekwepa kuweka taarifa hii ya ubia kati ya ndege hizi kwa *TGFA*. Kwa hiyo, anajua kwamba, tumelisema sana kwenye Kamati yetu ya *PAC,* lakini hakujachukuliwa hatua yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, faida gani itapata *ATCL* pia, kwa kuipa umiliki wa ndege zote? Ina maana kwamba, gharama zake za uendeshaji zitashuka kwa asilimia 30 na hasara kuondolewa kwa asilimia 171 ili ndege hizo ziweze kuonekana kwamba, kweli zina-*perform* vizuri. Kama *ATCL* itaweza kumiliki ndege zake zote itaweza kuanzisha *auxiliary services* zake ambazo ndio zinaleta faida kubwa katika mashirika ya ndege. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri Profesa Mbarawa akija kuhitimisha hotuba yake alieleze Bunge lako Tukufu kwa nini imechukua muda mrefu hivi *TGFA* kukabidhi ndege hizi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kunaundwa Kamati, tunajiuliza, hivi wakati ndege hizi zikiamuliwa kupelekwa *TGFA* Kamati ilichukua zaidi ya miaka miwili kuzungumza suala hili? Kwa ajili hiyo, niombe kwamba, Serikali ione athari hizi na ielewe kwamba, hili shirika pamoja na kwamba, tumeweka mikakati mingi, inatumia fedha nyingi za Serikali ambazo ni fedha za umma, lakini bado tumelifunga miguu na mikono halafu tunaliambia likimbie. *(Makofi)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe Serikali iweze kuweka wazi kwamba, kweli itatoa lini, iwe na *commitment* ambayo ile ya Katibu Mkuu huyu wa Ikulu ambaye sasa hivi ndiye Katibu Mkuu Kiongozi imeshindikana, mwaka mzima sasa hivi lakini hata hotuba ya Waziri haikuzungumzia suala hili. Kwa hiyo, inasikitisha

kwamba, Serikali imechukua muda mrefu sana kuona kwamba, *ATCL* inatakiwa ifanye kazi, iwe *competitive* sawa na mashirika mengine duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufikia hapo, nasema kwamba, hayo ndio yangu kwa leo. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naghenjwa. Waheshimiwa Wabunge tumefikia mwisho wa mjadala kwa mchana huu na tutaendelea jioni na tutaanza na Mheshimiwa Bakar Hamad Bakar, Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane, Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo, Mheshimiwa Yahya Omari Massare na wengine *list* inaendelea.

Waheshimiwa Wabunge, nina tangazo; nawakumbusha Waheshimiwa Wabunge wote kuwa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi itaendesha semina kuhusu Muundo na Majukumu ya Wizara pamoja na Sera ya Ubia na Shirika la Nyumba la Taifa *(NHC)*. Semina hiyo, itafanyika leo Siku ya Jumatatu, tarehe 22 Mei, 2023, mara baada ya kusitisha Shughuli za Bunge, Saa 7.00 mchana katika Ukumbi wetu wa Pius Msekwa.

Waheshimiwa Wabunge wote wanakaribishwa kuhudhuria semina hii muhimu ili kuwajengea uelewa kuhusu shughuli mbalimbali zinazotekelezwa na Wizara yetu ya ardhi.

Baada ya kusema hayo, basi nasitisha shughuli za Bunge hadi Saa kumi na moja jioni.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge lilisitishwa mpaka Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Bunge Lilirudia)*

*Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu.

**NDG. MICHAEL CHIKOKOTO – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano. Tunaanza na Mheshimiwa Bakar Hamad Bakar, Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane ajiandae. Mheshimiwa Francis.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuniona na kuwa mchangiaji wa kwanza katika Bajeti ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi jioni ya leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naipongeza Wizara yetu ya Ujenzi na Uchukuzi kwa namna ambavyo inachapa kazi katika kuhakikisha kwamba inaboresha miundombinu hapa nchini. Hongera sana Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Prof. Mbarawa, pamoja na Wasaidizi wako katika Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuanza kuchangia kwa kuizungumzia barabara inayoanzia katika Kijiji cha Nandete, inayopita katika Vijiji vya Gezaulole Mkoa wa Pwani, pamoja na Kijiji cha Tawi kwenda kutokea Nyamwage.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 16 Agosti, 2010 wakati wa maadhimisho ya kumbukizi za sherehe ya miaka 100 ya Majimaji, aliyekuwa Rais wetu wa Serikali ya Awamu ya Nne, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, alielekeza Mamlaka ya *TANROADS* iweze kuifungua hii barabara kutoka Nandete kupitia Gezaulole – Tawi kwenda kutokea Nyamwage yenye urefu wa kilometa 46 ili iweze kupandishwa daraja na kuwa barabara ya Mkoa. Lakini kwa masikitiko makubwa, napenda nieleze kwamba mpaka kuifikia leo hatujawahi kuona *dozer* wala *grader* likifika pale kuweza kuitengeneza hii barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ingawa watu wa *TANRODAS* wa Mkoa wa Lindi – kwa sababu mimi nilikuwa jikoni pale *TANROADS* Lindi – nilishuhudia ofisi yetu ya *TANROADS* wakati ule ikitengeneza *write-up* ya ujenzi wa ile barabara ambao ulitarajiwa kugharimu shilingi bilioni 1.2 kwa gharama za wakati ule ili iweze kufunguliwa, kukatwa milima, ku-*fill* kwenye mabonde lakini mwisho wa siku kuijenga kwa kiwango cha changarawe. Kwa hiyo kwa masikitiko makubwa nasema kwa miaka 13 sasa hii barabara ambayo iliahidiwa na Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wetu wa Serikali ya Awamu ya Nne, haijaweza kushughulikiwa hata kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kusikitisha kidogo kwa sababu kuna barabara juzijuzi hapa, mwaka 2021, kwa mfano kuna barabara ile inayoanzia Bigwa kwenda kutokea Kisaki pale Morogoro ambayo inapita kwenye Majimbo matatu, Jimbo la Mheshimiwa Abood, Jimbo la Mheshimiwa Innocent Kalogeris pamoja na jimbo la Mheshimiwa Taletale, yenyewe yalitolewa maagizo kama haya na Mheshimiwa Rais wetu, Hayati Dkt. John Joseph Pombe Magufuli wa Serikali ya Awamu ya Tano, na leo hii tumepewa taarifa hapa kwamba mwezi Juni utasainiwa mkataba kwa sababu taratibu za manunuzi zimefanyika, ile barabara inakwenda kujengwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunahitaji angalau changarawe tu kwa kuanzia zile kilometa 46 ili kuweza kuwainua kiuchumi wananchi wa Wilaya za Kilwa, Liwale pamoja na wananchi wa Wilaya ya Rufiji, Mkoa wa Pwani. Kwa hiyo ninaomba Serikali itilie uzito. Tusisubiri mpaka baadaye Kiongozi anafariki ndiyo unaanza kusema tunamuenzi kiongozi. Tumuenzi Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete akiwa hai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho wa siku niseme tu kwamba wananchi wa Kilwa Kaskazini kupitia mikutano yao ya Mabaraza mbalimbali tayari walishaibatiza jina hiyo barabara, walishasema ikitimia ikawa kwa kiwango cha lami wataiita barabara ya Jakaya Mrisho Kikwete. Kwa hiyo, ninaomba Serikali iishughulikie. Nina hakika ikitengwa bilioni 2.5 ile barabara inaweza kufunguliwa, kuwekwa makalavati na changarawe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda niizungumzie barabara ya pili inayotoka Njia Nne kwenda Kipatimu yenye urefu wa kilometa 50. Barabara hii kwa miaka miwili na nusu iliyopita imeweza kujengwa kwa kiwango cha lami kilometa 1.9 na hivyo kuacha kilometa 48.1 zikiwa hazijajengwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa *scenario* iliyopo inaonesha kumekuwa kukijengwa wastani wa mita 700 mpaka mita 600 kwa mwaka, kiwango ambacho ni kidogo sana. Ninaomba katika eneo hili Serikali ije na mradi wa kimkakati wa angalau kilometa 20 katika ile barabara mwaka ujao wa fedha ili mwaka huo unaofwata tuweze kuimaliza ile barabara kwa sababu itabaki eneo dogo tu. Kwa hiyo, niiombe Serikali iongeze fedha katika ile barabara kupitia bajeti ya mwaka 2023/2024 ili barabara ile iweze kuendelea kujengwa kwa kiwango cha lami na iweze kuwa na urefu wa kutosha wa kiwango hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya tatu ninayopenda kuizungumzia ni barabara ya Nangurukuru – Liwale. Nimesoma kwenye randama ya bajeti yetu ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, nimeona Serikali imekusudia kujenga umbali wa kilometa 50 kutoka Nangurukuru kwa kiwango cha lami. Lakini ile barabara ina urefu wa kilometa zaidi ya 230 toka Nangurukuru kwenda Liwale. Kwa hiyo ukiangalia kilometa 50 haifiki hata robo ya umbali ambao unatakiwa kujengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ninaiomba Serikali iongeze angalau kilometa 50 nyingine tuanze na kilometa 100 baadaye tujenge tena 100 ili katika mwaka wa tatu basi tuweze kumaliza. Ikiwezekana mwaka 2025/2026 tuweze kumaliza ile barabara kwa kiwango cha lami kwa sababu wananchi wameteseka kwa miaka mingi katika ujenzi wa ile barabara.

**MHE. ZEBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ndulane, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Kuchauka.

## TAARIFA

**MHE. ZEBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kumpa taarifa mzungumzaji kuhusiana na hiyo barabara ya Nangurukuru – Liwale kwamba siyo tu kwamba imetengwa fedha kilometa 50, mimi ombi langu ni kwamba hizo kilometa 50 fedha hizo zitoke kwenye bajeti hii.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Francis Ndulane, unaipokea hiyo taarifa?

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa yake nimeipokea kwa mikono miwili kwa kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la nne ambalo ninapenda kulizungumza siku ya leo ni kuhusiana na upanuzi wa barabara kulingana na Sheria ya Barabara ya mwaka 2007 *(The Roads Act, 2007)*. Katika mwaka 2007 upana wa barabara ulipanuliwa kwa barabara kuu kutoka mita 45 hadi mita 60 na zile barabara za mkoa zilipanuliwa upana kutoka mita 30 hadi mita 45.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwaambia kuwa hadi kufikia leo katika lile eneo ambalo barabara ilipanuliwa kwa mujibu wa Sheria ya Barabara ya mwaka 2007, wananchi wote wa Mkoa wa Lindi hawajalipwa fidia zao. Kwa hiyo ninaomba Serikali ije na maelezo ni lini itaanza kutekeleza mkakati wa kulipa fidia katika lile eneo ambalo waliliongeza kwa mujibu wa sheria.

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

## TAARIFA

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa mchangiaji kwamba, siyo kwake tu ambako bado hawa wananchi hawajalipwa, hata kwangu Mwibara wananchi wengi wanateseka kwa sababu hawajalipwa fidia zao. Tunaomba Serikali iwalipe fidia zao.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Francis.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naipokea taarifa yake rafiki yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hili inaonekana ni janga la Kitaifa, kwa hiyo naomba Wizara ikadirie fedha, ikiwezekana ianze kulipa kwa awamu katika hizi barabara wakianzia na barabara kuu baadaye waende kwenye barabara za Mikoa na nyinginezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho kabisa, kuna barabara inayotoka Rangitatu kwenda mpaka Kongowe, yenye urefu kama kilometa 12 hivi. Ile barabara ilipangwa kujengwa zaidi ya miaka 10 iliyopita, lakini sijasikia leo hapa kama kuna kasma yoyote imetengwa kwa ajili ya ujenzi wa barabara ile kwa kiwango cha barabara nne. Kwa hiyo, ninaomba wakati Mheshimiwa Waziri anakuja ku-*wind up* atuambie ni lini ile barabara itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami njia nne kutoka Kongowe mpaka Rangitatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Francis Ndulane. Tunaendelea na Mheshimiwa Florent Kyombo, Mheshimiwa Yahaya Massare ajiandae.

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi na mimi kuchangia katika Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nafasi ya pekee naomba nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi nzuri na hasa katika ujenzi wa barabara na miundombinu ndani ya Jimbo la Nkenge, Wilaya ya Misenyi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi hizi zinakwenda sambamba na salamu za Wasaidizi wa Mheshimiwa Rais, nikitoa pongezi kubwa kwa Mheshimiwa Waziri, Prof. Mbarawa, kwa kazi nzuri pia na Naibu Mawaziri wako Ndugu yangu, Mheshimiwa *Eng*. Kasekenya na Mheshimiwa Atupele Mwakibete kwa kazi nzuri

mnayoifanya katika eneo la ujenzi na uchukuzi. Pia niwapongeze Makatibu Wakuu wote wawili wa sekta zote mbili na Naibu Makatibu Wakuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, niwapongeze watendaji wenu ambao wako ndani ya Mkoa wa Kagera wakiongozwa na *Engineer* Yudas Msangi, Meneja wetu wa Mkoa wa Kagera pamoja na wasaidizi wake ndani ya ofisi hiyo, wanafanya kazi nzuri kwa yale malengo na kazi mnazowapangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nina mambo mawili makuu ambayo nitaongelea, nitashukuru lakini pia nitaomba. Suala la shukrani la kwanza, nishukuru Mheshimiwa Rais kupitia Wizara hii kwa kutujengea daraja zuri na kubwa la Kitengule, na Mheshimiwa Waziri umekuja pale, lile daraja limekamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na daraja hilo Mheshimiwa Waziri ukatuahidi barabara ya kilometa 25 ya kutoka Kibaoni – Bunazi kwenda mpaka Kitengule. Ninakushukuru sana kwa sababu uliahidi na manunuzi yameshafanyika na mkandarasi sasa hivi anafanya *mobilization* kwa ajili ya kuanza kazi. Kwa hiyo, ni faraja njema, nikufikishie salamu za upendo, na shukrani zimuendee pia Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru pia kwa kutekeleza ahadi za viongozi. Katika Serikali ya Awamu ya Tano, Mheshimiwa Rais aliahidi barabara ya Mutukula kwenda Minziro. Hii barabara ilikuwa inapita katikati ya msitu. Na Mheshimiwa Waziri mkamtuma Naibu Waziri, Mheshimiwa *Engineer* Kasekenya akaja pale akaona hali halisi. Leo tunavyoongea mmeshafumua ule msitu na barabara inaendelea kujengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri, ambacho ninaomba katika eneo hilo, *speed* ya utengenezaji wa barabara hiyo siyo nzuri. Mategemeo mazuri ya wananchi wa Mutukula na Minziro kurahisisha usafirishaji katika eneo hilo basi niombe kwa kazi nzuri mliyoianza iweze kukamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru kwa ujumla barabara zote zinazosimamiwa na *TANROADS,* nikiangalia barabara ya

Katoma kwenda Bukwali, ipo katika kiwango kizuri. Barabara ya Amshenyi kwenda mpaka Ruzinga iko katika kiwango kizuri, barabara ya Kibaoni – Kasambya – Mutukula – Minziro iko katika hali nzuri, barabara ya Bukoba Mjini – Mutukula iko katika hali nzuri. Kwa hiyo, hii ni kazi nzuri ambayo *TANROADS* mnafanya, tunachoomba ni maboresho na kuhakikisha kwamba sasa tunaboresha kutoka katika hatua tuliyopo kwenda katika hatua nzuri zaidi.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe maombi kwa ajili ya Wanamisenyi na Wanajimbo la Nkenge. Suala la kwanza Mheshimiwa Waziri, Profesa Mbarawa pamoja na Wasaidizi wako, Mheshimiwa Rais alifanya ziara Mkoani Kagera na akatembelea Wilaya ya Misenyi. Tukamuomba barabara ya Katoma – Bukwali, kilometa 35.7. Ni miaka 10 mpaka leo inajengwa, mpaka sasa hivi imejengwa takribani kilometa saba. Kila mwaka tunajenga mita 200, mita 500 Mheshimiwa Rais aliwapa matumaini mazuri Wanamisenyi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri, sasa kama ulitembea mara moja Wilaya ya Misenyi ukatupatia kilometa 25, hizi kilometa 35 ambazo umeshaanza kujenga zinakwama wapi? Nikuombe kwa bajeti hii ya mwaka huu tupatie angalau nusu ya kilometa za barabara ile ambayo ni kilometa 35, tukipata 17 mwaka unaokuja tukamaliza ili sasa tuweze kuomba barabara nyingine za lami za Amshonye kwenda Ruzinga au kutoka Kasambya kwenda Minziro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi najua hilo liko ndani ya uwezo wako, nikuombe sana katika eneo hili muweze kulifanyia kazi. Kwa sababu ukiangalia hata *Hansards* za Bunge, michango yangu yote katika Wizara yako kila siku tunaongea barabara hii. Mheshimiwa Profesa Mbarawa na wasaidizi wako, najua hili liko ndani ya uwezo wako. Ninakuomba baada ya kumaliza hii bajeti Jumatano mimi nitakuwa mteja wako wa kwanza ofisini kwako ili tuyajenge ili tuhakikishe kwenye orodha ya barabara ambazo kidogo umetengea bajeti, tuweze kuwa na bajeti ya barabara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee kwamba barabara ya Kyaka – Katoro – Ibwera na Kyetema. Barabara hii ambayo inaunganisha Wilaya ya Misenyi na Wilaya ya Bukoba Vijijini kwa Kaka yangu, Mheshimiwa Dkt. Jasson Rweikiza imeshafanyiwa usanifu. Tukuombe sana, ukitoka Kyaka – Katoro – Ibwera mpaka Kyetema ni barabara ya muhimu na ukiangalia katika barabara zako, barabara ambayo kidogo imechoka kuliko zote ni barabara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri, kwa hiyo kwa niaba ya wananchi wa Misenyi, lakini naunganisha na wananchi wa Bukoba Vijijini, nikuombe sana eneo hili uweze kulizingatia ili barabara yetu ipate uwezeshaji na iweze kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi lingine kwa niaba ya wananchi wa Misenyi ni barabara ya Mpakani, Mutukula mpaka Makao Makuu ya Mkoa. Mheshimiwa Waziri, hii ni barabara ya lami unaijua, inapitika, lakini inahitaji maboresho makubwa. Tunajua kwamba barabara hii iko katika mpango wa barabara za *East Africa,* lakini Mheshimiwa Waziri, ni miaka mingi barabara hii imekuwa kwenye programu hiyo. Kama ikionekana kwamba huu utaratibu wa barabara za *East Africa* kujengwa, basi Mheshimiwa Waziri tukuombe utafute mafungu mengine ili barabara ya Mutukula ambayo inapita kata za Nsunga, Kasambya, Kyaka, Bugorora mpaka kuja Bukoba Mjini iweze kujengwa kwa kiwango cha Afrika Mashariki na iweze kuwa katika *standard* inayotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri lakini kama tunaona sasa utaratibu huo uko mbali basi nikuombe barabara ile ni uso wa nchi ukiwa unatokea Uganda, hiyo inaonesha sura ya Tanzania kwa wenzetu wanaotoka Uganda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ukiangalia jinsi barabara ilivyo, basi tuiboreshe tuweke na taa za barabani kutoka Mutukula kupita Nsunga – Kasambya – Kyaka – Bugorora – Mushasha mpaka Bukoba Mjini, nafikiri inaweza ikawa na *image* ya nchi, mtu akiwa anaingia Tanzania anaona kweli hapa ni eneo ambalo ni Tanzania kwa sababu barabara zake zote ni nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, katika barabara hii wananchi wale ambao barabara hii ya *East Africa* itajengwa walisimamishwa kwa sababu maeneo yao yalichukuliwa kwa ajili ya upanuzi wa barabara mpaka leo wananchi hawajalipwa fidia. Sasa wananiuliza Mbunge, je, tuendelee na shughuli zetu au tusubiri barabara inakuja?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Prof. ninakuomba sana, kwa sababu nakuaminia, wakati wa kuja kuhitimisha utuambie kama tuendelee kusubiri tunasubiri, subira yavuta kheri. Lakini kama hilo wazo halipo basi Mheshimiwa Waziri nikuombe sasa uweze kuleta majibu ambayo yatatusaidia sisi wananchi wa Misenyi kuwa na jibu ambalo ni sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri, suala lingine ni suala la barabara ya Mutukula – Minziro. Nimeshukuru kama nilivyosema mwanzoni. Lakini katika eneo hili, kama nilivyosema, speed yake siyo nzuri na uwezeshaji unakuwa siyo mzuri, nafikiri bajeti siyo nzuri. Mimi niombe, kati ya vitu ambavyo nitaomba kuja ofisini kwako Jumatano baada ya bajeti, baada ya barabara ya Katoma – Bukwali basi na hii barabara ya Mutukula – Minziro ili uweze kuliangalia kwa mapana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri, ombi la Wanamisenyi na Wanakagera kwa ujumla lingine ni Uwanja wa Ndege wa Kimataifa Kajunguti. Hili tumekuwa tukilichangia, lakini Mheshimiwa Waziri, kwa weledi wako unafahamu sekta yako yote ya uchukuzi na ujenzi. Unajua kwamba uwanja huu ni uchumi mkubwa wa Mkoa wa Kagera na nchi yetu kwa ujumla. Unajua kwamba uwanja huu unaunganisha nchi yetu na Nchi sita za Uganda, Kenya, *South Sudan,* Rwanda na Burundi na hii itainua uchumi wa Mkoa wa Kagera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua kwamba sehemu hii, uwanja huu, wananchi walizuiliwa kuendeleza maeneo yao ili kupisha uwanja ni miaka mingi Na gharama za uthamini zilishafanyika. Mheshimiwa Waziri, nikuombe, wakati unakuja kuhitimisha basi na huu Uwanja wa Kajunguti uutolee neno tuone kwamba unakuja kuanza kujengwa au wananchi wanapewa fidia au uthamini unarudiwa upya? Tunaloomba kwa

Wanakagera ni kuona uwanja huu unaanza kujengwa au basi hatua za awali zinaanza kwa ajili ya kujenga uwanja huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi lingine la Wana-Misenyi ni kuona barabara zile zote ambazo ziko katika mpango wa matengenezo, ziendelee kutengenezwa. Vile vile kuna barabara ambazo zinazilisha hizo barabara zako ambazo zinaunganisha kwenda mpaka mpakani mwa nchi ya jirani. Kwa mfano, tukiangalia barabara ya Abunazi kwenda mpaka Kakunyu, kuna sehemu ambayo barabara hiyo inaenda inapita Mugango mpaka mpakani mwa Uganda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizo barabara ambazo zinaunganisha nchi nyingine ni za kwako, lakini ziko chini ya *TARURA* ambazo zimekuwa hazitengenezeki. Sasa wewe unatengeneza kipande cha nyuma chote vizuri, lakini kwa sababu bajeti haitoshi, ile barabara ya Bugango kwenda mpaka mpakani mwa Uganda, inakuwa iko katika kiwango kizuri. Pamoja na kwamba ni jukumu letu kuomba upandishwaji wa hadhi wa barabara hizo, lakini naomba kupitia ofisi yako na hilo ulione kwa sababu wewe unaunganisha Taifa na Mataifa ili barabara hiyo iweze kutengenezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi lingine ambalo ni la kitaifa lakini linagusa maeneo mengine ambayo nimeona hapa Dodoma, Mheshimiwa Waziri niwapongeze sana kwa ujenzi wa reli ya mwendoksi ambayo inaendelea vizuri, lakini wakati reli inajengwa kuna maeneo ambayo yalichukuliwa ambayo ni sehemu ya miundombinu ya barabara ambayo iliziba wale watu ambao walikuwa wanahudumiwa na hizo barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, nikiangalia katika eneo la Dodoma hapa, nikianzia Njedengwa na Kisasa juu kote ambapo barabara yenu ya *SGR* inapita, sasa maeneo hayo, pembeni mlijenga barabara ambayo ilikuwa inasaidia miundombinu ya magari ambayo yalikuwa yanajenga barabara ya mwendokasi, lakini sasa hivi mmeziba. Nimeona mmeweka *poles,* mnaziba. Sasa wale wananchi unakuta kulia ana nyumba, kushoto ana nyumba, barabara aliyokuwa anatokea ni hii ya mbele ambayo sasa hivi unaweka uzio na kuweka *fence*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua sheria ipo ndiyo mnayoisimamia, lakini naomba busara sasa itumike katika eneo hili ili wananchi hao, hii barabara ambayo ilitumika kipindi cha ujenzi, bila kuathiri miundombinu yetu ya *SGR* basi mweze kuona jinsi ambavyo mnaweza kuruhusu wananchi wakaitumia.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti baada ya kusema hayo, nakushukuru sana. Ninaunga mkono hoja. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Yahaya Omary Massare, Mheshimiwa Haji Amour Haji na Mheshimiwa Francis Isack Mtinga, ajiandae.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa nafasi. Nami namshukuru Mungu kwa kuniwezesha jioni ya leo kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kujadili na kuishauri Serikali katika bajeti hii ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachangia masuala machache tu. Kwanza nichukue fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri anayoifanya. Pia namshukuru Mheshimiwa Waziri wetu wa Wizara hii, Mheshimiwa Prof. Makame Mnyaa Mbarawa kwa kazi anazozifanya kwa weledi mkubwa na uadilifu mkubwa sana, na manaibu wake wawili ambao anaongoza nao, Makatibu Wakuu wote wawili na Naibu Makatibu Wakuu wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nasimama kuipongeza Serikali kwa kutekeleza ahadi zake ambazo imekuwa ni mara chache, lakini mara hii kwa Awamu hii ya Sita katika Jimbo langu la Manyoni Magharibi, nataka niseme, kongole sana watu wa Wizara ya Ujenzi. Tumeona barabara za kilomita 56 ambazo juzi

juzi tu tumesaini, lakini barabara za Mji wetu wa Itigi kilomita kumi na kilomita 56 tuna kilomita kama sitini na kitu ambazo zinatekelezwa pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upo upungufu pamoja na shukurani hizi, unapojenga barabara kuna matukio yanajitokeza. Pale kwenye barabara ya Itigi kumetokea shida kidogo, kuna watu baada ya kutengeneza ile barabara kumesukumiwa kama changamoto kidogo. Tulishaongea na Mheshimiwa Waziri na anajua, lakini kama Mtendaji Mkuu mtusaidie wale wananchi mwakani tena wasipate taabu ile ambayo wamepata mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kushauri na kuzungumzia kidogo kuhusu *LATRA*. *LATRA* imeboreshwa, ameteuliwa Mtendaji Mkuu mpya, tunaona mafanikio yake, lakini usimamizi na kusikiliza maoni ya wadau. Wamekuwa wasikivu mara hii kuliko mara zote kule nyuma. Ninayo rai moja, wanapoenda kutunga kanuni, tunahitaji zitungwe kanuni kwa maslahi mapana ya nchi. Tuangalie zaidi wananchi kuwawezesha kuliko kuwakomoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa na tabia kwamba wanapoachiwa mamlaka kutunga hizi kanuni, wanakuja na kanuni ambazo siyo rafiki kwa wananchi ili kutengeneza adhabu nyingi kwa wadau. Naomba sana nishauri *LATRA* mara hii, mje kama wadau ambao mtawawezesha Watanzania masikini ambao wana nia ya kujikwamua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na hoja moja, eti mtu akiwa na bodi ya kachina, hawezi kuweka *engine* ya nchi nyingine. Bodi ni bodi tu, *engine* yake ilishakufa, angalia ubora wa chombo kile ambacho kimeenda kubeba wananchi wa nchi hii, ndio kitu cha msingi. Kabadilisha difu, kafunga ya Mitsubishi, ina hasara gani? Tunataka tuone je, kile chombo katika ufanyaji wake wa kazi, kitafanya kazi vizuri?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo hivyo katika magari ya mizigo, na hivyo hivyo katika vyombo vingine. Tuangalie ufanisi, tusiangalie kutoka kwa mtengenezaji. Watengenezaji wengine

vitu vingine wameshindwa, wanakuja na sura nzuri ya bodi, *engine* mbovu, miaka mitano imekufa. Utachukua *engine* ya Mchina uende kuweka? Unachukua *engine* ambayo ni nzuri, *engine* ya Mzungu, unaifunga pale, gari ile inafanya kazi vizuri. Nilikuwa na rai hiyo nilitaka niwashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, liko jambo ambalo linaendelea, *VTS* ina miaka sita karibu saba sasa, lakini *VTS* hii haijathibitishwa na Mamlaka ya Ubora *(TBS),* lakini ni sharti la leseni. Linakujaje sharti la leseni, kitu ambacho ni *delicate?* Kwa hiyo, naomba wafungue milango mingine kwa watu wengine waweze kuleta vyombo ambavyo ni bora. Kama ni sharti la leseni, basi *TBS* wathibitishe, lakini ukaguzi wa magari udhibitiwe na *TBS*. Tusije na vitu vipya tukaharibu nchi ikawa ni milolongo na milolongo na milolongo. Ahsante Mheshimiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo la hawa wakandarasi ambao wanajenga reli yetu. Wakandarasi hawa kwenye *local content* hawapo kabisa. Wao wenyewe ni mkandarasi mkuu, yeye mwenyewe ndiye anayeunda kampuni tanzu, anaweka Mtanzania mmoja bosheni, anaonekana ni mbia kumbe hamna lolote. Ipo hiyo *Lot 1, Lot 2* na *Lot 3,* wanajua. Makampuni tanzu yapo, lakini ni ya Waturuki hao hao. Tunaomba sana lifanyiwe kazi, ikiwezekana TAKUKURU waingilie kati, waangalie hili jambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninalo jambo lingine ambalo nashauri leo, nataka nichangie, ni suala la namna gani bandari yetu itakwenda kufanya kazi na kuzihudumia hizi nchi ambazo zinategemea bandari hii? Leo hii watu wa Lubumbashi ambao ndio tegemeo letu, mizigo yao imeshaanza kwenda Durban. Kutoka Lubumbashi kuja Dar es Salaam, kuna tofauti ya kilomita 900, lakini mtu yuko tayari kwenda Durban kwa sababu hakuna usumbufu, yuko tayari kwenda Nakala kwa sababu hakuna usumbufu. Ipo sababu, sisi pia hata barabarani kuna usumbufu mkubwa sana, lakini *LATRA* wanaweka masharti mengine magumu kwa wasafirishaji. Kwa hiyo, nashauri twendeni tukatengeneze miundombinu rafiki, sheria rafiki kwa ajili ya bandari yetu ya Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bandari yetu, tunategemea sana hizi nchi, lakini tulitakiwa tuzitegemee sana nchi ambazo tumezikomboa. Tumepigana vita Uganda, leo tunasafirisha mizigo ya Uganda kwa asilimia mbili tu. Sababu ni nini? Bandari ya Mombasa wamefungua *Dry Porty* pale Kampala. Ukipakia mizigo yako pale, bandari ndiyo wanachukua ile mizigo aidha ni kwa treni, kwa Barabara, wanafikisha kwenye Bandari ya Mombasa. Wakishapakia ule mzigo kwenye meli, unaletewa *draft* uko Kampala. Ukishamaliza kuangalia *draft* yako kama vitu ulivyoweka ni sawa, una-*print*-iwa *bill* pale pale Kampala. Sisi msafirishaji wa *DRC* anatoka Lubumbashi inabidi aje Dar es Salaam, achuke *draft,* aangalie mzigo wake unakoenda, kusaini kama ni sawa, ndiyo a-*print*-iwe *bill,* aanze safari ya kurudi *DRC*. Lazima tuwe wabunifu, tutoke katika zama zile tulizokuwa nazo zamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kufungua *dry port* kweli Lubumbashi? Wanatutegemea, ukachukua mizigo nauli zile zile ukaziingiza gharama za usafirishaji kwa yule mteja, badala ya kusafiri, bandari inakuwa na mzigo ule, inafikisha Bandari ya Dar es Salaam; halafu pale pale Lubumbashi ana-*print draft,* baada ya *draft* ikitoka, akapata *bill* yake pale pale. Utampunguzia *risk* ya kusafiri kwa barabara kwa gari yake au kwa ndege, unatengeneza mteja mwingine kesho na kesho kutwa. Leo watu wanakwenda Durban kwa sababu hiyo.

Mheshimiwa Mwenytekiti, naomba kushauri Serikali yetu tubadilike, twendeni na wakati, tuifanye nchi hii iwe nchi kwa maslahi mapana ya nchi hii. Yapo mengine, muda hautoshi…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Yahaya Omary Massare. Tunaendelea na Mheshimiwa Haji Amour Haji, nilimtaja Mheshimiwa Francis Isack Mtinga na Mheshimiwa Deus Clement Sangu, ajiandae.

**MHE. HAJI AMOUR HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza nakushukuru sana kwa kuweza kunipatia nafasi hii. Pili, nampongeza Rais wetu, Mama Samia Suluhu Hassan kwa

namna ambavyo anafanya kazi kubwa ya kuweza kuipatia Wizara hii ya Ujenzi pamoja na Uchukuzi fedha nyingi sana katika kutimiza miradi yake. Kwa kweli Wizara hii ya Ujenzi na Uchukuzi ni Wizara mama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi ni Wizara kubwa sana na Wizara ambayo ni kiunganishi cha uchumi katika nchi yetu. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi tukiangalia kwa hali ya kawaida, maana yake uchumi wa nchi yetu unategemea Wizara hii. Ukiangalia suala la utalii, linategemea Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini ninazungumza hivyo? Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi imebeba mambo yote makubwa, tukiangalia barabara pamoja na masuala yote ya miundombinu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliangalie suala hili kiukweli kabisa katika Wizara ambayo imefanya mambo makubwa sana ni Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi. Wizara hii kwa kweli ni Wizara ambayo inatakiwa kupigiwa mfano wa hali ya juu sana. Nizungumze ukweli wangu, kwa namna yote ile na niweze kuwasifu viongozi wa Wizara hii akiwepo Mheshimiwa Prof. Mbarawa pamoja na timu yake, kwa kweli wanafanya kazi kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni mjumbe wa Kamati ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma. Bahati nzuri tumezunguka sehemu nyingi sana zenye miradi mikubwa sana, tukianzia suala la Mpanda kuelekea Uvinza, Uvinza – Kigoma, kwa kiasi fulani maana yake huko mahali kuna miradi ambayo ni mikubwa sana tukielekea na Mwanza kuangalia miradi ya meli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuzungumze ule ukweli, katika sekta ambayo imefanya kazi kubwa ni Wizara hii ya Ujenzi na Uchukuzi. Nazungumza hivi kutokana na kwamba, watu wanasema kwamba mwenye macho haambiwi tazama. Ukweli ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge, nasema labda pengine tungefanya safari ya kuzunguka katika maeneo ya Tanzania tukaona namna Wizara hii inavyofanya kazi, ni Wizara ambayo inafanya kazi kubwa sana, ni Wizara ambayo inafanya jitihada

kubwa sana. Kiukweli kama alivyozungumza mama kwamba kazi iendelee, miradi yote ambayo imeachwa na mtangulizi wake Marehemu John Pombe Magufuli, miradi yote mpaka sasa hivi kwa 70%, au 80% naweza kuthubutu kusema kwamba kupitia Wizara hii, maana yake imeshakamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije na suala langu la upande wa sekta ya *PPP* ambayo mara nyingi watu wanaizungumza sana hapa kwamba katika suala la uunganishaji, hii *Private Public Partnership* kwamba kuna suala la huu uunganishaji wa bandari yetu ya Tanzania kupitia Bandari ya Dar es Salaam, hili suala kwa kweli nasema kwamba ni suala zuri na ninaweza kusema kwamba kwa Tanzania nzima, maana yake ni suala ambalo tusiliache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili kwa upande wa Zanzibar, kitu kama hiki cha uwekezaji wa bandari, maana yake tayari Zanzibar wameshaingia mkataba na Kampuni ya *South Africa* katika suala la *PPP (Private Public Partnership),* sasa na sisi kwa kuangalia suala la ufanisi wa bandari yetu ni lazima suala hili tuliangalie katika hali kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mwingine mimi nitakuwa nashangaa sana kuona watu wanabeza suala la uwekezaji wa pande tatu; *Private Public Partnership* kwa dunia nzima. Maana yake kwa sasa hivi, maendeleo mengi makubwa yanaendeshwa kwa mpango wa *PPP*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la barabara ambalo nalo Mheshimiwa Waziri alizungumza kwamba kuna barabara ambayo nayo itakwenda kwa mfumo wa *PPP*. Mimi nadhani kwamba suala hili tujaribu kuliangalia katika hali ya umadhubuti mkubwa sana, isipokuwa suala ambalo ninalolishauri tuwe madhubuti ni katika suala la kuangalia sheria zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije katika suala la taasisi zetu hizi ambazo ziko chini ya uendeshaji wa Wizara yetu hii ya Ujenzi na Uchukuzi. Tukiangalia kwa mfano, kama taasisi ya *TEMESA,* inafanya kazi vizuri, lakini kama ilivyozungumzwa kwa upande wa hotuba ile ya Mheshimiwa Waziri kwamba *TEMESA* ipo kama ni kutoa huduma, nashauri *TEMESA* iwe ni taasisi ya kibiashara. Kwa

sababu inavyokwenda, haiendi katika suala la kuleta tija isipokuwa ni sekta ambayo iko upande wa kutoa *service*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naipongeza Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, nampongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na timu yake kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya katika utekelezaji wa majukumu yake. Pia namshukuru mama kwa kiasi kikubwa sana kwa kuweza kutekeleza miradi yote ambayo ipo ikiwemo ya barabara, ikiwemo ya reli, ikiwemo ya meli na miradi yote ya madaraja makubwa ikiwemo ya daraja la Kigongo - Busisi pamoja na Bwawa la Mwalimu Nyerere*. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Haji Amour. Nilimtaja Mheshimiwa Francis Mtinga, halafu Mheshimiwa Deus Sangu na Mheshimiwa Ramadhan Suleiman, wajiandae.

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia katika Wizara hii ambayo inaunganisha nchi na inaunganisha uchumi. Naomba nianze kwa kumshukuru na kumpongeza sana Rais wetu kwa jinsi ambayo amekuwa akiitendea haki Wizara hii ambayo ina miradi mikubwa yenye fedha nyingi na imeendelea bila kusimama na muda siyo mrefu nchi yetu itakuwa ipo katika hali ya juu sana katika miundombinu katika Afrika. Nimpongeze sana mtendaji wake mkubwa ambaye ni Waziri kwa jinsi ambavyo wanaitendea haki Wizara yao, wanafanya kazi vizuri na kwa kweli nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru pia Waziri, katika siku chache zilizopita amenikumbuka na mimi katika jimbo langu, amekubali tena kwa moyo mweupe katika bajeti hii kwamba atanipatia kilometa kumi za lami pamoja na taa katika Mji wangu wa Nduguti pale Wilaya mpya, katika barabara ambayo inatoka Iguguno kuelekea Bariadi mpaka Simiyu kupitia Sibiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri, pamoja na kunipa hii, basi mipango yake ya kuhakikisha

anaunganisha barabara hii kutoka Iguguno mpaka Simiyu asiiache mbali, kwa sababu ni barabara ya kiuchumi, kiasi kikubwa cha pamba kinachotoka Mkoa wa Mara, Mkoa wa Simiyu wanapita barabara hii na wanakuwa wameokoa kilomita nyingi sana badala ya kuzungukia Mwanza mpaka Shinyanga. Kwa hiyo, naomba ahakikishe barabara hii inaunganika ili wananchi wangu wa Mkalama na wa Mkoa wa Mara na Bariadi waweze kuunganishwa na nchi kirahisi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri, reli yetu inayotoka Manyoni kwenda Singida, kipande hiki kimesahaulika. Sehemu kubwa ya reli ya zamani imekarabatiwa na inafanya kazi. Mpaka leo kwenda kaskazini kule, watu wanaenda kwa treni, lakini kipande hiki muhimu sana kilichojengwa tangu enzi ya mkoloni kimesahaulika. Hii reli ni muhimu sana inaweza kuwa *feeder road* ya kupeleka mizigo kwenye *SGR* pale Manyoni. Kwa hiyo, nakuomba sana katika bajeti za ukarabati wa reli, kipande cha reli cha kutoka Manyoni kwenda Singida…

**MHE. ELIBARIKI I. KING:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**TAARIFA**

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Taarifa.

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa mchangiaji, kaka yangu Mheshimiwa Francis kwamba, siyo tu reli hii imesahaulika, bali Wana-Singida wanatamani kuona kipande cha *SGR* kinatoka Manyoni na kufika Singida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampa mchangiaji taarifa kwamba vitunguu vyote wanavyokula mikoa karibu ya Dodoma, Morogoro na Dar es Salaam, viazi vyote wanavyokula mikoa ya Dodoma na Dar es Salaam, vinatoka Singida. Kwa hiyo, kwa kuikumbuka reli hii, itakuwa imeleta ukombozi mkubwa sana kwa mikoa hii mingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpa mchangiaji taarifa hii.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Francis, taarifa.

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea taarifa hii kwa mikono miwili. Rafiki yangu Mheshimiwa Kingu amesahau, na kuku wote wa kienyeji katika nchi hii wanatoka njia hiyo. Kwa hiyo, kipande hiki ni cha muhimu. Hata ng'ombe, barabara zinaharibika kwa kupakia ng'ombe. Kwa hiyo, wakija na reli itakuwa ni vizuri. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri, kipande hiki mkikumbuke, kinajenga uchumi wa nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka tena nimwombe Mheshimiwa Waziri, katika reli yetu ya *SGR,* huduma karibu zitaanza. Nawaomba sana, wananchi wameisubiri reli hii kwa hamu kwamba huduma ya usafiri sasa itakuwa ni nyepesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napata hofu kidogo, niliona uwezekano wa nauli zitakabvyokuwa, watu wa chini naona kama watakuwa wanapata shida. Naomba sana, ziwepo *category* zote za nauli. Starehe ya juu kabisa tunaotaka kulipa mamilioni sijui malaki, ziwepo; wale wa uwezo wa kati iwepo, vile vile ziwepo madaraja ya chini kabisa ambayo wananchi wanaweza wakapanda, wakatumia. Wote kwa pamoja kwa uwezo wetu tuweze kutumia reli hii ya *SGR* itakapoanza kufanya huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jamii huduma zote zipo. Leo hii wako akina dada wanaovaa wigi la bei ndogo, lakini wapo wanaovaa wigi la Shlingi laki tano. Leo hii wapo watu wanavaa suti za mtumba na wengine wanavaa suti ya mamilioni, ili mradi ipo, wewe utaenda kwa uwezo wako. Kwa hiyo, naomba katika *SGR,* yale mabehewa yatakapoanza kufanya kazi, ziwepo nauli za bei ya chini, wananchi wa kawaida wapande; ya kati na ya juu yenye starehe zote iwepo, ili mtu apande kutokana na uwezo wake. Isije wananchi wetu wa hali ya chini wakawa wanaangalia tu treni ya *SGR* inakwenda kwa kasi, wanaiona kwa macho, wao wanahangaika na usafiri wa kutumia saa nyingi kufika maeneo ambayo wanataka kwenda. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa

Waziri, hili waliangalie sana huduma itakapoweza kuanza wakati huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo namwomba Mheshimiwa waziri, nashukuru kwamba barabara nyingi zinajengwa, lakini mpaka sasa nasikitika, bado kila barabara kubwa ukiiona, utaona wakandarasi ni Wachina, Wazungu ama vyovyote. Wakandarasi wetu wa ndani bado hawajapata kazi kubwa. Najua kitakachosemwa kikubwa ni mtaji. Hebu niombe kama Wizara, tuangalie namna ya kuwaunganisha Wakandarasi wetu wa ndani, ili waweze kuchukua kazi kubwa ili nasi fedha zetu za kigeni na uchumi wetu uweze kubaki ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwamba kwenye kilimo…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Francis Mtinga.

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nilikuwa naomba tu nimalizie kwamba nashukuru pale kwenye bwawa langu la msingi, mradi wa Shilingi bilioni 34 wamepewa Wakandarasi wazawa. Kwa hiyo, hata kwenye barabara kubwa kubwa wakipewa wazalendo tutaendelea kujenga uchumi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Deus Sangu, Mheshimiwa Ramadhan Suleiman Ramadhan, ajiandae.

**MHE. DEUS C. SANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa fursa hii, nami kuwa katika orodha ya wachangiaji kwenye bajeti hii muhimu ambayo ndiyo uti wa mgongo wa uchumi wa Taifa letu.

Mheshimwia Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt.

Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoifanya hasa katika sekta hii ya uchukuzi. Ameijali, na amekuwa akiijali kila wakati na kuipa bajeti ya kutosha kuendesha mambo yao wakati kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimpongeze Mheshimiwa Profesa Mbarawa na wasaidizi wake Manaibu, kazi yao ni nzuri na tunawapongeza sana. Vile vile watendaji walio chini yake, Katibu Mkuu na Watendaji wa Taasisi zilizo chini yao, nikianza na *TPA* pale, na bahati nzuri tuna kijana mzuri pale *MD* wa *TPA* Mbossa, na ndugu yangu Mativila wa *TANROADS* na wengine wote wanafanya kazi nzuri, nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mchango wangu leo nitakuwa na mambo mawili muhimu. La kwanza, nitaongelea mambo ya Mkoa wangu wa Rukwa, na pili nitakuja kushauri mambo makubwa kwa mustakabali wa Taifa letu la Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri, juzi alikuja mkoani kwetu kwa ajili ya kuanza mkataba wa kuanza ujenzi wa ndege pale Sumbawanga, halikadhalika Barabara yangu ile ya kutoka Mutendo – Muze ya zaidi ya Shilingi bilioni 45 pamoja na Barabara ya Mathai kwenda Kasesha, tukupongeze, na kweli tunamshukuru Mheshimiwa Rais kwa kutujali kwa kiwango kikubwa Mkoa wa Rukwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hayo, kuna jambo ambalo ameliongea hapa kwa msisitizo mkubwa kwenye hotuba yake, nilikuwa namsikia kwa umakini Profesa, juu ya meli kwenye Ziwa Tanganyika. Sisi uchumi wa mikoa mitatu hiyo kwa pamoja kwa maana ya Rukwa, Katavi na Kigoma tunategemea sana hiyo meli lili ika-boost uchumi wa maeneo hayo matatu. Ni sehemu ambayo nchi tunazopakana nazo kwa maana ya Burundi, *DRC* na maeneo mengine kama Zambia, yana bidhaa nyingi wanazozitegemea kutoa mikoa hiyo mitatu niliyoitaja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muda mrefu sana. Mwaka jana tulimpigia kelele hapa Bungeni juu ya meli, akatuahidi. Hivi leo amesema mwezi ujao Juni, mkandarasi ataanza kazi. Bahati nzuri, *commitment* aliyoifanya hapa iko kwenye *interval* ambayo

tutakuwa humu Bungeni, na tutakuwa hatujachangia Bajeti Kuu ya Serikali. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri, wananchi wana matumini makubwa na ahadi aliyotoa leo. Unaona katika maeneo mengine wana meli tano, sita, saba, lakini Ziwa Tanganyika lime-*collapse*, na ni ziwa ambalo linatu-*link* na nchi ambayo tukiwekeza vizuri, mikoa hii ita-*boost* na tutaongeza pato la Taifa. Kwa hiyo, naomba jambo la meli, tuko *serious* tumekaa nawe katika vikao vingi, naamini baada ya bajeti tena tutakaa utupe mpangokazi ili sisi wawakilishi wa maeneo hayo, tuwe na Imani sasa kwamba mnaenda ku-*address* tatizo la *Lake Tanganyika.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia namwomba Profesa, Barabara ya Ntendo – Muze ile alienda kufanyia *endorsement* kwa maana ya kwenda kumkabidhi mkandarasi, kazi inaendelea vizuri, lakini kwa bonde langu la Ziwa Rukwa ambapo Barabara yote hii kwa urefu ni kilometa 200, Ntendo – Muze mpaka Kilyamatundu ni Kilometa 200. Kule ndani ya bonde la Ziwa Rukwa sasa hivi kuna shughuli kubwa inaendelea ya *exploration*, ambayo tuna wawekezaji wa gesi ya *Helium*, ambao wame-invest zaidi ya kufanya tu utafiti zaidi ya Dola za Kimarekani milioni 30.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hii Barabara ina umuhimu mkubwa kwa sababu uchimbaji unaanza wa majaribio mwezi wa Nane. Kwa projections zilizopo, helium iliyopo bonde la Ziwa Rukwa inaenda kutupatia pato la Taifa zaidi ya Dola za Kimarekani milioni 100, ndani ya miaka mitano tutakuwa tuna-*hit* Dola za Kimarekani milioni 500. Kwa hiyo, hata hii *investment* tutakayoiweka kwenye Barabara hii itarudi ndani ya muda mfumi kwa sababu uchimbaji wa gesi ya *Helium* itakayofanyika pale itakuwa na *impact* kubwa, siyo tu kwa Mkoa wa Rukwa, lakini itakuwa na mchango mkubwa kwenye pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba hii Barabara tuiongezee sasa bajeti. Ina umuhimu, sio kwa Mkoa wa Rukwa lakini uchumi mkubwa wa Taifa letu la Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba sana Mheshimiwa Profesa, hili jambo akalimalize, kipande kile akiongezee hela, kilometa 200 zote ziwe kwenye operation zikamilike kutoka Muze

mpaka Kilyamatundu pale na baadaye kwenda Kasansa kwa ndugu yangu pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuongelea mambo ya jimboni, nije kwenye mambo muhimu ya kitaifa, na hapa profesa naomba tusikilizane kwa umakini. Kuna mambo mawili ambayo yamekuwa yaneleta dosari kubwa sana kwenye Wizara hii na dosari hii imekuwa ya muda mrefu na kila mwaka unavyoendelea dosari hii inazidi kuwa kubwa. Mambo mawili, riba kwa wakandarasi. Riba kwa wakandarasi imekuwa ni jambo ambalo linaumiza taifa hili. Mwaka 2021/2022 wa fedha uliokwisha, tutachulia tu shirika moja kama *TRC,* tulilipa riba ya Dola za Kimarekani 1.34 kwa sababu tu tumeshindwa kulipa *certificate* 24, na Profesa haya mambo yako ndani ya uwezo wako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kuna jamnbo la *VAT exemption,* ucheleweshaji, na haya yanafanyika kwenye Wizara ya Fedha ya ndugu yangu Mwigulu Nchemba, yanaletwa pale *exemption* zinachelewa. Mwaka jana. na nachukulia mfano wa *TRC,* tulilipa bilioni 8.35, kwa ajili ya kwamba *exemption* (riba) imechelewa. Sasa Profesa, leo hii nataka kesho utakapokuwa una *wind-up* bajeti yako utueleze umejipangaje kuondoa tatizo la kulipa *penalty* na hizo riba zisizokuwa na msingi? La sivyo, mimi binafsi nitataka shilingi yako utueleze umejipangaje. Bado tunakusubiri Novemba, baada ya kuja kujadili hapa ripoti ya *CAG*. Hizi taasisi zako zinapewa bilioni nyingi za fedha na riba inapotokea ni *billions of money,* ukizisoma zimekuwa zinakuwa kila mwaka. Sasa hii inatupelekea sisi ambao tunakuja ndani ya Bunge hili na pengine wewe mwenyewe tatizo hili halikuumi; ninaamini sasa kwa sauti yangu leo humu Bungeni utakwenda ku-*take action,* mfute riba, kwa sababu miradi mingine riba haina maana. Tunakuwa tumepewa fedha za mikopo na *World Bank* au taasisi nyingine, fedha iko pale, sasa mnapataje riba ilhali hela zipo, kazi imefanyika mme-*certify*, mnashindwaje kulipa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia *VAT exemption* haiwezi kuwa tatizo kwenye nchi, ni *internal communication* ndani ya Serikali, Wizara yako na Wizara ya Fedha; na bahati nzuri fedha hizi zinatoka Wizara ya Fedha zinakuja kwako kwenda kwenye utekelezaji lakini *VAT* ambayo iko ndani ya uwezo wetu

inatusababishia tulipe riba ya bilioni nane na bilioni nyingi za fedha. Kwa kweli profesa hili hatutakuelewa, tunaomba mje mtuambie mmejipangaje kwenye Serikali ili kukomesha tatizo la riba kwa wakandarasi ambalo linagharimu taifa na *VAT exemption* hizi ambazo ziko chini ya uwezo wetu kama Serikali? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia niongelee suala lingine, *variation* kwenye Miradi. Miradi hii inakuwa *designed,* maana tunafanya upembuzi yakinifu, tunakwenda kwenye *detailed designed,* tunakwenda kutanga za tenda, ghafla unakuta kuna *variation* zinakwenda asilimia 20, 30, 40, na baadaye unasema au kulikuwa na mchezo wa ku-*skip* baadhi ya *item* ili tuje tutumie *room* ya *variation* kufanya mambo yetu? Profesa hili jambo ukapitie kwenye taasisi zako kwenye miradi mikubwa kama vile *TRC, TANROAD, ATCL* na taasisi zote, huko una mabilioni ya fedha. Suala la *variation* limekuwa ni ugonjwa mkubwa ambao hauleti afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nafikiri muda umekwisha nakushukuru sana naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Deus Sangu, ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Ramdhan suleiman na Mheshimiwa Alexander Mnyeti ajiandae.

**MHE. RAMADHAN SULEIMAN RAMADHAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na mimi kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwenye hotuba iliyoko mbele yetu leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kutoa mchango wangu nichukue fursa hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa neema ya uhai na afya na kutujalia kuwa wazima na kuendelea kulitumikia taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nimshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mama yetu Samia Suluhu Hassan, kwa kuendelea kutoa fedha nyingi za kuendelea kumalizia miundombinu ya barabara na miradi mikubwa ya reli ya

*SGR* na mambo mengi kwa ajili ya kuendelea kuijenga nchi hii. Pia, nimshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mama Samia Suluhu Hassan, kwa kuendelea kumwamini Waziri Profesa Mbarawa, kuendelea kuishikilia Wizara hii. Wewe Profesa Mbarawa ni *true definition* ya maana ya kiongozi. Umeendelea kuwa shupavu, umekomaa kumsaidia Rais, tunakuombea dua Mwenyezi Mungu aendelee kukulinda, kukupa nguvu, wewe ni kiongozi mzalendo wa nchi hii. Kwa hiyo, tunakupongeza kwa juhudi kubwa unazozifanya kwa ajili ya kulitetea na kulileta maendeleo taifa hili, hasa kwenye suala la miundombinu ya taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa na mambo mawili kwenye mchango wangu. Jambo la kwanza, tuna masikitiko makubwa sisi wakazi wa Tanzania wanaokaa Pemba na Unguja. Shirika letu la Ndege la Taifa *(ATCL)* ni keki ya taifa. Masikitiko yetu sisi bado hatu-*enjoy* keki hiyo. Kuna tatizo kubwa sana la safari za ndege kutoka Pemba kwenda Unguja na kutoka Unguja kwenda Pemba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi ukitaka tiketi ya ndege inabidi uikate kwa wiki mbili kabla la sivyo huwezi kupata tiketi. Kukitokea dharura hakuna usafiri wa anga, usubiri meli na jambo ambalo nalo linasuasua. Kwa hiyo, wito wangu kwa Wizara hii waangalie uwezekano wa kutuwekea *route* japo mara moja kwa siku ili kutatua tatizo hili. Kama wamefanya tathimini na kuona ndege zao kubwa za *Dash 8 - Q400* ni kubwa kwenda Pemba kwa sababu zinahitaji abiria wengi, niwahakikishie abiria wapo au tusubiri hyo ndege yao ambayo iko matengenezoni huko Malta ya *Dash* 8 Q300 itakapokuja Mheshimiwa Waziri upambane uhakikishe wakazi wa Pemba na Unguja wanpata ku-*enjoy* na wao keki ya taifa ya kuzitumia ndege hizi za Shirika la ndege la taifa, tunateseka. Kwa hiyo, nafikiria hilo ni jambo ambalo Mheshimiwa Waziri kwa sababu ni mzikivu atali-*consider* au atalizingatia kwa mapana makubwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu wa pili ni kwamba, sisi Tanzania Mwenyezi Mungu ametujalia kuwa kwenye nchi kubwa sana kijiografia. Hiyo ni bahati tuliyopewa na Mwenyezi Mungu. Hii nchi tukisubiri tuijenge wote kwa pesa za

ndani aidha tutashindwa au tutachelewa. Hayo mambo mawili yanaweza yakatokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dunia imekwisha *move* huko, hao watu ambao wanatuzidi kila kitu, wanatuzidi *per capital income,* wanatuzidi makusanyo kwenye *revenues,* wanatuzidi kwenye *GDP,* wao aidha wako kwenye *PPP* au wako kwenye *EPC + Finance*. Kwa nini sisi masikini bado tunang'ang'ania kutumia kipato chetu kidogo tunachokipata kutaka kujenga miundombinu yote ya nchi hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, muda umefika tuwaachie *private sectors* waje wajenge baadhi ya sehemu kwenye miundombinu yetu. Viwanja vya ndege, bandari, barabara tunaziweza kuziendeleza tukazijenga kwa kiasi kikubwa kwa kutumia mtindo wa aidha *EPC + Finance* au *PPP,* ule ambao Serikali tutaona unafaa ili kusaidia hizi fedha kidogo ambazo tunazozikusanya au tunazipata zikaenda kusaidia kwenye mambo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo ni mengi; elimu Serikali, afya Serikali, *welfare* ya watu wa nchi hii Serikali, biashara Serikali, sasa tutafanya yote hayo na kipato chetu si cha kutosha? Kwa hiyo, tuwaachie *private sector* waingie waje watusaidie tuwabane kwenye *negotiations* ili wasaidie hiyo miundoimbinu ijengwe, hatutoweza kuvifanya vyote. Kama nchi kubwa kama Russia wamebakisha jeshi tu ndilo ambalo bado linahudumiwa na Serikali itakuwa sisi Tanzania? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanja vya ndege vyote ni *private owned* (vinamilikiwa na *private)* na Serikali wana-*joint venture,* wanakusanya kodi, wanapata kipato na maisha yanaendelea. Hatutaweza, hii Tanzania ni kubwa, na kila siku watu wanasogea kwenye maeneo ambayo mwanzo yalikuwa hayakaliwi na watu. Wakisogea watahitaji barabara, wakisogea watahitaji wajengewe miundombinu hatutaweza halafu tutachelewa. Kwa hiyo, ushauri wangu tuondoke huku tuondokane na huu uzamani. Tuwaruhusu *private sector* waje wajenge sisi tuwabane kwenye mikataba na *negotiations* za kutusaidia sisi wasije wakatubana mbele ya safari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchangiaji aliyepita, Mheshimiwa Sangu amelalamika hapa kuhusiana na matrilioni na mabilioni ya fedha zinazokusanya kwenye *certificates* kwa kuchelewa kulipa riba. Haya yote yanatokana na fedha zetu kuwa ni kidogo, hatuna uwezo wa kuzigawa zote kwa pamoja ukalipa wakandarasi, huku elimu inataka kuhudumiwa, huku hospitali zinataka kujengwa, haiwezekani. Kwa hiyo, tuwaachie watu wajenge sisi tuwakamate tukusanye kodi zetu maisha yaendelee. Huo ndio ushauri wangu na tunaweza kwenda kwenye nyanja zote…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. RAMADHAN SULEIMAN RAMADHAN**: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ahsante sana kwa nafasi hii na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ramadhan Suleiman. Nilimtaja Mheshimiwa Alexander Mnyeti, Mheshimiwa Massache Kasaka na Mheshimiwa Halima Mdee wajiandae.

**MHE. ALEXANDER P. MNYETI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nianze kwa kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama yetu Samia kwa kazi nzuri na kubwa anayoendelea kuifanya kwenye taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nina barabara ambayo imesemwa kwenye ilani ya mwaka 2000, ikasemwa kwenye ilani ya mwaka 2005, ikasemwa kwenye ilani ya mwaka 2010, ikasemwa 2015, imesemwa 2020, na barabara hii haikuwahi kujengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kumshukuru sana Waziri Mbarawa, kwa kuwasikia wana misungwi, kwamba barabara yao ya Ng'wanangwa – Misasi – Kahama sasa

inakwenda kujengwa kwa kiwango cha lami. Nitumie nafasi hii kwa niaba ya wana misungwi kukushukuru sana Mheshimiwa Waziri, kumshukuru sana Mheshimiwa Rais, kwamba barabara hii sasa inakwenda kujengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii ina faida nyingi na ndiyo maana faida hizi zimepelekea sasa Serikali kwenda kuijenga kwa kiwango cha lami, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais. Unajua tumekuwa tukimshukuru Mheshimiwa Rais, wengine wanahisi tunajipendekeza. Kama barabara imeshindwa kujengwa miaka yote hiyo Mama Samia amekuja kujenga kwa nini tusiseme ahsante? Tunashukuru sana, wananchi wa Misungwi wanashukuru na tutaendelea kushukuru sana kwa sababu Rais, huyu ameamua kuijenga barabara hii na tayari; juzi nilikuwa na kikao na Mheshimiwa Waziri, amepiga simu nikiwepo kuagiza tenda itangazwe wiki ijayo, tunashukuru sana. Kwa niaba ya wana Misungwi tunashukuru sana kwa habari hiyo. Kwa kweli tuna Imani kubwa sana na wewe Profesa na kazi hii tuna imani sasa wiki ijayo barabara inakwenda kutangazwa na mkandarasi apatikane mwadilifu na barabara iende ikajengwe ili wana misungwi waweze kupanua uchumi kwenye wilaya yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, nataka nishauri. Tuna miji mikubwa ambayo inayokua kwa kasi, Mheshimiwa Waziri anaifahamu, na tumekwisha omba habari ya taa hizi za barabarani. Tuna miji yetu kama ya Misasi, Mbarika, Misungwi, Igongwa, Usagara tupate taa za barabarani ambazo zinabadilisha hata ile sura za miji yetu ambayo inakuwa kwa *speed.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo pia ni siku ya kutoa shukrani zetu tu. Wana misungwi kila tulipokuwa tukiomba mambo haya yanafanyika. Fidia ya watu ambao barabara ilipokuwa inajengwa kutoka Usagala mpaka Geita wamelia kwa muda mrefu lakini leo watu hao tayari wamekwishapewa fidia yao, tunaishukuru sana Serikali hii. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri, kwa kweli tunakushukuru sana lakini pia tukushukuru sana, juzi tumesaini mkataba wa ujenzi wa kivuko kipya cha kutoka Mbarika mpka Buyagu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusiposhukuru kwa haya sijui tusubiri vitu gani ili tuweze kushukuru? Kila ambacho tumeomba Serikali ya awamu ya sita mmetekeleza. Tumeomba fidia mmetupa, tumeomba barabara mmetupa, tumeomba kivuko mmetupa, tukimshukuru Mheshimiwa Rais, mnasema tunajipendekeza; tufanye nini sasa zaidi ya hayo? Kwa sababu yote tuliyokuwa tunaomba, yote tuliyohitaji yafanyike Mheshimiwa Rais amekubali kuyafanya, zaidi ya hapo tufanye nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunamshukuru sana Mheshimiwa Waziri na Serikali na muendelee kuchapa kazi kwa *style* hiyo kwa sababu sisi kwa niaba ya wananchi wetu tunaona mnayoyafanya na tunaamini kila tunayoyaomba mnaendelea kuyatekeleza kadri ya mwongozo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri anisikilize kwa makini sana kuhusu bandari. Sisi ni wanasiasa lakini pia tunafanya na vibiashara vidogo vidogo. Tunapata adha kubwa sana tunapoagiza mizigo yetu kupitia kwenye Bandari yako ya Dar es salaam. Mimi ninaishi Mwanza, tunapoagiza mizigo kutoka China, Japan na maeneo mengine, mzigo unaweza ukakaa bandarini hata mwezi mzima haujapata mzigo wako. Hiii ni aibu, kama mimi Mtanzania nachukua muda wote huo hao wa nchi jirani wao wana maisha gani? Mheshimiwa Waziri, naomba utumie u-profesa wako kwenye hii bandari ili tuone matunda ya *degree* nne yako wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunamuomba Mheshimiwa Waziri, dunia imeshabadilika, dunia sasa hivi iko kwenye ushirikiano kati ya Serikali na watu binafsi, kati ya Serikali na Serikali na ndiko dunia ilikofikia. Nenda Marekani, Japan kote wanafanya ushirikiano; lakini sisi tuking'ang'ana Serikali kwa sisi wenyewe hatuwezi kufanya, kwa sababu hata tunavyovifanya sisi wenyewe vimetushinda. Kwa hiyo, nikuombe sana Mheshimiwa Pofesa Mbarawa, tuna Imani kubwa sana na wewe nenda ukalitafakari jambo hili vizuri uone nchi inakwenda kunufaika vipi ili tuweze kupata tija katika taifa letu. Kwa sababu hiyo, Mheshimiwa Waziri uwezo wako tunaufahmu hakika tunajua kwamba jambo hili litakwenda vizuri na tunaomba utulize sana akili ili nchi iweze kunufaika na bandari yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi hiyo naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Alxander Mnyeti, ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Masache Kasaka, Mheshimiwa Halima Mdee ajiandae.

**MHE. MASACHE N. KASAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia kwenye Wizara hii muhimu sana kwenye uchumi wa nchi yetu lakini kwenye maendeleo ya nchi yetu kwa sababu taasisi zote muhimu ambazo zinakwenda kuboresha uchumi wetu zipo chini ya Wizara hii. Nimpongeze Mheshimiwa Waziri, pamoja na wakuu wa taasisi zake zote wanafanya kazi nzuri sana na kazi ambazo tunaziona na ule usemi wa kwamba kazi iandelee, hapa kweli kazi inaendelea. Tunawapongeza sana ninaimani huu ni utekelezaji mzuri wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi chini ya Jemedari Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, hakika kazi inaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nina mambo kadhaa ya kuweza kuchangia kuhusu Wizara hii na nitapenda nianze na suala la barabara. Tumeona kwenye bajeti hii namna ambavyo barabara nyingi zimeoneshwa kwenda kutengenezwa na barabara nyingine ujenzi wake unaendelea na nyingine tayari zimekwisha zinduliwa. Tunaipongeza Serikali kwenye hili na nina imani zile barabara ambazo bado zimebakia zitakwenda kufanyiwa kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini moja kati ya barabara ambazo bado hazijaweza kujengwa barabara ya mkoa ni barabara ambayo inaunganisha kati ya Mkoa wa Mbeya pamoja na Mkoa wa Tabora na Singida. Barabra hii inapita ndani ya Wilaya ya Chunya ambako ndipo jimbo langu lilipo. Barabara hii ni muhimu sana kiuchumi kwa sababu barabara hii inakwenda inafungua Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini, Mikoa ya Kanda ya Kati na Kanda ya ziwa. Kwa hiyo, muiangalie barabara hii kwa jicho la kipekee. Maana yake ukiifungua barabara hii kwa kiwango cha lami maana yake sasa utakwenda kuifungua mikoa ya nyanda za juu kwa maana ina mipaka miwili kule, Mpaka wa

Tunduma na mpaka wa Malawi unakwenda kutuunganisha sasa na Mkoa wa Tabora na Singida ambapo tunakwenda moja kwa moja mpaka mikoa ya kanda ya ziwa. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri barabara hii ina umuhimu mkubwa sana, naomba uweze kuiangalia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naangalia hapa kwenye bajeti yako namna ambavyo miradi inaendelea. Mheshimiwa Waziri na hii barabara na yenyewe naomba uweze kuiweka kwenye mpango wa *EPC + F* ili na yenyewe iweze kujengwa. Tumeona mmeanza upande wa Mkiwa kilometa 56 lakini hizi ni kidogo sana. Kwa sababu barabara hii ina kilometa zaidi ya 350. Ukianza kilometa 56 upande wa Mkiwa mpaka uje ufike Makongolosi huku inaweza ikachukua miaka mingi sana. Niombe sasa, unapoanza upande wa Mkiwa kule ambako kazi inaendelea, sasa tuanze upande wa Makongolosi kwa maana ya Wilaya ya Chunya ili tuweze kwenda huko angalau tupate kilometa 100, tutaweza kwenda vizuri sana na barabara hii itaweza kukamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kuna barabara nyingine kuanzia Makongolosi ambayo inakwenda kutuunganisha na Mkoa wa Songwe na Wilaya ya Songwe. Barabara hii inaanzia Makongolosi inapita kwenye Mji wa Mkwajuni inakwenda kutuunganisha na Mbalizi. Barabara hii ni muhimu sana kwa uchumi wa Mkoa wa Songwe lakini kwenda kutuunganisha na Mkoa wa Songwe pamoja na Mkoa wa Mbeya. niombe Mheshimiwa Waziri, anapokwenda kupanga mipango yake na hii barabara pia aweze kuiweka kwenye mipango pia iweze kujengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumze kidogo barabara za mwendokasi. Barabara hizi zimeanza kujengwa kwenye Mji wa Dar es salaam lakini baadae zitaenea katika maeneo mbalimbali kwenye nchi yetu hii ya Tanzania. Barabara hizi ni nzuri, sasa hivi Mji wa Dar es Salaam unapendeza. Lakini, zinapokuwa zinajengwa hizi barabara kunakuwa na changamoto kwenye ujenzi wake. Tumeona, wakati wa awamu ya kwanza ya barabara inajengwa tumeona kwa maana ya kuanzia Barabara ya Morogoro, lengo kubwa lilikuwa ni kwenda kuzitoa daladala

ambazo tumekwishazoea kuzitumia siku zote. Hata hivyo, lengo hili lilishindwa kutimia kwa sababu wakati wanajenga havikujengwa vituo vya kusimamia dala dala za kawaida. Leo hii dala dala za kawaida zinasimama katikati ya Barabara, hali ambayo inapelekea foleni kubwa sana. Lengo la barabara ya mwendokasi ni kupunguza foleni lakini kwa sababu tulishindwa kuzitoa dala dala za kawaida na zenyewe zinasimama kwenye vituo zilivyozoea kusimama kule. Hii barabara inakuwa tena haitusaidii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilitegemea Mheshimiwa Waziri pamoja na wataalamu wake hasa wa *TANROADS,* kwamba baada ya kuona awamu ya kwanza tumeshindwa kuzitoa dala dala , awamu zinazofuata kwa maana ya kuanzia Barabara ya Kilwa *Road* kwenda Mbagala na hii ya Nyerere *Road* kwenda Gongo la Mboto tuweze kuweka *provision* ya vituo vya dala dala hata kama dala dala hizi tutakuja kuzitoa baadaye, hii *provision* ya vituo hivi vya dala dala itatumika pale mtu atakapokuwa amepata *emergence* gari itasukumwa itakwenda kusogezwa pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunavyosema na wewe gari inapopata tatizo lolote mtu anaweza kutembea kilometa mbili mpaka kikometa tatu ndipo aweze kupata mahali pa kuweza kujibanza. Hii tunaomba sana mlichukue na huko mbele mnapoendelea kujenga, na hata sasa hivi kwa kuwa bado ujenzi unaendelea, muone namna ambavyo mnaweza kulirekebisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie pia Uwanja wa Ndege wa Songwe. Tunaishukuru Serikali imefanya kazi nzuri sana uwanja wetu sasa hivi umekuwa ni mzuri, jengo letu la abiria sasa limefikia zaidi ya asilimia 98 na kwa kweli jengo linapendeza sana, lakini pia uzio kwenye uwanja wetu wa ndege umekamilika tunaipongeza Serikali kwa hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hili, mimi niombe sasa, ule uwanja jengo la abiria pale imeshakamilika, sasa, hizi asilimia zilizobakia ziweze kukamilika na baadae sasa jengo hili lizinduliwe ili sisi wananchi wa Mbeya na wananchi wa Nyanda za Juu Kusini

tuweze kufaidika na huduma bora ambazo zinapatikana ndani ya uwanja huu wa ndege, na hasa ukizingatia sasa hivi ndege zinaanza kutua usiku, kwa hiyo wananchi wengi sana hapa wanatumia ule uwanja. Nina imani jengo lile litakapokamilika huduma nyingine zitazidi kuboreka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye bei yake, ule uwanja sasa hivi hauna *cold room;* niombe wakati ujenzi huu unaendelea iweze kujengwa *cold room* kwa ajili ya *perishable goods.* Tuna amani, kwamba sasa hivi kuna parachichi pale zinazalishwa kwa wingi sana zitahitaji kusafirishwa kwenda nje, tuna mazao ya *horticulture* na mazao ya maua yatasafirishwa kupelekwa nje. Haya yote yanahitaji sana ile *cold room.* Kama ulivyosema kwenye hotuba yako, sasa ndege ya mizigo iko njiani inakuja, sasa, ndege ya mizigo hii kama iko njiani inakuja itashindwa kufanya vizuri kwa ufanisi kwa sababu *cold room* sasa hivi hatuna pale. Niombe sana hivi vyote viwili viweze kwenda kwa pamoja, vitaweza kutusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kidogo na upande wa *ATCL*, wanafanya kazi nzuri, lakini kumekuwa na changamoto kubwa sana ya *cancellation* ya safari. Sisi watu wa Mbeya mara nyingi sana tumekuwa tunasafiri kwa ndege hizi usiku. Tiketi inakuonyesha saa kumi na mbili jioni, mara saa mbili usiku unakuja kuondoka saa saba za usiku; na hii yote inakwenda hata taarifa haupewi, na baadaye unakuta tu hata kuombwa radhi inakuwa ni changamoto. Lakini sisi abiria ambao leo ukipata changamoto kama hiyo ukataka Kwenda kubadilisha tu tiketi yako, bei ya kubadilisha tiketi ni kubwa sana, ambapo ni bora ukate tiketi mpya kuliko kubadilisha tiketi ambayo inaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili wananchi wengi wakaosa mahali pa kusemea. Sasa sisi tuwaombe kupitia Wizara lakini kupitia watu wa *ATCL,* ninaimani *Engineer* Matindi ni msikivu sana, waliangalie kwa jicho la peke yake. Wananchi wanapotaka kubadilisha tiketi basi bei iwe *reasonable* ambayo kila mwananchi anaweza akafanya hivyo, lakini bila hivyo wananchi wengi wanaumia kiasi kwamba inafikia hatua mtu anaona ni bora aiche tiketi iende apate tiketi upya kuliko kubadilisha tiketi.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Masache Kasaka muda wako umeisha.

**MHE. MASACHE N. KASAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante, nilimtaja Mheshimiwa Halima Mdee, Mheshimiwa Athumani Maige, ajiandae.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, na mimi nitatoa mchango wangu. Nitambue *humbleness* ya Waziri na timu yake, hamna shida na mtu, mnasikiliza. Lakini kama kawaida mimi nitashauri na tukishauri naomba msichukulie *personal* badala ya kujibu hoja mnafanya *personal attacks,* tunashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya kwanza miradi ya barabara. Mheshimiwa Waziri nilipitia randama yako ambayo imeanisha miradi mbalimbali ambayo mnataka kuitekeleza.Nimefanya uchambuzi wa miradi 69 ya barabara yenye urefu wa kilometa 11,696.88. Kiwango cha fedha ambacho kimetengwa kwa mwaka huu wa fedha kujenga barabara mlizozianisha kwa mwaka huu wa fedha ni shilingi bilioni 434.66, miradi hii 69, sizungumzii miradi yote kiujumla wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukizungumzia gharama ya ujenzi wa kilometa moja ya lami, kilometa moja ya lami ni kati ya bilioni moja ama bilioni mbili. Kwa shilingi bilioni 434 zilizotajwa inatuambia, kama gharama za ujenzi ni bilioni moja kilometa moja maana yake katika kilometa 11,699 mlizozianisha zitajengwa kilometa 434 tu kwa hii miradi 69. Kama ni bilioni mbili mbili kwa kilometa moja ambayo ndio *standard* ya sasa hivi zitajengwa kilometa 217.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku zote nimekuwa nikisema kwamba Wabunge tunakuwa tunaleweshwa tukiona barabara

zetu zimetajwa, lakini tukienda kuangalia unaweza ukakuta, kuna hii Barabara ya Kibireshi unakuta kilometa 450 imepewa milioni tano. Sasa, bilioni tano ni kilometa mbili na nusu ama kilometa tatu. Sasa fikiria, ninazungumzia randama yenu. Kama nimekosea mtanisahihisha, lakini kibireshi imetengewa bilioni tano, na ni kilometa mbili. Sasa nawashauri wenzangu (*colleagues),* nendeni mkapitie randama halafu utoke ujue ulivyoambiwa umepewa kilometa 50 hela kwa mwaka umepangiwa kiasi gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana Waheshimiwa Wabunge hawaishi kulalamika CAG..

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba unilindie muda wangu.

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, atajibu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa mwache tu, mpe taarifa hiyo, Mheshimiwa Waziri.

**TAARIFA**

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mchango mzuri anaosema Mheshimiwa Halima, naomba kumpa taarifa kwamba miradi yote mikubwa ukiondoa darasa ambalo linajengwa kwa *force account* au zahanati miradi mingine yote inayojengwa kwanza *time frame* yake inazidi mwaka mmoja wa bajeti. Kwa mfano barabara ya kutoka Karatu kwenda mpaka Maswa haitarajiwi ijengwe ndani ya mwaka mmoja barabara ya kutoka Mikumi kwenda Lumecha mpaka Londo kule Songea haitarajiwi ijengwe mwaka mmoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Waziri…

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** …Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya kutoka Handeni, Kibireshi mpaka Singida haijengwi mwaka mmoja...

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa ananipotezea muda wangu. ulipewa dakika mbili Mheshimiwa Mwigulu utanijibu…

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** ...Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachofanyika inatolewa *down payment* na baada ya hapo *certificate* zinaanza kutolewa na kulipiwa kadri kazi inavyotekelezwa…

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa amesha kuelewa huyu. Mheshimiwa Halima.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Waziri wa Fedha anaona ni *value for money* kwa barabara moja kwa mwaka mmoja kujengwa kilometa mbili nina mashaka. *CAG* katika ripoti yake amesema hivi *TARURA* na *TANROADS,* hawa hapa, wana madeni kutokana na kwanza tunakuwa na *project* nyingi hatuna fedha za kulipa hatulipi wakandarasi kwa wakati matokeo yake ni nini? Tunaambiwa kutokana tu na madeni haya ya bilioni 673 tumetoa riba, malipo shilingi bilioni 69. Sasa *common sense* bilioni 69 unajenga kilometa 69 za barabara, kama thamani ni bilioni moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nilikuwa nasema, na uzuri Kamati ya Bunge ya Bajeti, Mwenyekiti wangu yupo hapa, Mheshimiwa Sillo, mwaka jana 2022/2023 wakati tunatoa hotuba yetu ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa 2022/2023 tulisema masula yafuatayo; kwanza tulishauri barabara zijengwe chache zisiibuliwe mpya ili kazi ikifanyika ifanyike kwa ukamilifu wake. Tulipendekeza mapendekezo mengi sana, tukaishauri Serikali, hamsikilizi, matokeo yake ni nini? riba *70 million, can you see?* Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili bandari yetu. Nitaomba nizungumze masula haya machache, la kwanza, hakuna mtu yoyote atakayepinga sekta binafsi isishirikiane na Serikali kwa

uwekezaji, hayupo, kwa sababu bila sekta binafsi mambo hayaendi. Lakini muhimu ni kujiuliza sekta binafsi hii ambayo tunataka kwenda kuichukua tumejifunza tulikotoka?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa na *TICTS for 20 years. TICTS* ilikuwa ni mwiba sugu Waheshimiwa Wabunge wa mwaka 2008 wako hapa. Baada ya Serikali kuingia chaka 2008 tukaweka *resolution,* kwamba ikavunje mkataba, ilishindikana, *TICTS* imekuwa donda ndugu mpaka mkataba ulivyoisha. Ndiyo maana leo Mheshimiwa Waziri unatueleza faida ya *TICTS* kuanzia 2012 mpaka 2021; hujatuambia, tangu mwaka 2001, mpaka 2010, Taifa limepata nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nashauri, ushauri, mtasikiliza mtaacha, tusikurupiuke, tufanye tathmini ya kina tulikosea wapi tunaendaje, tusije tukajikuta ndugu zangu makosa ya *TICTS* yanajirudia. Mmepewa dhamana lakini nchi hii ni ya Watanzania ninyi mnapita tu. Kwa hiyo *whichever decision* itakayofanyike ifanyike tathmini ya kina. Siyo tayari tunawawekezaji wetu kapuni tunakuja hapa Waheshimiwa Wabunge tunachangia hapa halafu tunashindwa kwenda kuisimamia Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hili la bandari, bandari ni usalama wa nchi, bandari ni roho ya nchi, bandari ndiyo *future* ya watoto wetu, tusifanye makosa, kukurupuka kwa sababu tuliamini miaka 20 iliyopita.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Halima, muda wako umeisha. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea nilimtaja Mheshimiwa Athuman Maige Mheshimiwa Anna Lupembe, ajiandae.

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kuniruhusu na mimi nichangie hoja hii ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nina mambo mawili ya kuchangia katika Wizara hii. Kwanza ni shukrani; na ninaipongeza sana Serikali kwa kazi nyingi na miradi mikubwa inayofanya na kwa kipindi hiki chote ambacho tumepita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi mikubwa imefanyika ikiwemo viwanja vya ndege, barabara, madaraja, meli zinazojengwa huko, vivuko na baba lao kabisa *SGR*. Baada ya miradi hii kukamilika Serikali itakuwa bingwa wa usafirishaji wa nchi kavu, pia usafiri wa baharini na katika maziwa kote nchini; lakini bila kusahau maombi ya wenzetu wana Ziwa Tanganyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nasema hongera sana kwa Mama Samia Suluhu Hassan na Wizara hii na hasa Profesa Mbarawa na wenzake wamefanya kazi kubwa sana. Sisi kule kwetu Unyamwezini tuna msemo unasema "hapana kujidharau" au kinyamwezi "*yaya kuibyeda.*" Hili ni jambo kubwa sana sana, hela za ndani na za nje lakini tumejenga barabara zetu madaraja na yale niliyoyasema yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu wa pili ni kuhusu suala la bandari ya Dar es salaam. Kwanza nikiri kwamba mimi ni mkandarasi daraja la kwanza, kwa hiyo naitumia sana bandari hii kuagizia vitu kutoka nje. Bandari ilivyo sasa ilifika wakati mimi nilipata hasara kandarasi tatu; mradi mkubwa wa *STR* pale Arusha na mradi wa *ZBC* kule Zanzibar na mradi wa Bunge hili. Wakati tukiagiza mitambo kupitia bandari palikuwa na matatizo makubwa sana, meli zilikuwa zinakaa nje muda mrefu mpaka leo zinakaa nje muda mrefu lakini vilevile kulikuwa na ukiritimba ambao ulifanya mimi nicheleweshe mizigo kuleta kwenye miradi kwa hiyo nikapigwa adhabu kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shughuli za bandari si huduma, ni biashara, na wafanyabiashara wanafanya biashara ili wapate faida, hakuna mfanya biashara anayependa kupata hasara; na bandari ina kipimo au *KPI,* na *KPI* kubwa ya bandari ni kutoa mizigo. Kama bandari haitoi mizigo inakuwa hasara kubwa sana. Lakini nimejifunza kwenye bandari nyingine, kwa sababu wakati fulani tuliacha kupitisha mizigo, nikiwemo mimi mwenyewe, kupitisha mizigo Bandari ya Dar es salaam tukapitisha Mombasa.

Muda wa kupeleka mizigo kule na kupeleka magari kuleta mizigo tena Dar es salaam au Arusha ilikuwa muda mfupi kuliko meli iliyokaa muda mrefu pale bandarini, kwa siku 21. Asubuhi unaambiwa meli yako imefika lakini bahati mbaya unaambiwa rudini meli iko nje siku 21na mzigo unatakiwa uje kwenye *site*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia hiyo ni bahati kama mzigo umefika moja kwa moja, lakini bahati mbaya zaidi ukifanyiwa *Tran sequent,* yaani mzigo unaokuja Dar es salaam meli inaona kwamba hautoshi mzigo kuja Dar es salaam inaancha mzigo Durban halafu meli nyingine ifuate kule inayokuja huku ikae wiki tatu inangojea mzigo kuja hapa, matokeo yake mzigo unachelewa sana, sababu ni nini uwezo wa bandari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu tusiangalie hapa usoni tuangalie huko mbele tunakokwenda. Ndani ya miaka mitano sita Bandari ya Dar es salaam haitafaa tena kufanyia kazi kubwa kwa sababu meli kubwa zinazoitwa kizazi cha nne na tano au *fourth and fifth generation,* hazitaweza kuweka nanga Bandari ya Dar es salaam mbili tatu au nne kwa pamoja kwa sababu bandari ni ndogo sana. Inatakiwa bandari hii ipanuliwe na iwe kubwa, lakini mpango mzurini kujenga Bandari kubwa ya Bagamoyo. Tunataka tufanye hivyo sisi, hatuna uwezo, hatuna hela za kujenga Bandari ya Dar es salaam, kuipanua kuweka vifaa vya kisas.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bandari nyingine kila dakika kumi contena tatu nne tano zinatoka sisi hapa kontena ngapi kwa siku? kontena ngapi kwa wiki? Meli zimepiga foleni kule nje tunataka aje mwekezaji ambaye atakuwa na nia ya kuendesha bandari kama ilivyo kule duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulishasema Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania haifanyi biashara, bandari siyo huduma ni biashara, kujitoa Serikali na kuweka mkandarasi, kuweka mwekezaji ambaye atakuwa na malengo mawili kwanza a-*operate* aendeshe bandari lakini licha ya kuendehs bandari ile awe na lengo la uwekezaji kuipanua bandari lakini bandari imefika kikomo haiwezi kupanuka ni ghali sana. Njia rahisi mwekezaji huyo anayekuja awe na wazo la kujenga Bandari

kubwa ya Bagamoyo ili tuweze kufanya biashara ya usafiri wa meli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi napata tabu sana watu ambao hawaoni umuhimu wa kuipanua bandari, kuikuza bandari, ni sawa na kuwa na ng'ombe mzuri mmoja au wawili umewakamata unasema wa kwangu. Watu wanakwambia ngoja tuwalishe hao ng'ombe wewe unasema a' a' ng'ombe ng'ombe wangu. Ndivyo ilivyo Bandari ya Dar es salaam tutaendelea kuikamata sisi bandari ile haitatusaidia baada ya miaka kumi, itakuwa *absolute,* haitafanya kazi na fedha hatuna, tuna miradi mikubwa sana ya kufanya huku bara kwenye maeneo mengine kuliko bandarini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nashauri na ninashauri kabisa, aje mkandarasi, lakini hatutaki mkandarasi aliyekuwa mbaya kama *TICTS,* tunataka mkandarasi ambaye atakuja na malengo yanayojulikana na Serikali ituhusushe wadau wote tuone atafanya nini, na tukubaliane mkandarasi atapata hiki na wananchi au Serikali ya Tanzania watapa hiki ili tuweze kuleta ufanisi wa bandari yetu. Sasa hivi bandari hii itatudodea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nina uhakika baada ya makubaliano mazuri ya mwekezaji mzuri, aje na malengo mazuri na Serikali ikubali, bandari itakuja kuwa eneo la biashara kubwa na kuingiza hela kwenye Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo nakushukuru sana kuniruhusu kuchangia, naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Almas Maige, nilimtaja Mheshimiwa Anna Lupembe, Mheshimiwa Neema Mgaya, ajiandae.

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia siku hii ya leo. Kwanza kabisa ninaomba nimshukuru Mungu ambaye ametupa uzima na uhai tuko hapa kwa ajili ya maendeleo ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mama yetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoendelea kuifanya kwa ajili ya Tanzania. Ninaomba nimpongeze Waziri pamoja na Naibu Mawaziri kwa kazi kubwa ambayo wanaendelea kuifanya katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sisi Mkoa wa Katavi ametujengea bandari, alitupa bilioni 47. Bandari imekwisha kwa asilimia 100, tunategemea bandari ile tuweze kupata mizigo. Sasa tunaipataje hii mizigo bila kuboresha Bandari ya Dar es Salaam, lazima sasa hivi Watanzania tukubali wawekezaji waje kwenye Bandari yetu ya Dar es Salaam wawekeze ili uchumi wa Watanzania uweze kuongezeka. Kwa sababu maendeleo tunayapenda, tukienda kwa wenzetu, nchi za wenzetu tunafurahi, tunasifia, sasa tunakuja kwetu kuhakikisha sasa maendeleo yanakuja, Serikali inajitahidi kuleta maendeleo, mabadiliko sisi wenyewe tunaanza kupinga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiki ni kitu ambacho hakikubaliki, Mheshimiwa Waziri songa mbele, weka wawekezaji Bandari ya Dar es Salaam wametujengea bandari ili wawekezaji waje, uchumi wa Watanzania uweze kuongezeka. Nakuja kwenye jimbo langu, fidia; Wabunge wenzangu wameongea hapa, najua Waziri anahangaika, safari hii bado hajaweka bajeti yake kuhakikisha analipa fidia, lakini tunaomba Serikali tujipange vizuri, tuhakikishe bajeti inayokuja tuweke pesa ilituweze kuwalipa wananchi wanaotudai fidia. Wengine sasa hivi wameshakufa, huko tukienda katika majimbo yetu watu wanalalamika. Tunaomba sana Serikali ijipange kuhusu fidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niingie kwa upande wa *TRC*. Naomba niishukuru Serikali kwa ajili ya *standard gauge* na kuhusu reli yetu ya kutoka Tabora - Kaliua mpaka Mpanda. Najua Serikali ina mkakati mzuri ina mpango mzuri kuhakikisha *gauge* zile zinabadilishwa ili treni yetu ya kutoka Tabora kuelekea Mpanda iweze kubadilika. Hata hivyo, nina masikitiko, tuna wafanyakazi ambao ni vibarua ambao wanakaa katika magenge. Wale vibarua wamekaa sasa takribani miaka 15, wengine miaka 20

mpaka leo bado vibarua, lakini wale ndio wanatulindia reli yetu, kwa sababu bila kutunzwa reli ile uharibifu unaweza ukatokea wakati wowote, halafu majanga yanaweza yakatokea wakati wowote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali iwatazame wale vibarua, kulipwa kwao ni shida. Hawalipwi kwa wakati, wanaweza kukaa miezi mitatu, wanakaa porini, wanakaa kwenye mazingira magumu. Naiomba Serikali iweze kuchukua jukumu hili kwenda kuonana nao hususan Mkurugenzi wa *TRC,* aende akaongee na hawa vibarua. Najua wana mipango mzuri, mikakati mizuri kwa ajili yao lakini waende wakaongee nao ili waweze kupata *morale* kwa ajili ya kuhakikisha wanakaa kwenye mazingira mazuri hususan wanaokaa Genge la Ugala, Kamini, Kabuziyoti, Katumba, lazima twende tukawaone tuwape moyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana mabehewa ni machache, wasafiri ni wengi. Tunaomba tuongezewe mabehewa, wananchi wanahangaika kutoka Mpanda behewa linakuwa moja au mabehewa mawili, wasafiri wako wengi. Tunaomba wasafiri wa kutoka Mpanda kuelekea Tabora tunaomba tuongezewe behewa. Tuongezewe behewa kwa sababu wananchi wanahangaika, usafiri umekuwa mzuri na usafiri ukiwa mzuri watu wanafurahia ndio maana wanatamani kupanda treni yao, basi tunaomba mabehewa yaongezeke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilituahidi barabara ya kutoka Kawajese ya lami kupitia Ugala na kujenga Daraja la Ugala. Barabara ile inaenda mpaka Kaliua, Kaliua mpaka Kahama. Naomba Waziri aje kutueleza barabara hii kwa kiwango cha lami na kujenga Daraja la Ugala, vitajengwa lini na lini tutaweka pesa, kwa sababu barabara hii iko kwenye Ilani ya Chama Cha Mapinduzi. Tunaomba sana barabara hii iweze kujengwa kwa sababu itafungua fursa kubwa sana kwa ajili ya kutoka Mpanda mpaka Kaliua, Kaliua mpaka Kahama, Kahama mpaka Mwanza, kwa ajili ya maendeleo na fursa mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tuna Ziwa Tanganyika, wenzangu wamesema, Ziwa Tanganyika hatuna meli. Tunaomba meli, tulikuwa tuna meli ilikuwa inapita, lakini toka ilivyosimamishwa meli ile mpaka leo hii hakuna meli ya aina yoyote inayofanya kazi katika Ziwa Tanganyika. Tunahitaji meli na sisi watu wa Ziwa Tanganyika tunataka tujengewe meli, kwa sababu maendeleo tunaona, wanatuletea maendeleo mengi na sasa hivi wanatujengea barabara ya lami kutoka Mpanda mpaka Kalema. Sasa ina maana mizigo itakuwa mingi, abiria wako wengi na ndio maana tunasema basi kama hivyo, tuwaweke wawekezaji ili waweze kufanya kazi hii ili maendeleo yaweze kukua katika Nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante naomba niunge mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Anna Lupembe nilimtaja Mheshimiwa Neema Mgaya, Mheshimiwa Innocent Kalogeris ajiandae.

**MHE. NEEMA W. MGAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya na uhai wa kuweza kusimama mbele ya Bunge letu hili Tukufu na kwa kuanza mchango wangu. Nianze kwa kumpongeza Rais wetu, Mama yetu kipenzi Dkt. Samia Suluhu Hassan. Hii ni mara ya kwanza katika historia ya nchi yetu kuwa na miradi mikubwa ya barabara yenye jumla ya kilometa 2,035, ambayo itagharimu zaidi ya trilioni 3.7 na ikatekelezwa kwa wakati mmoja. Hivyo basi nichukue fursa hii kumpongeza mama kwa kuona umuhimu wa kuweza kuifungua Tanzania yetu ili tuweze kukua kiuchumi. Kwa sababu panapokuwa na miundombinu mizuri ni moja kwa moja unachochea uchumi wa nchi yako. Rais Mheshimiwa Dkt. Samia anakwenda kufanikiwa katika hili nampongeza na namtia nguvu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Waziri wetu wa Ujenzi, Mheshimiwa Profesa Mbarawa pamoja na Naibu Mawaziri wake na Watendaji wote wa Wizara hii ya Ujenzi kwa kazi nzuri wanayoifanya. Sisi tuko nyuma yao kwa yale yote

watakayoyafanya ambayo wanajua yatakuwa yanaleta tija katika Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendeele kumshukuru Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kilometa 107.4 ya barabara ya kutoka Njombe pale Ramadhani kwenda Makete. Barabara ilishakamilika ilishaanza kufanya kazi, lakini kuna changamoto ndogo ndogo, tunaomba sasa wale wananchi ambao hawakulipwa fidia waweze kumaliza kulipwa fidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo pia tunaendelea kuishukuru Serikali kwa Barabara ya Mawengi – Lusitu, kilometa 50 kule Ludewa, lakini vile vile Lusitu - Itoni kilometa 50 kwenye Jimbo lile la Njombe Mjini kilometa 50, kazi inaendelea pale mkandarasi yuko *site,* lakini bado tunasisitiza changamoto ya kulipwa wananchi wetu fidia. Wananchi wanafurahia barabara, lakini bado wanakuwa na machungu ya kutokulipwa fidia. Tunaomba hili Wizara ilimalize ili tusiwe na dosari katika utekelezaji wa kazi hii nzuri inayofanywa na Rais wetu mpendwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Barabara ya kutoka Makambako kilometa 295 kwenda Songea. Hii barabara ni mbovu sana imejengwa tangu mwaka 1980. Barabara hii ina mashimo mengi, ni nyembamba inasababisha ajali nyingi, ni hatari hata kwa misafara ya Viongozi wa Kitaifa, ni hatari kwa wananchi, tumeona vifo vingi vinatokea katika barabara hii. Barabara hii ni muhimu sana kwa uchumi wa kusini, barabara hii ikiboreshwa ikitengenezwa kwa kiwango cha lami upya itasaidia hata ule usafirishaji wa makaa ya mawe ambayo yanaendelea kusafirishwa hivi sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa katika bajeti ijayo angalau waangalie kile kipande cha Makambo kuishia pale Njombe Mjini kwenye makutano ya Mkoa wa Njombe na Songea panaitwa Lukumburu, waangalie sana kipande hicho ni muhimu sana na waweze kukitengeneza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa niombe ombi rasmi la barabara hii ambayo tumekuwa tukiizungumza tangu mwaka 2010. Barabara ya Ramadhani – Ndandu - Iyayi kutokea Mbeya, hii barabara haina pesa kabisa na tunaomba iingie kwenye mpango mahususi ya kutafutiwa pesa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii ina sifa inaunganisha mkoa na mkoa, kwa maana Mkoa wa Njombe na Mkoa wa Mbeya, lakini imekuwa inajengwa kilometa tano tano inakuwa haileti tija, haina maana. Hebu ifike wakati sasa tuweke umakini katika barabara hii, ipewe pesa ya kutosha na ijengwe kwa mwenendo mzuri ili iweze kukamilika mapema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Barabara ya Kibena - *Stop* Lupembe, tunamshukuru Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kutoa kibali cha kujengewa kilometa 51 na hivi sasa kilometa 25 kutoka Kibena - Nyombo imeshaanza kuandaliwa, iko mwishoni katika kuandaa tenda. Tunaomba lakini wafanye haraka haraka ili kusudi barabara hii iweze kukamilika. Barabara hii ni muhimu inaunganisha Mkoa wa Njombe na Mkoa wa Morogoro, itafunguka kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Barabara ya Makete - Kitulo – Mbeya, kilometa 96, tulishapata mkandarasi lakini kinachosubiriwa ni *advance payment* ili mkandarasi huyu aweze kuanza kazi, kwa sababu ule mkataba ulishasainiwa tangu Desemba mwaka 2022. Tunaomba waanze haraka kule Makete mvua ni nyingi sana. Tuanze mapema kabla mvua za Novemba hazijaanza kunyesha, sasa hivi mvua zimetulia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Barabara ya Matamba – Kitulo, kilometa 51, barabara ya kimkakati ya kwenda kwenye Hifadhi ya Kitulo, barabara hii ni muhimu katika kufungua utalii wa Nyanda za Juu Kusini. Kuna Barabara ya Mlangali – Lupila – Ikonda, barabara hii tayari wameshajenga madaraja mazuri na barabara hii ni barabara ya kiusalama kutoka Mkoa wa Ruvuma, Njombe kwenda Mbeya. Tunaomba waiwekee umuhimu barabara hii ili iweze kujengwa katika kiwango cha lami na kuweza kuwasaidia sio lazima mtu anatoka Ruvuma anaenda Mbeya, aanze kuzunguka huku Njombe aende Makambako apite

Igawa, ndio aende tena Mbeya, hapana barabara hii ni nzuri kwa *shortcut* ya kutoka Ruvuma kwenda…

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. NEEMA W. MGAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie katika suala la airport; Njombe tunahitaji *airport* ni muhimu sana, sisi ni wazalishaji wakubwa wa zao la parachichi. Kuna ndege ya mizigo inakuja na katika wazalishaji wakubwa wa *horticulture* ikiwepo parachichi, mbogamboga pamoja na maua ni Mkoa wa Njombe. Kuna umuhimu sana wa Kiwanja cha Ndege cha Njombe kukamilika ili kusudi tuweze kusafirisha bidhaa hizi na kumfikia mlaji zikiwa na ubora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Neema Mgaya, nilimtaja Mheshimiwa Innocent Kalogeris, Mheshimiwa Aloyce Kwezi, Mheshimiwa Edward Olelekaita na Mheshimiwa Bonnah Kamoli wajiandae.

**MHE. INNOCENT E. KALOGERIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja ambayo iko mbele yetu ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Wizara muhimu katika uchumi wa Taifa letu. Nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama yetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa ambayo anaifanya katika kufungua uchumi wa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie pia nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Mbarawa na wasaidizi wake, Naibu wa Ujenzi na Naibu wa Uchukuzi, lakini vile vile na watendaji wote ambao wapo chini ya taasisi katika Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii nianze mchango wangu kwa *TANROADS*. Nimpongeze Mtendaji Mkuu wa *TANROADS* lakini vile vile nimpongeze Meneja wa Mkoa wa Morogoro wa *TANROADS* kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya katika ujenzi wa barabara na madaraja yanayoendelea hapa nchini. Nitumie nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuweza kujenga Barabara ya Bigwa – Kisaki kilometa 78 na madaraja mawili kwa kiwango cha lami, lakini vile vile kwa kujenga Barabara ya Ubena Zomozi – Ngerengere kilometa 11 kwa kiwango cha lami, lakini pia kufanya upembuzi yakinifu kwa ili kujenga kwa kiwango cha lami barabara ya kutoka Ngerengere – Mvua hadi Matemele kwenye Bwawa la Mwalimu Nyerere. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna kila sababu ya kumpongeza Mama yetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa maamuzi ya kuweza kujenga barabara hii. Kiuhalisia wananchi wa Morogoro, Wilaya ya Morogoro ambayo ina majimbo matatu, Jimbo la Morogoro Mjini, Jimbo la Morogoro Kusini Mashariki na Jimbo la Morogoro Kusini. Hii ni historia toka tumepata uhuru tulikuwa tunasikia lami kwa wenzetu, lakini kwa mara ya kwanza sasa tunajenga lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri ametuambia mpaka kufikia mwezi Juni, mkandarasi atatia saini ya ujenzi. Ombi langu tunaomba kazi hii ya kutia saini mkandarasi na Serikali ifanyike kwenye Wilaya ya Morogoro kwenye eneo lolote katika majimbo hayo matatu ili wananchi wajue kwamba kweli Serikali iko kazini na kazi inaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii vile vile kuishauri Serikali kwenye *TANROADS* pamoja na kazi nzuri ya ujenzi wa barabara na madaraja lakini tunahitaji vile vile kutunza barabara. Nimwombe Mheshimiwa Waziri tuangalie jinsi gani tunaendelea kutenga fedha kwa ajili ya ukarabati wa matengenezo ya mara kwa mara kwenye madaraja yetu na barabara zetu ili hizi barabara ambazo tunazitengeneza kwa gharama kubwa ziendelee kudumu kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile kwa *TANROADS* watumishi bado ni wachache, vitendea kazi bado ni vichache, lakini vile vile hata vifaa vya kupima ubora wa kazi ni vichache. Nimwombe Mheshimiwa Waziri tuendelee kutenga fedha nyingi kwa *TANROADS* ili watumishi wapatikane, vitendea kazi viwepo, lakini vifaa vya kupima ubora wa kazi wa fedha nyingi ambayo tunatumbukiza katika ujenzi wa barabara iwe imekamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru Mheshimiwa Waziri mimi ni mkandarasi, naomba ku-*declare interest*. Tunatumia fedha nyingi sana kutajirisha wakandarasi wa kigeni, lakini kwa mara ya kwanza naamini ushauri wa Kamati ya Miundombinu ambayo na mimi ni Mjumbe inaoneka Mheshimiwa Waziri ameusikiliza. Nimeona katika ukurasa wa Kitabu cha Bajeti, ukurasa wa 44 kuna miradi minne ambayo imetengewa wakandarasi wazawa, lakini kuna miradi mitano ambayo imetengewa wakandarasi wazawa wa kike, hongera sana Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa inaonesha tunataka kujenga uchumi uendelee kubaki nchini kwetu, lakini kuwatengeneza wakandarasi wetu sasa na wao waweze kutoka hata nje ya nchi kama Wachina wanavyotoka wakafanye kazi kule wakalete fedha nchini na kujenga uchumi wa kwetu. Ombi langu, wakandarasi tuna tatizo moja Mheshimiwa Waziri, tuna tatizo wa kuwa na utaalam wa *contract management,* lakini tuna tatizo la utalaam wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Mheshimiwa Waziri katika miradi hii minne ya wakandarasi wazawa, wanaume lakini hii miradi mitano ya wakandarasi wazawa wa kike, atengeneze utaratibu wa kuhakikisha kwamba kila mradi utakuwa na Mkandarasi Mshauri wa kuweza kuwasaidia wakandarasi hawa wazawa, lakini vile vile kuhakikisha kwamba fedha inapatikana wasiwe wanasuasua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua tulijaribu kwenye Daraja la Sibiti, lakini tumejaribu kwenye Barabara ya Ludewa – Kilosa, tumewapa wakandarasi lakini wakandarasi hawa wamepata wakati mgumu katika kufanya kazi hiyo kwa sababu ya ukosefu

wa utaalam katika uendeshaji wa miradi, lakini fedha za kufanya kazi. Kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Waziri aangalie hili alisimamie vizuri kama alivyosimamia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, nizungumzie kwenye *TPA*. Wabunge wote wanaridhia, nami naridhia, hatuna sababu ya uoga katika hili la kutafuta wawekezaji katika bandari yetu. Bandari ni lango ambalo linaenda kuleta fedha nyingi katika nchi hii. Tumekwenda Dubai, wengine wamekwenda India tumeshuhudia tumeona wenzetu wanavyofanya, sasa tuna sababu gani ya kuogopa? Hatuna sababu ya kuogopa. Nimwombe Mheshimiwa Waziri atuletee sheria Bungeni, tutunge sheria ili kusudi tuingize Sekta Binafsi kwenye bandari, waweze kuleta fedha na uchumi wa nchi yetu uweze kukua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nichangie *TRC,* kazi kubwa imefanyika na Mama yetu Samia Suluhu Hassan. Vipande vyote vya Reli vya *SGR* vina wakandarasi na wako kazini. Ombi langu kwa Serikali, tukikamilisha reli hii tunatarajia kusafirisha tani 17,000 kwa mwaka. Ombi langu ni moja, tukitegemea kwamba Serikali ijenge miundombinu, inunue mabehewa, inunue vichwa vya treni, ni kwamba hatuwezi kufikia lengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati huu tunajenga, nimwombe Mheshimiwa Waziri atuletee sheria Bungeni tena, tutengeneze utaratibu, wawekezaji binafsi nao waweze kununua vichwa vyao vya treni, wawekezaji binafsi waweze kununua mabehewa ili tutakapokuwa tumekamilisha ujenzi wa reli, kazi ianze moja kwa moja ili fedha irudi kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kwenye suala la *ATCL* tuna kila sababu ya kwanza, kuishauri Serikali yangu hili shirika tunalipa wakati mgumu sana, *Engineer* Matindi naamini kwamba anaweza akazeeka wakati muda bado siyo wa kuzeeka kwake kwa kazi kubwa ambayo tunampa. Haiwezekani Mheshimiwa Waziri shirika linakodishwa shilingi milioni 700 kwa mwezi linalipa Serikalini, eti kwa ajili imekodisha ndege za Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ndege hizo zikienda nje zinakamatwa kwa sababu ya madeni ya Serikali. Mimi ninaiomba

Wizara hebu liangalie hili tufute deni la *ATCL* ambayo ni shilingi bilioni 113. Tukifuta deni hilo ndege hizi wakabidhiwe *ATCL* hata ikiwezekana kwa kukopeshwa badala ya kulipa hiyo shilingi milioni 700 kwa mwezi ambayo haijulikani wanalipa nini, walau wakope baada ya muda wakimaliza madeni ndege hizi ziwe za shirika na kazi naamini itaendelea, tukifanya hivyo tutakuwa tumelisaidia shirika hilo na ninaamini kabisa tutakuwa tumefanya kazi kubwa sana katika nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwangu mimi ni faraja ni furaha, sina sababu ya kuendelea kuchangia mengi, naamini kabisa Wanamorogoro tunakwenda kuona lami sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba niunge mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Innocent Kalogeris. Nilimtaja Mheshimiwa Aloyce Kwezi, Mheshimiwa Edward Olelekaita, Mheshimiwa Bonnah Kamoli na Mheshimiwa Ramadhani Ighondo wajiandae.

**MHE. ALOYCE A. KWEZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba nichukue nafasi hii nikushukuru sana wewe kunipa nafasi nzuri ya kuchangia lakini nimpongeze sana Mheshimiwa Rais Dokta Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri na kuhakikisha nchi yetu iko salama, miradi inakwenda na hakuna mradi uliosimama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba nimpongeze Waziri pamoja na Naibu Mawaziri wake wote, pia niwapongeze watendaji wote, nisimsahau Mtendaji Mkuu wa *TANROADS* pamoja na Meneja wa Mkoa wa Tabora. Meneja wa Mkoa wa Tabora anafanya vizuri sana na sisi Wanatabora, Wanakaliua tunamshukuru sana kwa kazi nzuri anayoifanya katika Mkoa wetu wa Tabora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo mazuri nimeanza kupongeza kwa sababu kazi zinazofanyika Kaliua ni kazi ambazo hazijawahi kufanyika kwa miaka yote iliyopita. Kaliua kwanza tumenufaika kuna barabara inatokea Kaliua kwa maana ya

Chagu - Kazilambwa ya kilometa 36. Mheshimiwa Rais wetu ameleta shilingi bilioni 38 na barabara sasa hivi iko zaidi ya asilimia 90. Kwenye miradi ya reli *SGR,* ule Mkataba wa Tabora – Kigoma unapita Kaliua lakini ukarabati wa reli ya Kaliua – Mpanda unakwenda vizuri. Hii ndiyo sababu ya mimi kuanza kupongeza Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi chini Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namuomba Waziri mambo machache, jambo la kwanza kabisa pamoja na kumshukuru ninavyomwambia kwa sasa tunaendelea na kufunga taa pale Kaliua Mjini, lami sehemu kubwa imekamilika na wanaendelea na ufungaji wa taa kutoka relini Kaliua mpaka Kasungu na kwenda kwenye *T.* Zoezi hilo linatekelezwa na Mkandarasi mzalendo SAMOTA na nimuombe Mheshimiwa Waziri Mkandarasi yule kwenye Mkoa wa Tabora amefanya kazi kubwa sana, ukiangalia barabara ya kutoka Urambo kwenda Kaliua ni Mkandarasi huyo aliyeweza kuijenga. Wakandarasi hawa hebu muwa-*empower* mhakikishe kama wana madeni wanalipwa kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu kubwa kwa Mheshimiwa Waziri, pale Kaliua ile barabara yetu ya mchepuko kutoka Ushokola relini pale kwenda mpaka njiapanda ya kuunga Urambo zimebaki kilometa 2.3, nimeona kwenye bajeti inayoanza mwezi wa Julai mmeweka kilometa moja, Mheshimiwa Waziri nikikuangalia hivi najua ni *material* ya Kinyamwezi kabisa, kwa heshima zote nakuomba mwezi Julai tunapoanza ile kilometa moja hebu ongezeni ziwe kilometa mbili zikamilike ili mimi nitakaposimama mwakani tunasogea sogea kwenye mambo ya uchaguzi tuendelee kuimba CCM hoye, iyena iyena au siyo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ombi langu la kwanza linagusa Ushokola na ni hilo kubwa sana, Mtendaji wako ana taarifa zote na Meneja wako wa Mkoa wa Tabora anafahamu hili. Kwa hiyo, ombi langu la kwanza ni hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi la pili kubwa Mheshimiwa Waziri linagusa barabara ya kiuchumi, barabara ya kutoka Mpanda – Kaliua – Kahama. Mheshimiwa Waziri barabara hii

imewekwa kwenye Ilani zaidi ya mara tatu na mimi sitegemei nimebakiza miaka miwili kwenye kipindi hiki niendelee kuona maneno. Mimi ni muumini wa utekelezaji naamini na wewe ndivyo ulivyo. Nikuombe kwenye bajeti ya Katavi mmeweka ujenzi wa daraja, ninaomba daraja hilo lianze mara moja isiishie kwenye kuandika bila utekelezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mbunge wa Katavi nimeona anaongelea jambo hilo na mimi naungana naye, tuko pamoja tunategemea mazao ya tumbaku kutoka Mpanda kuja Kaliua kwenda Tabora na maeneo mengine yawe safari nzuri kabisa bila wasiwasi wowote. Pia mazao ya asali tunayategemea sana lakini mazao mengine ni mahindi pamoja na mchele. Niwaombe sana mhakikishe barabara hii inakamilika kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri juzi tulikaa na wewe hapa wiki iliyopita, ile barabara ya kwenda Kigoma zile kilometa 36 nilizozieleza, ule mchepuo wa kwenda Ugansa – Usinge ndiyo kilio kikubwa cha Wanakaliua. Mchepuo ule barabara iko chini ya ufadhili wa *OPEC* kama sikosei. Ulimpigia simu Mtendaji Mkuu na Mtendaji Mkuu akasema hana shida, leo mpo watatu hapa pamoja na Meneja wangu hebu malizeni jambo hili. Fedha ipo kwa nini wasianze? Wazee wa Usinge wanapiga simu kila siku hata hapa nikwambie tu nimepokea simu nyingi sana na nitawataja hawa wazee ili furaha yao ikamilike kwamba Mbunge wao Kwezi nimetamka kwako kwamba ile barabara ya mchepuo ya kilometa Saba inakamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wazee hawa walionituma ni George Kamsini, Mzee wa pili aliyenituma ni Juma Kitakala, Mzee wa tatu ni Malabe, Mzee wa nne ni Mademo, kijana Kakobe, Mama yangu Mama Mau na Rehema Hamisi wamepiga simu leo, wanataka lami Usinge. Mheshimiwa Waziri kilometa saba kitu gani na fedha ipo? Mtendaji Mkuu tena nimpongeze Mtendaji Mkuu ni msikivu sana, hata usiku ukituma *message* anajibu. Mtendaji Mkuu nakwambia Meneja wa Mkoa wa Tabora yuko hapa, mkitoka hapo nje anzeni na Kaliua tafadhali sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwathibitishie sisi Kaliua tuko na nyie, wilaya iko makini, iko salama chini ya Mkuu wa

Wilaya yetu Rashid Chuachua anasimama vizuri, hakikisheni jambo hili limekwisha, mnampa kero. Mnanipa kero, mnampa kero Mwenyekiti wangu wa Mkoa wa Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa kuongelea ni suala zima la reli. Jamani, Kaliua pale ni njiapanda kama ilivyo njia panda Tabora na kwenye upande wa reli ni vivyo hivyo. Niwaombe sana hizi ajira zinazojitokeza hakikisheni wenyeji wamepata ajira hizi, vijana wa Kaliua wapo wa kutosha, vijana wa Mpanda wapo wa kutosha, vijana wa Kigoma wako wa kutosha kwa sababu hizo reli zinatunufaisha wote. Wasihame na watu kutoka mbali sana kuhakikisha wanapata pale. Hata ule ukarabati fuatilieni ule ukarabati wa Kaliua – Mpanda tunahitaji wenyeji wapate. Zipo kazi ambazo hazihitaji shule, zinahitaji nguvu. Si mnasemaga mizigo mizito wape Wanyamwezi? Sasa mnakwepaje mnahama na watu? Niombe mlifuatilie hilo Mheshimiwa Waziri, tufanye kazi kwa pamoja tuhakikishe tunafaulu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo kubwa kwenye reli ambalo ni la mwisho kwangu nilikuwa naomba kuna vituo kabla ya stesheni na stesheni pale kati kati wanatozwa faini wananchi wanapovuka kutoka vijiji ‘A’ kwenda vijiji ‘B’ naomba ufuatilie jambo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema haya, Mheshimiwa Waziri nakutegemea sana, naunga mkono hoja. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Aloyce Kwezi. Nilimtaja Mheshimiwa Edward Olelekaita, Mheshimiwa Bonnah Kamoli ajiandae.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi, kwanza ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa afya njema na tuko hapa leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili tumpongeze Mheshimiwa Rais Mama Samia kwa kuja na ubunifu wa *EPC + Finance*.

Nilizungumza mwaka jana hapa kuhusu barabara hizi za Kongwa – Kiteto na Simanjiro na kwa kweli nimpongeze Profesa Mbarawa - Waziri wa Ujenzi, *Engineer* Kasekenya – Naibu Waziri Ujenzi, Mheshimiwa Mwakibete- Naibu Waziri Uchukuzi, Makatibu Wakuu na timu nzima kwa kazi kubwa ambayo kwa kweli mmefanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka nilizungumza hapa ilikuwa ni tarehe 17 Mei, 2021 nikawa nazungumza habari ya barabara hizi za Kongwa – Kiteto – Simanjiro mpaka Arusha, lakini nimezungumza habari ya barabara kutoka Kibirashi – Kijungu – Kibaya – Njoro – Chemba mpaka Singida. Leo jioni hii Mheshimiwa Waziri kwa kweli wananchi wa Kiteto wamefarijika sana. Nimesoma bajeti yako hapa na hotuba hapa ukurasa wa 11, kwamba Barabara ya Handeni – Kibirashi – Kijungu – Kibaya – Njoro – Orboloti – Talai – Chemba - Kwamtoro mpaka Singida, kilometa 460 ipo kwenye mpango wa bajeti. Kwa kweli, nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri na wananchi wa Kiteto kwa kweli wamefarijika sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili barabara ya kutoka Kongwa – Kibaya – Simanjiro mpaka Arusha vilevile naona hapa kwenye hizi barabara hizi kilometa 2,000 zinazojengwa kwa mpango huu wa *EPC + Finance*. Kwa kweli tumefarijika sana na hii kwa kweli itafungua sana siyo tu maendeleo kwenye Majimbo haya lakini uchumi kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzuri wa barabara hii ya Tanga mpaka Singida kupitia Kiteto kwa kuwa tumeshafanya maamuzi kama nchi kujenga bomba hili la mafuta kutoka Hoima – Uganda mpaka Chongoleani – Tanga, barabara hii itasaidia sana kufungua uchumi na itakuwa inaendana na bomba la mafuta. Kwa hiyo, kwa kweli *big up* huu ni mradi ambao kwa kweli uta-*complement* vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii ya Kongwa – Kibaya hizi barabara mbili hizi mimi naita ni barabara za vijijini. Kwangu tu Kiteto peke yake inapita zaidi ya vijiji 20, na kwa kweli Kiteto kutoka sasa kilometa nne za lami za pale Mjini ambazo hata taa hazina mpaka karibu kilometa 300 za lami baada ya hizi barabara zote mbili kujengwa, kwa kweli itafungua uchumi mkubwa sana.

Mheshimiwa Waziri huu mpango mpya wa *EPC + Finance* karibu sasa tutaitia majina ya watoto kule Majimboni *EPC + Finance* kwa sababu kila wakati tumekuwa tunasema kwenye mikutano ya hadhara, barabara zetu zitajengwa kwa *EPC + Finance*. Kwa hiyo, labda mtafute Kiswahili nzuri ya *EPC + Finance* kwa sababu ni kitu kizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hizi kwa umuhimu wake, kilimo, mifugo na usafiri kwa wananchi ambao wanapitiwa na barabara hizi kwa kweli itaondoa changamoto ya muda mrefu sana ambayo kwa kweli wananchi wamekuwa nayo. Kwa hiyo, kwa kweli kwa Kiteto simu leo zimekuwa nyingi sana kutoka Kiteto huko baada ya bajeti hii kusomwa na kwamba wananchi wale wamesikia barabara zao. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri nakushukuru sana na Mwenyezi Mungu awabariki sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili tunasubiri sana kama ulivyosema hapa kwamba sasa tunachosubiri ni kutiwa saini kwa ujenzi wa barabara hizi na vizuri uemesema ni kabla ya Juni mwaka huu. Kwa hiyo, kwa kweli tunasubiria sana na hii tarehe kwa kweli mtufahamishe, hata baadhi ya wananchi wanataka kuja kabisa hata kuona mikataba hii ikisainiwa. Hii kwa kweli italeta maana kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachoomba sasa kwa barabara hizi mbili kazi ambazo wananchi watakuwa na sifa nazo ni vema mkaongea na wakandarasi ili wananchi wanaotoka kwenye maeneo haya wakapate hizo kazi kwenye barabara hizi na mhakikishe kabisa kwamba wananchi wanalipwa. Kwa hivyo, kama wakandarasi kuna sifa za wananchi zipo huko basi na wananchi waweze kunufaika na *tender* za barabara hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie habari ya *ATCL* (Shirika la Ndege la Taifa). Mimi nadhani ni *expensive* sana *ticket* ya ndege ya *ATCL* ni ghali kidogo. Kwa hivyo, pengine ni vizuri mkaangalia namna kwa sababu Watanzania wanapenda kutumia ndege yao hii, imekuwa ni ghali kidogo. Jambo ambalo linasikitisha kidogo eti ni ukipiga simu saa mbili ya usiku wamelala! Sasa hiyo kwa kweli kwa nchi ambayo sasa imefunguka na tunataka tuanze kusafiri, inaeleweka kwa Uwanja wa Ndege wa

Dodoma hakuna taa sawa, lakini kwa Arusha na Kilimanjaro na Dar es Salaam na Mwanza kwa kweli nashangaa sana kwa nini hawa ndiyo wanaenda huko, na simu ya *customer care*, sasa wakienda kulala na wao saa mbili kweli itakuwa Hapana! Lazima hilo tubadilishe kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru Mheshimiwa Waziri nimeona pia barabara ya Dongo – Sunya – Kijungu mmetengea bajeti kwenye hotuba yako na kwa kweli kubwa kwangu leo unajua nimeishiwa maneno, leo kwa mara ya kwanza baada ya kuona hizi barabara hizi mbili hizi, barabara hizi mbili ambazo tumezipigia kelele kwa muda mrefu sana kuona leo kwamba ziko kwenye mpango wa *EPC + Finance* na faida zake zinajulikana, *for once* nimekosa cha kusema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa tuwapitishie bajeti wakafanye hii kazi haraka sana. Ninakushukuru ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Edward Olelekaita. Nilimtaja Mheshimiwa Bonnah Kamoli, Mheshimiwa Ramadhani Ighondo na Mheshimiwa Seif Gulamali ajiandae.

**MHE. BONNAH L. KAMOLI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nashukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kutoa mchango wangu katika Wizara ya Miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa ambayo anaifanya ya kuleta maendeleo katika nchi yetu, pia nimpongeze Waziri pamoja na Katibu Mkuu, Naibu Mawaziri wote wawili kwa kazi kubwa wanayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuombe sasa Mheshimiwa Waziri kwamba kuna mchakato ambao unaendelea kwenye Jimbo langu ni wa kulipa fidia ya wakazi wa Kata ya Kipawa, ambao sasa hivi imefikia sehemu nzuri nafikiri kwamba wameshaenda watu wa Wizara ya Miundombinu kufanya uhakiki

na ninajua watakapomalizika hawa basi itaenda Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuomba sana Mheshimiwa Waziri kwamba hili jambo sasa lifikie mwisho na ninawashukuru sana katika miaka yote karibu miaka 30, ambayo mmeweza sasa hivi kufanya tathmini lakini pia na kuhakikishia kwamba hawa watu mnawalipa kwa mwaka huu na tunamshukuru pia Mheshimiwa Rais. Wakazi wa Kata ya Kipawa Jimbo la Segerea wamenituma nije nitoe shukrani zao, kwanza kwa kuwafanyia tathmini mpya lakini kwa kuwaonesha kwamba watalipwa mwaka huu, nimshukuru sana Mkurugenzi wa *Airport. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya shukrani hizo naomba pia nishukuru kwa mara ya kwanza barabara yetu ya Kinyerezi – Bonyokwa – Kimara sasa ipo kwenye bajeti. Barabara hii kwa muda mrefu sana tumeiongelea ambayo ni kilometa sita *point* ngapi hizo. Tumeiongelea kwa muda mrefu sana kwamba tunaomba hii barabara ijengwe, hii barabara ni muhimu sana, kwa sababu hii barabara imepita kwenye Majimbo matatu na hii barabara ikijengwa Mheshimiwa Waziri itatusaidia sana wakazi wa Segerea lakini pia Jimbo la Ubungo lakini pia Jimbo la Kibamba, kwa hiyo tunaomba kama mlivyoiweka kwenye bajeti tunaomba basi wananchi wetu waweze kuiona imeanza kujengwa ili na sisi sasa tujue kwamba tatizo la miundombinu katika haya Majimbo yetu matatu yanakwisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine Mheshimiwa Waziri nililokuwa nataka kuongelea ni kuhusiana na madereva *taxi* wa *airport terminal two*. *Terminal two* pale kumekuwa na malalamiko mengi sana Mheshimiwa Waziri, madereva *taxi* wa *terminal two*. Jambo la kwanza wanacholalamikia ni kuhusiana na kwamba hawaruhusiwi kutoka *terminal two* kwenda *terminal three*. Kwa hiyo, tunaomba muwaruhusu waende *terminal three* kwa sababu baadhi ya hawa madereva *taxi* wa Jimbo la Segerea Mheshimiwa Waziri wengi wao wamechukua mikopo baada ya kuona *terminal three* inajengwa. Kwa hiyo, sasa hivi tunavyoendelea kuwazuia inawapa shida sana, tunaomba muwaruhusu na wenyewe waende *terminal three* waweze kufanya biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine katika *terminal two* pia Mheshimiwa Waziri tozo zimekuwa nyingi kwa hawa madereva *taxi.* Tozo zimekuwa nyingi wanakuwa wanalipa michango midogo midogo mingi, naomba kama itawezekana Mheshimiwa Waziri hawa watu waweze kupunguziwa hizi tozo, tozo ni nyingi sana na wanavyoendelea kuwekewa tozo nyingi, ndiyo wanafanya abiria waweze kuchukua *taxi* kwa bei ya ghali na wengine sasa kuchukua hizi ambazo zinaitwa *Uber.* Kwa hiyo, tunaomba sana muangalie hizo tozo pia kuangalia ni jinsi gani wanaweza wakaungana na wenzao *terminal three*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine Mheshimiwa Waziri nililokuwa nataka kuongelea ni kuhusiana na barabara ya Banana – Kitunda. Mheshimiwa Waziri hii barabara ni barabara ambayo inapitisha magari 5,000 au 8,000 kwa siku. Hii ni barabara kubwa sana ni barabara ya *TANROADS* sasa hivi ina hali mbaya sana kwa sababu ni barabara ya lami, lami imekwisha mpaka jana Mwenyekiti wa eneo hilo anaomba *grader* apitishe juu ya lami kutokana na yale mashimo. Kwa hiyo, tunaomba sana hii barabara iangaliwe kwa sababu ndiyo barabara ambayo inaenda mpaka Jimbo la Ukonga tukizingatia kabisa Jimbo la Ukonga ndilo lenye wananchi wengi wanaokaa kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaomba sana hii barabara iangaliwe kwa sababu ndiyo barabara ambayo inaenda mpaka Jimbo la Ukonga, tukizingatia kabisa Jimbo la Ukonga ndilo lenye wananchi wengi wanaokaa kule. Kwa hiyo, ukifika pale, sehemu ambayo unaitwa Matembele Mheshimiwa Waziri sehemu ambayo unaweza kwenda kwa dakika mbili, inabidi uende kwa dakika 20 kunatokana na yale mashimo lakini pia kutokana na wingi wa magari. Kwa hiyo tunaomba sana mtuangalizie hii barabara kama mnaweza kuifanyia *maintenance* ili iweze kufanya kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine Mheshimiwa Waziri ni barabara ambayo ni ya Tabata - Kinyerezi. Hii barabara pia inapitisha magari mengi na ni barabara ya *TANROADS,* imezidiwa. Nimeona mmeweka 'X' kwenye baadhi ya nyumba, lakini sasa hatujajua wale wananchi wanauliza, kwamba pamoja na kuwekewa 'X' huu mradi utaanza lini? Kwa hiyo, tulikuwa

tunaomba mnapofikia kuwawekea wananchi ‘X’ tuwe tayari tumeshajua wanaondoka lini na wanalipwa lini? Kwa sababu mnapowawekea ‘X’ wanaanza sasa yale maswali, kwamba tumeshawekewa ‘X’, miradi yao mingi haiwezi kuendelea, wanaanza kujiandaa kwa kuondoka, lakini pia hamjui mkishaweka ‘X’ mnakuwa mmeshaondoka. Kwa hiyo, tunaomba sana sana, hii ‘X’ ikiwekwa tuwe tumeshakaa na wananchi tunawaambia mradi unaanza lini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine la mwisho ninalotaka kuliongelea ni kuhusiana na *SGR*. Namshukuru sana na ninawapongeza sana *SGR* kwa kazi kubwa wanayooifanya. *SGR* imepita kwenye jimbo langu, kwenye kata tatu; Kipawa, Vingunguti, Mnyamani, na Buguruni. Hizi sehemu zote Mheshimiwa Waziri zimezibwa. Hatukatai maendeleo, tunakubali kwamba maendeleo yawepo na yakija maendeleo ni lazima tupate usumbufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kazi kubwa ambayo wanaifanya *SGR,* nawapongeza sana na nampongeza Mkurugenzi, lakini tunaomba katika hizi kata tatu tupatiwe sehemu moja ya kupitia. Kwa sababu sasa hivi mtu kama anatoka Mbezi inabidi azunguke aende mpaka Ukonga ndiyo aende *Airport*. Kwa hiyo, tungepatiwa sehemu moja ya kupita kwa sababu hii miradi, wataalam walisema itaisha baada ya miezi sita, lakini tulienda pale tukazunguka, miezi sita mpaka sasa hivi imeisha na mpaka sasa hivi watu bado wanaendelea kupata usumbufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hivyo tu, wanafunzi wameshajitengenezea sehemu nyingine za hatari za kupita. Kwa hiyo, tulikuwa tunaomba Mkurugenzi pamoja na Ma-*engineer* wa *SGR* waangalie katika hizi kata tatu, ni sehemu gani wanaweza wakaitengeneza kwa haraka ili sisi tuweze kupita hiyo sehemu? Kwa sababu sehemu zote zimezibwa. …

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**MHE. BONNAH L. KAMOLI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Ramadhani Ighondo, Mheshimiwa Seif Gulamali na Mheshimiwa Flatei Massay, ajiandae.

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nami fursa jioni ya leo niweze kutoa mchango wangu katika Wizara hii na hasa kuwasemea wananchi wenzangu wa Jimbo la Singida Kaskazini kuhusu miundombinu ya barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri anayoifanya katika kuhakikisha anawahudumia Watanzania ipasavyo hususan katika eneo hili la ujenzi wa miundombinu ya usafiri na barabara na mambo mengine hapa nchini kwetu. Pia nimpongeze kwa ukamilishaji wa Ikulu ya nchi, na sasa tunasema nchi iko Dodoma. Kwa hiyo, naomba pia nitumie fursa hii kulisema hilo, kwa sababu ni jambo ambalo kwa miaka nenda rudi lilikuwa mishipa katika nchi yetu. Kwa hiyo, nimpongeze Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nampongeza Waziri kwa uwasilishaji mzuri wa bajeti, hotuba yake na utendaji wake mzuri pamoja na Manaibu wake wote wawili, Katibu Mkuu na Watendaji kwa ujumla, bila kumsahau Meneja wa *TANROADS* kule mkoani kwetu Singida, ni mtu *very humble,* msikivu na pia ni mfuatiliaji, ni mpokeaji wa simu zetu tunapokuwa na changamoto, maana yake sisi kule barabara zetu nyingi ni za vumbi, kwa hiyo, simu ya Meneja wa Mkoa ni iko ubavuni kila dakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama jioni ya leo, naomba nizungumzie jambo kubwa moja kwa muda wangu wote. Barabara inayotoka Singida Mjini inakwenda Njuki - Ilongero ambapo ndiyo Makao Makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Singida, inakwenda Mtinko hadi Haydom. Barabara hii inaunganisha Mkoa wa Singida na Mkoa wa Manyara na vilevile

ni kiungo pia cha ile barabara inayokwenda mpaka Simiyu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwamba angalau upembuzi yakinifu wa barabara hiyo umekamilika, lakini kwa masikitiko makubwa, nataka niseme tu wazi hapa kwamba mimi nitaondoka hapa nikiwa na machozi na majonzi makubwa nikiwarudishia wananchi wenzangu kilio kule kwamba hatujapata hata kilometa moja ya lami kwenye hii barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nieleze umuhimu wa hii barabara. Kwanza inakwenda kwenye Makao Makuu ya Halmashauri ya Wilaya ambapo kuna watumishi zaidi ya 3,000 walioko pale Makao Makuu ya Wilaya, wanaitumia hii barabara kila siku zaidi ya mara tatu, lakini wanapata shida kwa sababu ya ubovu, ina mashimo. Kama haitoshi, barabara hii inakwenda kwenye Hospitali ya Wilaya iliyoko pale Ilongero, lakini mpaka kesho hii barabara ni mbovu, ni mashimo matupu, watu wanapata shida. Kama haitoshi, barabara hii inawahudumia wananchi wanaokwenda Hospitali ya Haydom, ukanda wote huu wa kati; Mkalama, Jimboni kwangu Singida Kaskazini, Hanang, wote wanakwenda kwenye hii Hospitali ya Haydom, tunapata huduma kule, lakini ni mavumbi, mashimo. Sasa sijui tuongee lugha gani ili mtuelewe leo ndugu zangu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii inakwenda kwenye hospitali moja muhimu sana ya St. Carolus iliyopo pale Mtinko Mji Mdogo, lakini kila tukizungumza hapa hamtuelewi. Kama hiyo, haitoshi hii barabara iko kwenye ukanda wa uzalishaji mazao makubwa ya biashara na ya chakula, yanapita kwenye hii barabara. Vitunguu tunavyovisema hapa, vinapita kwenye hii barabara, alizeti inapita kwenye hii Barabara, mpaka na hawa kuku tunaowala hapa kila siku wanapita kwenye hii barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa cha kusikitisha zaidi, hii barabara ni ahadi ya tangu wakati wa Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Amekuja Mzee Mwinyi pale Ilongero akaahidi akasema tutaijenga kwa lami, amekuja Hayati Mkapa akaahidi hii Barabara, tena wanakujaga kuombea kura pale.

Wanaombea kura hii Barabara. Amekuja Mzee Kikwete ameombea kura hii barabara, amekuja Hayati Dkt. John Magufuli, alisema kabisa tutakuja, tutaweka lami kwenye hii Barabara. Hata Rais wetu wa hivi sasa ambaye wakati huo alikuwa Makamu wa Rais, alikuja akaahidi akasema tutawawekea lami barabara hii. Kigugumizi kiko wapi? Shida ni nini kwenye hii barabara mnatutesa namna hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba hii barabara mwaka huu ionekane kwenye bajeti, tuweke lami hii barabara. Kama imeshindikana, tupeni basi kilometa hizi kumi ziende mpaka Makao Makuu ya Halmashauri, watumishi wanakimbia, wanakataa kukaa ofisini. Kila baada ya miezi miwili, anaripoti, wanaondoka, au nitoe machozi hapa ndiyo ninyi muone naongea ya kueleweka hapa? Nitoe machozi? Au nipande juu ya hii meza? Tatizo ni nini? Kwa nini hamtuelewi wananchi wa Singida Kaskazini tunapowaeleza kuhusu hii barabara? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii barabara isipoonekana, nisipoona hata kilomita kumi angalau ifike kwenye Makao Makuu ya Halmashauri, Mheshimiwa Waziri nachukua mshahara wako, tutakutana na wananchi kule Singida Kaskazini. Utaenda kuwaeleza mwenyewe, kwa nini hutupi fedha kwenye hii barabara. Kama mna mpango mwingine labda mtuambie leo. Sisi tunalipa kodi, tena wananchi wa Singida Kaskazini ni waaminifu kweli kwenye Serikali hii, ni wapigakura waaminifu kweli kwa Serikali hii ya CCM, tunaomba mtupe hii barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba chonde chonde tupate lami kwenye hii barabara. Nami leo hii naomba iwe ni mara ya mwisho kuzungumzia barabara ya Singida – Ilongero - Haydom. Baada ya hapa naomba sana nisizungumze tena kuhusu hii barabara. Nimechoka, nimeuliza maswali ya msingi, maswali ya nyongeza, majibu yanakuja ya pinduapindua kila siku. *This will be my last time to talk about this road.* Naomba niongee Kinyaturu ndiyo mtanielewa, maana yake Kiswahili hamnielewi. Naomba niongee Kinyaturu hapa pengine Waziri utanielewa. Niongee Kinyaturu hapa? *This will be my last time to talk about this road. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Singida Kaskazini wamechoka kudanganywa kuanzia, Hayati Nyerere! Sasa ninyi mnataka kuwafanya viongozi waliopita kuwa ni waongo! Marehemu ni waongo kweli! Ina maana viongozi wa nchi hii wakubwa ni waongo! Tekelezeni ahadi za viongozi wa kitaifa wanazoahidi wanapokuja kwenye maeneo yetu. Viongozi wanapokuja wanapoongea na wananchi, sisi ndio tunaachiwa mizigo tunaowawakilisha. Tunaambiwa ninyi mbona hamwaambii viongozi? Sisi ndio…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba hii barabara iwekwe lami. Mheshimiwa Waziri amenisikia, tena Waziri wa Fedha na wewe uko hapa, nakuomba sana *brother,* tusaidie hela, hela!

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Lete hela ile Barabara tuweke lami punda wapiti vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. Wananchi wanateseka, lakini Mheshimiwa Waziri kesho Shilingi yako naondoka nayo.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ramadhani Ighondo. Nilimtaja Mheshimiwa Seif Gulamali, Mheshimiwa Flatei Massay, na Mheshimiwa Kuchauka, ajiandae.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niweze kuchangia katika Wizara hii ya Ujenzi. Kwanza nitumie nafasi hii kumpongeza Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa ambayo ameendelea kuifanya katika sekta hii ya ujenzi hasa ununuzi wa ndege, ujenzi wa barabara, miundombinu, umaliziaji wa madaraja makubwa kama *Tanzanite* na pia kule Kigongo, Busisi, unaweza kuona ujenzi wa

treni ya umeme ambao unaendelea kutoka Dar es Salaam, Dodoma, Tabora - Mwaza, Tabora - Kigoma mpaka Katavi. Pia, nampongeza Waziri kwa kusimamia kwa ukaribu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi amemsikia vizuri sana mwenzangu Mheshimiwa Ighondo hapa, amezungumza juu ya barabara yake. Nafikiri Mheshimiwa Waziri yuko na sisi hapa, maana yake tunapozungumza hoja zetu na masikitiko makubwa ya wananchi, tunayawasilisha sisi wawakilishi wake hapa ndani ya Bunge lako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya kutoka Choma Chankola kuja Ziba, Ziba - Nkinga, Nkinga kwenda Huge kupitia Ndala ni ahadi Waheshimiwa Marais waliopita, zimekuwepo na bado zinaendelea kuwepo. Kama alivyosema Mheshimiwa Ighondo, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete alituahidi, Mheshimiwa Hayati Dkt. John Pombe Magufuli alituahidi, pia hata alipokuja Makamu wa Rais wakati ule na sasa ni Rais, aliahidi pia barabara hii kujengwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii ya Choma – Ziba, Ziba - Nkinga siyo tu ni muhimu kwa uchumi wa eneo letu kwa Mkoa wa Tabora, pia ni barabara ambayo ndani yake kuna Hospitali kubwa ya Rufaa ya Nkinga, na Chuo cha walimu pale Ndala. Kwa hiyo, unaweza ukaona umuhimu wa barabara hii. Vile vile ni njia fupi sana ambayo inatumiwa na wakazi wengi kusafiri na kusafirisha mizigo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri, ametuahidi mara nyingi, wakati mwingine anatuambia atatupatia kilometa kumi, anampigia simu na Mtendaji Mkuu, lakini hatuoni. Safari hii akatuambia atatuingizia fedha kwenye bajeti hii, hatuoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni mpaka tufanye nini? Mpaka turuke sarakasi kama wengine wanavyofanya? Haiwezekani! Tunamwomba Mheshimiwa Waziri, hebu tufikirie na sisi, tupate hizo kilometa za barabara. Sisi tuna haki, tunalipa kodi kama wanavyolipa kodi watu wengine, tupeni hizo kilometa za barabara tuweze kupunguza adha za watu wetu katika maeneo

yetu. Imekuwa ni ahadi, hasa kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi barabara hii imo, 2025 na tunaamini tena 2025 - 2030 sijui tutaenda kuwaambia tena tutatengeneza, kwa sababu imeshakuwemo vipindi viwili vya Ilani ya Uchaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri, tunaomba sana ulipe uzito, isifike uchaguzi barabara hii haijaanza kufanya kazi. Litakuwa ni jambo ambalo siyo la kiungwana na tutakuwa hatujawatendea haki wananchi wa Jimbo la Manonga, Wilaya ya Igunga Mkoa wa Tabora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri sehemu nyingine ambayo napenda nichangie katika Wizara hii ya Uchukuzi, kumekuwepo na mamlaka nyingi za udhibiti ndani yake. Naweza nikazungumza kidogo Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi na hili liko dunia nzima, kuwepo kwa mamlaka nyingi za udhibiti kama zilivyo ada ya kawaida, na hili ni lengo la kuhakikisha kwamba tunadhibiti masuala ya ulinzi na usalama wa nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye uchukuzi tunaweza kufanya maboresho katika hizi mamlaka, tukaunda angalau tuwe na tume, tukaunda idara. Napenda tutunge sheria ya udhibiti wa usafirishaji wa mizigo hatari. Najua ziko mamlaka nyingi zinazofuatilia kwa karibu hii mizigo hatari. Mfano, mizigo hatari hii tunaweza tukazungumza *petrol*. *Petrol* ni miongoni mwa mizigo hatari, *petrol* ni nishati, ina mamlaka ya *EWURA; petrol* ni kemikali ambayo inasimamiwa na Mamlaka *GCLA;* pia *petrol* inapokuja bandarini inakuwa chini ya mamlaka ya *TASAC*; pia *petrol* inapotembezwa ndani ya nchi, inapozungushwa inakuwa chini ya *LATRA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa napendekeza tuwe na chombo kimoja ambacho kinaweza kuwa na sheria na kanuni, kikawa na vitu vyote hivi kama vile ambavyo wenzetu Marekani wanayo Idara ya Usafirishaji inayo-*deal* na masuala haya ya usafirishaji. Inayo kodi kabisa na sheria imetungiwa. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri, kuiga kwa wenzetu siyo vibaya, hasa kwa mizigo hatari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata mfano wa pili, tumeweza kuangalia usafirishaji wa virushi na vipeto. Hivi vifurushi na vipeto pia unaweza kuona vina mamlaka nyingi. Kwa mfano, vifurushi na vipeto viko *TCRA,* kama ukiwa unasafirisha mizigo hatari, iko *GCLA*. Pia kama inahusu masuala ya afya, iko Wizara ya Afya; na pia kama inasambazwa ndani ya nchi, iko *LATRA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa naomba tuhakikishe kwamba ili hii sekta ya uchukuzi iwe na mfumo ambao unasimamiwa vizuri kuondoa hii mikanganyiko na hatari nyingi ambazo inaweza kusababishwa, na kuondoa kudumaza kwa sekta yenyewe, maana yake sekta ya usafirishaji ikidumaa *department* nyingine zinadumaa zaidi. Kwa hiyo, nashauri kwamba tutunge Sheria ya Kudhibiti Usafirishaji wa vifurushi na vipeto kwa njia ya barabara, kutoka *TCRA* na hii isimamiwe na *LATRA*.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Seif Gulamali.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Flatei Massay, Mheshimiwa Zuberi Kuchauka na Mheshimiwa Japhet Hasunga, ajiandae.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa nafasi hii. Kwanza nianze kumshukuru Mungu sana kwa kunipatia uhai na kunijalia kuwa hapa. Nawashukuru sana wananchi wa Jimbo la Mbulu Vijijini kunileta hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimshukuru sana Mheshimiwa Rais, ambaye hakika ametufanyia maajabu mengi sana kwa kutuletea miradi ya maendeleo kwenye maeneo yetu. Vilevile leo pia kwa mara ya kwanza nishumkuru sana Mheshimiwa Waziri Mbarawa na Naibu wake Kasekenya na Naibu mwingine Mwakibete na nishukuru sana Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nimekuja kwa namna nyingine kabisa ya shukurani, kwa sisi Wakristo kuna maneno kwenye Biblia

yanasema hivi *"Moyo usiyo shukuru hukausha mema yote."* Sasa mimi sitaki kuwa kama hivyo, ni siku mbili zimepita Mheshimiwa Waziri amekuja kwenye Jimbo langu na tumesaini mkataba wa kujengewewa kilomita 25 kwa lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo wananchi wa Jimbo la Mbulu Vijijini ambao hawakuona barabara hiyo tangu wamezaliwa, tumesaini mkataba. Sasa ninaposaini mkataba ni wazi kwamba ni ishara tosha kwa sisi Wakristo huwa tuna ndoa tunazifunga na mkataba ule tunauchukulia kama ndiyo ndoa mie na Serikali ya kujengewa barabara hiyo. Kwa maana hiyo basi naamini kabisa kutokana na kilichofanyika jimboni, ni wazi kwamba barabara itajengwa na wananchi wa Jimbo la Mbulu Vijijini wataona barabara ya lami mwaka huu. Naamini kwa mkataba tuliyo saini, hakika sina namna ya kushukuru na neno la shukrani siyo kubwa sana. Kwa lugha yetu ya Kiswahili unasema ahsante, ukiongeza sana unasema ahsante sana imeishia hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo kwa kingereza pia na unajua siyo neno refu ni *thank you* unamalizia *thank you very much,* hata ukiongea kwa lugha yangu nyingine ya mtani wangu Mwigulu unasema nini *songela* ukiongeza unasema *songela zigizigi,* hata kwa rafiki yangu Musukuma unasema *wabheja* halafu unaelekea kwenye *wabheja* sana. Sasa hizi ni shukurani na kwa sisi Wakristo huwa tukishukuru tuna namna yetu kwenye sala ya baba yetu unaposema "Baba yetu uliye mbinguni jina lako litukuzwe" una mshukuru huyu Mungu, halafu unaendelea tena unasema "utupe riziki za kila siku" maana yake unaomba tena. Sasa ndugu yangu Mheshimiwa Mbarawa kilomita 25 si ndogo, sasa si ndiyo naomba tena. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeiona barabara ile iko hapa na imetengewa fedha, imetengewa bilioni tano. Siyo ndogo kwa sababu si nilikuwa sina, ilikuwa *zero*. Sasa kwa sababu barabara ile ni kilomita 389, nimwombe Waziri huo mwanzo siyo mbaya, leo nimekuja kwa namna nzuri kabisa ya upole, ile sarakasi ya mwaka jana Waziri hataiona leo. Hataiona kwa sababu tumekubaliana tunajenga barabara na kwa ajili hiyo basi naomba ndugu yangu ameonyesha kabisa hapa anajenga kilomita zote hizi 389 kuanzia

Karatu, maana ataunganisha Mkoa wa Manyara na Arusha, atakuja Mbulu Mjini, atakuja Dongobesh, atakwenda Haydom, lakini pia atakwenda Sibiti utakwenda na Lalago *River* mpaka Meatu na Simiyu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpa tu taarifa ndugu yangu hapa kilomita 25 ni nzuri kwa hiyo tumeishai – *design* tayari, lakini naomba basi sasa barabara ile ijengwe kama nilivyosema na hawa Washirika wa Maendeleo ambao Waziri amewasema hapa *EPC + Finance,* lakini asisahau ile Barabara ya Dareda unakuja Dongobesh ambayo ameiwekea kilomita nane, lakini pia barabara ile pia ambayo inatoka Mugitu kuja Haydom kwa sababu Mheshimiwa Waziri ameahidi katika mkutano ule wa hadhara, naomba asiisahau hiyo barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukweli ni kwamba barabara hizo zitakavyojengwa, Waziri atakuwa amefungua maeneo ya uchumi katika eneo letu kubwa kabisa ambalo unakwenda moja kwa moja kutokea Meatu, hata watu wa Mara watapitia barabara ile hawana haja ya kuja Singida, hawana haja ya kwenda Babati wanapoenda Arusha hata wanapoenda Ngorongoro hawana haja ya kupitia kwenye Msitu ule wa Serengeti. Kwa hiyo barabara ile hakika ni ya kimaendeleo. Kwa bahati nzuri kule tunalima vitunguu, vitunguu saumu, mahindi, mbaazi, alizeti, kwa hiyo ni barabara ya kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, ombi langu kubwa sana hasa kwa Mheshimiwa Waziri wa Fedha tumeisha saini mkataba, isitokee ile tabia tunayoiona ya kusubirisha wakandarasi wasipate fedha. Naomba Mheshimiwa Mwigulu, yeye ni mtaalam wa mambo ya uchumi, awalipe hawa wakandarasi ambao sasa tumeshasaini, fedha ziende mara moja ili barabara ijengwe kabisa moja kwa moja. Sasa hivi kesi mimi na Waziri Mheshimiwa Mbarawa imeishia hapa kwa sababu najua tumeshasaini, kesi yangu inahamia kwa Mheshimiwa Mwigulu ili atoe hela na hela hizi anapozitoa maana yake ni barabara inajengwa. Nina hakika wananchi wa Mbulu ambao Mbulu imeanza mwaka 1905, ilikuwa haina barabara kwa kusaini huko basi, maana yake tutakwenda kujengewa barabara ambayo itaondoa kabisa ile hali ambayo ameisema Mheshimiwa Mbunge mmoja wa Singida hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hospitali ya Haydom ni hospitali kubwa sana, inategemewa sana na Mikoa mitano Simiyu, Singida, Manyara…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, ahsante sana.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru sana na kwa kweli leo niunge hoja mkono na nimalizie hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Zuberi Kuchauka, Mheshimiwa Japhet Hasunga na muda mchache utakaobaki atamalizia Mheshimiwa Ahmed Yahya. *(Makofi)*

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii iliyoko mbele yetu.  Kilichonisimamisha hapa ni kushukuru. Kwa kweli katika watu ambao wanatakiwa kushukuru sana na mimi ni miongoni mwao baada ya kuiona Barabara yangu ya Masasi – Nachingwea – Liwale na hii Barabara ya Nangurukuru – Liwale, kilomita 50 niseme ahsante sana, kwani sisi tumefundishwa kwamba asiyejua kumshukuru mtu mwenzie basi hata mwenyezi Mungu hawezi kumshukuru.  Hivyo, nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri pamoja na wasaidizi wake wote wawili na watendaji wote wa Wizara hii, kwa kweli wamenitendea haki mwaka huu kwenye bajeti, nawashukuru sana.  Kama ilivyo ada wanasema kushukuru ni kuomba tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli mama anavyoamua kuifungua nchi hii, niwaombe sana Watanzania na wasaidizi wake hasa wasaidizi wake, tumsaidie mama. Mama anakwenda kujenga *SGR,* ananunua ndege, anajenga bandari ya uvuvi, kama Bandari yetu hii ya Dar es salaam itabaki vile ilivyo, tutakuwa hatuja mtendea haki. Tuna shida gani? Tumesomesha

*Engineers*, Wanasheria, tunavutavuta miguu kwenda kuiboresha bandari yetu kwa sababu ipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sana sambamba na uboreshaji wa Bandari ya Dar es Salaam. Si tumesema tuna *PPP* hapa jamani, sasa tunavuta mguu kwa nini? Hivyo *SGR* tumeijenga kutoka Dar es Salaam mpaka Kigoma. Kama bandari yenyewe ndiyo ile ambayo kwa watu wengine wanaita mwalo, kule Mwanza wanaitwa mwalo kama mwalo tu hivi. Niwaombe sana tusivute miguu, kwenye hili watendaji wa Serikali wanaomsaidia Mama tusivute mguu, twende *PPP* tuboreshe Bandari yetu ya Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo kuna barabara wanayoijenga hii ya Masasi kwenda Mtwara wanaendelea kuiboresha na kuitengeneza, lakini barabara ile wasipojenga hii reli ya kutoka Mbambabay kwenda Mtwara barabara hii itaendelea kuteseka, kwa sababu kule makaa ya mawe yanayopita kwenye hiyo barabara wanakwenda kuichakaza hii Barabara. Nawaomba sana, sana hii reli ya Mtwara Mbambabay ijengwe, ni reli imetajwa muda mrefu imezungumzwa sana, nawaomba kwenye bajeti hii, hii reli iende ikajengwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile asubuhi hapa Mheshimiwa Mhata ameuliza swali muhimu sana. Kuna barabara inaunganisha wilaya nne, barabara hii inatoka Mangaka – Nachingwea mpaka Liwale, barabara hii inatoka Tunduru inaunganisha Wilaya ya Tunduru, Wilaya ya Nanyumbu, Wilaya ya Nachingwea mpaka Wilaya ya Liwale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona kwenye randama hapa au kwenye bajeti wameandika kuna upembuzi yakinifu wa barabara inayotoka Liwale kuelekea Mahenge. Barabara hii kiunganisho chake kikubwa ni barabara inayotoka hapa Tunduru, Nanyumbu. Barabara hii mpaka sasa hivi bado ina hudumiwa na *TARURA*. Niwaombe sana, sisi kwenye *RCC* yetu Mkoa wa Lindi tulishaiombea hii barabara iingie *TANROADS,* muda mrefu sana. Sasa umefika wakati naomba hii barabara itoke *TARURA* iende *TANROADS* ili iweze kujengwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirejee hapo hapo kwenye *TAZARA* imezungumzwa hapa tunaenda kuboresha *TAZARA*. Sambamba na *TAZARA* na hizo meli za uvuvi nilizozungumza, ni lazima tuhakikishe narudia tena wasaidizi wanaomsaidia Mheshimiwa Rais, Rais ameamua kuifungua nchi hii kiuchumi, hizi ni fursa ambazo tunataka kuzitumia, naomba tumsaidie kikweli kweli kwa kuiboresha Bandari yetu ya Dar es salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa na hayo tu machache, yanatosha kwa leo. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zuberi Kuchauka, ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Japhet Hasunga na muda utakaobakia atamalizia Mheshimiwa Ahmed Yahya.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipatia nafasi. La kwanza, nianze kuipongeza Serikali kwa kazi kubwa ambayo wamekuwa wakifanya katika kuwekeza katika miundombinu na maeneo mbalimbali. Tumeshuhudia namna uwekezaji ulivyo mkubwa kwenye kampuni yetu ya ndege, ndege mbalimbali zimenunuliwa na zingine ziko njiani zinakuja. Kwa kweli wamefanya kazi kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshuhudia uwekezaji kwenye *SGR* ambayo ni matrilioni ya fedha. Tumeshuhudia uwekezaji kwenye bandari, kwenye upanuzi wa bandari na wametumia zaidi ya milioni 421 dola za Marekani kwenye upanuzi wa Bandari ya Dar es Salaam na maeneo mengine. Kazi kubwa wameifanya tunawapongeza sana. Kwa hiyo tunaipongeza Wizara, tunawapongeza watendaji wote, watendaji wa taasisi zilizo chini ya Wizara hii wanafanya kazi nzuri sana. Hongera sana sana kwa kazi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Waziri kwanza kwa kutusaidia kuhakikisha kwamba Barabara ya Ruanda – Idiwili mapaka Nyimbili ikiwa inaelekea mpaka Itumba kwa kuiweka kwenye bajeti imepangiwa bilioni moja japo ni ndogo, lakini tumeona wameweka kilomita 21, tunawashukuru sana kwa kazi hiyo nzuri. Pia kuna Barabara ya Vwawa – Hasamba kwenda kwenye Kimondo, Kimondo cha aina yake ambayo wamekuwa

wakiijenga, wanaendelea kuijenga. Tunaamini wataendelea kutenga fedha ili kuhakikisha kwamba ile barabara inakamilika, kusudi watalii wanapoenda kwenye kimondo waweze kufika kiurahisi. Tunawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuna Barabara ya kutoka Ihanda kwenda Chindi kupitia Ipunga hii barabara wanaifanyia kazi, wanaihudumia, tunashukuru sana kwa wakiendelea kuihudumia. Kuna Barabara ya Hezya mpaka Itumba bado ilikuwa kwenye upembuzi yakinifu, sasa tunataka waikamilishe ili ile barabara sasa watu wa kutoka Malawi wanaweza wakapitia ile barabara mpaka kuja katika maeneo mengine, kwa hiyo tunaamini wataendelea kuifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Meneja wa Mkoa wa *TANROADS,* anafanya kazi nzuri sana. Huwezi kuamini wakati mwingine saa sita za usiku anakwambia naenda kuangalia sehemu fulani mkandarasi amekwama, naenda kufuatilia hiki, anafanya kazi nzuri sana na anatupa ushirikiano mzuri sana, nampa hongera kwa hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa zaidi pale Mpemba tunaomba Bandari Kavu. Tunataka mizigo ikisafirishwa na *TAZARA* kutoka Dar es Salaam iende mpaka pale Mpemba ili Nchi za *SADC,* ziende kuchukulia mizigo pale itarahisisha sana na itakuwa imetoa mchango mkubwa sana tunaomba sana hilo liweze kufanyika na tunaamini litatusaidia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sanjari na hilo Reli ya *TAZARA* ni muhimu ikaimarishwa, ikaboreshwa, mabehewa yakatafutwa, uwekezaji ukafanyika, ile sheria tukaipitia upya ili kuhakikisha kwamba iendelee kutoa mchango mkubwa katika eneo la kusini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo nchi yetu imebahatika kwa sababu ni nchi ambayo tuna bahari kubwa, tunayo Bahari ya Hindi, tunayo Maziwa na maeneo mengine. Nchi yoyote wenye bandari, yenye bahari haitakiwi kuwa maskini. Sisi tumebahatika kuwa na nchi ambayo tuna–*access* na bandari, sasa uwekezaji lazima ufanyike, natamani kuona Bandari ya Dar

es Salaam ifanane na Bandari ya Rotterdam, Bandari ya Singapore na bandari zingine kubwa duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya yote yanawezekana kwa kuwekeza na uwekezaji wa kwenye bandari unaweza ukawekeza kwa hela ya kukopa, unaweza ukawekeza kwa kukopa kutoka kwa wananchi kama walivyofanya Wamisri, Wamisri wakati wanajenga ule mfereji wa *Suez Canal* wa pili wao walikopa kwa wananchi, wakaamua kujenga mfereji wa pili ili meli ziwe zinapishana, waliamua na sisi tunaweza tukawekeza pale kwenye bandari kwa hela ya kutoka kwa wananchi au tukakopa nje au tukafanya lolote lile maadam bandari yetu tuongeze uwekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naunga mkono jitihada zinazofanywa na Serikali katika kuhakikisha bandari hii inapanuliwa, bandari hii ifanye kazi, tunataka kuona pale Bandari ya Rotterdam upana wa kule ni kilomita 42, sisi pale bado ni padogo. Kwa hiyo tunahitaji eneo hata lile lote la Kigamboni, watengeneze maeneo ya kuweka mizigo, waboreshe ili kusudi mizigo yote ya huku iweze kupitia pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji ujenzi wa Bandari ya Bagamoyo iwe tuna fedha iwe hatuna ambapo tumefanya maamuzi makubwa ya kukopa, ya kutafuta kila mahali tulivyowekeza na Bandari ya Bagamoyo atafutwe mwekezaji, ajenge na yenyewe ikiwezekana ile bandari nyingine kama itapatikana kokote tujenge ili tuweze kujenga uchumi imara wa nchi yetu. Tunaamini kwa kufanya hivyo, mizigo ya nchi jirani inaweza ikahudumiwa na nchi yetu ikapata fedha nyingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda nakushukuru kwa kunipatia nafasi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Japhet Hasunga ahsante sana na dakika zilizobaki atamalizia Mheshimiwa Ahmed Yahya.

**MHE. AHMED YAHYA ABDUWAKIL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili kuchangia bajeti hii ya

Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, ambayo ni bajeti mkombozi na Wizara ambayo inaweka ustawi mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda mbele zaidi napenda kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan na namna anavyotupendezesha na kutufurahisha katika uongozi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara ya mwanzo nilivyosimama kuongea kwenye kiriri hiki nilisema maajabu ya Reli ya *SGR,* leo Tanzania tunakuwa kama Marekani. Tunakuwa na reli ya kisasa ambayo ni sawasawa na Shirika la Reli la Marekani linaloitwa *FELA* na kama nasema uongo Balozi Mulamula analijua vizuri shirika hili. Kwa hiyo na sisi Tanzania tunaingia katika historia mpya kwa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiingia kwenye nukta ya pili tuseme tu kwamba nchi inasonga mbele, ndugu yangu Profesa Mbarawa na timu yake na *Engineers* wake wanafanya kazi usiku na mchana. Nimewahi kushuhudia daraja la Wami, kazi imemalizika kabla ya muda ambayo si rahisi kwasisi tunaoshughulika na shughuli za ujenzi, lakini Daraja la Wami limeokoa vifo kabla muda na limefunguliwa kabla ya muda. Hili niseme tu ni kwa sababu ya kuwa na watendaji wazuri na aliyevaa kiatu cha *TANROADS Engineer* Mativila lazima apongezwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda mbali zaidi kwa shukurani kwamba kwa sisi watu wa Kusini Zanzibar tunaitwa kwamba Profesa na timu yake "hawana lala" kucha kutwa "wa kazini" maana yake wao kutwa muda wote wako kazini. Kwa hiyo nampa hongera sana sana Profesa, anafanya kazi nzuri na timu yake yote, *Engineers* wote hapo Mwakibete na wenzio. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara nyingi humu katika Bunge imezungumzwa *Air Tanzania* ambayo inafanya kazi kubwa. Pamoja na matatizo madogo madogo yaliyokuwepo lakini *Air* Tanzania wanafanya kazi kubwa sana. Mashirika ya Ndege kama Ethiopia, *Alitalia American Air* na mengineyo hayakuanza hivyo, walianza kwa kusuasua mpaka yakatengemaa. Yapo matatizo

madogo madogo ya kiutendaji na *CEO* Matindi anachukua juhudi kubwa sana kuweka sawa. Kwa hiyo tuwapongeze, tungepata wapi kama si juhudi za Mama? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Timu ya Yanga Africans inakwenda Algeria kwa ndege yetu, tungepata wapi? Kwa jeuri tunaipeleka na kuirejesha, kwa hiyo kwa sifa hizo, naunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ahmed Yahya ambaye ni mchangiaji wetu wa mwisho kwa siku hii ya leo. Niwapongeze Waheshimiwa wote kwa michango yenu mizuri kwa Wizara hii ya Ujenzi na Uchukuzi, nikiamini kabisa kwamba ina dhamira njema kwa Taifa letu na Mheshimiwa Waziri na timu yake wako makini hapo kupokea yote ambayo mmekuwa mkiyazungumza. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge kabla ya kuahirisha shughuli za Bunge kuna Tangazo la Wageni ambao wapo jioni hii ambao ni wageni wa Mheshimiwa Stephen Byabato, Naibu Waziri wa Nishati ambao wanatoka Jimboni kwake Bukoba, Mkoa wa Kagera ambao ni Ndugu Seberian Buhaga na Ndugu Azzat Simba. Karibuni sana wageni wa Mheshimiwa Stephen Byabato. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya tangazo hilo, nawatakia jioni njema na naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu kamili asubuhi.

*(Saa 1.45 Usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumanne, Tarehe 23 Mei, 2023 Saa Tatu Asubuhi)*